ELLEN G. WHITE ESTATE

# Tangu Sasa Hata Milele

ELLEN G. WHITE

# TANGU SASA HATA MILELE

Ellen G. White

2011

Copyright © 2021
Ellen G. White Estate, Inc.

# Information about this Book

## Overview

This eBook is provided by the Ellen G. White Estate. It is included in the larger free Online Books collection on the Ellen G. White Estate Web site.

## About the Author

Ellen G. White (1827-1915) is considered the most widely translated American author, her works having been published in more than 160 languages. She wrote more than 100,000 pages on a wide variety of spiritual and practical topics. Guided by the Holy Spirit, she exalted Jesus and pointed to the Scriptures as the basis of one's faith.

## Further Links

A Brief Biography of Ellen G. White
About the Ellen G. White Estate

## End User License Agreement

The viewing, printing or downloading of this book grants you only a limited, nonexclusive and nontransferable license for use solely by you for your own personal use. This license does not permit republication, distribution, assignment, sublicense, sale, preparation of derivative works, or other use. Any unauthorized use of this book terminates the license granted hereby. (See EGW Writings End User License Agreement.)

## Further Information

For more information about the author, publishers, or how you can support this service, please contact the Ellen G. White Estate

at mail@whiteestate.org. We are thankful for your interest and feedback and wish you God's blessing as you read.

# Contents


Information about this Book . . . i
SABABU GANI INAKUPASA KUSOMA KITABU HIKI . . . xii
Kuinua Pazia Kwa Wakati Ujao . . . xiv
1 /UNABII WA HALI YA MWICHO WA ULIMWENGU . . . 21
Uharibifu wa Hekalu Tukufu . . . 23
Uvumilivu wa Mungu . . . 25
Alama za Musiba . . . 26
2 /WAKRISTO WA KWANZA -WAAMINIFU NA WA KWELI 30
Makundi Mawili ndani ya Kanisa . . . 32
3 /GIZA LA KIROYO KATIKA KANISA LA KWANZA . . . 35
Namna Sabato Ilivyogeuzwa . . . 36
Siku za Hatari kwa Kanisa . . . 39
Namna Mafundisho ya Uongo Yaliingia . . . 40
4 /WAFUASI WA WALDENSE WANAKINGA IMANI . . . 43
Roma Inakutana na Dini ya Biblia . . . 44
Damani (Bei) ya Mafundisho ya Ukweli . . . 46
Vijana Walifundishwa Kuwa Wajumbe (wa injili) . . . 48
Wenye Zambi Walimushota Kristo . . . 49
Kushambulia Ufalme wa Shetani . . . 49
Roma Inakusudia Kuangamiza Wavaudois (Waldenses) . . . 50
5 /NURU INANGAA KATIKA UINGEREZA . . . 52
Mvumbuzi Hodari wa Kosa . . . 53
Anashambuliwa na Ugonjwa wa Hatari . . . 56
Wycliffe Anakataa Kukana . . . 57
Mpinga Mbiu wa Wakati wa Sasa . . . 59
6 /KIFO KIMEWAFIKIA MACHONI WASHUJAA WAWILI . 61
Picha mbili Inamvuta Huss . . . 62
Prague Ikawekwa Chini ya Makatazo . . . 63
Mwenendo wa Salama Kutoka kwa Mfalme . . . 65
Ushindi Ulioonekana Mbele . . . 66
Huss Alikufa Juu ya Mti (Mti wa kufungia Watu wa Kuchomwa na Moto wanapo kuwa Wahai) . . . 68
Jerome Anatii Baraza . . . 69
Jerome Anapata Toba na Uhodari Mpya . . . 69

Akahesabiwa Kifungo na Mauti . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71
Kusalitiwa kwa Njia ya Upatanishi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73
7 /LUTHER, MTU KWA WAKATI WAKE . . . . . . . . . . . . . . . . 75
Kutafuta Amani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 76
Ukweli juu ya ngazi ya Pilato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 78
Huruma za kuuzisha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 79
Kazi ya Luther Inaanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 80
Luther Alikimbilia Tu kwa Biblia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 82
Kuokoka Toka Augsburg . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 85
Shida ya Kutisha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 86
8 /MSHINDI WA UKWELI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 89
Luther Anashitakiwa kuwa Mpinga Imani ya Dini . . . . . . . . 90
Luther Anaamuriwa Kufika Barazani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 91
Uhodari wa Mfia Dini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 92
Luther Anasimama Mbele ya Baraza . . . . . . . . . . . . . . . . . . 94
Luther Mbele ya Baraza Tena . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 96
Cheti cha Usalama cha Luther Katika Hatari . . . . . . . . . . . . 99
Juhudi kwa Ajili ya Masikilizano na Roma . . . . . . . . . . . . . 100
Mungu Anatumia Frederic wa Saxe . . . . . . . . . . . . . . . . . . 102
Usalama huko Wartburg . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 102
9 /NURU ILIWASHWA KATIKA USUISI . . . . . . . . . . . . . . 104
Zwingli Akaitwa Zurich . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 106
Uchuuzi wa cheti cha Kuachiwa Zambi katika Usuisi . . . . 107
Mabishano (Wafuasi wa kanisa la Roma) . . . . . . . . . . . . . . 108
10 /MAENDELEO KATIKA UJEREMANI . . . . . . . . . . . . . . 111
Tunda la Mafundisho Mapya Limeonekana (limetambulika) 112
Uwezo wa Neno . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 113
Maumivu Makuu ya Roho Sasa Yakalemea Juu ya Luther . 114
Kujifunza Biblia Mahali Pote . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 116
11 /USHUHUDA WA WAANA WA WAFALME . . . . . . . . . . 118
Mwishowe ikakusudiwa kwamba mahali ambapo . . . . . . . . 119
Ushindani Bora wa Waana wa Wafalme . . . . . . . . . . . . . . . 120
Makutano Huko Augsburg . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 122
12 /MAPAMBAZUKO KATIKA UFRANSA . . . . . . . . . . . . . 125
Agano Jipya la Kifransa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 127
Berquin Shujaa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 128
Berquin kwa Mti Wakufungia Watu wa Kochomwa Moto . 129
Mwito wa Calvin . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 129

Ushahidi kwa Mchomo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 130
Utawala wa Hofu Kuu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 132
Kupiga Chapa Kulikatazwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 133
Froment Mwalimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 136
Ngurumo ya Laana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 137
Ushindi kwa Ajili ya Matengenezo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 138
13 /KATIKA UHOLANDI NA SCANDANAVIA . . . . . . . . . . 140
Matengenezo Katika Danemark . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 142
Maendeleo katika Uswedi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 143
14 /UKWELI UNAENDELEA KATIKA UINGEREZA . . . . 145
Tyndale Anatafsiri Agano Jipya kwa Kiingereza . . . . . . . . . 146
Uwezo Kamili wa Maandiko . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 147
Yohana Knox . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 148
Maelfu ya Wachungaji (Pasteurs) Walifukuzwa . . . . . . . . . 149
Kuhesabiwa Haki kwa Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 150
Moyo wa Wesley “Kwa Jinsi Isiyo ya Kawaida Watiwa Joto” 151
Wesley Anaepuka Kifo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 152
Katika Utetezi wa Sheria ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . 154
Umoja wa Sheria na Injili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 155
15 /UTAWALA WA KUTISHA WA UFARANSA . . . . . . . . . 156
Sababu yake ya Kweli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 156
Utimilizo wa Ajabu wa Unabii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 158
Uadui Juu ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 158
Uovu Mbaya Sana Kupita Mengine . . . . . . . . . . . . . . . . . . 159
Uhodari wa Kutukana Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 161
Mungu wa Kike wa Kutumia Akili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 162
Ingeweza kuwa Nini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 163
Matokeo Yaliyopatwa katika Damu . . . . . . . . . . . . . . . . . . 165
Kosa la Hatari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 167
16 /KUTAFUTA UHURU KATIKA DUNIA MPYA . . . . . . . 169
Mungu akageuza matokeo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 170
Roger Williams . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 171
Barua ya maagano wa Uhuru . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172
Ulinzi wa kweli Kabisa wa Ukuu wa Taifa . . . . . . . . . . . . . 173
17 /AHADI ZA KURUDI KWA KRISTO . . . . . . . . . . . . . . . 175
Tetemeko la inchi lililotikisa Ulimwengu . . . . . . . . . . . . . . 177
Kutiwa giza kwa jua na Mwezi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 178
Mwezi kama Damu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 179

Mwito kwa Kuamka . . . 180
Ujumbe Uliotolewa na Watu Wanyenyekevu . . . 181
18 /NURU MPYA KATIKA DUNIA MPYA . . . 185
Miller Anapata Rafiki . . . 186
Kuja kwa Kristo mwenyewe . . . 188
Maandiko matakatifu na Taratibu ya Miaka . . . 189
Kuvumbua Oroza ya Wakati wa Unabii . . . 190
Mda wa Nyakati Mbili Zilianza Pamoja . . . 191
Habari Njema Imetolewa kwa Ulimwenguni . . . 192
Mwisho wa Kuhofisha . . . 192
"Wende na Ulihubiri kwa Uiimwengu" . . . 193
"Nyota Zitaanguka" . . . 194
Maonyo Yalitimilika . . . 196
Usikivu na Kutokuamini . . . 197
Wenye Mashaka na Wasioamini . . . 197
19 /SABABU GANI UCHUNGU MKUBWA ULE? . . . 200
"Wakati Umetimia" . . . 201
Kutoka kwa Kukata Tamaa na Kuelekea Uhakikisho Tumaini 203
Ujumbe wa Wanafunzi Ulilinganishwa na Ujumbe wa 1844 203
20 /UPENDO KWA AJILI YA KUJA KWA KRISTO . . . 206
Katika Inchi Mbalimbali kwa Wakati Moja . . . 207
Kupinga Maelezo ya Watu Wengi . . . 209
Uwezo katika Kitabu . . . 209
Ujumbe wa Waadventisti katika Uingereza . . . 210
Ufunuo Ukafunuliwa kwa Bengel . . . 211
Wahubiri Watoto wa Skandinavie . . . 212
Ujumbe Unatawanyika . . . 213
Maandiko Rahisi Yanaleta Hakikisho . . . 214
Habari llipingwa . . . 215
21 /KUTESWA KWA AJILI YA MWENENDO WA MPUMBAFU AO MJINGA . . . 218
Binadamu Anakataa Nuru . . . 219
Ujumbe Wa Malaika wa Kwanza . . . 220
Ujumbe wa Malaika wa Pili . . . 221
Uzinzi wa Kiroho . . . 221
Kujiunga Pamoja na Walimwengu . . . 223
Safari za Kwanza kutoka kwa Habari Njema . . . 223
22 /UNABII UNATIMILIKA . . . 227

Ukaidi wa Dini Unaonekana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 228
Kosa Linasahihishwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 230
"Kilio cha Usiku wa Manane" . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 231
Kukatishwa Tamaa Tena . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 232
Ujumbe Ulitolewa kwa Wakati Uliofaa . . . . . . . . . . . . . . . . 233
Imani Inaimarishwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 234
23 /SIRI YA WAZI YA PAHALI PATAKATIFU . . . . . . . . . . . 235
Pahali Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu . . . . . . . . . . . . 236
Vyumba Viwili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 237
Siri ya Mahali Patakatifu Inaelezwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . 239
Kutakaswa kwa Pahali Patakatifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 239
Siku Kuu ya Upatanisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 240
Uhakika wa Mbinguni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 241
Kazi ya Hukumu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 242
24 /KRISTO ANAFANYA KAZI GANI SASA? . . . . . . . . . . 244
Nani Atakayesimama? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 245
"Tazama, Bwana Arusi Anakuja" . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 245
Wanaongoja Bwana Wao . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 246
Kufunga Kazi ndani ya Pahali patakatifu . . . . . . . . . . . . . . . 246
25 /SHERIA YA MUNGU ISIYOGEUKA . . . . . . . . . . . . . . 250
Mwito kwa Kuabudu Muumba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 252
Kuinuka kwa Mamlaka Mpya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 253
Mnyama na Sanamu Yake . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 256
Kimya Kamili wa Agano Jipya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 258
Onyo la Malaika wa Tatu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 259
26 /WASHUJAA KWA AJILI YA UKWELI . . . . . . . . . . . . . 261
Sabato ya Kweli Kila Mara Ilishikwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . 262
Si Mapenzi ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 263
27 /UFUFUO WA KISASA UNAKUWA NA MAFANIKIO NAMNA GANI? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 265
Sheria ya Uhuru . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 267
Kukubali Zambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 268
Utakaso ni Nini? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 269
lla tu Kwa Njia ya Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 270
Utakaso wa Biblia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 271
28 /KUSIMAMA MBELE YA HABARI YA MAISHA YETU ZILIZOANDIKWA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 275
Mukusudi ya Siri . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 276

Kipimo cha Hukumu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 277
Bwana Anahamakia Shetani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 278
Kufutia Mbali kwa Zambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 279
Kwa Wakati Uliotajwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 279
Choyo lliyofichwa Imefunuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 280
Maombezi ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 281
Mwisho wa Wote Umekatwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 282
29 /SABABU GANI ZAMBI ILIRUHUSIWA? . . . . . . . . . . . 283
Manunguniko Miongoni mwa Malaika . . . . . . . . . . . . . . . . . 285
Uchuki Ukasitawishwa Katika Uasi wa Juhudi . . . . . . . . . . 286
Kufukuziwa Mbali Kutoka Mbinguni . . . . . . . . . . . . . . . . . 287
Mabishano kwa Ajiii ya Mtu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 289
30 /SHETANI NA MTU KATIKA VITA . . . . . . . . . . . . . . . . . 290
Adui Mwangalifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 291
31 /PEPO WACHAFU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 293
Malaika Walinzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 294
32 /NAMNA YA KUMSHINDA SHETANI . . . . . . . . . . . . . 297
Kweli Inatakasa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 298
Biblia Yote ni Kiongozi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 299
Makosa ya Hatari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 300
Mipaka ya Neno . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 301
Ushuhuda wa Kufaa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 302
33 /NI KITU GANI KINACHOLALA NG'AMBO YA PILI YA KABURI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 304
Uwongo Mkubwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 305
Ujushi wa Maumivu Mabaya ya Milele . . . . . . . . . . . . . . . 306
Wokovu wa Watu Wote Si Fundisho la Biblia . . . . . . . . . . . 307
Masharti Yameelezwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 308
Hawakutayarishwa Kuingia Mbinguni . . . . . . . . . . . . . . . . 309
Mshahara wa Zambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 310
Ufufuo wa Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 310
34 /NI WANANI WANAOKUWA "PEPO" KATIKA IMANI YA ROHO ZA WATU WALIOKUFA HURUDI NA KUJIONYESHA NA KUONGEA NA WATU? . . . . 314
Mwito Wa Shetani Kwa Wenye Akili . . . . . . . . . . . . . . . . . 315
Mwito kwa Kupenda Anasa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 316
Biblia llifananishwa kama Habari za Uwongo . . . . . . . . . . . 317
35 /UHURU WA ZAMIRI UNATISHWA . . . . . . . . . . . . . . . . 321

Mapatano na Ukubali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 322
Mfano Wa Kushangaza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 323
Umoja wa Upagani na Ukristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 324
Badiliko katika Kanisa la Protestanti . . . . . . . . . . . . . . . . . . 325
Kushika Siku ya Kwanza (Jumapili) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 326
Mnyama wa Pembe Mbili Mfano wa Mwana-Kondoo . . . . 328
36 /MAPIGANO YA KARIBU SANA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 331
Kuweka Kando Sheria ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 332
Kukosa Kiasi Kumetia Wengi Katika Mashaka . . . . . . . . . . 333
37 /MAANDIKO MLINDA SALAMA YETU PEKEE . . . . . 337
Kutukuza Mamlaka Ya Kibinadamu . . . . . . . . . . . . . . . . . . 338
Shuguli ya Kwanza na ya Juu Sana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 339
Matokeo ya Zarau ya Maombi na Kujifunza Biblia . . . . . . 340
38 /UJUMBE WA MUNGU ULIO WA MWISHO . . . . . . . . . 342
Jaribu Kubwa la Uaminifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 343
Machafuko Yanakaribia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 345
Upinzani Umeongezeka kwa Kimo Kipya . . . . . . . . . . . . . . 345
Mvua Ya Mwisho Na Kilio Cha Nguvu . . . . . . . . . . . . . . . . 346
39 /WAKATI WA TAABU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 348
Wakati wa Taabu ya Yakobo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 350
Maumivu Makuu ambao Mungu Atalaumiwa . . . . . . . . . . . 351
Zambi Zilifutiliwa Mbali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 351
Imani lnayovumilia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 352
Watu wa Mungu Hawataongozwa Vibaya . . . . . . . . . . . . . . 354
Makundi ya Malaika Wanalinda . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 356
40 /WATU WA MUNGU WANAKOMBOLEWA . . . . . . . . . . 359
Siku ya Bwana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 361
Mfalme wa Wafalme Anatokea . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 362
Katika Mji Mtakatifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 364
Wanadamu Wawili Wanakutana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 365
Waliokombolewa katika Utukufu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 366
41 /DUNIA KATIKA UHARIBIFU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 369
Malaika wa Mauti . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 370
Uhamisho wa Shetani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 371
42 /AMANI YA MILELE: VITA IMEMALIZIKA . . . . . . . . 374
Shambulio la Mwisho la Kumpinga Mungu . . . . . . . . . . . . . 375
Hukumu Inatangazwa Juu ya Waasi . . . . . . . . . . . . . . . . . . 376
Shetani Ameshindwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 378

Mwisho Mkali Sana wa Waovu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 380
Kumbusho ya Kusulubiwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 381
Ushindi wa Upendo wa Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 382
NYONGEZO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 384

# SABABU GANI INAKUPASA KUSOMA KITABU HIKI

Kwa mamilioni ya watu, maisha huonekana kuwa bila maana na upuuzi. Elimu maarifa ya ufundi, hata hekima na elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini, yameeleza wanadamu kama viumbe vya bahati tu. Lakini kwa kujua ama sivyo, wanaume na wanawake huona vigumu kukubali kuishi bila kusudi. Jeuri, kutokukubali na uasi, upimaji wa dawa ya sumu-vitu hivi ndivyo katika makazi mengi, yanayokuwa masemi ya upumbavu ya watu wenye kushindana na maangamizi yao ya kutofisha. Kama watoto waliowekwa mahali pa kuachana achana wakati wa vita wanapolia wanapokuwapekee yao, bila tumaini. Mimi ni nani? Wanani walikuwa wazazi wangu? Namna gani naweza kuwapata?

Wengi hugeukia elimu kwa kupata majibu, kwa kulinganisha madarubini ya radio zetu ndani kwa pigo la moyo la nyota, kama kuuliza, je kunakuwa mtu ye yote anayenijua? Nani anilindaye? Lakini elimu haina jibu. Elimu imewekwa kwa kuuliza maswali: chembe kilifanywa namna gani? Namna gani linawezakupasuliwa? Roho zetu hutumika namna gani? Namna gani ulimwengu ama vitu vyote vilifanyika?

Haiwezi (elimu) kumwambia sababu gani chembe linakuwako, sababu gani wanadamu wanakuwako, sababu gani ulimwengu unakuwako kabisa kabisa. Hata vile haitaweza kujibu maswali hayo ya namna ya pekee yanayohusu watu wenye kufikiri:

Ikiwa kunakuwa na maana na haki katika ulimwengu, sababu gani mwenye asiyekuwa na hatia huteseka pamoja na mwenye hatia?

Je, kunakuwa uzima baada ya mauti? Je, nafsi ya mwanadamu huendelea kuishi? Je, makanisa ya Kikristo ya siku hizi husema kweli kwa ajili ya Mungu? Kweli ni nini?

Ni nini wakati ujao wa dunia? Je, itaishia kwa kulialia kama mtoto anayeteseka kwa ajili ya pumzi ya mwisho katika hewa iliyochafuka, ao juu ya mshindo wa jehanum ya chembe usiozuiwa kutoka kwa tunda dogo jekundu la Ulaya la vitu vya mviringo chini

vilivyochongoka juu vya pua ICBM? Ao wanadamu-ambao katika historia iliyoandikwa hawakuonyesha kamwe uwezo wa kutawala choyo wala kujipenda wao wenyewe kwa msingi-kwa gafula hufaulu kwa kufukuza ubaya, vita, umaskini na hata kifo?

Kitabu hiki kinatoa majibu, na yanatumainisha. Maisha [ii] yanakuwa na maana! Hatupo peke yetu katika ulimwengu. Mtu mmoja mahali fulani hujali! fulani, kwa kweli, aliyejiingiza mwenyewe katika historia ya binadamu, aliyejiunga mwenyewe na taifa letu, ili tuweze kupita kwa njia yake na yeye kwetu; Mtu fulani ambaye mkono wake wa nguvu umekuwa juu ya sayari hii na atakayeiongoza irudi kwa amani--nabila kukawia.

Lakini miaka nyingi iliyopita kiumbe kimoja cha mambo ya ulimwengu kilichoshawishiwa kilijitahidi kutwaa uongozi wa dunia yetu na kupinga shauri la Mungu kwa furaha ya jamaa lake dunia. Katika usemi wa kueleza vizuri-kwa kweli, maelfu iliyozidishwa wameiita msemo uliopewa uongozi wa Mungu-mwandishi wa kitabu hiki hupasua pazia kwa maelezo hafifu yasiyojulikana na yaliyotolewa kwa woga maarifa ya nguvu hii lakini mtu asiyeonekana ambaye mkono wake umenyooka kushika mamlaka ya dunia yetu. Kwa mahali ya kibinadamu watawala wakishenzi na makanisa ya dini pia wamehatarishwa kama sehemu zenye hatia katika mapatano ya shauri.

Ila tu kwa miaka ya uhuru wa dini ndipo kitabu hiki kiliweza kuchapiwa na kutangazwa zaidi, kwani hukata kwa shida sana katikati ya mojawapo ya makao mengi yanayokuwa na uwezo kuliko, ya siku zetu. Kinasema sababu gani Matengenezo yanahitajiwa, na kwa sababu gani yalisimamishwa; historia ya huzuni ya makanisa ya uasi, ya muungano wa mapatano ya kutesa, wa mapatano ya kizushi ya kanisa na serkali ile itakayotenda sehemu yake ya aibu kabla vita kuu kati ya ubaya na wema kumalizika. Na katika vita hii kila mtu anakuwa mshiriki.

Hapa mwandishi ameandika habari ya vitu ambavyo havikuwako katika siku zake. Ameandika kwa uaminifu juu ya machafuko na vya kuhofisha. Matokeo ya vita ni makubwa sana na miti ya kufungia watu wa kuchomwa moto ni mirefu sana ambayo mtu fulani alipashwa kusema maneno haya ya maonyo na kuyaweka kwa muangaza.

Hakuna msomaji anayegeuza kurasa za kitabu hiki atakaye kiweka chini bila kushang'aa kama ilikuwa zaidi ya bahati iliyomwongoza kwa kukivumbua.

## [iii] Kuinua Pazia Kwa Wakati Ujao

Mbele ya kuingia kwa zambi, Adamu alipendezwa na ushirika wazi na Muumba wake; lakini tangu mtu alipojitenga mwenyewe na Mungu kwa njia ya uasi, taifa la kibinadamu likakatiliwa mbali na bahati hii kubwa. Kwa shauri la ukombozi, walakini, njia ilifunguka ambayo kwayo wakaaji wa dunia wanaweza tena kuwa na uhusiano na Mungu. Mungu aliongea pamoja na watu kwa njia ya Roho yake, na nuru ya kimungu ilitolewa kwa walimwengu kwa njia ya ufunuo kwa watumishi wake wateule. "Watu walisema yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu." 2 Petro 1:21.

Wakati miaka ya kwanza ya 2500 ya historia ya mwanadamu, hapakuwa na ufunuo ulioandikwa. Wale waliokuwa wakifundisha mambo ya Mungu walitoa habari zao kwa wengine, na zilipokelewa kutoka kwa baba na kwa mtoto, hata kwa vizazi vilivyofuatana. Matayarisho ya neno lililoandikwa yalianza kwa wakati wa Musa. Ufunuo ulioongozwa na Mungu ndipo ukapata kuwekwa katika kitabu cha Uongozi wa Mungu. Kazi hii ikaendelea kwa muda mrefu wa miaka 1600-tangu wakati wa Musa mwandishi wa historia ya kuumbwa na sheria, hata kwa wakati wa Yoane, mwandishi wa mambo ya kweli na bora zaidi ya injili.

Biblia huonyesha Mungu kama Mtengenezaji wa kitabu hicho; ingawa kiliandikwa na mikono ya wanadamu; na kwa namna mbalimbali ya vitabu vyenye kuachana huonyesha tabia za waandishi kadha wa kadha. Mambo ya kweli yaliyofunuliwa yote "limepewa kwa maongozi ya Mungu" 2 Timoteo 3:16; lakini yalielezwa katika maneno ya watu. Yeye asiye na mwisho kwa Roho wake Mtakatifu alitoa nuru kwa akili na mioyo ya watumishi wake. Alitoa ndoto na maono, mifano na sanamu; na hao ambao kweli ilifunuliwa kwao wakaweka wao wenyewe wazo katika msemo wa kibinadamu.

Viliandikwa katika nyakati mbalimbali, kwa watu walioachana sana katika cheo na kazi, na katika karama za akili na roho, vitabu vya Biblia vinaonyesha sura pana za kuachana, pia na tofauti katika hali ya vita vinavyonenwa bila kuelezwa. Aina mbambali

ya maelezo yalitumiwa na waandishi mbalimbali; mara kwa mara ukweli huo huo unakuwa wa kushangaza zaidi ulipotolewa na mojawapo kuliko mwengine. Na kwa namna waandishi wengi wanavyo fundisha fundisho kwa mifano mbalimbali na mahusiano, hapo panaweza kutokea, mambo ya juu juu, ya ovyo ovyo, ao msomaji mwenye kupendelea, kuwa tofauti wala mabishano, ambaye mwanafunzi wa heshima, na maoni wazi, hutambua asili ya umoja.

Kama ilivyoonyeshwa kwa watu mbalimbali, ukweli umeletwa [iv]
katika sura zake mbalimbali. Mwandishi mmoja anaweza kutiwa moyo kwa nguvu kwa kipande kimoja cha fundisho; anashika nikta ambazo zinapatana na ujizi wake ao uwezo wake wa kufahamu na shukrani; mwengine hushikilia kwa hali tofauti yake; na kila mmoja, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, hutoa kitu kinachotia moyo kwa nguvu kwa ajili yake mwenyewe-hali mbalimbali ya ukweli katika kila mmoja, lakini umoja kamili katika mambo yote. Na kweli zilizo funuiiwa hujiunga kufanya kitu kizima kamili, kinacholingana kukutana na shida za watu katika mambo yote na ujuzi wa maisha.

Mungu amependezwa kujulisha ukweli wake ulimwenguni kwa njia ya watu wajumbe, naye mwenyewe, kwa njia ya Roho wake Mtakatifu, watu wanaofaa na aliwawezesha kufanya kazi hii. Aliongoza akili katika uchaguzi wa mambo gani ya kusema na mambo gani ya kuandika. Hazina zilikabidhiwa kwa vyombo vya kidunia, lakini ni hivyo, kupana kitu kilichotoka mbinguni. Ushuhuda umetolewa kwa maneno zaifu ya lugha ya kibinadamu, lakini ni ushuhuda wa Mungu; na mtoto mtiifu, mwenye kuamini wa Mungu hushika ndani yake utukufu wa uwezo wa Mungu, amejaa neema na kweli.

Katika Neno lake, Mungu ameweka maarifa yake ya lazima kwa watu kwa wokovu. Maandiko Matakatifu yanafaa kukubaliwa kama ufunuo wenye nguvu, na wenye hakika ya mapenzi yake. Yanakuwa kanuni ao kipeo cha tabia yake, mvumbuaji wa mafundisho ya dini, na jaribu la maarifa. "Kila andiko limepewa kwa pumzi ya Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki; ili mtu wa Mungu awe mukamilifu, ametengenezwa kabisa kwa kila tendo jema." 2 Timoteo 3:16, 17.

Lakini ingawa Mungu amefungua mapenzi yake kwa watu kwa njia ya Neno lake, jambo hili halikufanya jambo lisilotakiwa kwa

kuwako kwake kuendelea na kuongoza kwa Roho Mtakatifu. Kwa kinyume, Roho iliahidiwa na Mwokozi wetu, kwa kufungua Neno kwa watumishi wake, kwa kuangazia na kutumia mafundisho yake. Na kwa sababu ilikuwa Roho ya Mungu iliyoongoza Biblia, haiwezekani kwamba mafundisho ya Roho ilipaswa kuwa kinyume kwa mafundisho ya Neno.

Roho haikutolewa-ama hata kuwekwa-kwa kutangua Biblia; kwa maana Maandiko hueleza wazi wazi kwamba Neno la Mungu ni kipao ambacho mafundisho yote na ujuzi yanapaswa kujaribiwa. Asemavyo mutume Yoane, "Musiamini kila roho, lakini jaribuni
[v] roho, kama zimetoka kwa Mungu; kwa sababu manabii wengi wa uwongo wametokea duniani." 1 Yoane 4:1. Na Isaya husema, "Kwa sheria na kwa ushuhuda! Kama hawasemi sawasawa na neno hili, kweli hapana asubui kwao." Isaya 8:20.

Laumu kubwa liliwekwa juu ya kazi ya Roho Mtakatifu kwa makosa ya aina ya wale, wanaodai mwangaza wake, wanaoungama kuwa na kutokuwa na haja zaidi tena ya uongozi kutoka kwa Neno la Mungu. Wanatawaliwa na maoni ambayo wanayozania kama sauti ya Mungu katika roho. Lakini roho ile inayowaongoza si Roho ya Mungu. Hii kwa kufuata maoni, kwa kutojali Maandiko, kunaweza kuongoza kwa machafuko tu, kwa udanganyifu na maangamizi. Hutumia tu makusudi zaidi ya yule muovu. Hivi kazi ya Roho Mtakatifu inakuwa ya maana sana kwa uzima wa kanisa la Kristo, ni mojawapo kati ya mashauri ya Shetani, kwa njia ya makosa ya wanaozidisha mambo kupita na washupavu kwa kutia zarau juu ya kazi ya Roho na kuletea watu wa Mungu kutojali asili ya nguvu ambayo Bwana wetu Mwenyewe ameitoa.

Katika mapatano pamoja na Neno la Mungu, Roho yake ilikuwa kwa kuendelea kazi yake katika muda wote wa mgawo wa injili. Kwa mda wa miaka wakati Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya yalikuwa yakitolewa, Roho Mtakatifu hakuacha kutoa nuru kwa roho za watu, isipokuwa mafunuo kuwekwa katika Sheria Takatifu. Biblia yenyewe inahubiri namna gani, kwa njia ya Roho Mtakatifu, watu walipokea maonyo, kemeo, shauri, na mafundisho, katika mambo katika kukosa namna kwa kuhatidia kwa kutolewa kwa Maandiko. Manabii walitajwa wa nyakati mbalimbali, ambao maneno yao hakuna yaliyoandikwa. Na kumbukumbu lilifanywa hivyo, baada ya kufungwa kwa sheria ya Maandiko, Roho Mtakatifu

alikuwa wakuendelea kazi yake, kwa kuangazia, kuonya, na kufariji waana wa Mungu.

Yesu aliahidi wanafunzi wake, “Mufariji, Roho Mtakatifu, ambaye Baba atakayemutuma kwa jina langu, yeye atawafundisha ninyi yote, na kuwakumbusha ninyi yote niliyowaambia ninyi.” “Lakini wakati anapokuja yule Roho ya kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli... naye atawatangazia ninyi habari za maneno yatakayokuja.” Yoane 14:26; 16:13. Maandiko yanafundisha wazi wazi kwamba ahadi hizi, hazikuwekewa mpaka kwa siku za mitume tu, zitaenea kwa kanisa la Kristo katika miaka yote. Mwokozi anaahidi wafwasi wake, “Mimi ni pamoja nanyi siku zote hata mwisho wa dunia.” Matayo 28:20. Na Paulo anasema kwamba zawadi na mafunuo ya Roho yaliwekwa katika kanisakwa ukamilifu wa watakatifu, kwa kazi ya hudumu ili mwili wa “Kristo ujengwe; [vi] hata sisi sote tufikie umoja wa imani, na kujua sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu muzima, hata kufika kipimo cha urefu wa utimilifu wa Kristo.” Waefeso 4:12, 13.

Kwa ajili ya waaminifu wa Efeso mtume aliomba, “Ili Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi *Roho ya hekima na wa ufunuo* katika kumjua yeye; *macho ya ufahamu wenu yatiwe nuru* ili mujue tumaini la kuita kwake, ... na *ukubwa wa kupita* wa uwezo wake kwetu tunaoamini.” Waefeso 1:17-19. Kazi ya huduma ya Roho wa Mungu katika kuangazia ufahamu na kufungua roho kwa vitu vingi vya Neno Takatifu la Mungu ilikuwa ndiyo baraka ambao Paulo aliomba sana kwa ajili ya kanisa la Waefeso.

Baada ya mafunuo ao maonyesho ya ajabu ya Roho Mtakatifu kwa Siku ya Pentekote, Petelo akaonya watu kwa ajili ya toba na ubatizo katika jina la Kristo, kwa ondoleo la zambi zao; na alisema: “Nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mtakatifu. Kwa sababu ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu.” Matendo 2:38, 39.

Katika uhusiano na gafula pamoja na tendo za siku kuu ya Mungu, Bwana kwa njia ya nabii Yoeli ameahidi ufunuo wa kipekee wa Roho Mtakatifu. Yoeli 2:28. Unabii huu ulipata sehemu ya utimilizo katika kumiminika kwa Roho siku ya Pentekote; lakini itafikia utimilizo wake kamili katika ufunuo wa neema ya Mungu ambao utafuatana na kufungwa kwa kazi ya injili, vita kuu kati

ya mema na mabaya itaongezeka kwa mkazo kwa mwisho kabisa wa wakati. Katika miaka ya hasira ya Shetani ilionekana juu ya kanisa la Kristo; na Mungu ameweka neema yake na Roho kwa watu wake kwa kuwatia nguvu kusimama kwa kupinga uwezo wa yule muovu. Wakati mitume wa Kristo walipashwa kupeleka injili yake duniani na kuiandika kwa ajili ya miaka yote ijayo, walipata karama ya kipekee ya mwangaza wa Roho. Lakini kwa namna kanisa linapokaribia ukombozi wake wa mwisho, Satana atatumika na uwezo mwingi. Ameshuka chini "mwenye hasira nyingi kwa sababu anajua ana wakati mufupi tu." Ufunuo 12:12. Atatumika "na uwezo wote, na alama na maajabu ya uwongo." 2 Watesalonika 2:9. Kwa miaka 6000 yule mwerevu mara alikuwa juu sana miongoni mwa malaika wa Mungu amegeuka kabisa kwa kazi ya madanganyifu na maangamizi. Na vina vya ustadi wa Shetani na ujanja alioupata, ujanja wote uliositawishwa wakati wa taabu ya miaka italetwa kwa kuchukuliwa juu ya watu wa Mungu katika vita ya
[vii] mwisho. Na katika wakati huu wa hatari wafwasi wa Kristo watapaswa kuchukua duniani maonyo ya kuja kwa mara ya pili kwa Bwana; na watu watapaswa kujitayarisha kusimama mbele yake kwa kuja kwake, "pasipo waa wala laumu." 2 Petro 3:14. Kwa wakati huu matoleo ya kipekee ya neema ya Mungu na uwezo haikose kuhitajiwa kwa kanisa kuliko katika siku za mitume.

Kwa njia ya mwangaza wa Roho Mtakatifu, tendo za vita yenye kuendelea wakati mrefu kati ya mema na mabaya vimefunguliwa kwa mwandishi wa kurasa hizi. Mara kwa mara nimeruhusiwa kutazama matengenezo ama kazi, katika miaka mbali mbali ya maisha, ya vita kuu kati ya Kristo, Mfalme wa uzima, Muumba wa wokovu wetu, na Shetani, mfalme wa uovu, asili ya zambi, muasi wa kwanza wa sheria takatifu ya Mungu. Uadui wa Shetani juu ya Kristo umeonekana juu ya wafuasi wake. Uchuki wa namna moja wa kanuni za sheria ya Mungu, mashauri ya namna moja ya udanganyifu, ambaye kosa limefanyika kuonekana kama kweli, ambaye sheria za kibinadamu zimebadilika kuwa pahali pa sheria ya Mungu, na watu wameongozwa kuabudu kiumbe kuliko Muumba, yapate kuandikwa katika historia yote ya wakati uliopita. Nguvu za Shetani kwa kusingizia tabia ya Mungu, kwa kulazimisha watu kutunza wazo la uongo la Muumba, na hivyo kumzania na hofu na uchuki kuliko kuwa na upendo; juhudi yake kwa kuweka pembeni

sheria ya Mungu, kuongoza watu kufikiri wao wenyewe kuwa na uhuru kwa matakwa yake; na mateso yake ya wale wanaothubutu kupinga hila zake, imefuatiwa kwa bidii sana katika miaka yote ya maisha. Yameweza kuandikwa katika historia ya wazee wakuu (patriarches), manabii, na mitume, ya wafia dini na watengenezaji.

Katika vita kuu ya mwisho, Shetani atatumia maongozi ya namna moja, kuonyesha roho ya namna moja, na kutumikia mwisho wa namna moja kama katika miaka yote iliyotangulia. Kile kilichokuwa, kitakuwa, isipokuwa kwamba taabu itakayokuja itafahamika na mkazo wa kutisha sana ambako dunia haijashuhudia. Madanganyo ya Shetani yatakuwa ya ujanja zaidi, mashambulio yake ya gafula yatakuwa ya makusudi zaidi. Kama ikiwezekana, angeongoza kwa kupoteza wachaguliwa. Marko 13:22.

Namna Roho ya Mungu ilivyofungua roho yangu mambo ya kweli makubwa ya Neno lake, na vitendo vya wakati uliopita na vya wakati ujao, nimeagizwa kujulisha wengine mambo yale yaliyo funiliwa-kwa kuandika historia ya vita katika miaka iliyopita, na hasa zaidi kwa kuitoa kama kutawanya nuru juu ya taabu inayokaribia upesi ya wakati ujao. Kwa kufuata kusudi hili, nimejitahidi kuchagua na kukusanya pamoja mambo katika historia ya kanisa kwa [viii]
namna hii, ili kuandika yasiyo funuliwa ya majaribu makubwa ya kweli ambayo kwa nyakati mbali mbali yametolewa ulimwenguni, yale yaliyoamsha hasira ya Shetani na uadui wa kanisa la upendo wa kidunia, na yale yaliyoshikwa kwa ushuhuda wa wale "wasiopenda maisha yao hata kufa."

Katika kumbusho hizi tunaweza kuona kivuli cha vita mbele yetu. Kwa kuzitazama katika nuru ya Neno la Mungu, na mwangaza wa Roho yake, tunaweza kuona kufunuliwa kwa mashauri ya waovu na hatari wanazopashwa kuepuka yule angeweza kupatikana "bila kuwa na kosa" mbele ya Bwana wakati wa kuja kwake.

Matukio makubwa yaliyoonyesha maendeleo ya matengenezo katika miaka iliyopita yanakuwa mambo ya historia, yanayojulikana sana na kukubaliwa pote na ulimwengu wa Kiprotestanti; yanakuwa hakika ambayo hakuna mtu anaweza kuyakana. Historia hii niliyotolewa kwa kifupi, kwa kupatana na kusudi la kitabu na uchache wa maneno utakaochunguzwa, kweli kwamba kilipunguzwakuwa kidogo kinavyoonekana kwa kulingana sawa na ufahamu kamili wa matumizi yake. Katika mambo mengine mahali msimulizi ameku-

sanya matukio pamoja kama kwa kutoa, kwa kifupi, maoni ya ufahamu wa fundisho, ao maelezo ya muhitasari wa kutaja kila kitu katika namna inayofaa, maneno yake yameingizwa; lakini kwa mara mengine hakuna sifa njema kabisa imetolewa, kwa kuwa mateuzi (quotations) hayakutolewa kwa ajili ya kusudi la kutaja mwandishi yule kuwa mwenye mamlaka, lakini maneno yake hutoa zawadi ya rahisi na ya hodari ya mafundisho. Katika kusumulia maarifa na maoni ya wale wanaoendelea kuchukua kazi ya matengenezo katika wakati wetu wenyewe, matumizi ya namna moja yamefanywa kwa kazi zao za kutangaza.

Si zaidi sana kusudi la kitabu hiki kutoa mambo ya kweli mapya kwa ajili ya taabu za nyakati za kwanza kwa kutoa mambo na kanuni zinazokuwa na sura ya matukio yanayokuja. Kwani inaonekana kama sehemu ya vita kati ya nguvu za nuru na giza, hodari hizi zote za kumbukumbu za wakati uliopita zinaonekana kuwa na maana mpya; na kati yake nuru inatiwa juu ya wakati ujao, kuangazia njia ya wale, wanaopenda watengenezaji (reformateurs) wa miaka iliyopita, wataitwa, hata kwa hatari ya hali njema ya kidunia, kushuhudia "kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo."

[ix] Kwa kueleza tendo za vita kuu kati na ukweli na uongo; kwa kufunua hila za Shetani na makusudi ambayo angeweza kufaulu kushindana nayo; kutoa suluhu la kufanyikiwa kwa shida kuu ya uovu, kugawanya nuru ya namna hiyo juu ya tabia ya asili na ya mwisho ya zambi kama kufanya ufunuo kamili wa haki na wema wa Mungu katika mambo yake yote pamoja na viumbe vyake; na kuonyesha hali takatifu, isiyo badilika ya sheria yake, ndilo lengo la kitabu hiki. Ili kwa mvuto wake roho ziweze kukom'bolewa kutoka kwa uwezo wa giza na kuwa "washiriki wa urithi wa watakatifu katika nuru," kwa sifa ya Yeye aliyetupenda na alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu ni ombi la moyo la mwandishi.

Ellen G. White

# 1 /UNABII WA HALI YA MWICHO WA ULIMWENGU [1]

Kutoka kwa kilele cha Mizeituni, Yesu akatazama juu ya Yerusalema. Mbele ya makutano kulikuwa na majengo mazuri ya hekalu. Kushuka kwa jua kukaangazia weupe wa teluji wa kuta zake za marimari na kumulikia mnara wa zahabu na mnara mrefu mwembamba (Pinnacle). Mtoto gani wa Israeli aliweza kutazama juu ya maajabu haya bila kufurahi sana na kushangaa! Lakini mawazo mengine yalikuwa moyoni mwa Yesu. "Naye alipokaribia, akaona muji, akalia juu yake". Luka 19:41.

Machozi ya Yesu haikuwa kwa ajili yake mwenyewe, ingawa mbele yake kulikuwa Getesemane, mambo ya maumivu makubwa yaliyokaribia, na si mbali sana na, Kalvari, mahali pa kusulubiwa. Lakini haikuwa mambo hayo yaliyotia kivuli juu yake katika saa hii ya furaha. Alilia kwa ajili ya maelfu ya watu wa Yerusalema watakaoangamizwa.

Historia ya zaidi ya miaka elfu ya upendeleo wa kipekee wa Mungu na ulinzi mkubwa, ulifunuliwa kwa watu wachaguliwa, ilifunguliwa kwa macho ya Yesu. Yerusalema uliheshimiwa na Mungu juu ya dunia yote. Bwana "amechagua Sayuni ... kuwa kao lake". Zaburi 132:13. Kwa miaka mingi, manabii watakatifu walikuwa wakitoa ujumbe wa maonyo. Siku kwa siku damu ya wana kondoo ilikuwa ikitolewa, ikionyesha Mwana Kondoo wa Mungu.

Israeli kama taifa angalilinda utii wake kwa Mungu, Yerusalema ungalisimama milele, mchaguliwa wa Mungu. Lakini historia ya wale watu waliopendelezwa ilikuwa habari ya kukufuru na kuasi. Zaidi kuliko upendo wa huruma wa baba, Mungu alikuwa mwenye "huruma kwa watu wake na makao yake". 2 Mambo 36:15. Wakati maombi na makaripio yaliposhindwa, alituma zawadi bora sana ya mbinguni, Mwana wa Mungu Mwenyewe, kwa kutetea pamoja na muji usiotubu wa moyo mgumu.

Kwa miaka mitatu Bwana wa nuru na utukufu alikuwa akiingia na kutoka miongoni mwa watu wake. "Akifanya kazi njema

na kuponyesha wote walioonewa na Shetani". Kuhubiri wokovu kwa wafungwa, na vipofu kupata kuona tena, kuwezesha viwete kutembea, na viziwi kusikia, kutakasa wenye ukoma, kufufua wafu, na kuhubiri Habari Njema kwa masikini. Tazama Matendo 10:38; Luka 4:18; Matayo 11:5.

[2] Mtembezi asiye na makao, aliishi kwa kusaidia wenye mahitaji na kupunguza misiba ya watu, kuwasihi kukubali zawadi ya uzima. Mawimbi ya huruma yaliyopingwa na waie waliokuwa na mioyo migumu, yakarudia na mwendo wa nguvu wa huruma, upendo usioelezeka. Lakini Israeli akamuacha Rafiki wake mwema na Msaidizi wa pekee. Maombezi ya upendo wake yakazarauliwa.

Saa ya tumaini na musamaha ilikuwa ikipita upesi. Wingu lile ambalo lilikuwa likijikusanya katika miaka ya kukufuru na kuasi ilikuwa karibu kupasuka juu ya watu wenye kosa. Yeye ambaye peke yake alipashwa kuwaokoa kwa hatari yao ya kifo amezarauliwa, kutukanwa, kukataliwa, na alikuwa karibu kusulubiwa.

Kristo alipotazama Yerusalema, mwisho wa muji mzima, taifa lote, ulikuwa mbele yake. Alisikia malaika mwangamizi pamoja na upanga ulioinuka juu ya mji ambao ulikuwa kwa wakati mrefu makao ya Mungu. Katika mahali palepale ambapo baadaye pakashikwa na Tito na jeshi lake, akatazama kwa bonde viwanja vitakatifu na mabaraza. Na machozi machoni akaona kuta kuzungukwa na majeshi ya kigeni. Alisikia shindo la jeshi kutembea kwa vita, sauti za wamama na watoto walililia mkate ndani ya muji uliozungukwa. Aliona nyumba yake takatifu, majumba yake na minara, yakitolewa kwa ndimi za moto, fungu la kuharibika lenye kuwaka na kutoka moshi.

Kutazama katika nyakati, aliona watu wa ahadi kutawanyika katika kila inchi, "kama mavunjiko ya merikebu kwa pwani ya ukiwa". Huruma ya Mungu, upendo mkuu, yakapata usemi katika maneno ya kusikitisha: "Ee Yerusalema, unaoua manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kukusanya watoto wako pamoja, kama vile kuku anavyokusanya watoto wake chini ya mabawa yake, lakini ninyi hamukutaka"! Matayo 23:37.

Kristo aliona katika Yerusalema mfano wa ulimwengu uliokazana katika kutoamini na kuasi, ukijiharakisha kwa kukutana na hukumu za kulipiza kisasi cha Mungu. Moyo wake ukashikwa

na huruma kwa ajili ya waliohuzunishwa na walioteswa na dunia. Alitamani sana kuwafariji wote. Alitaka kutoa roho yake kwa kifo kwa kuleta wokovu karibu nao.

Mtukufu wa mbinguni katika machozi! Mambo ile huonesha namna gani ni vigumu kuokoa mwenye kosa kwamatokeo ya kuharibu sheria ya Mungu. Yesu aliona ulimwengu kujitia katika madanganyo kama yale ambayo yalileta uharibifu wa Yerusalema. Zambi kubwa ya Wayahudi ilikuwa ni kukataa Kristo; zambi kubwa ya ulimwengu ingekuwa kukataa sheria ya Mungu, msingi wa serekali yake katika mbingu na dunia. Mamilioni katika utumwa wa [3]
zambi,ambao watahukumiwa kwa mauti ya pili, waliweza kukataa kusikiliza maneno ya kweli katika siku yao ya hukumu.

## Uharibifu wa Hekalu Tukufu

Siku mbili kabla ya Pasaka, Kristo akaenda tena na wanafunzi wake kwa mlima wa Mizeituni kutazama mji. Mara moja tena akatazama hekalu katika fahari ya kungaa kwake, taji la uzuri. Solomono, aliyekuwa mwenye busara kuliko wafalme wa Israeli, alimaliza hekalu la kwanza, jengo nzuri kuliko ambalo dunia haijaona. Baada ya maangamizi yake kwa Nebukadneza, ikajengwa tena karibu miaka mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Lakini hekalu la pili halikulingana na la kwanza katika uzuri. Hakuna wingu la utukufu, hakuna moto kutoka mbinguni, ulioshuka juu ya mazabahu yake. Sanduku, kiti cha rehema, na meza ya ushuhuda havikupatikana pale. Hakuna sauti kutoka mbinguni iliyojulisha kuhani mapenzi ya Mungu. Hekalu la pili halikutukuzwa na wingu la utukufu wa Mungu, lakini lilitukuzwa na kuwako kwa uhai kwa yule ambaye alikuwa Mungu mwenyewe katika mwili. "Mapenzi ya mataifa yote" yalikuja kwa hekalu lake wakati Mtu wa Nazareti alipofundisha na kuponyesha katika viwanja takatifu. Lakini Israeli alikataa zawadi ya matoleo ya mbinguni. Pamoja na Mwalimu mnyenyekevu aliyepita kutoka kwa mlango wake wa zahabu siku ile, utukufu ukatoka hata milele kwa hekalu. Maneno ya Mwokozi yalitimia: "Nyumba yenu imeachwa kwenu tupu". Matayo 23:38.

Wanafunzi walishangazwa sana kwa utabiri wa Kristo wa maangamizi ya hekalu, na walitamani kufahamu maana ya maneno

yake. Herode Mkubwa alitoa kwa ukarimu juu ya hekalu hazina za Waroma na Wayahudi. Vipande vikubwa vya marimari nyeupe, vilipelekwa kutoka Roma, vikafanya sehemu ya ujenzi wake. Kwa mambo haya wanafunzi waliita uangalifu wa Bwana wao, kusema: “Tazama mawe na majengo haya”! Marko 13:1.

Yesu akatoa jibu la wazi na la kushitusha: kweli ninawambia ninyi, Halitabaki jiwe juu ya jiwe pasipo kubomolewa”. Matayo 24:2. Bwana aliwaambia wanafunzi kwamba atakuja mara ya pili. Kwa hiyo, alipotaja hukumu juu ya Yerusalema, mafikara yao yakarejea kwa kurudi, na wakauliza: “Maneno haya yote yatakuwa wakati gani? na nini alama ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia”? Matayo 24:3.

Kristo akaonyesha mbele yao ishara ya mambo makubwa ya kuonekana kabla ya kufungwa kwa wakati. Unabii alioutaja ulikuwa
[4] na sehemu mbili maana yake. Wakati ulipokuwa ukitabiri uharibifu wa Yerusalema, unabii huu ulionyesha pia mfano wa matisho ya siku kubwa ya mwisho.

Hukumu zilipashwa kuwekwa juu ya Israeli kwa sababu walikataa na wakasulubisha Masiya. “Basi wakati munapoona chukizo la uharibifu lililosemwa na Danieli nabii, likisimama kwa pahali patakatifu (yeye anayesoma afahamu), halafu wale walio katika Yudea wakimbie kwa milima”. Matayo 24:15,16. Tazama vile vile Luka 21:20,21. Wakati kawaida za kuabudu sanamu za Waroma zitakapo wekwa katika kiwanja kitakatifu inje ya kuta za mji, ndipo wafuasi wa Kristo watapashwa kutafuta usalama katika kukimbia. Wale watakao okoka hawapashwe kuchelewa. Kwa ajili ya zambi zake, hasira ilikwisha kutajwa juu ya Yerusalema. Ugumu wa kuto kuamini kwake ulifanya maangamizo yake ya kweli. Tazama Mika 3:9-11.

Wakaaji wa Yerusalema walimshitaki Kristo kwa chanzo cha taabu zote ambazo zilifika juu yao katika matokeo ya zambi zao. Ingawa walimjua yeye kuwa bila kosa, wakatangaza kifo chake kuwa cha lazima kwa ajili ya salama yao kama taifa. Wakapatana katika maamuzi ya kuhani wao mkuu kwamba inafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu wote, wala taifa lote lisiangamie. Tazama Yoane 11:4753.

Wakati waliua Mwokozi wao kwa sababu alikemea zambi zao, wakajizania wao wenyewe kama watu waliopendelewa na Mungu na kutumainia Bwana kuwakomboa kwa adui zao!

## Uvumilivu wa Mungu

Karibu miaka makumi ine Bwana alikawisha hukumu zake. Kulikuwa kungali Wayahudi, wajinga ambao hawakujua tabia na kazi ya Kristo. Na watoto hawakufurahia nuru ambayo wazazi wao waliikataa kwa zarau katika mahubiri ya mitume, Mungu aliwezesha nuru kuangaza juu yao. Waliona namna gani unabii ulitimia, si katika kuzaliwa tu na maisha ya Kristo, bali katika kifo chake na ufufuo. Watoto hawakuhukumiwa kwa ajili ya zambi za wazazi; lakini wakati walipokataa nuru ingine waliopewa, wakawa washiriki wa zambi za wazazi na wakajaza kipimo cha uovu wao.

Wayahudi katika ugumu wa mioyo yao wakakataa shauri la mwisho la rehema. Ndipo Mungu akaondoa ulinzi wake kwao. Taifa likaachwa kwa utawala wa mwongozi lililo mchagua. Shetani akaamsha tamaa kali sana na mbaya kuliko za roho. Watu wakakosa akili wakatawaliwa na nguvu na hasira ya upofu, ya [5]
shetani katika ukaidi wao. Marafiki na ndugu wakasalitiana wao kwa wao. Wazazi wakaua watoto wao, na watoto wazazi wao. Watawala hawakuwa na uwezo wa kujitawala wao wenyewe. Tamaa ikawafanya kuwa wajeuri. Wayahudi wakakubali ushuhuda wa uwongo kwa kuhukumu Mwana wa Mungu asiye na kosa. Sasa mashitaki ya uwongo yakafanya maisha yao kuwa si ya haki. Kuogopa Mungu hakukuwashitusha tena. Shetani alikuwa akiongoza taifa.

Waongozi wa makundi ya upinzani wakaanguka mmoja juu za mwingine na kuwa bila huruma. Hata utakatifu wa hekalu haukuweza kuzuia ukali wao wa kutisha. Mahali patakatifu pakanajisiwa na miili ya waliouawa. Lakini washawishi wa kazi hii ya kishetani walitangaza kwamba hawakuwa na hofu yo yote kwamba Yerusalema ingeharibiwa! Ulikuwa mji wa Mungu. Hata wakati majeshi ya Waroma walipozunguka hekalu, makundi yalisimama imara kwa wazo kwamba Aliye juu angejitia kati kwa kushinda kwa maadui wao. Lakini Israeli alitupia mbali ulinzi wa Mungu, na sasa hakuwa na ulinzi.

## Alama za Musiba

Unabii uliyotolewa na Kristo kwa ajili ya uharibifu wa Yerusalema yalitimia wazi wazi. Dalili na maajabu yalitokea. Kwa muda wa miaka saba mtu aliendelea kupanda na kutelemuka katika njia za Yerusalema, kutangaza misiba itakayokuja. Kiumbe hiki cha ajabu kilifungwa gerezani na kuazibiwa, lakini kwa matusi mabaya hayo akajibu tu, "Ole, ole kwa Yerusalema"! Aliuawa katika mitego ya maadui aliyotabiri.

"Hakuna Mkristo hata mmoja aliyeangamia katika uharibifu wa Yerusalema. Baada ya Waroma chini ya uongozi wa Cestius walipozunguka mji, kwa gafula wakaacha mazingiwa wakati kila kitu kilionekana kuwa cha kufaa kwa shambulio. Mkuu wa Roma akaondoa majeshi yake bila sababu ndogo wazi. Alama iliyoahidiwa ilitolewa kwa Wakristo waliokuwa wakingojea. Luka 21:20,21.

Mambo yakafanyika kwa namna ambayo hata Wayahudi ama Waroma hawakupinga kukimbia kwa Wakristo. Katika kushindwa kwa Cestius, Wayahudi wakafuata, na wakati majeshi hayo mawili yalipokutana, Wakristo popote katika inchi waliweza kufanya kimbilio lao bila kusumbuliwa mahali pa salama, kwa mji wa Pella.

Majeshi ya Wayahudi, yalipokuwa yakifuata Cestius na jeshi lake wakaangukia upande wao wa nyuma. Ni kwa shida sana
[6] Waroma walifaulu katika kukimbia kwao. Wayahudi pamoja na mateka yao wakarudia na ushindi Yerusalema. Lakini kufaulu kwa namna hii kuliwaletea ubaya tu. Jambo hilo liliwasukuma kwa ile roho ya ukaidi wa kupinga kwa Waroma ambao kwa upesi wakaleta msiba mubaya sana juu ya muji uliohukumiwa.

Hasara zilikuwa za ajabu zile zilianguka juu ya Yerusalema wakati mji ulizungukwa tena na Titus. Mji ulizungukwa wakati wa Pasaka, wakati mamilioni ya Wayahudi walipokusanyika ndani ya kuta zake. Duka za akiba zikaharibiwa kwanza kwa ajili ya kisasi cha makundi ya mabishano. sasa matisho yote ya njaa yakawafikia. Wanaume wakatafuna ngozi ya mikaba yao na viatu na kifuniko cha ngao zao. Hesabu kubwa ya watu wakaenda kwa uficho usiku inje kwa kukusanya mimea fulani ya pori yaliyokuwa yakiota inje ya kuta za mji, ingawa wengi walikuwa wakizunguukwa na kuuawa na mateso makali, na mara kwa mara wale waliokuwa wakirudia katika usalama ndani ya mji walinyanganywa akiba walizopata kwa shida

sana. Waume wakaiba wake wao, na wake waume wao. Watoto wakanyanganya chakula kinywani mwa wazazi wazee wao.

Waongozi wa Roma kuogopesha sana Wayuda iliwakubali wameshindwa. Wafungwa waliazibiwa, kuteswa, na kusulubiwa mbele ya ukuta wa mji. Kwa bonde la Yosafati na Kalvari, misalaba ikasimamishwa kwa wingi sana. Ilikuwa vigumu kupitia katikati ya misalaba hiyo. Ndivyo lilivyo timilika agizo la kutisha lililotajwa na Wayahudi mbele ya kiti cha hukumu cha Pilato: "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu". Matayo 27:25.

Tito alijazwa na hofu kuu alipoona miili ya wafu kulala kwa malundo katika mabonde. Kama mtu aliye katika maonyo, akatazama hekalu nzuri na akatoa agizo kwamba kusiwe hata jiwe moja lake linalopaswa kuguswa.. Akatoa mwito wa nguvu kwa waongozi wa Wayahudi wasimulazimishe kuchafua mahali patakatifu kwa damu. Kama wakiweza kupigania mahali po pote pengine, hapana Muroma atapashwa kutendea jeuri utakatifu wa hekalu! Yosefu mwenyewe, aliwasihi, akawaomba kujitoa, kwa kujiokoa wenyewe, mji wao na mahali pao pa ibada. Lakini maneno yake yakajibiwa kwa laana chungu. Mishale ya makelele ikatupwa kwake, mwombezi wao wa mwisho wa kibinadamu. Juhudi za Tito ili kuokoa hekalu zilikuwa bure. Mmoja aliyekuwa mkuu kuliko yeye alitangaza kwamba halitabaki jiwe juu ya jiwe pasipo kubomolewa.

Mwishowe Tito akaamua kukamata hekalu kwa gafula, akakusudia kwamba ikiwezekana ilipaswa kuokolewa kwa maangamizi.
Lakini maagizo yake hayakujaliwa. Kinga cha moto kikatupwa [7]
upesi na askari mmoja kwa tundu ndani ya ukumbi, na mara moja vyumba vilivyokuwa na miti ya mierezi kuzunguuka hekalu takatifu vikawaka moto. Tito akaenda kwa haraka mahali pale, na akaagiza waaskari kuzima ndimi za moto. Maneno yake hayakufuatwa. Katika hasira yao waaskari wakatupa vinga vya moto ndani ya vyumba vya karibu na hekalu, na tena pamoja na panga zao wakaua hesabu kubwa ya wale waliokimbilia ndani ya Pahali patakatifu. Damu ikatiririka kama maji juu ya vipandio vya hekalu.

Baada ya kuangamizwa kwa hekalu, mara mji wote ukawa mikononi mwa Waroma. Waongozi wa Wayahudi wakaacha minara yao isiyoshindika. Alipokwisha kuitazama na mshangao, akasema kwamba ni Mungu mwenyewe aliyeitoa mikononi mwake; kwani hakuna mashini za vita, hata zenye nguvu, zingeweza kushinda

minara kubwa sana. Mji pamoja na hekalu vilibomolewa tangu msingi, na mahali ambapo nyumba takatifu ilikuwa imesimama "palilimwa kama shamba linavyolimwa" Yeremia 26:18. Zaidi ya milioni wakaangamia; waliookoka wakapelekwa kama mateka, wakauzishwa kama watumwa, wakakokotwa chini hata Roma, wakatupwa kwa wanyama wa pori ndani ya viwanda vya michezo, ao kutawanywa mahali pote kama watembezi wasio na makao.

Wayahudi walijaza wao wenyewe kikombe cha kisasi. Kuangamizwa kwa taifa lao na mabaya yote yaliyofuata kutawanyika kwao, ilikuwa ndiyo kuvuna mavuno ambayo mikono yao yenyewe ilipanda "O, Israel, umejiharibu wewe mwenyewe "kwa maana umeanguka sababu ya uovu wako". Hosea 13:9; 14:1. Mateso yao yanaonyeshwa mara kwa mara kama azabu iliwafikia ya hukumu ya Mungu. Ni kwa sababu hiyo mdanganyi mkuu hujitahidi kuficha kazi yake mwenyewe. Kwa kukataa sababu ya hukumu kwa upendo wa Mungu na rehema, Wayahudi walilazimisha ulinzi wa Mungu kuondolewa kwao.

Hatuwezi kujua namna gani tunapashwa kushukuru Kristo kwa ajili ya amani na ulinzi tunaofurahia. Ni nguvu ya Mungu inayozuia wanadamu kuanguka kabisa katika mikono ya Shetani. Waasi na wasio na shukrani wanakuwa na sababu kubwa ya kushukuru Mungu kwa ajili ya rehema yake. Lakini wakati watu wanapo pitisha mipaka ya uvumilivu wa Mungu, ulinzi huondolewa. Mungu hasimame kama mwuaji wa mhukumu juu ya kosa. Huacha wanaokataa rehema zake kuvuna walichopanda. Kila mushale wa nuru uliokataliwa ni mbegu iliyopandwa inayozaa lazima mavuno yake. Roho ya Mungu, ikipingwa kwa bidii, mwishowe itaondolewa. Kwa hiyo, hakuna
[8] tena nguvu ya kuzuia tamaa mbaya za roho, hakuna ulinzi kwa uovu na uadui wa Shetani.

Uharibifu wa Yerusalema ni onyo la kutisha kwa wote wanaopinga maombezi ya rehema za Mungu. Unabii wa Mwokozi juu ya hukumu ya Yerusalema inakuwa na utimilizo mwengine. Katika hukumu ya mji muchaguliwa tunaona maangamizo ya ulimwengu ambao ulikataa rehema za Mungu na kukanyaga sheria yake. Habari ya shida ya mwanadamu ambayo dunia imeshuhudia ni ya giza. Matokeo ya kukataa mamlaka ya Mungu ni ya kuogopesha. Lakini mambo ya giza zaidi yanaonyeshwa katika ufunuo ya wakati ujao. Wakati ulinzi wa Roho ya Mungu utaondolewa kabisa,

haitawezekana tena kuzuia kuripuka kwa tamaa ya kibinadamu na hasira ya uovu, ulimwengu utashika, kwa namna isivyofanyika mbele, matokeo ya mamlaka ya Shetani.

Katika siku ile, kama katika uharibifu wa Yerusalema, watu wa Mungu watakombolewa. Tazama lsaya 4:3; Matayo 24:30,31. Kristo atakuja mara ya pili kukusanya waaminifu wake kwake mwenyewe. “Halafu kabila zote; na mataifa yote ya dunia yataomboleza, nao watamuona Mwana wa watu akija katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa. Naye atatuma malaika zake na sauti kubwa ya baragumu, nao watakusanya wachaguliwa wake toka pepo ine, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho ule”. Matayo 24:30,31.

Watu wajihazari ili wasizarau maneno ya Kristo. Kama alivyoonya wanafunzi wake juu ya uharibifu wa Yerusalema ili wapate kukimbia, vile vile ameonya watu juu ya siku ya uharibifu wa mwisho. Wote watakao wapate kukimbia hasira ijao. “Na kutakuwa alama katika jua na mwezi, na nyota; na katika dunia taabu ya mataifa”. Luka 21:25. Tazama vile vile Matayo 24:29; Marko 13:24-26; Ufunuo 6:12-17. “Basi angalieni”, ndiyo maneno ya Kristo ya onyo la upole. Marko 13:35. Wale wanaokubali onyo hili hawataachwa gizani.

Ulimwengu hauko tayari zaidi kusadiki (amini) ujumbe kwa wakati huu kuliko walivyokuwa Wayahudi kwa kupokea onyo la Mwokozi juu ya Yerusalema. Njoo ingalipo wakati, siku ya Mungu itakuja gafula kwa waovu. Wakati maisha inapoendelea katika mviringo wake wa siku zote; wakati watu wanaposhugulika katika anasa, katika kazi, katika kukusanya pesa; wakati waongozi wa dini wanapotukuza maendeleo ya dunia, na watu wanapotulizwa katika salama ya uwongo-ndipo, kama mwizi wa usiku wa manane huiba kwa gafula, ndivyo uharibifu utakuja kwa gafula juu ya wazarau na waovu, “wala hawatakimbia”. Tazama 1 Watesalonika 5:2-5.

[9] ## 2 /WAKRISTO WA KWANZA -WAAMINIFU NA WA KWELI

Yesu alifunulia wanafunzi wake maarifa ya watu wake tangu wakati ambao alipaswa kuchukuliwa kutoka kwao, hata kurudi kwake katika uwezo na utukufu. Kuingia ndani sana ya wakati ujao, jicho lake likaona zoruba kali zilipaswa kupiga juu ya wafuasi wake kwa miaka iliyokuwa karibu ya mateso. Tazama Matayo 24:9,21,22. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kupitia kwa njia ya namna moja ya laumu na mateso ambayo Bwana wao alipitia. Uadui juu ya Mkombozi wa ulimwengu ulipaswa kuonekana juu ya wote wanaopaswa kuamini jina lake.

Upagani ulifahamu kwamba injili ikishinda, hekalu na mazabahu zake yalipaswa kuondolewa; kwa sababu hii mioto ya mateso ikawashwa. Wakristo walinyanganywa mali zao na kufukuzwa nyumbani mwao. Hesabu kubwa ya wenye cheo na watumwa, watajiri na masikini, wenye elimu na wajinga, waliuawa bila huruma.

Ya kianzia chini ya utawala wa Nero, mateso yakaendelea kwa karne nyingi. Wakristo walitangazwa kwa uongo kuwa ni wao walioleta njaa, tauni, na matetemeko ya inchi. Wachongezi wakasimama tayari, kwa ajili ya faida tu, kwa kusaliti wasio na kosa kama waasi na tauni kwa jamii. Hesabu kubwa wakatupwa kwa nyama wa pori ama kuchomwa wahai katika viwanja vya michezo (amphitheatres). Wengine wakasulubiwa; wengine wakafunikwa na ngozi za nyama wa pori na kusukumwa kwa nguvu katika uwanja (arena) wa kuchezea ili kupasuliwa kwa waimbwa. Kwa siku kuu za wote makutano mengi sana yalikusanyika kwa kufurahisha macho na kusalimia walioumizwa kwa kifo na kuwachekeleya na kushangilia.

Wafuasi wa Kristo walilazimishwa kutafuta maficho katika mahali pa ukiwa na pekee. Chini ya milima inje ya muji wa Roma, vyumba virefu vilifunuliwa katika inchi na miamba kwa maelfu ngambo ya pili ya kuta za mji. Ndani ya makimbilio haya ya chini ya udongo wafuasi wa Kristo wakazika wafu wao, na hapo pia walipaswa kukimbilia, walipozaniwa maovu na kugombezwa, walipata

makao. Wengi wakakumbuka maneno ya Bwana wao, kwamba kama wakiteseka kwa ajili ya Kristo, inafaa wafurahi sana. Zawadi yao itakuwa kubwa mbinguni, kwa maana ndivyo walivyotesa manabii waliokuwa mbele yao. Tazama Matayo 5:11,12.

Nyimbo za ushindi zikapanda katikati ya ndimi za moto zenye [10]
kutatarika. Kwa imani waliona Kristo na malaika wakiwatazama pamoja na usikizi mwingi sana na kutazama kusimama imara kwao pamoja na kibali. Sauti ikaja kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu: "Uwe mwaminifu mpaka kufa, nami nitakupa taji ya uzima". Ufunuo 2:10.

Nguvu za Shetani kwa kuharibu kanisa la Kristo kwa mauaji zilikuwa bure. Watumishi wa Mungu waliuawa, lakini injili iliendelea kutawanyika na wafuasi wake kuongezeka. Mkristo mmoja akasema: "Tunazidi kuongezeka kwa hesabu namna munavyozidi kutuuwa, damu ya Wakristo ni mbegu".

Shetani basi, ili aweze kushinda Mungu alikata shauri ya kusimamisha mwenge wake ndani ya kanisa la Kristo, ili apate ujanja kile alichoshindwa kupata kwa nguvu. Mateso yakakoma. Kwa mahali pake kukawekwa mvuto wa mafanyikio ya kidunia heshima za muda. Waabudu sanamu wakaongozwa kupokea sehemu ya imani ya kikristo, wakikataa mambo ya ukweli yaliyo ya maana . Wakatangaza kumkubali Yesu kama Mwana wa Mungu na kuamini kufa na kufufuka kwake, lakini bila kukubali hali yao ya zambi, na hawakusikia lazima ya kuungama au badiliko la moyo waweze kuungana katika mafikara ya imani katika Kristo.

Sasa kanisa lilikuwa katika hofu ya maangamizo. Kifungo, mateso, moto, na upanga vilikuwa ni mibaraka kwa kulinganisha pamoja na jambo hili. Baadhi ya Wakristo walisimama imara, kutangaza kwamba haikupasa kufanya mapatano. Wengine walikubali kugeuza imani yao. Chini ya vazi ya kondoo ya ukristo unaodaiwa, Shetani alikuwa akijificha yeye mwenyewe ndani ya kanisa, kwa kuchafua au kuharibu imani yao.

Wakristo wengi mwishowe walikubali kushusha kanuni ya imani yao. Na umoja ukafanyika kati ya ukristo na upagani. Ingawa waabudu sanamu walijifanya kuwa washiriki wa makanisa walizidi kujiunga kwa ibada ya sanamu zao, ila tu wakageuza vyombo vya ibada yao kwa sanamu za Yesu, na hata za Maria na watakatifu. Mafundisho mabaya, kawaida za kuabudu mambo ya uchawi, na

sherehe za ibada ya sanamu zikaunganishwa katika imani ya kanisa na ibada. Dini ya Kikristo ikaharibika, na kanisa likapoteza utakatifu (usafi) na uwezo wake. Wengine lakini, hawakudanganyika. Waliendelea kushika uaminifu wao kwa Muumba wa ukweli.

## [11] Makundi Mawili ndani ya Kanisa

Kulikuwa makundi mawili miongoni mwa wale waliojidai kuwa wafuasi wa Kristo. Wakati kundi moja lilijifunza maisha ya Mwokozi na kwa uangalifu wakatafuta kuhakikisha makosa yao na kufuata Mfano, kundi lingine likaepuka mambo ya kweli wazi wazi yaliyofunua makosa yao. Hata katika hali yake bora, washiriki wa kanisa wote hawakuwa wa kweli, safi, na amini. Yuda aliunganishwa na wanafunzi, ili kwa njia ya mafundisho na mifano ya Yesu angeweza kugeuka kwa kuona makosa yake. Lakini kwa upendeleo katika zambi akaalika majaribu ya Shetani. Akakasirika wakati makosa yake yalihakikishwa na ndipo akaongozwa kusaliti Bwana wake. Tazama Marko 14:10,11.

Anania na Safira wakajidai kutoa kafara kamili kwa Mungu wakati walizuia kwa tamaa sehemu kwa ajili yao wenyewe. Roho wa ukweli akafunua kwa mitume tabia ya kweli ya wajanja hawa, na hukumu za Mungu zikaokoa kanisa kwa laumu mbaya kwa usafi wake. Tazama Matendo 5:1-11. Mateso yalipokuja juu ya wafuasi wa Kristo, wale tu waliotaka kuacha vyote kwa ajili ya ukweli walitamani kuwa wanafunzi wake. Lakini kwa vile mateso yalipokoma, waongofu waliongezeka wasiokuwa wa kweli, na njia ikafunguliwa kwa ajili ya Shetani kupata pa kuwekea mguu.

Wakati Wakristo walipokubali kujiunga pamoja na wale waliogeuka kwa nusu tu kutoka katika ushenzi, Shetani akashangilia. Ndipo akawatia moyo kutesa wale waliodumu kuwa waaminifu kwa Mungu. Wakristo hawa wakufuru (waasi), walipoungana na wenzao nusu wapagani wakaelekeza vita yao juu ya mambo ya kanuni (zaidi) ya mafundisho ya Kristo. Ilitakiwa shindano kali sana kusimama imara juu ya madanganyo na machukizo yaliyoingizwa kanisani. Biblia haikukubaliwa kuwa msingi wa imani. Mafundisho ya uhuru wa dini yakaitwa uwongo, na watetezi wake wakaondolewa.

Baada ya mapigano marefu, waaminifu waliona kwamba mutengano ulikuwa wa lazima kabisa. Hawakusubutu kuvumilia

wakati mrefu zaidi makosa yaliyokuwa hatari kwa roho zao, na kufanya mfano mbaya ungaliweza kuhatarisha imani ya watoto wao na watoto wa watoto wao. Waliona kwamba amani ingepatikana kwa bei kali sana kwa kafara ya kanuni. Kama umoja ungalifanyiwa tu kwa kuvunja ukweli, heri tofauti iwepo, na hata vita.

Wakristo wa kwanza walikuwa kweli watu wa kipekee. Wachache katika hesabu, bila utajiri, cheo, wala majina ya heshima, walikuwa wakichukiwa na waovu, hata kama vile Abeli alivyochukiwa na Kaini. Tazama Mwanzo 4:1-10. Tangu siku za Kristo [12]
hata sasa, wanafunzi wake waaminifu wameamsha chuki na upinzani wa wale wanaopenda zambi.

Namna gani, basi, injili inaweza kuitwa habari ya amani? Malaika waliimba kwa uwanja wa Betelehemu: "Utukufu kwa Mungu aliye juu, na salama duniani, katika watu wanaomupendeza". Luka 2:14. Kwa inje hapo kuna kinyume kati ya maneno ya unabii huu na maneno ya Kristo: "Sikuja kuleta salama lakini upanga". Matayo 10:34. Lakini yanafahamika vizuri, maneno haya mawili yanapatana vizuri kabisa. Injili ni ujumbe wa amani. Dini ya Kristo, ikikubaliwa na kutii, ingeeneza amani na furaha duniani pote. Ilikuwa kazi ya Yesu kupatanisha watu kwa Mungu, na kwa mtu kwa mwenzake. Lakini ulimwengu wote unakuwa katika utawala wa Shetani, adui mkali wa Kristo. Injili huonyesha kanuni za maisha kuwa zinazokuwa kinyume cha tabia na mapenzi yao, nazo zinapinga injili yake. Huchukia usafi unaofunua na kuhukumu zambi zao, na hutesa na kuangamiza wale wanaotangaza haki na utakatifu. Ni kwa maana hii kwamba injili huitwa upanga. Tazama Matayo 10:34.

Wengi wanaokuwa wazaifu katika imani wanakuwa tayari kuacha tumaini lao katika Mungu kwa sababu anakubali watu waovu kusitawi, wakati watu wema na safi wanapoteseka na uwezo wa ukali wao. Swali, namna gani, Mungu mwenye haki na rehema, ambaye uwezo wake hauna mwisho, anaweza kukubali uzalimu na mateso ya namna hiyo? Mungu ametupa ushuhuda wa kutosha wa upendo wake. Hatuwezi kuwa na mashaka juu ya wema wake kwani hatuwezi kufahamu maongozi yake. Mwokozi alisema, "Kumbukeni neno nililowaambia ninyi: Mtumwa si mkubwa kuliko Bwana yake. Kama walinitesa mimi, watawatesa ninyi vile vile". Yoane 15:20.

Wale wanaoitwa kwa kuvumilia mateso na mauti ya wafia dini wanapaswa kutembea kwa nyayo za Mwana mpendwa wa Mungu.

Wenye haki huwekwa katika tanuru ya taabu ili wao wenyewe wapate kutakaswa, ili mfano wao upate kuvuta wengine kwa haki ya imani na wema, na kwamba mwenendo wa uaminifu wao upate kuhukumu waovu na wasioamini. Mungu huruhusu waovu kusitawi na kufunua uadui wao juu yake ili wote wapate kuona haki yake na rehema zake katika uharibifu wao kabisa. Kiia tendo la ukali juu ya waaminifu wa Mungu litaazibiwa kama kwamba lilitendewa Kristo mwenyewe.

Paulo anasema kwamba "wote wanaotaka kuishi maisha ya utawa katika Kristo watapata mateso". 2 Timoteo 3:12. Sababu gani, basi, kwamba mateso huonekana yamesinzia? Sababu moja
[13] tu kwamba kanisa lilijiweka kwa kawaida ya kidunia na kwa hivyo haliamushi tena upinzani. Dini katika siku zetu si safi kama imani takatifu ya Kristo na mitume wake. Kwa sababu mambo ya kweli ya Neno la Mungu yanazaniwa kwa ubaridi, kwa sababu kunakuwa utawa kidogo sana katika kanisa, Ukristo unapendwa na watu wote. Acha imani ya kanisa la kwanza ifufuke, na mioto ya mateso itawashwa tena.

# 3 /GIZA LA KIROYO KATIKA KANISA LA KWANZA [14]

Mtume Paulo alisema kwamba siku ya Kristo haingepaswa kuja "ila maasi yale yafike mbele, na mtu yule wa kuasi akafunuliwe, mwana wa uharibifu, yeye mpinzani na kujionyesha mwenyewe juu ya yote yanayoitwa Mungu ao kuabudiwa, hata kuketi ndani ya hekalu la Mungu akijionyesha mwenyewe kama yeye ndiye Mungu". Na zaidi, "Maana siri ya uasi hata sasa inatenda kazi". 2 Watesalonika 2:3,4,7. Hata kwa tarehe ile ya mwanzo mtume aliona, makosa kuingia kimya polepole, yale yangetayarisha njia kwa ajili ya Kanisa la Kipapa.

Pole pole, "siri ya uasi" ikaendesha kazi yake ya Kudanganya. Desturi za kipagani zikapata njia zao katika kanisa la Kikristo, zilipozuiwa wakati wa mateso makali chini ya upagani; lakini wakati mateso yalipokoma, ukristo ukaweka kando unyenyekevu wa Kristo kwa ajili ya fahari ya mapadri wa kipagani na watawala. Kugeuka kwa jina tu kwa Constantini ukaleta furaha kubwa. Sasa kazi ya maovu ikaendelea kwa upesi. Upagani, ulionekana kushindwa kabisa.. Mafundisho yake na mambo ya uchawi yakaingia katika imani ya waliojidai kuwa wafuasi wa Kristo.

Mapatano haya kati ya upagani na ukristo yakatokea katika "mutu wa zambi" aliyetabiriwa katika unabii. Dini ile ya uwongo kazi bora ya Shetani, juhudi yake kwa kukaa mwenyewe juu ya kiti cha ufalme kwa kutawala dunia kufuatana na mapenzi yake.

Ni mojawapo ya mafundisho ya Kiroma ya msingi kwamba Papa amepewa mamlaka kuu juu ya maaskofu na wachungaji (pasteurs) katika ulimwengu wote. Zaidi ya jambo hili ameitwa "Bwana Mungu Papa" na ametangaziwa kuwa asiyeweza kukosa. (Tazama Mwisho wa Kitabu (Nyongezo)) Madai ya namna moja yallazimishwa na Shetani katika jangwa la majaribu yangali yakiendeshwa naye kati ya Kanisa la Kirumi, na hesabu kubwa wanamtolea heshima kubwa.

Lakini wale wanaoheshimu Mungu wanapigana majivuno haya kama vile Kristo alipambana na adui mwerevu: “Utaabudu Bwana Mungu wako,yeye peke utamutumikia”. Luka 4:8. Mungu hakuagiza kamwe mtu ye yote kuwa kichwa cha kanisa. Utawala wa kipapa unakuwa kinyume kabisa na Maandiko. Papa hawezi kuwa na mamlaka juu ya Kanisa la Kristo isipokuwa kwa njia ya kunyanganya. Warumi huleta juu ya Waprotestanti madai ya kwamba kwa mapenzi
[15] yao walijitenga kwa kanisa la kweli. Lakini ni wao waliacha “imani waliyopewa watakatifu mara moja tu”. Yuda 3.

Shetani alijua vizuri kwamba ilikuwa kwa Maandiko matakatifu ambayo Mwokozi alishindana na mashambulio yake. Kwa kila shambulio, Kristo alionyesha ngabo ya kweli ya milele, kusema, “Imeandikwa”. Kwa kudumisha uwezo wa utawala wake juu ya watu na kuanzisha mamlaka ya Papa munyanganyi, anapaswa kuendelea kufunga, watu katika kutojua Maandiko matakatifu. Mambo ya kweli matakatifu yake yalipaswa kufichwa na komeshwa. Kwa mda wa miaka mamia ya uenezaji wa Biblia ulikatazwa na Kanisa la Roma. Watu wakakatazwa kuisoma. Mapadri na waaskofu wakatafsiri mafundisho yake kwa kuendesha madai yao. Kwa hiyo Papa akajulikana pote kama msaidizi wa Mungu ulimwenguni.

## Namna Sabato Ilivyogeuzwa

Unabii ulitangaza kwamba Kanisa la Kiroma “litafikiri kugeuza nyakati na sheria”. Danieli 7:25. Kwa kutoa badala kwa ibada ya sanamu, ibada ya masura sanamu na masalio kumbukumbu, jambo hilo likaingizwa kidogo kidogo katika ibada ya Kikristo. Agizo la baraza la kawaida (Tazama mwisho wa kitabu (Nyongezo)) mwishowe likaanzisha ibada hii ya sanamu. Roma ikasubutu kufutia mbali amri ya pili ya sheria ya Mungu, inayokataza ibada ya sanamu, na kugawanya amri ya kumi ili kulinda hesabu.

Waongozi wasiotakaswa wa kanisa wakageuza amri ya ine vile vile, kwa kutangua Sabato ya zamani, siku ambayo Mungu alibariki na kutakasa (Mwanzo 2:2,3) na mahali pake wakatukuza siku kuu iliyolazimishwa na wapagani kama “siku tukufu ya jua”. Katika karne za kwanza Sabato ya kweli ilishikwa na Wakristo wote, lakini Shetani akatumika kwa kuleta kusudi lake. Siku ya jua (siku ya kwanza) (Dimanche) ikafanywa kuwa siku kuu kwa ajili ya ufu-

fuko wa Kristo. Huduma za dini zilifanyika kwa siku hiyo, lakini ilizaniwa kama siku ya pumziko, Sabato ikaendelea kushikwa na utakatifu.

Shetani akaongoza Wayahudi, kabla ya kuja kwa Kristo mara ya kwanza, kulemeza Sabato kwa lazimisho makali, kuifanya kuwa mzigo. Sasa, kwa kutumia nuru ya uongo ambamo alilete sabato kutazamiwa, akaitupia zarau kama sheria ya "Wayahudi". Wakati Wakristo kwa kawaida waliendelea kushika siku ya kwanza (Dimanche) kama siku kuu ya shangwe, akawaongoza kufanya Sabato kuwa siku ya huzuni na giza ili kuonyesha machukio kwa Kiyahudi.

Mfalme Constantini akatoa amri kufanya Siku ya kwanza (Di- [16]
manche) siku kuu ya watu wote popote katika ufalme wa Roma (Tazama Mwisho wa Kitabu ama Nyongezo). Siku ya jua ilikuwa ikitukuzwa na watu wake wapagani na kuheshimiwa na Wakristo. Alilazimishwa kufanya hivi na maaskofu wa kanisa. Walipoongozwa na hamu ya mamlaka, waliona ya kuwa kama siku hiyo moja ilishikwa kwa wote ni kusema Wakristo na wapagani, ingeendelesha uwezo na utukufu wa kanisa. Lakini wakati Wakristo wengi wenye kumcha Mungu walipoongozwa kuzania Siku ya kwanza (Dimanche) kama yenye kuwa na cheo cha utakatifu, waliendelea kushika Sabato ya kweli na kuitukuza katika utiifu wa amri ya ine.

Mdanganyi mkuu hakutimiza kazi yake. Alikusudia kutumia uwezo wake kwa njia ya mjumbe wake, askofu mwenye kiburi anayejidai kuwa mjumbe wa Kristo. Mabaraza makubwa yalifanywa ambamo wakuu walikusanyika kutoka pote duniani. Karibu kila baraza Sabato iligandamizwa chini kidogo, wakati siku ya kwanza (Dimanche) ikatukuzwa. Kwa hiyo siku kuu ya wapagani mwishowe ikatukuzwa kama sheria ya Mungu, lakini sabato ya Biblia ikatangazwa kuwa kumbukumbu ya dini ya Kiyahudi na kawaida zake zikatangazwa kuwa za laana.

Mkufuru akafaulu katika kujionyesha mwenyewe "juu ya yote yanayoitwa Mungu, ao kuabudiwa." 2 Watesalonika 2:4. Alisubutu kugeuza amri moja tu ya sheria ya Mungu inayoonyesha Mungu wa kweli na wa uhai. Katika amri ya ine, Mungu hufunuliwa kama Muumba. Kama ukumbusho wa kazi ya kuumba, siku ya saba ikatakaswa kama siku ya pumziko la mtu, iliyokusudiwa kulinda Mungu wa uhai siku zote mbele ya akili za watu kama kitu cha ibada. Shetani hujitaidi kugeuza watu kwa utii wa sheria ya Mungu; kwa

hivyo huelekeza nguvu zake zaidi sana juu ya amri ile inayoonyesha Mungu kama Muumba.

Waprotestanti sasa wanalazimisha kwamba ufufuo wa Kristo Siku ya Kwanza (Dimanche) uliifanya kuwa Sabato ya Kikristo. Lakini hapana heshima ya namna hiyo iliyotolewa kwa siku ile na Kristo au mitume wake. Kawaida ya Siku ya Kwanza (Dimanche) ilikuwa na asili yake katika ile "siri ya uasi" (2 Watesalonika 2:7), ambayo, hata katika siku ya Paulo, ilianza kazi yake. Sababu gani inayoweza kutolewa kwa mageuzi ambayo Maandiko hayakuruhusu?

Katika karne ya sita, askofu wa Roma alitangazwa kuwa kichwa cha kanisa yote nzima. Dini ya kipagani ikatoa nafasi kwa kanisa la Roma. Joka akamupa nyama "nguvu zake", na kiti chake cha ufalme na mamlaka nyingi". Ufunuo 13:2 (Tazama Nyongezo).

[17] Sasa ikaanza miaka 1260 ya mateso ya Papa iliyotabiriwa katika mambo ya unabii wa Danieli na Ufunuo. Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7. Wakristo walilazimishwa kuchagua au kuacha uaminifu wao na kukubali huduma na ibada za Papa, au kutoa maisha yao katika gereza, au kuuawa. Sasa maneno ya Yesu yalitimilika: "Nanyi mutatolewa hata na wazazi wenu, na ndugu, na jamaa, na rafiki, na wengine wenu watawaua. Na mutachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu" Luka 21:16, 17.

Ulimwengu ukawa shamba kubwa sana la vita. Kwa mamia ya miaka kanisa la Kristo lilipaswa kuishi katika maficho na giza. "Yule mwanamuke akakimbia hata pori; kule ana pahali palipotengenezwa na Mungu ili wamulishe kule siku elfu moja mia mbili na makumi sita" Ufunuo 12:6.

Kutawazwa kwa utawala wa Kanisa la Roma kulionyesha mwanzo wa miaka ya giza. Imani ikahamishwa kutoka kwa Kristo na kwenda kwa Papa wa Roma. Badala ya kutumainia Mwana wa Mungu kwa ajili ya musamaha wa zambi na wokovu wa milele, watu wakatazamia Papa, na mapadri ambao aliwatolea mamlaka yake. Papa alikuwa mpatanishi wao wa kidunia. Alisimama kwa mahali pa Mungu kwa ajili yao. Kwenda pembeni ya mapenzi yake ilikuwa sababu ya kutosha kwa azabu kali. Kwa hiyo akili za watu zikatoka kwa Mungu zikageukia watu wapotevu, wabaya, niseme nini tena, kwa mfalme wa giza anayetumia uwezo wake kupita wao. Wakati Maandiko yanapokomeshwa na mtu anapojiona mwenyewe

kuwa kama mkubwa kabisa, kitu kitakacho tazamiwa tu ni hila, madanganyo, na upunguo wa tabia njema.

## Siku za Hatari kwa Kanisa

Wachukuzi wa bendera waaminifu walikuwa wachache sana. Hapo hapo ilionekana kwamba makosa ingekuwa karibu kushinda kabisa, na dini ya kweli kuondolewa duniani. Injili ilisahauliwa na watu wakalemewa na azabu kali. Walifundishwa kutumainia kazi zao wenyewe kwa malipo ya zambi zao. Safari ndefu za kwenda kuzuru patakatifu, matendo ya kitubio, ibada ya masalio ya mambo ya watakatifu wa kale, majengo ya makanisa, na mazabahu, malipo ya mali mingi kwa kanisa-haya yalilazimishwa kwa kutuliza hasira ya Mungu ao kujipatia upendeleo wake.

Karibu ya mwisho wa karne ya mnane, wafuasi wa Papa wa Roma wakaendelea kulazimisha kwamba katika siku za kwanza za kanisa maaskofu wa Roma walikuwa na uwezo wa kiroho sawa sawa na ule ambao wanachukuwa sasa. Maandiko ya uwongo [18]
yakaandikwa na watawa wakidanganya kwamba ni ya zamani sana. Maagizo ya baraza ambayo hayakusikiwa mbele ya kuimarisha ukubwa wa Papa tangu nyakati za kwanza, yakavumbuliwa (Tazama Nyonge 20).

Waaminifu wachache waliojenga juu ya msingi wa kweli. (1 Wakorinto 3:10,11) wakafazaika. Kuchoka kwa ajili ya kupigana na mateso, udanagnyifu, kila kizuizi kingine ambacho Shetani angevumbua, watu fulani ambao walikuwa waaminifu wakakata tamaa. Kwa ajili ya upendo wa amani na salama kwa mali yao na maisha yao, wakaacha msingi wa kweli. Wengine hawakuongopeshwa na upinzani wa adui zao.

Ibada ya sanamu ikawa kawaida. Mishumaa (bougies) iliwashwa mbele ya masanamu, na maombi yakatolewa kwao. Desturi zisizo za maana na kuabudu uchawi zikawa na uwezo. Hata hakili yenyewe ikaonekana kupoteza nguvu zake. Kwa sababu mapadri na maaskofu wao wenyewe walikuwa wenye kupenda anasa, na rushwa, watu waliotazamia uongozi kwao wakatazamia katika ujinga na makosa.

Katika karne ya kumi na moja, Papa Gregoire VII akatangaza kwamba kanisa halijakosa kamwe, na halitakosa kamwe, kwa kutokana na Maandiko. Lakini hakika za Maandiko hazikufuatana na

maneno yale. Askofu mwenye kiburi alidai pia uwezo wa kuondoa wafalme. Mfano moja wa tabia ya uonevu huyu anaotetea madai ya kutoweza kukosa ni jambo alilotendea mfalme wa Ujeremani, Henry IV. Kwa sababu alijaribu kuzarau mamlaka ya Papa, mfalme huyu akatengwa kwa kanisa na akatoshwa kwa kiti chake cha ufalme. Watoto wake wenyewe wa kifalme wakashawishiwa na mamlaka ya Papa katika uasi juu ya baba yake.

Henry akaona lazima ya kufanya amani pamoja na Roma. Pamoja na mke wake na mtumishi wake mwaminifu akavuka milima mirefu (Alpes) katika siku za baridi kali, ili apate kujinyenyekea mbele ya Papa. Alipofikia ngome ya Gregoire, akapelekwa katika uwanja wa inje. Kule, katika baridi kali ya wakati wa majira ya baridi, na kichwa wazi na vikanyagio, alingoja ruhusa ya Papa kuja mbele yake. Ni baada ya siku tatu za kufunga na kuungama, ndipo askofu akamtolea rehema. Na hivyo ni katika hali ya kwamba mfalme alipaswa kungoja ruhusa ya Papa kwa kupata tena alama za cheo ao kutumia uwezo wa kifalme. Gregoire, alipofurahia ushindi wake, akatangaza ya kwamba kazi yake ilikuwa ni kuangusha kiburi cha wafalme.

Ni ajabu ya namna gani tofauti kati ya askofu mwenye kiburi
[19] na upole na utulivu wa Kristo anayejionyesha mwenyewe kama mwenye kuomba ruhusa kwa mlango wa moyo. Alifundisha wanafunzi wake: "Naye anayetaka kuwa wa kwanza katikati yenu atakuwa mtumwa wenu" Matayo 20:27.

Hata mbele ya kuanzishwa kwa cheo cha Papa mafundisho ya watu wapagani wenye maarifa wakapata usikizi na kutumia muvuto wao katika kanisa. Wengi waliendelea kujifungia kwa mafundisho ya maarifa zote ya kipagani na wakalazimisha wengine kujifunza elimu ile kama njia ya kueneza mvuto wao katikati ya wapagani. Ndipo makosa makubwa yakaingizwa katika imani ya Kikristo.

## Namna Mafundisho ya Uongo Yaliingia

Mojawapo miongoni mwa makosa haya makubwa ya wazi ni imani ya kutokufa kwa roho ya mtu na ufahamu wa nafsi katika mauti. Mafundisho haya yaliweka msingi ambao Roma ikaanzisha sala kwa watakatifu na ibada ya Bikira Maria. Kutokana na hiyo,

uzushi juu ya mateso ya milele kwa ajili ya mtu asiyetubu, ambayo yaliingizwa mwanzoni katika imani ya Papa.

Ndipo njia ikatengenezwa kwa kuingiza uvumbuzi mwingine wa kipagani, ambao Roma iliita "toharani", na iliotumiwa kwa kuogopesha makundi ya wajinga na ya kuamini mambo ya uchawi. Usishi huu uliamini kuwako kwa pahali pa mateso ambapo roho zisizostahili hukumu ya milele, zinapaswa kuteseka juu ya malipizi ya zambi zao, na kutoka pale, zikiisha takaswa, zinakubaliwa mbinguni (Tazama Nyongezo).

Uvumbuzi mwingine ukahitajiwa, kuwezesha Roma kupata faida kwa njia ya woga na makosa ya wafuasi wake. Huu ulitolewa na mafundishojuu ya ununuzi wa huruma (indulgences). Ondoleo nzima la zambi za sasa, zilizopita na za wakati ujao liliahidiwa kwa wale waliojitoa kwa vita vilivyofanywa na Papa kwa ajili ya kupanua mamlaka yake, kwa kulipiza adui zake ao kuangamiza wale waliosubutu kukataa mamlaka yake ya kiroho. Kwa njia ya kulipa mali katika kanisa wanaweza kujiokoa katika zambi zao, na pia kuokoa roho za rafiki zao zinazoteseka katika miako ya moto. Kwa njia hiyo Roma ikajaza masanduku makubwa yake na kusaidia fahari yake, anasa na uovu wa kujidai kuwa wajumbe wa Yule asiyekuwa na pahali pa kuweka kichwa chake (Tazama Nyongezo).

Meza ya Bwana likapigwa na kafara ya ibada ya sanamu ya misa. Mapadri wa Papa wakajidai kufanya mkate na divai vya Meza
ya Bwana kuwa mwili wa kweli na damu ya kweli ya Bwana Yesu [20]
Kristo". Kwa majivuno ya kutukana Mungu, kwa wazi wakadai uwezo wa kuumba Mungu, Muumba wa vitu vyote. Wakristo wakalazimishwa maumivu ya kifo, kuungama imani yao katika uzushi wa machukizo ya kutukana mbingu.

Katika karne ya kumi na tatu kile chombo kikali sana kati ya vyombo vya Papa kikaanzishwa-Baraza kuu la kuhukumia wazushi wa dini (Inquisition). Katika mabaraza yao ya siri Shetani na malaika zake walitawala roho za watu waovu. Bila kuonekana katikati Malaika wa Mungu alisimama, alipoandika kwa uaminifu ukumbusho wa maagizo yao maovu ya kutisha na kuandika historia ya matendo yao mabaya sana kuonekana machoni pa watu. "Babeli Mkuu" "analewa kwa damu ya watakatifu". Tazama Ufunuo 17:5,6. Miili iliyoteseka ya mamilioni ya wafia dini (martyrs) ikalalamika mbele ya Mungu kwa ajili ya kisasi juu ya ule uwezo wa mkufuru.

Papa akawa mtawala mkali peke yake wa dunia yote. Wafalme na wafalme wakubwa (empereurs) walitii maagizo ya askofu wa Roma. Kwa muda wa mamia ya miaka mafundisho ya Roma yakakubaliwa na wengi. Waongozi wake wakaheshimiwa na kusaidiwa sana. Kamwe tangu wakati ule, kanisa la Roma lilikuwa halijafikia kadiri ya cheo kikubwa, cha fahari, ao uwezo wa namna ile.

Lakini "azuhuri ya cheo cha Papa ilikuwa usiku wa manane wa wanadamu".

Maandiko matakatifu yalikuwa karibu bila kujulikana. Waongozi wa kanisa la Roma walichukia nuru iliyofunua zambi zao. Sheria ya Mungu, kipimo cha haki, ilipoondolewa, wakatumia uwezo bila kizuio. Majumba makubwa ya Papa na maaskofu yalikuwa monyesho ya upotovu wa machukizo. Maaskofu wengine walikuwa na makosa ya maovu sana hata wakajaribu kuwaondosha kama wanyama wa kutisha wasioweza kuvumiliwa. Kwa muda wa karne nyingi Ulaya haikufanya maendeleo kamwe katika maarifa ya kweli, mambo ya ufundi na maendeleo ya jamii. Ukristo ukapatwa na kupooza kwa tabia na maarifa... Ndiyo yalikuwa matokeo ya kufukuza Neno la Mungu!

# 4 /WAFUASI WA WALDENSE WANAKINGA IMANI [21]

Katika mda mrefu wa mamlaka ya Papa, kulikuwa washahidi wa Mungu waliolinda imani katika Kristo kama mpatanishi wa pekee kati ya Mungu na mtu. Walishika Biblia kama kiongozi pekee kwa maisha, na kuheshimu Sabato ya kweli. Wakahesabiwa kama wapinga dini, maandiko yao yakakomeshwa, kuelezwa vibaya, ao kuondolewa. Lakini wakasimama imara.

Wanakuwa na nafasi ndogo katika maandiko ya wanadamu, ila tu katika mashitaki ya watesi wao. Kila kitu "cha kupinga dini", ikiwa ni watu ao maandiko, Roma alitafuta kuharibu. Roma ilijitahidi vile vile kuharibu kila kumbukumbu la maovu wake mbele ya wasiokubali mafundisho yake. Kabla ya uvumbuzi wa ufundi wa kupiga chapa, vitabu vilikuwa vichache kwa hesabu; kwa hiyo juu ya uchache wa vitabu hii haikuzuia Waroma kutimiza kusudi lao. Kanisa la Roma lilipopata uwezo likanyoosha mikono yake kwa kuangamiza wote wale waliokataa kukubali utawala wake.

Katika Uingereza dini ya Kikristo zamani za kale ilikuwa imekwisha kupata mizizi, haikuharibiwa na ukufuru wa Waroma. Mateso ya wafalme wa kipagani yalikuwa tu zawadi ambayo makanisa ya kwanza ya Uingereza yalipata kwa Roma. Wakristo wengi waliokimbia mateso katika Uingereza wakipata kimbilio katika Scotland. Kwa hiyo ukweli ukachukuliwa katika nchi ya Irlande, na katika inchi hizi ukweli ulikubaliwa kwa furaha.

Wakati Wasaxons waliposhambulia Uingereza, upagani ukapata mamlaka, na Wakristo walilazimishwa kukimbilia milimani. Katika Scotland, karne moja baadaye, nuru ikaangazia inchi za mbali sana. Kutoka Irlande Columba akakuja na waidizi wake, waliofanya kisiwa cha pekee cha Iona kuwa makao ya kazi zao za kueneza injili. Miongoni mwa wainjilisti hawa kulikuwa mchunguzi wa Sabato ya Biblia, na kwa hivyo ukweli huu ukaingizwa miongoni mwa watu. Masomo yakaanzishwa pale Iona, ambamo wajumbe (missionnaires)

walitoka na kwenda Scotland, Uingereza, Ujeremani, Uswisi, na hata Italia.

### Roma Inakutana na Dini ya Biblia

Lakini Roma ilikusudia kuweka Uingereza chini ya mamlaka yake. Katika karne ya sita wajumbe (missionnaires) wake wakajaribu kutubisha Wasaxons wapagani. Jinsi kazi ilivyoendelea,
[22] waongozi wa kiPapa wakakutana na Wakristo wa zamani za kale -wapole, wanyenyekevu, wenye kupatana na maneno ya Maandiko katika tabia, mafundisho, na wa mwenendo mwema. Wale wakiroma walionyesha imani ya mambo ya uchawi, ukuu, na kiburi cha kipapa. Roma alilazimisha kwamba makanisa haya ya Kikristo yapate kukubali mamlaka ya askofu mkuu. Waingereza wakajibu kwamba Papa hakutajwa kuwa mkuu katika kanisa na wangeweza kumtolea tu utii ule unaofaa kwa kila mfuasi wa Kristo. Hawakujua bwana mwingine isipokuwa Kristo.

Sasa roho ya kweli ya kanisa la Roma ikafunuliwa. Akasema mwongozi wa Roma: "Kama hamutapokea wandugu wanaowaletea amani, mutapokea maadui watakaowaletea vita". Vita na udanganyifu vikatumiwa juu ya washahidi hawa kwa ajili ya imani ya Biblia, hata wakati makanisa ya Waingereza ya kaharibiwa au kulazimishwa kutii Papa.

Katika inchi iliyokuwa mbali na mamlaka ya Roma, kwa karne nyingi miili ya Wakristo iliishi na usalama kidogo bila uovu wa kipapa. Waliendelea kutumia Biblia kuwa kiongozi pekee cha imani. Wakristo hawa waliamini umilele wa sheria ya Mungu na walishika Sabato ya amri ya ine. Makanisa walioshika imani hii na kuitumia waliishi katika Afrika ya Kati na miongoni mwa Waarmenia wa Asia.

Kwa wale waliosimama imara mamlaka ya Papa, Wavaudois (Waldenses) walisimama wa kwanza. Katika inchi kanisa za Kiroma ziliimarisha kiti chake, makanisa ya Piedmont yakadumisha uhuru wao. Lakini wakati ukakuja ambapo Roma ilishurutisha juu ya utii wao. Lakini wengine, walikataa kujitoa kwa Papa ao maaskofu, wakakusudia kulinda usafi na unyenyekevu wa imani yao. Utengano ukatokea. Wale walioambatana na imani ya zamani sasa wakajitenga. Wengine, kwa kuacha inchi yao ya Alpes za milima mirefu

(Alps), wakainua mwenge ya ukweli katika inchi za kigeni. Wengine wakakimbilia katika ngome za miamba ya milima na huko wakalinda uhuru wao wa kuabudu Mungu.

Imani yao ya dini iliimarishwa juu ya Neno la Mungu lenye kuandikwa. Wakulima hao wanyenyekevu, waliofungiwa inje ya ulimwengu, hawakufikia wao wenyewe kwa ukweli katika upinzani wa mafundisho ya kanisa la uasi. Imani ya dini yao ilikuwa uriti wao kutoka kwa mababa zao. Walitoshelewa kwa ajili ya imani ya kanisa la mitume. "Kanisa jangwani", sio serekali ya kanisa la kiburi iliyotawazwa katika mji mkubwa wa ulimwengu, lililokuwa kanisa la kweli la Kristo, mlinzi wa hazina za ukweli ambazo Mungu alizoweka kwa watu wake kwa kutolewa kwa ulimwengu.

Miongoni mwa sababu muhimu zilizoongoza kwa utengano wa [23] kanisa la kweli kutoka kwa kanisa la KiRoma ilikuwa ni uchuki wa kanisa hili juu ya Sabato ya Biblia. Kama ilivyotabiriwa na unabii, mamlaka ya kanisa la KiRoma likagandamiza sheria ya Mungu katika mavumbi. Makanisa chini ya kanisa la Roma yakalazimishwa kuheshimu siku ya kwanza (Dimanche). Kwa kosa la kupita kawaida wengi miongoni mwa watu wa kweli wa Mungu wakafazaika sana hata ingawa walishika Sabato, wakaacha kutumika pia siku ya kwanza ya juma (Dimanche). Lakini jambo hilo halikuwafurahisha waongozi wa Papa. Walilazimishwa kwamba Sabato ichafuliwe, na wakashitaki wale waliosubutu kuonyesha heshima yake.

Mamia ya miaka kabla ya Matengenezo (Reformation) Wavaudois (Waldenses) walikuwa na Biblia katika lugha yao yenyewe. Jambo hili likawatelea kuteswa kulikowengine. Wakatangaza Roma kuwa Babeli mkufuru wa Ufunuo. Katika hatari ya maisha yao wakasimama imara kushindana na maovu yake. Katika miaka ya uasi kulikuwa Wavaudois (Waldenses) waliokana mamlaka ya Roma, wakakataa ibada ya sanamu kama kuabudu miungu, na wakashika Sabato ya kweli. (Tazama Nyongezo).

Nyuma ya ngome za juu sana za milima Wavaudois wakapata mahali pa kujificha. Hawa wakimbizi waaminifu wakaonyesha watoto wao urefu wa munara juu yao katika ukuu na wakasema juu ya yule ambaye Neno lake linakuwa la kudumu kama milima ya milele. Mungu aliimarisha milima; si mkono lakini ule unaokuwa na uwezo usio na mwisho ungaliweza kuihamisha. Kwa namna ile ile akaimar-

isha sheria yake. Mkono wa mtu haungeweza kuongoa milima na kuitupa kwa nguvu baharini, kama vile hauwezi kubadili sheria moja ya Mungu. Wasafiri hawa hawakunungunika kwa sababu ya taabu ya mateso yao; hawakuwa peke yao katika ukiwa wa milima. Walijifurahisha katika uhuru wao kwa ibada. Kutoka ngome ya juu waliimba sifa za Mungu, na majeshi ya Roma hawakuweza kunyamazisha nyimbo zao za shukrani.

### Damani (Bei) ya Mafundisho ya Ukweli

Mafundisho ya ukweli yalikuwa na bei kuliko nyumba na inchi, rafiki, jamaa, hata maisha yenyewe. Kutokea mwanzo wa utoto, vijana walifundishwa kuheshimu maagizo matakatifu ya sheria ya Mungu. Kurasa za Biblia zilikuwa chache; kwa hiyo maneno yake ya damani yaliwekwa kwa uwezo wa kukumbuka. Wengi waliweza kukariri sehemu nyingi za Agano la Kale na Agano Jipya.

[24] Walifundishwa toka utoto kuvumilia ugumu na kufikiri na kutenda kwa ajili ya wao wenyewe. Walifundishwa kuchukua madaraka, kujilinda kwa usemi, na kufahamu hekima ya utulivu. Neno moja la ujinga linaposikiwa kwa maadui wao lingeweza kuleta hasara ya maisha ya mamia ya wandugu, kwani kama vile mbwa mwitu katika kuwinda mawindo, maadui wa kweli wanawinda wale waliosubutu kutangaza uhuru wa imani ya dini.

Wavaudois kwa uvumilivu walitaabika kwa ajili ya chakula chao. Kila mahali padogo pa udongo wa kulimiwa katikati ya milima palitumiwa vizuri. Kiasi katika utumizi wa feza na kujikana yakafanya sehemu ya elimu yao ambayo watoto walijifunza. Kazi ilikuwa ya taabu lakini yakufaa kwa afya, basi ndicho mtu anachohitaji katika hali yake ya kuanguka. Vijana walifundishwa kwamba nguvu zao zote ni za Mungu, zipate kusitawishwa kwa ajili ya kazi yake.

Makanisa ya Wavaudois yalifanana na kanisa la nyakati za mitume. Kukataa mamlaka ya Papa na askofu, walishika Biblia kuwa na mamlaka yasiyoweza kukosa. Wachungaji wao, hawakufanana na mapadri wa kiburi wa Roma, wakalisha kundi la Mungu, kuwaongoza katika malisho ya majani mabichi na chemchemi ya Neno takatifu lake. Watu walikusanyika si ndani ya makanisa ya maridadi ao makanisa makuu ya majimbo, bali katika mabonde ya Milima mirefu, ao, katika wakati wa hatari, ndani ya ngome ya miamba,

kwa kusikiliza maneno ya ukweli kutoka kwa watumishi wa Kristo. Wachungaji hawakuhubiri injili tu, walizuru wagonjwa na wakatumika kwa kuamusha umoja na upendo wa ndugu. Kama Paulo fundi wa kufanya hema, kila mmoja wao alijifunza kazi fulani ambayo kwayo, kama ni lazima, kingemusaidia kwa kujitegemea mwenyewe.

Vijana walipata mafundisho yao kwa wachungaji wao. Biblia ilifanywa kuwa masomo ya mhimu. Injili za Matayo na Yoane ziliwekwa katika ukumbusho, pamoja na barua nyingine.

Mara zingine katika mapango ya giza udongoni, kwa nuru ya mienge (torches), Maandiko matakatifu yaliandikwa, mstari kwa mstari. Malaika kutoka mbinguni wakazunguuka watumishi hawa waaminifu.

Shetani alilazimisha mapadri wa Papa na maaskofu kuzika Neno la Ukweli chini ya machafu ya makosa na ibada ya uchawi. Lakini kwa namna ya ajabu likalindwa bila kuchafuliwa wakati wa miaka yote ya giza. Kama safina juu ya mawimbi mazito, Neno la Mungu linashinda zoruba zinazolitisha kuliharibu. Kama vile dini yamefikia bamba la jiwe lenye zahabu na feza iliyofichwa chini upande wa juu, ni vivyo hivyo Maandiko matakatifu yanakuwa na hazina ya [25]
ukweli iliyofunuliwa tu kwa wanyenyekevu, wanaopenda kuomba Mungu alichagua Biblia kuwa kitabu cha mafundisho ya wanadamu wote kuwa ufunuo wake mwenyewe. Kila ukweli uliotambuliwa ni uvumbuzi mupya wa tabia ya Mwandishi wake.

Kutoka kwa vyuo vyao katika milima vijana wengine walitumwa kujifunza katika Ufaransa ao Italia, ambapo palikuwa na nafasi kubwa zaidi kwa mafundisho na uchunguzi kuliko katika inchi yao ya milima mirefu. Vijana waliotumwa walijihatarisha kwa majaribu. Walipambana na wajumbe wa Shetani waliowalazimisha mambo ya kipinga ukweli wa dini na madanganyo ya hatari. Lakini elimu yao tokea utoto ikawatayarisha kwa jambo hili.

Katika vyuo po pote walipokwenda hawakuweka tumaini lao kwa kitu cho chote. Mavazi yao yalitayarishwa kama kuficha hazina zao kubwa-Maandiko. Mara kwa mara walivyoweza waliweka kwa uangalifu sehemu za maandiko njiani mwa wale ambao mioyo yao ilionekana kufunguliwa kwa kupokea ukweli. Waiiotubu na kukubali imani ya kweli walipatikana katika vyuo hii vya elimu, mara kwa mara mafundisho ya imani ya kweli ikaenea kwa chuo

chote kizima. Huku waongozi wa Papa hawakuweza kupata mwanzo wa kile walichoitwa "Upinzani wa mafundisho ya dini".

### Vijana Walifundishwa Kuwa Wajumbe (wa injili)

Wakristo Wavaudois walijisikia kuwa na madaraka makuu ya kutoa nuru yao iangaze. Kwa uwezo wa Neno la Mungu walitafuta kuvunja utumwa ambao Roma ililazimisha. Wahudumu wa Wavaudois walipaswa kutumika kwa miaka tatu katika shamba la misioni kabla ya kuongoza kanisa nyumbani--chanzo cha kufaa kwa maisha ya mchungaji katika nyakati ambazo roho za watu zinajaribiwa. Vijana waliona mbele yao, si utajiri wa kidunia na sifa, bali taabu na hatari na labda mateso ya wafia dini. Wajumbe walitembea wawili wawili, kama vile Yesu alivyowatuma wanafunzi wake.

Kama wangejulisha ujumbe wao wangeuletea kushindwa. Kila mhuburi alikuwa na ujuzi wa kazi fulani ao ufundi, na wajumbe waliendesha kazi yao chini ya kifuniko cha mwito wa kazi ya dunia , kwa kawaida kama mfanya biashara ao ya mchuuzi. "Walichukua mavazi ya hariri, vitu vilivyofanyizwa kwa zahabu, na vitu vingine, ... na walikaribishwa vizuri kama wafanya biashara mahali wangezarauliwa kama wajumbe (missionnaires)" Walichukua kwa siri nakala
[26] za Biblia, nzima ao kipande. Mara kwa mara shauku ya kusoma Neno la Mungu ilipoamushwa, sehemu fulani za Biblia ziliachwa kwa wale waliozihitaji.

Kwa miguu wazi na mavazi machafu na safari ya udongo mzito, wajumbe hawa walipita katika miji mikubwa na kuingia kwa inchi za mbali. Makanisa yakasimamishwa kwa haraka njiani walimopita, na damu ya wafia dini ikashuhudia ukweli. Kwa uficho na ukimya, Neno la Mungu likitukana na kupokelewa kwa furaha ndani ya nyumba na mioyoni mwa watu.

Wavaudois waliamini kwamba mwisho wa vitu vyote haukuwa mbali sana. Walipokuwa wakijifunza Biblia walikuwa wanatia moyo kwa kazi yao ya kujulusha wengine juu ya ukweli Walipata faraja, tumaini, na amani kwa kumwamini Yesu. Namna nuru ilifurahisha mioyo yao, walitamani sana kutawanya nyali zake kwa wale waliokuwa katika giza la makosa la kipapa.

Chini ya uongozi wa Papa na mapadri, wengi walifundishwa kutumainia kazi ao matendo yao mazuri kwa kuokolewa. Walikuwa

wakijiangalia wao wenyewe, akili zao zilikuwa zikiishi katika hali yao ya zambi, kutesa moyo na mwili, lakini bila kurijika. Maelfu walipoteza maisha yao katika viumba vya watawa (moines). Kwa mafungo ya mara kwa mara na kutesa mwili, kukesha usiku wa manane, kwa kusujudia mahali pa baridi, mawe ya maji maji, kwa safari ndefu--za kwenda kuzuru Pahali patakatifu--kwa kuogopa ya hasira ya kisasi cha Mungu--wengi waliendelea kuteseka hata kuchoka kukadumisha. Bila nyali moja ya tumaini wakazama ndani ya kaburi.

## Wenye Zambi Walimushota Kristo

Wavaudois walitamani sana kufungulia mioyo hizi zilizoumia na njaa ya habari za amani katika ahadi za Mungu na kuwaonyesha kwa Kristo kama tumaini lao la pekee la wokovu. Mafundisho kwamba matendo mema yanaweza kuwa pahali pa zambi yaliyotambuliwa kwa kuwa msingi wake niwa uongo. Tabia nzuri za Mwokozi aliyesulibiwa na kufufuka zinakuwa, ndiyo msingi wa imani ya kikristo. Hali ya matumaini ya moyo kwa Kristo inapaswa kuwa karibu sana kama vile kiungo kwa mwili ao cha tawi kwa mzabibu.

Mafundisho ya wapapa na wapadri yaliongoza watu kutazama Mungu na hata Kristo kama wakali na wa kugombeza, kwa hiyo bila huruma kwa mtu kwamba uombezi wa wapadri na watakatifu ulipaswa kuombwa. Wale ambao akili zao zimeangaziwa walitamani sana kuondoa vizuizi ambavyo Shetani amevijaza, ili watu waweze [27]
kuja mara moja kwa Mungu, kuungama zambi zao, na kupokea msamaha na amani.

## Kushambulia Ufalme wa Shetani

Ujumbe wa Wavaudois kwa uangalifu ukatoa sehemu zilizoandikwa kwa uangalifu za Maandiko matakatifu. Nuru ya ukweli ikaingia kwa akili nyingi za giza, hata Jua la Haki likaangaza katika moyo nyali zake za kupenya. Kila mara msikilizaji alihitaji sehemu ya Maandiko ipate kukaririwa, kana kwamba apate kuhakikisha kwamba alisikia vizuri.

Wengi waliona ni bure namna gani uombezi wa watu kwa ajili ya wenye zambi hauna faida. Wakapiga kelele kwa furaha, “Kristo

ni kuhani wangu; damu yake ni kafara yangu; mazabahu yake ni mahali pangu pa kuungamia". Ilikuwa mufuriko mkubwa wa nuru uliyo kuwa juu yao, hata walionekana kwao kwamba walichukuliwa mbinguni. Hofu yote ya kifo ikafutika. Sasa waliweza kutamani gereza kama wangeweza kwa hiyo kutukuza Mkombozi wao.

Katika mahali pa siri Neno la Mungu lililetwa na kusomwa, mara zingine kwa roho moja, wakati mwingine kwa kundi ndogo la watu lililotamani sana nuru. Mara nyingi usiku mzima ulitumiwa kwa namna hii. Mara kwa mara maneno kama haya yakasemwa: "Je, Mungu atakubali sadaka yangu? Atanifurahia? Atanisamehe"? Jibu lilikuwa, soma, "Kujeni kwangu, ninyi wote munaosumbuka na wenye mizigo mizito, nami nitawapumzisha ninyi". Matayo 11:28.

Roho zile zenye furaha zikarudia nyumbani mwao kutawanya nuru, kukariri kwa wengine, kwa namna walivyoweza, maarifa mapya yao. Walipata ukweli na njia ya uhai! Maandiko yalisemwa kwa mioyo ya wale wanaotamani ukweli.

Mjumbe wa ukweli alikwenda kwa njia yake. Kwa namna ninyi wasikilizaji wake hawakuuliza alitoka wapi ao alikwenda wapi. Walikuwa wamekwisha kupatwa na ushindi kwa hiyo hawakuwa na wazo kwa kumuuliza. Aliweza kuwa malaika kutoka mbinguni! Walitaka maelezo zaidi juu ya jambo hilo.

Katika mambo mengi mjumbe wa ukweli alifanya njia yake kwa inchi nyingine ao alikuwa akipunguza maisha yake katika gereza ao labda mifupa yake iligeuka nyeupe mahali aliposhuhudia ukweli. Lakini maneno aliyoacha nyuma yalikuwa yakitenda kazi yao.

Waongozi wa Papa waliona hatari kutoka kwa kazi za hawa watu wanyenyekevu wa kuzunguka zunguka. Nuru ya ukweli ingefutia
[28] mbali mawingu mazito ya kosa lililofunika watu; ingeongoza akili kwa Mungu peke yake na mwisho kuharibu mamlaka ya Roma.

Watu hawa, katika kushika imani ya kanisa la zamani, ilikuwa ni ushuhuda imara kwa uasi wa Roma na kwa hivyo ikaamsha chuki na mateso. Kukataa kwao kwa kuacha Maandiko ilikuwa ni kosa ambalo Roma haikuweza kuvumilia.

### Roma Inakusudia Kuangamiza Wavaudois (Waldenses)

Sasa mapigano makali kuliko yote juu ya watu wa Mungu yakaanza katika makao yao milimani. Wapelelezi (quisiteurs) wali-

wekwa kwa nyayo yao. Tena na tena mashamba yao yaliyokuwa na baraka yakaharibiwa, makao yao na makanisa madogo yao yakaondolewa. Hakuna mashitaka iliyoweza kuletwa juu ya tabia njema ya namna hii ya watu waliokatazwa. Kosa lao kubwa lilikuwa kwamba hawakuabudu Mungu kufuatana na mapenzi ya Papa. Kwa ajili ya “kosa hili” kila tukano na mateso ambayo watu ao Shetani waliweza kufanya yaliwekwa juu yao.

Wakati Roma ilikusudia kukomesha dini hii (secte) iliyochukiwa, tangazo likatolewa na Papa kuwahukumu kama wapingaji wa dini na kuwatoa kwa mauaji. (Tazama Nyongezo). Hawakusitakiwa kama wavivu, wasio waaminifu, ao wasio na utaratibu; lakini ilitangazwa kwamba walikuwa wenye mfano wa wenye utawa na utakatifu uliovuta “kondoo la zizi la kweli”. Tangazo hili likaita washiriki wote wa kanisa kuungana kwa mapigano yawapingaji wa dini Kama vile kuchochea tangazo hili liliachia viapo vyovyote wote waliokubali kwenda kwa vita; tangazo hili likawatolea haki kwa kila mali waliweza kupata kwa wizi, nalika ahidi ondoleo la zambi zote kwa yule angeweza kuua mpinga dini yeyote. Jambo hilo likavunja mapatano yote yaliyofanywa kwa upendeleo wa Wavaudois, wakakataza watu wote kuwapa msaada wowote, na kuwapa uwezo watu wote kukamata mali yao”. Andiko hii linafunua wazi wazi mungurumo wa joka, na si sauti ya Kristo. Roho ya namna moja iliyosulibisha Kristo na kuua mitume, ile ilisukuma Nero mwenye hamu ya kumwaga damu juu ya waaminifu katika siku zake, ilikuwa kazini kwa kuondoa juu ya dunia ya wale waliokuwa wapendwa wa Mungu.

Bila kutazama vita ya Papa juu yao na mauaji makali sana waliyoyapata, watu hawa wanaogopa Mungu waliendelea kutuma wajumbe (Missionnaires) kutawanya ukweli wa damani. Waliwindwa hata kuuwawa, lakini damu yao ilinywesha mbegu iliyopandwa na
kuzaa matunda. [29]

Kwa hivyo Wavaudois walishuhudia Mungu kwa karne nyingi kabla ya Luther. Walipanda mbegu ya Matengenezo (Reformation) yale yaliyoanza wakati wa Wycliffe, yakaota na kukomaa katika siku za Luther, na yanapaswa kuendelea hata mwisho wa wakati.

[30] # 5 /NURU INANGAA KATIKA UINGEREZA

Mungu hakukubali Neno lake liharibiwe kabisa. Katika inchi mbalimbali za Ulaya watu waliosukumwa na Roho ya Mungu kwa kutafuta ukweli kama vile hazina zilizofichwa. Kwa bahati njema waliongozwa na Maandiko matakatifu, wakipendezwa kukubali nuru kwa bei yo yote itakayohitajiwa kwao wenyewe. Ingawa hawakuona vitu vyote wazi, walikuwa wakiwezeshwa kutambua mambo mengi ya ukweli yaliyozikwa ao fichwa tangu zamani.

Wakati ulifika kwa Maandiko kupewa kwa watu katika lugha yao wenyewe. Dunia ilikwisha kupitisha usiku wake wa manane. Katika inchi nyingi kukaonekana dalili za mapambazuko.

Katika karne ya kumi na ine "nyota ya asubuhi ya Matengenezo (Reformation)" ikatokea katika Uingereza. John Wycliffe alijulikana huko college kuwa mtu wa utawa wa elimu sana. Alielemishwa na hekima ya elimu, kanuni za kanisa, na sheria ya serkali, alitayarishwa kuingia katika kazi ngumu kubwa kwa ajili ya raia na uhuru wa dini. Alipata malezi ya elimu ya vyuo, na akafahamu maarifa ya watu wa mashule. Cheo na ukamilifu wa ufahamu wake viliamuru heshima za rafiki na maadui. Adui zake walizuiwa kutupa zarau juu ya chazo cha Matengenezo kwa kuonyesha ujinga ao uzaifu wa wale walioikubali.

Wakati Wycliffe alipokuwa akingaliki huko college, akaingia majifunzo ya Maandiko matakatifu. Hata sasa Wicliffe alijifahamu kuwa mwenye hitaji kubwa, ambao hata mafundisho ya elimu yake wala mafundisho ya kanisa hayataweza kumtoshelea. Katika Neno la Mungu aliona kile ambacho alikuwa anatafuta bila mafanikio. Hapa akamuona Kristo akitangazwa kama mteteaji pekee wa mtu. Akakusudia kutangaza ukweli aliyovumbua.

Kwa mwanzo wa kazi yake, Wycliffe hakujitia mwenyewe katika upinzani na Roma. Lakini kwa namna alivyotambua wazi zaidi, makosa ya kanisa la Roma, akazidi kwa bidii kufundisha mafundisho ya Biblia. Aliona kwamba Roma iliacha Neno la Mungu kwa ajili ya desturi za asili za watu. Akashitaki bila oga upadri kwa kuweza

kuondoshea mbali Maandiko, na akataka kwa lazima kwamba Biblia irudishwe kwa watu na kwamba uwezo yake uwekwe tena ndani ya kanisa. Alikuwa mhubiri hodari na mwenye maneno ya kuamsha moyo, na maisha yake ya kila siku yalionyesha ukweli aliyohubiri. Ufahamu wake wa Maandiko, usafi wa maisha yake, na bidii yake na ukamilifu aliouhubiri yakampa heshima kwa wote. Wengi wakaona uovu katika Kanisa la Roma. Wakapokea kwa shangwe isiyofichwa [31]
kweli ambazo zililetwa waziwazi na Wycliffe. Lakini waongozi wa kiPapa wakajazwa na hasira: Mtengenezaji huyu alikuwa akipata mvuto mkubwa kuliko wao.

## Mvumbuzi Hodari wa Kosa

Wycliffe alikuwa mvumbuzi hodari wa kosa na akapambana bila woga juu ya matumizi mabaya yaliyoruhusiwa na Roma. Alipokuwa padri wa mfalme, akawa shujaa kwa kukataa malipo ya kodi yaliyodaiwa na Papa kutoka kwa mfalme wa Uingereza. Majivuno ya Papa ya mamlaka juu ya watawala wa ulimwengu yalikuwa kinyume kwa vyote viwili kweli na ufunuo. Matakwa ya Papa yalichochea hasira, na mafundisho ya Wycliffe yalivuta akili za uongozi wa taifa. Mfalme na wakuu walikusanyika kwa kukataa malipo ya kodi.

Watu waliojitenga na mambo ya dunia, maskini wakajaa katika Uingereza, kumwanga sumu juu ya ukubwa na kufanikiwa kwa taifa. Maisha ya watawa (moines) ya uvivu na uombaji wa vitu ao mali haikuwa tu gharama kubwa juu ya mali ya watu, wageuza kazi nzuri kuwa ya kuzarauliwa. Vijana walipotoka na kuharibika. Wengi walishawishwi kujitoa wao wenyewe kwa maisha ya watawa si kwa kukosa ukubali wa wazazi tu, bali bila ufahamu wao na kinyume cha mwito wao. Kwa "chukizo hili lisilo la kibinadamu" kama vile Luther baadaye alilitia "kuonyesha dalili ya mbwa mwitu zaidi na mjeuri kuliko ya Mkristo na mtu, "ilivyokuwa" mioyo ya watoto ikiwa migumujuu ya wazazi wao.

Hata wanafunzi katika vyuo vikubwa (universites) walidanganywa na watawa na kuvutwa kwa kuungana namaagizo yao. Mara waliponaswa katika mtego ilikuwa haiwezekani kupata uhuru. Wazazi wengi walikataa kutuma vijana wao katika vyuo vikubwa. Vyuo vikazoofika, na ukosefu wa elimu ukaenea pote.

Papa akatoa kwa watawa hawa uwezo kwa kusikia maungamo na kutoa rehema-shina la uovu mkubwa. Wakageuka kwa kuzidisha faida zao, watu waliojitenga kwa mambo ya kidunia walikuwa tayari kabisa kutoa masamaha hata wavunja sheria walikuwa wakienda mara kwa mara kwao, na makosa mabaya zaidi yakaongezeka kwa haraka. Zawadi zilizopasa kusaidia wagonjwa na maskini zikaenda kwa watawa. Utajiri wa watu waliojitenga kwa mambo ya kidunia ukaongezeka daima, na majumba yao makubwa na meza za anasa vikaonyesha zaidi kuongezeka kwa umaskini kwa
[32] taifa. Huku watawa wakaendelea kukaza uwezo wao juu yawengi waliokuwa katika imani ya uchawi na wakawaongoza kuamini kuwa kazi yote ya dini iliyoonyesha ukubali wa mamlaka ya Papa, kusujudu watakatifu, kufanya zawadi kwa watawa, hili lilikuwa la kutosha kwa kujipatia nafasi mbinguni!

Wycliffe kwa maarifa safi, akashambulia mizizi ya uovu, kutangaza kwamba utaratibu wenyewe ni wa uongo na ulipaswa kuondolewa kabisa. Mabishano na maswali yalikuwa yakiamshwa. Wengi walikuwa wakiongozwa kujiuliza kwamba hawakupaswa kutafuta rehema zao kwa Mungu zaidi kuliko kwa askofu wa Roma. (Tazama Nyongezo). “Watawa na mapadri wa Roma,” wakasema, “wako wanatula kama ugonjwa unaoitwa (cancer), Mungu anapashwa kutuokoa, kama sivyo watu wataangamia”. Watawa waombezi waliojidai kwamba walikuwa wakifuata mfano wa Mwokozi, kutangaza kwamba Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakisaidiwa kwa ajili wema wa watu. Madai haya yakaongoza watu wengi kwa Biblia kujifunza ukweli wao wenyewe.

Wycliffe akaanza kuandika na kuchapa vimakaratasi na tuvitabu juu ya watawa, kuita watu kwa mafundisho ya Biblia na Muumba wake. Si kwa njia ingine bora kuliko angeweza kutumia kwa kumuangusha yule mnyama mkubwa ambaye Papa alimufanyiza, na ndani yake mamilioni waliokamatwa watumwa.

Wycliffe alipoitwa kwa kutetea haki za ufalme wa Uingereza juu ya kujiingiza kwa Roma, alitajwa kuwa balozi wa kifalme katika inchi ya Hollandi. Hapo ilimfanya rahisi kupelekeana habari na mapadri kutoka Ufaransa, Italia, na Ispania, na alikuwa na bahati ya kutazama nyuma matukio yaliyofichwa kwake huko Uingereza. Katika wajumbe hawa kutoka kwa baraza ya hukumu ya Papa akasoma tabia ya kweli ya serekali ya kanisa. Akarudi Uingereza

kukariri mafundisho yake ya kwanza na juhudi kubwa, kutangaza kuwa kiburi na udanganyifu vilikuwa miungu ya Roma.

Baada ya kurudi Uingereza, Wycliffe akapokea kutoka kwa mfalme kutajwa kuwa kasisi ya Lutterworth. Jambo hili lilikuwa uhakikisho kwamba mfalme alikuwa bado hajachukiwa na kusema kwake kwa wazi. Muvuto wa Wycliffe ukaonekana katika muundo wa imani ya taifa.

Radi za Papa zikatupwa upesi juu yake. Matangazo matatu ya Papa yakatumwa kuamuru mipango ya gafula ya kunyamazisha mwalimu wa "upinzani wa mafundisho ya dini"

Kufika kwa matangazo ya Papa kukawekwa agizo katika Uingereza pote kufungwa kwa mpinga wa dini. (Tazama Nyongezo). Ilionekana kweli kwamba Wycliffe alipashwa kuanguka upesi kwa [33]
kisasi cha Roma. Lakini yeye aliyetangaza kwa mmojawapo wa zamani, "usiogope ...: mimi ni ngabo yako" (Mwanzo 15:1), akanyosha mkono wake kulinda mtumishi wake. Kifo kikaja, si kwa Mtengenezaji, lakini kwa askofu aliyeamuru uharibifu wake.

Kifo cha Gregoire XI kulifuatwa na uchaguzi wa mapapa wawili wapinzani. (Tazama Nyongezo). Kila mmoja akaita waaminifu wake kufanya vita kwa mwengine, kukaza maagizo yake ya hofu kuu juu ya wapinzani wake na ahadi za zawadi mbinguni kwa wafuasi wake. Makundi ya wapinzani yalifanya yote yaliweza kufanya mashambuliano mmoja kwa mwengine, na Wycliffe kwa wakati ule alikuwaakipumzika.

Mutengano pamoja na bishano yote na uchafu ambayo vilitayarisha njia kwa Mategenezo kwa kuwezesha watu kuona hakika hali ya kanisa la Roma. Wycliffe akaita watu kuzania kama mapapa hawa wawili hawakuwa wakisemea ukweli katika kuhukumiana mmoja kwa mwengine kama mpinga Kristo.

Akakusudia kwamba nuru inapaswa kuenezwa kila pahali katika Uingereza, Wycliffe akatengeneza kundi la wahubiri, kujishusha, watu waliojitoa waliopenda ukweli na kuamania kuipanua. Watu hawa walikuwa wakifundisha katika barabara za miji mikubwa,na katika njia inchini, wakitafuta wazee, wagonjwa, na maskini, na wakawafungulia habari za furaha za neema ya Mungu.

Kule Oxford, Wycliffe akahubiri Neno la Mungu ndani ya vyumba vikubwa vya chuo kikuu. Akapata cheo cha Daktari (Docteur) wa injili. Lakini kazi kubwa mno ya maisha yake ilikuwa

kutafsiri kwa Maandiko katika lugha ya Kiingereza, ili kila mtu katika Uingereza aweze kusoma kazi za ajabu za Mungu.

### Anashambuliwa na Ugonjwa wa Hatari

Lakini kwa gafula kazi zake zikasimamishwa. Ingawa alikuwa hajaeneza miaka makumi sita, taabu isiyokoma, kujifunza, na mashambulio ya maadui yalilegeza nguvu zake nakumfanya aonekane mzee upesi. Akashambuliwa na ugonjwa wa hatari. Watawa walifikiri kwamba atatubu kwa uovu alioufanya kwa kanisa, na wakaenda haraka kwa chumba chake ili wasikilize maungamo yake. "Unakuwa na kifo kwa midomo yako", wakasema; "uguswe basi kwa makosa yako, na ukane mbele yetu mambo yote uliyosema kwa hasara yetu".

Mtengenezaji akasikiliza kwa utulivu. Ndipo akamwambia [34] mlinzi wake kumuinua katika kitanda chake. Katika kuwakazia macho kwa imara, akasema katika sauti hodari ya nguvu ambayo ilikuwa ikiwaletea kutetemeka mara kwa mara, "Sitakufa, bali nitaishi; na tena nitatangaza matendo maovu ya watawa". Waliposhangazwa na kupata haya, watawa wakatoka chumbani kwa haraka.

Wycliffe aliishi kwa kuweka katika mikono wana inchi wake silaha za nguvu sana kwa kupinganisha Roma-Biblia, mjumbe wa mbinguni waliyewekwa kwa kutoa utumwani, kuangazia na kuhubiri watu. Wycliffe alijua kwamba ni miaka michache tu ya kazi iliyobaki kwake; aliona upinzani aliopashwa kukutana nao; lakini kwa kutiwa moyo na ahadi za Neno la Mungu, akaendelea. Katika nguvu zote zake za akili, na tajiri kwa matendo, alitayarishwa na maongozi ya Mungu kwa jambo hili, kazi yake kubwa kuliko zote. Mtengenezaji katika nyumba yake ya ukasisi huko Lutterworth, alizarau wimbi lililosirika, akajitia mwenyewe kwa kazi yake aliyoichagua.

Mwishowe kazi ikatimilika-tafsiri ya kwanza ya Biblia kwa kingereza. Mtengenezaji akaweka katika mikono ya watu wa Kiingereza nuru ambayo haipashwi kuzimishwa kamwe. Alifanya mengi zaidi kuvunja vifungo vya ujinga na kufungua na kuinua inchi yake kuliko ilivyo kwisha kufanyiwa na washindi kwa shamba za vita.

Ni kwa kazi ya taabu tu nakala za Biblia ziliweza kuzidishwa. Mapezi yalikuwa makubwa sana kupata kitabu kile, kwa sababu

ilikuwa vigumu kwa wenye kufanya nakala kuweza kumaliza maombi ya watu. Wanunuzi watajiri walitamani Biblia nzima. Wengine wakanunua tu kipande. Katika hali nyingi, jamaa zilijiunga kununua nakala moja. Biblia ya Wycliffe kwa upesi ikapata njia yake nyumbani mwa watu.

Wycliffe sasa akafundisha mafundisho ya kipekee ya Kiprotestanti-wokovu kwa njia ya imani katika Kristo na haki moja tu ya Maandiko. Imani mpya ikakubaliwa karibu nusu ya Wangereza.

Tokeo la Maandiko likaleta hofu kwa watawala wa kanisa. Wakati ule hapakuwa na sheria katika inchi ya Uingereza ya kukataza Biblia, kwa sababu ilikuwa haijaandikwa bado katika lughanyingine. Sheria za namna ile zilifanyika baadaye na zikakazwa kwa nguvu.

Tena waongozi wa papa wakafanya shauri mbaya kwa kunyamazisha sauti ya Mtengenezaji. Kwanza, mkutano wa waaskofu ukatangaza maandiko yake kuwa ya kupinga mafundisho ya dini. Walipovuta mfalme kijana, Richard II, upande wao, wakapata agizo la kifalme kufunga wote wanaohukumu mafundisho yaliyokatazwa na Roma.

Wycliffe akaitwa toka kwa mkutano kwenda kwa baraza kuu la [35]
taifa (parlement). Kwa uhodari akashitaki serkali ya Kanisa la Rome mbele ya baraza la taifa na akaomba matengenezo ya desturi mbaya zilizotolewa na kanisa. Adui zake wakakosa lakufanya. Ilikuwa ikitazamiwa kwamba Mtengenezaji, katika miaka yake ya uzee, peke yake bila rafiki, angeinama kwa mamlaka ya mfalme. Lakini baadala yake, Baraza likaamsha na mwito wa kugusa moyo uliofanywa na ghasia (makelele) za Wycliffe, ukavunja amri ya kuteso, na Mtengenezaji alikuwa huru tena.

Mara ya tatu aliletwa hukumunu, na mbele ya mahakama makuu ya Kanisa ya kifalme. Hapa sasa kazi ya Mtengenezaji itasimamishwa. Hii ilikuwa mawazo ya wafuasi wa Papa. Kama walitimiza kusudi zao, Wycliffe atatoka katika nyumba ya hukumu na na kuelekea kwenye nyali za moto.

### Wycliffe Anakataa Kukana

Lakini Wycliffe hakukana. Pasipo hofu akashikilia mafundisho yake na sukumia mbali mashitaka ya watesi wake. Akaalika wasik-

ilizi wake mbele ya hukumu la Mungu na akupima uzito wa madanganyo na wongo wao katika mizani ya ukweli ya milele. Uwezo wa Roho Mtakatifu ulikuwa juu ya wasikilizaji. Kama mishale kutoka kwa mfuko wa mishale ya Bwana, maneno ya Mtengenezaji yakatoboa mioyo yao. Mashitaka ya upinga dini, waliyoyaleta juu yake, akayarudisha kwao.

"Pamoja na nani, munavyo fikiri," akasema, "munayeshindana naye? na mzee anaye kuwa kwa ukingo wa kaburi? la! pamoja na ukweli-Ambayo unakuwa na nguvu kuliko wewe, na utakushinda". Aliposema vile, akatoka na hata mtu moja wa maadui zake hakujaribu kumzuia.

Kazi ya Wycliffe ilikuwa karibu kutimizwa, lakini mara nyingine tena alipashwa kutoa ushuhuda wa injili. Aliitwa kwa kusikilizwa mbele ya baraza la kuhukumu la kipapa kule Roma, ambalo kila mara lilikuwa likimwanga damu ya watakatifu. Msiba wa kupooza ulizuia safari ile. Lakini ingawa sauti yake haikuweza kusikiwa pale Roma, aliweza kusema kwa njia ya barua. Mtengenezaji akamwandikia Papa barua, ambayo, ingawa ya heshima na kikristo moyoni, ilikuwa kemeo kali kwa ukuu na kiburi kya jimbo la Papa.

Wycliffe akaonyesha kwa Papa na maaskofu wake upole na unyenyekevu wa Kristo, muonyesha wazi si kwao tu bali kwa miliki ya Wakristo wote tofauti kati yao na Bwana ambaye wanajidai kuwa wajumbe wake.

[36] Wycliffe alitumainia kabisa kwamba maisha yake yangekuwa bei ya uaminifu wake. Mfalme, Papa na maaskofu wakajiunga kwa kutimiza maangamizi yake, na ilionekana kweli kwamba kwa mda wa miezi michache ikiwezekana wangemletea kifo kwa ajili ya imani ya dini. Lakini uhodari wake ulikuwa imara.

Mtu ambaye kwa wakati wote wa maisha yake alisimama imara katika kutetea ukweli hakuna mtu wakusumbuliwa kwa ajili ya adui zake. Bwana alikuwa mlinzi wake; na sasa, wakati adui zake walipohakikisha kupata mawindo yao, mkono wa Mungu ukamuhamisha mbali yao. Katika kanisa lake huko Lutterworth, wakati alipotaka kufanya ibada ya meza ya Bwana, akaanguka na kupinga kupooza communion), anakauka viungo, na kwa wakati mfupi akakata roho yake.

## Mpinga Mbiu wa Wakati wa Sasa

Mungu alitia neno la ukweli katika kinywa cha Wycliffe. Maisha yake yalilindwa na kazi zake zikazidishwa hata msingi ukawekwa kwa ajili ya Matengenezo (Reformation). Hapakuwa mtu aliyekwenda mbele ya Wycliffe ambaye kwa kazi yake aliweza kutengeneza utaratibu wake wa matengenezo. Alikuwa mpinga mbiuwa wakati wa sasa. Bali katika ukweli ambayo alioonyesha, kulikuwa umoja na ukamilifu ambao watengenezaji waliofuata hawakuzidisha, na ambao wengine hawakuufikia. Mjengo ulikuwa imara na wa kweli, hata hapakuwa na mahitaji ya kugeuzwa na wale waliokuja baada yake.

Kazi kubwa ambayo Wycliffe alianzisha ni kufungua mataifa yaliyofungwa na Roma wakati mrefu iliyokuwa na msingi wake katika Biblia. Hapa ndipo chemchemi ya kijito cha mibaraka kilicho tiririka tokea zamani za miaka tangu karne ya kumi na ine. Aliye fundishwa kuona Roma kama utawala usiekuwa na kosa na kukubali heshima isiyokuwa na swali kwa heshima ya mafundisho na desturi za miaka elfu, Wycliffe akageukia mbali na mambo haya yote ili kusikiliza Neno Takatifu la Mungu. Badala ya kanisa inayosema kwa njia ya Papa, alitangaza mamlaka moja tu ya kweli kuwa sauti ya Mungu inayosema kwa njia ya Neno lake. Na alifundisha kwamba Roho Mtakatifu ndiyo mtafsiri wake pekee.

Wycliffe alikuwa mmoja wapo wa Watengenezaji wakubwa. Alikuwa sawa sawa na wachache waliokuja nyuma yake. Usafi wa maisha, juhudi imara katika kujifunza na kazi, uaminifu daima, na upendo kama ule wa Kristo, vilikuwa tabia ya mtangulizi wa watengenezaji wa kwanza. [37]

Biblia ndiyo iliyomfanya vile alivyokuwa. Majifunzo ya Biblia itakuza kile fikara, mawazo ya ndani, na mvuto wa roho ambao kujifunza kwengine hakuwezi. Hutoa msimamo wa kusudi, uhodari na ushujaa. Juhudi, kujifunza kwa heshima kwa Maandiko hutolea ulimwengu watu wa akili nyingi, pia na wa kanuni bora, kuliko hekima ya kibinadamu.

Wafuasi wa Wycliffe, walijulikana kama "Wycliffites" na "Lollards", wakatawanyika kwa inchi zingine, wakichukua injili. Sasa kwa sababu mwongozi wao aliondolewa, wahubiri wakatumika na juhudi nyingi kuliko mbele. Matukano makubwa wakaja kusikiliza.

Wengine wa cheo kikubwa, na hata bibi wa mfalme, walikuwa miongoni mwa waliogeuka. Katika pahali pengi mifano ya sanamu ya dini ya Roma iliondolewa kutoka ndani ya makanisa.

Lakini mateso makali yakazukia kwa wale waliosubutu kukubali Biblia kama kiongozi chao. Kwa mara ya kwanza katika historia ya inchi ya Uingereza amri ya kifocha wafia upinzani wa kufungia watu wa dini kiliamriwa juu ya wanafunzi wa injili. Kifo ao mateso ya wafia dini ikafuatana na kufuatana. Wakawindwa kama adui za kanisa na wasaliti wa nchi, wateteaji wa ukweli wakaendelea kuhubiri katika mahali pa siri, kutafuta kimbilio katika nyumba za maskini, na mara nyingi kujificha mbali ndani ya matundu na mapango.

Ukimia, uvumilivu, wa kutokubali uchafu wa imani ya dini ukaendelea kuenezwa kwa karne nyingi. Wakristo wa wakati ule wa mwanzo walijifunza kupenda Neno la Mungu na kwa uvumilivu waliteswa kwa ajili yake. Wengi wakatoa mali yao ya kidunia kwa ajili ya Kristo. Wale walioruhusiwa kukaa katika makao yao kwa furaha wakakaribisha ndugu zao waliofukuzwa, na wakati wao pia walipofukuzwa, wakakubali kwa furaha ya waliotupwa. Hesabu haikuwa ndogo ya waliojitoa bila woga ushuhuda kwa ukweli katika gereza za hatari na katikati ya mateso na miako ya moto wakifurahi kwamba walihesabiwa kwamba walistahili kujua "ushirika wa mateso yake". Machukio ya watu wa Papa hayakuweza kutoshelewa wakati mwili wa Wycliffe ulidumu katika kaburi. Zaidi ya miaka makumi ine baada ya kufa kwake, mifupa yake ikafufuliwa na ikaunguzwa mbele ya watu, na majibu yake ikatupwa kwa kijito kando kando. "Kijito hiki", asema mwandishi mzee,majifu yake "yakachukuliwa katika Avon, Avon katika Severn, Severn katika bahari nyembamba, bahari nyembamba katika bahari kubwa. Na kwa hivyo majifu ya Wycliffe inakuwa mfano wa mafundisho yake,
[38] ambayo sasa yametawanyika ulimwenguni mwote."

Katika mafundisho ya Wycliffe, Jean Huss wa Bohemia aliongozwa kuachana na makosa mengi ya kanisa la Roma. Kutoka Bohemia kazi ikapanuka kwa inchi zingine. Mkono wa Mungu ulikuwa ukitayarisha njia kwa ajili ya Matengenezo makubwa.

# 6 /KIFO KIMEWAFIKIA MACHONI WASHUJAA WAWILI [39]

Mwanzoni kwa karne ya tisa Biblia ilikuwa imekwisha kutafsiriwa na ibada ya watu wote ikafanyika katika lugha ya watu wa Bohemia. Lakini Gregoire VII alikusudia kuweka watu utumwani, na tangazo likatolewa kukataza ibada ya watu katika lugha ya Kibohemia. Papa akatangaza kwamba "ilikuwa ni furaha kwa Mwenye enzi yote kwamba ibada yake ifanyiwe katika lugha isiyojulikana." Lakini Mungu anaweka tayari wajumbe kwa kulinda kanisa. Wavaudois wengi na Waalbigenses, walipofukuzwa kwa ajili ya mateso, wakaja Bohemia. Wakatumika kwa bidii katika siri. Kwa hiyo imani ya kweli ikalindwa.

Mbele ya siku za Huss kulikuwa watu katika Bohemia waliohukumu machafu ndani ya kanisa. Vitisho vya serkali ya kanisa vikaamshwa, na mateso yakafunguliwa juu ya injili. Baada ya mda ikaamriwa kwamba wote waliotoka kwa ibada ya kanisa la Roma walipaswa kuchomwa. Lakini Wakristo, wakaendelea mbele kushinda kwa kusudi lao. Mmoja akatangaza alipokuwa akifa, "Kutainuka mmoja kutoka miongoni mwa watu, bila upanga wala mamlaka, na juu yake hawataweza kumushinda." Tayari mmoja alikuwa akipanda, ambaye ushuhuda wake wa kupinga Roma utashitusha mataifa.

Yohana Huss alikuwa mnyenyekewa tangu kuzaliwa na alikuwa ameachwa mapema yatima kwa ajili ya kifo cha baba yake. Mama yake mtawa, kuzania elimu na kuogopa ya Mungu kama hesabu kuwa thamani ya vile tunavyo, akatafuta kulinda urithi huu kwa ajili ya kijana wake. Huss alijifunza kwa chuo cha jimbo, baadaye akaenda kwa chuo kikubwa (universite) kule Prague, kwa sababu ya umaskini wake akapokelewa kwa bure.

Kwa chuo kikubwa, kwa upesi Huss akajitofutisha kwa ajili ya maendeleo yake ya upesi. Upole wake, alipokwisha kupata mwenendo (tabia) ukampatia heshima ya ulimwengu. Alikuwa mshiriki mwaminifu wa Kanisa la Roma na mwenye kutafuta na

juhudi mibaraka ya kiroho. Kanisa la Roma linajidai kutoa. Baada ya kutimiza majifunzo yake ya college, akaingia katika ukasisi (upadri). Kwa haraka alipofikia cheo kikuu, akapelekwa kwa jumba la mfalme. Akafanywa pia mwalimu (fundi) wa chuo kikuu na baadaye mkuu wa chuo kikuu (recteur). Mwanafunzi mwema munyenyekevu akawa kiburi cha inchi yake, jina lake likajulikana po pote katika Ulaya.

[40] Jerome, ambaye baadaye alishirikiana na Huss, akaleta toka Uingereza maandiko ya Wycliffe. Malkia wa Uingereza, aliyegeuzwa na mafundisho ya maisha ya Wycliffe, alikuwa binti wa mfalme wa Bohemia. Kwa njia ya mvuto wake kazi za Mtengenezaji zikatangazwa sana katika inchi yake ya kuzaliwa. Huss akainama na kukubali kwa heshima matengenezo yaliyoletwa. Tayari, ingawa hakuijua, akaingi kwa njia ambayo iliweza kumwongoza mbali sana ya Roma.

### Picha mbili Inamvuta Huss

Kwa wakati huu, wageni wawili kutoka Uingereza, watu wa elimu, walipokea nuru na wakaja kuieneza katika Prague. Kwa upesi wakanyamazishwa, lakini kwa sababu hawakutaka kuacha kusudi lao, wakatafuta mashauri mengine. Walipokuwa wafundi pia wahubiri, katika mahali wazi mbele ya watu wakachora picha mbili. Moja ikaonyesha kuingia kwa Kristo katika Yerusalema, “Mpole, naye amepanda mwana punda” (Matayo 21:5) na akafuatwa na wanafunzi wake katika mavazi ya kuzeeka juu ya safari na miguu wazi. Picha ingine ilieleza mwandamano wa askofu-papa katika kanzu zake za utajiri na taji tatu, mwenye akapanda farasi ambaye amepambwa vizuri sana, ametanguliwa na wapiga tarumbeta na kufuatwa na wakuu wa baraza ya papa (cardinals) na maaskofu katika mavazi ya kifalme.

Makutano yakaja kutazama mapicha. Hapana mtu aliweza kushindwa kusoma maana. Kukawa makelele mengi katika Prague, na wageni wakaona kwamba inafaa kuondoka. Lakini picha ikaleta wazo kubwa kwa Huss na ikamwongoza karibu sana na uchunguzi wa Biblia na wa maandiko ya Wycliffe.

Ingawa alikuwa hakujitayarisha bado kukubali matengenezo yote yaliyotetewa na Wycliffe, aliona tabia ya kweli ya kanisa la

Roma, na akalaumu kiburi, tamaa ya nguvu, na makosa ya mamlaka ya dini.

### Prague Ikawekwa Chini ya Makatazo

Habari zikapelekwa Roma, na Huss akaitwa kwa kuonekana mbele ya Papa. Kutii kungalileta kifo cha kweli. Mfalme na malkia wa Bohemia, chuo kikuu, washiriki wa chuo kikuu, na wakuu wa serkali, wakajiunga katika mwito kwa askofu kwamba Huss aruhusiwe kubaki huko Prague na kujibu kwa njia ya ujumbe. Baadaye, Papa akaendelea kuhukumu nakulaumu Huss, na akatangaza mji wa Prague kuwa chini ya makatazo. [41]

Katika mwaka ule hukumu hii ikatia kofu. Watu walimuzania Papa kama mjumbe wa Mungu, wa kushika funguo za mbingu na jehanamu na kuwa na uwezo kuita hukumu. Iliaminiwa kwamba mpaka ilipaswa kupendeza Papa kutosha laana, wafu wangefungiwa kutoka kwa makao ya heri. Kazi zote za dini zikakatazwa. Makanisa yakafungwa. Ndoa zikaazumishwa katika uwanja wa kanisa. Wafu wakazikwa bila kanuni ndani ya mifereji ao mashambani.

Prague ikajaa na msukosuko. Kundi kubwa ya watu wakalaumu Huss na wakadai kwamba alazimiswe kwenda Roma. Kwa kutuliza makelele, Mtengenezaji akapelekwa kwa mda katika kijiji chake cha kuzaliwa. Hakuacha kazi zake, bali alisafiri katika inchi na kuhubiri makutano ya hamu kubwa. Wakati mwamsho katika Prague ulipotulia, Huss akarudi kuendelea kuhubiri Neno la Mungu. Adui zake walikuwa hodari, lakini malkia na wenye cheo kikuu wengi walikuwa rafiki zake, na watu katika hesabu kubwa wakamfuata.

Huss alisimama peke yake katika kazi yake. Sasa Jerome akajiunga katika matengenezo. Wawili hawa baadaye wakajiunga katika maisha yao, na katika mauti hawakuweza kuachana. Katika watu bora hawa ambao huleta nguvu ya kweli ya tabia, Huss alikuwa mkubwa zaidi. Jerome, kwa kujinyenyekea kwa kweli, akapata thamani yake na kunyenyekea kwa mashauri yake. Chini ya kazi zao za muungano matengenezo yakazambaa kwa upesi.

Mungu akaruhusu nuru kuangaza juu ya akili za watu hawa wateule, kuwafunulia makosa mengi ya Roma, lakini hawakupokea nuru yote ya kutolewa ulimwenguni. Mungu alikuwa akiongoza watu kutoka katika giza ya Kanisa la Roma, na akazidi kuwaon-

goza, hatua kwa hatua, namna waliweza kuichukua. Kama utukufu wote wa jua la azuhuri kwa wale waliodumu gizani mda mrefu, nuru kamili ingewaletea kurudi nyuma. Kwa hiyo aliifunua kidogo kidogo, jinsi ilivyowezekana kupokelewa na watu.

Matengano katika kanisa likaendelea. Mapapa watatu sasa walikuwa wakishindania mamlaka. Ushindano wao ukajaza jamii ya mataifa ya Wakristo wote machafuko. Hakutoshelewa na kuvurumisha laana, kila mmoja ni kununua silaha na kupata waaskari. Kwa kweli feza ziweko; kwa kupata hizi, zawadi, fazili, na mibaraka ya kanisa yalitolewa kwa ajili ya biashara. (Tazama Nyongezo)

Pamoja na uhodari ulioongezeka Huss akapiga ngurumo juu ya machukizo yaliyo vumiliwa katika jina la dini. Watu wakashitaki Roma wazi wazi kuwa chanzo cha shida iliyoharibu miliki ya kikristo.

Tena Prague ilionekana kukaribia ugomvi wa damu. Kama
[42] katika miaka ya zamani, mtumishi wa Mungu walishitakiwa kuwa "yeye mtaabishaji wa Israeli". 1 Wafalme 18:17. Mji ukawekwa tena chini ya mkatazo, na Huss akarudishwa tena katika kijiji chake cha kuzaliwa. Akasema kuanzia mahali pa kubwa sana pa wazi, kwa jamii ya Wakristo wote, kabla ya kukata roho yake kama mshuhuda kwa ajili ya ukweli.

Baraza kubwa likaitwa kukutana kule Constance (Udachi wa kusini na magharibi), likaitwa kwa mapenzi ya mfalme Sigismund na mmoja wapo wa mapapa wapinzani watatu, Yohana XXIII. Papa Yohana, ambaye tabia yake na maongozi yaliweza kufanya uchunguzi mbaya, hakusubutu kupinga mapenzi ya Sigismund. (Tazama Nyongezo). Makusudi makuu yaliyopashwa kutimizwa yalikuwa kuponya msukosuko katika kanisa kungoa mafundisho ya imani yasiyopatana na yale yaliyotangazwa na kanisa kuwa kweli. Wapinzani wawili hawa wa Papa wakaitwa kwenda mbele pamoja na John Huss. Wa kwanza walituma wajumbe wao. Papa John akaja na mashaka mengi, kuogopa kuhesabiwa kwa makosa ambayo yalileta haya kwa taji pia kwa ajili ya zambi zilizo ilinda. Huku alifanya kuingia kwake katika mji wa Constance na baridi kubwa, lililofanyiwa na mapadri na maandamano ya wafuasi wa mfalme. Juu ya kichwa chake chandarua cha zahabu, kuchukuliwa na waamuzi wane wakubwa. Mwenyeji (host) aliletwa mbele yake, na kupambwa kwa

utajiri wa wakuu (cardinals) na watu wa cheo kikubwa vika urembo wakushangaza.

Wakati ule ule msafiri mwengine alikuwa akikaribia Constance. Huss aliachana na rafiki zake kama kwamba hawataonana tena, kufikiri vile safari yake ilikuwa ikimwongoza kwa kingingi (mti wa kufungia watu wa kuchomwa moto). Alipata hati (ruhusa ya kupita) kwa mfalme wa Bohemia na hati ingine vile vile kwa mfalme Sigismund. Lakini alifanya matengenezo yake yote katika maoni yanayoweza kuelekea kifo chake.

## Mwenendo wa Salama Kutoka kwa Mfalme

Katika barua kwa rafiki zake akasema: "Ndugu zangu, ... nimefanya safari pamoja na mwenendo wa usalama kutokuwa ya mfalme kwakukutana na maadui wangu wengi wa kibinadamu. ... Yesu Kristo aliteswa kwa ajili ya wapenzi wake; na kwa hiyo hatupaswe kushangazwa kwamba alituachia mfano wake? ... Kwa hiyo, wapenzi, kama kifo changu kinapaswa kutoa sehemu kwa utukufu wake, naomba kwamba kipate kunifikia upesi, na kwamba aweze [43]
kuniwezesha kuvumilia mateso kubwa yangu yote kwa uaminifu. ... Hebu tuombe kwa Mungu ... kwamba nisipate kuvunja haki hata ndogo ya ukweli ya injili, ili nipate kuacha mfano bora utakao fuatwa na ndugu zangu."

Katika barua ingine, Huss alisema kwa unyenyekevu wa makosa yake mwenyewe, kujishitaki mwenyewe "kwa kupendezwa kwa kuvaa mavazi ya utajiri na kuweza kupoteza wakati katika shuguli zisizo na maana." Ndipo akaongeza, "hebu utukufu wa Mungu na wokovu wa mioyo utawale akili yako, na si upato wa faida na mashamba. Epuka kuipamba nyumba yako zaidi ya roho yako; na, juu ya yote, toa uangalifu wako kwa kiroho. Uwe mtawa na mpole na maskini, na usimalize chakula chako katika kufanya karamu."

Huko Constance, Huss alipewa uhuru kamili. Kwa mwenendo wa salama wa mfalme kuliongezwa uhakikisho wa ulinzi wa Papa. Lakini, katika mvunjo wa metangazo haya yaliyokuwa yakikaririwa, kwa mda mfupi Mtengenezaji akufungwa kufuatana na agizo la Papa na wakuu (cardinals) na kusukumwa ndani ya gereza mbaya la chini ya ngome. Baadaye akahamishwa kwa ngome ya nguvu ngambo ya mto Rhine na huko mfungwa alikuwa akilindwa. Papa

kwa upesi baadaye akawekwa kwa gereza ile ile. Alishuhudiwa kuwa mwenye hatia ya makosa mabaya, kuua mtu kwa kusudi zaidi, kufanya biashara ya mambo matakatifu ya dini, na uzinzi, "zambi zisizofaa kutajwa." Baadaye akanyanganywa taji lake. Mapapa wapinzani pia wakaondolewa, na askofu mpya akachaguliwa.

Ingawa pape mwenyewe alikuwa mwenye hatia ya makosa makubwa kuliko Huss aliyoyaweka juu ya mapadri, bali ni baraza lile lile lililoondoa cheo cha askofu likadai kuangamiza Mtengenezaji. Kifungo cha Huss kikaamsha hasira nyingi katika Bohemia. Mfalme, alipokataa kuvunja mwenendo wa usalama, akapinga mambo juu yake. Lakini maadui wa Mtengenezaji wakaendelea kuleta mabishano kushuhudia kwamba "imani haipaswi kushikwa pamoja na asiyefundisha makwa ya kanisa ao mtu anayezaniwa na upinzani wamafundisho ya kanisa, hata wakiwa watu wanoakuwa na mwenendo wa usalama kutoka kwa mfalme na wafalme."

Kuwa mzaifu sababu ya ugonjwa-gereza lenye baridi na maji maji likaleta homa ambayo karibu kumaliza maisha yake-mwishowe Huss akaletwa mbele ya baraza. Mwenye kufungwa minyororo akasimama mbele ya mfalme, ambaye juu ya imani nzuri aliyokuwa nayo aliaahidi kumlinda. Akashikilia ukweli kwa nguvu na kutoa ushuhuda wa kutokubali maovu ya waongozi wa dini. Akashurutishwa kuchagua au kukana mafundisho yake ao kuuwawa,
[44] akakubali kifo cha wafia dini.

Neema ya Mungu ikamsaidia. Mda wa juma ya kuteseka kabla ya hukumu ya mwisho, amani ya mbinguni ikajaa rohoni mwake. "Ninaandika barua hii", akasema kwa rafiki, "katika gereza langu, na mkono wangu katika minyororo, kutazamia hukumu yangu ya kifo kesho. ... Wakati, kwa msaada wa Yesu Kristo, tutakutana tena katika amani ya kupendeza sana ya maisha yajayo, mtajifunza namna gani Mungu wa rehema amejionyesha mwenyewe mbele yangu, namna gani ya kufaa amenisaidia katikati ya majaribu na mashindano yangu."

### Ushindi Ulioonekana Mbele

Katika gereza hii ya chini ya ngome aliona ushindi wa imani ya kweli. Katika ndoto zake aliona Papa na maaskofu wakifuta

picha za Kristo alizofananisha kwa ukuta za kanisa ndogo huko Prague. "Njozi hii ilimsumbua: lakini kesho yake akaona wapaka rangi wengi walikuwa wakitumika katika kurudisha picha hizi katika hesabu kubwa na rangi zenye kung'aa. ... Wapaga rangi, ... wakazungukwa na makutano mengi, wakasema kwa nguvu, Sasa Papa na maaskofu waje; hawatayafuta tena kamwe!" Akasema Mtengenezaji, "Sura ya Kristo haitafutwa kamwe. Walitamani kuuharibu, lakini utapakaliwa tena, upya katika mioyo yote na wahubiri bora kuliko mimi mwenyewe."

Kwa wakati wa mwisho, Huss akapelekwa mbele ya baraza, mkutano mkubwa na kungaa--mfalme, watoto wa kifalme, makamu (deputes) ya kifalme, wakuu (cardinals) maaskofu-mapadri, na makundi makubwa.

Alipoitwa juu ya hukumu yake ya mwisho, Huss akatangaza makatao yake kuwa hata kana. Kwa kukazia macho mfalme ambaye kwa haya neno lake la ahadi halikutimizwa kamwe, akatangaza: "Nilikusudia, kwa mapenzi yangu, nionekane mbele ya baraza hili, chini ya ulinzi wa watu wote na imani ya mfalme anayekuwa hapa." Sigismuna akageuka uso kwa haya, namna macho ya wote yaligeuka kumwangalia.

Hukumu ilipokwisha kutangazwa, sherehe ya haya ikaanza. Tena akaombwa kukana. Huss akajibu, kwa kugeukia watu: "kwa uso gani, basi, napaswa kuangalia mbinguni? Namna gani naweza kuangalia makutano haya ya watu ambao nimewahubiri injili kamilifu? Sivyo; ninaheshimu wokovu wao zaidi kuliko mwili huu zaifu, am- [45]
bayo sasa unaamriwa kufa." Mavazi ya ukasisi yakavuliwa moja kwa moja, kila askofu kutamka laana wakati alipokuwa akitimiliza sehemu yake ya sherehe. Mwishowe, "wakaweka juu ya kichwa chake kofia ao kofia ya kiaskofu ya umbo la jengo la mawe ya kartasi, ambapo sanamu za kuogofya za pepo mbaya zilipakwa rangi, na neno "Mzushi mkuu" yenye kuonekana kwa mbali mbele. "Furaha kubwa kuliko," akasema Huss, "nitavaa taji la haya kwa ajili ya jina lako, o Yesu. Kwa ajili yangu ulivaa taji la miiba."

## Huss Alikufa Juu ya Mti (Mti wa kufungia Watu wa Kuchomwa na Moto wanapo kuwa Wahai)

Sasa akachukuliwa. Maandamano makubwa yakafuata. Wakati kila kitu kilikuwa tayari kwa ajili ya moto kuwashwa, mfia dini akashauriwa mioyo tena kuokoa maisha yake kwa kukana makosa yake. “Makosa gani”, akasema Huss, “nitakayokanusha? Najua mimi mwenyewe kwamba sina kosa. Namuita Mungu kushuhudia kwamba yote niliyoandika na kuhubiri ilikuwa na nia ya kuokoa myoyo kutoka zambini na kupotea milele; na, kwa hiyo, ‘furaha kubwa zaidi nitahakikisha kwa damu yangu ukweli ule ambayo nimeuandika na ku uhubiri.”

Wakati nyali za moto zilipowashwa kwa ajili yake, akaanza kuimba, “Yesu wewe Mwana wa Daudi, unihurumie”, na hivyo akaendelea hata sauti yake ikanyamazishwa milele. Mfuasi wa kanisa la Roma mwenye bidii, alipoelekeza mauti ao mateso ya wafia dini Huss, na Jerome, aliyekufa baadaye, akasema: “Walijitayarisha kwa moto kama kwamba walikuwa wakienda kwa karamu ya ndoa. Hawakutoa kilio cha maumivu. Wakati miako ilipopanda, wakaanza kuimba nyimbo; na mara haba ukali wa moto iliweza kukomesha kuimba kwao.”

Mwili wa Huss ilipoteketea, majifu yake yalikusanywa na kutupwa katika jito la Rhine na kupelekwa baharini ikiwa kama mbegu iliyotawanyika katika inchi zote za ulimwengu. Katika inchi zisizo julikana bado mbegu ile itazaa matunda mengi y kushuhudia ukweli. Sauti katika nyumba ya baraza la Constance likaamsha minongono ya kusikika miaka yote iliyofuata. Mfano wake utasaidia makundi ya watu wengi kusimama imara mbele ya mateso makali na kifo. Kifo chake kilionyesha wazi ubaya wa Roma. Maadui wa ukweli walikuwa wakisaidia shauri ambalo walikusudia kuangamiza!

Lakini damu ya mushuhuda mwengine ilipaswa kushuhudia ukweli. Jerome alikuwa akimshauria Huss kwa uhodari na nguvu,
[46] kutangaza kwamba kama ni lazima kwake kuanguka kwa hatari,
angeruka kwa kumsaidia. Aliposikia habari ya kufungwa kwa Mtengenezaji, mwanafunzi mwaminifu akajitayarisha kutimiza ahadi yake. Bila ruhusa mwenendo wa usalama akashika njia kwenda Constance. Alipofika, akasadiki kwamba alijiingiza yeye mwenyewe hatarini ya kupotea bila kuwa na namna ya kufanya

lolote kwa ajili ya Huss. Akakimbia lakini akafungwa na akarudishwa anapofungwa na minyororo. Kwa kutokea kwake kwa kwanza mbele ya baraza majaribio yake kwa kujibu yalikutana na makelele, "Kwa myako ya moto pamoja naye!" Akatupwa gerezani chini ya ngome na akalishwa mkate na maji. Mateso ya kufungwa kwake yakaleta ugonjwa na kutiisha maisha yake; na adui zake kuogopa kwamba angeweza kuwakimbia, wakamtendea si kwa ukali sana, japo akidumu katika gereza mda wa mwaka moja.

### Jerome Anatii Baraza

Mvunjo wa hati ya Huss ukaamsha zoruba ya hasira. Baraza ikakusudia kwamba, badala ya kuchoma Jerome, yafaa kumshurutisha kukana. Akapewa kuchagua kati ya mambo mawili kukana mambo ya kwanza au kufa juu ya mti. Alipo zoofishwa na ugonjwa, kwa ajali ya mitetemo ya gereza na mateso ya mashaka na wasi wasi, kutengana na marafiki, na kuhofishwa kwa ajili ya kifo cha Huss, nguvu za Jerome zikafifia. Akakubali imani ya kikatolika na uamuzi wa baraza uliohukumu wycliffe na Huss, lakini akasimamia "kweli takatifu" walizofundisha.

Lakini katika upekee wa gereza lake aliona wazi jambo alilofanya. Aliwaza juu ya uhodari na uaminifu wa Huss na akafikiri kukana kwake mwenyewe kwa ukweli. Akafikiri habari ya Bwana Mungu ambaye kwa ajili yake mwenyewe alivumilia msalaba. Kabla ya kukana kwake alipata usaada ndani ya mateso katika hakikisho la wapenzi wa Mungu, lakini sasa majuto na mashaka yakatesa roho yake. Alijua kwamba mambo ya kujikana kwingine yalipaswa kufanywa kabla ya yeye kuweza kuwa na amani pamoja na Roma. Njia ambayo aliingia ilipaswa kuishia tu katika ukufuru kamili.

### Jerome Anapata Toba na Uhodari Mpya

Upesi akapelekwa tena mbele ya baraza. Waamzi hawakutoshelewa na kujitaa kwake. Ila tu kwa kukataa wazi wazi kwa ukweli ndipo Jerome angaliweza kuokoa maisha yake. Lakini alikusudia kukubali imani yake na kufuata ndugu yake mfia dini kwa miako [47]
ya moto.

Alikataa kujikania kwake kwa kwanza na, kama mtu mwenye kufa, akadai kwa heshima apewe bahati ajitetee. Maaskofu wakashikilia kwamba angekubali tu ao kukana mashitaka yaliyoletwa juu yake. Jerome akakataa juu ya udanganyifu kama ule. “Mumenishika bila kusema siku mia tatu na makumi ine katika gereza la kutiisha,” akasema; “Munanileta basi mbele yenu, na kutoa sikio lenu kwa adui zangu za kibinadamu, munakataa kunisikia. ... Mujihazari kuto kufanya zambi juu ya haki. Lakini mimi, niko binadamu zaifu; maisha yangu ni ya maana kidogo; na ninapo waonya si kwa kutoa hukumu isiyo kuwa ya haki, nasema machache kwa ajili yangu mwenyewe kuliko kwa ajili yenu.”

Maombi yake mwishowe yakakubaliwa. Mbele ya waamzi wake, Jerome akapiga magoti na akaomba kwamba Roho ya Mungu ipate kutawala mawazo yake, ili asiweze kusema kitu cho chote kinacho kuwa kinyume cha ukweli ao kisichofaa kwa Bwana wake. Kwake siku ile ahadi ikatimia “Wakati wanapowapeleka ninyi, musisumbuke namna gani ao neno gani mutakalolisema; kwa sababu mutapewa saa ile neno mutakalosema. Kwa maana si ninyi munaosema, lakini Roho ya Baba yenu anayesema ndani yenu.” Matayo 10:19, 20.

Kwa mwaka wote mzima Jerome alikuwa katika gereza, bila kuweza kusoma ao hata kuona. Kwani maneno yake yalitolewa kwa hali ya kuwa na mwangaza sana na uwezo kama kwamba hakusumbuliwa wakati kwa kujifunza. Akaonyesha wasikilizi wake mstari mrefu wa watu watakatifu waliohukumiwa na waamzi wasiohaki. Karibu kila kizazi wale waliokuwa wakitafuta kuinua watu wa wakati wao wakafukuzwa. Kristo mwenyewe alihukumiwa kama mfanya maovu kwa baraza la hukumu lisiyo haki.

Jerome sasa akatangaza toba yake na kutoa ushuhuda kwamba Huss hana kosa na kwamba ni mtakatifu. “Nilimjua tokea utoto wake,” akasema. “Alikuwa mtu bora zaidi, mwenye haki na mtakatifu; alihukumiwa, ijapokuwa hakuwa na kosa ... niko tayari kwa kufa. Sitarudia nyuma mbele ya maumivu mabaya yale yanayotayarishwa kwa ajili yangu na adui zangu na mashahidi wa uongo, ambao siku moja watatoa hesabu ya mambo yao ya ujanja mbele ya Mungu Mkuu, ambaye hakuna kitu kinaweza kudanganya.”

Jerome akaendelea: “Kwa zambi zote nilizozifanya tangu ujana wangu, hakuna moja inayokuwa na uzito sana katika akili yangu, na

kuniletea majuto makali, kama ile niliyofanya katika mahali hapa pa kufisha, wakati nilipokubali hukumu mbaya sana iliyofanywa juu ya Wycliffe, na juu ya mfia dini mtakatifu, John Huss, bwana [48] wangu na rafiki yangu. Ndiyo! Ninatubu kutoka moyoni mwangu, na natangaza kwa hofu kuu kwamba nilitetemeka kwa haya sababu ya hofu ya mauti, nililaumu mafundisho yao. Kwa hiyo ni naomba ... Mwenyezi Mungu tafazali unirehemu zambi zangu, na hii kwa upekee, mbaya kuliko zote."

Kuelekeza kwa waamuzi wake, akasema kwa uhodari, "Muliwahukumu Wycliffe na John Huss ... mambo ambayo walihakikisha, na yasiyo ya udanganyifu, nafikiri, pia vile vile na kutangaza, kama wao."

Maneno yake yakakatwa. Maaskofu wakitetemeka na hasira, wakapaza sauti: "Haja gani iko pale ya ushuhuda zaidi? Tunaona kwa macho yetu wenyewe wingi wa ukaidi wa wapinga dini!"

Bila kutikiswa na tufani, Jerome akakaza sauti: "Nini basi! munafikiri kwamba naogopa kufa? Mulinishika mwaka mzima katika gereza la kutisha, la kuchukiza kuliko mauti yenyewe. ... Siwezi bali naeleza mshangao wangu kwa ushenzi mkubwa wa namna hii juu ya Mkristo."

### Akahesabiwa Kifungo na Mauti

Tena zoruba ya hasira ikatokea kwa nguvu, na Jerome akapelekwa gerezani kwa haraka. Kwani kulikuwa wengine ambao maneno yake yaliwagusa na kuwapa mawazo mioyoni na walitamani kuokoa maisha yake. Alizuriwa na wakuu wenye cheo na kumuomba sana kutii baraza. Matumaini mazuri yalitolewa kama zawadi.

"Shuhudieni kwangu kwa Maandiko matakatifu kwamba niko katika makosa," akasema, "na nitaikana kwa kiapo."

"Maandiko matakatifu"! akapaza sauti mmoja wao wa wajaribu wake, "je, kila kitu basi ni kuhukumiwa kwa yale Maandiko? Nani anaweza kuyafahamu mpaka kanisa ameyatafsiri?"

"Je, maagizo ya watu yanakuwa na bei kuliko injili ya Mwokozi wetu?" akajibu Jerome.

"Mpunga dini!" lilikuwa jibu. "Natubu kwa kutetea wakati mrefu pamoja nanyi. Naona kwamba unashurutishwa na Shetani".

Kwa gafula akapelekwa mahali pale pale ambapo Huss alitoa maisha yake. Alikwenda akiimba njiani mwake, uso wake ukang'aa kwa furaha na amani. Kwake mauti ilipoteza kutisha kwake. Wakati mwuaji, alipotaka kuwasha kundi, akasimama nyuma yake, mfia dini akapaza sauti, "tieni moto mbele ya uso wangu, Kama nilikuwa nikiogopa, singekuwa hapa."

[49] Maneno yake ya mwisho yalikuwa ni maombi: "Bwana Baba Mwenyezi, unihurumie, na unirehemu zambi zangu; kwa maana unajua kwamba nilikuwa nikipenda sikuzote Ukweli." Majifu ya mfia dini yakakusanyiwa na, kama yale ya Huss, yakatupwa katika Rhine. Basi kwa namna hii wachukuzi wa nuru waaminifu wa Mungu waliangamizwa.

Kuuawa kwa Huss kuliwasha moto wa hasira na hofu kuu katika Bohemia. Taifa lote likamtangaza kuwa mwalimu mwaminifu wa ukweli. Baraza likawekewa mzigo wa uuaji wa mtu kwa makusudi. Mafundisho yake yakaleta mvuto mkubwa kuliko mbele, na wengi wakaongozwa kukubali imani ya Matengenezo. Papa na mfalme wakaungana kuangamiza tendo hili la dini, na majeshi ya Sigismund yakatupwa juu ya Bohemia. Kwa kushambulia wenye imani ya matengenezo.

Lakini Mwokozi akainuliwa juu. Ziska, mmojawapo wa wakuu wa waskari wa wakati wake, alikuwa mwongozi wa watu wa Bohemia. Tumaini katika usaada wa Mungu, watu wale wakashindana na majeshi ya nguvu yale yangaliweza kuletwa juu yao. Mara nyingi mfalme alikashambulia Bohemia, ila tu kwa kufukuzwa. Wafuasi wa Huss wakainuliwa juu ya hofu ya mauti, na hakukuwa kitu cha. Mshujaa Ziska akafa, lakini pahali pake pakakombolewa na Procopius, kwa heshima fulani alikuwa mwongozi wa uwezo zaidi.

Papa akatangaza pigano juu ya maovu (crusade) juu ya wafuasi wa Huss. Majeshi mengi akatumbukia juu ya Bohemia, kwa kuteswa tu na maangamizi. Pigano lingine la maovu likatangazwa. Katika inchi zote za dini ya Roma katika Ulaya, mali na vyombo vya vita vikakusanywa. Watu wengi wakaja kwa bendera ya kanisa la Roma.

Majeshi makubwa yakaingia Bohemia. Watu wakakusanyika tena kuwafukuza. Majeshi mawili wakakribiana hata mto tu ndio uliokuwa katikati yao. "Wapiga vita juu ya maovu (crusade) walikuwa katika jeshi bora kubwa na la nguvu, lakini badala ya kuharakisha ngambo ya kijito, na kumaliza vita na wafuasi wa Huss,

ambao walikuja toka mbali kukutana nao, wakasimama kutazama kwa kimya wale wapingaji."

Kwa gafula hofu kuu ya ajabu ikaangukia jeshi. Bila kupiga kishindo jeshi kubwa lile likatiishwa na likatawanyika kama kwamba lilifukuzwa na nguvu isiyoonekana. Wafuasi wa Huss wakawafuata wakimbizi, na mateka makubwa yakaanguka mikononi mwa washindi. Vita badala ya kuleta umaskini, ikawaletea wa Bohemia utajiri.

Miaka michache baadaye, chini ya Papa mpya, pigano juu ya [50]
maovu lingine likawekwa. Jeshi kubwa likaingia Bohemia. Wafuasi wa Huss wakarudi nyuma mbele yao, kuvuta maadui ndani zaidi ya inchi, kuwaongoza kuwaza ushindi ulikwisha kupatikana.

Mwishowe jeshi la askari la Procopius likasogea kuwapiganisha vita. Namna sauti ya jeshi lililo karibia iliposikiwa, hata kabla wafuasi wa Huss kuonekana mbele ya macho, hofu kubwa tena ikaanguka iuu ya wapigani wa crusade. Wafalme, wakuu, na waaskari wa kawaida, wakatupa silaha zao, wakakimbia pande zote. Maangamizo yalikuwa kamili, na tena mateka makubwa yakaanguka mikononi mwa washindi.

Kwa hiyo mara ya pili jeshi la watu hodari kwa vita, waliozoea vita, wakakimbia bila shindo mbele ya watetezi wa taifa ndogo na zaifu. Adui waliuawa na hofu kubwa isiyo ya kibinadamu. Yule aliyekimbiza majeshi ya Wamidiani mbele ya Gideoni na watu miatatu wake, alinyosha tena mkono wake. Tazama Waamuzi 7:1925; Zaburi 53:5.

### Kusalitiwa kwa Njia ya Upatanishi

Waongozi wa Papa mwishowe wakatumia njia ya upatanisho. Mapatano likafanya ambalo kwalo likasaliti wa Bohemia katika utawala wa Roma. Watu wa Bohemia wakataja sharti inne kwa ajili ya amani kati yao na Roma: (1) uhuru wa kuhubiri Biblia; (2) haki ya kanisa lote katika mambo mawili hayo ya mkate na divai katika ushirika na matumizi ya lugha ya kienyeji katika ibada ya Mungu; (3) Kutenga waongozi wa dini la kikristo kwa kazi zote za kidunia na mamlaka; na, (4) wakati wa kosa, hukumu ya baraza za serkali juu ya mapadri na wasiokuwa mapadri iwe sawa sawa. Hukumu za Papa zikakubali kwamba mambo mane yale yakubaliwe, "lakini

haki ya kuyaeleza ... inapaswa kuwa kwa baraza--katika maneno mengine, kwa Papa na kwa mfalme.” Roma ikashinda kwa unafiki na madanganyo mambo ambayo kwa njia ya vita alishindwa. Kukubalia Roma uwezo wa kutafsiri maandishi ya wafuasi wa Huss, kama juu ya Biblia, iliweza kupotosha maana kwa kupendeza makusudi yake.

Hesabu kubwa ya watu katika Bohemia, kuona kwamba jambo lile lilisaliti uhuru wao, hawakuweza kukubali mapatano. Kutopatana kukaumka, na kuletaugomvi kati yao wenyewe. Procopius mwenye cheo akashindwa, na uhuru wa watu wa Bohemia ukakoma.

[51] Tena majeshi ya waaskari ya kigeni yakashambulia Bohemia, na wale waliodumu kuwa waaminifu kwa injili wakawa katika hatari kwa mateso ya damu. Kwani walisimama imara. Wakakazwa kutafuta kimbilio katika mapango, wakaendelea kukusanyika kusoma Neno la Mungu na kujiunga katika ibada yake. Kwa njia ya wajumbe kwa siri wakatuma kwa inchi mbali mbali wakajifunza “kwamba katikati ya milima ya Alps (safu ya milima mirefu) kulikuwa kanisa la zamani, la kudumu juu ya misingi ya Maandiko, na kukataa maovu ya ibada ya sanamu ya Roma.” Kwa furaha kubwa, uhusiano wa kuandikiana ukawa kati yao na Wakristo wa Waendense furaha kubwa, (Vaudois).

Msimamo imara wa injili, watu wa Bohemia wakangoja usiku kucha wa mateso yao, katika saa ya giza kuu hata wakageuza macho yao kwa upeo kama watu wanaokesha hata asubui.

# 7 /LUTHER, MTU KWA WAKATI WAKE [52]

Wakwanza miongoni mwa wale walioitwa kuongoza kanisa kutoka gizani mwa mafundisho ya Kanisa la Roma kwa nuru ya imani safi zaidi kukasimama Martin Luther. Hakuogopa kitu chochote bali Mungu, na kukubali msingi wowote kwa ajili ya imani bali Maandiko matakatifu. Luther alikuwa mtu anayefaa kwa wakati wake.

Miaka ya kwanza ya Luther ilitumiwa katika nyumba masikini ya mlimaji wa Ujeremani. Baba yake alimukusudia kuwa mwana sheria (mwombezi), lakini Mungu akakusudia kumufanya kuwa mwenye mjengaji katika hekalu kubwa ambalo lilikuwa likiinuka pole pole katika karne nyingi. Taabu, kukatazwa, na maongozi magumu yalikuwa ni masomo ambamo Hekima lsiyo na mwisho ilimtayarisha Luther kwa ajili ya kazi ya maisha yake.

Baba wa Luther alikuwa mtu wa akili ya kutenda. Akili yake safi ikamwongoza kutazama utaratibu wa utawa na mashaka. Hakupendezwa wakati Luther, bila ukubali wake, akuingia katika nyumba ya watawa (monastere). Ilichunkua miaka miwili ili baba apatane na mtoto wake, na hata hivyo maoni yake yakibaki yale yale.

Wazazi wa Luther wakajitahidi kulea watoto wao katika kumjua Mungu. Bidii zao zilikuwa za haki na kuvumilia kutayarisha watoto wao kwa maisha ya mafaa. Nyakati zingine walitumia ukali sana, lakini Mtengenezaji mwenyewe aliona katika maongozi yao mengi ya kukubali kuliko ya kuhukumu.

Katika masomo Luther alitendewa kwa ukali na hata mapigano. Akiteswa na njaa mara kwa mara. Mawazo ya giza, na juu ya mambo ya ibada ya sanamu ya dini iliodumu wakati ule ikamuogopesha. Akilala usiku na moyo wa huzuni, katika hofu ya daima kwa kufikiria Mungu kama sultani mkali, zaidi kuliko Baba mwema wa mbinguni.

Wakati alipoingia kwa chuo kikubwa (universite) cha Erfurt, matazamio yake yalikuwa mazuri sana kuliko katika miaka yake ya kwanza. Wazazi wake, kwa akili walioipata kwa njia ya matumizi

mazuri ya pesa na bidii, waliweza kumusaidia kwa mahitaji yote. Na rafiki zake wenye akili sana wakapunguza matokeo ya giza ya mafundisho yake ya kwanza. Kwa mivuto ya kufaa, akili yake ikaendelea upesi. Matumizi ya bidii upesi ikamutia katika cheo kikuu miongoni mwa wenzake.

Luther hakukosa kuanza kila siku na maombi, moyo wake kila mara ukipumuamaombi ya uongozi. “Kuomba vizuri, “akisema kila
[53] mara, “ni nusu bora ya kujifunza.”

Siku moja katika chumba cha vitabu (librairie) cha chuo kikubwa akavumbua Biblia ya Kilatini (Latin), kitabu ambacho hakukiona kamwe. Alikuwa akisikia sehemu za Injili na Nyaraka (Barua), ambazo alizania kuwa Biblia kamili. Sasa, kwa mara ya kwanza, akatazama, juu ya Neno la Mungu kamili. Kwa hofu na kushangaa akageuza kurasa takatifu na akasoma yeye mwenyewe maneno ya uzima, kusimama kidogo kwa mshangao, “O”, kama Mungu angenipa kitabu cha namna hii kwangu mwenyewe!” Malaika walikuwa kando yake. Mishale ya nuru kutoka kwa Mungu yakafunua hazina za kweli kwa ufahamu wake. Hakikisho kubwa la hali yake kuwa mwenye zambi likamushika kuliko zamani.

## Kutafuta Amani

Mapenzi ya kupata amani pamoja na Mungu yakamwongoza kujitoa mwenyewe kwa maisha ya utawa. Hapa alikuwa akitakiwa kufanya kazi ngumu za chini sana na kuomba omba nyumba kwa nyumba. Akaendelea kwa uvumilivu katika kujishusha huku,akiamini hii kuwa lazima sababu ya zambi zake.

Alijizuia mwenyewe saa zake za usingizi na kujinyima hata wakati mdogo wakula chakula chake kichache, akapendezwa na kujifunza Neno la Mungu. Alikuta Biblia iliyofungiwa mnyororo kwa ukuta wa nyumba ya watawa, na kwa hiki (Biblia) akaenda mara kwa mara.

Akaanza maisha magumu sana zaidi, akijaribu kufunga,kukesha, na kujitesa kwa kutisha maovu ya tabia yake. Akasema baadaye, “Kama mtawa angeweza kupata mbingu kwa kazi zake za utawa, hakika ningepaswa kustahili mbingu kwa kazi hiyo. ... Kama ingeendelea wakati mrefu, ningepaswa kuchukua uchungu wangu

hata kufa." Kwa bidii yake yote, roho ya taabu yake haikupata usaada. Mwishowe akafika karibu hatua ya kukata tamaa.

Wakati ilionekana kwamba mambo yote yamepotea, Mungu akainua rafiki kwa ajili yake. Staupitz akafungua Neno la Mungu kwa akili wa Luther na akamwomba kutojitazama mwenyewe na kutazama kwa Yesu. "Badala ya kujitesa mwenyewe kwa ajili ya zambi zako, ujiweke wewe mwenyewe katika mikono ya Mwokozi. Umutumaini, katika haki ya maisha yake, malipo ya kifo chake...Mwana wa Mungu alikuwa mtu kukupatia uhakikisho wa toleo ya kimungu. ... Umpende yeye aliyekupenda mbele." Maneno yake yakafanya mvuto mkubwa kwa ajili ya Luther. Amani ikakuja kwa roho yake iliyataabika.

Alipotakaswa kuwa padri, Luther akaitwa kwa cheo cha mwal- [54] imu katika chuo kikuu (universite) cha Wittenberg. Akaanza kufundisha juu ya Zaburi, Injili, na kwa barua kwa makundi ya wasikilizi waliopendezwa. Staupitz, mkubwa wake akamwomba kupanda kwa mimbara na kuhubiri. Lakini Luther akajisikia kwamba hastahili kusema kwa watu katika jina la Kristo. Ilikuwa tu baada ya juhudi ya wakati mrefu ndipo alikubali maombi ya rafiki zake. Alikuwa na uwezo mkubwa katika Maandiko, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Kwa wazi uwezo ambao alifundisha nao ukweli ukasadikisha ufahamu wao, na nguvu yake ikagusa mioyo yao.

Luther alikuwa akingali mtoto wa kweli wa Kanisa la Roma, hakuwa na wazo kwamba atakuwa kitu kingine cho chote. Akaongozwa kuzuru Roma, aliendelea safari yake kwa miguu, kukaa katika nyumba za watawa njiani. Akajazwa na ajabu hali nzuri na ya damani ambayo alishuhudia. Watawa (moines) walikaa katika vyumba vizuri, wakajivika wao wenyewe katika mavazi ya bei kali, na kujifurahisha kwa meza ya damani sana. Mafikara ya Luther yalianza kuhangaika.

Mwishowe akaona kwa mbali mji wa vilima saba. Akaanguka mwenyewe chini udongoni, kupaaza sauti: "Roma mtakatifu, nakusalimu!" Akazuru makanisa akasikiliza hadizi za ajabu zilizokaririwa na mapadri na watawa, na kufanya ibada zote zilizohitajiwa. Po pote, mambo yakamushangaza --uovu miongoni mwa waongozi, ubishi usiofaa kwa maaskofu. Akachukizwa na (unajisi) wao hata wakati wa misa. Akakutana upotevu, usharati. "Hakuna mtu anaweza kuwazia," akaandika, "zambi gani na matendo maovu

sana yako yakitendeka katika Roma. ... Watu huzoea kusema, ‘ Kama kunakuwa na jehanumu, Roma inajengwa juu yake.’”

### Ukweli juu ya ngazi ya Pilato

Kuachiwa kuliahidiwa na Papa kwa wote watakaopanda juu ya magoti yao “Ngazi ya Pilato,” waliozania kuwa ilichukuliwa kwa mwujiza toka Yerusalema hata Roma. Luther siku moja alikuwa akipanda ngazi hizi wakati sauti kama radi ilionekana kusema, “Mwenye haki ataishi kwa imani.” Waroma 1:17. Akaruka kwa upesi kwa magoti yake kwa haya na hofu kuu. Tangu wakati ule akaona kwa wazi kuliko mbele neno la uongo la kutumaini kazi za binadamu kwa ajili ya wokovu. Akageuza uso wake kwa Roma. Tangu wakati ule mutengano ukakomaa kuwa hata akakata uhusiano wote na kanisa la Roma.

[55] Baada ya kurudi kwake kutoka Roma, Luther akapokea cheo cha mwalimu (docteur) wa mambo ya Mungu. Sasa alikuwa na uhuru wa kujitoa wakfu mwenyewe kwa Maandiko ambayo aliyapenda. Akaweka naziri (ya ibada ya Mungu) kuhubiri kwa uaminifu Neno la Mungu, si mafundisho ya waPapa. Hakuwa tena mtawa tu, bali mjumbe aliyeruhusiwa wa Biblia, aliyeitwa kama mchungaji (pasteur) kwa kulisha kundi la Mungu lillokuwa na njaa na kiu ya ukweli. Akatangaza kwa bidii kwamba Wakristo hawapaswe kupokea mafundisho mengine isipokuwa yale ambayo yanayojengwa juu ya mamlaka ya Maandiko matakatifu.

Makundi yenye bidii yakapenda sana maneno yake. Habari ya furaha ya upendo wa Mwokozi, hakikisho la msamaha na amani katika damu ya kafara yake ikafurahisha mioyo yao. Huko Wittenberg nuru iliwashwa, ambayo nyali yake iongezeke kungaa zaidi kwa mwisho wa wakati.

Lakini kati ya ukweli na uongo kunakuwa vita. Mwokozi wetu Mwenyewe alitangaza: “Musifikiri ya kama nimekuja kuleta salama duniani, sikuja kuleta salama lakini upanga.” Matayo 10:34. Akasema Luther, miaka michache baada ya kufunguliwa kwa Matengenezo: “Mungu ... ananisukuma mbele ... nataka kuishi katika utulivu; lakini nimetupwa katikati ya makelele na mapinduzi makuu.”

## Huruma za kuuzisha

Kanisa la Roma lilifanya Biashara ya Neema ya Mungu. Chini ya maombi ya kuongeza mali kwa ajili ya kujenga jengo la Petro mtakatifu kule Roma, huruma kwa ajili ya zambi zilizotolewa kwa kuuzishwa kwa ruhusa ya Papa. Kwa bei ya uovu hekalu lilipaswa kujengwa kwa ajili ya ibada ya Mungu. Ilikuwa ni jambo hili ambalo liliamusha adui mkubwa sana wa kanisa la Roma na kufikia kwa vita ambayo ilitetemesha kiti cha Papa na mataji matatu juu ya kichwa cha askofu huyu.

Tetzel, mjumbe aliyechaguliwa kuongoza uujishaji wa huruma katika Ujeremani, alikuwa amehakikishwa makosa mabaya juu ya watu na sheria ya Mungu, lakini alitumiwa kwa kuendesha mipango ya faida ya Papa katika Ujeremani. Akasema bila haya mambo ya uongo na hadizi za ajabu kwa kudanganya watu wajinga wanaoamini yasiyo na msingi. Kama wangekuwa na neno la Mungu hawangedanganywa, lakini Biblia ilikatazwa kwao.

Wakati Tetzel alipoingia mjini, mjumbe alimutangulia mbele, kutangaza: "Neema ya Mungu na ya baba mtakatifu inakuwa milangoni mwenu". Watu wakamkaribisha mtu wa uwongo [56]
anayetukana Mungu kama kwamba angekuwa Mungu mwenyewe. Tetzel, kupanda mimbarani ndani ya kanisa, akatukuza uujisaji wa huruma kama zawadi za damani sana za Mungu. Akatangaza kwamba kwa uwezo wa sheti cha msamaha, zambi zote ambazo mnunuzi angetamani kuzitenda baadaye zitasamehewa na "hata toba si ya lazima." Akahakikishia wasikilizi wake kwamba vyeti vyake vya huruma vilikuwa na uwezo wa kuokoa wafu; kwa wakati ule kabisa pesa inapogonga kwa sehemu ya chini ya sanduku lake, roho inayolipiwa pesa ile itatoroka kutoka toharani (purgatoire) na kufanya safari yake kwenda mbinguni.

Zahabu na feza zikajaa katika nyumba ya hazina ya Tetzel. Wokovu ulionunuliwa na mali ulipatikana kwa upesi kuliko ule unaohitaji toba, imani, na kufanya bidii kwa kushindana na kushinda zambi. (Tazama Nyongezo)

Luther akajazwa na hofu kuu. Wengi katika shirika lake wakanunua vyeti vya msamaha. Kwa upesi wakaanza kuja kwa mchungaji (pasteur) wao, kwa kutubu zambi na kutumainia maondoleo ya zambi, si kwa sababu walitubu na walitamani maten-

genezo, bali kwa msingi wa sheti cha huruma. Luther akakataa, na akawaonya kwamba isipokuwa walipaswa kutubu na kugeuka, walipaswa kuangamia katika zambi zao. Wakaenda kwa Tetzel na malalamiko kwamba muunganishaji wao alikataa vyeti vyake, na wengine wakauliza kwa ujasiri kwamba mali yao irudishwe. Alipojazwa na hasira, mtawa (religieux) akatoa laana za kutisha, akataka mioto iwake mbele ya watu wote, na akatangaza kwamba "alipata agizo kwa Papa kuunguza wapinga dini wote wanaosubutu kupinga, vyeti vyake vya huruma takatifu zaidi."

## Kazi ya Luther Inaanza

Sauti ya Luther ikasikiwa mimbarani katika onyo la kutisha. Akaweka mbele ya watu tabia mbaya sana ya zambi na kufundisha kwamba haiwezekani kwa mtu kwa kazi zake mwenyewe kupunguza zambi zake ao kuepuka malipizi yake. Hakuna kitu bali toba kwa Mungu na imani katika Kristo inaoweza kuokoa mwenye zambi. Neema ya Kristo haiwezi kununuliwa; ni zawadi ya bure. Akashauri watu kutokununua vyeti vya huruma, bali kutazama kwa imani kwa Mkombozi aliyesulubiwa. Akasimulia juu ya habari mambo ya maisha yake ya uchungu na akahakikisha wasikilizaji wake kwamba kwa kuamini Kristo ndipo mtu atapata amani na furaha.

[57] Wakati Tetzel alipoendelea na kiburi chake cha kukufuru, Luther akajitahidi kusema kutokukubali kwake. Nyumba ya kanisa la Wittenberg ilikuwa na picha (reliques) ambayo kwa sikukuu fulani yalionyeshwa kwa watu. Maondoleo kamili ya zambi yalitolewa kwa wote waliozuru kanisa na waliofanya maungamo. Jambo moja la mhimu sana la nyakati hizi, sikukuu ya Watakatifu Wote, ilikuwa ikikaribia. Luther, alipoungana na makundi yaliyo jitayarisha kwenda kanisani, akabandika kwa mlango wa kanisa mashauri makumi tisa na tano juu ya kupinga ya uuzishaji wa vyeti (musamaha).

Makusudi yake yakavuta uangalifu wa watu wote. Yakasomwa na kuyakariri po pote, yakasitusha sana watu katika mji wote. Kwa maelezo haya yalionyeshwa kwamba uwezo kwa kutoa masamaha ya zambi na kuachiliwa malipizi yake haukutolewa kwa Papa ao kwa mtu ye yote. Ilionyeshwa wazi wazi kwamba neema ya Mungu ilitolewa bure kwa wote wanaoitafuta kwa toba na imani.

Mambo yaliyoandikwa na Luther yakatawanyika pote katika Ujeremani na baada ya majuma machache yakasikilika pote katika Ulaya. Wengi waliojifanya kuwa watu wa kanisa la Roma wakasoma mashauri haya (mambo yalioandikwa na Luther) kwa furaha, kutambua ndani yao sauti ya Mungu. Walijisikia kwamba Bwana aliweka mkono wake kufunga maji yaliyotomboka ya uovu ulioletwa kutoka kwa Roma. Waana wa wafalme na waamuzi kwa siri wakafurahi kwamba kizuio kilipashwa kuwekwa juu ya mamlaka ya kiburi ambayo ilikataa kuacha maamuzi yake.

Wapadri wa hila, kuona faida zao kuwa hatarini, wakakasirika. Mtengenezaji (Reformateur) alikuwa na washitaki wakali wakushindana naye. “Nani asiyejua, ” akajibu, “kwamba si mara nyingi mtu kuleta mawazo mpya bila. kushitakiwa kukaamsha mabishano? ... Sababu gani Kristo na wafia dini wote waliuawa? Kwa sababu ... walileta mambo mapya bila kupata kwanza shauri la unyenyekevu la mtu wa hekima na maoni ya zamani.”

Makaripio ya adui za Luther, masingizio yao juu ya makusudi yake, mawazo yao ya uovu juu ya tabia yake yakawajuu yake kama garika. Alikuwa ameamini kwamba waongozi watajiunga naye kwa furaha katika matengenezo. Mbele ya wakati aliona siku bora zikipambazuka kwa kanisa.

Lakini kutiia moyo kukageuka kuwa karipio. Wakuu wengi wa kanisa na jamii ya watu wa serkali kwa upesi wakaona kwamba ukubali wa mambo haya ya kweli karibu ungaliharibu mamlaka ya Roma, kuzuia maelfu ya vijito vinavyotiririka sasa katika nyumba ya hazina yake, na vivi hivi kupunguza anasa ya waongozi wa Papa. Kufundisha watu kumutazama Kristo peke yake kwa ajili ya wokovu [58]
kungeangusha kiti cha askofu na baadaye kuharibu mamlaka yao wenyewe. Kwa hiyo wakajiunga wao wenyewe kupinga Kristo na kweli kuwa wapinzani kwa mtu aliyetumwa kwa kuwaangazia.

Luther akatetemeka wakati alipojiangalia mwenyewe--mtu mmoja akapinga watu wa nguvu nyingi wa dunia. “Mimi nilikuwa nani?” akaandika, “kupinga enzi ya Papa, mbeie yake ... wafalme wa dunia na ulimwengu wote ulitetemeka? ... Hakuna mtu anaweza kujua namna gani moyo wangu uliteseka mda wa miaka hii miwili ya kwanza na katika kukata tamaa, naweza kusema katika kufa moyo, nilizama.” Lakini wakati usaada wa kibinadamu ulishindwa,

alitazama kwa Mungu peke yake. Aliweza kuegemea katika usalama juu ya ule mkono ulio wa guvu zote.

Kwa rafiki Luther akaandika: "Kazi yako ya kwanza ni kuanza na ombi. ... Usitumaini kitu kwa kazi zako mwenyewe, kwa ufahamu wako mwenyewe: Tumaini tu katika Mungu, na katika mvuto wa Roho Mtakatifu." Hapa kuna fundisho la maana kwa wale wanaojisikia kwamba Mungu amewaita kutoa kwa wengine ibada ya dini ya kweli kwa wakati huu. Katika vita pamoja na mamlaka ya uovu kunakuwa na mahitaji ya kitu kingine zaidi kuliko akili na hekima ya kibinadamu.

### Luther Alikimbilia Tu kwa Biblia

Wakati adui walikimbilia kwa desturi na desturi ya asili, Luther alikutana nao anapokuwa na Biblia tu, bishano ambayo hawakuweza kujibu. kutoka mahubiri ya Luther na maandiko kulitoka nyali za nuru ambazo ziliamsha na kuangazia maelfu. Neno la Mungu lilikuwa kama upanga unaokata ngambo mbili, unaokata njiayake kwa mioyo ya watu. Macho ya watu, kwa mda mrefu yaliongozwa kwa kawaida za kibinadamu na waombezi wa kidunia, sasa walimugeukia Kristo katika imani na Yeye aliyesulubishwa.

Usikizi huu ukaamsha woga kwa mamlaka ya Papa. Luther akapokea mwito kuonekana huko Roma. Rafiki zake walijua vizuri hatari ile iliyomngoja katika mji mwovu huo, uliokwisha kunywa damu ya wafia dini wa Yesu. Wakauliza kwamba apokee mashindano yake katika Ujeremani.

Jambo hili likatendeka, na mjumbe wa Papa akachaguliwa kusikiliza mambo yenyewe. Katika maagizo kwa mkubwa huyu, alijulishwa kwamba Luther alikwisha kutangazwa kama mpingaji wa imani ya dini. Mjumbe alikuwa basi ni "kutenda na kulazimisha
[59] bila kukawia." Mjumbe akapewa uwezo wa "kumufukuza katika kila upande wa Ujeremani; kumfukuzia mbali, kumlaani, na kutenga wale wote walioambatana naye", Kuwatenga na cheo cho chote kikiwa cha kanisa ao cha serkali, ila tu mfalme, hatajali kumkamata Luther na wafuasi wake na kuwatoa kwa kisasi cha Roma.

Hakuna alama ya kanuni ya kikristo ao hata haki ya kawaida inapaswa kuonekana katika maandiko haya. Luther hakuwa na nafasi ya kueleza wala kutetea musimamo wake; lakini alikuwa

amekwisha kutangazwa kuwa mpingaji wa imani ya dini na kwa siku ile ile alishauriwa, kushitakiwa, kuhukumiwa, na kulaumiwa.

Wakati Luther alihitaji sana shauri la rafiki wa kweli, Mungu akamtuma Melanchthon kule Wittenberg. Shida ya hukumu ya Melanchthon, ikachanganyika na usafi (utakatifu) na unyofu wa tabia, ikashinda sifa ya watu wote. Kwa upesi akawa rafiki mwaminifu sana wa Luther--upole wake, uangalifu, na usahihi ikawazidisho la bidii na nguvu za Luther.

Augsburg palitajwa kuwa mahali pa hukumu, na Mtengenezaji (Reformateur) akaenda huko kwa miguu. Vitisho vilifanywa kwamba angeuawa njiani, na rafiki zake wakamuomba asijihatarishe. Lakini maneno yake yalikuwa, "Ninakuwa kama Yeremia, mtu wa ushindano, na ugomvi; lakini kwa namna matisho yao yalizidi, ndipo furaha yangu iliongezeka... Wamekwisha kuharibu heshima (sifa) yangu na mwenendo wangu. ... Kuhusu roho yangu, hawawezi kuikamata. Yeye anayetaka kutangaza neno la Kristo ulimwenguni, inampasa kutazamia kifo wakati wowote."

Akari ya kufika kwa Luther huko Augsburg kukaleta kushelewa kukubwa kwa mjumbe wa Papa. Mpinga mafundisho ya dini anayeamsha ulimwengu akaonekana sasa kuwa chini ya uwezo wa Roma; hakupaswa kuponyoka. Mjumbe alikusudia kulazimisha Luther kukana, ao isipowezekana alazimishe kwenda Roma kufuata nyayo ya Huss na Jerome. Mjumbe wa Papa akatuma watu wake kumwambia Lutter afike bila ahadi ya ulinzi salama wa mfalme na matumaini yake mwenyewe wema wake. Kwa hiyo mtengenezaji akakataa. Hata wakati alipopata ahadi ya ulinzi wa mfalme mkuu ndipo akakubali kuonekana mbele ya mjumbe wa Papa. Kama mpango wa busara, watu wa Roma wakakusudia kumpata Luther kwa njia ya kujioyesha kama wapole. Mjumbe akajionyesha kawa rafiki mkubwaa, lakini akaomba kwamba Luther ajitoe kabisa kwa kanisa na kukubali kila kitu bila mabishano wala swali. Luther, kwa kujibu, akaonyesha heshima yake kwa ajili ya kanisa, mapenzi yake kwa ajili ya ukweli, kuwa tayari kwa kujibu makatazo yote kuhusu yale aliyoyafundishwa, na kuweka mafundisho yake chini [60]
ya uamuzi wa vyuo vikubwa (universites). Lakini alikataa juu ya mwendo wa askofu katika kummulazimisha kukana bila kuonyesha na kuhakikisha kosa lake.

Jibu moja tu lilikuwa, “uKane, ukane”! Mtengenezaji akaonyesha kwamba msiimamo wake unakubaliwa na Maandiko. Hakuweza kukana ukweli. Mjumbe, aliposhindwa kujibu kwa mabishano ya Luther, akamulemeza na zoruba ya laumu, zarau, sifa ya uongo maneno kutoka kwa kiasili (traditions), na mezali (maneno) ya Wababa, akikatalia Mtengenezaji nafasi ya kusema. Luther mwishowe, bila kupenda, akamupa ruhusa ya kutoa jibu lake kwa maandiko.

Akasema,akiandika kwa rafiki, “Mambo yaliyoandikwa ingeweza kutolewa kwa mawazo ya wengine; na jambo la pili, mtu anakuwa na bahati nzuri sana ya kutumika kwa hofu nyingi, kama si kwa zamiri, ya bwana wa kiburi na wa kusema ovyo ovyo ambaye njia ingine angeshinda kwa kutumia maneno yake makali.”

Kwa mkutano uliofuata, Luther akaonyesha maelezo mafupi na ya nguvu ya mawazo yake, yanayoshuhudiwa na Maandiko. Kartasi hii, baada ya kusoma kwa sauti nguvu, akaitoa kwa askofu, naye akaitupa kando kwa zarau, kuitangaza kuwa mchanganyiko wa maneno ya bure na mateuzi yasiyofaa. Sasa Luther akakutana na askofu wa kiburi kwa uwanja wake mwenyewe--mambo ya asili na mafundisho ya kanisa--na kuangusha kabisa majivuno yake.

Askofu akapoteza kujitawala kote na katika hasira akapandisha sauti, “ukane! ao nitakutuma Roma”. Na mwishowe akatangaza, katika sauti ya kiburi na hasira, “uKane, ao usirudi tena.”

Mtengenezaji kwa upesi akaondoka pamoja na rafiki zake, hivyo kutangaza wazi kwamba asingoje kwake kwamba atakana. Hili si jambo ambalo askofu alilokusudia. Kutoka kwa Luther Sasa, akaachwa peke yake pamoja na wasaidizi wake, wakatazamana wao kwa wao na huzuni kwa kushindwa kusikotazamiwa katika mipango yake.

Makutano makubwa yaliyokuwa pale wakawa na nafasi ya kulinganisha watu wawili hawa na kuhukumu wao wenyewe roho iliyoonyeshwa nao, vivyo hivyo na nguvu na ukweli wa nia zao. Mtengenezaji, munyenyekevu, mpole, imara, kwa kuwa na ukweli kwa upande wake; mjumbe wa Papa, mwenye kujisifu, mwenye kiburi, mpumbavu, bila hata neno moja kutoka kwa Maandiko, lakini wa juhudi ya kupandisha sauti, “uKana, ao utumwe Roma.”

## Kuokoka Toka Augsburg [61]

Rafiki za Luther wakasihi sana kwamba hivi ilikuwa bure kwake kubakia, heri kurudi Wittenberg bila kukawia, na lile onyo halisi lifuatwe. Kwa hiyo akaondoka Augsburg kabla ya mapambazuko juu ya farasi, akisindikizwa na mwongozi moja tu aliyetolewa na mwamuzi. Kwa siri akafanya safari yake katika njia za giza za mji. Maadui, waangalifu tena wauaji, walikuwa wakifanya shauri la kumuangamiza. Nyakati hizo zilikuwa za mashaka na maombi ya juhudi. Akafikia mlango katika ukuta wa mji. Ulifunguliwa kwa ajili yake, na pamoja na mwongozi wake akapita ndani yake. Kabla mjumbe kupata habari ya safari ya Luther, alikuwa mbali ya mikono ya watesi wake Kwa habari ya kutoroka kwa Luther mjumbe akajazwa na mshangao na hasira. Alitumaini kupokea heshima kubwa kwa ajili ya mambo angatendea mtu huyu anaye sumbuake kanisa. Katika barua kwa Frederick, mchaguzi wa waSaxony, akashitaki Luther kwa ukali, kuomba kwamba Frederick amtume Mtengenezaji Roma ao amfukuze kutoka Saxony.

Mchaguzi alikuwa hajafahamu sana mafundisho ya mtengenezaji, lakini alivutwa sana kwa nguvu na usikivu wa maneno ya Luther. Frederick akaamua kuwa, mpaka wakati mtengenezaji atahakikisha kuwa na kosa. Frederick akawamlinzi wake katika jibu kwa mjumbe wa Papa akaandika: "Tangu Mwalimu Martino alipoonekana mbele yenu huko Augsburg, mungepashwa kutoshelewa. Hatukutumainia kwamba mungemulazimisha kukana bila kumsadikisha kwamba alikuwa na makosa. Hakuna wenye elimu hata mmoja katika utawala wetu aliyenijulisha ya kwamba mafundisho ya Martino yalikuwa machafu, yakupinga Kristo ao ya kupinga ibada ya dini." Mchaguzi aliona kwamba kazi ya matengenezo ilihitajiwa kwa sisi akafurahi kuona mvuto bora ulikuwa ukifanya kazi yake katika kanisa.

Mwaka mmoja tu ulipita tangu Mtengenezaji alipoweka mabishano kwa mlango wa kanisa, lakini maandiko yake yaliamusha mahali pote usikizi mpya katika Maandiko matakatifu. Si kwa pande zote tu za Ujeremani, bali kwa inchi zingine, wanafunzi wakasongana kwa chuo kikuu. Vijana walipokuja mbele ya Wittenberg kwa mara ya kwanza "wakainua mikono yao mbinguni, na

kusifu Mungu kwa kuweza kuleta nuru ya ukweli kuangaza kutaka mji huu."

Luther alikuwa amegeuka nusu tu kwa makosa ya kanisa la Roma. Lakini aliandika, "Ninasoma amri za maaskofu, na ... sijui kama Papa ndiye anayekuwa mpinzani wa Kristo yeye mwenyewe,
[62] ao mtume wake, zaidi ya yote kristo ameelezwa vibaya kabisa na kusulubiwa ndani yao."

Roma ikazidi kukasirishwa na mashambulio ya Luther. Wapinzani washupavu, hata waalimu (docteurs) katika vyuo vikuu vya Kikatoliki, wakatangaza kwamba yule angeweza kumua mtawa yule angekuwa bila zambi. Lakini Mungu alikuwa mlinzi wake. Mafundisho yake yakasikiwa po pote--"katika nyumba ndogo na nyumba za watawa (couvents), ... katika ngome za wenye cheo, katika vyuo vikubwa, katika majumba ya wafalme."

Kwa wakati huu Luther akaona ya kwamba ukweli mhimu juu ya kuhesabiwa haki kwa imani ilikuwa ikishikwa na Mtengenezaji, Huss, wa Bohemia. "Tumekuwa na vyote" akasema Luther, "Paul, Augustine, na mimi mwenyewe, Wafuasi wa Huss bila kujua!" "ukweli huu ulihubiriwa ... karne iliyopita na ikachomwa!"

Luther akaandika basi mambo juu ya vyuo vikuu: "Ninaogopa sana kwamba vyuo vikuu vitaonekana kuwa milango mikubwa ya jehanumu, isipokuwa vikitumika kwa bidii kwa kueleza Maandiko matakatifu, na kuyakaza ndani ya mioyo ya vijana. ... Kila chuo ambamo watu hawashunguliki daima na Neno la Mungu kinapaswa kuharibika."

Mwito huu ukaenea po pote katika Ujermani. Taifa lote likashituka. Wapinzani wa Luther wakamwomba Papa kuchukua mipango ya nguvu juu yake. Iliamriwa kwamba mafundisho yake yahukumiwe mara moja. Mtengenezaji na wafuasi wake, kama hawakutubu, wangepaswa wote kutengwa kwa Ushirika Mtakatifu.

## Shida ya Kutisha

Hiyo ilikuwa shida ya kutisha sana kwa Matengenezo. Luther hakuwa kipofu kwa zoruba karibu kupasuka, lakini alitumaini Kristo kuwa egemeo lake na ngabo yake. "Kitu kinacho karibia kutokea sikijui, na sijali kujua. ... Hakuna hata sivile jani linawezakuanguka, bila mapenzi ya Baba yetu. Kiasi gani zaidi atatuchunga!

Ni vyepesi kufa kwa ajili ya Neno, kwani Neno ambalo lilifanyika mwili lilikufa lenyewe." Wakati barua ya Papa ilimufikia Luther, akasema: Ninaizarau, tena naishambulia, kwamba niya uovu, ya uongo.... Ni Kristo yeye mwenyewe anayelaumiwa ndani yake. Tayari ninasikia uhuru kubwa moyoni mwangu; kwani mwishowe ninajua ya kwamba Papa ni mpinga kristo na kiti chake cha ufalme ni kile cha Shetani mwenyewe."

Lakini mjumbe wa Roma halikukosa kuwa na matokeo. Wazaifu na waabuduo ibada ya sanamu wakatetemeka mbele ya amri ya Papa, na wengi wakaona kwamba maisha yalikuwa ya damani sana kuhatarisha. Je, kazi ya Mtengenezaji ilikuwa karibu kwisha? [63]

Luther angali bila woga. Kwa uwezo wa kutisha akarudisha juu ya Roma yenyewe maneno ya hukumu. Mbele ya makutano ya wanainchi wa vyeo vyote Luther akachoma barua ya Papa. Akasema, "Mapigano makali yameanza sasa. Hata sasa nilikuwa nikicheza tu na Papa. Nilianza kazi hii kwa jina la Mungu; si mimi atakaye imaliza, na kwa uwezo wangu.... Nani anayejua kama Mungu hakunichagua na kuniita na kama hawapashwe kuogopa hiyo, kwa kunizarau, wanazarau Mungu Mwenyewe? ...

"Mungu hakuchagua kamwe kuhani aokuhani mkuu wala mtu mkubwa yeyote; bali kwa kawaida huchagua watu wa chini na wenye kuzarauliwa, hata mchungaji kama Amosi. Kwa kila kizazi, watakatifu walipaswa kukemea wakuu, wafalme, wana wa wafalme, wakuhani, na wenye hekima, kwa hatari ya maisha yao. ... Sisemi kwamba niko nabii; lakini nasema kwamba wanapashwa kuogopa kabisa kwa sababu niko peke yangu na wao ni wengi. Ninakuwa hakika ya jambo hili, kwamba neno la Mungu linakuwa pamoja nami, na kwamba haliko pamoja nao."

Kwani haikuwa bila vita ya kutisha kwamba yeye mwenyewe ambaye Luther aliamua juu ya kutengana kwa mwisho na kanisa: "Ee, uchungu wa namna gani ilinileteа, ijapo nilikuwa na Maandiko kwa upande wangu, kuhakikisha mimi mwenyewe kwamba ningepaswa kusubutu kusimama pekee yangu kumpinga Papa, na kumutangaza kuwa kama mpinzani wa Kristo! Mara ngapi sikujiuliza mwenyewe kwa uchungu swali lile ambalo lilikuwa mara nyingi midomoni mwa watu wa Papa: 'Ni wewe peke yako mwenye hekima? Je, watu wote wanadanganyika? Itakuwa namna gani, kama, mwishoni wewe mwenyewe ukionekana kuwa na kosa na ni

wewe anayeshawishi katika makosa yako roho nyingi kama hizo. Ni nani basi atakayehukumiwa milele? Hivi ndivyo nilipigana na nafsi yangu na Shetani hata Kristo, kwa neno lake la hakika, akaimarisha moyo wangu juu ya mashaka haya."

Amri mpya ikaonekana, kutangaza mtengano wa mwisho wa Mtengenezaji kutoka kwa kanisa la Roma, kumshitaki kama aliyelaaniwa na Mbingu, na kuweka ndani ya hukumu ilete wale watakaopokea mafundisho yake.

Upinzani ni sehemu ya wote wale ambao Mungu hutumia kwa kuonyesha ukweli zinazofaa hasa kwa wakati wao. Kulikuwa na ukweli wa sasa katika siku za Luther; kuna ukweli wa sasa kwa ajili
[64] ya kanisa leo. Lakini ukweli hautakiwe na watu wengi leo kuliko ilivyokuwa na watu wa Papa waliompinga Luther. Wale wanaoonyesha ukweli kwa wakati huu hawapaswi kutazamia kupokewa na upendeleo mwingi zaidi kuliko watengenezaji wa zamani. Vita kuu kati ya kweli na uwongo, kati ya Kristo na Shetani, itaongezeka kwa mwisho wa historia ya ulimwengu huu. Tazama Yoane 15:19, 20; Luka 6:26.

# 8 /MSHINDI WA UKWELI [65]

Mfalme mpya, Charles V, akamiliki kwa kiti cha ufalme wa Ujeremani. Mchaguzi wa Saxony ambaye alisaidia Charles kupanda kwa kiti cha ufalme, akamwomba kutotendea Luther kitu chochote mpaka wakati atakapo ruhusu kumusikiliza. Kwa hiyo mfalme akawa katika hali ya mashaka na wasiwasi. Watu wa Papa hawangerizishwa na kitu chochote isipokuwa kifo cha Luther. Mchaguzi akatangaza "Mwalimu Luther anapashwa kutolewa haki (ruhusa ya usalama), ili apate kuonekana mbele ya baraza ya hukumu ya waamzi wenye elimu, watawa, na wa haki wasio na upendeleo."

Makutano wakakusanyika huko Worms. Kwa mara ya kwanza watoto wa kifalme wa Ujeremani walipashwa kukutana na mfalme wao kijana katika mkusanyiko. Wakuu wa kanisa na wa serkali na mabalozi wa inchi za kigeni wote wakakusanyika kule Worms. Bali jambo ambalo lililoamusha usikivu mwingi lilikuwa la Mtengenezaji. Charles alimuamuru mchaguzi kumleta Luther pamoja naye, kumuhakikishia ulinzi na kuahidi mazungumzo huru juu ya maswali katika mabishano. Luther akamwandikia mchaguzi: "Ikiwa kama mfalme ananiita, siwezi kuwa na mashaka huo ni mwito wa Mungu mwenyewe. Kama wakitaka kutumia nguvu juu yangu, ... Ninaweka jambo hili mikononi mwa Bwana. ... Kama hataniokoa, maisha yangu ni ya maana kidogo. ... Unaweza kutazamia lolote kutoka kwangu ... isipokuwa kukimbia na mimi kukana maneno ya kwanza. Kukimbia siwezi, na tena kukana ni zaidi."

Kwa namna habari ilienea kwamba Luther alipashwa kuonekana mbele ya baraza, msisimuko ukawa pahali pote. Aleander, mjumbe wa Papa, kwa kujulishwa hatari na akakasirika. Kuchunguza juu ya habari ambayo Papa alikwisha kutolea azabu ya hukumu ingekuwa kuzarau mamlaka ya askofu. Na tena, zaidi mabishano yenye uwezo ya mtu huyu yanaweza kugeuza watoto wa wafalme wengi kutoka kwa Papa. Akamuonya Charles juu ya kutoruhusu Luther kufika Worms na akashawishi mfalme kukubali.

Bila kutulia juu ya ushindi huu, Aleander akaendelea kuhukumu Luther, kushitaki Mtengenezaji juu ya "fitina, uasi, ukosefu wa heshima, na matukano". Lakini ukali wake ukafunua roho ambayo aliyokuwa ndani yake. "Anasukumwa na fitina na kulipisha kisasi.

Kwa juhudi zaidi tena Aleander akasihi sana mfalme kutimiza amri za Papa. Aliposumbuliwa sana na maombi ya mjumbe Charles
[66] akamwomba kuleta kesi yake kwa baraza. Kwa wasiwasi mwingi wale waliopendelea Mtengenezaji wakaendelea kuyatarajia maneno yakasomewa na Aleander. Mchaguzi wa Saxony hakuwa pale, lakini baazi ya washauri wake wakaandika yaliyosemwa na mjumbe wa Papa.

## Luther Anashitakiwa kuwa Mpinga Imani ya Dini

Kwa kujifunza na usemaji unaokolea, Aleander akajitahidi mwenyewe kuangusha Luther kama adui wa kanisa na serekali. "Haki,, makosa ya Luther yametosha", akatangaza kwa kushuhudia kuchomwa kwa mamia elfu wapinga imani ya dini."

"Ni wanani watu hawa wote wa Luther? Kundi la waalimu wenye kiburi, mapadri waovu, watawa wapotovu, wanasheria wajinga, na wenye cheo walioaibishwa. ...Kundi la katoloki si linawapita mbali sana kwa wingi, kwa akili na kwa uwezo! Amri ya shauri moja la kusanyiko hili tukufu litaangazia wanyenyekevu, litaonya wasio na busara, litaamua wenye mashaka na kuimarisha wazaifu."

Mabishano ya namna ile ile ingali inatumiwa juu ya wote wanaosubutu kutoa mafundisho kamili ya Neno la Mungu. "Ni wanani hawa wahubiri wa mafundisho mapya? Wanakuwa si wenye elimu, wachache kwa hesabu, na wa cheo cha maskini sana. Lakini wakijidai kuwa na ukweli, na kuwa watu waliochaguliwa na Mungu. Wanakuwa wajinga na waliodanganyiwa. Namna gani kanisa letu ni kubwa sana kwa hesabu na mvuto!" Mabishano haya hayako na nguvu zaidi sasa kuliko siku za Mtengenezaji.

Luther hakuwa pale, pamoja na maneno ya kweli wazi wazi na ya kusadikisha ya Neno la Mungu, kwa kushinda shujaa Papa. Watu karibu wote walikuwa tayari, si kwa kumuhukumu tu, yeye na mafundisho yake, bali, ikiwezekana, kuongoa upinzani wa imani ya dini. Yote Roma iliweza kusema katika kujitetea mwenyewe

imesemwa. Lakini tofauti kati ya ukweli na uwongo ingeonekana wazi zaidi namna wangeweza kujitoa wazi wazi kwa vita.

Sasa Bwana akagusa moyo wa mshiriki mmoja wa baraza atoe maelezo ya matendo ya jeuri ya Papa. Duc Georges wa Saxe akasimama katika mkutano huu wa kifalme; na akaonyesha sawasawa kabisa uwongo na machukizo ya kanisa la Roma:

"Kuzulumu ... kunapaza sauti juu ya Roma. Haya yote imewekwa kando na shabaha yao moja tu ni ... pesa, pesa, pesa, ... ili wahubiri wanaopashwa kufundisha ukweli, wasinene kitu kingine isipokuwa uongo, na si kuwavumilia tu, lakini kuwalipa, [67]
kwani namna wanazidi kusema uongo, ndipo wanazidi kupata faida. Ni kwa kisima hiki kichafu maji haya machafu hutiririka. Mambo ya washerati na ulevi. Hunyoosha mkono kwa uchoyo ... Ole! ni aibu iliyoletwa na askofu kinachotupa roho maskini nyingi katika hukumu ya milele. Matengenezo ya mambo yote inapaswa kufanyika." Sababu mnenaji alikuwa adui maalumu wa Mtengenezaji alitoa mvuto mkubwa kwa maneno yake.

Malaika wa Mungu wakatoa nyali za nuru katika giza ya uovu na ikafungua mioyo kwa ukweli. Uwezo wa Mungu wa ukweli ukatawala hata maadui wa Matengenezo na ukatayarisha njia kwa kazi kubwa ambayo ilikaribia kutimizwa. Sauti ya Mmoja mkuu kuliko Luther ikasikiwa katika mkutano ule.

Baraza ikawekwa kwa kutayarisha hesabu ya mambo yote yaliyo kuwa magandamizo ambayo yalikuwa mazito kwa watu wa Ujeremani. Oroza hii ikaonyeshwa kwa mfalme, na kumuomba achukue hatua kwa kusahihisha mambo mabaya haya. Wakasema waombaji, "Ni wajibu wetu kuzuia maangamizi na aibu ya watu wetu. Kwa sababu hiyo sisi wote pamoja tunakuomba kwa unyenyekevu sana, lakini kwa namna ya haraka sana, kuagiza matengenezo ya mambo yote na kufanya itimilike."

## Luther Anaamuriwa Kufika Barazani

Baraza sasa likaomba kuonekana kwa Mtengenezaji. Mwishowe mfalme akakubali, na Luther akaalikwa. Mwito ukafwatana na ruhusa ya kusafiri salama. Hati hizo mbili zikapelekwa Wittenberg na mjumbe aliyeagizwa kumusindikiza Worms.

Kujua chuki na uadui juu yake, rafiki za Luther waliogopa kwamba cheti cha kusafiri salama hakitaheshimiwa. Akajibu: “Kristo atanipa Roho yake kwa kushinda wahuduma hawa wa uongo. Nina wazarau katika maisha yangu; nitawashinda kwa kifo changu. Huko Worms wanashugulika sana kwa kunilazimisha; ni kane kukana kwangu kutakuwa huku: Nilisema zamani kwamba Papa alikuwa kasisi wa Kristo; sasa na tangaza kwamba yeye ni mpinzani wa Bwana, na mtume wa Shetani.”

Zaidi ya mjumbe wa mfalme, rafiki watatu wakakusudia kumsindikiza Luther. Moyo wa Melanchton ukaambatana kwa moyo wa Luther, na akatamani sana kumfuata. Lakini maombi yake yakakataliwa. Akasema Mtengenezaji: “Kama sitarudi, na adui zangu wakiniua, endelea kufundisha, na kusimama imara katika
[68] ukweli. Utumike kwa nafasi yangu. ... Kama ukizidi kuishi, mauti yangu itakuwa ya maana kidogo.”

Mioyo ya watu ikagandamizwa na maono ya huzuni. Waliambiwa kwamba maandiko ya Luther yalihukumiwa huko Worms. Mjumbe, huogopa kwa ajili ya usalama wa Luther kwa baraza, akauliza kama alikuwa akiendelea kutamani kwenda. Akajibu: “ijapokuwa nilikatazwa katika kila mji, nitaendelea.”

Huko Erfurt, Luther akapitia katika njia alizokuwa akipitia kila mara, akazuru kijumba chake cha nyumba ya watawa, na akafikiri juu ya mapigano ambamo nuru iliojaa sasa katika Ujeremani imetawanywa juu ya roho yake. Akalazimishwa kuhubiri. Jambo hili alikatazwa kulifanya, lakini mjumbe akamtolea ruhusa, na mtu aliyefanywa zamani mtu wa kazi ngumu za nyumba ya watawa, sasa akaingia kwa mimbara.

Watu wakasikiliza kwa kushangaa sana. Mkate wa uzima ulivunjwa kwa roho hizo zenye njaa. Kristo aliinuliwa mbele yao na juu ya wapapa, maaskofu, wafalme (wakuu), na wafalme. Luther hakusema juu ya maisha yake katika hatari yake. Katika Kristo alikuwa amejisahau mwenyewe. Akajificha nyuma ya Mtu wa Kalvari, akitafuta tu kuonyesha Yesu kama Mkombozi wa wenye zambi.

## Uhodari wa Mfia Dini

Wakati Mtengenezaji alipoendelea mbele, makundi kwa hamu kubwa kwa kusongana karibu naye na kwa sauti za upole waka-

muonya juu ya Waroma. “Watakuchoma”, akasema mwengine, “na kugeuza mwili wako kuwa majivu, kama walivyomfanya Jean Huss.” Luther akajibu, “ijapo wangewasha moto njiani mote toka Worms hata Wittenberg, ... ningetembea kati kati yake kwa jina la Bwana; ningeonekana mbele yao, ... kushuhudia Bwana Yesu Kristo.”

Kukaribia kwake huko Worms kukafanya msukosuko mkubwa. Rafiki wakatetemeka kwa ajili ya usalama wake; maadui wakaogopa kwa ajili ya maneno yao. Kwa ushawishi wa wapadri akalazimishwa kwenda kwa ngome ya mwenye cheo mwema, mahali, ilitangazwa, magumu yote yangeweza kutengenezwa kwa kirafiki. Warafiki wakaonyesha hatari zilizomngoja. Luther, bila kutikisika, akatangaza: “Hata kukiwa mashetani wengi ndani ya mji wa Worms kama vigae juu ya nyumba, lazima nitaingia.”

Alipofika Worms, makundi ya watu wengi sana yakakusanyika kwa milango ya mji kwa kumukaribisha. Kulikuwa wasiwasi nyingi sana. “Mungu atakuwa mkingaji wangu,” akasema Luther alipokuwa [69]
akishuka kwa gari lake. Kufika kwake kulijaza wapadri hofu kuu. Mfalme akawaita washauri wake. Ni upande gani unaopashwa kufuatwa? Padri mmoja mkali akatangaza: “Tumeshauriana mda mrefu juu ya jambo hili. Mfalme mtukufu uondoshe mbio mtu huyu. Upesi, Sigismund hakuwezesha John Huss kuchomwa? Hatulazimishwe kutoa cheti cha mpinga imani ya dini wala kuliheshimu.m “Hapana,” akasema mfalme, “tunapashwa kushika ahadi yetu.” Tulipatana kwamba Mtengenezaji angepashwa kusikiwa.

Mji wote ulitamani kuona mtu huyu wa ajabu. Luther, mwenye kuchoka sababu ya safari, alihitaji ukimya na pumziko. Lakini alifurahia pumziko ya saa chache wakati watu wa cheo kikuu, wenye cheo, wapadri, na wanainchi walimuzunguka kabisa. Kati ya watu hawa walikuwa wenye cheo walioomba na juhudi kwa mfalme matengenezo ya matumizi mabaya ya kanisa. Maadui pamoja na rafiki walifika kumtazama mwa shujaa. Kuvumulia kwake kulikuwa imara na kwa uhodari. Uso wake mdogo wakufifia, ulikuwa uso wa upole na hata wa furaha. Juhudi nyingi ya maneno yake ikatoa uwezo ambao hata maadui zake hawakuweza kusimama kabisa. Wengine walisadikishwa kwamba mvuto wa Mungu ulikuwa naye; wengine wakatangaza, kama walivyofanya wafarisayo juu ya Kristo: “Ana pepo.” Yoane 10:20.

Kwa siku iliyofuata afisa mmoja wa mfalme akaagizwa kumpeleka Luther kwa chumba kikubwa cha wasikilizaji. Kila njia ilijaa na washahidi wenye shauku ya kutazama juu ya mtawa aliyesubutu kushindana na Papa. Jemadari mzee mmoja, aliyeshinda vita nyingi, akamwambia kwa upole: "Maskini mtawa, unataka sasa kwenda kufanya vita kubwa kuliko vita mimi ao kapiteni wengine waliofanya katika mapigano ya damu nyingi. Lakini, ikiwa kama madai yako ni ya haki, ...endelea katika jina la Mungu,na usiogope kitu chochote. Mungu hatakuacha."

## Luther Anasimama Mbele ya Baraza

Mfalme akaketi kitini, anapozungu kwa na watu wa cheo wenye sifa katika ufalme. Martin Luther sasa alipashwa kujibu kwa ajili ya imani yake. "Kuonekana huku kulikuwa kwenyewe ishara (alama) ya ushindi juu ya cheo cha Papa. Papa alimhukumu mtu huyu, na mtu huyu alisimama mbele ya baraza ya hukumu iliyowekwa juu ya Papa. Papa alimweka chini ya makatazo, akakatiwa mbali ya chama
[70] cha kibinadamu, na huku akaalikwa katika manemo ya heshima, na kupokelewa mbele ya mkutano wa heshima sana katika ulimwengu. ... Roma ilikuwa ikishuka kutoka kitini chake, nailikuwa ni sauti la mtawa lililomushusha."

Mzaliwa mnyenyekevu Mtengenezaji akaonekanamwenye kutishwa na kufazaika. Wafalme wengi, wakamkaribia, na mmoja akamnongoneza "Musiwaogope wanaoua mwili lakini hawawezi kuua nafsi." Mwengine akasema: "Na mutakapopelekwa mbele ya watawala na wafalme kwa ajili yangu, mtapewa kwa njia ya roho wa baba yenu lile mtakalo lisema." Tazama Matayo 10:28, 18, 19.

Ukimya mwingi ukawa juu ya mkutano uliosongana. Ndipo afisa mmoja wa mfalme akasimama na, kushota kwa maandiko ya Luther, akauliza kwamba Mtengenezaji ajibu maswali mawili-ao atayakubali kwamba ni yake, na ao atakusudia kukana mashauri yanayoandikwa humo. Vichwa vya vitabu vilipokwisha kusomwa, Luther, kwa swali la kwanza, akakubali vitabu kuwa vyake. "Kwa swali la pili," akasema, ningetenda bila busara kama ningejibu bila kufikiri. Ningehakikisha kidogo kuliko hali ya mambo inavyotaka, ao zaidi kuliko kweli inavyotaka. Kwa sababu hiyo ninaomba mfalme mtukufu,

kwa unyenyekevu wote, unitolee wakati, ili nipate kujibu bila kukosa juu ya neno la Mungu."

Luther akasadikisha makutano kwamba hakutenda kwa hasira ao bila kufikiri. Utulivu huu, na kujitawala, isiyotazamiwa kwa mtu aliyejionyesha kuwa mgumu na asiyebadili shauri yakamwezesha baadaye kujibu kwa busara na heshima ikashangaza maadui zake na kukemea kiburi chao.

Kesho yake alipashwa kutoa jibu lake la mwisho. Kwa mda moyo wake ukadididimia. Maadui zake walionekana kwamba wangeshinda. Mawingu yakakusanyika kando yake na yakaonekana kumtenga na Mungu. Katika maumivu ya roho akatoa malalamiko yale ya kuhuzunisha sana, ambayo Mungu tu anaweza kuyafahamu kabisa.

"Ee Mwenyezi Mungu wa milele!" akapaza sauti; "kama ni kwa nguvu za ulimwengu huu tu ambapo napashwa kutia tumaini langu, yote imekwisha. ... Saa yangu ya mwisho imefika, hukumu yangu imekwisha kutangazwa. ... Ee Mungu, unisaidie juu ya hekima yote ya ulimwengu. ... Mwanzo ni wako, ... na ni mwanzo wa haki na wa milele. Ee Bwana, unisaidie! Mungu mwaminifu na asiyebadilika, mimi si mtumainie mtu ye yote. ... Umenichagua kwa kazi hii. ... Simama kwa upande wangu, kwa ajili ya jina la mpendwa wako Yesu Kristo, anayekuwa mkingaji wangu, ngao yangu, na mnara wangu wa nguvu."

Lakini haikuwa hofu ya mateso, maumivu, wala mauti yake [71]
mwenyewe ambayo ilimlemea na hofu kuu. Alijisika upungufu wake. Katika uzaifu wake madai ya ukweli yangeweza kupata hasara. Si kwa usalama wake mwenyewe, bali kwa ajili ya ushindi wa injili alishindana na Mungu. Katika ukosefu wa usaada imani yake ikashikilia juu ya Kristo, Mkombozi mkuu. Hangeonekana pekee yake mbele ya baraza. Amani ikarudi kwa roho yake, na akafurahi kwamba aliruhusiwa kuinua Neno la Mungu mbele ya watawala wa mataifa.

Luther akawaza juu ya jibu lake, akachunguza maneno katika maandiko yake, na akapata kwa Maandiko matakatifu mahakikisho ya kufaa kwa kusimamia maneno yake. Ndipo, akatia mkono wake wa kushoto kwa Kitabu Kitakatifu, akainua mkono wake wa kuume mbinguni na akaapa kwa kiapo "kukua mwaminifu kwa injili, na

kwa uhuru kutangaza imani yake, hata ingeweza kutia mhuri kwa ushuhuda wake kwa kumtia damu yake."

## Luther Mbele ya Baraza Tena

Wakati alipoingizwa tena ndani ya Baraza, alikuwa mwenye ukimya na amani, lakini shujaa mwenye tabia nzuri, kama mshuhuda wa Mungu miongoni mwa wakuu wa dunia. Ofisa wa mfalme akauliza uamuzi wake. Je, alitaka kukana? Luther akatoa jibu lake kwa sauti ya unyenyekevu, bila ugomvi wala hasira. Mwenendo wake ulikuwa wa wasiwasi na wa heshima; lakini akaonyesha tumaini na furaha ambayo ilishangaza makutano.

"Mfalme mwema sana, watawala watukufu, mabwana wa neema," akasema Luther, "naonekana mbele yenu leo, kufuatana na agizo nililopewa jana. Kama katika ujinga, ningevunja desturi utaratibu wa mahakama, ninaomba munirehemu; kwani sikukomalia katika ma nyumba ya wafalme, bali katika maficho ya nyumba ya watawa."

Ndipo akasema kwamba katika kazi zake zingine zilizochapwa alieleza habari ya imani na matendo mema; hata maadui zake walizitangaza kuwa za kufaa. Kuzikana ingehukumu kweli ambazo wote walikubali. Aina ya pili ni ya maandiko ya kufunua makosa na matumizi mabaya ya cheo cha Papa. Kuharibu haya ni kuimarisha jeuri ya Roma na kufungua mlango kuwa wazi sana kwa ukosefu wa heshima kwa Mungu. Katika aina ya tatu alishambulia watu waliosimamia maovu yanayokuwako. Kwa ajili ya mambo haya akakiri kwa uhuru kwamba alikuwa mkali zaidi kuliko ilivyofaa. Lakini hata vitabu hivi hataweza kuvikana kwani adui za ukweli
[72] wangepata nafasi kwa kulaani watu wa Mungu kwa ukali mwingi zaidi.

Akaendelea, "Nitajitetea mwenyewe kama Kristo alivyofanya: Kama nimesema vibaya, kushuhudia juu ya uovu' ... Kwa huruma za Mungu, ninakusihi, mfalme asio na upendeleo, na ninyi, watawala bora, na watu wote wa kila aina, kushuhudia kutoka kwa maandiko ya manabii na mitume kwamba nilidanganyika. Mara moja ninapokwisha kusadikishwa kwa jambo hili, nitakana makosa yote, na nitakuwa wa kwanza kushika vitabu vyangu na kuvitupa motoni. ...

“Bila wasiwasi, ninafurahi kuona kwamba injili inakuwa sasa kama kwa nyakati za zamani, ambayo ni chanzo cha taabu na fitina. Hii ni tabia, na mwisho wa neno la Mungu. ‘Sikuja kuleta salama duniani lakini upanga,’alisema Yesu Kristo. ... Mujihazali kwamba kwa kuzania munazuia ugomvi musitese Neno takatifu la Mungu na kuangusha juu yenu garika la kutisha la hatari kubwa za misiba ya sasa, na maangamizi ya milele.”

Luther alisema kwa Kijeremani; Sasa aliombwa kukariri maneno yaleyale kwa Kilatini. Akatoa tena maneno yake wazi wazi kama mara ya kwanza. Uongozi wa Mungu ulimusimamia katika jambo hili. Watawala wengi walipofushwa sana na makosa na ibada ya sanamu hata mwanzoni hawakuona nguvu ya mawazo ya Luther, lakini kukariri kukawawezesha kuelewa wazi wazi mambo yaliyoonyeshwa.

Wale waliofunga macho yao kwa nuru juu ya ugumu wakakasirishwa na uwezo wa maneno ya Luther. Mnenaji mkuu wa baraza akasema kwa hasira: “Haujajibu swali lililotolewa kwako. ... Unatakiwa kutoa jibu la wazi na halisi. ... Utakana wala hutakana?”

Mtengenezaji akajibu: “Hivi mtukufu mwema na mwenye uwezo sana unaniomba jibu wazi, raisi,aawa sawa, nitakutolea moja, na ni hili: Siwezi kutoa imani yangu kwa Papa ao kwa baraza, kwa sababu ni wazi kama siku ambayo walikosa na mara kwa mara kubishana wenyewe kwa wenyewe. Ila tu nikisadikishwa na ushuhuda wa Maandiko,... *Siwezi na sitakana,* kwani si salama kwa Mkristo kusema kinyume cha zamiri yake. Ni hapa ninasimamia, siwezi kufanya namna ingine; basi Mungu anisaidie. Amen.”

Ndivyo mtu huyu wa haki alivyosimama. Ukuu wake na usafi wa tabia, amani yake na furaha ya moyo, vilionekana kwa wote alipokuwa akishuhudia ukubwa wa imani hiyo inayoshinda ulimwengu. Kwa jibu lake la kwanza Luther alisema na adabu, kwa hali ya utii kabisa. Watu wa Papa walizania kwamba kuomba wakati ilikuwa tu mwanzo wa kukana. Charles mwenyewe, alipoona hali ya mateso ya mtawa, mavazi yake yasiyokuwa ya zamani, na urahisi wa hotuba yake, akatangaza: “Mtawa huyu hatanifanya kamwe kuwa [73]
mpinga imani ya dini.” Lakini ushujaa na nguvu alioshuhudia sasa, uwezo wa akili yake, ukashangaza watu wote. Mfalme aliposhangaa sana, akapaza sauti: “Mtawa huyu anasema bila kuogopa na moyo usiotikisika.”

Wafuasi wa Roma wakashindwa. Wakatafuta kushikilia mamlaka yao, si kwa kukimbilia kwa Maandiko, bali kwa vitisho, inayokuwa kawaida la Roma. Musemaji wa baraza akasema: "Kama hutaki kukana, mfalme na wenye vyeo wa ufalme wataona jambo gani la kufanya juu ya mpinga imani ya diniasiye sikia nashauri."

Luther akasema kwa utulivu: "Mungu anisaidie, kwani siwezi kukana kitu kamwe."

Wakamwomba atoke wakati watawala walipokuwa wakishauriana pamoja. Kukataa kutii kwa Luther kungeuza historia ya Kanisa kwa myaka nyingi. Wakakata shauri kwa kumpatia nafasi tena ya kukana. Tena swali likaulizwa. Je, angewezekana mafundisho yake? "Sina jibu lingine la kutoa," akasema, "kuliko lile nililokwisha kutoa."

Waongozi wa Papa wakahuzunika kwamba uwezo wao ulizarauliwa na mtawa maskini. Luther alisema kwa wote kwa heshima inayomfaa Mkristo na utulivu, maneno yake hayakuwa na hasira wala masingizio. Akajisahau mwenyewe na kujiona kwamba alikuwa mbele tu ya yeye aliye mkuu wa mwisho sana kuliko wapapa, wafalme, na wafalme (wakuu). Roho ya Mungu ilikuwa pale, kuvuta mioyo ya wakubwa wa ufalme.

Watawala wengi wakakubali wazi wazi haki ya maneno ya Luther. Kundi lingine kwa wakati ule halikuonyesha imani yao, lakini kwa wakati uliokuja wakasaidia bila woga matengenezo.

Mchaguzi Frederic, akasikiliza maneno ya Luther na kuchomwa moyo. Kwa furaha na moyo akashuhudia ushujaa wa mwalimu na kujitawala kwake, na akajitahidi kusimama imara zaidi katika kumtetea. Aliona kwamba hekima ya wapapa, wafalme, na waaskofu inaonekana bure kwa uwezo wa ukweli.

Mjumbe wa Papa alipoona mvuto wa maneno ya Luther, akaamua kutumia njia yote ya uwezo wake ili kumwangamiza Mtengenezaji. Kwa elimu na akili ya ujanja akaonyesha mfalme kijana hatari ya kupoteza urafiki usaada wa Roma kwa ajili ya maneno ya mtawa asiye na maana.

Kesho yake ya jibu wa Luther, Charles akatangaza kwa baraza kusudi lake kwa kudumisha na kulinda dini ya Katoliki. Mashauri ya nguvu yalipashwa kutumiwa juu ya Luther na mambo ya upin-
[74] zani wa imani ya dini aliyofundisha: "Nitatoa mfalme zangu kafara, hazina zangu , rafiki zangu, mwili wangu, damu yangu, roho yangu

na maisha yangu. ... Nitamushitaki na wafuasi wake, kama waasi wapinga imani ya dini, kwa kuwatenga kwa Ushirika takatifu, kwa mkatazo, na kwa namna yo yote iliyofikiriwa kwa kuwaangamiza." Lakini, mfalme akatangaza, hati ya kupita salama ya Luther inapaswa kuheshimiwa. Anapashwa kuruhusiwa kufika nyumbani mwake salama.

## Cheti cha Usalama cha Luther Katika Hatari

Wajumbe wa Papa tena wakaagiza kwamba hati ya kupita salama ya Mtengenezaji isiheshimiwe. "Rhine (jina la mto) unapashwa kupokea majivu yake, kama ulivyopokea yale majivu ya John Huss kwa karne iliyopita." Lakini watawala wa Ujeremani, ingawa walijitangaza kuwa adui kwa Luther, wakakataa kuvunja ahadi iliotolewa mbele ya taifa. Wakataja misiba ambayo iliyofuata kifo cha Huss. Hawakusubutu kuleta juu ya Ujeremani maovu makali mengine.

Charles, kwa kujibu kwa shauri mbaya, akasema: "Ijapo heshima na imani ingepaswa kufutwa mbali ulimwenguni mwote, vinapaswa kupata kimbilio ndani ya mioyo ya wafalme." Akalazimishwa na maadui wa Luther wa kipapa kumtendea Mtengenezaji kama vile Sigismund alivyomtendea Huss. Lakini akakumbuka Huss alipoonyesha minyororo yake kati ya makutano na kumkumbusha mfalme juu ya imani yake aliyoahidi, Charles V akasema, "Singetaka kufazaika kama Sigismund."

Lakini kwa kusudi tu Charles akakataa ukweli uliotolewa na Luther. Alikataa kuacha njia ya desturi kwa kutembea katika njia za kweli na haki. Kama baba zake, alitaka kupigania dini ya Papa. Kwa hiyo akakataa kukubali nuru mbele ya wazazi wake.

Kwa siku zetu, kuna wengi wanaoshikilia desturi za asili za mababa zao. Wakati Bwana anapotuma nuru mpya wanakataa kuipokea kwa sababu haikupokelewa na wababa wao. Hatutakubaliwa na Mungu tunapotazama kwa wababa wetu kwa kuamua wajibu wetu pahali pa kutafuta Neno la Kweli kwa ajili yetu wenyewe. Tutaulizwa juu ya nuru mpya inayoangaza sasa juu yetu kutoka kwa Neno la Mungu.

Uwezo wa Mungu ulisema kupitia Luther kwa mfalme na watawala wa Ujeremani. Roho yake iliwasihi kwa mara ya mwisho kwa wengi katika mkutano ule. Kama Pilato, karne nyingi mbele

[75] yao, kama vile Charles V, katika kujitoa kwa jeuri ya ulimwengu, akaamua kukana nuru ya ukweli.

Mashauri juu ya Luther yakaenea pote, yakaleta wasiwasi katika mji wote. Rafiki wengi, walipojua ukali wa hila ya Roma, wakakusudia kwamba Mtengenezaji hakupaswa kutolewa kafara. Mamia ya wenye cheo wakaahidi kumlinda. Kwa milango ya nyumba na katika pahali pa watu wote matangazo ya kubandikwa ukutani yakawekwa, mengine yalikuwa yakuhukumu na mengine ya kumkubali Luther. Kwa tangazo moja kukaandikwa maneno ya maana, "Ole wako, Ee inchi, wakati mfalme wako ni mtoto." Muhubiri 10:16. Furaha nyingi kwa ajili ya Luther ikasadikisha mfalme na baraza kwamba kila jambo lisilo la haki lililoonyeshwa kwake lingehatarisha amani ya ufalme na nguvu ya kiti cha mfalme.

### Juhudi kwa Ajili ya Masikilizano na Roma

Frederic wa Saxony akaficha kwa uangalifu mawazo yake ya kweli kwa ajili ya Mtengenezaji. Kwa wakati ule akamlinda kwa uangalifu sana, kulinda mazunguko yake na yale ya maadui zake. Lakini wengi hawakujaribu kuficha huruma yao kwa Luther. "Chumba kidogo cha mwalimu," akaandika Spalatin, "hakiwezi kuenea wageni wote waliojileta wenyewe kwa kumuzuru." Hata wale wasiokuwa na imani katika mafundisho yake hawakuweza kujizuia lakini kushangalia ule ukamilifu uliomuongoza kuvumilia mauti kuliko kuvunja zamiri yake.

Juhudi nyingi zikafanyika kwa kupata kuwezesha Luther kupatana na Roma. Wenye cheo na watawala wakamuonyesha kwamba kama akifanya hukumu yake pekee kupinga kanisa na baraza, hatahamishwa kukatiwa mbali ya ufalme na bila ulinzi. Tena akaombwa sana, kutii hukumu ya mfalme. Kwa hiyo hangaliogopa kitu. "Ninakubali," akasema kwa kujibu, "na moyo wangu wote, kwamba mfalme, watawala, na hata Mkristo mnyonge sana, anapashwa kujaribu na kuhukumu kazi zangu; lakini kwa kanuni moja, kwamba wakamate neno la Mungu kuwa kipimo chao. Watu hawana kitu cha kufanya bali kukitii."

Kwa mwito mwengine akasema: "Ninakubali kukana cheti cha usalama wangu. Naweka nafsi yangu na maisha yangu katika mikono ya mfalme, lakini neno la Mungu--kamwe!" Akataja

mapenzi yake kwa kutii baraza la watu wote, lakini kwa kanuni kwamba baraza itakiwe kuamua kufuatana na Maandiko. “Kwa ile inayohusu neno la Mungu na imani, kila Mkristo anakuwa muhukumu mwema kama Papa, ingawa anatetewa na milioni ya [76] mabaraza.” Wote wawili rafiki na maadui, mwishowe, wakasadikishwa kwamba juhudi zaidi juu ya mapatano ingekuwa bure.

Kama Mtengenezaji angelikubali jambo moja tu, Shetani na majeshi yake wangalipata ushindi. Lakini msimamo wake imara usiotikisika ulikuwa njia ya kuweka kanisa kwa uhuru. Mvuto wa mtu mmoja huyu aliyesubutu kufikiri na kutenda kwa ajili yake mwenyewe ulipashwa kwa kugeuza kanisa na ulimwengu, si kwa wakati wake mwenyewe tu, bali kwa vizazi vyote vya baadaye.

Luther aliagizwa upesi na mfalme kurudi nyumbani mwake. Tangazo hili lingefuata kwa upesi na hukumu yake. Mawingu ya kutisha yakafunika njia yake, lakini kama alivyotoka Worms, moyo wake ukajaa na furaha na sifa.

Baada ya kuondoka kwake, ili musimamo wake imara usizaniye kuwa uasi, Luther akaandika kwa mfalme: “Ninakuwa tayari kwa kutii kwa moyo kabisa kwa utukufu wako, katika heshima wala katika zarau, katika maisha ao katika mauti, na kuto kukubali kitu kingine cho chote isipokuwa Neno la Mungu ambalo mtu huishi kwa ajili yake. ... Wakati faida ya milele,inahusika mapenzi ya Mungu si mtu anapashwa kujiweka chini ya mtu. Kwani kujitoa kwa namna ile katika mambo ya kiroho ni kuabudu kwa kweli, na kunapaswa kutolewa kwa Muumba peke yake.”

Kwa safari kutoka Worms, watawala wa kanisa wakakaribisha kama mfalme mtawa aliyetengwa kwa kanisa, na watawala wa serkali wakamheshimu mtu aliyelaumiwa na mfalme. Akalazimishwa kuhubiri, na bila kujali makatazo ya mfalme, akaingia tena kwa mimbara. “Siku ahidi kamwe mimi mwenyewe kufunga neno la Mungu kwa mnyororo,” akasema, “ama sitalifunga.”

Mda kidogo baada ya kutoka Worms, wasimamizi wa Papa wakamshawishi mfalme kutoa amri juu yake. Luther alitangazwa kama “Shetani mwenyewe chini ya umbo la mtu anayevaa kanzu ya watawa.” Mara ruhusa yake ya kupita inapomalizika, mipango ilipaswa kukamatwa kwa ajili ya kukataza kumkaribisha, kumupa chakula wala kinywaji, ao kwa neno ao tendo, msaada wala kushirikiana naye. Alipashwa kutolewa mikononi mwa watawala,

wafuasi wake pia kufungwa na mali yao kunyanganywa. Maandiko yake yalipashwa kuharibiwa, na mwishowe, wote wangesubutu kutenda kinyume cha agizo hili walihusika katika hukumu yake. Mchaguzi wa Saxe na watawala wote, waliokuwa rafiki sana wa Mtengenezaji, walipotoka Worms baada kidogo ya kutoka kwake, na agizo la mfalme likapokea ukubali wa baraza. Waroma wal-
[77] ishangilia. Wakaamini mwicho wa Mtengenezaji kutiwa mhuri kabisa.

## Mungu Anatumia Frederic wa Saxe

Jicho la uangalifu lilifuata mwendo wa Luther, na moyo wa kweli na bora ulikusudia kwa kumwokoa. Mungu ukamtolea Frederic wa Saxe mpango kwa ajili ya ulinzi wa Mtengenezaji. Kwa safari ya kurudi nyumbani Luther akatengana na wafuasi wake na kwa haraka akapelekwa kwa njia ya mwitu kwa jumba la Wartburg, ngome ya ukiwa juu ya mlima. Maficho yake yalifanywa na fumbo ambalo hata Frederic mwenyewe hakujua mahalialipopelekwa. Ujinga huu ulikuwa na kusudi; hivi mchaguzi hakujua kitu, hangeweza kufunua kitu. Akatoshelewa kwamba Mtengenezaji alikuwa salama, akatulia.

Mvua wa nyuma, wakati wajua kali, na wakati wa masika ukapita, na wakati wa baridi ukafika, na Luther aliendelea kuwa mfungwa. Aleander na wafuasi wake wakafurahi. Nuru ya injili ikaonekana karibu kukomeshwa. Lakini nuru ya Mtengenezaji ilipaswa kuendelea kuangaza kwa nguvu zaidi.

## Usalama huko Wartburg

Katika salama ya urafiki wa Wartburg, Luther akafurahi kuwa inje ya fujo ya vita. Lakini kwa sababu ni mtu aliyezoea maisha ya kazi na magumu makali, hangevumilia kukaa bila kufanya lolote. Wakati wa siku za upekee, hali ya kanisa ikafika kwa mawazo yake. Akaogopa kuzaniwa kuwa mwoga kwa kujitosha kwa mabishano. Ndipo akajilaumu mwenyewe kwa uvivu wake na kujihurumia mwenyewe.

Lakini, kila siku alifanya kazi ya ajabu kuliko ingeonekana mtu mmoja kuweza kufanya. Kalamu yake haikukaa bure. Adui zake walishangaa na kufazaika kwa ushuhuda wazi kwamba alikuwa

angali akitumika. Kwa wingi wa vitabu vidogo vya kalamu yake vikaenea katika Ujeremani pote. Akatafsiri pia Agano Jipya kwa lugha ya Ujeremani. Kutoka kwa mwamba wake wa Patemo, akaendelea kwa mda karibu mwaka mzima kutangaza injili na kukemea makosa ya nyakati. Mungu akavuta mtumishi wake kutoka kwa jukwaa ya maisha ya watu. Katika upekee na giza ya kimbilio lake mlimani, Luther akatengwa kwa misaada ya kidunia na kukosa sifa ya kibinadamu. Aliokolewa basi kwa kiburi na kujitumainia vinavyoletwa mara nyingi na ushindi.

Namna watu wanavyofurahia kwa uhuru ambao kweli inawaletea, Shetani anatafuta upotosha mawazo yao na upendo
kutoka kwa Mungu na kuwaimarisha kwa wajumbe wa kibinadamu, [78]
kuheshimu chombo na kutojali Mkono ambao unaoongoza mambo ya Mungu. Mara nyingi waongozi wa dini wanaposifiwa huongozwa kujitumainia wenyewe. Watu wanakuwa tayarikuwaangalia juu ya uongozi badala ya Neno la Mungu. Kutoka katika hatari hii Mungu alitaka kulinda Matengenezo. Macho ya watu yalimugeukia Luther kama mfasi wa ukweli; aliondolewa ili macho yale yote yapate kuongozwa kwa Mwenyezi wa milele wa ukweli.

# [79] 9 /NURU ILIWASHWA KATIKA USUISI

Juma chache baada ya kuzaliwa kwa Luther katika kibanda cha mchimba madini katika Saxe, Ulric Zwingli akazaliwa katika nyumba ndogo ya wachungaji katika milima mirefu ya Alpes. Alipokelewa pahali penye maubule makubwa, akili yake mwanzoni tu ikavutwa na utukufu wa Mungu. Kando ya babu wake mwanamke, alisikiliza hadizi chache za damani za Biblia alizokusanya kwa shida kutoka kwa hadizi na mafundisho ya kanisa yaliyotokea zamani.

Kwa umri wa miaka kumi na mitatu akaenda Berne, mahali palipokuwa shule lililokuwa la sifa sana katika Usuisi. Hapa, lakini, kukatokea hatari. Juhudi nyingi zikafanywa na watawa kwa kumvuta katika nyumba ya watawa. Kwa bahati baba yake akapata habari ya makusudi ya watawa. Aliona kwamba mafaa ya wakati ujao ya mwanawe yalikuwa ya kufa kwa ajili ya imani ya dini na akamwongoza kurudi nyumbani.

Agizo likasikiwa, lakini kijana hakuweza kurizika katika bonde lake la kuzaliwa, akaenda kufuata masomo yake huko Ba le. Ni hapo ambapo Zwingli alisikia mara ya kwanza injili ya neema ya Mungu isiononuliwa. Huko Wittembach, alipokuwa akijifunza (kiyunani) Kigiriki na Kiebrania, akaongozwa kwa Maandiko matakatifu, kwa hivyo nyali za nuru ya Mungu ikatolewa katika akili za wanafunzi aliokuwa akifundisha. Akatangaza kwamba kifo cha Kristo ni ukombozi wa kipekee wa mwenye zambi. Kwa Zwingli maneno haya ni nyali ya kwanza ya nuru unayotangulia mapambazuko.

Zwingli akaitwa upesi kutoka Bale kwa kuingia kwa kazi yake ya maisha. Kazi yake ya kwanza ilikuwa katika vilaya ya milima mirefu. Akatakaswa kama padri, "akajitoa wakfu na roho yake yote kwa kutafuta kweli ya Mungu."

Namna alizidi kutafuta Maandiko, zaidi tofauti ikaonekana kwake kati ya ukweli na mambo ya kupinga imani ya dini ya Roma. Akajitoa mwenyewe kwa Biblia kama Neno la Mungu, amri moja tu inayofaa na ya haki. Aliona kwamba Biblia inapaswa kuwa mfariji wake mwenyewe. Akatafuta usaada wowote kwa kupata ufahamu

kamili wa maana yake, na akaomba usaada wa Roho Mtakatifu. "Nikaanza kumuomba Mungu kwa ajili ya nuru yake, "baadaye akaandika, "na Maandiko yakaanza kuwa rahisi zaidi kwangu."

Mafundisho yaliyohubiriwa na Zwingli hayakupokewa kutoka kwa Luther. Yalikuwa mafundisho ya Kristo. "ikiwa Luther anahubiri Kristo," akasema Mtengenezaji wa Usuisi, "anafanya ninavyofanya. ... Hakuna hata neno moja lililoandikwa nami kwa Luther [80]
wala lililoandikwa na Luther kwangu. Ni kwa sababu gani? ... Ili ipate kuonyeshwa namna gani Roho wa Mungu anakuwa katika sauti moja kwake mwenyewe, hivi sisi wawili, bila mgongano, tunafundisha mafundisho ya Kristo kwa ulinganifu kama huo."

Katika mwaka 1516 Zwingli akaalikwa kuhubiri katika nyumba ya watawa huko Einsiedeln. Hapa alipashwa kutumia kama Mtengenezaji mvuto ambao ungesikiwa mbali hata kuvuka milima mirefu (Alpes) alipozaliwa.

Katika vitu vya mvuto wa Einseideln ni sanamu ya Bikira, walisema kwamba ilikuwa na uwezo wakufanya. Juu ya mlango wa nyumba ya watawa kulikuwa na maandiko, "Ni hapa kunapatikana msamaha wa zambi zote." Makundi mengi wakaja kwa mazabahu ya Bikira kutoka pande zote za Usuisi, na hata kutoka Ufaransa na Ujeremani. Zwingli akapata nafasi ya kutangaza uhuru kwa njia ya injili kwa watumwa hawa wa mambo ya ibada ya sanamu.

"Musizani," akasema, "kwamba Mungu yuko katika hekalu hii zaidi kuliko kwa upande mwingine wauumbaji. ... Je, kazi zisizofaa, safari za taabu, sadaka, masanamu, sala za Bikira ao za watakatifu zingeweza kuwapatia neema ya Mungu? ... Ni manufaa gani ya kofia ya kungaa, kichwa kilichonolewa vizuri, kanzu ndefu na yenye kuvutwa, ao viato vyenye mapambo ya zahabu?" "Kristo," akasema, "aliyetolewa mara moja juu ya msalaba, ni toko na kafara, alifanya kipatanisho kwa ajili ya zambi za waaminifu hata milele."

Kwa wengi lilikuwa uchungu wa kukatisha tamaa kuambiwa kwamba safari yao ya kuchokesha ilikuwa ya bure. Hawakuweza kufahamu rehema waliyotolewa bure katika Yesu Kristo. Njia ya mbinguni iliyowekwa na Roma iliwatoshelea. Ilikuwa ni rahisi sana kutumaini wokovu wao kwa wapadri na Papa kuliko kutafuta usafi wa moyo.

Lakini kundi lingine wakapokea kwa furaha habari za ukombozi kwa njia ya Kristo, na katika imani wakakubali damu ya Muokozi

kuwa kipatanisho chao. Hawa wakarudi kwao kuonyesha wengine nuru ya damani waliyoipokea. Kwa hivi ukweli ukapelekwa mji kwa mji, na hesabu ya wasafiri kwa mahali patakatifu pa Bikira ikapunguka sana. Sadaka sasa zikapunguka, na kwa sababu hiyo mshahara wa Zwingli uliyokuwa ukitoka humo. Lakini jambo hilo lilimletea tu furaha namna alivyoona kwamba uwezo wa ibada ya sanamu ulikuwa ukivunjwa. Ukweli ukapata uwezo kwa mioyo ya watu.

## [81] Zwingli Akaitwa Zurich

Baada ya miaka mitatu Zwingli akaitwa kuhubiri katika kanisa kubwa la Zurich, mji mkubwa sana wa ushirika wa Suisi. Mvuto uliotumiwa hapa ulisikuwa mahali pengi. Wapadri waliomwita kwa kazi hiyo wakawa na uangalifu wa kumfahamisha hawakutaka mageuzi:

"Utaweka juhudi yote kukusanya mapato kwa mfululizo bila kusahau kitu cho chote. ... Utakuwa na juhudi ya kuongeza mapato kutoka kwa wagonjwa, kwa misa, na kwa kawaida kutoka kwa kila agizo la dini." "Juu ya uongozi wa sakramenti, mahubiri, na ulinzi wa kundi, ... unaweza kutumia mtu mwingine, na zaidi sana katika mahubiri."

Zwingli akasikiliza kwa ukimya kwa agizo hili, na akasema kwa kujibu, "Maisha ya Kristo yamefichwa mda mrefu kwa watu. Nitahubiri juu habari yote ya Injili ya Mtakatifu Matayo. ... Ni kwa utukufu wa Mungu, kwa sifa ya mwana wake, kwa wokovu wa kweli wa roho, na kwa kujijenga katika imani ya kweli, ambapo nitajitoa wakfu kwa kazi yangu."

Watu wakajikusanya kwa hesabu kubwa kwa kusikia mahubiri yake. Akaanza kazi yake kwa kufungua Injili na kueleza maisha, mafundisho, na mauti ya Kristo. "Ni kwa Kristo," akasema, "ambapo natamani kuwaongoza ninyi--kwa Kristo, chemchemi ya kweli ya wokovu." Wenye maarifa ya utawala, wanafunzi, wafundi, na wakulima wakasikiliza maneno yake. Akakemea makosa bila hofu na maovu ya nyakati. Wengi wakarudi kutoka kwa kanisa kuu wakimusifu Mungu. "Mtu huyu," wakasema, "ni mhubiri wa ukweli. Atakuwa Musa wetu, kutuongoza kutoka katika giza hii ya Misri."

Baada ya wakati upinzani ukaanza. Watawa wakamushambulia kwa zarau na matusi; wengine wakatumia ukali na matisho. Lakini Zwingli akachukua yote kwa uvumilivu.

Wakati Mungu anapojitayarisha kuvunja viungo vya pingu vya ujinga na ibada ya sanamu Shetani anatumika na uwezo mkubwa sana kwa kufunika watu katika giza na kufunga minyororo yao kwa nguvu zaidi. Roma ikaendelea kutia nguvu mpya kwa kufungua soko yake katika mahali pote pa Ukristo, ukitoa msamaha kwa mali. Kila zambi ilikuwa na bei yake, na watu walipewa chetibila malipo kwa ajili ya zambi kama hazina ya kanisa ililindwa yenyekujaa vizuri. ... Hivi mashauri mawili haya yakaendelea--Roma kuruhusu zambi na kuifanya kuwa chemchemi ya mapato yake, Watengenezaji kulaumu zambi na kuonyesha Kristo kama kipatanisho na mkombozi. [82]

## Uchuuzi wa cheti cha Kuachiwa Zambi katika Usuisi

Katika Ujermani biashara ya kuachiwa (zambi) iliongozwa na mwovu sana Tetzel. Katika Usuisi biashara hii ilikuwa chini ya uongozi wa Samson, mtawa wa Italia. Samson alikuwa amekwisha kujipatia pesa nyingi kutoka Ujeremani na Usuisi kwa kujaza hazina ya Papa. Sasa akapitia Usuisi, kunyanganya wakulima masikini mapato yao machache na kulipisha zawadi nyingi kutoka kwa watajiri. Mtengenezaji kwa upesi akaanza kumpinga. Kufanikiwa kwa Zwingli kulikuwa namna hiyo kufunua kujidai kwa mtawa huyu hata akashurutisha kutoka kwenda sehemu zingine. Huko Zurich, Zwingli akahubiri kwa bidii juu ya wafanya biashara ya msamaha. Wakati Samson alipokaribia mahali pale akakutana na mjumbe aliyemtetea neno kutoka kwa baraza kwa kumwaambia aanze kazi, akatumia mwingilio wa hila, lakini, akarudishwa bila kuuzisha hata barua moja ya msamaha, kwa upesi akatoka Usuisi.

Tauni, au Kifo Kikubwa, kikapitia kwa Usuisi kwa nguvu sana katika mwaka 1519. Wengi wakaongozwa kuona namna ilikuwa bure na bila damani masamaha yaliokuwa wakinunua; wakatamani sana msingi wa kweli wa imani yao. Huko Zurich, Zwingli akagonjwa sana, na habari ikatangazwa sana kwamba alikufa. Kwa saa ile ya kujaribiwa akatazama kwa imani msalaba wa Kalvari, akatumaini kwamba kafara ya Kristo ilikuwa ya kutosha kwa ajili ya zambi. Aliporudi kutoka kwa milango ya mauti, ilikuwa kwa ajili

ya kuhubiri injili kwa bidii kubwa sana kuliko mbele. Watu wao wenyewe walitoka kuangalia mgonjwa karibu ya kifo, wakafahamu vizuri kuliko mbele, damani ya injili.

Zwingli alifikia hali ya kuelewa wazi juu ya ukweli na kupata ujuzi ndani yake uwezo wake unaogeuza. "Kristo," akasema, "... alitupatia ukombozi wa milele ... mateso yake ni ... kafara ya milele, na huleta kupona kwa milele; huridisha haki ya Mungu kwa milele kwa ajili ya wale wote wanaotegemea juu ya kafara yake kwa imani ya nguvu na ya imara. ... Panapokuwa imani katika Mungu, kunakuwa na juhudi inayoendesha na kusukuma watu kwa kazi njema."

Hatua kwa hatua Matengenezo yakaendelea katika Zurich. Katika mushtuko adui zake wakaamka kwa kushindana kwa bidii. Mashambulio mingi yakafanywa juu ya Zwingli. Mwalimu wa wapinga imani ya dini anapashwa kunyamazishwa. Askofu wa
[83] Constance akatuma wajumbe watatu kwa Baraza la Zurich, kumshitaki Zwingli juu ya kuhatarisha amani na utaratibu wa jamii. Kama mamlaka ya kanisa ikiwekwa pembeni, akasema, machafuko kote ulimwenguni yatatokea.

Baraza likakataa kukamata mpango juu ya Zwingli, na Roma ikajitayarisha kwa shambulio jipya. Mtengenezaji akapaliza sauti: "Muache waje"; Ninawaogopa kama vile mangenge yanayo tokajuu yakimbiavyo mavimbi yanayo mgurumo kwa miguu yake." Juhudi za waongozi wa kanisa ziendelesha kazi waliotamani kuharibu. Kweli ikaendelea kusambaa. Katika Ujeremani wafuasi wake, walipohuzunishwa kwa kutoweka kwa Luther, wakatiwa moyo tena walipoona maendeleo ya injili katika Usuisi. Namna Matengenezo yaliimarishwa katika Zurich, matunda yake yalionekana zaidi kabisa katika kuvunjwa kwa uovu na kuendeleshwa utaratibu.

### Mabishano (Wafuasi wa kanisa la Roma)

Kwa kuona namna mateso ya kutangaza kazi ya Luther katika Ujeremani haikufanya kitu, Warumi wakakusudiakuwe mabishano na Zwingli. Walikuwa na hakika ya ushindi kwa kuchagua si makali tu pa vita bali waamuzi waliopashwa kuamua kati ya wabishanaji. Na kama wangeweza kupata Zwingli katika uwezo wao, wangefanya angalisho ili asikimbie. Shauri hili, basi, likafichwa kwa uangalifu.

Mabishano yalipaswa kuwa huko Bade. Lakini Baraza la Zurich, kuzania makusudi ya watu wa Papa na walipoonywa juu ya vigingi vya moto vilivyowashwa katika makambi ya wakatoliki kwa ajili ya washahidi wa injili, wakamkataza mchungaji wao kujihatarisha maisha yake. Kwa kwenda Bade, mahali damu ya wafia dini kwa ajili ya ukweli ilikuwa imetiririka, ingeleta kifo kweli. Oecolampadius na Haller wakachaguliwa kuwa wajumbe wa Watengenezaji, wakati Dr. Eck mwenye sifa, akisaidiwa na jeshi la watu wenye elimu sana na wapadri, alikuwa ndiye shujaa wa Roma.

Waandishi wakachaguliwa wote kwa wakatoliki, na wengine wakakatazwa kuandika ao wasipotii wauwawe. Mwanafunzi mmoja, aliyeshiriki katika mabishano akaandika abari kila jioni juu ya mabishano yaliyofanyika mchana ule. Wanafunzi wawili wengine wakaagizwa kutoa kila siku barua za Oecolampadius, kwa Zwingli huko Zurich. Mtengenezaji akajibu, anapotoa shauri. Kwa kuepuka uangalifu wa mlinzi wa milango ya mji, wajumbe hawa walileta vikapo vya bata juu ya vichwa vyao na wakaruhusiwa kupita bila kizuizi.

Zwingli “alitumika zaidi,” akasema Myconius, “kwa mawazo [84] yake, kukesha kwake usiku, na shauri alilopeleka Bade, kuliko angeweza kufanya kwa kubishana mwenyewe katikati ya adui zake.”

Wakatoliki wakafika Bade na mavazi ya hariri ya fahari sana ya mapambo ya vitu vya damani. Wakasafiri na anasa sana, na kukaa kwa meza zilizojaa vyakula vitamu sana na divai nzuri sana. Kukawa tofauti kubwa sana kati yao na Watengenezajiambao chakula chao cha kiasi kikawakalisha kwa mda mfupi tu mezani. Mwenyeji wa Oecolampade, aliyempeleleza chumbani mwake, akamkuta akijifunza kila wakati ao akiomba, na akajulisha kwamba mpinga imani ya dini huyo alikuwa “mtawa sana.”

Katika mkutano, “Eckakapanda na majivuno katika mimbara iliyopambwa vizuri sana, lakini mnyenyekevu Oecompade, aliyevaa mavazi ya kiasi, akalazimishwa kuchukua kiti chake mbele ya mpinzani wake kwa kiti kilichochorwa vibaya sana.” Sauti ya nguvu ya Eck na majivuno mingi hakumtisha. Mtetezi wa imani alikuwa anatazamia mshahara mzuri. Wakati alipokosa mabishano bora, akatumia matukano na hata maapizo ama laana.

Oecolampade, mwenye adabu na mwenye kujihazari, akakataa kushiriki katika mabishano. Ingawa alikuwa mpole na adabu katika mwenendo, akajionyesha mwenyewe kuwa na uwezo na imara.

Mtengenezaji akashikamana kwa nguvu katika Maandiko. "Desturi," akasema, "haina uwezo katika Usuisi wetu, isipokuwa kwa sheria; sasa katika mambo ya imani, Biblia ndiyo sheria yetu."

Utulivu, kutumia akili kwa Mtengenezaji, unyenyekevu na adabu ulioonyeshwa, ikavuta mafikara na watu wakachukia majivuno ya kiburi cha Eck.

Mabishano yakaendelea kwa mda wa siku kumi na mnane. Wakatoliki wakadai ushindi. Kwa namna wajumbe wengi walikuwa wa upande wa Roma, na baraza ikatangaza kwamba Watengenezaji walishindwa na pamoja na Zwingli, waondoshwe kanisani. Lakini mashindano yakatokea katika mvuto wa nguvu kwa ajili ya Waprotestanti. Baada ya mda mfupi tu, miji mikubwa ya Berne na Bâ le ikajitangaza kuwa kwa upande wa Matengenezo.

# 10 /MAENDELEO KATIKA UJEREMANI [85]

Kutoweka kwa ajabu kwa Luther kukaweka Ujeremani wote katika hofu kubwa. Habari ikatangazwa na wengi wakaamini kwamba aliuawa. Kukawa maombolezo makubwa, na wengi wakaapa kwa kitisho kulipiza kisasi cha kifo chake.

Ijapo waiishangilia mara ya kwanza kwa ajili ya kifo kilichozaniwa cha Luther, adui zake walijazwa na hofu kuwa sasa kwamba amekuwa mfungwa. "Njia moja tu inayotubakilia kwa kuokoa kesi letu," akasema mmoja wao, "ni kuwasha mienge, na kumuwinda Luther katika ulimwengu wote na kumrudisha kwa taifa linalomwita." Kusikia kwamba Luther alikuwa salama, ijapo alikuwa mfungwa, jambo hili likatuliza watu, huku wakisoma maandiko yake kwa bidii sana kuliko mbele. Hesabu ya wale walioongezeka wakajiunga kwa kisa cha mshujaa aliyetetea Neno la Mungu.

Mbegu ambayo Luther alipanda ikatoa matunda mahali pote. kutokuwapo kwake kukafanya kazi ambayo kuwako kwake hakungeweza kufanya. Na sasa mwongozi wao mkuu ameondolewa, watumikaji wengine wakafanya bidii ili kazi ya maana sana iliyoanzishwa isipingwe.

Sasa Shetani akajaribu kudanganya na kuangamiza watu kwa kuwapokeza kazi iliyogeuzwa kwa hila pahali pa kazi ya kweli. Kwa namna kulikuwa Wakristo wa uongo kwa karne la kwanza, ndipo kukatokea manabii wa uongo kwa karne ya kumi na sita.

Watu wachache wakajizania wenyewe kupokea mafumbulio ya kipekee kutoka Mbinguni na kuchaguliwa na Mungu kwa kutimiza kazi ya Matengenezo ambayo ilianzishwa kwa uzaifu na Luther. Kwa kweli, walibomoa kile Mtengenezaji alichofanya. Walikataa kanuni ya Matengenezo kwamba Neno la Mungu ni amri moja tu, ya kutosha ya imani na maisha. Kwa kiongozi kile kisichokosa wakaweka maagizo yao yasiyokuwa ya hakika, ya mawazo yao wenyewe na maono.

Wengine kwa urahisi wakaelekea kwa ushupavu na kujiunga pamoja nao. Mambo ya wenye bidii hawa yakaleta mwamsho

mkubwa. Luther alikuwa ameamsha watu kuona haja ya Matengenezo, na sasa watu wengine waaminifu wa kweli wakaongozwa vibaya na madai ya "manabii" wapya.

Waongozi wa kazi wakaendelea pale Wittenberg na wakalazimisha madai yao juu ya Melanchton: "Tumetumwa na Mungu kwa kufundisha watu. Tulikuwa na mazungumzo ya kawaida pamoja
[86] na Mungu; tunajua jambo litakalotokea; kwa neno moja, tunakuwa mitume na manabii, na tunatoa mwito kwa Mwalimu Luther."

Watengenezaji wakafazaika. Akasema Melanchton; hapa panakuwa kweli roho za ajabu katika watu hawa; lakini roho gani? ... Kwa upande mwengine tujihazari kuzima Roho wa Mungu, na kwa upande mwengine, kwa kudanganywa na roho ya Shetani."

### Tunda la Mafundisho Mapya Limeonekana (limetambulika)

Watu wakaongozwa kuzarau Biblia ao kuikataa yote kabisa. Wanafunzi wakaacha mafundisho yao na kutoka kwa chuo kikubwa. Watu waliojizania kwamba ni wenye uwezo kwa kurudisha nafsi na kuongoza kazi ya Matengenezo wakafaulu tu kuileta katika uharibifu. Sasa Wakatoliki wakapata tumaini lao, nakulalamika kwa furaha. "Juhudi ya mwisho tena, na wote watakuwa wetu."

Luther huko Wartburg, aliposikia mambo yaliyotendeka, akasema na masikitiko sana: "Nilifikiri wakati wowote kwamba Shetani angetumia mateso haya." Akatambua tabia ya kweli ya wale waliojidai kuwa "manabii." Upinzani wa Papa na mfalme haukumletea mashaka makubwa sana na shida kama sasa. Miongoni mwa waliojidai kuwa "rafiki" za Matengenezo, kukatokea adui zake wabaya kuliko kwa kuamsha vita na kuleta fujo.

Luther aliongozwa na Roho wa Mungu na kupelekwa mbali ya kujisikia binafsi. Huku kila mara alikuwa akitetemeka kwa matokeo ya kazi yake: "Kama ningelijua kwamba mafundisho yangu yaliumiza mtu mmoja, mtu mmoja tu, ingawa mnyenyekevu na mnyonge-lisipoweza kuwa, kwani linakuwa ni injili yenyewe--ningekufa mara kumi kuliko mimi kuikana."

Wittenberg yenyewe ilikuwa ikianguka chini ya mamlaka ya ushupavu wa dini isiyo ya akili na machafuko. Katika Ujeremani pote adui za Luther wakatwika mzigo huo juu yake. Katika uchungu wa roho akajiuliza, "Je, ni hapo basi kazi hii kubwa ya Matengenezo

ilipaswa kumalizikia?" Tena, kama vile alikuwa akishindana na Mungu katika sala, amani ikaingia moyoni mwake. "Kazi si yangu, bali ni yako mwenyewe," akasema. Lakini akakusudia kurudi Wittenberg.

Alikuwa chini ya laana ya ufalme; Adui zake walikuwa na uhuru wa kumuua, rafiki walikatazwa kumlinda. Lakini aliona kwamba kazi ya injili ilikuwa katika hatari, na katika jina la Bwana akatoka bila uwoga kupigana kwa ajili ya ukweli. Ndani ya barua kwa mchaguzi, Luther akasema: "Ninaenda Wittenberg chini ya ulinzi wa yule anayekuwa juu kuliko ule wa wafalme na wachaguzi. Sifikiri [87]
kuomba usaada wa fahari yako, wala kutaka ulinzi wako, ningependa kukulinda mimi mwenyewe. ... Hakuna upanga unaoweza kusaidia kazi hii. Mungu peke yake anapashwa kufanya kila kitu." Katika barua ya pili, Luther akaongeza: "Niko tayari kukubali chuki ya fahari yako na hasira ya ulimwengu wote. Je, wakaaji wa Wittenberg si kondoo zangu? Na hainipasi, kama ni lazima, kujitoa kwa mauti kwa ajili yao?"

## Uwezo wa Neno

Makelele haikukawia kuenea katika Wittenberg kwamba Luther alirudi na alitaka kuhubiri. Kanisa likajaa. Kwa hekima kubwa na upole akafundisha na kuonya: "Misa ni kitu kibaya; Mungu huchukia kitu hiki; kinapaswa kuharibiwa. ... Lakini mtu asiachishwe kwacho kwa nguvu. ... Neno ... la Mungu linapasa kutenda, na si sisi. ...Tunakuwa na haki kusema: hatuna na haki kutenda. Hebu tuhubiri; yanayobaki ni ya Mungu. Nikitumia nguvu nitapata nini? Mungu hushika moyo na moyo ukikamatwa, umekamatika kabisa. ...

"Nitahubiri, kuzungumza, na kuandika; lakini sitamshurutisha mtu, kwani imani ni tendo la mapenzi. ... Nilisimama kumpinga Papa, vyeti vya kuachiwa zambi, na wakatoliki, lakini bila mapigano wala fujo. Ninaweka Neno la Mungu mbele; nilihubiri na kuandika--ni jambo hili tu nililolifanya. Na kwani wakati nilipokuwa nikilala, ... neno ambalo nililohubiri likaangusha mafundisho ya kanisa la Roma, ambaye hata mtawala ao mfalme hawakulifanyia mambo mengi mabaya. Na huku sikufanya lolote; neno pekee lilitenda vyote."

Neno la Mungu likavunja mvuto wa mwamusho wa ushupavu. Injili ilirudisha katika njia ya Kweli watu waliodanganywa.

Miaka nyingi baadaye ushupavu wa dini ukainuka pamoja na matokeo ya ajabu. Akasema Luther: "Kwao Maandiko matakatifu yalikuwa lakini barua yenye kufa, na wote wakaanza kupaaza sauti, 'Roho! Roho! ' Lakini kwa uhakika sitafuata mahali ambapo roho yao inawaongoza."

Thomas Munzer, alikuwa na bidii zaidi miongoni mwa washupavu hawa, alikuwa mtu wa uwezo mkubwa, lakini hakujifunza dini ya kweli. "Alipokuwa na mapenzi ya kutengeneza dunia, na akasahau, kama wenye bidii wote wanavyofanya, kwamba ilikuwa kwake mwenyewe ambaye Matengenezo ilipashwa kuanzia." Hakutaka kuwa wa pili, hata kwa Luther. Yeye mwenyewe akajidai kwamba alipokea agizo la Mungu kuingiza Matengenezo ya kweli: "Ye yote
[88] anayekuwa na roho hii, anakuwa na imani ya kweli, ijapo hakuweza kuona Maandiko katika maisha yake."

Waalimu hawa wa bidii wakajifanya wenye kutawaliwa na maono, kuona kuwa kila mawazo na mvuto kama sauti ya Mungu. Wengine hata wakachoma Biblia zao. Mafundisho ya Munzer yakakubaliwa na maelfu. Kwa upesi akatangaza kwamba kutii watawala, ilikuwa kutaka kumtumikia Mungu na Beliali.

Mafundisho ya uasi ya Munzer yakaongoza watu kuvunja mamlaka yote. Sherehe za kutisha za upinzani zikafuata, na mashamba ya Ujeremani yakajaa na damu.

### Maumivu Makuu ya Roho Sasa Yakalemea Juu ya Luther

Wana wa wafalme wa upande wa Papa wakatangaza kwamba uasi ulikuwa tunda ya mafundisho ya Luther. Mzigo huu hakupashwa lakini kuleta huzuni kubwa kwa Mtengenezaji kwamba kisa cha kweli kilipaswa kuaibishwa kwa kuhesabiwa pamoja na ushupavu wa dini wa chini zaidi. Kwa upande mwengine, waongozi katika uasi walimchukia Luther. Hakukana madai yao kwa maongozi ya Mungu tu, bali akawatangaza kuwa waasi juu ya mamlaka ya serkali. Katika uhusiano wakamshitaki yeye kuwa mdai wa msingi.

Roma ilitumainia kushuhudia muanguko wa Matengenezo. Na wakamlaumu Luther hata kwa ajili ya makosa ambayo alijaribu kwa bidii sana kusahihisha. Kundi la ushupavu, likadai kwa uongo

kwamba lilitendewa yasiyo haki, wakapata huruma ya hesabu kubwa ya watu na kuzaniwa kuwa kama wafia dini. Kwa hiyo wale waliokuwa katika kupingana na Matengenezo wakahurumiwa na kusafishwa. Hii ilikuwa kazi ya roho ya namna moja ya uasi wa kwanza uliopatikana mbinguni.

Shetani hutafuta kila mara kudanganya watu na kuwaongoza kuita zambi kuwa haki na haki kuwa zambi. Utakatifu wa uongo, utakaso wa kuiga, ungali ukionyesha roho ya namna moja kama katika siku za Luther, kugeuza mafikara kutoka kwa Maandiko na kuongoza watu kufuata mawazo na maono kuliko sheria za Mungu.

Kwa uhodari Luther akatetea injili kwa mashambulio. Pamoja na Neno la Mungu akapigana juu ya mamlaka ya manyanganyi ya Papa, wakati aliposimama imara kama mwamba kupinga ushupavu uliojaribu kujiunga na Matengenezo.

Pande zote za upinzanihuweka pembeni Maandiko matakatifu, kwa faida ya hekima ya kibinadamu kutukuzwa kawa chemchemi ama asili ya ukweli. Kufuata akili za kibinadamu kwa kusudi [89]
lakuabudu kama Mungu na kufanya hii kanuni kwa ajili ya dini. Kiroma kinadai kuwa na uongozi wa Mungu ulioshuka kwa mustari usiovunjika toka kwa mitume na kutoa nafasi kwa ujinga na uchafu vifichwe chini ya agizo la "mitume". Maongozi yaliyodaiwa na Munzer yalitoka kwa mapinduzi ya mawazo. Ukristo wa kweli hukubali Neno la Mungu kama jaribio la maongozi yote.

Kwa kurudi kwake Wartburg, Luther akatimiza kutafsiri Agano Jipya, na injili ikatolewa upesi kwa watu wa Ujeremani katika lugha yao wenyewe. Ufasiri huu ukapokewa kwa furaha kubwa kwa wote waliopenda ukweli.

Wapadri wakashtushwa kwa kufikiri kwamba watu wote wangeweza sasa kuzungumza pamoja nao Neno la Mungu na kwamba ujinga wao wenyewe ungehatarishwa. Roma ikaalika mamlaka yake yote kuzuia mwenezo wa Maandiko. Lakini kwa namna ilivyozidi kukataza Biblia, ndivyo hamu ya watu ikazidi kujua ni nini iliyofundishwa kwa kweli. Wote walioweza kusoma wakaichukua kwao na hawakuweza kutoshelewa hata walipokwisha kujifunza sehemu kubwa kwa moyo. Mara moja Luther akaanza utafsiri wa Agano la Kale.

Maandiko ya Luther yakapokewa kwa furaha sawasawa katika miji na katika vijiji. "Yale Luther na rafiki zake waliyoandika,

wengine wakayatawanya. Watawa, waliposadikishwa juu ya uharamu wa kanuni za utawa, lakini wajinga sana kwa kutangaza neno la Mungu ... wakauzisha vitabu vya Luther na rafiki zake. Ujeremani kwa upesi ukajaa na wauzishaji wa vitabu wajasiri."

### Kujifunza Biblia Mahali Pote

Usiku waalimu wa vyuo vya vijiji wakasoma kwa sauti kubwa kwa makundi madogo yaliyokusanyika kando ya moto. Kwa juhudi yote roho zingine zikahakikishwa kwa ukweli. "Kuingia kwa maneno yako kunaleta nuru; kunamupa mujinga ufahamu." Zaburi 119:130.

Wakatoliki walioachia mapadri na watawa kujifunza Maandiko sasa wakawaalika kwa kuonyesha uwongo wa mafundisho mapya. Lakini, wajinga kwa Maandiko, mapadri na watawa wakashindwa kabisa. "Kwa huzuni," akasema mwandishi mmoja mkatoliki, "Luther alishawishi wafuasi wake kwamba haikufaa kuamini maneno mengine isipokuwa Maandiko matakatifu." Makundi yakakusanyika kusikia mambo ya kweli yaliyotetewa na watu wa elimu ndogo. Ujinga wa hawa watu wakuu ukafunuliwa kwa kuonyesha uongo wa mabishano yao kwa msaada wa mafundisho rahisi ya
[90] Neno la Mungu. Watumikaji, waaskari, wanawake, na hata watoto, wakajua Biblia kuliko mapadri na waalimu wenye elimu.

Vijana wengi wakajitoa kwa kujifunza, kuchunguza Maandiko na kujizoeza wenyewe na kazi bora ya watu wa zamani. Walipokuwa na akili yenye juhudi na mioyo hodari, vijana hawa wakapata haraka maarifa ambayo kwa wakati mrefu hakuna mtu aliweza kushindana nao. Watu wakapata katika mafundisho mapya mambo ambayo yalileta matakwa ya roho zao, na wakageuka kutoka kwa wale waliowalea kwa wakati mrefu na maganda ya bure ya ibada za sanamu na maagizo ya wanadamu.

Wakati mateso yalipoamshwa juu ya waalimu wa ukweli, wakafuata agizo hili la Kristo: "Na wakati wanapo watesa ninyi katika mji huu, kimbilieni kwa mji mwengine." Matayo 10:23. Wakimbizi wakapata mahali mlango karibu ulifunguka kwao, na waliweza kuhubiri Kristo, wakati mwengine ndani ya kanisa ao katika nyumba ya faragha ao mahali pa wazi. Kweli ikatawanyika kwa uwezo mkubwa usio wa kuzuia.

Ni kwa bure watawala wa kanisa na wa serkali walitumia kifungo, mateso, moto, na upanga. Maelfu ya waaminifu wakatia muhuri kwa imani yao kwa kutumia damu yao, na huku mateso ilitumiwa tu kupanua ukweli. Ushupavu ambao Shetani alijaribu kuunganisha hayo, matokeo yalikuwa wazi kinyume kati ya kazi ya Shetani na kazi ya Mungu.

[91] # 11 /USHUHUDA WA WAANA WA WAFALME

Mojawapo ya shuhuda "maalum"uliotamkwa zaidi kwa ajili ya Matengenezo ulikuwa Ushuhuda uliotolewa na watawala Wakristo wa Ujeremani huko kwa baraza la Spires mwaka 1529. Uhodari na msimamo wa watu wale wa Mungu vikaimarisha uhuru wa zamiri kwa karne zilizofuata, na wakatoa kwa kanisa lililotengenezwa jina la Protestanti.

Maongozi ya Mungu yakazuia nguvu zilizopinga ukweli. Charles Quint akakusudia kuangamiza Matengenezo, lakini mara kwa mara alipoinua mkono wake kwa kupinga akalazimishwa kugeukia kando ya pigo. Tena na tena kwa wakati wa hatari majeshi ya Turki valipotokea kwa mpaka, ao mfalme wa Ufransa ao Papa mwenyewe alifanya vita kwake. Kwa hiyo miongoni ya vita na fujo ya mataifa, Matengenezo yakapata nafasi ya kujiimarisha na kujipanua.

Lakini, wakati ukafika ambao wafalme wakatoliki wakafanya tendo la umoja juu ya kupinga Watengenezaji. Mfalme akaitisha baraza kukutanika huko Spires munamo mwaka 1529 na kusudi la kuharibu upingaji wa imani ya dini. Kama mpango huo ukishindwa kwa njia ya imani Charles alikuwa tayari kutumia upanga.

Wakatoliki huko Spires wakaonyesha uadui wao kwa wazi juu ya Watengenezaji. Akasema Melanchton: "Tunakuwa maapizo na takataka ya ulimwengu; lakini Kristo atatazama chini kwa watu wake maskini, na atawalinda." Watu wa Spires wakawa na kiu cha Neno la Mungu, na, ingawa kulikuwa makatazo, maelfu wakakutanika kwa huduma iliyofanywa ndani ya kanisa ndogo la mchaguzi wa Saxony. Jambo hili likaharakisha shida. Uvumilivu wa dini ukaimarishwa kwa uhalali, na vikao vya injili vikakusudia kupinga uvunjaji wa haki zao. Luther hakuruhusiwa kuwa Spires lakini pahali pake pakatolewa kwa wafuasi wake na watawala ambao Mungu aliinua kwa kutetea kazi yake. Frederic wa Saxony akatengwa na kifo, lakini Duke Jean, muriti wake (aliyemfuata), akakaribisha kwa furaha Matengenezo na akaonyesha uhodari mkubwa.

Mapadri wakadai kwamba taifa ambalo lilikubali Matengenezo liwe chini ya mamlaka ya Warumi. Watengenezaji kwa upande mwengine, hawakuweza kukubali kwamba Roma ilipashwa tena kuleta mataifa yale chini ya utawala wake yale yaliyopokea Neno la Mungu.

Matengenezo haikuanzishwa bado, Amri ya Worms ilipaswa kutumiwa kwa nguvu; na kwamba "Mahali ambapo watu hawangeweza kuilazimisha bila hatari ya uasi, hawakupasa kuingiza matengenezo mapya, ... hawakupashwa kupinga ibada ya misa, hawakupashwa kuruhusu mkatoliki wa Roma kukubali dini ya Luther." Shauri hili likakubaliwa katika baraza, kwa kutoshelewa ukubwa kwa mapadri na maaskofu. [92]

### Mwishowe ikakusudiwa kwamba mahali ambapo

Kama amri hii ingekazwa "Matengenezo hayangeweza kuenezwa ... ao kuanzishwa kwa misingi ya nguvu ... mahali ambapo ilikwisha kuwako." Uhuru ungalikatazwa. Mazungumzo hayangaliruhusiwa. Matumaini ya ulimwengu yangeonekana kukomeshwa.

Washiriki wa kundi la injili wakaangaliana kwa hofu: "Kitu gani kinachofaa kufanywa?" "Je, wakuu wa Matengenezo wanapaswa kutii, na kukubali amri hiyo? ... Waongozi wa Luther wakapewa uhuru wa ibada ya dini yao. Fazili ya namna moja ikatolewa kwa wale wote waliokubali Matengenezo kabla ya kuwekwa kwa amri walikuwa wamekwisha kukubali maoni ya matengenezo. Je, jambo hilo halinge wapendeza? ...

"Kwa furaha wakaangalia kanuniambapo matengenezo yaliwekwa kwa msingi ulioazimiwa, na wakatenda kwa imani. Kanuni ile ilikuwa nini? Ilikuwa haki ya Warumi kushurutisha zamiri na kukataza uhuru wa kuuliza swali. Lakini, hawakuwa wao wenyewe na watu wao Waprotestanti kuwa na furaha ya uhuru wa dini? Ndiyo, kama fazili ya upekee iliyofanywa katika mapatano, lakini si kama haki. ... Ukubali wa matengenezo yaliyotakiwa kwamba ruhusa ya kuingia uhuru ya dini ilipashwa kuwa tu kwa mategenezo ya Saxony na kwa pande zingine zote za misiki ya kikristo uhuru wa kuuliza swalina ushuhuda wa imani ya matengenezo vilikua kuasi na vilipashwa kuuzuriwa kifungoni na kifo cha kuchomwa kwa mti.

Je, waliweza kuruhusu kutumia mahali maalum kwa uhuru wa dini? . . . Je, Watengenezaji wangeweza kujitetea kwamba walikuwa bila kosa kwa damu ya wale mamia na maelfu ambao katika kufuata kwa mapatano haya, wangetoa maisha yao katika inchi zote za kanisa la Roma?"

"Hebu tukatae amri hii," wakasema watawala. "Katika mambo ya zamiri uwingi wa watu hawana uwezo." Kulinda uhuru wa zamiri ni kazi ya taifa, na huu ndiyo mpaka wa mamlaka yake katika mambo ya dini.

Wakatoliki wakakusudia kuvunja kile walichoita "ushupavu hodari (uhodari usio wa kuachia mtu nafasi yoyote)." Wajumbe wa miji iliyokuwa na uhuru waliombwa kutangaza kwamba wangekubali
[93] maneno ya mashauri yaliyo kusudiwa. Waliomba muda, lakini kwao hawakukubaliwa. Karibu nusu ya watu walikuwa kwa upande wa Watengenezaji, wakijua kwamba musimamo wao utawapeleka kwa hukumu ijayo na mateso. Mmoja akasema, "Tunapashwa kukana neno la Mungu, ao kuchomwa."

## Ushindani Bora wa Waana wa Wafalme

Mfalme Ferdinand, mjumbe wa mfalme, akajaribu ufundi wa mvuto. "Akaomba waana wa wafalme kukubali amri, kuwahakikishia kwamba mfalme angependezwa sana nao." Lakini watu hawa waaminifu wakajibu kwa upole: "Tutamtii mfalme kwa kila kitu kitakacholeta amani na heshima ya Mungu."

Mwishowe mfalme akatangaza kwamba "njia yao moja tu inayobaki ilikuwa ni kujiweka nchini ya walio wengi." Alipokwisha kusema basi, akaenda zake, bila kuwapa Watengenezaji nafasi ya kujibu. "Wakatuma ujumbe kusihi mfalme arudi : Akajibu tu, "Ni jambo lilokwisha kukatwa; kutii ni kitu tu kinachobaki."

Watu wa kundi la mfalme wakajisifu wenyewe kwamba sababu ya mfalme na Papa ilikuwa na nguvu, na kwamba ile ya Watengenezaji ni zaifu. Kama Watengenezaji wangetumainia usaada wa mtu tu, wangalikuwa wazaifu kama walivyo zaniwa na wafuasi wa Papa. Lakini wakaita "kutoka kwa taarifa la baraza kuelekea Neno la Mungu, na badala ya mfalme Charles, kwa Yesu Kristo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana."

Kama vile Ferdinand alivyokataa kujali nia za zamiri yao, watawala wakakusudia bila kujali kukosekana kwake, bali kuleta ushuhuda wao mbele ya baraza la taifa bila kukawia. Tangazo la heshima likaandikwa na kuwekwa kwa mkutano:

"Tunashuhudia kwa wanaokuwa hapa ... kwamba sisi, kwa ajili yetu na kwa ajili ya watu wetu, hatukubali wala kupatana katika namna yote kwa amri iliyokusudiwa, katika kila kitu kinachokuwa kinyume kwa Mungu, kwa Neno lake takatifu, kwa zamiri yetu ya haki, kwa wokovu wa roho zetu ... kwa sababu hii tunakataa utumwa ambao unaotwikwa juu yetu. ... Na vilevile tunakuwa katika matumaini kwamba utukufu wake wa kifalme utatenda mbele yetu kama mfalme Mkristo anayempenda Mungu kupita vitu vyote; na tunatangaza sisi wenyewe kuwa tayari kulipa kwake, na kwenu pia, watawala wa neema, upendo wote na utii unavyokuwa wajibu wetu wa haki na wa sheria."

Wengi wakajaa na mshangao na mshituko wa hofu kwa ushujaa [94] wa washuhuda. Fitina, ushindano, na kumwaga damu ilionekana bila kuepukwa. Lakini Watengenezaji, katika kutumainia silaha ya mamlaka Kuu, walikuwa wenyekujazwa na "uhodari tele na ujasiri."

"Kanuni zilizokuwa katika ushuhuda huu wa sifa ... ilianzisha msingi kabisa wa Kiprotestanti. ... Kiprotestanti kinatia uwezo wa zamiri juu ya muhukumu na mamulaka ya Neno la Mungu juu ya kanisa linaloonekana ... Husema pamoja na manabii na mitume "Imetupasa kutii Mungu kuliko mwanadamu. Kuwako kwa taji la Charles V kiliinua taji la Yesu Kristo." Ushuhuda wa Spires ulikuwa ushuhuda wa heshima juu ya ushupavu wa dini na madai ya haki ya watu wote kwa kuabudu Mungu kwa kupatana na zamiri zao wenyewe.

Maarifa ya Watengenezaji bora hawa yanakuwa na fundisho kwa ajili ya vizazi vyote vinavyofuatana. Shetani angali anapinga Maandiko yaliyofanywa kuwa kiongozi cha maisha. Kwa wakati wetu kuna haja ya kurudi kwa kanuni kubwa ya ushuhuda--Biblia, na ni Biblia peke, kama kiongozi cha amri ya imani na kazi. Shetani angali anatumika kwa kuharibu uhuru wa dini. Uwezo wa mpinga Kristo ambao washuhuda wa Spires walikataa sasa unatafuta kuanzisha mamlaka yake iliyopotea.

## Makutano Huko Augsburg

Watawala wa injili walinyimwa kusikiwa na Mfalme Ferdinand, lakini kwa kutuliza magomvi yaliyosumbua ufalme, Charles V katika mwaka uliofuata Ushuhuda wa Spires akaita makutano huko Augsburg. Akatangaza kusudi lake kwa kuongoza mwenyewe. Waongozi wa Kiprotestanti wakaitwa.

Mchaguzi wa Saxony akashurutishwa na washauri wake asionekane kwa makutano: "Je, hivyo si kujihatarisha kwa kwenda kwa kila kitu na kujifungia ndani ya kuta za muji pamoja na adui wenye nguvu?" Lakini wengine wakamwambia kwa uhodari "Acha watawala tu wapatane wao wenyewe na uhodari na hoja ya Mungu itaokoka." "Mungu ni mwaminifu: hatatuacha," akasema Luther.

Mchaguzi akashika safari kwenda Augsburg. Wengi wakaenda kwenye mkutano na uso wa huzuni na moyo wa taabu. Lakini Luther aliyewasindikiza hata Coburg, akaamsha imani yao kwa kuimba wimbo ulioandikwa walipokuwa safarini, "ngome yenye uwezo ndiye Mungu wetu'. Mioyo nyingi yenye uzito ikawa nyepesi kwa sauti za juhudi za kutia moyo.

[95] Watawala walioongoka wakakusudia kuwa na maelezo ya maono yao, pamoja na ushuhuda kutoka kwa Maandiko, ya kuonyesha mbele ya mkutano. Kazi ya matayarisho yake ikapewa Luther, Melanchton na washiriki wao. Ungamo hili likakubaliwa na Waprotestanti, na wakakusanyika kwa kutia majina yao kwa maandiko ya mapatano.

Watengenezaji walitamani zaidi bila kuchanganisha hoja yao na maswali ya siasa. Kama vile watawala Wakikristo waliendelea kutia sahihi ya ungamo, Melanchton akaingia kati, na kusema, "Ni kwa wachunguzi wa mambo ya dini na wahubiri kwa kutoa shauri la mambo haya; tuchunge maoni mengine kwa ajili ya mamlaka ya wakuu wa inchi." "Mungu anakataza" akajibu Jean wa Saxony, "Kwamba mgenitenga. Ninakusudia kutenda yaliyo haki, bila kujihangaisha mimi mwenyewe juu ya taji langu. Natamani kungama Bwana. Kofia yangu ya uchaguzi na ngozi ya mapendo ya wahukumu si vya damani kwangu kama msalaba wa Yesu Kristo." Akasema mwengine katika watawala alipochukua kalamu, "Kama heshima ya Bwana wangu Yesu Kristo huidai, niko tayari ... kuacha mali na maisha yangu nyuma." "Tafazali ningekataa mambo yangu

na makao yangu, zaidi kutoka inchini mwa baba zangu na fimbo mkononi," akaendelea, "kuliko kukubali mafundisho mengine mbali na ambayo yanayokuwa katika ungamo hili."

Wakati ulioagizwa ukafika. Charles V, akazungukwa na wachaguzi na watawala, akakubali kuonana na Watengenezaji wa Waprotestanti. Katika mkutano tukufu ule mambo ya kweli ya injili yakatangazwa wazi wazi na makosa ya kanisa la Papa yakaonyeshwa. Siku ile ikatangazwa "siku kubwa sana ya Matengenezo, na siku mojawapo ya utukufu katika historia ya Kikristo na ya wanadamu."

Mtawa wa Wittenberg akasimama peke yake huko Worms. Sasa mahali pake kukawa watawala hodari kuliko wa ufalme. "Ninafurahi sana," Luther akaandika, "kwamba nimeishi hata kwa wakati huu, ambao Kristo ametukuzwa wazi wazi na mashahidi bora kama hawa, na katika mkutano tukufu sana."

Ujumbe ambao mfalme alioukataza kuhubiriwa kwa mimbara ukatangazwa kwa jumba lake la kifalme. Maneno ambayo wengi waliifikiri kama yasiyofaa hata mbele ya watumikaji, yalisikiwa kwa mshangao na mabwana wakubwa na watawala wa ufalme. Wafalme walikuwa wahubiri, na mahubiri yalikuwa kweli aminifu ya Mungu. "Tangu wakati wa mitume hapakuwa kazi kubwa kuliko, ao maungamo mazuri zaidi."

Mojawapo ya kanuni imara zaidi iliyoshikwa nguvu na Luther ilikuwa kwamba haifae kutumainia uwezo wa kidunia katika kusaidia Matengenezo. [96] Alifurahi kwamba injili ilitangazwa na watawala na ufalme; lakini wakati walipokusudia kuungana katika chama cha utetezi, akatangaza kwamba "mafundisho ya injili itatetewa na Mungu peke yake. ... Uangalifu wote wa siasa uliokusudiwa ulikuwa katika maoni yake, kwamba ulitolewa na hofu isiyofaa na shaka ya zambi."

Kwa tarehe ya baadaye, kufikiri juu ya mapatano yaliyoazimiwa na Wafalme walioongoka, Luther akatangaza kwamba silaha ya pekee tu katika vita hii inapashwa kuwa "upanga wa Roho." Akaandika kwa mchaguzi wa Saxony: "Hatuwezi kwa zamiri yetu kukubali mapatano yaliyokusudiwa. Msalaba wa Kristo unapaswa kuchukuliwa. Hebu utukufu wako uwe bila hofu. Tutafanya mengi zaidi kwa maombi yetu kuliko maadui wetu wote kwa majivuno yao."

Kutoka kwa pahali pa siri pa sala kukaja uwezo uliotetemesha ulimwengu katika Matengenezo. Huko Augsburg Luther "hakupitisha siku bila kujitoa kwa maombi kwa masaa tatu." Ndani ya chumba chake cha siri alikuwa akisikia kumiminika kwa roho yake mbele ya Mungu kwa maneno "yanayojaa na kuabudu na hofu na matumaini." Kwa Melanchton akaandika: "Kama sababu si ya haki, tuiache; kama sababu ni ya haki, sababu gani kusingizia ahadi za yule anaye tuagiza kulala bila hofu?" Watengenezaji wa Kiprotestanti walijenga juu ya Kristo. Milango ya kuzimu haitalishinda!

# 12 /MAPAMBAZUKO KATIKA UFRANSA [97]

Ushuhuda wa Spires na Ungamo la Augsburg yalifuatwa na miaka ya vita na giza. Yakazoofishwa na migawanyiko, Kiprotestanti kikaonekana katika hali ya kuangamizwa.

Lakini wakati wa ushindi huu wa wazi mfalme akapigana sana na kushindwa. Mwishowe akalazimishwa kukubali kuachia uhuru mafundisho ambayo ilikuwa tamaa ya nguvu katika maisha yake ya kuyaharibu. Aliona majeshi yake kuangamizwa na vita, hazina zake kutiririka, watu wengi wa ufalme wake kutiishwa na uasi, na po pote ambapo imani aliyojitahidi kukomesha ikaenea. Charles V alikuwa akigombeza uwezo wa Mwenye mamlaka yote. Mungu alisema, "Nuru iwe," lakini mfalme akataka kudumisha giza. Aliposhindwa kutimiza makusudi yake, akazeeka upesi, akajitosha kitini cha ufalme na akaenda kujizika mwenyewe katika nyumba ya watawa.

Katika Uswisi, hivi makambi mengi yalikubali imani ya Matengenezo, wengine wakajifungia kwa imani ya Roma. Mateso juu ya wafuasi ikaamka kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Zwingli na wengi waliojiunga katika Matengenezo wakaanguka kwa shamba la damu la Cappel. Roma ikawa na ushindi na katika mahali pengi ikaonekana kupata yote aliyopoteza. Lakini Mungu hakusahau kazi yake wala watu wake. Kwa upande mwengine akainua watumishi kuendesha kazi ya Matengenezo.

Katika Ufransa mmojawapo wa kwanza kupata nuru alikuwa ndiye Lefévre; mwalimu katika chuo kikuu cha Paris. Katika uchunguzi wake wa vitabu vya maandiko ya zamani, uangalifu wake ukaongozwa kwa Biblia, na akaingiza mafundisho yake miongoni mwa wanafunzi wake. Akaanza kutayarisha historia ya watakatifu wa wafia dini kama ilivyotolewa katika mapokeo ya kanisa, na alikuwa amekwisha kufanya maendeleo ya namna sana kwa hayo, alipofikiri kwamba angeweza kupata usaada kutoka kwa Biblia, akaanza mafundisho yake. Na hapa kweli akapata watakatifu, lakini si kama vile ilionekana katika kalenda ya Roma (Kanisa la Katoliki).

Katika machukio akaenda zake kwa kazi aliyojiagizia mwenyewe na akajitoa wakfu kwa Neno la Mungu.

Katika mwaka 1512 kabla ya Luther ao Zwingli walikuwa hawajaanza kazi ya Matengenezo, Lefévre akaandika, "Ni Mungu anayetupatia, kwa imani, haki ile ambayo kwa neema pekee hutuhesabia haki kwa uzima wa milele." Na wakati alipofundisha kwamba
[98] utukufu wa wokovu ni wa Mungu tu, na akatangaza pia kwamba kazi ya kutii ni ya binadamu.

Wengine miongoni mwa wanafunzi wa Lefévre wakasikiliza kwa bidii maneno yake na wakati mrefu baada ya sauti ya mwalimu kunyamaza, wakaendelea kutangaza ukweli. Mmoja wao alikuwa William Farel. Alikelewa kwa wazazi watawa na mkatoliki mwenye juhudi, alitamani sana kuharibu kila kitu kilichojaribu pinga kanisa. "Ningesaga meno yangu kama mbwa mwitu mkali," akasema baadaye. "Ninaposikia mtu ye yote kusema kinyume cha Papa." Lakini ibada ya watakatifu, kuabudu mbele ya mazabahu, na kupambwa na zawadi za mahali patakatifu hakukuweza kuleta amani ya roho. Kusadikishwa kwa zambi kukaimarishwa juu yake, ambako matendo yote ya toba yalishindwa kumupa uhuru. Akasikiliza maneno ya Lefévre: "Wokovu ni kwa neema." "Ni msalaba wa Kristo tu unaofungua milango ya mbinguni, na kufunga milango ya kuzimu."

Kwa kutubu kama kule kwa Paulo, Farel akageuka kutoka kwa utumwa wa asili hata kwa uhuru wa wana wa Mungu. "Baada ya moyo wa uuaji wa mbwa mwitu mkali," akarudi akasema, "kwa kimya kama mwana kondoo mwema na mpole, moyo wake wote umeondolewa kwa Papa, na ukatolewa kwa Yesu Kristo."

Wakati Lefévre alipokuwa akitawanya nuru miongoni mwa wanafunzi, Farel akaendelea kutangaza kweli wazi wazi. Mkuu mmoja wa kanisa, askofu wa Meaux, akajiunga mara kwao. Waalimu wengine wakaungana katika kutangaza injili, na ikavuta wafuasi kutoka kwa makao ya wafundi na wakulima hata kwa jumba la mfalme. Dada wa Francis I akakubali imani ya Matengenezo. Kwa matumaini bora ya Watengenezaji walitazamia wakati ambapo Ufransa ulipaswa kuvutwa kwa injili.

## Agano Jipya la Kifransa

Lakini matumaini yao hayakutimia. Majaribu na mateso ikangoja wanafunzi wa Kristo. Walakini, wakati wa amani ukafika, ambao wangeweza kupata nguvu kwa kukutana na tufani, na matengenezo yakafanya maendeleo ya upesi. Lefévre akaanza kutafsiri wa Agano Jipya; na kwa wakati uleule ambapo Biblia ya Jeremani ya Luther ilipomalizika kutoka kwa mtambo wa kupigia chapa katika Wittenberg, Agano Jipya la Kinfransa likachapwa huko Meaux. Kwa upesi wakulima wa Meaux wakapata Maandiko matakatifu. Watu wa kazi katika mashamba, wafundi katika kiwanda cha kufanyia kazi, wakafurahishwa na kazi yao ya kila siku kwa kuzungumza habari ya damani ya kweli ya Biblia. Ijapo walikuwa watu wa cheo cha chini [99] kabisa, bila elimu na kazi ngumu ya ukulima, matengenezo, uwezo unaogeuza, wa neema ya Mungu ukaonekana katika maisha yao.

Nuru iliyoangaza huko Meaux ikatoa nyali yake mbali. Kila siku hesabu ya waliogeuka ilikuwa ikiongezeka. Hasira kali ya serkali ya kanisa ikakomeshwa kwa mda kwa kizuio cha mfalme, lakini wafuasi wa Papa wakashinda mwishowe. Mti wakuchoma wa pinga dini kukawashwa. Wengi walioshuhudia juu ya ukweli wakawa katika miako ya moto.

Ndani ya vyumba vikubwa vya majumba na majumba ya kifalme, kulikuwa roho za kifalme ambamo ukweli ulikuwa wa damani kuliko utajiri ao cheo ao hata maisha. Louis de Berquin alikuwa mzaliwa wa jamaa ya cheo kikubwa, aliyejitoa kwa majifunzo, mwenye kuadibishwa na tabia isiyolaumiwa. "Akakamilisha kila namna ya wema kwa kushika mafundisho ya Luther katika machukio makuu ya kipekee." Lakini, kwa bahati njema akaongozwa kwa Biblia, akashangazwa kupata pale "si mafundisho ya Roma, bali mafundisho ya Luther." Akajitoa mwenyewe kwa kazi ya injili.

Mamlaka ya Papa ya Ufransa ikamtia gerezani kama mpinga imani ya dini, lakini akafunguliwa na mfalme. Kwa miaka nyingi Francis alikuwa akisitasita kati ya Roma na Matengenezo. Mara tatu Berquin akafungwa na mamlaka ya Papa, na akafunguliwa na mfalme, aliyekataa kumtoa kafara kwa ukorofi wa serkali ya kanisa. Berquin akazidi kuonywa juu ya hatari iliyotaka kumpata katika Ufransa na akalazimishwa kufuata hatua za wale waliok-

wenda kutafuta usalama katika kuhamishwa kwa mapenzi mbali na kwao.

## Berquin Shujaa

Lakini juhudi ya Berquin ikazidi kuwa na nguvu. Akakusudia mpango wa nguvu zaidi. Hakusimama tu kwa kutetea ukweli, lakini akashambulia kosa. Adui zake waliokuwa na juhudi na ukaidi zaidi walikuwa watawa wenye elimu kutoka kwa idara ya elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini (theologie) katika chuo kikubwa (université) cha Paris, mojawapo ya mamlaka ya kanisa ya juu sana katika taifa. Kwa maandiko ya waalimu hawa, Berquin akapata makusudi kumi na mbili ambayo akaitangaza wazi wazi kuwa kinyume cha Biblia," na akauliza mfalme kujifanya muamzi katika shindano.

Mfalme, kwa kuwa na furaha ya nafasi ya kushusha majivuno ya hawa watawa wenye kiburi, akaalika wakatoliki kutetea jambo lao kwa kufuata Biblia. Silaha hii haingewasaidia zaidi; mateso na kifo
[100] cha mtu wa kuchoma ilikuwa ndizo silaha ambazo walizifahamu zaidi namna ya kutawala. Sasa wakajiona wenyewe kuanguka katika shimo walilotumaini kumtumbukiza Berquin. Wakatafuta wenyewe namna gani ya kujiepusha.

"Kwa wakati ule wakaona kando ya mojawapo ya njia sanamu ya bikira iliyovunjwa." Makundi yakakusanyika mahali pale, wakilia na hasira. Mfalme akachomwa moyo sana . "Haya ndiyo matunda ya mafundisho ya Berquin," watawa wakapaza sauti. "Kila kitu ni karibu kugeuzwa--dini, sheria, kiti cha ufalme chenyewe kwa mapatano hii ya Luther."

Mfalme akatoka Paris, na watawa wakaachiwa huru kufanya mapenzi yao. Berquin akahukumiwa na kuhukumiwa kifo. Kwa hofu kwamba Francis angetetea tena kwa kumwokoa, hukumu ikafanyika kwa siku ile ile ilio tamkwa. Kwa sasa sita za mchana msongano wengi ukakusanyika kwa kushuhudia jambo hili, na wengi wakaona kwa mshangao kwamba mtu aliyeteswa alichaguliwa miongoni mwa watu bora na wahodari zaidi wa jamaa bora za Ufransa. Mshangao, hasira, zarau, na uchuki wa uchungu yakahuzunisha nyuso za kundi lile, lakini kwa uso mmoja haukuwa na kivuli. Mfia dini alikuwa na zamiri tu ya kuwako kwa Bwana wake.

Uso wa Berquin ulikuwa ukingaa na nuru ya mbinguni. Alivaa vazi kama joho laini la kungaa, chuma puani na soksi ya zahabu.” Alikuwa karibu kushuhudia imani yake mbele ya Mfalme wa wafalme, na hakuna dalili iliyopasa kusingizia furaha yake.

Wakati mwandamano ulipokuwa ukisogea polepole katika njia zilizosongana, watu wakapatwa na mshangazo wa ushindi wa furaha wa uvumilivu wake. “Yeye anakuwa,” wakasema, “kama mmoja anayekaa katika hekalu, na akififikiri vitu vitakatifu.”

## Berquin kwa Mti Wakufungia Watu wa Kochomwa Moto

Katika mti Berquin akajitahidi kusema maneno machache kwa watu; lakini watawa wakaanza kupaza sauti na askari kugonganisha silaha zao, na makelele yao yakazamisha sauti ya mfia dini. Hivi kwa mwaka 1529 mamlaka kubwa sana ya kanisa na elimu ya Paris “ikatoa kwa watu wa 1793 mfano wa msingi wa kusongwa juu ya jukwaa (mahali pa kunyongwa) maneno takatifu ya wenye kufa.” Berquin akanyongwa na mwili wake ukateketezwa katika miako ya moto.

Waalimu wa imani ya matengenezo wakaenda katika mashamba mengine ya kazi. Lefévre akaenda Ujermani. Farel akarudi kwa mji wake wa kuzaliwa upande wenashariki ya Ufransa, kutawanya [101] nuru katika makao ya utoto wake. Ukweli aliuofundisha ukapata wasikizaji. Kwa upesi akafukuzwa mbali ya mji. Akapitia vijijini, akifundisha katika makao ya upekee na mashamba ya majani ya uficho, kutafuta kimbilio katika pori na katika mapango ya miamba yaliyokuwa makao yake katika utoto wake.

Kama katika siku za mitume, mateso “yametokea zaidi kwa kuendesha Habari Njema.” Wafilipi 1:12. Walipofukuzwa kutoka Paris na Meaux, “Wale waliosambazwa wakaenda pahali po pote wakihubiri neno.” Matendo 8:4. Ni kwa namna hiyo nuru ilitawanyika mahali pengi katika majimbo ya mbali ya Ufransa.

## Mwito wa Calvin

Katika mojawapo ya mashule ya Paris, kulikuwa kijana mmoja mwangalifu, mtulivu, kijana aliyeonekana na maisha yasiyokuwa na kosa, kwa ajili ya bidii ya elimu na kwa ajili ya ibada ya dini. Tabia

yake na matumizi vikamufanya kuwa majivuno ya chuo kikubwa, na ilikuwa ikitumainiwa kwa siri kwamba Jean Calvin angekuwa mmojawapo miongoni mwa watetezi wenye uwezo sana, wa kanisa. Lakini mshale wa nuru ukaangazia kuta za elimu nyingi na ibada ya sanamu ambayo Calvin amajifungia. Olivetan, binamu mtoto wa ndungu wa Calvin, alijiunga na Watengenezaji. Ndugu hawa wawili wakazungumza pamoja juu ya maneno ambayo yanasumbua jamii la kikristo. "Hapo kuna dini mbili tu ulimwenguni," akasema Olivetan, Mprotestanti. "Ile ... ambayo watu wamevumbua, ambamo mtu hujiokoa mwenyewe kwa sherehe na kazi nzuri; ingine ni ile dini ambayo inayofunuliwa katika Biblia, na ambayo hufundisha mtu kutumaini wokovu tu kwa neema bila bei kutoka kwa Mungu."

"Sitaki mafundisho yenu mapya," akajibu Calvin; "Unafikiri kwamba nimeishi katika kosa siku zangu zote?" Lakini peke yake chumbani akatafakari maneno ya binamu (cousin) wake. Akajiona mwenyewe kuwa bila mpatanishi mbeie ya Mhukumu mtakatifu na wa haki. Matendo mazuri, sherehe za kanisa, yote yalikuwa bila uwezo kwa upatanisho kwa ajili ya zambi. Ungamo, kitubio, hayakuweza kupatanisha roho pamoja na Mungu.

## Ushahidi kwa Mchomo

Calvin akapitia siku moja katika uwanja mkubwa, kwa bahati njema akaona mpinga ibada ya dini anapokufa kwa moto. Miongoni mwa mateso ya kifo cha kuhofisha na chini ya kukatiwa hukumu kwa kanisa, mfia dini akaonyesha imani na uhodari ambao mwanafunzi
[102] kijana kwa uchungu aliona ni kinyume kwa ukosefu wa tumaini lake mwenyewe na giza. Juu ya Biblia, alijua, "wazushi" walidumisha imani yao. Akakusudia kujifunza Biblia yenyewe na kuvumbua siri ya furaha yao.

Ndani ya Biblia akampata Kristo. "Ee Baba," akalia, "Kafara yake ilituliza hasira yako; Damu yake imesafisha takataka zangu; Msalaba wake ulichukua laana yangu; Mauti yake ilitoa kafara kwa ajili yangu. ... Umegusa moyo wangu, ili niweze kusimama katika matendo mema mengine yote kama mahukizo isipokuwa matendo mema ya Yesu.

Sasa akakusudia kutoa maisha yake kwa injili. Lakini kwa tabia alikuwa mwenye woga na alitamani kujitoa mwenyewe kuji-

funza. Maombi ya bidii ya rafiki zake, lakini, mwishowe yakashinda ukubali wake kwa kuwa mwalimu wa watu wote. Maneno yake yalikuwa kama umande unaoanguka kwa kuburudisha udongo. Alikuwa sasa katika mji wa jimbo chini ya ulinzi wa binti kifalme Margeurite, ambaye, kwa kupenda injili, akaeneza ulinzi wake kwa wanafunzi wake. Kazi ya Calvin ikaanza pamoja na watu nyumbani mwao. Wale waliosikia ujumbe wakachukua Habari Njema kwa wengine. Akaendelea, kuweka msingi wa makanisa yaliyopaswa kutoa ushuhuda hodari kwa ajili ya ukweli.

Mji wa Paris ulipashwa kupokea mwaliko mwengine kwa kukubali injili. Mwito wa Lefévre na Farel ulikataliwa, lakini ujumbe ulipashwa kusikiwa tena kwa vyeo vyote katika mji mkuu ule. Mfalme alikuwa hajakamata mpango wa kuwa upande wa Roma kupinga Matengenezo. Margeurite (dada yake) alitamani kwamba imani ya Matengenezo ihubiriwe katika Paris. Akaagiza mhubiri wa Kiprotestanti kuhubiri katika makanisa. Jambo hili likakatazwa na mapadri wa Papa, binti mfalme akafungua jumba. Ikatangazwa kwamba kila siku hotuba inapaswa kufanyika, na watu wakaalikwa kuhuzuria. Maelfu wakakusanyika kila siku.

Mfalme akaagiza kwamba makanisa mawili ya Paris yalipaswa kufunguliwa. Kamwe mji ulikuwa haujavutwa na Neno la Mungu kama wakati ule. Kiasi, usafi, utaratibu, na utendaji, mambo yale yakachukua pahali pa ulevi, uasherati, shindano, na uvivu. Weakati walikubali injili, walio wengi wa watu wakaikataa. Wakatoliki wakafaulu kupata tena uwezo wao. Tena makanisa yakafungwa na mti wa kufungia watu wakuchomwa ukasimamishwa.

Calvin alikuwa akingali Paris. Mwishowe mamlaka ikakusudia kumleta kwa ndimi za moto. Hakuwa na mawazo juu ya hatari wakati rafiki walikuja kwa haraka kwa chumba chake na habari kwamba wakuu walikuwa njiani mwao kumfunga. Kwa wakati ule [103]
sauti ya bisho likasikiwa kwa mlango wa inje. Hapo hapakuwa na wakati wa kupoteza. Rafiki wakakawisha wakuu mlangoni na wengine wakasaidia Mtengenezaji kumshusha chini kwa dirisha, na kwa haraka akaenda kwa nyumba ndogo ya mtu wa kazi aliyekuwa rafiki wa Matengenezo. Akajigeuza mwenyewe kwa mavazi ya mwenyeji wake na, kuchukua jembe mabegani, akaanza safari yake. Akasafiri upande wa Kusini, akapata tena kimbilio katika utawala wa Margeurite.

Calvin hakuweza kubakia wakati mrefu bila kazi. Mara msukosuko ulipotulia akaenda kutafuta shamba mpya ya kazi huko Poities, mahali makusudi mapya yalikuwa ya kufaa kukubaliwa. Watu wa namna zote walisikiliza kwa furaha habari njema. Kwa namna hesabu ya wasikilizaji ilivyokuwa ikiongezeka, wakafikiri kwamba ni vyema kukusanyikia inje ya mji. Kwa pango mahali miti na miamba ya juu ya uficho pakachaguliwa kuwa mahali pa mkutano. Katika mahali hapa pa uficho Biblia ikasomwa na kufasiriwa. Hapo ibada ya meza ya Bwana ikafanyika kwa mara ya kwanza kwa Waprotestanti wa Ufransa. Kwa kanisa ndogo hilo kukatoka wahubiri wengi waaminifu.

Mara ingine tena Calvin akarudi Paris, lakini akakuta karibu kila mlango wa kazi umefungwa. Yeye mwishowe akakusudia kwenda Ujeremani. Kwa shida aliacha Ufransa wakati zoruba ilitokea juu ya Waprotestanti. Watengenezaji wa Ufransa wakakusudia kupambana na pigo hodari juu ya mambo ya ibada ya sanamu ya Roma ile iliyopashwa kuamsha taifa lote. Matangazo kwa kushambulia misa katika usiku moja yakawekwa kwa Ufransa pote. Mahali pa kuendeleza kazi ya Matengenezo, tendo hilo la upumbavu likawapa Warumi sababu ya kudai kuangamizwa kwa "wapinga ibada ya dini" kama wafitini wa hatari kwa usitawi wa kiti cha mfalme na amani ya taifa.

Mojawapo ya matangazo liliwekwa kwa mlango wa chumba cha pekee cha mfalme. Uhodari wa upekee wa kujiingiza kwa maneno ya kushangaza haya mbele ya mfalme na jambo hilo likaamsha hasira ya mfalme. Ghazabu yake ikapata usemi katika maneno makali: "Wote wakamatiwe bila tofauti wanaozaniwa kuwa wafuasi wa Luther. Nitawaangamiza wote." Mfalme akajiweka kwa upande wa Roma.

### Utawala wa Hofu Kuu

Mfuasi maskini wa imani ya matengenezo aliyezoea kuita
[104] waaminifu kwa mikutano ya siri akakamatwa. Kwa kutishwa juu ya kifo cha gafula kwa mti wa kuchomwa, akaamuriwa kuongoza mjumbe wa Papa kwa nyumba ya kila mprotestanti katika mji. Hofu ya ndimi ya moto ikawa nyingi sana, na akakubali kusaliti ndugu zake. Morin, polisi wa mfalme, pamoja na msaliti, kwa

polepole na ukimya akapita katika njia za mji. Walipofika mbele ya nyumba ya mtu mmoja wa Luther, msaliti akafanya ishara, lakini bila kusema neno. Mwandamano ukasimama, wakaingia nyumbani, jamaa likakokotwa na kufungwa minyororo, na mfuatano wa kutisha ukaendelea katika kutafuta watu wengine wapya wa kutesa. "Morin akatetemesha mji wote. ... Ulikuwa utawala wa hofu kuu."

Watu walioteswa wakauawa kwa mateso makali, ikaamriwa kwamba moto upunguzwe ili kuzidisha mateso yao. Lakini walikufa kama washindaji, musimamo wao usiotikisika, amani yao kamili. Watesi wao wakajiona wenyewe kwamba walishindwa. "Watu wa Paris wote wakapata nafasi ya kuona aina gani ya watu mawazo mapya yaliweza kuleta. Hakuna mimbara ilikuwako kwa kulinganishwa na mjumba kubwa la wafia dini. Furaha ikaangazia nyuso kunjufu za watu hawa wakati walipokuwa wakielekea ... pahali pa kuuawa ... na kuomba kwa usemaji wa kushangaza kwa ajili ya injili."

Waprotestanti wakasitakiwa kwamba walikusudia kuua wakatoliki, kupindua serkali, na kumua mfalme. Hawakuweza kutoa hata kivuli cha ushahidi kwa kushuhudia mambo yenyewe. Huku ukali ukapiga juu ya Waprotestanti wasio na kosa ukaongezeka kwa uzito wa malipizi, na katika karne zilizofuata kukatokea maangamizi ya namna ile waliyotabiri juu ya mfalme, serkali yake, na raia wake. Lakini yakaletwa na wakafiri na wakatoliki wao wenyewe.

Kuvunja dini ya Kiprotestanti ndiko kulileta juu ya Ufransa misiba hii ya kutisha. Mashaka, hofu, na vitisho sasa vikaenea kwa makundi yote ya jamii. Mamia wakakimbia kutoka Paris, wakajihamisha wenyewe kutoka inchini mwao ya kuzaliwa, wengi kati yao wakatoa ishara ya kwanza kwamba walikubali imani ya matengenezo. Wafuasi wa Papa wakashangazwa na hesabu kubwa ya "wapinga ibada ya dini" isiyofikiriwa iliyovumiliwa miongoni mwao.

## Kupiga Chapa Kulikatazwa

Francis I akapendezwa kukusanya kwa uwanja wake watu wenye elimu ya maandiko kutoka kwa inchi zote. Lakini, wenye mafikara [105]
na juhudi ya kukomesha uzushi, baba huyu wa elimu akatoa amri kutangaza kwamba uchapaji wa vitabu umeondolewa pote katika

Ufransa! Francis I ni mojawapo wa mifano ya historia kuonyesha kwamba akili ya masomo hailinde watu juu ya ushupavu wa dini na mateso.

Wapadri wakadai kwamba aibu iliyofanyiwa Mbingu ya juu kwa hukumu ya misa isafishwe katika damu. Tarehe 21 Januari 1535, iliwekwa juu ya sherehe ya kutisha. Mbele ya kila mlango mwenge wa moto ukawashwa kwa ajili ya heshima ya "sakramenti takatifu." Mbele ya usiku kucha makutano yakakutanika kwa jumba la mfalme.

"Majeshi yakachukuliwa na askofu wa Paris chini ya chandaluwa nzuri, ... Baada ya majeshi kutembeza mfalme ... Francis I kwa siku ile hakuvaa taji, wala kanzu ya cheo." Kwa kila mazabahu akainama kwa kujinyenyekea, si kwa ajili ya makosa iliyonajisi roho yake, ao damu isiyo na kosa iliyoharibu mikono yake, bali kwa ajili ya "zambi ya mauti" ya watu wake waliosubutu kuhukumu misa.

Katika chumba kikubwa cha mjumba la askofu mfalme akatokea na katika maneno ya usemi wa hasira akasikitikia "makosa, matukano, siku ya huzuni na haya," ambayo ilikuja juu ya taifa. Na akaalika waaminifu wake wa ufalme kusaidia kungoa baala ya "uzushi" ambayo ilitisha Ufransa kwa uharibifu. Machozi yakajaa kwa usemi wake, na mkutano wote ukaomboleza, kwa umoja wakasema kwa nguvu, "Tutaishi na kufa kwa ajili ya dini yaKikatoliki!"

"Neema ile iletayo wokovu" ilionekana, lakini Ufransa ilipoangaziwa na mwangaza wake, ikautupilia mbali, ikachagua giza zaidi kuliko nuru. Wakaita ubaya wema, na wema ubaya, hata walipoanguka kuwa watu wa kuteswa kwa hila yao ya ukaidi. Nuru ambayo ingeweza kuwaokoa kwa udanganyifu, kwa kuchafua roho zao na kosa ya uuaji, wakaikataa kwa kuasi.

Tena mkutano ukafanyika. "Kwa mwendo mfupi (majukwaa) mahali pa kunyongea watu yakajengwa mahali Wakristo wa Kiprotestanti walipashwa kuchomwa motoni wakiwa hai, na ilitengenezwa kwamba matata yawashwe wakati mfalme alipokaribia, na kwamba mwandamano ulipashwa kusimama kwa kushuhudia wauaji." Hapakuwa na kutikisika kwa upande wa watu waliopashwa kufa. Kwa kushurutishwa kukana, mmoja akajibu: "Mimi naamini tu yale manabii na mitume waliyohubiri mbele na yale jamii lote la

watakatifu waliamini. Imani yangu inakuwa na tumaini kwa Mungu ambaye atashinda mamlaka yote ya kuzimu."

Katika kufikia jumba la mfalme, makutano yakatawanyika na mfalme na maaskofu wakaondoka, walipokuwa wakishangilia wenyewe kwamba kazi ingeendelea kwa kutimiza maangamizo ya [106] wapinga ibada ya dini."

Habari Njema ya amani ambayo Ufransa ilikataa ilipashwa kungolewa kweli, na matokeo yalikuwa ya kutisha. Tarehe 21 ya Januari 1793, mwandamano mwengine ukapita katika njia za Paris. "Tena mfalme alikuwa mwongozi mkuu; tena kukawa fujo na kulalamika; tena kukasikiwa kilio cha watu wengi walioteswa; tena kukawa majukwaa meusi; na matukio ya siku yakamalizika kwa mauaji na sana; Louis XVI, alipokuwa akishindana mikononi mwa walinzi wake wa gereza na wanyongaji, akakokotwa kwa gogo, na hapo akashikwa kwa nguvu nyingi hata shoka lilipoanguka, na kichwa chake kilichokatwa kikajifingirisha kwa jukwaa." Karibu na mahali pale pale watu 2800 wakaangamizwa na machine yenye kisu cha kukata watu kichwa (guillotine). Matengenezo ikaonyesha kwa ulimwengu Biblia yenye kufunguliwa. Upendo usio na mwisho ukajulisha watu kanuni za mbinguni. Wakati Ufransa ilipokataa zawadi ya mbinguni, ikapanda mbegu ya uharibifu. Hakukuwa namna ya kuepuka matokeo yaliyotendeka ambayo mwisho ulikuwa mapinduzi na utawala wa kuhofisha.

Farel shujaa na mwenye uhodari akalazimishwa kukimbia kutoka kwa inchi yake ya kuzaliwa na kwenda Uswisi. Lakini akaendelea kutumia mvuto uliokusudiwa juu ya matengenezo katika Ufransa. Pamoja na usaada wa watu wengine waliofukuzwa, maandiko ya Watengenezaji wa Ujeremani yakatafsiriwa katika Kifransa na pamoja na Biblia ya Kifransa ikachapwa kwa wingi sana. Kwa njia ya watu wa vitabu vya dini vitabu hivyo vikauzishwa kwa eneo kubwa sana katika Ufransa.

Farel akaingia kwa kazi yake katika Uswisi kwa mwenendo mnyenyekevu wa mwalimu, akaingiza kwa werevu kweli za Biblia. Wengine wakaamini, lakini wapadri wakaja kusimamisha kazi, na watu wenye ibada ya sanamu wakaharakishwa kuipinga. "Hiyo haiwezi kuwa injili ya Kristo," wapadri wakashurutisha, "kuona kuihubiri hakuwezi kuleta amani, bali vita."

Akaenda mji kwa mji, kuteseka na njaa, baridi, na kuchoka,na mahali pote katika ajali ya maisha yake. Akahubiri sokoni, ndani ya makanisa, mara zingine katika mimbara ya makanisa makubwa. Zaidi kuliko mara moja akapigwa karibu kufa. Lakini akaendelea mbele. Mwishowe akaona miji mikubwa na midogo iliokuwa ngome za kanisa la Katoliki yakafungua milango yao kwa injili.

Farel alitamani kusimamisha bendera ya Waprotestanti katika Geneve. Kama mji huu ungaliweza kupatikana, ungalikuwa mahali
[107] pa kubwa kwa ajili ya Matengenezo katika Ufransa, Uswisi, na Italia. Miji mingi iliyokuwa kandokando ya miji midogo ikaamini.

Pamoja na rafiki mmoja akaingia Geneve. Lakini akaruhusiwa kuhubiri mara mbili tu. Mapadri wakamwalika mbele ya baraza la kanisa, wakaja na silaha zilizofichwa chini ya makanzu yao, wakakusudia kutoa maisha yake. Inje ya chumba kulikuwa na watu wengi wenye hasira kuhakikisha kifo chake kama akiepuka baraza. Kuwako kwa waamzi na waaskari, ingawa hivyo wakamwokoa. Mapema sana asubuhi akapelekwa karibu ya ziwa mahali pa salama. Ndivyo ilivyokuwa mwisho wa juhudi yake ya kwanza ya kueneza injili huko Geneve.

Kwa kusikilizwa mara ya pili, wakachagua chombo kizaifu sana; alikuwa kijana munyonge kwa sura hata akapokelewa bila furaha na marafiki wanaojidai kusimamia Matengenezo. Lakini mtu wa namna hii angeweza kufanya nini mahali Farel alikataliwa? "Mungu alichagua vitu zaifu vya dunia kupatisha vitu vya nguvu haya." 1 Wakorinto 1:27.

## Froment Mwalimu

Froment akaanza kazi yake kama mwalimu. Kweli alizofundisha watoto chuoni wakayakariri nyumbani mwao. Mara wazazi wakasikia Biblia ilipokuwa ikielezwa. Agano Jipya na vitabu vidogo vikatolewa bure. Baada ya mda mtumikaji huyu pia alipashwa kukimbia, lakini kweli alizofundisha ikaingia mioyoni mwa watu. Matengenezo yakapandwa. Wahubiri wakarudi, na ibada ya Kiprotestanti ikaanzishwa katika Geneve.

Miji ulikuwa ukmekwisha kutangazwa kuwa upande wa Matengenezo wakati Calvin, alipoingia katika milango yake. Alikuwa

njiani kwenda Basel alipolazimishwa kupitia njia ya kuzunguka zunguka kupitia Geneve.

Katika kuzuru huku Farel akatambua mkono wa Mungu. Ingawa Geneve ilikubali imani ya Matengenezo, lakini kazi ya kuongoka ilipaswa kutendeka ndani ya moyo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, si kwa amri za mabaraza. Wakati watu wa Geneve walipokataa mamlaka ya Roma, hawakuwa tayari kabisa kuacha makosa yaliyositawishwa chini ya amri yake.

Kwa jina la Mungu Farel akamsihi kwa heshima mhubiri kijana kudumu na kufanya kazi huko Calvin akarudi nyuma kuonyesha hatari. Akajitenga ili asipambane kwa ha tari na roho ya ukali ya watu wa Geneve. Alihitaji kupata mahali pa amani na ukimya kwa majifunzo, na pale kwa njia ya vitabu angeweza kufundisha [108]
na kujenga makanisa. Lakini hakujaribu kukataa. Ilionekana kwake "kwamba mkono wa Mungu ulishuka kutoka mbinguni, kwamba ukamushika, na ukamukaza bila kubadilika kubakia mahali alipokuwa na haraka ya kutoka."

## Ngurumo ya Laana

Laana za Papa zikanguruma juu ya Geneve. Namna gani mji huu mdogo ulishindana na mamlaka hodari ya kanisa ambalo lilitetemesha wafalme na watawala kutii?

Kushinda kwa kwanza kwa Matengenezo kukapita, Roma ikakusanya nguvu mpya kwa kutimiza maangamizi yake. Amri ya Wa-Jesuite ikaanzishwa, kali zaidi, ya tabia mbaya, na hodari kuliko washujaa wote wa Papa. Hawakujali upendo wa kibinadamu, na zamiri yote ikanyamazishwa, hawakujali amri, upendo, lakini ile ya agizo lao. (Tazama mwisho wa kitabu.)

Injili ya Kristo iliwezesha wafuasi wake kuvumilia mateso, bila kukatishwa tamaa na baridi, njaa, kazi ngumu na umaskini, kushindania kweli machoni pa mbao (zenye vyango) za kutundikia, gereza, na kigingi. Kijesuitisme kikatia wafuasi wake moyo mamlaka ya kweli silaha zote za udanganyifu. Hawakuogopa kufanya kosa kubwa ao kutumia uwongo wa haya, kwao kujigeuza sura kwa uwongo haikuwa taabu. Ilikuwa shabaha yao waliyojifunza kukomesha dini ya Kiprotestanti na kuimarisha utawala wa Papa.

Walivaa vazi la utakatifu, wakizuru nyumba za gereza na mahospitali, kusaidia wagonjwa na maskini, na kuchukua jina takatifu la Yesu, aliyekwenda akifanya matendo mema. Lakini chini ya umbo la inje lisilo na kosa, makusudi mabaya na ya uuaji yalikuwa yakifichwa.

Ilikuwa kanuni ya asili ya amri kwamba “mwisho huthibitisha njia. Uongo, wizi, ushuhuda wa uongo, mauaji ya siri, yaliruhusiwa yalipotumiwa kwa faida ya kanisa. Kwa siri Wajesuite walikuwa wakiingia ndani ya maofisi ya serkali nakupanda juu, kuwa washauri wa mfalme na kuongoza mashauri ya mataifa. Wakajifanya watumishi kwa kupeleleza mabwana wao. Wakaanzisha vyuo vikubwa kwa ajili ya watoto wa watawala na watu wakuu, na vyuo kwa ajili ya watu wote. Watoto wa wazazi wa Kiprotestanti kwa njia ya vyuo hivyo walikuwa wakivutwa kushika kanuni za kanisa la Papa. Kwa hivyo uhuru ambao mababa zao walikuwa wakishindania na kutoka damu ukasalitiwa na watoto wao. Po pote, Wajesuites
[109] walipokwenda, kukafuata mwamsho wa mafundisho ya kanisa la Papa.

Kwa kuwapatia uwezo mwingi, tangazo la Papa likatolewa kwa kuimarisha (“Inquisition”) (Baraza kuu la kuhukumia wapinga ibada ya dini la Papa. Mahakama haya ya kutisha yakawekwa tena na wajumbe wa kanisa la Roma, na mambo mabaya ya kutisha kwa kuweza kuonyeshwa mchana yakakaririwa ndani ya gereza za siri (cachots). Katika inchi nyingi maelfu na maelfu ya watu--wa faida kuu kwa taifa, wenye elimu sana na waliojifunza zaidi, waliuawa ao kulazimishwa kukimbilia kwa inchi zingine. (Tazama Nyongezo.)

### Ushindi kwa Ajili ya Matengenezo

Ndizo zilikuwa njia ambazo Roma ilitumia kuzima nuru ya Matengenezo, kwa kuondolea watu Neno la Mungu, na kwa kuimarisha ujinga na ibada ya sanamu ya Miaka ya Giza. Lakini chini ya mibaraka ya Mungu na kazi za watu bora ambao aliinua kwa kufuata Luther, dini ya Kiprotestanti haikukomeshwa. Si kwa wema ao kwa silaha za wafalme ambaye iliweza kupata nguvu zake. Inchi ndogo sana na mataifa zaifu zaidi yakawa ngome zake. Ilikuwa Geneve ndogo; ilikuwa Hollande, kushindana juu ya ukorofi wa Espagne;

ilikuwa Suede ya ukiwa na ukame, ambazo zilipata ushindi kwa ajili ya Matengenezo.

Karibu miaka makumi tatu Calvin alitumika Geneve kwa ajili ya maendeleo ya Matengenezo pote katika Ulaya. Mwenendo wake haukuwa bila kosa, wala mafundisho yake kukosa kuwa na makosa. Lakini alikuwa chombo cha kutangaza ukweli ya maana ya kipekee; katika kuimarisha dini ya Kiprotestanti juu ya mwendo wa kurudi kwa upesi kufaulu kwa kanisa la Papa, na kwa ajili ya kuingiza katike makanisa ya Matengenezo unyofu na usafi wa maisha.

Kutoka Geneve, wakaenda kutangaza mafundisho ya Matengenezo. Hapo, inchi zote za watu walioteswa wakatafuta kupata mafundisho na kutiwa moyo. Mji wa Calvin ukawa kimbilio la Watengenezaji waliowindwa katika Ulaya yote ya Magharibi. Wakakaribishwa vizuri na kutunzwa vizuri sana; na wakapata makao pale, wakaletea mji uliowapokea mibaraka ya ufundi wao, elimu yao, na utawa wao. John Knox, Mtengenezaji hodari wa Scotland (Ecosse), si hesabu ndogo ya watu wanyofu wa Uingereza, Waprotestanti wa Hollande na wa Espagne, na wa Huguenots wa Ufaransa, wakachukua kutoka Geneve mwenye wa ukweli kuangazia giza kwa inchi zao za kuzaliwa.

## [110] 13 /KATIKA UHOLANDI NA SCANDANAVIA

Katika Uholandi ukali wa Papa ukaleta haraka upinzani. Miaka mia saba kabla ya Luther, askofu wa Roma kwa uhodari akashitakiwa na maaskofu wawili, waliotumwa kuwa mabalozi huko Roma, wakajifunza tabia ya kweli ya "jambo takatifu la askofu"; "Unakaa mwenyewe ndani ya hekalu la Mungu; baada ya mchungaji unakuwa mbwa mwitu kwa kondoo, ... lakini ulipashwa kuwa mtumishi wa watumishi, kama upendavyo kujiita mwenyewe, unatumaini kuwa bwana wa mabwana. ... Unaleta haya kwa amri za Mungu."

Wengine wakatokea katika karne zote kukariri kukataa huku. Biblia ya Wavaudois ilitafsiriwa katika lugha ya Kijeremani. Wakatangaza "kwamba hapo kulikuwa faida ndani yake; hakuna mizaha wala uongo, wala mambo ya michezo, wala udanganyifu, bali maneno ya kweli." Ndivyo waliandika rafiki za imani ya zamani tangu karne ya kumi na mbili.

Sasa wakati wa mateso ya kanisa la Roma ikaanza; lakini waaminifu wakaendelea kuongezeka, kutangaza kwamba Biblia ni mamlaka pekee ya haki katika dini na kwamba "hakuna mtu anayepashwa kushurutishwa kuamini, bali angepashwa kusadikishwa kwa njia ya mahubiri."

Mafundisho ya Luther yakapata katika Uholandi watu wa juhudi na waaminifu kwa kuhubiri injili. Menno Simons, mtu wa elimu mkatoliki na aliyetakaswa kwa upadri, alikuwa mjinga kabisa wa Biblia na hakuisoma kwa ajili ya hofu ya upinzani wa ibada ya dini. Kwa ondoleo la zambi akajitahidi kunyamazisha sauti ya zamiri, lakini bila manufaa. Baada ya wakati akaongozwa kujifunza Agano Jipya; hili pamoja na maandiko ya Luther ikamletea kukubali imani ya matengenezo. Kwa mda kitambo akashuhudia mtu aliyeuawa kwa sababu alibatizwa mara ya pili. Jambo hili likamwongoza kujifunza Biblia kwa ajili ya ubatizo wa watoto wadogo. Aliona kwamba toba na imani vinahitajiwa kuwa sababu ya ubatizo.

Menno akatoka kwa kanisa la Roma na akajitoa wakfu kwa kufundisha maneno ya ukweli aliyokubali. Katika Ujeremani na Uholandi kundi la washupavu likatokea, kuharibu kanuni na adabu, na kuendelea kufanya maasi. Menno kwa nguvu zake zote akapinga mafundisho ya uongo na mashauri ya ushenzi ya washupavu. Kwa miaka makumi mbili na tano akapitia Uhollande na upande wa kaskazini ya Ujeremani, kutumia mvuto mkubwa sana, kufananisha katika maisha yake mwenyewe mafundisho aliyofundisha. Alikuwa mtu wa haki, mpole na mtulivu, mwaminifu na mwenye bidii. [111]
Hesabu kubwa ya watu wakageuka sababu ya kazi zake.

Katika Ujeremani Charles V alikomesha Matengenezo, lakini watawala wakasimama kama boma juu ya utawala wa ukaidi wake. Katika Uhollande mamlaka yake ilikuwa kubwa sana. Amri za mateso zikafuatana kwa upesi. Kwa kusoma Biblia, kuisikia ao kuihubiri, kumwomba Mungu kwa siri, kukataa kusujudu mbele ya sanamu ao kuimba Zaburi ilikuwa azabu ya kifo. Maelfu waliangamia chini ya Charles na Philip II.

Kwa wakati moja jamaa lote lilipelekwa mbele ya watu wa hekimu (Inquisiteurs), juu ya kutokwenda kwa misa na kuabudu nyumbani. Kijana wa mwisho katika jamaa akajibu "Tunapiga magoti yetu, na kuomba kwamba Mungu apate kuangaza akili zetu na kusamehe zambi zetu; tunaombea utawala wa mfalme wetu, ili ufalme wake upate kusitawi na maisha yake yawe ya furaha; tunawaombea waamzi wetu, ili Mungu apate kuwalinda." ''Baba na mmojawapo wa watoto wake wakahukumiwa kifo cha (kigingi) mti wa kuchoma upinzani wa ibada ya dini."

Si wanaume tu lakini wanawake na vijana wanawake wakatumia ujasiri imara. "Bibi waliweza kusimama kwa vigingi vya waume wao, na wakati walipokuwa wakivumilia mchomo wa moto wangenongoneza maneno ya faraja ao kuimba zaburi kuwatia moyo." "Wasichana wakalazwa ndani ya kaburi zao kana kwamba walikuwa wakiingia katika chumba chao kulala usiku; ao kwenda kwa jukwaa na moto, wakijivika kwa mapambo yao mazuri sana, kana kwamba walikuwa wakienda kwa ndoa yao."

Mateso yakazidisha hesabu ya washuhuda kwa ajili ya ukweli. Mwaka kwa mwaka mfalme akashurutisha kazi yakeya ukatili, lakini hakufaulu. William wa Orange mwishowe akaleta uhuru wa kuabudu Mungu katika Holandi.

## Matengenezo Katika Danemark

Katika inchi za kaskazini injili ilipata mwingilio wa amani. Wanafunzi huko Wittenberg waliporudi nyumbani walikuwa wakichukua imani ya matengenezo huko Scandinavia. Maandiko ya Luther pia yakatawanya nuru. Watu hodari wa upande wa kaskazini, wakageuka kutoka maovu na ibada ya sanamu ya Roma na kupokea kwa furaha kweli ya maisha bora ya Biblia.

Tausen, "Mtengenezaji wa Danemark," kama mtoto mwanzoni,
[112] akaonyesha akili ya nguvu na akaingia kwa nyumba ya watawa. Mtihani ulimtambulisha kuwa na talanta iliyoahidi kufanya kazi nzuri kanisani. Mwanafunzi kijana akaruhusiwa kujichagulia mwenyewe chuo kikubwa cha Ujeremani ama cha Uholandi, ila kwa sharti moja tu: hakupashwa kwenda Wittenberg kuhatarishwa na uzushi. Watawa wakasema hivyo.

Tausen akaenda Cologne, mojawapo ya ngome ya Kiroma. Hapo hakukawia kuchukizwa. Ni wakati ule ule aliposoma maandiko ya Luther kwa furaha na akatamani sana kujifunza mafundisho ya kipekee ya Mtengenezaji. Lakini kwa kufanya vile alipashwa kujihatarisha kupoteza usaada wa wakuu wake. Kwa upesi kusudi lake likafanyika na mara akawa mwanafunzi huko Wittenberg.

Kwa kurudi Danemark, hakuonyesha siri yake, lakini akajitahidi kuongoza wenzake kwa imani safi. Akafungua Biblia na akahubiri Kristo kwao kama tumaini pekee la mwenye zambi la wokovu. Hasira ya mkuu wa nyumba ya watawa ilikuwa kubwa sana, walioweka matumaini ya juu juu kwake kuwa mtetezi wa Roma. Akahamishwa mara moja kutoka kwa nyumba yake mwenyewe ya watawa kwenda kwa ingine na kufungiwa kwa chumba chake kidogo. Katika fito za chuma za chumba chake kidogo Tausen akazungumza na wenzake maarifa ya kweli. Kama mababa wema wale wa Danois wangalipatana katika shauri la kanisa juu ya uzushi, sauti ya Tausen haingalisikiwa tena kamwe; lakini badala ya kumzika hai kwa gereza la chini ya udongo, wakafukuzwa kwa nyumba ya watawa.

Amri ya mfalme, ikatangazwa, ikatolea ulinzi kwa elimu ya mafundisho mapya. Makanisa yakafunguliwa kwa ajili yake, na watu wakajaa tele kusikiliza. Agano Jipya katika Kidanois kikaenezwa mahali pengi. Juhudi ya kuangusha kazi ikaishia kwa kuitawanya,

na kwa hiyo Danemark ikatangaza ukubali wake wa imani ya matengenezo.

## Maendeleo katika Uswedi

Katika Uswedi vilevile vijana kutoka Wittenberg wakachukua maji ya uzima kwa watu wa kwao. Waongozi wawili wa Matengenezo katika Swede, Olaf na Laurentius Petri, walijifunza chini ya Luther na Melanchton. Kama mtengenezaji mkuu, Olaf akaamsha watu kwa ufundi wake wa kusema, hivyo Laurentius, sawasawa na Melanchton, alikuwa na uangalifu na utulivu. Wote wawili walikuwa na uhodari imara. Mapadri wakikatoliki wakasukuma watu wajinga na wa ibada ya sanamu kwa nyakati nyingi. Olaf Petri kwa shida akaokoka na maisha yake. Watengenezaji hawa walikuwa,
basi, wakilindwa na mfalme, aliyekusudia juu ya Matengenezo na [113]
akakaribisha hawa wasaidizi hodari katika vita ya kupinga Roma.

Mbele ya mfalme na watu waliojifunza wa Swede, Olaf Petri kwa uwezo mkubwa akatetea imani ya matengenezo. Akatangaza kwamba mafundisho ya mababa yanapaswa kukubaliwa tu kama yakipatana na Maandiko; akatangaza kwamba mafundisho mhimu ya imani yanayofundishwa katika Biblia kwa hali ya wazi ili wote waweza kuyafahamu.

Shindano hili linaonyesha watu wa namna gani wanaokuwa katika jeshi la Watengenezaji. Hawakuwa wajinga, watu wa kujitenga, wenye mabishano wa fujo--mbali ya ile. Walikuwa watu waliojifunza Neno la Mungu na waliojua vizuri kutumia silaha walizozipata kwa gala ya silaha ya Biblia. (Walikuwa) wanafunzi na wanafunzi wa elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini (Theologie), watu wakamilifu waliozoea mambo ya ukweli wa injili, na walioshinda kwa urahisi wenye kutumia maneno ya ovyo ya uongo wa vyuo na wakuu wa Roma."

Mfalme wa Swede akakubali imani ya Waprotestanti, na baraza la taifa likatangaza ukubali wake. Kwa matakwa ya mfalme ndugu hawa wawili wakaanza utafsiri wa Biblia nzima. Ikaagizwa na baraza kwamba po pote katika ufalme, wachungaji walipashwa kueleza Maandiko, na kwamba watoto katika vyuo walipashwa kufundishwa kusoma Biblia.

Walipookoka na magandamizo ya Roma, watu wa taifa la Uswedi wakafikia hali ya nguvu na ukubwa wasiofikia mbele. Baada ya karne moja, taifa hili ndogo na zaifu likawa la kwanza katika Ulaya lililosubutu kutoa mkono wa usaada--kwa ukombozi wa Ujermani mda wa shindano ndefu la Vita ya miaka makumi tatu. Ulaya yote ya Kaskazini ilionekana kuwa tena chini ya ukorofi wa Roma. Majeshi ya Swede ndiyo yaliwezesha Ujeremani kupata uhuru wa dini kwa ajili ya Waprotestanti na kurudisha uhuru wa zamiri kwa inchi zile ambazo zilikubali Matengenezo.

# 14 /UKWELI UNAENDELEA KATIKA UINGEREZA [114]

Wakati Luther alipokuwa akifungua Biblia iliyofungwa kwa watu wa Ujeremamy, Tyndale akasukumwa na Roho wa Mungu kufanya tendo lilelile katika Uingereza. Biblia ya Wycliffe ilitafsiriwa kutoka kwa Kilatini, ambamo mulikuwa makosa mengi. Bei ya kurasa zilizoandikwa ilikuwa juu sana na kwa hiyo mtawanyiko wake ulikuwa wa shida.

Kwa mwaka 1516, kwa mara ya kwanza Agano Jipya likachapwa katika lugha ya asili ya Kigiriki. Makosa mengi ya tafsiri ya kwanza yakasahihishwa, na maana yakarudishwa vizuri zaidi. Nakala zile zikaletea watu waliojifunza ufahamu bora kwa kweli na zikatoa mwendo mpya kwa kazi ya matengenezo. Lakini sehemu kubwa ya watu walikosa Neno la Mungu. Tyndale alipaswa kutimiza kazi ya Wycliffe katika kutoa Biblia kwa watu wa inchi yake.

Akahubiri bila woga mambo ya hakika yake. Kwa tangazo la Papa kwamba ni kanisa lililotoa Biblia, na ni kanisa pekee linaloweza kuieleza, Tyndale akajibu: "Kamwe haukutupatia Maandiko, ni wewe uliyeyaficha kwetu; ni wewe uliyewachoma wale walioyafundisha, na kama ungaliweza, ungalichoma Maandiko yenyewe."

Mahubiri ya Tyndale yakaamsha usikizi kubwa. Lakini mapadri wakajitahidi kuharibu kazi yake. "Ni kitu gani kinapaswa kufanywa?" akapaza sauti. "Siwezi kuwa po pote. Ee! kama Wakristo wangalikuwa na Maandiko matakatifu katika lugha yao wenyewe, wangaliweza wao wenyewe kushindana na wenye kutumia maneno madanganyifu hawa. Bila Biblia haiwezekani kuimarisha watu katika kweli."

Nia mpya ikaja katika mawazo yake. "Injili haitasema lugha ya Ungereza miongoni mwetu? ... Kanisa linapaswa kuwa na nuru ndogo kwa wakati wa azuhuri kuliko wakati wa mapambazuko yake? ... Wakristo wanapashwa kusoma Agano Jipya katika lugha yao ya kuzaliwa." Ila tu kwa njia ya Biblia watu waliweza kufikia ukweli.

Mtaalamu mmoja wa Katoliki katika mabishano pamoja naye akapaza sauti ya mshangao, "Ingekuwa vema kutokuwa na sheria za Mungu kuliko kukosa zile za Papa." Tyndale akajibu, "Ninazarau Papa na sheria zake zote; na kama Mungu angenipatia maisha, kabla ya miaka mingi nitawezesha kijana anayeongoza jembe la kukokotwa na ngombe kufahamu Maandiko zaidi kuliko ninyi."

## [115] Tyndale Anatafsiri Agano Jipya kwa Kiingereza

Alipofukuzwa nyumbani kwa ajili ya mateso, akaenda Londoni na huko kwa mda akatumika bila kizuizi. Lakini tena Wakatoliki wakamlazimisha kukimbia. Uingereza wote ukaonekana wenye kufungwa kwake. Katika Ujeremani akaanza uchapaji wa Agano Jipya kwa lugha ya kingereza. Alipokatazwa kuchapa katika mji moja, akaenda kwa mji mwengine. Mwishowe akasafiri kwenda Worms, ambako, miaka michache mbele, Luther alipotetea injili mbele ya baraza. Katika mji ule kulikuwa rafiki wengi wa Matengenezo. Vitabu elfu tatu vya Agano Jipya vikachapwa, na mchapo mwengine ukafuata.

Neno la Mungu likapenya kwa siri kule Londoni na kuenezwa po pote katika inchi. Wakatoliki wakajaribu kukomesha ukweli, lakini haikuwezekana. Askofu wa Durham akanunua kwa muuzavitabu akiba yote ya Mabiblia kwa kusudi la kuviharibu, kufikiri kwamba jambo hili lingesimamisha kazi. Lakini mali ikatoa vyombo vilivyonunuliwa kwa ajili ya mchapo mpya na bora kuliko. Wakati Tyndale alipofungwa baadaye, uhuru ukatolewa kwake isipokuwa ataje majina ya wale waliomsaidia kwa zawadi zao kwa mchapo wa Mabiblia. Akajibu kwamba askofu wa Durham alifanya zaidi kuliko kila mtu ye yote kwa kulipa bei kubwa kwa ajili ya vitabu vilivyobaki mkononi.

Mwishowe Tyndale akashuhudia imani yake kwa mauti ya mfia dini; lakini silaha alizozitayarisha ziliwezesha waaskari wengine kupigana katika karne nyingi, hata kwa wakati wetu.

Latimer akasema juu ya mimbara kwamba inafaa kusoma Biblia katika lugha ya watu. "Tusichague njia zinazopingana, bali Neno la Mungu lituongoze: tusifuate ... mababu zetu, wala kufuata yale waliyotenda, bali yale waliyopaswa kufanya."

Barnes na Frith, Ridley na Cranmer, waongozi katika Matengenezo ya Uingereza walikuwa wataalamu, wakaheshimiwa sana kwa bidii ao kwa utawa katika ushirika wa Kiroma. Upinzani wao kwa kanisa la Roma ulikuwa ni matokeo ya maarifa yao ya kuvumbua makosa ya "kiti kitakatifu".

## Uwezo Kamili wa Maandiko

Kanuni kubwa iliyoshikwa na Watengenezaji hawa--ni ile ile iliyoshikwa na Wavaudois, Wycliffe, Huss, Luther, Zwingli, na wafuasi wao--ni uwezo kamilifu wa Maandiko matakatifu. Kwa mafundisho yake wakajaribu mafundisho ya dini yote na madai yote. Ni imani katika Neno la Mungu iliyosaidia watu hawa watakatifu [116] walipotoa maisha yao kwa kigingi. "Muwe wakufarijika," akasema Latimer kwa wenzake wafia dini wakati sauti zao zilikuwa karibu kunyamazishwa na ndimi za moto, "tutawasha leo mshumaa, kwa neema ya Mungu, katika Uingereza, jinsi ninavyo tumaini hautazimika."

Kwa mamia ya miaka baada ya makanisa ya Uingereza yalipotii mamlaka ya Roma, wale wa Scotland (Ecosse) wakashika uhuru wao. Kwa karne ya kumi na mbili, hata hivyo, dini ya papa ikaimarishwa katika inchi, na sehemu zote zikafunikwa na giza nzito. Lakini miali ya nuru ikaja kuangazia giza hiyo. Wa Lollards, kutoka Uingereza pamoja na Biblia na mafundisho ya Wycliffe, wakafanya mengi kwa kulinda maarifa ya injili. Kwa kufunguliwa kwa Matengenezo kukaja maandiko ya Luther na Agano Jipya la Kingereza la Tyndale. Wajumbe hawa kwa ukimya wakapitia milimani na katika mabonde, wakawasha katika maisha mapya mienge ya kweli iliyokuwa karibu kuzimika na kufanya upya tena kazi ambayo iligandamizwa na karne inne za mateso.

Ndipo waongozi wa kanisa la Papa, mara wakaamshwa kwa hatari iliyohofisha kazi yao, wakapandisha watoto wengi wa watu bora wa Scotland (Ecosse) kwa kigingi. Washahidi hawa waliokufa po pote katika inchi wakafurahisha roho za watu na kusudi isiyokufa ya kuvunja minyororo za Roma.

## Yohana Knox

Hamilton na Wishart, pamoja na mstari mrefu wa wanafunzi wapole, wakatoa maisha yao kwa kigingi. Lakini kutoka kwenye tuta la kuni moto wa Wishart kukatokea mtu ambaye ndimi za moto hazikumunyamazisha, mtu ambaye, chini ya uongozi wa Mungu ilipashwa kupinga onyo la mauti kwa kanisa la Papa katika inchi ya Scotland.

John Knox akatupia mbali maagizo ya asili ya kanisa na akajilisha kwa ukweli wa Neno la Mungu. Mafundisho ya Wishart yakathibitisha kusudi lake la kuachana na Roma na kujiunga mwenyewe na Watengenezaji walioteswa.

Aliposhurutishwa na wenzake kufanya kazi ya kuhubiri, akarudi anapotetemeka mbele ya madaraka kama hayo. Ilikuwa tu baada ya siku za vita kali pamoja naye ndipo akakubali. Lakini alipokubali, akaendelea mbele na uhodari wa kutisha. Ujasiri huu wa mtengenezaji haukuogopa mtu. Alipoletwa uso kwa uso na malkia wa Scotland, Yohana Knox hakukubali kushindwa kwa sababu ya
[117] kubembelezwa; hakutetemeka juu ya vitisho. Kwamba Malkia akatangaza kwamba alifundisha watu kukubali dini iliyokatazwa na serekali, na kwa hivyo alivunja pia amri ya Mungu inayolazimisha watu kutii watawala wao. Knox akajibu kwa ujasiri: "Kama watoto wa Izraeli wote walikubali dini ya Farao ambao walikuwa watu wake, nakuuliza, Bibilia, ni dini ya namna gani ingaliweza kuwa katika dunia? Ao kama watu wote katika siku za mitume, wangalikuwa wa dini ya wafalme wa Roma, ni dini ya namna gani ingalikuwa mbele ya uso wa dunia?"

Akasema Marie: "Mnatafsiri Maandiko kwa namna ingine, na (Wakatoliki wa Roma) wanatafsiri kwa namna ingine; nitamwamini nani, na ni nani atakuwa mwamzi?"

"Utamwamini Mungu, ile inasemwa wazi katika Neno lake," akajibu Mtengenezaji. ... Neno la Mungu linakuwa wazi ndani yake lenyewe; na kama kukionekana giza lolote katika mahali fulani, Roho Mtakatifu, asiyekuwa na mabishano kati yake mwenyewe, hueleza namna moja wazi zaidi mahali pengine."

Kwa moyo usio na hofu Mtengenezaji shujaa, kwa ajili ya maisha yake, akaendelea na kusudi lake, hata Scotland ikapata uhuru kutoka kwa kanisa la Papa.

Kuimarishwa kwa dini ya Kiprotestanti kama dini ya taifa katika Uingereza kulituliza mateso lakini bila kuikomesha kabisa. Mengi katika maagizo ya Roma yaliendelea. Mamlaka ya Papa ilikataliwa, lakini mahali tu ambapo mfalme alipewa kiti kama kichwa cha kanisa. Katika ibada watu walikuwa wakingali mbali na utakatifu wa injili. Uhuru wa dini ulikuwa haujafahamika. Ijapo matatizo ya kutisha ambayo Roma ilitumia ilipata kimbilio lakini kwa shida na wakuu wa Kiprotestanti, kwani haki ya kila mtu kuabudu Mungu kufuata zamiri yake mwenyewe haikukubaliwa. Wakaidi walipata mateso kwa mamia ya miaka.

### Maelfu ya Wachungaji (Pasteurs) Walifukuzwa

Katika karne ya kumi na saba maelfu ya wachungaji walifukuzwa na watu wakakatazwa kuhuzuria mikutano yo yote ya dini isiyokuwa ile iliyoruhusiwa na kanisa. Ndani ya kimbilio la vilindi mwituni, wale watoto wa Bwana walioteswa walikusanyika kwa kumimina roho zao katika maombi (sala) na kusifu. Wengi waliteseka kwa ajili ya imani yao. Gereza zilijaa, jamaa zikatengana. Lakini mateso hayakunyamazisha ushuhuda wao. Wengi walilazimishwa kuvuka bahari kwenda Amerika na hapo ndipo paliwekwa msingi wa utaalamu na uhuru wa dini. [118]

Ndani ya gereza kulijaa na watu waliofanya makosa makubwa, John Bunyan, akapumua hewa ya mbinguni na akaandika mizali yake ya ajabu ya safari ya msafiri kutoka kwa inchi ya uharibifu kwenda kwa mji wa mbinguni. *Pilgrim's Progress* [Maendeleo ya Msafiri] na *Grace Abounding to the Chief of Sinners* [Neema nyingi kwa mkuu wa wenye zambi] vimeongoza nyayo nyingi kwa njia ya uzima.

Katika siku ya giza ya kiroho Whitefield na Wesleys wakatokelea kama wachukuzi wa nuru kwa ajili ya Mungu. Chini kanisa lililoanzishwa watu wakarudia zambini ambayo ni vigumu kutofautisha kwa ushenzi. Watu wa vyeo vya juu wakacheka uchaji wa Mungu; watu wa vyeo vya chini wakazamishwa kwa maovu. Kanisa halikuwa na uhodari ao imani kwa kusaidia maanguko ya neno la kweli.

### Kuhesabiwa Haki kwa Imani

Mafundisho makubwa ya kuhesabiwa haki kwa imani, yaliyofundishwa wazi wazi na Luther, yalikuwa karibu kusahauliwa kabisa; kanuni ya kanisa la Roma ya kutumaini matendo mema kwa ajili ya wokovu yakakamata nafasi yake. Whitefield na Wesleys wawili walikuwa watafuti wa kweli kwa ajili ya wema wa Mungu. Hii walifundishwa kuwekwa salama kwa njia ya wema na kushika maagizo ya dini.

Wakati Charles Wesley kwa wakati moja alipopata ugonjwa na akatumaini kwamba kifo kilikuwa karibu, akaulizwa, msingi wa tumaini lake la uzima wa milele ulikuwa juu ya kitiu gani. Jibu lake: "Nimetumia juhudi yangu bora kumtumikia Mungu." Rafiki ilionekana hakutoshelewa kabisa kwa jibu hili. Wesley akafikiri: "Nini! ... Anatamani kuninyanganya juhudi yangu? Sina kitu kingine cha kutumainia." Hiyo ndiyo ilikuwa giza ambayo iliyoimara kwa kanisa, kugeuza watu kutoka kwa tumaini lao pekee la wokovu--damu ya Mkombozi aliyesulubiwa.

Wesley na washiriki wake wakaongozwa kufahamu kwamba sheria ya Mungu inafikishwa mawazoni pia kwa maneno na matendo. Kwa juhudi za kazi na maombi wakafanya bidii ya kushinda maovu ya moyo wa asili. Wakaishi maisha ya kujinyima na kujishusha, wakachunguza kwa uaminifu kila mpango waliochukua ambao ungeweza kuwa wa kusaidia kwa kupata utakatifu ule ambao uliweza kutunza wema wa Mungu. Lakini juhudi zao wenyewe
[119] hazikuweza kuwapa uhuru kutoka kwa hukumu ya zambi ao kuvunja uwezo wake.

Mioto ya ukweli wa Mungu, ambayo ilikuwa karibu kuzimika juu ya mazabahu ya dini ya Kiprotestanti, ilipashwa kuwashwa kutoka kwa mwenge wa zamani uliotolewa na Wakristo wa Bohemia. Wengine miongoni mwao, wakapata kimbilio katika Saxe (Saxony), wakalinda imani ya zamani. Kutoka kwa Wakristo hawa nuru ikaja kwa Wesley.

Yohana na Charles wakatumwa kwa ujumbe kuenda Amerika. Katika meli kulikuwa na kundi la waMoravians. Wakakutana na zoruba kali sana, na Yohana, akawa uso kwa uso na kifo, akajisikia kwamba hakuwa na hakikisho la amani na Mungu. Lakini Wajeremani wakaonyesha utulivu na kutumaini kwamba alikuwa

mgeni. “Tangu zamani,” akasema, “nilichunguza umuhimu mkuu wa mwenendo (tabia) wao. ... Wakawa sasa na bahati ya kujaribu kwamba walikuwa huru bila mafikara ya woga pia na ile ya kutokuwa na kiburi, hasira na kulipisha kisasi. Katikati ya zaburi kwa kazi yao ilianza, bahari ikapasuka, na kupasua tanga kubwa kwa vipande vipande, ikafunika merikebu, na kumwanga kati kati ya sakafu kana kwamba kilindi kikuu kimekwisha kutumeza. Kilio cha nguvu kikaanza miongoni mwa Waingereza. Wajeremani kwa utulivu wakaendelea kuimba. Nikauliza mmojawapo wao baadaye,‘Hamkuwa na hofu? ‘ Akajibu Namshukuru Mungu, hapana.’ Nikauliza, ‘Lakini wake wenu na watoto hawakuwa na hofu?’ Akajibu kwa upole, ‘Sivyo; wake wetu na watoto hawaogopi kufa.’”

### Moyo wa Wesley “Kwa Jinsi Isiyo ya Kawaida Watiwa Joto”

Kwa kurudi kwake Uingereza, Wesley akafikia kwa kufahamu wazi wazi imani ya Biblia chini ya mafundisho ya mtu wa Moravia. Kwa mkutano wa chama cha Wamoravian katika Londoni maneno yakasomwa kutoka kwa Luther. Namna Wesley alipokuwa akisikiliza, imani ikawashwa ndani ya roho yake. “Nilisikia moyo wangu kutiwa joto ngeni,” akasema. “Nilisikia kwamba nilimtumaini Kristo, Kristo pekee, kwa ajili ya wokovu: na tumaini likatolewa kwangu, kwamba aliondoa mbali zambi zangu, hata zangu, na aliniokoa kutoka kwa sheria ya zambi na mauti.’ ‘

Sasa aliona kwamba neema aliyojitahidi kupata kwa njia ya maombi na kufunga na kujinyima ilikuwa zawadi, “bila mali na bila bei.” Roho yake yote ikawaka na mapenzi ya kutangaza po pote injili utukufu ya neema huru ya Mungu. “Nikatazama juu ya ulimwengu wote kama mtaa wangu,” akasema; “po pote ninapokuwa, ninazania [120]
kwamba, nina haki, na wajibu wangu wa lazima, kutangaza kwa wote wale wanaotamani kusikia, habari za furaha za wokovu.”

Akaendelea na maisha yake halisi na ya kujinyima, si sasa kama *msingi,* bali *matokeo* ya imani; si *shina*, bali *tunda* la utakatifu. Neema ya Mungu katika Kristo itaonekana katika utii. Maisha ya Wesley ilitolewa kuwa wakfu kwa kuhubiri kweli kubwa aliyoyakubali--kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika damu ya kafara ya Kristo, na uwezo mpya wa Roho Mtakatifu kwa moyo, kuendelea kuleta matunda katika maisha yanayofanana kwa mfano wa Kristo.

Whitefield na Wesleys wawili waliitwa kwa wakati ule "Methodistes" na wanafunzi wenzao wabaya -jina ambalo kwa wakati huu linazaniwa kuwa la heshima. Roho Mtakatifu aliwalazimisha kuhubiri Kristo na Yeye aliyesulubiwa. Maelfu waliogeuka kwa kweli. Ilikuwa ni lazima kwamba kondoo hizi zilindwe kutoka mbwa mwitu wenye wazimu. Wesley hakuwa na wazo la kuanzisha dini lingine, lakini aliwatengeneza chini ya kile kilichoitwa mwunganisho wa Methodiste.

Ulikuwa ushindani wa siri na taabu ya uinzani ambayo wahubiri hawa walipambana nayo kwa kuanzisha kanisa--kwani kweli ilikuwa na mwingilio mahali milango labda ingedumu kuendelea yenye kufungwa. Wakuu wengine wa dini wakaamka kwa mshangao wa tabia yao na wakawa wahubiri wa juhudi katika mitaa yao wenyewe.

Kwa wakati wa Wesley, watu wa vipawa mbalimbali hawakulinganisha kila sehemu ya mafundisho ya dini. Tofauti kati ya Whitefield na Wesleys wawili ilitisha wakati moja kuleta fitina, lakini kwa namna walijifunza upole katika chuo cha Kristo, uvumilivu na upendo vikawapatanisha. Hawakuwa na wakati wa kubishana, wakati ambao makosa na maovu yalijaa pote.

## Wesley Anaepuka Kifo

Watu wa mvuto wakatumia uwezo wao kinyume chao. Wakuu wengi wa kanisa wakaonyesha uchuki, na milango ya makanisa ikafungwa juu ya imani safi. Padri, akiwalaumu juu ya mimbara, akachochea watu wajinga wa giza na waovu. Mara na mara Wesley akaepuka kifo kwa muujiza wa uhuruma ya Mungu. Wakati ilionekana kwamba hakuna njia ya kuepuka, malaika katika umbo
[121] la kibinadamu alikuja upande wake na kundi lilianguka na mtumishi wa Kristo akapita katika usalama kutoka hatarini.

Kwa ajili ya ulinzi wake, mojawapo wa matukio hayo, Wesley akasema: "Ingawa wengi walijaribu kukamata ukosi wa shingo yangu ao mavazi, kuniangusha, hawakuweza kufunga kamwe: ila mmoja tu alishika upindo wa kisibau changu ambacho kikabaki mara mkononi mwake; na upindo mwengine, ndani ya mfuko ambao ulikuwamo noti ya benki, ilipasuka lakini nusu yake. ... Mtu wa nguvu nyuma yangu akanipiga mara nyingi, na fimbo kubwa ya mti wa Ulaya (che ne); ambayo kama angalinipaga mara moja tu kwa

upande wa nyuma wa kichwa changu, ingalikuwa ni mwisho wangu. Lakini kila mara, pigo likapotoka, sijui namna gani; kwani sikuweza kwenda kuume wala kushoto."

Wamethodiste wa siku ile walivumilia kicheko na mateso, mara nyingi mauaji. Kwa nyakati zingine, matangazo kwa watu wote libandikwa, kuita wale waliotaka kuvunja madirisha na kunyanganya katika nyumba za Wamethodiste ili wakusanyike kwa wakati ulitolewa na mahali. Mateso ya desturi yakafanyika juu ya watu ambao kosa moja tu lilikuwa ni kutafuta kugeuza wenye zambi kutoka kwa njia ya uharibifu na kuwaingizisha kwa njia ya utakatifu!

Uharibifu wa kiroho katika Uingereza kabla ya wakati wa Wesley ulikuwa katika hali kubwa matokeo ya mafundisho kwamba Kristo alifuta kanuni ya mema na mabaya na kwamba Wakristo hawakuwa na lazima ya kuishika. Wengine wakasema kwamba ilikuwa si lazima kwa wachungaji kuonya watu kutii amri zake, kwani wale ambao Mungu aliowachagua kwa wokovu "wataongozwa kufuata utawa na wema" wakati wale waliohukumiwa laana ya milele "hawakuwa na uwezo kwa kutii sheria ya Mungu."

Wengine wakishikilia kwamba "wateule hawawezi kukosa neema ya Mungu wala, kunyanganywa kibali cha Mungu," walipofikia mwisho kwamba "matendo mabaya wanayotenda si maovu, ... na kwamba, baadaye, hawana na nafasi wala kuungama zambi zao ao kuyaacha kwa njia ya toba." Kwa hiyo, wakatangaza, hata zambi moja katika zambi mbaya kuliko" zilizozaniwa kwa wote kuwa mvunjo mkubwa zaidi wa amri za Mungu kama si zambi mbele za Mungu "kama ikitendwa na mmojawapo wa wateule." Hawawezi kufanya kitu cho chote kisicho mpendeza Mungu ao kilichokatazwa na sheria."

Mafundisho haya mabaya yanakuwa sawa sawa na mafundisho ya mwisho kwamba hakuna sheria ya Mungu inayogeuka kama kipimo cha haki, lakini tabia hiyo ilionyeshwa na chama chenyewe na mara kwa mara ilipaswa kubadirishwa. Mawazo haya yote yalitoka kwake ambaye miongoni mwa wakaaji wasio na kosa wa mbinguni [122]
alianza kazi yake kwa kuvunja amri za haki za sheria ya Mungu.

Mafundisho haya mabaya juuya amri za Mungu, zisizogeuka kwa kuimarisha tabia ya watu iliongoza wengi kukataa sheria ya Mungu. Wesley kwa uhodari akapinga mafundisho haya ambayo yaliongoza watu kupinga amri ya Mungu, mafundisho juu ya hali

ya kila mtu (Predestination). "Neema ya Mungu inayoleta wokovu imeonekana kwa *watu wote*." "Mungu Mwokozi wetu anayetaka *watu wote* waokolewa na kupata ujuzi wa kweli. Kwani kuna Mungu mmoja, na mupatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja, yule mtu ni Kristo Yesu, aliyejitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya *wote*. " Kristo "Nuru ya kweli inaangazia nuru *kila mtu* anayekuja katika ulimwengu.' ' Tito 2:11; 1 Timoteo 2:3-6; Yoane 1:9. Watu wanaoshindwa kupata wokovu ni wale wanaokataa kwa mapenzi yao zawadi ya uzima.

## Katika Utetezi wa Sheria ya Mungu

Katika kujibu madai kwamba wakati wa kifo cha Kristo, amri kumi ziliondolewa pamoja na sheria za kawaida, Wesley akasema: "Sheria ya tabia, inayokuwa katika Amri Kumi na ikatiliwa nguvu na manabii, hakuitosha. Hii ni sheria ambayo haiwezi kamwe kuvunjwa, ambayo 'inasimama imara kama shuhuda mwaminifu mbinguni.'"

Wesley akatangaza umoja kamilifu wa sheria na injili. "Kwa upande moja sheria kwa kuendelea kutuongoza kwa injili, kwa ngambo ingine injili huendelea kutuwezesha kutimiza utimilifu inafanya njia kuwa na sheria, kwa mfano, inatuamuru kumpenda Mungu, kupenda jirani wetu, kuwa wapole, wanyekevu ao watakatifu. Tukijisikia kwamba hatutoshi kwa mambo haya; ... lakini tunaona ahadi ya Mungu kutupatia upendo huo, na kutufanya wanyenyekevu, wapole, na watakatifu: tunashika injili hii, ya habari ya furaha: ... ' haki ya sheria hutimilika ndani yetu; kwa njia ya imani inayokuwa katika Yesu Kristo. ...

"Katika daraja la juu sana za maadui wa injili ya Kristo," akasema Wesley, "ni wale ... wanaofundisha watu kuvunja ... si moja tu, wala ndogo ao kubwa sana, bali amri zote kwa jumla. ... Wanamheshimu kama Yuda alivyofanya aliposema, 'salamu, Rabi; akamubusu' ... Hakuna namna ingine isipokuwa kumusaliti kwa kumubusu, kuzungumza juu ya damu yake, na kunyanganya taji lake; kuweka nuru kwa kila sehemu ya sheria yake, chini ya ujanja wa kuendesha injili yake."

## Umoja wa Sheria na Injili [123]

Kwa wale wanaoshurtisha kwamba “hotuba ya injili hujibu vikomo vyote vya sheria,” Wesley akajibu: “Wajibu wa kwanza kabisa wa sheria, yaani, kusadikisha watu juu ya zambi, kuamsha wale wangali katika usingizi kwa ukingo wa Gehena ya moto. ... Ni uwongo, basi kutoa mganga kwa wenye afya, ao wanaojizania wao wenyewe kuwa na afya. Inafaa kwanza kuwasadikisha kwamba wako wagonjwa, kama sivyo hawatakushukuru kwa kazi yako. Inakuwa vilevile uwongo kunena habari ya Kristo kwa wale ambao roho yao haijavunjika.”

Na katika kuhubiri injili ya neema ya Mungu, Wesley kama Bwana wake, alitafuta “kutukuza sheria, na kuifanyiza kuwa na heshima.” Isaya 42:21. Matokeo yalikuwa ya utukufu aliyoruhusiwa kuona. Kwa mwisho wa juu nusu ya karne aliyotumia katika kazi, wafuasi wake wakahesabika zaidi kuliko nusu ya milioni. Lakini wengi wa roho zilizoinuliwa kutoka kwa upotovu wa zambi kwa maisha ya juu na safi hauwezi kamwe kujulikana hata jamaa lote la waliokombolewa wanapokusanyika katika ufalme wa Mungu. Maisha yake inaonyesha fundisho la thamani isiyohesabika kwa kila Mkristo.

Ilipendeza Mungu kwamba imani na unyenyekevu, juhudi isiyolegea, kujinyima na uchaji wa kweli wa mtumishi huyu wa Mungu yapate kurudisha nuru katika makanisa ya leo!

[124] # 15 /UTAWALA WA KUTISHA WA UFARANSA

### Sababu yake ya Kweli

Mataifa mengine yalikaribisha Matengenezo kuwa ujumbe wa mbinguni. Katika inchi zingine nuru ya maarifa ya Biblia ilikuwa karibu kufungwa kabisa. Katika inchi ingine kweli na uongo vikashindaniya uwezo kwa karne nyingi. Mwishowe ukweli wa mbinguni ukasongwa. Kiasi cha Roho ya Mungu kikaondolewa kwa watu wale waliozarau zawadi ya neema yake. Na ulimwengu wote ukaona matunda ya kukataa nuru kwa makusudi.

Vita ya kupinga Biblia katika Ufransa ikatimilika wakati wa mapinduzi, ambayo ni matokeo halali kwa Roma kutosoma Maandiko. (Tazama Nyongezo.) Ni onyesho la ajabu sana lililoshuhudia mwisho wa mafundisho ya kanisa la Roma.

Ufunuo ulitangaza matokeo ya kutisha yaliyopaswa kuongezeka zaidi kwa Ufransa kutoka kwa utawala wa "mtu wa zambi":

"Na kiwanja kilicho inje ya hekalu la Mungu, uache inje, wala usipime kwa maana imetolewa kwa mataifa, nao watakanyaga mji mutakatifu miezi makumi ine na miwili. Nami nitawapa washuhuda wangu wawili nguvu, nao watatoa unabii siku elfu moja mia mbili makumi sita, wamevikwa mavazi ya gunia. ... Hata watakapomaliza ushuhuda wao, yule nyama anayetoka katika shimo pasipo mwisho atafanya vita nao; naye atawashinda na kuwaua. Na maiti yao yatalala katika njia ya mji ule mkubwa, unaoitwa kwa kiroho Sodomo na Misri, ambapo tena Bwana wetu aliposulubiwa. ... Na wale wanaokaa juu ya dunia watafurahi juu yao na kuchekelea, watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa sababu manabii hawa wawili waliwatesa wao wanaokaa juu ya dunia. Na kiisha siku tatu na nusu, Roho ya uhai inayotoka kwa Mungu ikaingia ndani yao, wakasimama kwa miguu yao; na woga mkubwa ukawaangukia watu wote waliowaona." Ufunuo 11:2-11.

"Miezi makumi ine na miwili" na siku elfu moja mia mbili na makumi sita" ni sawa sawa, wakati ambao kanisa la Kristo lilipaswa

kuteswa na magandamizo ya Roma. Miaka 1260 ilianza katika mwaka 538 A.D. na ikamalizika kwa mwaka 1798 AD. (Tazama Nyongezo.) Kwa wakati ule majeshi ya Ufaransa likamfanya Papa kuwa mfungwa, na akafa mbali na kwao. Mamlaka ya Papa ikakosa uwezo wa kuimarisha utawala wake wa zamani.

Mateso hayakudumu hata mwisho katika miaka 1260 yote. [125]
Katika huruma zake kwa watu wake, Mungu akafupisha mda wa taabu yao kali kwa mvuto wa Matengenezo.

"Washahidi wawili" ni mfano wa Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya, washuhuda wakuu kwa mwanzo na umilele wa sheria za Mungu, na pia kwa mpango wa wokovu.

"Nao watatoa unabii siku elfu moja mia mbili makumi sita, wamevikwa mavazi ya gunia." Wakati Biblia ilipokatazwa, ushuhuda wake ukageuzwa vibaya; wakati wale walipojaribu kutangaza ukweli wake wakasalitiwa, kuteswa, kuuawa kama wafia dini kwa ajili ya imani yao ao kulazimishwa kukimbia--ndipo "washuhuda" waaminifu wakatabiri "katika mavazi ya gunia." Katika nyakati za giza kabisa watu waaminifu wakapewa hekima na mamlaka kwa kutangaza kweli wa Mungu. (Tazama Nyongezo.)

"Na kama mtu yeyote akitaka kuwaumiza, moto utatoka katika vinywa vyao na kumeza adui zao. Na kama mtu yeyote akitaka kuwaumiza, anapashwa kuuawa namna hii." Ufunuo 11:5. Watu hawawezi bila kuwa na hofu ya kupata malipizi kwa kuzarau Neno la Mungu!

"Hata watakapomaliza ushuhuda wao." Wakati washuhuda hawa wawili walipokaribia mwisho wa kazi yao katika giza, vita ilipaswa kufanywa juu yao na "yule nyama anayetoka katika shimo pasipo mwisho." Hapa kunaonekana onyesho mpya la uwezo wa Shetani.

Ilikuwa busara ya Roma, kushuhudia heshima kwa ajili ya Biblia, kwa kuifungisha kwa lugha isiyojulikana, ikafichwa kwa watu. Chini ya amri yake washahidi wakatabiri "katika mavazi ya gunia. " Lakini " yule nyama anayetoka katika shimo pasipo mwisho" alipashwa kufunguliwa na kufanya vita wazi wazi kwa Neno la Mungu.

"Mji mkubwa" katika njia zake ambazo washahidi hawa wawili waliuawa, na mahali maiti yao ililala ni "kwa kiroho" ni Misri. Kwa mataifa yote katika historia ya Biblia, Misri ndiyo iliyozidi kukana kuwako kwa Mungu na ikapinga amri zake. Hakuna mfalme aliyeasi kwa ujasiri sana juu ya mamlaka ya mbingu kama mfalme wa Misri

alivyofanya, Farao: "Simjui Bwana, na vilevile sitaruhusu Israeli kwenda." Kutoka 5:2. Hii ni kusema hakuna Mungu (atheisme), na taifa linalowakilisha Misri lingetaja mfano wa namna moja wa Mungu na kuonyesha roho ya namna moja ya uasi.

"Mji mkubwa" unafananishwa vile vile, "kwa kiroho," na Sodomo. Maovu ya Sodomo yalionekana zaidi katika uasherati. Zambi hizi zilipaswa kuwa vile vile tabia ya taifa lililopasa kutimiza
[126] andiko hili.

Kwa kupatana na nabii, ndipo, mbele kidogo ya mwaka 1798 uwezo moja wa tabia ya uovu ukainuka kwa kufanya vita na Biblia. Na katika inchi ambapo "washuhuda wawili wa Mungu walipashwa kunyamazishwa, hapo pangekuwa onyesho la kutokujali kuwako kwa Mungu kwa Farao na usherati wa Sodomo.

### Utimilizo wa Ajabu wa Unabii

Unabii huu ulipata utimilizo wa ajabu katika historia ya Ufransa wakati wa Mapinduzi (Revolution), katika mwaka 1793. "Ufransa ulikuwa ni taifa pekee katika historia ya dunia, ambayo kwa amri ya baraza la sheria, likatangaza kwamba hakuna Mungu, na ambaye wenyeji wote wa mji mkuu, na sehemu kubwa ya watu popote, wanawake na wanaume pia, wakacheza na kuimba kwa furaha kwa kukubali tangazo hili."

Ufransa ukaonyesha pia tabia ambazo zilipambanua Sodomo. Mwandishi wa historia anaonyesha pamoja kukana Mungu na uasherati wa Ufransa: "Kwa uhusiano na sheria hizi juu ya dini, ilikuwa ile ambayo ilivunja muungano wa ndoa--maagano takatifu kuliko ambayo watu wanaweza kufanya, na kudumu ni wa lazima kwa ulinzi wa jamaa--ukageuzwa kuwa kwa hali ya mapatano ya adabu ya hivi hivi tu ya mda, na kwamba watu wawili wanaweza kuunga na kuvunja kwa mapenzi. ... Sophie Arnoult, mtendaji wa kike wa sifa kwa mambo ya kuchekesha akasema, akaeleza kuwa ndoa ya serkali ni kama 'sakramenti ao siri ya uzinzi.'"

### Uadui Juu ya Kristo

"Mahali pia Bwana wetu alisulibiwa." Jambo hili vile vile lilitimilika kwa Ufransa. Hakuna inchi ambayo ukweli ulikutana na

upinzani wa ukaidi kama Ufransa. Katika mateso iliyozuriwa kwa washahidi wa injili, Ufransa ulisulibisha Kristo katika mwili wa wanafunzi wake.

Karne kwa karne damu ya watakatifu ilikuwa ikimwangika. Huku Wawaldense (Vaudois) walitoa maisha yao kwa milima ya Piedmont (kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo," ushuhuda wa namna ile ile uliochukuliwa na Albigeois wa Ufransa. Wanafunzi wa Matengenezo waliouawa kwa mateso ya ajabu. Mfalme na wakuu, wanawake wa kizazi cha juu na wabinti wazuri walishibisha macho kwa maumivu makuu ya wafia dini wa Yesu. Wahuguenots washujaa walimwaga damu yao pahali pa mapigano makali, kuwindwa kama [127] wanyama wa mwitu.

Wazao wachache wa Wakristo wa zamani waliobaki kwa karne ya kumi na nane wakajificha katika milima ya Kusini, wakalinda imani ya mababa zao. Wakatembea kwa shida kwa maisha marefu ya utumwa ndani ya mashua ya vita (galères). Watu wa malezi safi sana na wenye akili wa Ufransa waliishi katika minyororo, katika mateso mabaya sana, kati ya wanyanganyi na wauaji. Wengine wakapigwa risasi na kuanguka katika damu ya baridi wanapoanguka kwa magoti yao katika sala. Inchi yao, ikateketezwa kwa upanga, shoka, na kwa moto, "ikageuka kuwa jangwa kubwa, la giza." "Mambo haya mabaya sana yakaendelea ... katika nyakati zisizokuwa za giza bali katika wakati wa nuru wa Louis XIV. Elimu iliongezeka, vitabu ao maarifa yakaendelea vizuri, walimu wa elimu ya tabia na sifa za Mungu wa baraza ya hukumu na wa mji mkuu walikuwa wenye maarifa (savants) na wasemaji, wakavutwa na neema ya upole na upendo."

## Uovu Mbaya Sana Kupita Mengine

Lakini uovu mbaya zaidi miongoni mwa matendo maovu ya karne za kutisha ilikuwa machinjo ao mauaji matakatiifu ya Saint-Bartheiemy. Chini ya mkazo wa mapadri na maaskofu, mfalme wa Ufransa akatoa ukubali wake. Kengele kulia katika ukimya wa usiku, ikatoa ishara ya mauaji. Maelfu ya Waprotestanti, walipokuwa wakilala nyumbani mwao, wakitumaini neno la heshima la mfalme wao, wakakokotwa na kuuawa.

Machinjo yakaendelea kwa siku saba katika Paris. Kwa agizo la mfalme mauaji yakaenea kwa miji yote mahali Waprotestanti walikuwako. Wakuu na wakulima, wazee na vijana, wamama na watoto, wakachinjwa pamoja. Katika Ufransa po pote kulikuwa nafsi 70.000 za ua la taifa wakauawa.

"Wakati habari ya mauaji ilipofika Roma, furaha ya mapadri haikujua mpaka. Askofu wa Lorraine akatolea mjumbe zawadi ya mataji elfu; mzinga wa Saint-Ange mtakatifu akapiga ngurumo ya salamu za furaha; na kengele zikalia kwa minara ya makanisa yote; mioto ya furaha ikageuza usiku kuwa mchana; na Papa Gregoire XIII, pamoja na maaskofu na wakuu wengine wa kanisa, wakaenda kwa mwandamano mrefu kwa kanisa la Saint-Louis, mahali askofu wa Lorraine aliimba Te Deum. ... Nishani ikapigwa kwa kumbukumbu la machinjo. ... Padri wa Ufransa ... akasema kwa ajili ya'siku ile akijaa na kicheko na furaha, wakati baba mtakatifu
[128] alipokea habari, na akaenda kwa hali ya heshima kwa kumshukuru Mungu na Mtakatifu Ludoviko."

Roho mbaya ya namna moja iliyosukuma kuuawa kwa Saint-Barthelemy akaongoza pia katika maonyesho za Mapinduzi. Yesu Kristo akatangazwa kuwa kama mjanja, na kilio cha makafiri wa Ufransa kikawaangamiza wamaskini," maana yake Kristo. Matukano na uovu yakaenda pamoja. Katika haya yote, ibada ilitolewa kwa Shetani, wakati Kristo, katika tabia zake za kweli, usafi, na upendo wake wa kupendelea wengine kuliko yeye mwenyewe, alisuubiwa."

"Yule nyama anayetoka katika shimo pasipo mwisho atafanya vita nao; naye atawashinda na kuwaua." Ufunuo 11:7. Mamlaka ya kukana kumjua Mungu iliyotawala katika Ufransa wakati wa Mapinduzi na utawala wa Hofu kuu ilipigana vita ya namna hiyo kumpinga Mungu na Neno lake. Ibada ya Mungu ikakomeshwa na baraza la Taifa. Vitabu vya Biblia vikakusanywa na kuchomwa mbele ya watu wote. Vyama vya Biblia vikaharibiwa. Siku ya kustarehe ya juma ikakatazwa, na mahali pake kila siku kumi ikatengwa kwa makutano. Ubatizo na ushirika Mtakatifu (Meza ya Bwana) vikakatazwa. Matangazo yakawekwa kwa mahali pa maziko kutangaza kwamba mauti ni usingizi wa milele.

Ibada ya dini yote ikakatazwa, ila tu ile ya uhuru na ya inchi. "Askofu wa kushika sheria wa Paris akaletwa ... kwa kutangaza kwa

mapatano kwamba dini aliyofundisha kwa miaka nyingi ilikuwa, katika heshima yote, sehemu ya ujanja wa mapadri, ambayo haikuwa na msingi hata katika historia ao ukweli takatifu. Katika maneno ya kutisha sana na ya wazi, akakana kuwako kwake Mungu ambako alijitakasa kwa ajili yake."

"Nao wanaokaa juu ya dunia watafurahi juu yao na kuwachekelea. Watapelekeana zawadi moja kwa wengine, kwa sababu manabii hawa wawili waliwatesa wao wanaokaa juu ya dunia." Ufunuo 11:10. Ufransa kafiri ukanyamazisha sauti yenye kulaumu ya washahidi wawili wa Mungu. Neno la ukweli likalala chini kama maiti" katika njia zake, na wale waliochukia sheria za Mungu wakafurahi. Watu kwa wazi wakachafua Mfalme wa mbinguni.

Te Deum : Wimbo wa kushukuru wa kanisa la kikatoliki unaoanza na maneno haya : ''Bwana tunakusifu".

**Uhodari wa Kutukana Mungu**

Mmojawapo wa "mapadri" wa agizo jipya akasema: "Mungu, kama Unakuwako, lipisha kisasi cha matukano yanayofanywa kwa kutukana jina iako. Ninakualika! Unakaa kimya; Husubutu kutuma [129]
ngurumo zako. Nani baada ya hii atakayeamini kuwako kwako tena?" Ni jibu gani hili la swali la Farao: "Bwana ni nani, nisikie sauti yake?"

"Mupumbafu amesema moyoni mwake: Hakuna Mungu." Na Bwana anasema, "Upumbafu wao utaonyeshwa wazi kwa watu wote." Zaburi 14:1; 2 Timoteo 3:9. Wakati Ufransa ulipokataa ibada ya Mungu mwenye uhai haukukawia kushuka katika ibada ya haya ya kuabudu Mungu wa kike wa Akili (kutumia akili), mwanamke msharati. Ibada hii ikaanzishwa kwa msaada wa mkutano wa taifa! Mojawapo wa sherehe ya wakati huu wa wazimu kusimama inayopita yote kwani upumbafu ilichanganyika na ukosefu wa heshima kwa Mungu. Milango ya mapatano ikafunguliwa wazi wazi. ... Washiriki wa utawala wa mji wakaingia katika mwandamano wa taratibu, kuimba wimbo kwa sifa za uhuru, na kufuatana, kama kitu cha ibada ya wakati ujao, mwanamke mmoja aliyefunikwa, waliyemwita Mungu wa Kike wa Kutumia Akili. Alipokuwa katika baraza ya hukumu, wakamvua mwili wote kwa heshima, na wakamweka upande wa kuume wa msimamizi, ambapo alipoju-

likana kwa kawaida kama binti mchezaji wa mchezo wa kuigiza (opera).

### Mungu wa Kike wa Kutumia Akili

"Kusimamisha Mungu wa Kike wa Kutumia Akili kukafanywa upya na kuigwa na taifa po pote, katika mahali ambapo wakaaji walitaka kujionyesha wenyewe kulingana na usitawi wote wa Mapinduzi."

Wakati "mungu wa kike" alipoletwa kwa Mapatano; msemaji akamkamata kwa mkono, na akageukia makutano akasema: "Wanadamu, muache kutetemeka mbele ya ngurumo zaifu za mungu ambazo wogo wenu umezifanya. Tangu leo msikubali tena umungu mwengine bali Kutumia Akili. Ninawapongoatia picha yake bora na safi sana; kama kunapaswa kuwa na sanamu, mjitoe tu kwa hii. ...

"Mungu wa kike alipokwisha kukumbatiana na msimamizi, akapandishwa kwa gari tukufu kabisa, na akapelekwa kwa kanisa kubwa la Notre Dame, kupata nafasi ya Umungu. Hapo akainuliwa kwa mazabahu ya juu, na kuabudiwa na wote waliokuwako."

Dini ya Papa alianza kufanya kazi ambayo kukana Mungu kulikuwa kukitimiza, kuharakisha Ufransa kwa uharibifu. Waandishi kwa kutaja machukizo ya Mapinduzi wakasema kwamba mazidio haya yalipaswa kuwekwa juu ya kiti cha mfalme na kanisa. (Tazama Nyongezo.) Kwa haki yote, mazidio haya inapaswa kuwekwa juu
[130] ya kanisa. Kanisa la Papa lilipotosha mafikara ya wafalme juu ya Matengenezo. Ujanja wa Roma ilisababisha ukali na ugandamizi kutoka kwa uliotumiwa mamlaka ya mfalme.

Po pote injili ilikubaliwa, mafikara ya watu yakaamshwa. Wakaanza kutupa minyorori (viungo vya pingu vilivyowashikilia) kuwa watumwa wa ujinga na ibada ya sanamu. Wafalme waliviona na wakatetemeka kwa ajili ya uonevu wao.

Roma ikaharakisha kuwasha vitisho vyao vya wivu. Katika mwaka 1525, Papa akasema kwa watawala wa Ufransa: "Huyu wazimu shetani (Dini ya Kiprotestanti) hatatoshelewa kuchafua dini na kuiangamiza, bali mamlaka zote, cheo kikubwa, sheria, amri, na hata madaraja tena." Tangazo la Papa likaonya mfalme: "Waprotestanti watapindua amri yote ya serkali na ya dini pia. ...

Kiti cha mfalme kinakuwa hatarini kama vile mazabahu." Roma ikafaulu kupanga Ufransa kwa kupinga Matengenezo.

Mafundisho ya Biblia yangeimarisha katika mioyo ya watu kanuni za haki, kiasi, na kweli, vinavyokuwa jiwe la pembeni kwa usitawi wa taifa. "Haki inainua taifa." Maana "Kiti cha ufalme kinasimamishwa kwa haki." Mezali 14:34; 16:12. Tazama Isaya 32:17. Yeye anayetii sheria ya Mungu atazidi kwa kweli kuheshimu na kutii amri za inchi. Ufransa ulikataza Biblia. Karne kwa karne watu wa haki, wa ukamilifu wa elimu na matendo mema, waliokuwa na imani kwa kuteseka kwa ajili ya kweli, wakaenda kwa taabu kama watumwa katika jahazi, wakaangamizwa kwa kigingi (tita), ao kuoza ndani ya pango za gereza. Maelfu wakapata usalama katika kukimbia kwa miaka 250 baada ya kufunguliwa kwa Matengenezo.

"Labda hapakuwa na kizazi cha Ufransa, kwa mda wa wakati ule mrefu ambao hawakushuhudia wanafunzi wa injili kukimbia mbele ya mauaji kali ya wazimu ya watesi wao, na kuchukua akili yao pamoja nao, vitu vya ufundi, utendaji, na roho yao ya utaratibu, kwa kutangulia wakapita, kwa kutayarisha inchi ziiizowapatia kimbilio. ... Kama hawa wote sasa waliofukuza wangalirudi Ufransa, ingalikuwa inchi ya namna gani ... kubwa, ya usitawi, na ya furaha--mfano kwa mataifa--ingalikuwa! Lakini bidii isiyo ya akili ya upofu na kizazi kisichokuwa na huruma kikafukuza kwa inchi yake kila mwalimu wa nguvu, kila shujaa wa roho ya utaratibu, kila mtetezi mwaminifu wa kiti cha mfalme. ... Mwishowe uharibifu wa taifa ukatimilika."

Matokeo yake yalikuwa Mapinduzi pamoja na machafuko.

## Ingeweza kuwa Nini [131]

Kukimbia kwa Wahuguenots,ufungufu na inchi nzima ukawa katika Ufransa. Miji ya usitawi kwa viwanda ikaanguka kwa uharibifu. ... Ikakadirishwa kwamba, kwa mwanzo wa Mapinduzi, maelfu mia mbili ya wamaskini katika Paris wakadai mapendo kwa mikono ya mfalme. Wajesuites peke yao walifanikiwa katika taifa lililoharibika."

Injili ingalileta suluhu kwa magumu hayo yaliyoshinda mapadri wake, mfalme, na wafanya sheria, na mwishowe wakaingiza taifa katika uharibifu. Lakini chini ya utawala wa Roma watu wakapoteza

mafundisho ya Mwokozi ya kujinyima na upendo wa choyo kwa ajili ya mazuri ya wengine. Mtajiri hakuwa na karipio kwa ajili yakugandamiza maskini; maskini hawakuwa na msaada kwa uzaifu wao. Choyo ya mtajiri na uwezo yakazidi kulemea. Kwa karne nyingi, watajiri wakakosea wamaskini, na wamaskini wakawachukia matajiri.

Katika majimbo mengi madaraka ya wafanyakazi yalikuwa chini ya wenyeji na walilazimishwa kutii maagizo ya kupita kiasi. Madaraja ya katikati na ya chini ya wafanya kazi wakalipishwa kodi ya nguvu kwa watawala wa serkali na wa dini. "Wakulima na wakaaji wa vijiji waliweza kuteswa na njaa, kwani watesi wao hawakujali. ... Maisha ya watumikaji wakulima yalikuwa ya kazi isiyokuwa na mwisho na taabu isiyokuwa na kitulizo; maombolezo yao ... yaiizaniwa kuwa zarau ya ushupavu. ... Mambo mabaya ya rushwa yakakubaliwa kwa hakika na waamzi. ... Ya kodi, ... nusu ya feza ikaenda kwa hazina ya mfalme ao ya askofu; inayobaki ikatumiwa ovyo ovyo katika anasa ya upotovu. Na watu waliozoofisha hivi wenzao wakaachiliwa wenyewe bila kulipa kodi na walikuwa na haki kwa sheria ao kwa desturi, kwa maagizo yote ya serkali. ... Kwa ajili ya furaha yao mamilioni walihukumiwa maisha mabaya bila tumaini." (Tazama Nyongezo.)

Zaidi ya nusu ya karne mbele ya Mapinduzi kiti cha ufalme kilikaliwa na Louis XV, aliyetambulika nakuwa mfalme mvivu, asiyejali, na waanasa. Kwa habari ya feza ya serkali wakawa na matatizo na watu wakakasirishwa, haikuhitajiwa jicho la nabii kuona maasi makali. Ilikuwa vigumu kuharakisha hoja ya kufanya matengenezo. Ajali iliyongojea Ufransa ilielezwa katika jibu la kujipenda ama choyo cha mfalme, "Baada yangu, garika!"

Roma ilivuta wafalme na vyeo vya watawala kuweka watu katika utumwa, kukusudia kufunga wote watawala na watu katika vifungo
[132] vyake vya minyororo juu ya roho zao. Huku hali mbaya ya tabia njema ambayo ni matokeo ya siasa hii ilikuwa ya kutisha zaidi mara elfu kuliko mateso ya kimwili. Kukosa Biblia, na kujitia katika kujipendeza, watu wakajifunika katika ujinga na kuzama katika maovu, kabisa hawakuweza kujitawala.

### Matokeo Yaliyopatwa katika Damu

Baadala ya kudumisha watu wengi katika utii wa upofu kwa mafundisho yake, kazi ya Roma ikaishia katika kuwafanya makafiri na wapinduzi. Dini ya Roma wakaizarau kama ujanja wa wapadri. Mungu mmoja waliomujua ni mungu wa Roma. Waliangalia tamaa yake na ukatili kama tunda la Biblia, na hawakutaka tena kusikia habari yake.

Roma ilieleza vibaya tabia ya Mungu, na sasa watu wakakataa vyote viwili Biblia na Muumba wake. Katika urejeo, Voltaire na wafuasi wake wakakataa kabisa Neno la Mungu yote pamoja kutawanya kukana Mungu. Roma ikakanyaga watu chini ya kisigino chake cha chuma; na sasa watu wengi wakatupia mbali kuzuiwa kote (amri). Walipokasirishwa, wakakataa kweli na uongo pamoja.

Kwa kufunguliwa kwa Mapinduzi, kwa ukubali wa mfalme, watu wakapata kwa mitaa ya kawaida mfano wa juu kuliko ule wa wakuu na mapadri pamoja. Kwa hivyo kipimo cha uwezo kulikuwa katika mikono yao; lakini hawakutayarishwa kukitumia kwa hekima na utaratibu (kiasi). Watu waliotendewa vibaya wakakusudia kulipiza kisasi wao wenyewe. Walioonewa wakatumia fundisho walilojifunza chini ya uonevu na wakawa watesi wa wale waliowatesa.

Ufransa ukavuna katika damu mavuno ya utii wake kwa Roma. Mahali Ufransa, chini ya Kanisa la Roma, uliweka tita (kigingi) la kwanza kwa mwanzo wa Matengenezo, hapo Mapinduzi yakaweka mashini yake ya kukata watu vichwa ya kwanza. Ni mahali pale ambapo, kwa karne ya kumi na sita, wafia dini wa kwanza wa imani ya Kiprotestanti walichomwa, watu wa kwanza walikatwa vichwa kwa karne ya kumi na mnani. Wakati amri za sheria ya Mungu ziliwekwa pembeni, taifa likaingia katika giza na machafuko ya mambo ya utawala. Vita juu ya Biblia katika historia ya ulimwengu ikajulikana kwa jina la Utawala wa hofu kuu. Yeye aliyeshinda leo akahukumiwa kesho yake.

Mfalme, waongozi wa dini, na wakuu wakalazimishwa kujiweka chini ya mambo ya mabaya ya watu wenye wazimu. Wale walioamuru kifo cha mfalme mara wakamfuata kwa jukwaa. Machinjo makubwa ya wote waliozaniwa kuwa na uchuki kwa Mapinduzi [133] yakakusudiwa. Ufransa ukawa shamba kubwa la mabishano, yaliyowayawaya kwa hasira kali ya tamaa. “Katika Paris,fujo ikafuata

fujo ingine, na wakaaji wakajitenga katika machafuko ya fitina, yaliyoonekana yenye bidii si kwa kitu kingine bali kusudi moja. ... Inchi ilikuwa karibu kushindwa, majeshi yalikuwa yakifanya fujo kwa ajili ya deni ya malipo, wakaaji wa Paris walikuwa na njaa, mitaa ikaangamizwa na wanyanganyi, na utamaduni na maendeleo vilikuwa karibu kukomeshwa katika machafuko ya mambo ya utawala na upotovu."

Kwa yote haya watu wakajifunza mafundisho ya ukali na mateso ambayo Roma ilifundisha kwa nguvu sana. Haikuwa sasa wanafunzi wa Yesu waliokokotwa kwa kigingi. Ni Zamani walikuwa ao kuchinjwa wala kulazimishwa kujihamisha. "Damu ya wapadri ilitiririka juu ya majukwaa. Majahazi na gereza, zamani zilikuwa zikijaa na Wahuguenots, yakajaa sasa na watesi wao. Wakafungiwa na minyororo kwa viti vyao na kukokota kwa gasia, wapadri wa Katoliki wa Roma wakajua misiba ile yote ambayo kanisa lao lilipatisha kwa bure kabisa juu ya wazushi wapole." (Tazama Nyongezo.)

"Ndipo siku zile zikaja ... wakati wapelelezi walijificha kwa kila pembe; wakati mashine ya kukatia vichwa ilikuwa ndefu na ya nguvu kwa kazi kila asubuhi: wakati magereza zikijaa kama kiwanja kama chumba cha chini cha merikebu ya watumwa; wakati damu na uchafu vikawa kama pofu na kutiririka katika mifereji ya mabati hata mto seine" ... mistari mirefu ya watumwa yalisukumwa chini kwa marisaa makubwa. Matundu yalifanywa katika upande wa chini wa mashua kubwa iliosongana. ... Hesabu ya vijana wanaume na wanawake wa miaka kumi na saba waliuawa kwa serekali ile mbaya sana, inajulikana kuwa mamia. Watoto wachanga waliotengwa kwa kifua cha mama wakarushwa kutoka kwa mkuki na kwa mkuki mwengine kwa cheo cha wa Jacobins." (Tazama Nyongezo.)

Haya yote yalikuwa ni mapenzi ya Shetani. Amri yake ni madanganyo na makusudi yake ni kuleta uharibifu juu ya watu, kutia haya kiumbe cha Mungu, kwa kuharibu kusudi la Mungu la upendo, na kwa hiyo kuleta sikitiko mbinguni. Basi kwa mambo yake ya ufundi ya kudanganya, huongoza watu kutupa laumu juu ya Mungu, kana kwamba mateso haya yote yalikuwa matokeo ya shauri la Muumba. Wakati watu waliona dini ya Roma kuwa danganyifu, akawashurutisha kuzania dini yote kama danganyifu na Biblia kama hadisi (uongo).

## Kosa la Hatari [134]

Kosa la mauti ambalo lilileta msiba wa namna hiyo kwa Ufransa lilikuwa kuitokujali kwa ukweli huu mmoja mkubwa; uhuru wa kweli unaokuwa katikati ya makatazo ya sheria ya Mungu. "Laiti ungalisikiliza maagizo yangu! Ndipo salama yako ingalikuwa kama mto, na haki yako kama mawimbi ya bahari." Isaya 48:18. Wale ambao hawatasoma fundisho kutoka kwa Kitabu cha Mungu wanaalikwa kulisoma katika historia.

Wakati Shetani alitenda kwa njia ya kanisa la Roma kuongoza watu kuacha utii, kazi yake ikageuka.. Kwa kazi ya Roho wa Mungu makusudi yake yakazuiwa kufikia matumizi yao kamili. Watu hawakutafuta matokeo kwa mwanzo wake na kuvumbua asili ya taabu zao. Lakini katika mapinduzi sheria ya Mungu iliwekwa kando kwa wazi na Baraza la Taifa. Na katika Utawala wa Hofu Kuu uliofuata, kazi na matokeo yaliweza kuonekana kwa wote.

Kuvunja sheria ya haki na nzuri matunda yake inapaswa kuwa maangamizi. Roho wa Mungu wa kiasi, ambaye analazimisha uaguzi juu ya uwezo mkali wa Shetani, uliotoka kwa kiasi kikubwa, na yule ambaye furaha yake ni taabu ya watu aliruhusiwa kufanya mapenzi yake. Wale waliochagua uasi waliachiwa kuvuna matunda yake. Inchi ikajaa na zambi. Kutoka mitaa iliyoteketezwa na miji iliyoangamizwa kilio, cha kutisha kilisikiwa cha maumivu makali. Ufransa ukatikisishwa kama kwa tetemeko. Dini, sheria, kanuni ya watu wote, jamaa, serkali, na kanisa--vyote vikashindwa na mkono mpotovu ambao uliinuliwa kupinga sheria ya Mungu.

Washuhuda waaminifu wa Mungu, waliochinjwa kwa uwezo wa dini ya yule "anayotoka katika shimo pasipo mwisho," hawakubakia kimya." Na nyuma ya siku tatu na nusu, roho ya uhai ikatoka kwa Mungu ikaingia ndani yao, wakasimama juu ya miguu yao; woga mkubwa ukaangukia watu wote waliowatazama." Ufunuo 11:11. Katika mwaka 1793 Baraza la Taifa la Ufransa likaweka amri za kutenga Biblia kando. Miaka mitatu na nusu baadaye, shauri la kutangua amri hizi likakubaliwa na mkutano ule ule. Watu wakatambua lazima ya imani katika Mungu na Neno lake kama msingi wa uwezo na maarifa ya wema na ubaya.

Kwa habari ya "washuhuda wawili" (Maagano ya Kale na Jipya) nabii akatangaza zaidi: "Wakasikia sauti kubwa kutoka mbingu

ikisema kwao: Pandeni hata hapa. Wakapanda mbinguni katika wingu, adui zao wakiwatazama." Ufunuo 11:12. "Washahidi hawa wawili wa Mungu" wakaheshimiwa zaidi kuliko mbele. Katika
[135] mwaka 1804 Chama cha Biblia cha Uingereza na inchi za kigeni kikatengenezwa, kikafuatwa na matengenezo ya namna hii juu ya bara la Ulaya. Katika mwaka 1816 chama cha Biblia cha Waamarica kikaimarishwa. Biblia ikatafsiriwa tangu hapo katika mamia mengi ya lugha na matamko. (Tazama Nyongezo).

Mbele ya mwaka 1792, uangalifu kidogo ukatolewa kwa watu waliopasha kwenda kufundisha na inchi za kigeni. Lakini karibu ya mwisho wa karne ya kumi na mnane mabadiliko kubwa yakafanyika. Watu wakawa hawatoshelewi na kufuata akili za binadamu na wakapatwa na lazima ya ufunuo wa mambo ya kimungu na dini ya hakika. Tokea wakati huu kazi za ujumbe wa kigeni zikapata maendeleo kuliko mbele. (Tazama Nyongezo.)

Maendeleo katika ufundi wa uchapishaji ulisaidia sana kwa maenezi ya Biblia. Kupotea kwa upendeleo usio na haki wa zamani na ubaguzi wa taifa na mwisho wa uwezo wa ulimwengu, askofu wa Roma kukafungua njia kwa mwingilio wa Neno la Mungu. Sasa Biblia ikachukuliwa kwa kila sehemu ya dunia.

Kafiri Voltaire akasema: "Nachoka kusikia kukariri kwamba watu kumi na mbili walianzisha dini ya kikristo." Nitawaonyesha kwamba mtu mmoja anatosha kwa kuiangamiza" (N.B Missine,sentence). Mamilioni ya watu wakajiunga katika vita juu ya Biblia. Lakini ni mbali kwa kuiangamiza. Mahali palikuwa mia kwa wakati wa Voltaire, sasa panakuwa vitabu ama nakala mamia ya maelfu ya Kitabu cha Mungu. Katika maneno ya Mtengenezaji wa mwanzo, "Biblia ni chuma cha mfinyanzi iliyomaliza nyundo nyingi." Chochote kitu kilichojengwa juu ya mamlaka ya mtu kitaangushwa; lakini kile ambacho kilijengwa juu ya mwamba wa Neno la Mungu, kitasimama milele

# 16 /KUTAFUTA UHURU KATIKA DUNIA MPYA [136]

Ijapo mamlaka na imani ya Roma mambo yale yalikataliwa, kanuni nyingi ziliingizwa katika ibada ya Kanisa la Uingereza. Ilidaiwa kwamba mambo yasiyokatazwa katika Maandiko hayakuwa na uovu wa hatari. Kwa kuyashika kunafaa kwa kupunguza shimo kubwa ambalo lilitenga makanisa ya matengenezo na Roma, na ilishurtishwa kwamba wangesaidia Wakatoliki kukubali imani ya Kiprotestanti.

Kundi lingine halikuamua vile. Waliangalia desturi hizi kama dalili ya utumwa ambao walikombolewa. Walifikiri kwamba Mungu katika Neno lake ameimarisha maagizo kwa kutawala ibada yake, na kwamba watu hawana uhuru wa kuongeza kwa haya ao kutosha kwa haya. Roma ikaanza kulazimisha yale Mungu hakukataza,na ikaishia kukataza yale aliyo amuru wazi wazi.

Wengi wakaangalia desturi za Kanisa la Kiingereza kama nguzo za ukumbusho wa ibada ya sanamu, na hawakuweza kujiunga kwa ibada yake. Lakini Kanisa lilisaidiwa na mamlaka ya serkali, haingeruhusu mafarakano. Mikutano isiyoruhusiwa kwa ajili ya ibada ilikatazwa chini ya malipizi ya kufungwa, kuhamishwa ao mauti.

Kuwindwa, kuteswa, na kufungwa, watu walioishi maisha safi ya unyofu hawakuweza kutambua ahadi ya siku bora. Wengine wakakusudia kutafuta kimbilio katika Uhollande, wakasalitiwa katika mikono ya adui zao. Lakini wakavumilia kwa uaminifu na mwishowe wakashinda, na wakapata kimbilio katika pwani za urafiki.

Waliacha nyumba zao na mali yao ya uchumi. Walikuwa wageni katika inchi ya kigeni, kurudia kwa kazi mpya ili wapate mkate wao. Lakini hawakupoteza wakati kwa uvivu ao kusikitika. Walimshukuru Mungu kwa ajili ya mibaraka waliyopata na wakawa na furaha katika ushirika wa kiroho wa raha ambao haukusumbuluwa.

## Mungu akageuza matokeo

Wakati mkono wa Mungu ulionekana ukiwashota kuvuka bahari kwenda kwa inchi ambayo wanaweza kupata inchi na kuachia watoto wao uriti wa uhuru wa dini, wakaendelea katika njia ya maongozi ya Mungu. Mateso na kujihamisha vilikuwa vikifungua njia kwa uhuru.

Wakati mara ya kwanza walipolazimishwa kujitenga kutoka kwa kanisa la Kiingereza, Watu walioishi maisha safi wakajiunga waowenyewe kwa maagano kama watu huru wa Bwana "kwa
[137] kutembea pamoja katika njia zake zote zilizojulishwa ao zinazopaswa kujulishwa kwao." Hapa ndipo palikuwa na kanuni ya maana sana ya Kiprotestanti. Kwa kusudi hili Wasafiri wakatoka Uholandi kutafuta makao katika Dunia Mpya. Yohana Robinson, mchungaji wao, katika hotuba yake ya kuaga kwenda kwa mahamisho akasema:

"Nawaagiza mbele ya Mungu na malaika wake wenye kubarikiwa kwamba munifuate si mbali kama nilivyomfuata Kristo. Kama Mungu angepashwa kufunua kitu cho chote kwenu kwa chombo kingine chake, muwe tayari kukikubali kwa furaha mliyokuwa nayo kukubali ukweli wa kazi yangu ya kuhubiri; kwa maana ninakuwa na tumaini kwamba Bwana anakuwa na ukweli zaidi na nuru kuangazia ya neno lake takatifu."

"Kwa upande wangu mimi, siwezi kusikitikia ya kutosha hali ya makanisa ya matengenezo, ambayo ...haitaenda sasa mbali zaidi kuliko wasimamizi wao wa matengenezo. Haiwezekani kuvuta watu wa dini ya Luther kufanya hatua moja zaidi mbali kuliko Luther alivyoona; ... na watu wa imani ya Calvin, munawaona wanabakia pale ambapo mutu mkuu wa Mungu aliwaacha, ambaye hata hivyo hakuona mambo yote. ... Ijapo walikuwa taa za kuwaka na kuangaza katika wakati wao, lakini hawakujua shauri lote la Mungu, lakini kama wangaliishi leo, wangekubali nuru mpya zaidi kama ile waliyokubali mara ya kwanza."

"Kumbukeni ahadi yenu na agano pamoja na Mungu na pamoja na mtu kwa mwenzake, kukubali nuru yo yote na ukweli utakaojulishwa kwenu kutoka kwa neno lake lililoandikwa; lakini zaidi, mjihazari, nawasihi, kuhusu mnayokubali kwa ajili ya kweli, na kuilinganisha na kupima uzito wake kwa maandiko mengine ya uk-

weli mbele ya kuikubali; kwani haiwezekani kwa dunia la Kikristo ambayo ilitoka giza nzito kwa kuchelewa ifikie maarifa kamili mara moja."

Haja ya uhuru wa zamiri ikaongoza Wasafiri kuvuka bahari, kuvumukia magumu ya jangwani, na kuweka msingi wa taifa kubwa. Lakini Wasafiri hawakufahamu bado kanuni ya uhuru wa dini. Uhuru ambao walijitolea kafara sana kwa ajili yao wenyewe, hawakuwa tayari kuutolea wengine. Mafundisho ambayo Mungu alitolea Kanisa haki ya kuongoza zamiri na kuleza wazi na kuazibu uzushi ni mojawapo ya makosa makubwa ya Kanisa la Roma. Watengenezaji hawakuwa na uhuru kabisa kwa roho ya Roma ya kutovumilia. Giza kubwa sana ambayo Roma ilifunika Kanisa la Kikristo haikuondolewa kabisa.

Kanisa la serkali lilitengenezwa na wagandamizi, waamuzi walioruhusiwa kukomesha uzushi. Kwa hiyo uwezo wa serkali ulikuwa mikononi mwa Kanisa. Mipango hii haikuleta matokeo [138]
mengine isipokuwa mateso.

## Roger Williams

Kama vile Wasafiri wa kwanza, Roger Williams akaja kwa Dunia Mpya kufurahia uhuru wa dini. Lakini aliufahamu kwa namna ingine si kama Wasafiri, akaona mambo ambayo watu wachache tu waliona, kwamba uhuru huu ulipashwa kuwa haki kwa watu wote. Alikuwa mtafuti (atafutaye) wa bidii wa kweli. Williams alikuwa mtu wa kwanza katika Ukristo wa kisasa kwa kuanzisha serkali inayosimamia kwa mafundisho ya uhuru wa zamiri." "Watu ao waamuzi wanaweza kukata shauri," akasema, "ni nini inastahili kati ya mtu na mtu; lakini wanapojaribu kufafanua wajibu wa mtu kwa Mungu, hapa wanaachana na Mungu, na hapo hapawezi kuwa na salama; kwani ni wazi kwamba kama mwamuzi anakuwa na uwezo, angeweza kuamuru shauri fulani ao imani leo na ingine kesho; kama ilivyokuwa ikifanyika katika Uingereza na wafalme wa kuachana na wamalkia, na mapapa wa kuachana na mabaraza katika Kanisa la Roma."

Kuhuzuria katika kanisa lililosimamishwa ililazimishwa chini ya malipo ao kifungo. "Kushurutisha watu kuungana pamoja na wale wa imani ya kuachana, yeye (Williams) aliangalia jambo hilo

kama kutendea zambi kwa wazi kwa haki zao halisi, kukokota watu wasio kuwa wa dini kwa ibada na wasiopenda, ilikuwa ni kukuza unafiki... Hakuna mutu alipashwa kulazimishwa kuabudu Mungu, ao, akaongeza, kushikilia ibada, kinyume cha ukubali wake mwenyewe!"

Roger Williams aliheshimiwa, lakini haja yake kwa ajili ya uhuru wa dini haukuweza kuvumiliwa. Kwa kuepuka kufungwa akalazimishwa kukimbilia kati kati ya baridi ng zoruba ya majira ya baridi katika poli usiokatwa bado.

"Kwa muda wa majuma kumi na inne," akasema, "Nikarushwa sana katika majira ya uchungu, bila kuwa na mkate ao kitanda." Lakini "Kunguru wakanilisha jangwani," shimo ndani ya mti nikaitumia mara kwa mara kuwa ficho." Akaendelea na ukimbizi wake wa uchungu katika theluji na mwitu usio na njia hata akapata kimbilio pamoja na kabila la Wahindi ambao aliopata matumaini na upendo wao.

Akaweka msingi wa jimbo la kwanza la nyakati za kisasa lile lililo tambua haki "kwamba kila mutu alipashwa kuwa na uhuru kwa kuabudu Mungu kufuatana na nuru ya zamiri yake mwenyewe." Jimbo lake ndogo, Kisiwa cha Rhode, likaongezeka na kusitawi hata
[139] kwa kanuni zake za msingi--uhuru wa serekali na wa dini--vikawa mawe ya pembeni ya Jamuhuri ya Amerika.

### Barua ya maagano wa Uhuru

Tangazo la Amerika la Uhuru likatangazwa: "Tunashika kweli hizi kuwa zamiri binafsi, kwamba watu wote waliumbwa kuwa sawasawa; na kwamba Muumba aliwapa haki fulani zisizoondolewa; ambazo katika hizo kuna uzima, uhuru, na kutafuta furaha." Serkali (ya Amerika) iliahidi heshima ya zamiri: "Baraza kuu halitaweza kufanya sheria hata moja inayosimamia kwa dini, ao inayokataza uhuru wa dini."

"Watengenezaji wa Serkali wakatambua kanuni ya milele kwamba uhusiano wa mtu na Mungu wake unakuwa juu ya sheria ya binadamu, na haki zake za zamiri ya daima... Ni kanuni yakuliwa ambayo hakuna kitu kitakacho weza kuiondoa."

Habari ikaenezwa katika Ulaya kwamba kuna inchi ambapo kila mtu anaweza kufurahiwa matunda ya kazi yake na kutii zamiri yake.

Maelfu wakasongana kwa pande za pwani za Dunia Mpya. Katika miaka makumi mbili kutoka siku ya kufika mara ya kwanza huko Plymouth (1620), jinsi maelfu mengi ya Wasafiri walikaa katika Uingereza Mpya.

"Hawakuomba kitu kwa inchi bali zawadi za kweli za kazi yao... Waliishi kwa uvumilivu wa taabu ya jangwani, wakanyunyizia maji ya mti wa uhuru kwa machozi yao, na jasho ya vipaji vya nyuso zao, hata ukatia mizizi yake chini sana katika inchi."

## Ulinzi wa kweli Kabisa wa Ukuu wa Taifa

Kanuni za Biblia zilikuwa zikifundishwa katika jamaa, chuoni, na kanisani; matunda yake yalionekana katika uangallifu wa kutumia feza, akili, usafi, na kiasi. Mtu mmoja angeweza kwa muda wa miaka "bila kuona mlevi, ao kusikia kiapo, wala kukutana na muombaji." Kanuni za Biblia ndizo kingo ao walinzi wa kweli kabisa wa ukuu wa taifa. Inchi zaifu zilizokuwa chini ya utawala wa inchi ingine (colony) zilifanikiwa na kuwa majimbo yenye uwezo, na dunia ikaona usitawi wa "kanisa bila Papa, na serkali bila mfalme."

Lakini hesabu iliongezeka ya watu waliovutwa na Amerika kwa makusudi tofauti na Wasafiri wa kwanza. Hesabu iliyoongezeka ni ya wale waliotafuta tu faida ya kidunia.

Mabwana wa kwanza wakaruhusu washiriki wa kanisa tu kwa kuchagua ao kuongoza kazi katika Serkali. Mpango huu ulikubaliwa kwa kulinda usafi wa Serkali; ukaleta matokeo ya uharibifu wa [140]
kanisa. Wengi wakajiunga na kanisa bila badiliko la moyo. Hata katika kazi ya injili kulikuwa wale waliokuwa wajinga wa uwezo mpya wa Roho Mtakatifu. Tangu siku za Constantine hata wakati huu, kujaribu kujenga kanisa kwa usaada wa serkali, ambapo inaweza kuonekana kuleta ulimwengu karibu ya kanisa, kwa kweli huleta kanisa karibu ya ulimwengu.

Makanisa ya Protestanti ya Amerika, na yale ya Ulaya pia, yakashindwa kuendelea mbele katika njia ya matengenezo. Wengi, kama Wayahudi wa siku za Kristo ao wakatoliki katika wakati wa Luther, walirizika kuamini kama mababa zao walivyoamini. Makosa na ibada ya sanamu vilishikwa. Matengenezo polepole yakafa, hata kukawa haja kubwa sana ya matengenezo katika makanisa ya Kiprotestanti hata katika kanisa la kiRoma wakati wa Luther.

Hapo kulikuwa heshima ya namna moja kwa maoni ya watu na kutia mafikara ya binadamu kwa nafsi ya Neno la Mungu. Watu wakaacha kutafuta Maandiko na kwa hiyo wakaendelea kutunza mafundisho ambayo haikuwa na msingi katika Biblia.

Kiburi na upotovu (ujinga) yakalindwa chini ya umbo la dini, na makanisa yakaharibika. Mambo ya asili ambayo yalipaswa kuharibu mamilioni ya watu yalikuwa yakipata mizizi ya nguvu. Kanisa lilikuwa likishika mambo ya asili haya baadala ya kushindana kwa ajili ya "imani ambayo iliyotolewa kwa watakatifu."

Ndiyo namna kanuni ziliunguzwa heshima (aibishwa) ambazo Watengenezaji walizotesekea sana.

# 17 /AHADI ZA KURUDI KWA KRISTO [141]

Ahadi ya kuja kwa Kristo mara ya pili ili kutimiza kazi kubwa ya ukombozi ni msingi wa Maandiko matakatifu. Tangu Edeni, watoto wa imani wamengojea kuja kwa Yule Aliyeahidiwa kwa kuwaleta tena kwa Paradiso iliyopotea.

Enoki, mtu wa saba katika uzao kutoka kwa wale ambao waliokaa katika Edeni, ambaye kwa karne tatu alitembea pamoja na Mungu, akatangaza, "Angalia, Bwana anakuja na watakatifu wake, elfu kumi, ill afanye hukumu juu ya watu wote," Yuda 14,15. Yobu katika usiku wa taabu akapaaza sauti, "Lakini ninajua ya kuwa Mkombozi wangu ni hai, Na ya kuwa katika siku za mwisho atasimama juu ya inchi:... pasipo mwili wangu nitamuona Mungu: Na mimi mwenyewe nitamuona. Na macho yangu yatamutazama, wala si mwingine." Yoba 19:25-27. Washairi (poets) na manabii wa Biblia walieleza sana juu ya kuja kwa Kristo katika maneno yenye mwangaza wa moto. "Mbingu zifurahi, na inchi ishangilie, ... Mbele ya Bwana, kwa maana anakuja; Kwa maana anakuja kuhukumu inchi. Atahukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa kwa kweli yake." Zaburi 96:11-13.

Akasema Isaya: "Katika siku ile itasemwa, Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Tumemungoja, ... Tutashangilia na tutafurahi katika wokovu wake." Isaya 25:9.

Mwokozi akafariji wanafunzi wake na tumaini ya kuwa atakuja tena: "Katika nyumba ya Baba yangu ni makao mengi ... ninakwenda, kuwatengenezea ninyi makao. Na kama ninakwenda, ... nitakuja tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu." "Mwana wa watu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika wote pamoja naye, halafu ataketi juu ya kiti cha utukufu wake; na mbele yake mataifa yote watakusanyika." Yoane 14:2,3; Matayo 25:31,32.

Malaika walikariri kwa wanafunzi ahadi ya kurudi kwake; "Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni." Matendo 1:11. Na Paulo akashuhudia: "Kwa sababu Bwana

mwenyewe atashuka toka mbinguni, na sauti kubwa, na sauti ya malaika mkubwa, pamoja na baragumu ya Mungu." 1 Watesalonika 4:16. Akasema nabii wa Patemo: "Tazama, anakuja na mawingu; na kila jicho litamwona." Ufunuo 1:7.

Halafu desturi ndefu iliyoendelea ya uovu itavunjika: "Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala hata milele na milele." Ufunuo 11:15. "Na
[142] kama shamba linalochipuza vitu vilivyopandwa ndani yake: ndivyo Bwana Mungu ataotesha haki na sifa mbele ya mataifa yote." Isaya 61:11.

Halafu ufalme wa amani wa Masiya utaimarishwa "Maana Bwana atafariji Sayuni; atafariji pahali pake pote pa pori; atafanya jangwa lake kuwa kama Edeni, na jangwa lake kama shamba la Bwana." Isaya 51:3.

Kuja kwa Bwana kumekuwa katika vizazi vyote tumaini la wafuasi wake wa kweli. Kati ya taabu na mateso, "na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mkubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristo" lilikuwa "tumaini la baraka." Tito 2:13. Paulo alionyesha kwamba ufufuo utafika wakati wa kurudi kwa Mwokozi, wakati waliokufa katika Kristo * watakapofufuka, na pamoja na wahai kuchukuliwa juu kukutana na Bwana katika mawingu. "Na hivi" akasema, "tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi mufarijiane kwa maneno haya." 1 Watesalonika 4:17.

Kule Patemo mwanafunzi mpendwa akasikia ahadi, "Ndiyo: ninakuja upesi." Na jibu lake linasimamia ombi la kanisa. "Amina, kuja Bwana Yesu." Ufunuo 22:20.

Kati ya gereza, kigingi, mahali wanaponyongwa kwa sheria, pahali watakatifu na wafia dini waliposhuhudia kwa ajili ya kweli, kutoka kwa karne nyingi za usemi wa imani yao na tumaini." Walipohakikishwa na ufufuo wa Yesu mwenyewe, na baadaye ufufuo wao wenyewe wakati wa kuja kwake, kwa sababu hii, "akasema mmojawapo wa Wakristo hawa," walizarau mauti, na wakapatikana kuwa juu yake, wa Waldenses walitunzaimani ile ile, Wyccliffe, Luther, Calvin, Knox, Ridley, na Baxter walitazamia kwa imani kurudi kwa Bwana. Ndiyo iliyokuwa tumaini la kanisa la mitume, la "kanisa katika jangwa," na la Watengenezaji.

Unabii hautabiri tu namna na kusudi la kuja kwa Kristo mara ya pili, bali huonyesha ishara ambazo watu wanapashwa kujua wakati

siku ile inapokaribia. “Na kutakuwa na ishara katika jua na mwezi na nyota.” Luka 21:25. “...jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa nuru yake, na nyota za mbingu zitaanguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika. Na wakati ule wataona Mwana wa watu akikuja katika mawingu pamoja na uwezo kubwa na utukufu.” Marko 13:24-26.

Muonyeshaji (nabii) basi anaonyesha mojawapo wa ishara zitakazo tangulia kuja kwa mara ya pili: “... tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la inchi, jua likakuwa jeusi kama gunia la manyoya, na mwezi wote ukakuwa kama damu.” Ufunuo 6:12.

### Tetemeko la inchi lililotikisa Ulimwengu [143]

Kwa kutimilika kwa unabii huu kulitokea katika mwaka 1755 tetemeko la inchi lililokuwa la kutisha zaidi lililoandikwa. Lilijulikana kama tetemeko la inchi la Lisbon, likaenea Ulaya, Afrika, na Amerika. Likasikiwa Groenland, Upande wa Magharibi ya Uhindi, katika Antilles, Norvege na Swede, Uingereza na Irland, kwa eneo si chini kuliko kilometres milioni ine kwa mraba. Katika Afrika mshindo ulikuwa karibu sana wa nguvu kama katika Ulaya. Sehemu Kubwa ya Algiers (Mji mkuu wa Algeria) ikaharibiwa. Wimbi kubwa la kutisha likazamisha pwani ya Espagne na ya Afrika na kudidimiisha miji.

Milima, “ingine katika milima inayo kuwa kubwa sana katika Portugal, ikatikiswa kwa nguvu sana, tangu kwa misingi yao; na ingine kati yao ikafunguka kwa vilele vyao, ambayo ilipasuka na kutengana kwa namna ya ajabu, mafungu makubwa yao kutupwa katika mabonde ya karibu. Ndimi za moto imehadiziwa kutoka kwa milima hizo.”

Huko Lisbon “Sauti ya ngurumo ilisikiwa chini ya udongo, na bila kukawia baadae kishindo kikali kikaangusha sehemu kubwa ya mji ule. Katika mwendo wa dakika karibu sita watu elfu makumi sita wakaangamizwa. Bahari mara ikarudi, na ikaacha kivuko kikavu; na kurudi ndani yake, nakuinuka juu mita makumi tano ao zaidi juu ya daraja lake la kawaida.”

Tetemeko la inchi lilifanyika kwa sikukuu, wakati makanisa na nyumba za watawa zilijaa na watu, wachache sana tu waliokoka.” “Hofu ya watu ilikuwa ya kupita kiasi kwa kuieleza. Hakuna mtu aliyelia; hapakuwa na machozi mbele ya msiba kama huo. Wakakim-

bia huko na huko, wakipayuka payuka na hofu na mshangao, wakipiga nyuso zao na vifua, kulia, ‘ Mesericordia! Ni mwisho wa dunia?’ Wamama wakasahau watoto wao, na kukimbia njiani pamoja na sanamu za misalaba. Kwa bahati mbaya, wengi wakakimbilia kwa makanisa kutafuta kimbilio; lakini sacramenti iliwekwa kwa bure; kwa bure viumbe maskini walikumbatia mazabahu; masanamu, mapadri, na watu wakazikwa katika uharibifu moja mbaya wa wote pamoja.”

## Kutiwa giza kwa jua na Mwezi

Miaka makumi mbili na tano baadaye ishara ingine iliotajwa katika unabii ikaonekana -Kutiwa giza kwa jua na mwezi. Wakati wa kutimilika kwake kulionyeshwa kabisa katika mazungumzo ya Mwokozi na wanafunzi wake juu ya mlima wa Mizeituni. “Katika
[144] siku zile nbaada ya mateso yale, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa nuru yake.” Marko 13:24. Siku 1260, ao miaka, zilimalizika katika mwaka 1798, robo ya karne mbele, mateso yalikuwa karibu kuisha kabisa. Kufuata mateso haya, jua likatiwa giza. Kwa tarehe 19 mai 1780, unabii huu ukatimilika.

Shahidi aliyejionea kwa macho katika Massachusetts akaeleza jambo hili kama ifuatavyo: “Wingu nzito sana likatawanyika juu ya mbingu nzima isipokuwa ukingo mwembamba juu ya upeo wa macho, na ilikuwa giza kama inavyokuwa kwa kawaida saa tisa kwa majira ya baridi jioni...

“Woga, mashaka, na hofu polepole vikajaa mioyoni mwa watu. Wanawake wakasimama mlangoni, kutazama juu ya kipande cha inchi ya giza; watu wakarudi kutoka kazini mwao katika mashamba; sermala akaacha vyombo vyake, mhunzi kuacha kiwanda chake, mchuuzi kuacha meza yake. Vyuo vikafungwa, na kwa kutetemeka watoto wakakimbilia kwao. Wasafiri wakaenda kutafuta kimbilio karibu sana ya nyumba ya mashamba. “Ni kitu gani kita kuja?” Swali hili lilikuwa katika midomo yote na ndani ya moyo. Ilionekana kwamba zoruba kali ilitaka kupita inchini, ao siku ya maangamizi ya vitu vyote.

“Mishumaa ikatumiwa, mioto ya nyumbani ikaangaza kwa mwangaza mwingi kama usiku wa wakati wa baridi, bila mwezi... Kuku wakatoka na kwenda kwa vituo vyao na kwenda kulala,

mifugo ikakusanyika kwa fito za malisho na kulala, vyura vikalia, ndege wakaimba nyimbo zao za jioni, na popo wakaruka. Lakini watu walijua kwamba usiku ulikuwa haujafika bado...

“Makutano yakaja pamoja kwa mahali ... pengi. Maneno kwa hotuba zisizo za kawaida kwanza zilikuwa zile zisizogeuka za kuonyesha kwamba giza ililingana na unabii wa Maandiko... Giza ilikuwa nyingi zaidi kwa upesi baada ya saa tano.”

“Kwa sehemu nyingi za inchi ilikuwa kubwa sana katika nyakati za mchana, ambaye watu hawakuweza kutaja saa wala kwa saa ndogo ao kubwa, wala kula chakula, ao kufanya kazi zao za nyumbani, bila nuru ya mishumaa.”

## Mwezi kama Damu

“Giza ya usiku haikukosa kuwa ya ajabu na ya kutisha kama ile ya mchana; ingawa mwezi ulikuwa karibu kuwa mzima, hakuna kitu kilikuwa cha kutambulikana ila tu kwa msaada wa nuru isiyokuwa ya asili, ambayo, kama ikionekana kwa nyumba za jirani na mahali pengine kwa mbali ilionekana kama katika ile giza ya Misri am- [145]
bayo ilionekana karibu kama isiyopenyeka kwa miale.” “Kama kila kitu chenye kung’aa katika ulimwengu kilifunikwa katika giza isiyopenyeka, ao kingeondolewa, giza haingalikuwa kamili kabisa.” Baada ya usiku wa manane giza ikatoweka, na mwezi, wakati ulionekana mara ya kwanza, ulikuwa na rangi ya damu.

Tarehe 19 ya Mai 1780, inakuwa katika historia kama “Siku ya Giza.” Tangu wakati wa Musa hakuna giza ya namna ile nzito, kubwa, na yakuendelea iliyoandikwa. Maelezo yaliyotolewa kwa washuhuda waliojionea ni jibu la maneno yaliyoandikwa na Yoeli miaka 2500 mbele: “Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu mbele ya kutimia kwake ile siku kubwa ya Bwana yenye kuogopesha.” Yoeli 2:31.

“Wakati maneno haya yanapoanza kuja,” akasema Kristo, “tazameni juu, munyanyue vichwa vyenu kwa sababu ukombozi wenu umekaribia.” Alitolea wafuasi wake mfano wa mti uliochipuka wakati ya mwaka ya kukua ao kuota kwa mimea: “Wakati inapochipuka, munaona na kutambua ninyi wenyewe ya kwamba mavuno yamekwisha kuwa karibu. Vile nanyi, wakati munapoona maneno

haya yanapotokea jueni ya kwamba ufalme wa Mungu ni karibu." Luka 21:28, 30, 31.

Lakini katika kanisa upendo kwa ajili ya Kristo na imani katika kuja kwake vilipoa. Waliojidai kuwa watu wa Mungu walipofushwa kwa mafundisho ya Mwokozi juu ya ishara za kuonekana kwake. Mafundisho ya kuja kwa mara ya pili yalizarauliwa, hata ikiwa kwa, eneo kubwa, haikujaliwa na ikasahauliwa, hasa zaidi kule Amerika. Tamaa ya mali, kupigania sifa na uwezo, vikaongoza watu kuweka mbali kwa wakati ujao siku ile kubwa ambapo mambo yote ya sasa yatapaswa kupita.

Mwokozi alitabiri hali ya kukufuru ilipashwa kuwako mbele ya kuja kwake kwa mara ya pili. Kwa wale wanaoishi kwa wakati huu, onyo la Kristo ni: "Mujiangalie, mioyo yenu isipate kulemewa na ulafi na ulevi, na masumbuko ya maisha haya, siku ile isije kwenu gafula kama mutego." "Lakini tazameni kila wakati, mukiomba mupate nguvu ya kukimbia maneno haya yote yatakayokuwa, na kusimama mbele ya Mwana wa watu." Luka 21:34, 36.

Ilikuwa jambo la maana sana kwamba watu waamshwe kwa kujitayarisha kwa ajili ya mambo makubwa yanayo husiana na kufungwa kwa rehema. ''Siku ya Bwana ni kubwa na ya kuogopesha, nani anayeweza kuivumilia?" Nani atakayesimama wakati atakapoonekana yeye anayekuwa na "macho safi zaidi hata asiweze
[146] kutazama mabaya," na hawezi "kutazama ukaidi"? "Nami nitaazibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake, na wenye zambi kwa sababu ya uovu wao, nami nitakomesha kiburi cha wenye majivuno; nami nitaangusha chini majivuno ya wenye ukali." "Wala feza zao wala zahabu zao hazitaweza kuwaponyesha;" "Na utajiri wao utakuwa mateka, na nyumba zao ukiwa." Yoeli 2:11; Habakuki 1:13; Isaya 13:11; Zefania 1:18, 13.

### Mwito kwa Kuamka

Kwa maoni ya siku ile kubwa Neno la Mungu linaita watu wake kutafuta uso wake katika toba:

"Siku ya Bwana inakuja, kwani imekaribia." "Takaseni kufunga chakula, iteni kusanyiko la dini; kusanyeni watu, takaseni makutano, kusanyeni wazee, kusanyeni watoto: ... Makuhani, watumishi wa Bwana, lia katikati ya baraza na mazabahu." "Geukeni kwangu na

moyo wenu wote, na pamoja na kufunga chakula, na kutoa machozi na kuomboleza; na pasueni moyo wenu, wala si mavazi yenu, geukeni kwa Bwana, Mungu wenu; kwa kuwa ni mwenye neema na, anayejaa huruma, si mwepesi kwa kukasirika, na mwenye rehema nyingi." Yoeli 2:1, 15-17, 12,13.

Kwa kutayarisha watu kusimama kwa siku ya Mungu, kazi kubwa ya matengenezo ilipashwa kutimilika. Katika huruma zake alikuwa karibu kutuma mjumbe kwa kuamsha waliojidai kuwa watu wake na kuwaongoza kujitayarisha kwa kuja kwa Bwana.

Onyo hili linaonyeshwa katika Ufunuo 14. Hapa kunakuwa na namna tatu ya ujumbe unaoonyeshwa kama unatangazwa na viumbe vya mbinguni na mara moja ukafuatwa na kuja kwa Mwana wa mtu kwa kuvuna "mavuno ya dunia." Nabii aliona malaika akiruka "katikati ya mbingu, mwenye Habari Njema ya milele, awahubiri wale wanaokaa juu ya dunia, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kubwa: Ogopeni Mungu, na kumutukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Mukamwabudu yeye aliyezifanya mbingu na dunia na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:6. 7.

Ujumbe huu ni sehemu ya "Habari Njema ya milele." Kazi ya kuhubiri ilipewa wala kuaminishwa kwa watu. Malaika watakatifu huongoza, lakini tangazo la sasa la habari njema linafanywa na watumishi wa Kristo duniani. Watu waaminifu, watiifu kwa maongozi ya Roho wa Mungu na mafundisho ya Neno lake, walipashwa kutangaza onyo hili. Walikuwa wakitafuta maarifa ya Mungu, kuihesabu "vema kuliko biashara ya feza, na faida yake ni nyororo [147]
kuliko zahabu safi." "Siri ya Bwana ni pamoja nao wanaomwogopa; Naye atawaonyesha agano lake." Mezali 3:14; Zaburi 25:14.

## Ujumbe Uliotolewa na Watu Wanyenyekevu

Kama wanafunzi wa elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini walikuwa walinzi waaminifu, wenye bidii na wenye kuomba kuchunguza Maandiko, wangaliweza kujua wakati. Mambo ya unabii yangeweza kuwafungulia matokeo yaliyopashwa kuwa. Lakini ujumbe ulitolewa na watu wanyenyekevu. Wale waliozarau kutafuta nuru wakati inapokuwa karibu nao waliachwa gizani. Lakini Mwokozi anatangaza, "Yeye anayenifuata hatatembea katika giza,

lakini atakuwa na nuru ya uzima." Yoane 8:12. Kwa roho ile nyota fulani ya mwangaza wa mbinguni itatumwa kwake kwa kumwongoza katika ukweli wote.

Kwa wakati wa kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo wakuhani na waandishi wa mji Mtakatifu wangaliweza kutambua "ishara za wakati" na kutangaza kuja kwa yule Aliyeahidiwa. Mika aliandika mahali pale pa kuzaliwa, Danieli, wakati wa kuja kwake. Mika 5:2; Danieli 9:25. Waongozi wa Wayahudi walikuwa bila sababu kama hawakujua. Ujinga wao ulikuwa matokeo ya zarau lenye zambi.

Kwa faida kubwa sana waongozi wa Israeli wangalipashwa kujifunza pahali, wakati, hali ya mambo, ya tukio kubwa sana katika historia ya dunia--kuja kwa Mwana wa Mungu. Watu walipashwa kukesha ili wapate kumkaribisha Mkombozi wa ulimwengu. Lakini kule Betelehemu wasafiri wawili waliochoka kutoka Nazareti wakapitia njia nyembamba kwa mwisho wa upande wa mashariki ya mji, kutafuta kimbilio sababu ulikuwa usiku bila kuona mahali pa kupangia. Hakuna milango iliyofunguliwa kwa kuwapokea. Katika kibanda kibovu kilichotayarishwa kwa ajili ya mifugo, mwishowe wakapata kimbilio, na hapo Mwokozi wa ulimwengu akazaliwa.

Malaika wakaagizwa kuchukua habari ya furaha kwa wale waliojitayarisha kuipokea na walioweza kwa furaha kuijulisha. Kristo alijishusha hata akajivika hali ya binadamu, kuchukua taabu isiyo na mwisho namna alipashwa kutoa roho yake sadaka kwa ajili ya zambi. Lakini malaika walitamani kwamba hata katika kujishusha kwake Mwana wa Aliyejuu angeweza kuonekana mbele ya watu na heshima na utukufu unaofaa tabia yake. Je, wakuu wa inchi hawangekusanyika kwa mji mkuu wa Israeli kusalimia kuja kwake? Je, malaika hawangemwonyesha kwa makutano yaliyomungojea?

[148] Malaika mmoja alizuru ulimwengu kuona wanani waliojitayarisha kumkaribisha Yesu. Lakini hakusikia sauti ya sifa kwamba mda wa kuja kwa Masiya umefika. Akakawia juu ya mji uliochaguliwa na hekalu ikasimama kwa mda mahali kuwako kwa Mungu kulionekana kwa miaka nyingi, lakini hata pale palikuwa na kutojali kwa namna moja. Wakuhani katika sherehe na kiburi walikuwa wakitoa kafara za unajisi. Mafarisayo kwa sauti kuu wakawaambia watu ao wakafanya maombi ya kujisifu kwa pembe za njia. Wafalme, watu wa elimu zote (philosophes), waalimu, wote walikuwa wa-

siokumbuka jambo la ajabu kwamba Mkombozi wa watu alikuwa karibu kuonekana.

Kwa mshangao mjumbe wa mbinguni alikuwa karibu kurudi mbinguni pamoja na habari ya aibu sana, wakati alipovumbua kundi la wachungaji wakilinda makundi yao. Wakatamani sana kuja kwa Mkombozi wa ulimwengu. Hapa palikuwa na kundi la watu waliojitayarisha kumpokea mjumbe wa mbinguni. Kwa gafula utukufu wa mbinguni ukajaa pote katika uwanda, kundi lisilohesabika la wamalaika likafunuliwa; na kana kwamba furaha ilikuwa kubwa kwa ajili ya mjumbe kutoka mbinguni, wingi wa masauti kuimba wimbo wa furaha ambao mataifa yote ya waliookolewa wataimba siku moja: "Utukufu kwa Mungu aliye juu, na salama duniani, katika watu wanaomupendeza." Luka 2:14.

Fundisho la namna gani linakuwa kwa historia ya ajabu hii ya Betelehemu! Namna gani inakemea kutokuamini kwetu, kiburi chetu na hali ya kuwaza tunatosheka nafsini. Namna gani inatuonya kwa kujihazari, ili sisi vile vile tusishindwe kutambua ishara za nyakati na kwa hiyo hatutajua siku ya kuzuriwa kwetu.

Si miongoni mwa wachungaji tu ambamo malaika walipata walinzi kwa ajili ya kuja kwa Masiya. Katika inchi ya wapagani vile vile kulikuwa wale waliomtazamia--watajiri, watu bora wenye akili—wenye elimu zote wa Mashariki. Kutoka kwa Maandiko ya Kiebrania walikuwa wakijifunza habari ya nyota kutokea kwa Yakobo. Kwa mapenzi ya bidii walingojea kuja kwake yeye aliyepashwa kuwa si "Faraja la Israeli" tu, bali "Nuru ya kuangazia Mataifa," na "kuwa wokovu hata mwisho wa dunia." Luka 2:25, 32; Matendo 13:47. Mbingu--ikatuma nyota ikaongoza wageni wa mataifa kwa mahali pa kuzaliwa kwa Mfalme mpya aliyezaliwa.

Ni kwa "wale wanaomungojea" Kwamba Kristo "ataonekana mara ya pili, si tena kwa zambi, lakini kuokoa wale wanaomungojea kwa wokovu." Waebrania 9:28. Kama habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi, ujumbe wa kuja kwa mara ya pili haukutolewa kwa waongozi wa dini ya watu. Walikataa nuru kutoka mbinguni; kwa [149]
hiyo hawakuwa katika hesabu ya wale waliotajwa na mtume Paulo: "Lakini ninyi ndugu, si katika giza, hata siku ile iwapate ninyi kama mwizi: sababu ninyi wote ni wana wa nuru, na wana wa mchana: sisi hatuko wana wa usiku wala wa giza." 1 Watesalonika 5:4, 5.

Walinzi juu ya kuta za Sayuni walipashwa kuwa wa kwanza kupata habari ya kuja kwa Mwokozi, wa kwanza kutangaza ukaribu wa kuja kwake. Lakini walikuwa kwa raha, wakati watu walikuwa katika usingizi wa zambi zao. Yesu aliona kanisa lake, kama mti wa mtini usiozaa, umefunikwa na majani ya fahari, lakini pasipo kuwa na matunda ya damani. Roho ya unyenyekevu wa kweli, uvumilivu, na imani ilikosekana. Hapo kulikuwa kiburi, unafiki, uchoyo, ugandamizi. Kanisa laukufuru lilifunga macho yao kwa alama za nyakati. Wakatoka kwa Mungu na wakajitenga wao wenyewe kwa upendo wake. Namna walivyokataa na mapashwa yaliyowekwa, ahadi zake hazikutimizwa kwao.

Wengi waliojidai kuwa wafuasi wa Kristo wakakataa kupokea nuru kutoka mbinguni. Kama Wayahudi wa zamani, hawakujua wakati wa kuzuriwa kwao. Bwana akapita pembeni yao na akafunua ukweli wake kwa wale ambao, kama wachungaji wa Betelehemu na Waakili wa Mashariki, walipewa usikizi kwa nuru yote walioyopokea.

# 18 /NURU MPYA KATIKA DUNIA MPYA [150]

Mkulima mwaminifu, wa haki, ambaye alitamani kujua ukweli, alikuwa mtu aliyechaguliwa na Mungu kuongoza katika kutangaza kuja kwa Kristo mara ya pili. Kama watengenezaji wengi wengine, William Miller alipigana na umaskini na akajifunza fundisho la kujikana.

Hata katika utoto alitoa ushuhuda wa uwezo wa akili zaidi kuliko ule wa kawaida. Kwa kukomaa kuwa mtu mzima, akili yake ilikuwa ya utendaji na ikaendelea sana, na alikuwa na kiu cha bidii kwa maarifa. Upendo wake wa kujifunza na tabia ya mafikara ya uangalifu kuambatana na ujuzi vikamfanya kuwa mtu wa hukumu na maono ya uchunguzi. Alikuwa na tabia ya matendo mema isiyolaumiwa na sifa nzuri. Alifanya kazi za serkali na za kiaskari pamoja na sifa njema. Utajiri na heshima vilionekana kufunguliwa sana kwake.

Katika utoto alikuwa mtu wa mawazo ya dini. Mawazo ya mtu mkubwa, kwa hivi akajiingiza katika jamii ya watu wanaokuwa na imani katika Mungu (deistes), mvuto wake ulikuwa wa nguvu kwa jambo kwamba walikuwa karibu raia wema,wapole na wakarimu. Kuishi kati ya vyama vya Kikristo, tabia zao zilikuwa za kadiri zilizofanywa na wale waliowazunguuka. Kwa ajili ya wema ambao uliwapatia heshima, wakawapashwa kushukuru Biblia, na zawadi hizi nzuri zikawaongoza kwa kutumia mvuto juu ya Neno la Mungu. Miller akaongozwa kuitika nia zao.

Mafasiri ya kisasa ya Maandiko yalionyesha magumu ambayo ilionekana kwake kwamba kubwa sana; lakini imani mpya yake, kwa kuweka Biblia kando, haikumsaidia kitu, na akawa mbali ya kutoshelewa. Lakini wakati Miller alipokuwa na miaka makumi tatu na ine, Roho Mtakatifu akamfahamisha moyo wake kwa hali aliyokuwamo kama mwenye zambi. Hakuona tumaini la furaha

ngambo ya pili ya kaburi. Wakati ujao ulikuwa giza na huzuni. Kwa kutazama mawazo yake ya moyo kwa wakati huu, akasema: [1]

“Mbingu zilikuwa kama shaba juu ya kichwa changu, na dunia kama chuma chini ya miguu yangu... Nilipofikiri zaidi hukumu
[151] zangu zikatawanyika. Nikajaribu kukataza mawazo yangu, lakini mawazo yangu haikuweza kutawalika. Nikawa maskini kwa kweli, lakini bila kufahamu sababu. Nikanungunika na kulalamika, lakini sikujua juu ya nani. Nikajua kwamba kosa lilikuwako, lakini sikujua namna gani ao mahali gani kupata haki.”

## Miller Anapata Rafiki

“Kwa gafula,” akasema, “tabia la Mwokozi likaonekana kabisa kwa akili yangu. Inaonekana kwangu kufahamu kwamba kuna Kiumbe kizuri sana na chenye huruma kwa kufanya mwenyewe upatanisho wa makosa yetu, na kutuokoa kwa kuteseka kwa azabu ya zambi... Lakini swali likatokea, Namna gani itawezekana kuhakikisha kwamba kiumbe cha namna hii kinakuwako? Inje ya Biblia, niliona kwamba sikuweza kupata ushahidi wa kuwako kwa Mwokozi wa namna ile, ao hata hali ya wakati ujao...

“Niliona kwamba Biblia ilionyesha tu Mwokozi wa namna ninayehitaji: na nilifazaika kuona namna gani kitabu kisichoongozwa na Mungu kilipashwa kukuza kanuni zilizolingana kabisa kabisa kwa matakwa ya ulimwengu ulioanguka. Nikalazimishwa kukubali kwamba Maandiko yanapashwa kuwa ufunuo kutoka kwa Mungu. Yakawa mapenzi yangu; na katika Yesu napata rafiki. Mwokozi akawa kwangu mkuu kuliko miongoni mwa wakuu elfu kumi; na Maandiko, ambayo mbele yalikuwa giza na kinyume, sasa yakawa taa kwa miguu yangu... Niliona Bwana Mungu kuwa Mwamba katikati ya bahari ya maisha. Biblia sasa inakuwa fundisho langu kuu, na ninaweza kusema kweli, niliitafuta kwa furaha kubwa... Nilishangaa sababu gani sikuona uzuri wake na utukufu mbele, na nikashangaa namna gani ningaliweza kuikataa... Nikapoteza onyo yote ya kusoma vitabu vingine, nikatumia moyo wangu kwa kupata hekima kutoka kwa Mungu.”

[1] Deism : ni imani kwamba Mungu anakuwako na aliumba ulimwengu, lakini baadaye hakutumia uongozi juu yake ao kujali maisha ya watu; imani kwamba akili inatosha kwa maarifa ya kweli, kwa hiyo wakakataa ufunuo. Webster’s New World Dictionary.

Miller akaungama wazi wazi imani yake. Lakini rafiki zake wasiokuwa waaminifu wakaendeleya mbele na mabishano, hayo yote ambayo yalishurutisha mwenyewe kupinga Maandiko. Akafikiri kwamba kama Biblia ni ufunuo wa Mungu, Kitabu hicho kinapaswa kujieleza chenyewe. Akakusudia kujifunza Maandiko na kupata kama kila mabishano ya wazi yapate kupatanishwa.

Akaacha maelezo yo yote, akalinganisha maandiko kwa maandiko kwa usaada wa kumbukumbu ya upande na upatanifu (concordance). Kuanzia kwa Mwanzo, kusoma shauri kwa shauri, alipoona kitu cho chote cha giza ilikuwa desturi yake kukilinganisha pamoja na maneno yote yanayoweza kuwa na uhusiano na fundisho [152] lenyewe. Kila neno likaruhusiwa kuwa na tegemeo lake juu ya maneno yenyewe. Kwa hiyo wakati wo wote alipokutana maneno magumu kwa kufahamu alipata maelezo katika sehemu ingine ya Maandiko. Akajifunza kwa maombi ya juhudi kwa ajili ya nuru ya kiMungu maneno ya mwandishi wa zaburi: "kufunua kwa maneno yako kunaleta nuru; Kunamupa mujinga ufahamu." Zaburi 119:130.

Kwa usikizi mwingi akajifunza kitabu cha Danieli na Ufunuo na akaona ya kwamba mifano ya unabii inaweza kufahamika. Aliona ya kwamba mifano yote mbalimbali, mezali, vifani, kama hayakuelezwa kwa maneno yaliyotangulia haya, hupata penginepo maelezo yake kwa muunganiko wake mwenyewe ao kuelezwa kwa maandiko mengine na kufahamika kwa kweli. Kiungo kwa kiungo cha mnyororo wa kweli na kuwa ni shani ya bidii yake. Hatua kwa hatua akafuatisha mistari ya unabii. Malaika wa mbinguni walikuwa wakiongoza akili yake.

Akatoshelewa kwamba maoni ya watu wengi ya miaka elfu (millennium) mbele ya mwisho wa dunia hayakukubaliwa na Neno la Mungu. Mafundisho haya,ya kuonyesha miaka elfu ya amani mbele ya kuja kwa Bwana, ni kinyume cha mafundisho ya Kristo na mitume wake, waliotangaza kwamba ngano na magugu yanapashwa kukuwa pamoja hata wakati wa mavuno, mwisho wa dunia, na kwamba "watu wabaya na wadanganyifu wataendelea na kuzidi kuwa waovu." 2 Timoteo 3:13.

## Kuja kwa Kristo mwenyewe

Mafundisho juu ya kugeuka kwa ulimwengu na utawala wa Kristo wa kiroho hayakushikwa na kanisa la mitume. Kwa kawaida hayakukubaliwa na Wakristo hata karibu ya mwanzo wa karne ya kumi na mnane. Ilifundisha watu kutazamia mbali kwa wakati ujao kuja kwa Bwana na kuwakataza kwangalia ishara za kurudi kwake. Iliongoza watu kutojali kujitayarisha kwa kumlaki Bwana wao.

Miller akaona kuja kwa Kristo halisi kulikofundishwa wazi katika Maandiko. "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, na sauti kubwa, na sauti ya malaika mkubwa, na pamoja na baragumu ya Mungu." "Nao wataona Mwana wa watu akija katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa." "Kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaonekana hata mangaribi; ni hivi kuja kwa Mwana wa watu kutakavyokuwa." "Mwana wa watu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika
[153] yote pamoja naye." "Naye atatuma malaika zake na sauti kubwa ya baragumu, nao watakusanya wachaguliwa wake." 1 Watesalonika 4:16, 17; Matayo 24:30, 27; 25:31; 24:31.

Kwa kuja kwake wafu wenye haki watafufuka na wenye haki waliohai watabadilika. "Sisi sote hatutalala, lakini sisi sote tutabadilika, kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho, kwa baragumu ya mwisho: sababu baragumu italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na kuoza, na tutabadilika. Maana sharti ule mwili wenye kuoza uvae kutokuoza, na huu wa mauti uvae kutokufa." "Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliobaki, tutanyanyuliwa pamoja nao katika mawingu, kukutana na Bwana katika hewa, na hivi tutakuwa pamoja na Bwana milele." 1 Wakorinto 15:51-53; 1 Watesalonika 4:16, 17.

Mtu katika hali ya sasa ni wa kufa, wakuoza; lakini ufalme wa Mungu utakuwa wakutokuoza. Kwa hivyo mtu kwa hali yake ya sasa hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu. Wakati Yesu atakuja, atatoa kutokufa kwa watu wake, na kuwaita kuriti ufalme ambao hawakuuriti hata sasa.

## Maandiko matakatifu na Taratibu ya Miaka

Haya pamoja na maandiko mengine kwa wazi yakamshuhudia Miller kwamba utawala wa amani wa watu wote na kuimarishwa kwa ufalme wa Mungu duniani ungekuwa baada ya kuja kwa mara ya pili. Tena, hali ya ulimwengu ililingana na maelezo ya unabii wa siku za mwisho. Alilazimishwa kwa mwisho kwamba mda uliogawanywa kwa dunia katika hali yake ya sasa ulikuwa karibu kuisha.

Namna ingine ya ushuhuda ambao kwa nguvu ulichoma moyo wangu." Akasema, "ulikuwa utaratibu wa Maandiko... Niliona kwamba mambo yaliyotabiriwa, yalitimilika katika wakati uliopita, mara kwa mara yalitukia karibu ya wakati uliotolewa... Matokeo ... yanapokuwa tu mambo ya unabii, ... yalitimia katika upatano wa yale yaliotabiriwa."

Wakati alipoona nyakati za taratibu ya miaka ambayo ilifikia kwa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo, hangaliweza lakini kuzitazama kama "nyakati zilizoonyeshwa mbele", ambazo Mungu alifunulia watumishi wake. "Vitu vile vilivyofunuliwa ni vyetu, na vya wana wetu milele." Bwana alitangaza kwamba "hatafanya lolote, lakini anafunulia watumishi wake manabii siri yake." Torati 29:29; Amosi 3:7. Wanafunzi wa Neno la Mungu wanaweza kutazamia kwa hakika kuona mambo makubwa kuliko katika historia ya [154] wanadamu iliyoonyeshwa kwa wazi katika Maandiko.

"Nilisadikishwa kabisa," akasema Miller, "kwamba kila andiko lililopewa kwa maongozi ya Mungu linafaa kwa mafundisho; kwamba liliandikwa; wakati watu watakatifu walikuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu, yameandikwa kwa majifunzo yetu, kwamba kwa subira na faraja ya maandiko tuwe na tumaini ... kwa hiyo mimi niliona kwamba katika kujitahidi kufahamu kile Mungu alikuwa nacho katika huruma zake kinachoonekana kufaa kwa kufunuliwa kwetu, sikuwa na haki kupita inje ya nyakati za unabii."

Unabii ambao ulionekana wazi zaidi kwa kufunua wakati wa kuja kwa mara ya pili ulikuwa Danieli 8:14: "Hata mangaribi na asubui elfu mbili mia tatu; halafu Pahali patakatifu patasafishwa." Kufanya Maandiko mfasiri wake mwenyewe, Miller akajifunza kwamba siku moja katika unabii ni mwaka moja. (Tazama Nyongezo.) Aliona kwamba siku 2300 za unabii, ao miaka kabisa,

ingefikia mbali sana ya mwisho wa mugawo wa Wayahudi, kwa hiyo haikuweza kutaja juu ya mahali patakatifu pa mugawo ule.

Miller akakubali maelezo ya kawaida kwamba katika miaka ya Kikristo ulimwengu ni "mahali patakatifu," na kwa hiyo akafahamu kwamba kusafishwa kwa mahali patakatifu kulikotabiriwa katika Danieli 8:14 ilikuwa mfano wa kutakaswa kwa dunia na moto kwa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo. Kama mahali kamili pa kuanzia pangeweza kupatikana kwa ajili ya siku 2300, akamaliza kwamba wakati wa kuja kwa mara ya pili ungeweza kufunuliwa.

## Kuvumbua Oroza ya Wakati wa Unabii

Miller akaendelea na uchunguzi wa mambo ya unabii, wakati wa usiku wote pamoja na wakati wa mchana zikatolewa kwa majifunzo ambayo sasa yalionekana kuwa ya maana kubwa. Katika sura yanane ya Danieli hakuweza kupata dalili kwa mahali halisi pa kuanzia siku 2300; malaika Gabrieli, ingawa aliagizwa kwa kufahamisha Danieli njozi, akamupa tu sehemu ya maelezo. Kwa sababu mateso ya kutisha ilifaa kuanguka juu ya kanisa ilikuwa haikufunuliwa kwa njozi ya nabii, hakuweza kuvumilia tena. Danieli "akazimia, na kugonjwa siku chache." "Nikashangaa kwa maono," akasema, "lakini hakuna aliyeyafahamu." Danieli 8:27.

Lakini Mungu akaagiza mjumbe wake, "Fahamisha mtu huyu maono." Kwa kutii, malaika akarudi kwa Danieli, kusema: "Nimekuja sasa ili nikupe akili upate kufahamu ... kwa sababu hii
[155] elewa maneno haya na kufahamu maono." Jambo moja la maana katika sura ya 8 liliachwa bila kufasiriwa, yaani, siku 2300; kwa hiyo malaika, kwa kuendelea na maelezo yake, akaeleza sana juu ya wakati:

"Mda wa majuma makumi saba umeamriwa juu ya watu wako na juu ya mji wako mtakatifu... Ujue basi na kufahamu ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kujenga Yerusalema hata mupakaliwa, masiya mkubwa, yatakuwa majuma saba na majuma makumi sita na mawili; njia kuu itajengwa tena, na ukuta, hata katika nyakati za taabu. Na nyuma ya majuma makumi sita na majuma mawili massiah atakataliwa mbali, lakini ni kwake mwenyewe: ... Naye atafanya agano la nguvu pamoja na wengi kwa juma moja:

na kwa nusu ya juma atakomesha kafara na toleo." Danieli 8:16; 9:22,23, 24-27.

Malaika alitumwa kwa Danieli kwa kueleza jambo aliloshindwa kufahamu "Hata mangaribi na asubui ya siku elfu mbili mia tatu; ndipo Pahali patakatifu patasafishwa." Maneno ya kwanza ya malaika ni haya, "Mda wa majuma makumi saba umeamriwa juu ya watu wako na juu ya mji wako." Neno umeamriwa kwa halisi maana yake "atakatiliwa mbali." Majuma makumi saba, miaka 490, ilipaswa kukatiliwa mbali kuwekwa kando kwa ajili ya Wayahudi.

### Mda wa Nyakati Mbili Zilianza Pamoja

Lakini kukatiliwa mbali kwa nini? Hivi siku 2300 zilikuwa ni mda tu wa wakati uliotajwa katika sura 8, majuma makumi saba yanapaswa basi kuwa sehemu ya siku 2300. Nyakati mbili hizo zinapaswa kuanza pamoja, majuma makumi saba tangu "kuwekwa amri" ya kutengeneza na kujenga Yerusalema. Kama tarehe ya amri hii ingeweza kupatikana, ndiyo ingekuwa mwanzo wa uhakika wa siku 2300.

Katika sura ya saba ya Ezra amri inapatikana, ilitolewa na Artasasta, mfalme wa Persia, katika mwaka 457 B.C. Wafalme watatu katika kuanzisha na kutimiza amri, wakaifanya kwa utimilivu uliotakiwa na unabii kwa kutia alama ya mwanzo wa mwaka 2300. Kukamata miaka 457 B.C., wakati amri ilipotimia, kama tarehe ya "amri", kila hatuwa ya majuma makumi saba ikaonekana katika kutimilika. (Tazama Nyongezo.)

Kwa kuendelea kwa kutengeneza na kujenga Yerusalema hata Masiya Mfalme itakuwa majuma saba, na majuma makumi sita na mawili"majuma makumi sita na kenda, ao miaka 483. Amri ya Artasasta ikatendeka katika wakati wa masika wa mwaka 457 B.C. Kutoka tarehe hii, miaka 483 ikafikia kwa wakati wa masika wa [156]
mwaka 27 A.D. Kwa wakati ule unabii huu ukatimilika. Katika wakati wa masika wa mwaka 27 A.D.Kristo akabatizwa na Yoane na akapakwa mafuta ya Roho. Baada ya ubatizo wake akaenda Galilaya, "akihubiri Habari njema ya ufalme wa Mungu akisema: Wakati umetimia." Marko 1:14, 15.

## Habari Njema Imetolewa kwa Ulimwenguni

"Naye ataimarisha na wengi muda wa juma moja" mwisho wa miaka saba ya mda uliogawanywa kwa Wayahudi. Kwa wakati huu, kutoka kwa mwaka 27 A.D. hata A.D. 34, Kristo na wanafunzi wake wakaeneza mwaliko wa Habari Njema zaidi kwa Wayahudi. Agizo la Mwokozi lilikuwa: "Musiende katika njia ya Mataifa, wala musiingie mji wo wote wa Wasamaria; lakini zaidi kwendeni kwa kondoo wapotevu za nyumba ya Israeli." Matayo 10:5, 6.

"Na kwa nusu ya juma atakomesha sadaka na toleo." Katika mwaka A.D. 31,miaka tatu na nusu baada ya ubatizo wake, Bwana wetu alisulibishwa. Kwa kafara kubwa iliyotolewa kule Golgota, mfano ukakutana na kilicho asili ya mfano. Kafara zote na sadaka za kawaida za ibada zilipashwa kukomeshwa.

Miaka 490 iliyogawanyiwa kwa Wayahudi ikamalizika katika mwaka A.D. 34. Kwa wakati ule, kwa njia ya tendo la Baraza (Sanhedrin) la Wayahudi, taifa likatia mhuri wa kukataa injili kwa kifo cha Stefano na mateso ya wafuasi wa Kristo. Ndipo ujumbe wa wokovu ukatolewa ulimwenguni. Wanafunzi wakalazimishwa na mateso kukimbia toka Yerusalema, "wakakwenda pahali po pote wakihubiri neno." Matendo 8:4.

Kwa hiyo maelezo yote ya mambo ya unabii yakatimia kwa ajabu sana. Mwanzo wa majuma makumi saba ukaimarishwa bila swali lo lote kwa mwaka 457 B.C., na kumalizika kwayo katika mwaka A.D. 34. Majuma makumi saba (siku 490) kukatwa kutoka kwa 2300, hapo kulikuwa siku 1810 zilizobakia. Baada ya mwisho wa siku 490, siku 1810 zilipashwa kutimia. Kutoka A.D. 34, miaka 1810 ikafika kwa mwaka 1844. Kwa hiyo siku 2300 za Danieli 8:14 zikamalizika katika 1844. Kwa kumalizika kwa mda kubwa huu wa unabii, "Pahali patakatifu patasafishwa"--ambaye wafafanisi wengi zaidi wanachanganya na kuja kwa mara ya pili--kukaimarishwa. (Tazama chart, p. 220.)

## [157] Mwisho wa Kuhofisha

Kwa mwanzo Miller hakuwa na matumaini hata kidogo ya kufikia mwisho ambao sasa alifikia. Yeye mwenyewe aliweza kwa

shida sana kusadiki matokeo ya uchunguzi wake. Lakini ushuhuda wa Maandiko ulikuwa wazi kabisa kwa kuwa pembeni.

Katika mwaka 1818 akafikia hakika maalum kwamba katika miaka makumi mawili na tano karibu Kristo angeonekana kwa ajili ya ukombozi wa watu wake. "Si hitaji kusema," akasema Miller, "juu ya furaha ambayo inajaa moyoni mwangu kuhusu maoni ya matazamio ya kupendeza sana, wala ya uvumilivu wa bidii wa roho yangu kwa ajili ya ushirika katika furaha ya waliokombolewa... Aa, kweli ya mwanga na utukufu ya namna gani iliyotokea! ...

"Swali likaja nyumbani kwangu kwa nguvu nyingi kuhusu habari ya kazi yangu kwa ulimwengu, katika maoni ya ushuhuda ambao ulihusu roho yangu mwenyewe." Hakuweza lakini kufikiri kwamba ilikuwa wajibu wake kutoa kwa wengine nuru ambayo aliyoipata. Alitazamia upinzani kwa wasiomcha Mungu, lakini alikuwa na tumaini kwamba Wakristo wote watafurahi katika tumaini la kukutana na Mwokozi. Alisita kufundisha juu ya wokovu wa utukufu, upesi' kutimilika, isiwe angekuwa katika kosa na kukosesha wengine. Kwa hiyo akaongozwa kukumbusha na kufikiri kwa uangalifu magumu yote ambayo ilionekana yenyewe kwa roho yake. Miaka tano ya kujifunza ikamletea kusadikishwa kwa usahihi wa musimamo wake.

### "Wende na Ulihubiri kwa Uiimwengu"

"Wakati nilikuwa katika kazi zangu," akasema, "nikasikia sauti kukariri katika masikio yangu, 'Wende na uambie ulimwengu hatari yao.' Maneno haya yalikuwa yakitokea daima kwangu: 'Wakati ninapomwambia mwovu; kama mwovu Ee mwovu, hakika utakufa, wala husemi kuonya mwovu aache njia yake; mwovu yule atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako.' Nikaona kama mwovu angeweza kuonywa, wengi miongoni mwao wangalitubu; na kama hawakuonywa, damu yao ingeweza kutakwa mkononi mwangu." Maneno yalikuwa yakimrudia kwa akili yake: "Wende na ulihubiri kwa ulimwenguni; damu yao nitaitaka mkononi mwako." Akangoja mda wa miaka tisa, mzigo ulizidi kulemea kwa roho yake, hata katika mwaka 1831 yeye kwa mara ya kwanza kwa wazi akatoa sababu za imani yake.

Alikuwa sasa na miaka makumi tano, hakuzoea kusema mbele [158]
ya watu wengi, lakini kazi zake zikabarikiwa. Mafundisho yake ya

kwanza yakafuatwa na mwamusho wa dini. Jamaa kumi na tatu isipokuwa tofauti ya watu wawili,zilitubu. Alikuwa akilazimishwa kuhubiri kwa mahali pengine, na karibu pahali pote wenye zambi walikuwa wakigeuka. Wakristo waliamshwa kwa utakaso mkubwa, na watu wenye imani ya kuwako kwa Mungu lakini hawakubali mambo ya dini na makafiri (wasioamini) wakaongozwa kwa maarifa ya ukweli wa Biblia. Mahubiri yake yakaamsha akili ya watu na kuzuia mambo ya anasa ya kidunia yaliyokuwa yakikua na ya kutamanisha maisha.

Katika mahali pengi makanisa ya Kiprotestanti karibu aina zote wakamfungulia kwake, na mialiko mara kwa mara ikaja kutoka kwa wahuduma. Ilikuwa desturi yake ya kutotumika mahali wasipomwalika, lakini kwa upesi akajiona mwenyewe hawezi kutimiza hata kwa nusu ya mialiko iliyokuwa ikimfikia. Wengi wakasadikishwa kwa hakika na ukaribu wa kuja kwa Kristo na mahitaji yao ya kujitayarisha. Katika miji mikubwa mingine, wenye duka ya vileo vikali na wakageuza duka zao kuwa vyumba vya mikutano; nyumba za michezo ya kamari zikavunjwa; makafiri na hata na wapotovu walioachwa wengi wakabadilika. Mikutano ya maombi ikaanzishwa na makanisa mbali-mbali karibu kila saa, wachuuzi wakakusanyika wakati wa jua kali kwa kuomba na kusifu. Hapo hapakuwa na wasiwasi wa kupita kiasi. Kazi yake kama ile ya Watengenezaji wa kwanza ikaamsha zamiri kuliko kuchocheza tamaa tu.

Katika mwaka 1833 Miller akapokea ruhusa ya kuhubiri kwa Kanisa la Baptiste. Hesabu kubwa ya wahuduma wa kanisa lake wakakubali kazi yake; ilikuwa ni kwa ukubali wao wa kawaida ambao akaendelea na kazi zake. Akasafiri na kuhubiri bila kukoma, bila kupokea mali ya kutosha kwa ajili ya gharama ya kusafiri kwa mahali alipoalikwa, hivi kazi yake kwa ajili ya watu wote ilikuwa kodi nzito kwa mali yake.

## "Nyota Zitaanguka"

Katika mwaka 1833 ishara za mwisho zikaonekana zilizoahidiwa na Mwokozi kama dalili ya kuja kwake kwa mara ya pili: "Nyota zitaanguka toka mbinguni." Na Yoane katika Ufunuo akasema, "Na nyota za mbinguni zikaanguka juu ya dunia kama vile mtini unavyotupa matunda mabichi yake, wakati unapotikiswa na upepo

mkubwa.” Matayo 24:29; Ufunuo 6:13. Unabii huu ulipata utimilifu wa kushangaza katika wingi wa vimondo (nyota ipitayo upesi mbinguni) vya Novemba 13, 1833, ni tamasha ya kushangaza [159]
ya nyota ambayo historia hulinda kumbukumbu yake. “Kamwe mvua haikuanguka tena kubwa kuliko vimondo vilivyoanguka juu ya dunia; mashariki, mangaribi, kaskazini na kusini, ilikuwa namna moja. Katika neno moja, mbinguni pote kulionekana katika mwendo... Tangu saa nane hata asubui, mbingu kuwa bila mawingu kabisa na kweupe, mwendo wa daima wa miangaza yenye kungaa ya ajabu ikalindwa mbinguni mwote.”

Ilionekana kwamba nyota zote za mbinguni zilipatana kukutana pahali pa karibu pa opeo, na zilikuwa zikiendelea kurushwa wakati ule ule, kwa upesi wa umeme, kwa pande zote za upeo wa macho; na huku hazikuisha--maelfu kwa upesi katika njia za maelfu, kama kwamba ziliumbwa kwa ajili ya tukio lile.” “Picha halisi zaidi ya mtini kuangusha tini zake zinapopeperushwa na upepo wa nguvu, ndiyo si vyepesi kueleza tukio hili.”

Katika gazeti la biashara la New York la tarehe 14, Novemba 1833, kukatokea nakala kwa ajili ya jambo hili; “Hakuna mtu wa elimu ya elimu zote (philosophe) wala mwalimu aliyetoa habari wala kuandika tukio, ninawaza, kama lile la jana asubui. Nabii miaka elfu moja mia nane iliyopita akaitabiri sawasawa, kama tukiwa kwa hatari ya kufahamu kwamba kuanguka kwa nyota hakika ni kuanguka kwa nyota,... katika maana ya pekee kwamba inawezekana kwa kweli.”

Ndivyo ilivyokuwa onyesho la dalili zile za kuja kwake, kuhusu habari ambazo Yesu aliambia wanafunzi wake: “Wakati munapoona maneno haya yote, mjue ya kuwa yeye ni karibu, hata kwa milango.” Matayo 24:33. Wengi walioshuhudia kuanguka kwa nyota walikutazama kama mjumbe wa hukumu ijayo.

Katika mwaka 1840 utimilizo kubwa mwingine wa unabii ukaamsha usikizi wa mahali pengi. Miaka miwili mbele, Josiah Litch akatangaza habari ya Ufunuo 9, kutabiri kuanguka kwa Ufalme wa Ottoman “Katika A.D. 1840, siku moja katika mwezi wa Agosti.” Siku chache tu mbele ya kutimilika kwake akaandika: “Itamalizika kwa tarehe 11 ya Agosti, 1840, wakati mamlaka ya Ottoman katika Constantinople kuweza kutazamiwa kuvunjika.”

## Maonyo Yalitimilika

Kwa wakati kabisa uliotajwa, Turkey ilikubali ulinzi wa mamlaka za mapatano ya Ulaya na kwa hivyo ikajitia yenyewe chini ya utawala wa mataifa ya Kikristo. Jambo kwa halisi kweli likatimiliza ukashiri. (Tazama Nyongezo.) Watu wengi walisadikishwa na
[160] kanuni za maelezo ya unabii yaliyokubaliwa na Miller na wafuasi wake. Watu wenye elimu na cheo wakajiunga pamoja na Miller katika kuhubiri na kutangaza maonyo yake. Tangu 1840 hata 1844 kazi ikaenea kwa upesi.

William Miller alikuwa na akili za kichwa cha nguvu, na akaongeza kwa haya hekima ya mbinguni kwa kujiunga mwenyewe na Chemchemi ya hekima. Aliamuru heshima po pote, ukamilifu na tabia njema vilitumiwa. Kwa damani unyenyekevu wa Kikristo, alikuwa muangalifu na mpole kwa wote, tayari kusikiliza wengine na kupima mabishano yao. Alijaribu maelezo yote kwa Neno la Mungu, na mawazo yake halisi na maarifa ya Maandiko vikamwezesha kukanusha makosa.

Lakini, kama pamoja na Watengenezaji wa kwanza, kweli alizoonyesha hazikukubaliwa na walimu wengi wa dini. Kwa hivyo hawa hawakuweza kudumisha hali yao kwa Maandiko, wakarejea kwa mafundisho ya watu, haya kiasili cha Wababa. Lakini Neno la Mungu lilikuwa ni ushuhuda pekee uliokubaliwa na wahubiri wa kweli wa kuja kwa Yesu. Cheko na zarau vilitumiwa kwa upande wa adui katika kusingizia wale waliotazamia kwa furaha juu ya kurudi kwa Bwana wao na walikuwa wakijitahidi kuishi maisha takatifu na kutayarisha wengine kwa kuonekana kwake. Ilifanyika kuonyesha zambi kwa kujifunza mambo ya unabii wa kuja kwa Kristo na mwisho wa dunia. Kwa hivyo kazi ya mapadri wa watu wengi ikapunguza imani katika Neno la Mungu. Mafundisho yao yakafanya watu kuwa watu kutokuwa Waaminifu, na wengi wakajiruhusu kwa kutembea kwa tamaa mbaya. Halafu watenda maovu wakayaweka yote juu ya Waadventisti.

Ingawa Miller akavuta makundi ya wasikilizi wenye akili, jina lake lilitajwa kwa shida na magazeti ya dini isipokuwa tu kwa cheko ao mashitaki. Waovu, waliposukumwa na walimu wa dini, wakakimbilia kwa mabisho ya matukano juu yake na kazi yake. Mzee huyu mwenye imvi aliyeacha makao yake ya kupendeza kwa

kusafiri kwa garama yake mwenyewe kuletea dunia onyo kubwa la hukumu inayokaribia akasitakiwa kama upumbavu.

## Usikivu na Kutokuamini

Usikivu ukaendelea kuongezeka. Kutoka kwa makumi mawili na mamia, makutano yakaongezeka kwa maelfu mengi. Lakini baada ya wakati, upinzani ulionekana juu ya hawa waliogeuka, makanisa yakaanza kuchukua hatua za kutiisha kwa wale waliokubali maoni ya Miller. Jambo hili likaita jibu kwa kalamu yake: "Kama tu- [161]
nakuwa wakosefu ninawaomba mtuonyeshe kwa namna gani kosa letu linakuwa kutoka katika neno la Mungu; tulichekwa ya kutosha; na ile haiwezi kutusadikisha kwamba tunakuwa katika kosa; Neno la Mungu pekee linaweza kugeuza maoni yetu. Hukumu yetu ilifanyika kwa kusudi pamoja na maombi, kama tulivyoona ushuhuda katika Maandiko."

Wakati uovu wambele ya garika ulipomsukuma Mungu kuleta garika duniani, kwanza akawajulisha kusudi lake. Kwa miaka 120 likasikiwa onyo kwa kutubu. Lakini hawakuliamini. Wakazarau mjumbe wa Mungu. Kama ujumbe wa Noa ulikuwa wa kweli, sababu gani watu wote wa dunia hawakuuona na kuuamini? Tendo la kudai haki la mtu mmoja kupinga hekima ya maelfu! Hawakuweza kuamini onyo wala kutafuta kimbilio ndani ya safina.

Watu wa zarau wakaonyesha kwa mwandamano usiobadilika wa majira, mbingu za rangi ya samawi zisizonyesha mvua kamwe. Katika zarau wakatangaza mhubiri wa haki kama mwenye juhudi ya kishenzi. Wakaenda zao, kujikaza zaidi kwa njia zao mbovu kuliko mbele. Lakini kwa wakati uliotajwa Hukumu za Mungu zikaanguka juu ya waliokataa huruma yake.

## Wenye Mashaka na Wasioamini

Kristo alisema kwamba kama vile watu wa siku za Noa "hawakujua hata garika ilipokuja na kuwaondosha wote; ndivyo kutakavyokuwa kuja kwa Mwana wa watu." Matayo 24:39. Wakati watu wanaojidai kuwa watu wa Mungu wanapojiunga pamoja na dunia, wakati anasa ya dunia inakuwa anasa ya kanisa, wakati wote wanapotazamia miaka nyingi ya mafanikio ya kidunia--ndipo, kwa

gafula kama nuru ya umeme, utakuja mwisho wa matumaini yao ya uongo. Kama vile Mungu alivyotuma mtumishi wake kwa kuonya dunia juu ya kuja kwa Garika, ndivyo alivyotuma wajumbe waliochaguliwa kujulisha ukaribu wa hukumu ya mwisho. Na kama watu wa wakati wa Noa walichekelea kwa kuzarau ubashiri wa muhubiri wa haki, ndivyo hivyo katika siku za Miller wengi kati ya wale wanaojidai kuwa watu wa Mungu wakachekelea maneno ya maonyo.

Hapo hapakuwa tena na ushahidi wa mwisho wakuonyesha kwamba makanisa yalitoka kwa Mungu kuliko machukio yaliyoamshwa na ujumbe huu uliotumwa na Mungu.

Wale waliokubali mafundisho ya kuja waliona kwamba ilikuwa
[162] wakati wa kukamata msimamo. "Mambo ya umilele yakawa kwao kitu cha kweli. Mbingu ililetwa karibu, na walijiona wao wenyewe kuwa na kosa mbele za Mungu." Wakristo walifanywa kuona kwamba wakati ulikuwa karibu, mambo walipashwa kutendea wenzao yalipaswa kufanywa kwa upesi. Umilele ulionekana kufunguliwa mbele yao. Roho wa Mungu alitoa uwezo kwa miito yao kujitayarisha kwa ajili ya siku ya Mungu. Maisha yao ya siku kwa siku ilikuwa mi laumu kwa washiriki wa kanisa wasiotakaswa. Hawa hawakutaka kusumbuliwa katika furaha yao, kutafuta feza, na tamaa ya nguvu kwa ajili ya heshima ya kidunia. Ndipo wakapinga imani ya kiadventisti.

Wapinzani wakajitahidi kupinga uchunguzi kwa kufundisha kwamba mambo ya unabii yalitiwa muhuri. Kwa hiyo Waprotestanti wakafuata nyayo za washiriki wa kanisa la Roma. Makanisa ya Waprotestanti wakadai kwamba sehemu kubwa ya Maandiko matakatifu--yale yanayotoa nuru kwa Neno la Mungu, sehemu ile inayofaa zaidi kwa wakati wetu, haikuweza kufahamika. Wachungaji wakasema kwamba Danieli na Ufunuo vilikuwa vitabu vya siri isiyoweza kufahamika kwa wanadamu.

Lakini Kristo aliongoza wanafunzi wake kwa maneno ya nabii Danieli, "Yeye anayesoma *afahamu*." Matayo 24:15. Na kitabu cha Ufunuo *kinapaswa* kufahamika. "Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa na Mungu aonyeshe watumishi wake maneno yaliyopaswa kuwa upesi... *Heri* anayesoma nao wanao*sikia* maneno ya unabii huu, na *kushika* maneno yaliyoandikwa ndani yake; kwa maana wakati ni karibu." Ufunuo 1:1-3, matoleo ya herufi za italics.

"Heri anayesoma" kunakuwa na wale hawatasoma; na "nao wanaosikia" hapo kuna wengine wanaokataa kusikia kitu cho chote juu ya mambo ya unabii; "na kusikia maneno yaliyoandikwa ndani yake" wengi wanakataa kusikia mafundisho katika Ufunuo; hakuna kati ya hawa anayeweza kudai mibaraka iliyoahidiwa.

Namna gani watu husubutu kusingizia kwamba Ufunuo ni siri inayopita fahamu ya wanadamu? Ni siri iliyofunuliwa, kitabu kilichofunuliwa. Ufunuo unaongoza mawazo kwa Danieli. Wote wawili wanaonyesha mafundisho makubwa juu ya mambo makubwa kwa mwisho wa historia ya dunia.

Yoane aliona hatari, vita, na kukombolewa kwa mwisho kwa watu wa Mungu. Aliandika mambo ya ujumbe wa mwisho unaopasa kukamilisha mavuno ya dunia, au kwa gala la mbinguni au kwa moto wa uharibifu, ili wale wanaogeuka kutoka kwa mabaya hata kwa ukweli waweze kufundishwa juu ya hatari na mapigano yanayo kuwa mbele yao.

Sababu gani, basi, juu ya ujinga huu unaoenea sana juu ya se- [163]
hemu kubwa hii ya Maandiko matakatifu? Ni matokeo ya juhudi iliyokusudiwa ya mfalme wa giza kwa kuficha watu yale yanayofunua madanganyifu yake. Kwa sababu hii, Kristo Bwana wa Ufunuo huu, kwa kuona mbele ya wakati vita juu ya fundisho la Ufunuo, akatangaza baraka kwa wote watakaoweza kusoma, kusikia, na kushika unabii.

[164] 

# 19 /SABABU GANI UCHUNGU MKUBWA ULE?

Kazi ya Mungu huonyesha mwaka kwa mwaka, mfano wa kutisha kila matengenezo makubwa ao mwenendo wa dini. Kanuni za matengenezo ya Mungu kuhusu watu yanakuwa mamoja daima. Mabadiliko makubwa ya sasa yanakuwa na uhusiano na yale ya wakati uliopita, na maarifa ya kanisa katika vizazi vya kwanza yanakuwa na mafundisho kwa wakati wetu.

Mungu kwa Roho Mtakatifu wake kwa upekee huongoza watumishi wake duniani katika kuepeleka mbele kazi ya wokovu. Watu ni vyombo katika mkono wa Mungu. Kwa kila chombo kulitolewa sehemu ya nuru ya kutosha kwa kumwezesha kufanya kazi aliyopewa kufanya. Lakini hakuna mtu kamwe aliyefikia ufahamu kamili wa kusudi la Mungu katika kazi kwa wakati wake mwenyewe. Watu hawafahamu kabisa katika uchukuzi wake wote ujumbe ambao wanaoutoa katika jina lake. Hata manabii hawakufahamu kabisa mambo ya ufunuo yaliyotolewa kwao. Maana ya ufunuo ilikuwa ya kufunuliwa toka kizazi kwa kizazi. Petro anasema: "Katika habari za wokovu huu manabii walitafuta na kuchunguza, wao waliotabiri juu ya neema itakayowafikia ninyi; walichunguza nini ao *wakati wa namna gani* Roho ya Kristo aliyekuwa ndani yao aliwaonyesha wakati aliposhuhudia mbele mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakao yafuata. Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili *yao wenyewe* lakini ni kwa ajili *yetu* waliohudumiwa." 1 Petro 1:10-12, Ni sisi herufi tofauti(italics). Fundisho la namna gani kwa watu wa Mungu katika kizazi cha ukristo! Watu hao "watakatifu wa Mungu" walitafuta na kuchunguza "kwa bidii" kwa ajili ya mafunuo zilizotolewa kwa vizazi ingawa vilikuwa havijazaliwa bado. Kemeo gani kwa ukavu wa macho wa wapenda dunia ambayo wanatosheka kutangaza kwamba mambo ya unabii hayawezi kufahamiwa.

Si mara chache mafikara hata ya watumishi wa Mungu yanakuwa ya kupofushwa sana kwa manebo ya asili na mafundisho ya uwongo ambayo wanashika kwa nusu tu mambo yaliyofunuliwa katika Neno la Mungu. Wanafunzi wa Kristo, hata wakati Mwokozi alikuwa

pamoja nao, walikuwa na wazo la kupendwa na watu wote juu ya Masiya kama mfalme wa mda aliyepashwa kuinua Israel; kwa mamlaka ya wakati wote. Hawakuweza kufahamu maneno yake yaliyotabiri mateso na mauti yake.

## "Wakati Umetimia" [165]

Kristo aliwatuma na ujumbe: "Wakati umetimia, ufalme wa Mungu ni karibu. Tubuni mukaamini Habari Njema." Marko 1:15. Ujumbe ule ulikuwa na msingi katika unabii wa Danieli 9. ''Majuma makumi sita na tisa" yalipashwa kufikia kwa Mfalme na wanafunzi walitazamia mbele kuimarishwa kwa ufalme wa Masiya kule Yerusalema ili atawale juu ya dunia yote nzima.

Wakahubiri habari iliyotolewa kwao, ingawa walikosa kufahamu maana yake. Wakati matangazo yao msingi wake ulikuwa katika Danieli 9:25, hawakuona katika shairi lililofuata kwamba Masiya alipashwa "kukatiliwa mbali." Mioyo yao ilikuwa juu ya utukufu wa utawala wa kidunia; jambo hili likapofusha akili yao.

Kwa wakati kabisa walipotumainia kuona Bwana wao kupanda kwa kiti enzi cha Dawidi, walimwona akikatwa, kupigwa, kuzihakiwa, na kuhukumiwa juu ya msalaba. Kukata tamaa kwa namna gani na uchungu yaliumiza mioyo ya wale wanafunzi!

Kristo alikuja kwa wakati halisi uliotabiriwa. Maandiko yalitimia katika habari yote. Neno na Roho wa Mungu ilishuhudia agizo la Mwana wake. Lakini mafikara ya wanafunzi yalifunikwa na mashaka. Kama Yesu alikuwa Masiya wa kweli wangetumbukia katika sikitiko na uchungu? Hili ndilo swali lililotesa roho zao wakati wa saa za kukata tamaa za Sabato ile iliyokuwa katikati ya kifo chake nakufufuka kwake.

Lakini hawakuachwa. "Nikikaa katika giza, Bwana atakuwa nuru kwangu... Atanileta inje kwa nuru na nitatazama haki yake." "Kwa wenye haki nuru inangaa gizani." "Nitafanya giza kuwa nuru mbele yao; na pahali pa kupotoka patanyoshwa. Maneno haya nitawafanyia, wala sitawaacha." Mika 7:8, 9; Zaburi 112:4; Isaya 42:16.

Matangazo yaliyofanywa na wanafunzi yalikuwa halisi "Wakati umetimia, ufalme wa Mungu ni karibu." "Kwa mwisho wa wakati" majuma makumi sita na tisa ya Danieli 9 ambayo yalipashwa kufikia

kwa Masiya, "Mupakaliwa"--Kristo alipokea mafuta ya Roho baada ya ubatizo wake kwa Yoane. "Ufalme wa Mungu" haikuwa, kama walivyofundishwa kuamini, ufalme wa kidunia. Wala ule ujao, ufalme wa milele ambao "na wote wenye mamlaka watamutumikia na kumutii." Danieli 7:27.

Neno hili "Ufalme wa Mungu" linatumiwa kutaja mambo yote mawili ufalme wa neema na ufalme wa utukufu Mtume anasema: "Basi, tukaribie kiti cha neema pasipo woga," ili tupate huruma
[166] na kuona neema. Waebrania 4:16. Kuwako kwa kiti cha ufalme kunaonyesha kuwako kwa ufalme. Kristo anatumia neno la "Ufalme wa mbinguni" kutaja kazi ya neema juu ya mioyo ya watu. Kwa hiyo kiti cha utukufu kinaonyesha ufalme wa utukufu. Matayo 25:31, 32. Ufalme huu ukingali wa wakati ujao. Hautasimamishwa hata wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili.

Wakati Mwokozi alipotoa maisha yake na akalia kwa sauti kubwa, "imekwisha," ahadi ya wokovu iliyo fanywa kwa mme na mke wenye zambi katika Edeni ikatimilika. Ufalme wa neema, ambao ulikuwako mbele kwa ahadi ya Mungu, ukaimarishwa.

Kwa hiyo kifo cha Kristo jambo ambalo wanafunzi walitazamia kama maangamizi ya tumaini lao ilikuwa ni milele kwa kweli. Wakati ilileta uchungu mkali, ilikuwa ushahidi kwamba imani yao ilikuwa halisi. Jambo lililowatumbukiza katika kukata tamaa likafungua mlango wa tumaini kwa waaminifu wote wa Mungu katika vizazi vyote.

Zahabu safi ya upendo wa wanafunzi kwa ajili ya Yesu ilichanganyika na msingi wa tamaa mbaya ya choyo. Maono yao yalivutwa na kiti cha ufalme, taji, na utukufu. Kiburi chao cha moyo, kiu cha utukufu wa kidunia, vikawaongoza kupita bila kujali maneno ya Mwokozi ya kuonyesha asili ya kweli ya ufalme wake, na kuonyesha zaidi kifo chake. Makosa haya yaliishia kwa jaribio ambalo liliruhusiwa kwa ajili ya kusahihishwa kwao. Kwa wanafunzi ilikuwa ni kutolewa Habari Njema ya utukufu ya Bwana wao aliyefufuka. Kuwatayarisha kwa kazi hii, maarifa ambayo yalionekana machungu sana yaliruhusiwa.

Baada ya kufufuka kwake Yesu akajionyeshea kwa wanafunzi wake njiani kwenda Emausi, na, "akawaelezea maana ya maneno yote yaliyo andikwa juu yake." Ilikuwa kusudi lake kukaza imani yao juu ya "neno la kweli la unabii." (Luka 24:27; 2 Petro 1:19).

Si kwa ushuhuda wake mwenyewe tu, bali kwa mambo ya unabii wa Agano la Kale. Na kama hatua ya kwanza kabisa katika kutoa maarifa haya, Yesu akaongoza wanafunzi kwa "Musa na manabii wote" wa Maandiko ya Agano la Kale.

### Kutoka kwa Kukata Tamaa na Kuelekea Uhakikisho Tumaini

Kwa namna kamilifu zaidi kuliko wakati wote wa mbele wanafunzi walikuwa "wamemwona, yule ambaye Musa katika sheria, na manabii, waliandika, juu yake." Mashaka, kukata tamaa, yakatoa nafasi kwa uhakikisho, kwa imani isiyokuwa na wingu. Walipita [167] katika jaribio kubwa lisiloawezekana na waliona namna gani neno la Mungu lilipata ushindi kwa kutimilika. Toka sasa na kuendelea nikitu gani kingeweza kutisha imani yao? Katika huzuni kali zaidi walipata "faraja yenye nguvu", tumaini lililokuwa kama "nanga ya roho, vyote viwili kweli na kusimama imara." Waeb. 6:18, 19.

Asema Bwana: "Watu wangu hawatapatishwa haya kamwe." "Kilio kinakawia kwa usiku, lakini furaha asubui." Yoeli 2:26; Zaburi 30:5. Kwa siku ya kufufuko kwake wanafunzi hawa wakakutana na Mwokozi, na mioyo yao ikawaka ndani yao walipokuwa wakisikiliza maneno yake. Kabla ya kupanda kwake, Yesu akawaagiza, "Kwendeni katika duniani pote, mukahubiri Habari Njema," akaongeza "Na tazama, mimi ni pamoja nanyi siku zote." Marko 16:15; Matayo 28:20. Kwa siku ya Pentekote Mufariji aliyeahidiwa akashuka, na roho za waaminifu zikasisimka na kwa kuona kuwapo kwa Bwana wao aliyepanda (mbinguni).

### Ujumbe wa Wanafunzi Ulilinganishwa na Ujumbe wa 1844

Maarifa ya wanafunzi kwa kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo yalikuwa na sehemu yake katika maarifa ya wale waliotangaza kuja kwake kwa mara ya pili. Kama vile wanafunzi walivyohubiri, "Wakati umetimia, ufalme wa Mungu ni karibu,'' vilevile Miller na washiriki wake walitangaza kwamba mda wa unabii wa mwisho katika Biblia ulikuwa karibu kuisha, kwamba hukumu ilikuwa karibu, na kwamba ufalme wa milele ulipashwa kuingizwa. Mahubiri ya wanafunzi kwa habari ya nyakati yalisimamia juu ya majuma makumi saba ya Danieli 9. Ujumbe uliotolewa na Miller na washiriki

wake ulitangaza mwisho wa siku 2300 za Danieli 8:14, mahali ambamo majuma makumi saba yanakuwa Sehemu moja. Mahubiri ya kila mojawapo yalisimamia juu ya utimilifu wa sehemu mbalimbali za mda wa unabii ule ule.

Kama wanafunzi wa kwanza, William Miller na washiriki wake hawakufahamu kabisa ujumbe waliuochukua. Makosa yaliyoanzishwa mda mrefu katika kanisa yakazuia maelezo sahihi ya jambo kubwa katika unabii. Kwa hiyo, ijapo walitangaza ujumbe ambao Mungu aliwatolea, lakini katika kukosa kufahamu maana yake wakateseka kwa kukata tamaa.

Miller akaingiza maoni ya kawaida kwamba dunia ni "mahali patakatifu," na akaamini kwamba "kutakasika kwa mahali patakat-
[168] ifu" kulionyesha kutakasika kwa dunia na moto kwa kuja kwa Bwana. Kwa hiyo, mwisho wa siku 2300, akazani, zilifunua wakati wa kuja kwa Yesu mara ya pili.

Kutakaswa kwa mahali patakatifu ilikuwa kazi ya mwisho iliyofanywa na kuhani mkuu katika utaratibu wa huduma wa mwaka. Ilikuwa ni kufunga kazi ya upatanisho--kuondoa ao kuweka mbali zambi za Israeli. Ilionyesha picha la kufunga kazi ya Kuhani Mkuu wetu mbinguni katika kuondoa ao kufutia mbali zambi za watu wake zilizoandikwa katika vitabu mbinguni. Kazi hii inaleta uchunguzi, kazi ya hukumu, na inatangulia bila kukawia kuja kwa Kristo katika mawingu ya mbingu, kwani atakapokuja kila jambo litakuwa limekwisha kukatwa. Asema Yesu: "Na mshahara wangu ni pamoja nami, kulipa kila mtu kama ilivyo kazi yake." Ufunuo 22:12. Ni hii kazi ya hukumu inayotangazwa na ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:7. "Ogopeni Mungu, na kumutukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

Wale waliotangaza onyo hili walitoa ujumbe wa haki kwa wakati unaofaa. Namna wanafunzi walikuwa hawakufahamu juu ya ufalme wa kusimamishwa kwa mwisho wa "majuma makumi saba," vivyo hivyo Waadventisti hawakufahamu habari ya jambo lililopashwa kufanyika kwa mwisho wa "siku 2300." Katika mambo mawili haya makosa inayopendwa na watu wengi ikapofusha akili kwa kutojua ukweli. Wote wawili wakatimiza mapenzi ya Mungu kwa kutoa ujumbe aliotamani utolewe, na wote wawili katika kukosa kufahamu maana ya ujumbe wao wakateseka kwa kukata tamaa.

Lakini Mungu alitimiza kusudi lake katika kuruhusu onyo la hukumu kutolewa kama ilivyokuwa. Katika maongozi yake ujumbe ulikuwa kwa ajili ya uchunguzi na utakaso wa kanisa. Je, upendo wao ulikuwa juu ya dunia ao juu ya Kristo na mbingu? Je walikuwa tayari kuacha tamaa zao mbaya za dunia na kukaribisha kuja kwa Bwana wao?

Uchungu vile ungechunguza mioyo ya wale waliojidai kupokea onyo. Je, wangetupilia mbali tumaini lao katika Neno la Mungu walipoitwa kwa kuvumilia makemeo ya dunia na jaribu la kukawia na kukata tamaa? Kwani hawakufahamu mara moja mambo ya Mungu, je wangetupa pembeni kweli iliyo kubaliwa na ushuhuda wazi wa Neno lake? Jaribu hili linge fundisha hatari ya kukubali maelezo ya watu baadala ya kufanya Biblia mtafsiri wake mwenyewe. Watoto wa imani wangeongozwa kujifunza kwa bidii sana Neno, na kuchunguza kwa uangalifu zaidi msingi wa imani yao, na kukataa kila kitu, hata kilikubaliwa sana na Wakristo wa kidunia, kile kisichokuwa na msingi kutika kwa Maandiko. [169]

Kile ambacho katika saa ya taabu kilionekana giza baadaye kingewekwa wazi. Ijapokuwa taabu ilitokea kwa makosa yao, wangejifunza kwa maarifa ya mibaraka yao kwamba Bwana ni " Mwenye rehema sana, mwenye huruma", kwamba njia zote zake ni " huruma na kweli kwao wanaoshika agano lake na shuhuda wake." Yakobo 5:11; Zaburi 25:10. " Hata mangaribi na asubui 2300: halafu Pahali patakatifu patasafishwa."

[170] # 20 /UPENDO KWA AJILI YA KUJA KWA KRISTO

6Uamsho mkubwa wa dini umetabiriwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14. Malaika moja ameonekana akiruka "katikati ya mbingu, mwenye Habari Njema ya milele, ahubiri kwao wanaokaa juu ya dunia, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa." "Kwa sauti kubwa" akatangaza: "Ogopeni Mungu, na kumutukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Mukamwabudu yeye aliyefanya mbingu na dunia na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:6,7.

Malaika ni mfano wa tabia bora ya kazi inayopaswa kutimizwa kwa ujumbe na uwezo na utukufu, ambavyo vinapaswa kuishugulikia. Kuruka kwa malaika "katikati ya Mbingu," "sauti kubwa," na matangazo yake "kwa kila taifa na kabila na lugha na jamaa" inatoa ushuhuda wa kuenea kwa upesi, katika dunia nzima kwa tendo. Kwa habari ya wakati ambao inapaswa kufanyika, inatangaza kufunguliwa kwa hukumu.

Ujumbe huu ni sehemu ya habari njema (injili) ambayo ingeweza kutangazwa tu katika siku za mwisho, ambapo tu ndipo inaweza kuwa hatika kwamba saa ya hukumu yake imekuja. Sehemu ile ya unabii wake ambao inaelekea kwa siku za mwisho, Danieli aliagizwa kufunga na kutia muhuri "hata wakati wa mwisho." Danieli 12:4. Mpaka wakati huu ndipo ujumbe juu ya hukumu utangazwe, wenye msingi na kutimilika kwa unabii.

Paulo alionya kanisa lisitazamie kuja kwa Kristo katika siku zake. Mpaka baada ya uasi mkubwa na utawala mrefu wa "mtu wa zambi" tunaweza kutazamia kuja kwa Bwana wetu. Tazama 2 Watesalonika 2:3. "Mtu wa zambi" vilevile "siri ya uasi," "mwana wa uharibifu," na "yule mwenye uovu," ni mfano wa cheo cha Papa, ambacho kilikuwa kwa kushikilia mamlaka yake kwa miaka 1260. Mda huu ulimalizika kwa mwaka 1798. Kuja kwa Kristo hakungefanyika mbele ya wakati ule. Paulo anaeneza onyo lake kwa ile inayohusu Wakristo wote hata kwa mwaka 1798. Kwa upande huu wa wakati

ule, ujumbe wa Kuja kwa Kristo mara ya pili ukatangazwa. Sivyo ujumbe wa namna ile haujatolewa kamwe kwa vizazi vilivyopita. Paulo, kama tulivyoona, hakuuhubiri; aliuweka mbali kwa wakati ujao ujumbe wa kuja kwa Bwana. Watengenezaji hawakuutangaza. Martin Luther aliweka siku ya hukumu karibu ya miaka 300 zijazo kutoka kwa siku zake. Lakini tangu 1798 kitabu cha Danieli kilifunuliwa, na wengi wakatangaza ujumbe wa hukumu kuwa karibu.

### Katika Inchi Mbalimbali kwa Wakati Moja [171]

Kama Matengenezo ya karne ya kumi na sita, Mwendo (kazi), la Kuja kwa Yesu likaonekana katika inchi mbalimbali kwa wakati moja. Watu wa imani wakaongozwa kujifunza mambo ya unabii na wakaona ushuhuda wa kusadikisha kwamba mwisho ulikuwa karibu. Makundi mbali mbali ya Wakristo, kwa kujifunza Maandiko tu, wakafikia kwa kuamini kwamba kuja kwa Mwokozi kulikuwa karibu.

Miaka mitatu baada ya Miller kufikia kwa maelezo yake ya mambo ya unabii. Dr. Joseph Wolff, “Mjumbe kwa ulimwengu,” akaanza kutangaza kukaribia kwa kuja kwa Bwana. Alizaliwa katika Ujeremani, wazazi wake Wayahudi. Alikuwa Kijana sana wakati ule, akasadikishwa kwa habari ya kweli ya dini ya kikristo. Alikuwa msikizi mwenye bidii sana kwa mazungumzo katika nyumba ya baba yake mahali Wayahudi waaminifu walikuwa wakikusanyika kila siku kwa kuzungumzia matumaini ya watu wao, utukufu wa kuja kwa Masiya, na kuimarishwa tena kwa Israeli. Siku moja, kusikia Yesu wa Nazareti kutajwa, kijana akauliza kujua alikuwa nani. “Muyahudi wa talanta kubwa mno” wakajibu” Lakini alipojidai kuwa Masiya, baraza la hukumu la Wayahudi likamkatia hukumu ya kifo.”

“Sababu gani,” akafuatisha mwenye kuuliza, “je, Yerusalema iliharibiwa, na sababu gani tunakuwa katika utumwa?”

“Ole, ole,” akajibu baba yake, “kwa sababu Wayahudi waliua manabii.” Mara moja wazo likaja moyoni mwa mtoto: “Pengine Yesu pia alikuwa vilevile nabii, na Wayahudi wakamuua wakati alikuwa bila kosa.” Ingawa alikatazwa kuingia katika kanisa la Kikristo, akakawia mara kwa mara inje kusikiliza mahubiri. Alipokuwa na miaka saba tu ya kuzaliwa, alikuwa akijisifu kwa jirani wake mkristo juu ya kushinda kwa Israel wakati ujao wa

kuja kwa Masiya. Mzee akasema kwa upole: "Kijana mpenzi, nitakwambia nani aliyekuwa Masiya wa kweli: alikuwa Yesu wa Nazareti,... ambaye wababu wako walimsulubisha... Wende nyumbani na usome sura ya makumi tano na tatu ya Isaya, na utasadikishwa kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu."

Akaenda nyumbani na akasoma Maandiko. Kwa ukamilifu wa namna gani ilitimilika kwa Yesu wa Nazareti. Je, maneno ya mkristo yule ni ya haki? Kijana akauliza baba yake maelezo ya unabii lakini akakutana na ukimya bila huruma na hakusubutu tena kamwe kusema inayoelekea fundisho lile pamoja naye.

Wakati alipokuwa na miaka kumi na moja tu ya kuzaliwa, akaenda duniani kupata elimu, kuchagua dini yake na kazi yake ya maisha. Peke yake na bila senti hata moja, alipashwa kutafuta njia
[172] yeye mwenyewe. Akajifunza kwa bidii, na kujisaidia mwenyewe kwa mahitaji yake kwa kufundisha Kiebrania. Akaongozwa kukubali imani ya dini ya Roma na akaenda kufuata mafundisho yake katika College ya "Propagande de la Foi" (kutangaza imani). Hapo akashambulia kwa wazi matumizi mabaya ya kanisa na akalazimisha matengenezo. Baada ya mda, akatoshwa. Ikawa wazi kwamba hakuweza kamwe kuletwa kwa kutii utumwa wa dini ya Roma. Akatangazwa kuwa mtu asiyeweza kusahihshwa na kuachwa kwenda mahali palipompendeza. Akaenda Uingereza na akajiunga na kanisa la Uingereza. Baada ya miaka miwili ya majifunzo akaanza kazi yake mwaka 1821.

Wolff aliona kwamba mambo ya unabii hutangaza kuja kwa Kristo mara ya pili kwa nguvu na utukufu. Alipotafuta kuongoza watu wake kwa Yesu wa Nazareti kama Ni yule aliyeahidiwa, kuwaonyesha kuja kwake kwa mara ya kwanza kama kafara kwa ajili ya zambi, akawafundisha pia juu ya kuja kwake kwa mara ya pili.

Wolff aliamini kuja kwa Bwana kuwa karibu. Maelezo yake ya nyakati za unabii yakamfanya kuzania kurudi huko kama tarehe iliyoonyeshwa na Miller. "Je, Bwana wetu ... hakututolea ishara za wakati, kusudi tupate kujua hata, kukaribia kwa kuja kwake, jinsi mmoja anavyojua kukaribia kwa wakati wa jua kali kwa mtini na kutoa majani yake? Inatosha ... itajulikana kwa ishara za wakati, kwa kutushawishi kujitayarisha kwa ajili ya kuja kwake, kama vile Noa alivyotayarisha safina."

### Kupinga Maelezo ya Watu Wengi

Kufuatana na namna watu wotewalivyo tafsiri ao kutambua Maandiko, Wolff akaandika: "Sehemu kubwa sana ya kanisa la Kikristo imepotoka kutoka kwa maana kamili ya Maandiko, na ... wanapofikiri kwamba wakati wanaposoma habari ya *Wayahudi*, wanapaswa kufahamu Mataifa,na wanaposoma Yerusalema, wanapaswa kufahamu *kanisa*; na kama inasemwa *dunia*, maana yake ni *mbingu*; na kwa kurudi kwa *Bwana* wanapaswa kufahamu *maendeleo ya vyama vya wajumbe:* na kupanda juu ya mlima wa nyumba ya Bwana, maana yake ni *mkutano wa kundi kubwa la wamethodistes.*"

Tangu miaka 1821 hata 1845, Wolff akasafiri katika Misri, Abisinia, Palestina, Syria, Persia, Bokhara, India, na Amerika.

### Uwezo katika Kitabu

Dr. Wolff alisafiri katika inchi zilizokuwa za kishenzi kabisa bila ulinzi, kwa kuvumilia taabu na kuzunguukwa na hatari nyingi. [173] Akateswa bila chakula, na baridi, kuuzwa kama mtumwa, mara tatu akakatiwa hukumu ya kifo, akaviziwa na wezi, na mara zingine karibu kufa kwa kiu cha maji. Mara moja akanyanganywa vyote na akaachwa na kusafiri mwendo wa mamia yakilometres kwa miguu katika milima, teluji zikipiga katika uso wake na nyanyo zisizo naviatu zikagandamizwa na udongo wa baridi sana.

Walipomshauria kwamba si vema kusafiri bila silaha katika makabila yenye ukaidi na uadui, akasema mwenyewe "kuwa na silaha "maombi, bidii kwa ajili ya Kristo, na tumaini katika usaada wake." "Nimejazwa vilevile na upendo wa Mungu na jirani wangu katika moyo wangu, na Biblia inakuwa mikononi mwangu." "Nilisikia nguvu zangu kuwa ndani ya Kitabu hiki, na kwamba uwezo wake utanilinda."

Akavumilia mpaka wakati ujumbe ungeweza kupelekwa katika sehemu kubwa ya ulimwengu inayo katiwa na watu. Miongoni mwa Wayahudi, Turks, Parsis, Wahindi, na mataifa na makabila akagawanya Neno la Mungu katika lugha mbalimbali, na mahali po pote akatangaza kukaribia kwa kuja kwa Masiya.

Katika safari yake huko Boukhari akakutana mafundisho ya kurudi kwa Bwana yakifundishwa na watu waliokaa peke yao. Waarabu wa Yemen, akasema, wanakuwa na kitabu kinachoitwa Seera, ambacho kina tangazo la kuja kwa Kristo mara ya pili na ufalme wake wa utukufu; na wanatazamia mambo makuu kutendeka katika mwaka 1840." "Nikakuta wana wa Israeli, wa kabila la Dani, ... wanaotazamia, pamoja na wana wa Rekabu, kufika kwa upesi kwa Masiya katika mawingu ya mbingu."

Imani ya namna moja ilipatikana kwa mjumbe mwengine katika Tartares. Padri mmoja wa Tartares akauiiza wakati gani Kristo angekuja mara ya pili. Wakati mjumbe (missionaire) alijibu, kwamba hakujua kitu kwa jambo lile, padri akashangaa kwa ujinga wa namna ile kwa mwalimu wa Biblia, na akaeleza habari ya imani yake mwenyewe, yeye msingi kwa unabii, kwamba Kristo angekuja karibu mwaka 1844.

## Ujumbe wa Waadventisti katika Uingereza

Mwanzoni wa mwaka 1826 ujumbe wa kuja kwa kristo ukaanza kuhubiriwa katika Uingereza. Kwa kawaida, tarehe kamili ya kurudi kwa Yesu haikufundishwa, lakini ukweli wa kuja kwa Kristo mwenye uwezo na utukufu ukatangazwa kwa watu wengi. Mwan-
[174] dishi mmoja wa Kingereza akasema kwamba karibu wahuduma 700 wa kanisa la Uingereza walijitoa katika kuhubiri "habari njema hii ya ufalme."

Ujumbe ulioonyesha mwaka 1844 kuwa wakati wa kuja kwa Bwana ukatolewa vilevile katika Uingereza. Maandiko juu ya habari ya kurudi yakatangazwa sana kutoka America. Katika mwaka 1842 Robert Winter, Mwingereza aliyeamini kurudi kwa Yesu alipokuwa America, akarudi katika inchi yake na kutangaza habari ya kuja kwa Bwana. Watu wengi wakajiunga naye katika kazi ndani ya sehemu mbalimbali za Ungereza.

Katika upande wa America ya kusini, Lacunza, "Jesuite" wa Espania, akakubali ukweli wa kristo kurudi upesi. Kutaka kuepuka karipio la Roma, akatangaza habari yake chini ya jina la kujitwalia la Rabbi-Ben-Ezra, akajionyesha mwenyewe kama Muyahudi aliyegeuka. Karibu ya mwaka 1825 kitabu chake kitatafsiriwa katika

Kiingereza. Kilitumiwa kwa kuongeza usikizi uliokwisha kuamshwa katika Uingereza.

### Ufunuo Ukafunuliwa kwa Bengel

Katika Ujeremani ujumbe huu ulifundishwa na Bengel, mhubiri wa kiLuther na mwalimu wa Biblia. Wakati alipokuwa akitayarisha mahubiri kutoka kwa Ufunuo 21, nuru ya kuja kwa Kristo mara ya pili ikaangaza katika mafikara yake. Unabii wa Ufunuo ukafunuliwa kwa ufahamu wake. Alipofunikwa kwa ukubwa na utukufu wa mambo yaliyoonyeshwa na nabii, akalazimishwa kuacha fundisho hilo kwa mda. Katika mimbara fundisho hilo likamjia tena kwa nguvu. Tangu wakati ule akajitoa mwenyewe kujifunza mambo ya unabii na kwa upesi akafikia kwa imani kwamba kurudi kwa Kristo kulikuwa karibu. Tarehe ambayo aliyoiweka kama wakati wa kurudi kwa mara ya pili kulikuwa katika miaka michache karibu ya wakati ule ambao Miller alitangaza baadaye.

Maandiko ya Bengel yakaenezwa katika jimbo lake mwenyewe la Wurtemberg na kwa sehemu zingine za Ujeremani. Ujumbe wa kurudi ukasikiwa katika Ujeremani, na kwa wakati uleule ujumbe huo ukavuta uangalifu katika inchi zingine.

Huko Geneve, Gaussen akahubiri ujumbe wa kurudi kwa Yesu. Wakati alipoingia katika kazi ya kuhubiri akaelekea kwa mafundisho ya mashaka. Katika ujana wake akapendezwa na mambo ya unabii. Baada ya kusoma *Ancient History* [Historia ya zamani] ya Rollin, uangalifu wake ukawa kwa sura ya pili ya Danieli. Akashangazwa na namna unabii ulitimilika kwa uaminifu. Hapa palikuwa na ushuhuda [175] kwa maongozi ya Maandiko. Hakuweza kudumu kutoshelewa na akili za kibinadamu, na katika kujifunza Biblia akaongozwa kwa imani ya hakika.

Akafikia kwa imani kwamba kuja kwa Bwana kulikuwa karibu. Alipovutwa na umuhimu wa ukweli huu, akakusudia kuupeleka mbele ya watu. Lakini imani ya watu wengi kwamba mambo ya unabii wa Danieli hayawezi kufahamika ilikuwa kizuizi kikubwa. Mwishowe akakusudia--kama vile Farel alivyofanya mbele yake katika kuhubiri Genève--kwa kuanza na watoto, kwa njia yao akatumainia kuwa wazazi watavutwa. Akasema, "Nikusanya wasikilizaji watoto; kama kundi linaongezeka kuwa, kubwa, kama

likionekana kwamba wanasikiliza, wanapendezwa, wanakuwa na usikizi, kwamba wanafahamu na kueleza fundisho, nina hakika kuwa na kundi la pili karibu, na wao, watu wakubwa wataona kwamba ni faida yao kukaa na kujifunza. Wakati jambo hili linapotendeka, ushindi utapatikana."

Alipokuwa akisema na watoto, watu wakubwa wakaja kusikiliza. Vyumba vya kanisa lake vikajaa na wasikilizaji, watu wa heshima na wenye elimu, na wageni wa inchi zingine wakazuru Geneve. Kwa hivyo ujumbe ukapelekwa kwa sehemu zingine.

Alipotiwa moyo, Gaussen akatangaza mafundisho yake na matumaini ya kuanzisha mafundisho ya vitabu vya unabii. Baadaye akawa mwalimu katika chuo cha elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini, akiendelea kwa siku ya juma pili na kazi yake kama mwalimu wa katikisimu, kusema kwa watoto na kuwafundisha katika Maandiko. Kwa kiti cha mwalimu, kwa njia ya vitabu (chapa) na kama mwalimu wa watoto, yeye kwa miaka mingi alikuwa chombo katika kuita uangalifu wa wengi kwa mambo ya unabii ambayo yalionyesha kwamba kuja kwa Bwana kulikuwa karibu.

### Wahubiri Watoto wa Skandinavie

Katika Skandinavie vilevile ujumbe wa kurudi kwa Yesu alitangazwa. Wengi wakasimama kutubu na kuacha zambi zao na kutafuta rehema katika jina la Kristo. Lakini padri wa kanisa la mahali pale akapinga mabadiliko, na wengine waliohubiri ujumbe wakatupwa gerezani.

Mahali pengi ambapo wahubiri wa kuja kwa Bwana kwa karibu walinyamazishwa, Mungu akapendezwa kutuma ujumbe kwa njia ya watoto wadogo. Kama vile walikuwa chini ya umri wa maisha ya mtu mzima, serkali haikuweza kuwafunga, na wakaruhusiwa kusema bila kusumbuliwa.

[176] Katika makao yake ya umasikini watu wakakusanyika kusikia maonyo. Wahubiri wengine watoto hawakuwa zaidi ya umri wa miaka sita ao mnane; ijapo maisha yao yalishuhudia kwamba walimpenda Mwokozi, wakaonyesha tu kwa kawaida akili na uwezo vinavyoonekana katika watoto wa umri ule. Wakati waliposimama mbele ya watu, lakini, walibadilishwa na mvuto mbali ya zawadi zao za kawaida. Sauti na tabia vikageuka, na pamoja na uwezo mkubwa

wakatoa maonyo ya hukumu, "Ogopeni Mungu, na kumutukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

Watu wakasikiliza kwa kutetemeka. Roho wa Mungu akasema mioyoni. Wengi wakaongozwa kwa kutafuta Maandiko, wasiokuwa na kiasi wakatengenezwa, na kazi ikafanywa kwa kuonyesha kwamba hata wachungaji wa kanisa la pale walilazimishwa kukubali kwamba mkono wa Mungu ulikuwa katika mabadiliko.

Ilikuwa mapenzi ya Mungu kwamba habari ya kuja kwa Mwokozi ilipashwa kutolewa katika Skandinavie, na akaweka Roho yake juu ya watoto ili kazi iweze kutendeka. Wakati Yesu alipokaribia Yerusalema, watu, wakaogopeshwa na mapadri na watawala, wakaacha tangazo lao la furaha walipokuwa wakiingia kwa milango ya Yerusalema. Lakini watoto katika viwanja vya hekalu wakachukua kiitikio, na wakapaaza sauti, "Hosana kwa Mwana wa Daudi!" Matayo 21:8-16. Kwa namna Mungu alitenda kazi kwa njia ya watoto kwa wakati wa kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, ndivyo hivyo akatumika kwa njia yao katika kutoa ujumbe wa kuja kwake kwa mara ya pili.

## Ujumbe Unatawanyika

Amerika ikawa mahali pakubwa pa kazi ya kutangaza kurudi kwa Yesu. Maandiko ya Miller na ya washiriki wake yakaenezwa duniani pote. Mbali na katika eneo kubwa habari njema ya milele: "Ogopeni Mungu, na kumutukuza kwa maana hukumu yake imekuja."

Mambo ya unabii ambayo ilionekana kuonyesha kuja kwa Kristo katika majira ya 1844 yakashikwa sana rohoni mwa watu. Wengi wakasadikishwa kwamba mabishano juu ya nyakati za unabii yalikuwa ya haki, na wakaacha kiburi na mafikara yao, wakakubali kweli kwa furaha. Wachungaji wengine wakaacha mishahara yao na wakajiunga katika kutangaza kuja kwa Yesu. Karibu wachungaji wachache, walakini, walikubali habari hii; kwa hivyo ikatolewa zaidi kwa watu wanyenyekevu wasiokuwa mapadri. Wakulima wakaacha mashamba yao; wafundi wa mashini, wakaacha vyombo vyao; wachuuzi wakaacha biashara yao; wafundi wa kazi wakaacha vyeo [177]
vyao. Kwa mapenzi wakavumilia kazi ngumu, taabu, na mateso, ili

wapate kuita watu kwa toba kwa wokovu. Ukweli wa kurudi kwa Yesu ukakubaliwa na maelfu ya watu.

### Maandiko Rahisi Yanaleta Hakikisho

Kama Yoane Mbatizaji wahubiri waliweka shoka katika shina la miti na kusihi sana wote kuzaa "matunda yanayofaa kwa toba." Kwa kuonyesha tofauti kwa uhakikika wa amani na salama vilivyosikiwa kwa mimbara ya watu wengi, ushuhuda rahisi wa Maandiko ukaleta hakikisho ambalo wachache waliweza kabisa kabisa kupinga. Wengi wakamtafuta Bwana kwa toba. Kwa kuacha mapenzi ambayo walishikamana nayo wakati mrefu ya mambo ya kidunia sasa wakatazama mbinguni. Kwa mioyo ya upole na polepole wakajiunga kwa kupaza sauti: "Ogopeni Mungu, na kumutukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja."

Wenye zambi wakauliza kwaa machozi: "Ninapashwa kufanya nini ili niokolewe?" Wale waliokosea jirani zao wakajiharakisha kwa kutengeneza kosa. Wote waliopata amani katika Kristo wakatamani kuijulisha kwa wengine. Mioyo ya wazazi ikarudia kwa watoto wao, na mioyo ya watoto kwa wazazi wao. Malaki 4:5, 6. Vizuizi vya kiburi na matengano vikatupiliwa mbali. Maungamo ya kweli yakafanywa. Mahali po pote roho zilikuwa zikiomboleza mbele ya Mungu. Wengi walitumia usiku wote mzima katika maombi kwa ajili ya hakika kwamba zambi zao zilisamehewa, ao kugeuka kwa jamaa zao wala jirani.

Makundi yote, watajiri na maskini, watu wa juu wala wa chini, wakawa na hamu ya kusikia mafundisho ya kuja kwa maraa ya pili. Roho ya Mungu ikatoa uwezo kwa ukweli wake. Kuwako kwa Malaika watakatifu kulisikiwa katika makutano haya, na wengi walikuwa wakiongezeka kila siku kwa waaminifu. Makutano makubwa wakasikiliza kwa utulivu kwa maneno ya heshima. Mbingu na dunia vilionekana kukaribiana. Watu wakarudi nyumbani na sifa kwa midomo yao, na sauti ya furaha ikavuma kwa utulivu wa usiku. Hakuna aliyehuzuria mikutano hiyo angaliweza kamwe kusahau maono ya usikizi mwingi.

## Habari llipingwa

Tangazo la wakati kamili wa kuja kwa Kristo kukaleta mabishano sana kwa wengi wa makundi yote, tokea kwa wachungaji [178] katika mimbara hata kwa mkubwa miongoni mwa wenye zambi. Wengi walitangaza kwamba hawakuwa na kizuizi kwa mafundisho ya kurudi kwa Yesu; walikataa tu wakati kamili. Lakini jicho la Mungu linaloona vyote likasoma mioyo yao. Hawakutamani kusikia habari ya kuja kwa Kristo ili aihukumu dunia kwa haki. Matendo yao hayangevumilia uchunguzi wa moyo unaomtafuta Mungu, na waliogopa kukutana na Bwana wao. Kama Mayahudi kwa wakati wa kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza hawakujitayarisha kumpokea Yesu. Hawakukataa tu kusikiliza mabishano ya wazi kutoka kwa Biblia lakini wakachekelea wale waliokuwa wakitazamia Bwana. Shetani akatupa laumu kwa uso wa Kristo kwamba wanaojidai kuwa watu wake walikuwa na upendo mdogo sana kwake hata hawakutaka kuonekana kwake.

"Hakuna mtu anayejua habari za siku ile na saa ile," ilikuwa ubishi mara kwa mara ulioendelea kuletwa na waliokataa imani ya kurudi kwa Yesu. Andiko ni: ''Habari za siku ile na saa ile hakuna mtu anayejua, hata malaika walio mbinguni, ... ila Baba peke yake." Matayo 24:36. Maelezo wazi ya maneno haya yalitolewa na wale waliokuwa wakitazamia Bwana, na matumizi mabaya yake ya wapinzani wao yalionyeshwa kwa wazi.

Usemi moja la Mwokozi haupashwi kutumiwa kwa kuharibu lingine. Ingawa hakuna mtu anayejua siku wala saa ya kuja kwake, tunaagizwa kujua wakati unakuwa karibu. Kukataa wala kutojali kujua wakati wa kuja kwake kunapokuwa karibu kutakuwa kwetu kama hatari kwetu kama ilivyokuwa katika siku za Noa bila kujua wakati gani garika ilipashwa kuja. Kristo anasema, "Lakini, usipoangalia, nitakuja kwako kama mwizi, wala hutajua saa nitakapokuja kwako." Ufunuo 3:3.

Paulo anasema kwa habari za wale waliojali onyo la Mwokozi: "Lakini ninyi ndugu, si katika giza, hata siku ile iwapate ninyi kama mwizi: sababu ninyi wote ni wana wa nuru, na wana wa mchana." 1 Watesalonika 5:2-5.

Lakini wale waliotamani sababu ya kukataa kweli wakafunga masikio yao kwa maelezo haya, na maneno "Hakuna mtu anayejua

siku ao saa" yakaendelea kukaririwa na watu wa zarau na hata wanaojidai kuwa wahubiri wa Kristo. Wakati watu walipoanza kuuliza njia ya wokovu, walimu wa dini wakajitia kati yao na ukweli kwa kufasiri kwa uongo Neno la Mungu.

Waaminifu zaidi katika makanisa walikuwa kwa kawaida wa kwanza kupokea habari. Mahali ambapo watu hawakuwa
[179] wakiongozwa na wapadri, mahali ambapo wangeweza kutafuta Neno la Mungu wao wenyewe, mafundisho ya kurudi yalihitaji tu kulinganishwa pamoja na Maandiko juu ya kuimarisha mamlaka yake ya kimungu.

Wengi waliongozwa vibaya na waume, wake, wazazi, ao watoto na walifanywa kuamini jambo hili kama zambi hata kwa kusikiliza mambo ya "uzushi"ya namna hiyo kama iliyofundishwa na Waadventisti. Malaika waliagiza kuwa na ulinzi aminifu juu ya roho hizi, kwa maana nuru ingine ilipaswa kuangaza juu yao kutoka kwa kiti cha Mungu.

Wale waliokubali habari walingojea kuja kwa Mwokozi wao. Wakati ambao walitazamia kukutana naye ulikuwa karibu. Wakakaribisha saa hii kwa utulivu wa heshima. Hakuna aliyekuwa na maarifa hii anayeweza kusahau saa hizo za tamani za kungoja. Kwa maana juma chache mbele ya wakati ule, kazi ya kidunia kwa sehemu kubwa iliwekwa pembeni. Waaminifu wa kweli kwa uangalifu wakachunguza mioyo yao kama kwamba katika saa chache kufunga macho yao kwa maono ya kidunia. Hapo hapakuwa kushona "mavazi ya kupanda nayo" (Tazama Nyongezo), lakini wote wakasikia haja ya ushuhuda wenyewe kwamba walikuwa wakijitayarisha kuonana na Mwokozi. Mavazi yao meupe yalikuwa usafi wa roho--tabia zilizotakaswa na damu ya kafara ya Kristo. Hebu kwamba kungekuwa vivyo na watu wa Mungu na moyo wa namna moja wa kuchunguza, imani yenye juhudi.

Mungu alitaka kuonyesha watu wake. Mkono wake ulifunika kosa katika kuhesabu nyakati za unabii. Wakati wa kutazamia ule ukapita, na Kristo hakuonekana. Wale waliotazamia Mwokozi wao wakajua uchungu mkali. Lakini Mungu alikuwa akichunguza mioyo ya wale waliojidai kungoja kuonekana kwake. Wengi waliongozwa kwa hofu. Watu hawa wakatangaza kwamba hawakuamini kamwe kwamba Kristo atakuja. Walikuwa miongoni mwa wa kwanza kuchekelea huzuni ya waamini wa kweli.

Lakini Yesu na jeshi lote la mbinguni walitazamia kwa upendo na huruma juu ya waaminifu ijapo walikuwa wenye kukatishwa tamaa. Kama kifuniko kinachotenga dunia na vile vinavyoonekana kwa visivyoonekana kikiinuliwa, malaika wangaliweza kuonekana wakisogea karibu na roho hizi za uaminifu na kuzilinda kwa mishale ya Shetani.

[180] # 21 /KUTESWA KWA AJILI YA MWENENDO WA MPUMBAFU AO MJINGA

William Miller na wasaidizi wake walitafuta kuamsha walimu wa dini kwa tumaini la kweli la kanisa na mahitaji yao ya maarifa makubwa ya kikristo. Walitumika pia kwa kuamsha wasiogeuka kwa toba na mabadiliko. “Hawakujaribu kutubisha watu kwa dini fulani. Walitumika bila uchaguzi w makundi ao dini fulani. ” Akasema Miller, “Nilifikiri kusaidia wote. Niliwaza kwamba Wakristo wote wangefurahi katika kutazamia kuja kwa Kristo, na kwamba wale hawakuweza kuona kama mimi hawangekosa kupenda wale waliopashwa kukubali kwa moyo mafundisho haya, sikuwaza kwamba kungeweza kuwa na lazima ya mikutano ya kuachana... Hesabu kubwa ya wale waliogeuka chini ya kazi zangu walijiunga na makanisa mbalimbali iliyokuwako.”

Lakini kwa sababu waongozi wa dini walipinga juu ya mafundisho ya Adventiste, walikatalia washiriki wao haki ya kuhuzuria kuhubiri juu ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Wala hata kusema kwa ajili ya tumaini lao katika kanisa. Waaminifu walipenda kanisa zao.

Lakini walipoona haki yao kwa kuchunguza mambo ya unabii unakanwa, waliona kwamba uaminifu kwa Mungu unawakataza kuwatii. Kwa hiyo waliona kwamba walikuwa na haki kujitenga. Wakati wa kipwa cha mwaka 1844 karibu elfu makumi tano wakatoka kwa makanisa.

Katika makanisa mengi, kwa miaka nyingi kuongezeka kulikuwako lakini kwa kidogo kufuatana na matendo ya dunia iloyolingana na upungufu kwa maisha ya kiroho. Lakini kwa mwaka ule kulikuwa ushuhuda wa upunguo mkubwa ndani ya makanisa yote ya inchi. Jambo lilielezwa sana kwa magazeti na mimbarani.

Bwana Barnes, mwandishi wa maelezo na mchungaji wa mojawapo wa makanisa makubwa ya Philadelphia, “akasema kwamba ... Sasa *hakuna maamsho, hapana kugeuka,* hakuna kuonekana sana kwa maendeleo katika neema katika walimu, na hakuna anayekuja kwa mafundisho yake kwa kuzungumza juu ya wokovu wa roho

zao...kunakuwa kuongezeka kwa akili ya kidunia *Ni vile inakuwa katika makanisa yote.*"

Katika mwezi wa Februari wa mwaka ule ule, Mwalimu Finney wa Oberlin College akasema: "Kwa kawaida, makanisa ya Kiprotestanti ya inchi yetu, yanavyoonekana, yalikuwa ao baridi ao adui ya matengenezo yote ya tabia na usafi vya wakati huu ... ubaridi wa kiroho unatawala karibu kote kwa wingi wa kutisha; kwa [181] hiyomagazeti ya dini ya inchi yote yanashuhudia ile. ...Kwa wingi sana washiriki wa kanisa wanatawaliwa na mtindo wakisasa (mode),yanaunga mkono mwovu katika makundi ya anasa, katika michezo, katika furaha. ... *Makanisa kwa kawaida yanakuwa kwa huzuniyenye kurudia kwa ushenzi.* Yalikwisha kwenda mbali ya Bwana na amekwisha kujiondoa mwenyewe kwao.'‘

## Binadamu Anakataa Nuru

Giza ya kiroho inafika, si kwa sababu ya kuondolewa kwa neema ya kumungu kwa upande wa Mungu bila sababu, bali ni kwa upande wa binadamu aliyekataa nuru. Wayahudi, kwa kupenda dunia na kumsahau Mungu, walikuwa katika ujinga juu ya kuja kwa Masiya. Katika kutoamini kwao wakamkataa Mkombozi. Mungu hakukatia mbali taifa la Wayahudi kwa mibaraka ya wokovu. Wale waliokataa kweli waliweka "giza kwa nuru, na nuru kwa giza." Isaya 5:20.

Baada ya kukataa kwao kwa habari njema Wayahudi wakaendelea kushika kanuni zao za zamani, wakati ambapo walikubali kwamba Mungu kakuwa tena kati yao. Unabii wa Danieli ulionyesha kwa wazi wakati wa kuja kwa Masiya na kutabiri vilevile kifo chake. Kwa hivyo walitia mashaka majifunzo yake, na mwishowe wa rabbis wakatangaza laana kwa wote wangejaribu kukadirisha wakati. Katika upofu na ugumu wa moyo Waisraeli wakati wa karne zilizofuatana wakasimama, bilakujali zawadi za neema ya wokovu, bila akili ya mibaraka ya habari njema, maonyo nzito na la kutisha kwa ajili ya hatari ya kukataa nuru kutoka mbinguni.

Yeye anayezuia hakikisho lamapashwa yake kwa sababu yanapingana na tamaa zake mwishowe atapoteza uwezo wa kuchagua kati ya ukweli na kosa. Roho hutengana na Mungu. Mahali ukweli wa Mungu unakataliwa kwa zarau, kanisa litakuwa katika giza, imani na upendo vitapunguka, na fitina huingia. Washiriki wa

kanisa hutia nguvu zao katika mambo ya kidunia, na wenye zambi hugeuka kuwa wagumu katika ugumu wa moyo wao.

### Ujumbe Wa Malaika wa Kwanza

Ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14 ulitolewa kwa kutenga wale wanaojidai kuwa watu wa Mungu kutoka kwa mivuto mibaya. Katika ujumbe huu, Mungu alituma kwa kanisa onyo ambalo
[182] balo kama lingelikubaliwa, lingaliweza kusahihisha maovu ambayo yalikuwa yakiwafunga mbali na yeye. Kama wangalikubali ujumbe, kushusha mioyo yao na kutafuta matayarisho kwa kusimama mbele yake, Roho wa Mungu angalionekana. Kanisa lingalifikia tena umoja ule, imani, na upendo wa siku za mitume, wakati waaminifu "walikuwa na moyo mmoja" na wakati "Bwana aliongezea kwa kanisa kila siku wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 4:32; 2:47.

Kama watu wa Mungu wangalipokea nuru kutoka kwa Neno lake, wangalifikia umoja ule ambao mtume anaeleza, "umoja wa Roho katika kifungo cha salama". Anasema, "Mwili ni mmoja, na Roho mmoja, kama vile mulivyoitwa katika tumaini moja la mwito wenu; Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja." Waefeso 4:3-5.

Wale waliokubali ujumbe wa kurudi kwa Yesu walikuja kutoka makanisa mbalimbali, na vizuizi vyao vya dini vikatupwa chini kwa nguvu. Kanuni za imani za mabishano zikavunjika kwa vipande vipande. Maoni ya uwongo juu ya kuja kwa mara ya pili yakasahihiswa. Makosa ya kanyoshwa, mioyo ikaungana katika upatano wakupendeza. Upendo ukatawala sana. Mafundisho haya yangefanya vile kwa wote, kama wote wangelikubali.

Wahuduma, ambao kama walinzi walipashwa kuwa wa kwanza kutambua dalili za kuja kwa Yesu, walishindwa kujifunza ukweli kutoka kwa manabii ao kwa ishara za wakati. Upendo kwa Mungu na imani katika Neno lake vikapunguka, na mafundisho juu ya kurudi kwa kristo ikaamsha tu kutokuamini kwao. Kama kwa zamani ushuhuda wa Neno la Mungu ukakutana na swali: "Nani katika wakubwa ao Wafarisayo aliyemwamini?" Yoane 7:48. Wengi walipinga majifunzo ya unabii, kufundisha kwamba vitabu vya unabii vilitiwa muhuri na havikuwa vya kufahamika. Makundi, kwa kutumainia wachungaji wao, wakakataa kusikiliza; na wengine, ingawa walisadikishwa na ukweli, hawakusubutu kukiri ili wasipate

"kutoshzwa katika sunagogi." Yoane 9:22. Ujumbe Mungu alioutuma kwa kujaribu kanisa ulionyesha namna gani watu walikuwa wengi waliotia mapendo yao kwa dunia hii kuliko kwa Kristo.

Kukataa maonyo ya malaika wa kwanza kulisababisha na hali ya kutisha ya tabia ya kupenda anasa ya kidunia, kuacha dini, na mauti ya kiroho ambayo yalikuwa katika makanisa katika mwaka 1844.

## Ujumbe wa Malaika wa Pili

Katika Ufunuo 14 malaika wa kwanza amefuatwa na wa pili, kutangaza, "Umeanguka, umeanguka, Babeli mji ule mkubwa, [183] kwani umefanya mataifa yote kunywa mvinyo ya gazabu ya uasherati wake." Ufunuo 14:8. Neno "Babeli" lilitoka kwa "Babel," na maana yake ni machafuko. Katika Maandiko inaonyesha namna mbalimbali ya dini ya uongo ao ukufuru wa dini. Katika Ufunuo 17 Babeli inafananishwa kama mwanamke--mfano uliotumiwa katika Biblia kama mfano wa kanisa, mwanamke mwema hufananishwa na kanisa safi; mwanamke mwovu ni kama kanisa lililokufuru.

Katika Biblia ushirika kati ya Kristo na kanisa lake unafananishwa na ndoa. Bwana anasema: "Na nitakuoa kuwa wangu kwa milele, ndiyo, nitakuoa kwa haki." "Mimi ni mme wenu." Na Paulo anasema: "Niliwapatanisha ninyi kwa mme mmoja, ili niletee Kristo bikira safi." Hosea 2:19; Yeremia 3:14; 2 Wakorinto 11:2.

## Uzinzi wa Kiroho

Kanisa, Kutokuwa na uaminifu kwa Kristo katika kuruhusu mambo ya kidunia kutawala moyo ni kama kuvunja kwa kiapo ya ndoa. Zambi ya Israeli katika kumwacha Bwana inaonyeshwa chini ya mfano huu. "Kama vile mke anavyoacha mme wake kwa udanganyifu, ndivyo mulivyonitendea mimi kwa udanganyifu, Ee nyumba ya Israeli, anasema Bwana." "Mke wa kufanya uasherati! anayekaribisha wageni pahali pa mme wake!" Yeremia 3:20; Ezekieli 16:32.

Asema mtume Yakobo: "Ninyi wazini, hamujui ya kwamba kuwa rafiki ya dunia ni kuwa adui ya Mungu? Basi kila mtu

anayetaka kuwa rafiki ya dunia anageuka kuwa adui ya Mungu." Yakobo 4:4.

Mwanamke (Babeli) yule "amevikwa nguo ya rangi ya zambarau na nyekundu, amepambwa kwa zahabu, na mawe ya bei kubwa, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha zahabu mkononi mwake, kinachojaa machukizo, na machafu... Na katika kipaji cha uso wake jina limeandikwa, SIRI, BABELI MKUBWA, MAMA YA MAKAHABA." Anasema nabii: "Nikaona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu na kwa damu ya washuhuda wa Yesu." Babeli "ni mji ule mkubwa unaotawala juu ya wafalme wa dunia." Ufunuo 17:4-6, 18.

Mamlaka ambayo kwa karne nyingi ilidumisha uwezo juu ya wafalme wa jamii ya Wakristo wote ni Roma. Rangi ya zambarau, na nyekundu, zahabu, mawe ya bei kubwa, na lulu, vinaonyesha fahari iliyovaliwa na askofu mwenye kiburi wa Roma. Hakuna mamlaka ingine iliyoweza kutangazwa kwa kweli "amelewa kwa damu ya
[184] watakatifu" kama kanisa lile ambalo lilitesa kwa ukali wafuasi wa Kristo.

Babeli inasitakiwa vilevile kwa uhusiano usio wa sheria pamoja na "wafalme wa ulimwengu." Kwa kuachana na Bwana kupatana na wapagani kanisa la Wayahudi likawa kahaba, na Roma, katika kutafuta usaada wa mamlaka ya kidunia, inapokea hukumu ya namna moja.

"Babeli ni mama ya makahaba." *Binti* zake wanapashwa kuwa makanisa yanayoshika mafundisho yake na kufuata mfano wake wa kuacha kweli ili kufanya mapatano pamoja na dunia. Ujumbe unaotangaza *kuanguka* kwa Babeli unapaswa kulinganishwa na makundi ya ushirika wa dini yaliyokuwa safi zamani na imegeuka kuwa potovu. Kwa hivi ujumbe huu unafuata onyo la hukumu, unapaswa kutolewa katika siku za mwisho. Kwa hiyo haiwezi kutumiwa kwa kanisa la Roma tu, kwa maana lile lilikuwa katika hali ya maanguko muda wa karne nyingi.

Tena, watu wa Mungu wanaitwa kutoka katika Bebeli. Kufuatana na maandiko haya, watu wa Mungu wengi wakingali katika Babeli, Na ni katika makundi gani ya dini ambamo munakuwa sehemu kubwa ya wafuasi wa Kristo? Katika makanisa inayokiri imani ya Kiprotestanti. Kwa wakati wa kutokea kwao makanisa haya yalipata msimamo bora kwa ajili ya kweli, na mibaraka ya

Mungu ilikuwa pamoja nao. Lakini wakashindwa kwa tamaa ya namna moja ileile ambayo ilikuwa uharibifu wa Israeli kuiga desturi na kujipendekeza na urafiki wa wasiomwogopa Mungu.

### Kujiunga Pamoja na Walimwengu

Makanisa mengi ya kiprotestanti yamefuata mfano wa uhusiano pamoja na "wafalme wa dunia" makanisa ya taifa, kwa uhusiano wao na serkali; na makanisa mengine, kwa kutafuta mapendeleo ya dunia. Neno "Babeli" machafuko--linaweza kutumiwa kwa makundi haya yanayojidai kwamba yalipata mafundisho yao kutoka kwa Biblia, lakini yamegawanyika katika makundi isiyohesabika pamoja na kanuni ya imani za mbalimbali.

Kazi ya kanisa la kikatolika la Roma inabisha kwamba "kama kanisa la Roma lingekuwa na kosa ya ibada ya sanamu katika uhusiano kwa watakatifu, binti yake, kanisa la Uingereza, linakuwa na kosa ya namna moja, kwa sababu lina makanisa kumi inayojiweka wakfu kwa Maria kwa namna moja linalojiweka wakfu kwa Kristo."

Na Dr. Hopkin husema: "Hakuna sababu ya kufikiri kwamba [185]
roho na kanuni za mpinga kristo na vitendo kusongwa kwa ile ambayo inaitwa sasa Kanisa la Roma. Makanisa ya Kiprotestanti yanakuwa na umpinga kristo ndani yao, na yanakuwa mbali kabisa ya matengenezo kwa ... maovu na ubaya."

Juu ya Kanisa la Presbyteria kujitenga kwa Roma, Dr. Guthrie anaandika: "Miaka mia tatu iliyopita, kanisa letu, pamoja na Biblia iliyofunguliwa kwa mwenge yake, na maneno haya maalum: "Tafuteni maandiko" kwa mabendera yake, lilitoka kwa milango ya Roma. Ndipo akauliza swali hili la muhimu: Je, waligeuka kuwa safi walipotoka kwa Babeli ? "

### Safari za Kwanza kutoka kwa Habari Njema

Namna gani kanisa lilitoka mara ya kwanza kwa unyenyekevu wa habari njema? Kwa njia ya kupatana na kipagani, ili wapagani wakubali wepesi dini ya kikristo. "Karibu kufikia mwisho wa kumalizia karne ya pili karibu makanisa mengi yalikubali sura mpya... Kama wanafunzi wa zamani walipopumzika katika makaburi yao, watoto wao pamoja na waliogeuka wapya, ... wakaendelea

mbele na kutoa mfano mpya kwa dini." "Wingi wa wapagani, kujaa katika kanisa, kuchukua pamoja nao desturi zao, tamaa, na ibada ya sanamu." Dini ya Kikristo ikategemea mapendeleo na usaada wa watawala wa dunia. Ikakubaliwa kwa jina tu na wengi. "Lakini wengi wakadumu katika mambo ya kipagani, zaidi kuabudu kwa uficho sanamu zao."

Je, matendo ya namna ile haikufanyika karibu katika kila kanisa linalojiita lenyewe Protestanti? Kwa namna wenye kulianzisha waliokuwa na roho ya kweli ya matengenezo walikufa, wazao wao wakatoa mfano mpya." Kukataa kwa upofu kukubali kweli yo yote mbele ya yale wababa zao waliona, watoto wa watengenezaji wakatoka kwa mfano wao wa kujinyima na kuacha dunia.

Aa, kwa wingi wa namna gani makanisa ya watu wengi yalitoka kwa kanuni ya Biblia! Akazungumzia juu ya pesa, John Wesley akasema: " Usipoteze sehemu ya talenta hii ya damani kwa kupamba nyumba yako na vyombo vya ufundi; katika mapicha ya bei kali, kupamba... Wakati wote utakapovaa mavazi ya rangi ya zambarau nyekundu na kitani,' na zaidi' kuwa na maisha ya anasa kila siku,' bila shaka wengi watashangilia uzuri wa tamaa yako, kwa ukarimu wako na utu wema wako. Lakini utoshelewe zaidi na heshima itokayo kwa Mungu."

Watawala, watu wa siasa, wanacheria, waganga, wachuuzi,
[186] wanajiunga kanisani kwa kusudi la kwendesha faida zao za kidunia. Makundi mbalimbali ya dini, yakaja kusaidiwa na utajiri wa hawa wakidunia waliobatizwa, kuwa njia nzuri sana ya kuvuta watu wengi. Makanisa mazuri sana, na garama nyingi yakajengwa. Mshahara wa juu sana ulilipwa kwa mchungaji mwenye kipawa cha kukaribisha watu. Mahubiri yake yalipaswa kuwa rahisi na kupendeza kwa masikio ya siku hizi. Kwa hiyo zambi za siku hizi zinafichwa chini ya hila za wema, mfano wakuogopa Mungu.

Mwandishi mmoja katika New York *Independent* akasema hivi juu ya dini ya Methodiste kama inavyokuwa: "Msitari wa mtengano kati ya wanaomwogopa Mungu na waovu unapotea katika namna ya kivuli, na watu wa bidii kwa pande zote mbili hujitahidi kutupia mbali tofauti yote kati ya desturi zao za kutenda na furaha."

Katika mwendo huu wa kutafuta anasa, kujinyima kwa ajili ya Kristo karibu kulipotea kabisa. "Kama feza zinahitajiwa sasa, ... hakuna mtu anayepashwa kuitwa kwa kutoa. Aa hapana! kuta-

yarisha maonyesho ya biashara, michezo ya kuingiza picha, michezo ya bahati (loterie), chakula cha jioni (banquet), wala kitu cha kula--kila kitu cho chote kwa kupendeza watu.”

Robert Atkins anaonyesha picha ya upungufu wa kiroho katika Uingereza: ‘‘ *Uasi, uasi, uasi,* tazama neno lililochorwa mbele ya makanisa yote; na wangejua, na waliiisikia na kungekuwa na tumaini; lakini, ole! Wakalalamika: “Sisi ni tajiri, tumepata vitu vingi; wala hatuhitaji kitu chochote.”‘ Zambi kubwa iliyoshitakiwa Babeli ni kwamba “amefanya mataifa yote kunywa mvinyo ya gazabu ya uasherati wake. “Kikombe hiki ni mfano wa mafundisho ya uongo yale aliyokubali kama matokeo ya urafiki pamoja na dunia. Kwa nafasi yake hutumia mvuto wa uovu juu ya dunia kwa kufundisha mafundisho yaliyopinga maneno wazi ya Biblia.

Kama haingekuwa kwamba dunia inaleweshwa na mvinyo wa Babeli, wengi wangalisadikishwa na kungeuzwa kweli kamili za Neno la Mungu. Lakini imani ya dini inaonekana kuwa na machafuko sana na kutopatana hata watu hawaujui kitu gani cha kuamini. Zambi ya dunia isiyotubiwa inalala mlangoni mwa kanisa.

Ujumbe wa malaika wa pili haukutmilika katika mwaka 1844. Makanisa basi yalianguka kiroho kwa kukataa nuru ya ujumbe wa kurudi kwa Yesu, lakini hayakuanguka kabisa. Namna walikuwa wakiendelea kukataa mambo ya ukweli wa pekee kwa ajili ya wakati huu waliendelea kuanguka chini na kuendelea chini. Bado, lakini, itawezekana kusemwa kwamba “Babeli imeanguka, ... kwa sababu amefanya *mataifa yote* kunywa mvinyo wa hasira ya uasherati wake.” [187]
Makanisa ya Kiprotestanti yanakuwa ndani ya masitaka ya malaika wa pili. Lakini kazi ya uasi haijafikia hatua yake ya mwisho.

Mbele ya kuja kwa Bwana, Shetani atatumika “na uwezo wote, na ishara na maajabu ya uwongo, na udanganyifu wote wa uzalimu”; na wale ambao “hawakupokea mapendo kwa kweli, wapate kuokolewa,” wataachwa kupokea “nguvu ya upotevu, hata waamini uwongo.” 2 Watesalonika 2:9-11. Hata muungano wa kanisa pamoja na dunia utakapotimia kabisa ndipo kuanguka kwa Babeli kutakuwa kamili. Mabadiliko ni ya kidogo kidogo na kutimilika kamili kwa Ufunuo 14:8 kunakuwa kwa wakati ujao.

Bila kutazama giza ya kiroho inayokuwa katika makanisa yanaosimamisha Babeli, wengi wa wanafunzi wa kweli wa Kristo wangali wanapatikana katika ushirika wao. Wengi hawajaona

kamwe kweli za kipekee kwa ajili ya wakati huu. Wengi ni wale wanaotamani nuru kamili zaidi. Wanatazama bila kuona sura ya Kristo katika makanisa ambamo wanaambatana nayo.

Ufunuo 18 huonyesha wakati ambao watu wa Mungu ambao wakingali katika Babeli wataitwa kujitenga kwa ushirika wake. Ujumbe huu, wa mwisho unaopaswa kutolewa kwa dunia, itatenda kazi yake. Nuru ya kweli itaangaza juu ya wote ambao mioyo yao inafunguliwa kwa kuipokea, na wana wote wa Bwana wanaokuwa katika Babeli watasikia mwito: "Tokeni kwake, watu wangu." Ufunuo 18:4.

# 22 /UNABII UNATIMILIKA [188]

Wakati ulipopita ambapo kuja kwa Bwana kulipotazamiwa kwanza--wakati wa masika ya mwaka 1844--wale waliotazamia kuonekana kwake walikuwa katika mashaka na kutokuwa na hakika. Wengi wakaendelea kuchunguza katika Maandiko, kwa kupima tena ushuhuda wa imani yao. Maneno ya unabii, ya wazi na ya nguvu, yalionyesha kuja kwa Kristo kuwa karibu. Kugeuka kwa waovu na uamsho wa kiroho miongoni mwa Wakristo kulishuhudia kwamba ujumbe ulikuwa wa mbinguni. Walihangaishwa na mambo ya unabii, ambayo walizania kama, kulingana na wakati wa kuja kwa mara ya pili, ilikuwa fundisho la kuwatia moyo kwa kungoja na uvumilivu katika imani,ili mambo yaliokuwa giza kwa akili yao sasa ifunuliwe. Miongoni mwa mambo haya ya unabii ilikuwa Habakuki 2:1-4. Hakuna mtu, hata, aliyefahamu kwamba kukawia kwa wazi--wakati wa kungojea--unakuwa katika unabii. Baada ya uchungu, andiko hili likaonekana kuwa la maana sana: "Maono haya ni kwa wakati ulioamuriwa, lakini kwa mwisho yatasema, wala hayatasema uwongo; hata yakikawia, uyangoje; kwa sababu yatakuja kweli, hayatachelewa. . . Mwenye haki ataishi kwa imani yake."

Unabii wa Ezekieli pia ulikuwa faraja kwa waaminifu:

"Bwana Mungu anasema hivi... Siku ni karibu, na kutimia kwa kila maono ... Nitasema, na neno nitakalolisema litatimizwa; wala halitakawishwa tena." "Neno nitakalolisema litatimia." Ezekieli 12:2325,28.

Wale waliokuwa wakingoja wakafurahi. Yeye anayejua mwisho tangu mwanzo aliwapa tumaini. Kama mafungu kama haya ya Maandiko hayangekuwako, imani yao ingalianguka.

Mfano wa mabikira kumi wa Matayo 25 pia unaonyesha mambo ya maisha ya Waadventiste. Hapo paonyeshwa hali ya kanisa wakati wa siku za mwisho. Mambo yao ya maisha yamefananishwa na tendo la ndoa ya mashariki:

"Halafu ufalme wa mbinguni utafananishwa na mabikira kumi waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kukutana na bwana arusi.

Watano wao walikuwa wapumbafu na watano wenye akili. Wale walio kuwa wapumbafu, walichukua taa zao, bila mafuta; lakini wenye akili walicukua mafuta ndani ya vyombo vyao pamoja na taa zao. Basi wakati bwana arusi alipokawia, wao wote wakasinzia na kulala usingizi. Lakini saa sita ya usiku kulikuwa kelele: Tazama, bwana arusi! tokeni kukutana naye." Matayo 25:1-6.

[189] Kuja kwa Kristo kama kulivyotangazwa na ujumbe wa malaika wa kwanza, kulifahamika kuwa mfano wa kuja kwa bwana arusi. Kuenea kwa matengenezo chini ya kutangaza kwa kuja kwa karibu kwa Kristo kukajibu kwa mfano wa mabikira. Katika mfano huu, wote walichukua taa zao, Biblia, "na wakaenda kukutana na bwana harusi." Lakini wakati wapumbafu "hawakuchukua mafuta pamoja nao," "wenye akili walichukua mafuta ndani ya vyombo vyao pamoja na taa zao." Wa nyuma wakajifunza Maandiko ili kuchunguza ukweli na wakawa na akili ya kipekee, imani kwa Mungu ambayo haingeangushwa na kukata tamaa na kukawia. Wengine wakaendeshwa na musukumo, hofu yao ikaamshwa na ujumbe. Lakini imani yao ilijengwa juu ya imani ya ndugu zao, walitoshelewa na nuru yenye kuwayawaya ya maono, bila ufahamu kamili wa kweli wala kazi halisi ya neema ndani ya moyo. Hawa wakaendelea "kukutana" na Bwana katika matazamio ya zawadi ya mara moja lakini hawakutayarishwa kwa kukawia na uchungu. Imani yao ikaanguka.

"Wakati bwana arusi alipokawia, wao wote wakasinzia na kulala usingizi." Kwa kukawia kwa bwana arusi ni mfano wa kupitisha wakati, kukata tamaa, ni kukawia kwenye kuonekana kwa inje. Wale ambao imani yao iliimarishwa juu ya ujuzi wa kipekee wa Biblia walikuwa na mwamba chini ya miguu yao ambayo mawimbi ya uchungu hayakuweza kuharibu. "Wao wote wakasinzia na kulala usingizi," kundi moja katika kuacha imani yao, lingine likangoja kwa uvumilivu hata mwangaza wazi zaidi ulipaswa kutolewa. Wale wa kijuujuu hawakuweza tena kuegemea kwa imani ya ndugu zao. Kila mmoja anapaswa kusimama ao kuanguka yeye mwenyewe.

## Ukaidi wa Dini Unaonekana

Tangu wakati huu, ushupavu wa dini ukaanza kuonekana. Wengine wakaonyesha juhudi za ukaidi. Mawazo yao ya ukaidi

yakakutana na kutokuwa na huruma kwa jamii kubwa ya Waadventiste, ndipo wakaleta laumu juu ya kazi ya ukweli.

Shetani alikuwa akipoteza watu wake, na kwa kuleta laumu kwa kazi ya Mungu, akatafuta kudanganya wengine waliokubali imani na kuwaendesha kwa nguvu kwa kupita kipimo. Ndipo wajumbe wake wakawa tayari wakivisia kupata kosa lo lote, kila kitu kisichokuwa kitendo cha kukubaliwa, na kulishikilia katika hali ya kupita kipimo ili kufanya Waadventiste wachukiwe. Kama angeweza kuleta watu wengi wa kutangaza imani ya kuja kwa mara ya pili, wakati uwezo wake ungeendelea kutawala mioyo yao, angepata faida Kubwa. [190]

Shetani ni "mushitaki wa ndugu zetu." Ufunuo 12:10. Roho yake inaongoza watu kutazama makosa ya watu wa Bwana na kuwashikilia akiwatangaza, lakini matendo yao mema yanapita bila kutajwa.

Katika historia yote ya kanisa hakuna matengenezo yaliyofanywa bila kukutana na vizuizi vikubwa. Po pote ambapo Paulo alisimamisha kanisa wengine waliojidai kupokeo imani wakaingiza ujushi. Luther pia alivumilia kwa watu washupavu waliojidai kwamba Mungu alinena kwa njia yao, walioweka mawazo yao wenyewe juu ya Maandiko. Wengi walidanganywa kwa njia ya waalimu wapya na wakaungana na Shetani kwa kuondoa kwa nguvu mambo ambayo Mungu aliongoza Luther kujenga. Wesleys alikutana na werevu wa Shetani katika kusukuma katika ushupavu watu wasiyokuwa imara na wasiotakaswa.

William Miller hakuwa na huruma kwa ushupavu. "Ibilisi," akasema Miller, "anakuwa na nguvu nyingi kwa mioyo ya wengine kwa siku ya leo." "Mara nyingi, uso wa kungaa na upendo, shavu, lililolowana, maneno ya kukatwa na machozi, vimenipa ushahidi wa utawa wa moyo kuliko makelele yote katika ukristo."

Katika matengenezo adui zake wakashitakiwa maovu ya ushupavu juu ya wale waliokuwa wakiomba sana kukataa ushupavu. Mwendo wa namna ileile ulikuwa ukifuatwa na wapinzani wa kazi ya kiadventiste. Hawakutoshelewa na kuzidisha makosa ya ushupavu, wakaeneza taarifa ambazo hazikuwa hata na uhusiano kidogo wa kweli. Amani yao ilikuwa ikisumbuliwa na kutangazwa kwa Kristo kuwa mlangoni. Waliogopa ingeweza kuwa kweli, huku wakatumaini kwamba haikuwako. Hii ilikuwa siri ya vita yao kwa kupinga Waadventiste.

Mahubiri ya ujumbe wa malaika wa kwanza yalielekea mara kukomesha ushupavu. Wale walioshirikiana kwa kazi hizi kubwa walikuwa katika umoja; mioyo yao ilijazwa na upendo wa mtu kwa mwenzake na kwa ajili ya Yesu, ambaye walimtazamia kumwona upesi. Imani moja, tumaini la baraka moja, wakahakikisha ngabo juu ya mashambulio ya Shetani.

### Kosa Linasahihishwa

"Basi wakati bwana arusi alipokawia, wao wote wakasinzia na kulala usingizi. Lakini saa sita ya usiku kulikuwa kelele: Tazama bwana arusi anakuja! tokeni kukutana naye." Katika wakati wa
[191] jua kali wa mwaka 1844 ujumbe ukatangazwa katika maneno ya Maandiko kabisa.

Kile kilichoongoza kwa maendeleo haya kilikuwa ni uvumbuzi kwamba amri ya Artasasta kwa ajili ya kurudishwa kwa Yerusalema, ambayo ilisaidia kujua mwanzo wa hesabu ya siku 2300, ikafanyika katika masika ya mwaka wa 457 B.C., na si kwa mwanzo wa mwaka, kama ilivyoaminiwa. Hesabu kutoka masika ya mwaka 457, miaka 2300 ikamalizika wakati wa masika ya mwaka 1844. Mifano ya Agano la Kale pia ilielekeza kwa wakati wa masika kama wakati ambao "kutakaswa kwa mahali patakatifu" kulipaswa kufanyika.

Kuchinjwa kwa Kondoo wa Pasaka kulikuwa ni kivuli cha mauti ya Kristo, mfano ulitimilika, si kwa tukio tu, bali na kwa wakati. Kwa siku ya kumi na ine ya mwezi wa kwanza wa Wayuda, siku ile kabisa na mwezi ambapo kwa karne nyingi kondoo wa Pasaka alikuwa akichinjwa, Kristo akaanzisha karamu hiyo ambayo ilikuwa kwa kukumbuka mauti yake mwenyewe "Mwana-kondoo wa Mungu." Kwa usiku uleule akakamatwa kwa kusulibiwa na kuuawa.

Vivyo hivyo mifano ya kuelekea kwa kuja kwa mara ya pili inapaswa kutimizwa kwa wakati ulioonyeshwa katika kazi ya mfano. Kutakaswa kwa mahali patakatifu, ao Siku ya Upatanisho, kulitukia kwa siku ya kumi ya mwezi wa saba wa Wayuda wakati kuhani mkuu, alipokwisha kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli yote, na kwa hivyo akaondoa zambi zao kutoka kwa mahali patakatifu, akaja na kubariki watu. Kwa hiyo iliaminiwa kwamba Kristo angeonekana kuja kutakasa dunia kwa kuharibu zambi na wenye

zambi, na kubariki watu wake wanaomungojea kwa kuwapa kutokufa. Siku ya kumi ya mwezi wa saba, Siku kuu ya Upatanisho, wakati wa kutakaswa kwa mahali patakatifu, ambao katika mwaka 1844 ulianguka kwa tarehe ya makumi mbili na mbili ya Oktoba, ilizaniwa kama ni wakati wa kuja kwa Bwana. Siku 2300 zingemalizika wakati wa masika, na mwisho ikaonekana kuwa wazi bila ubishi.

### "Kilio cha Usiku wa Manane"

Maneno yakawa na hakikisho la nguvu, na "kilio cha usiku wa manane" kikasikiwa kwa maelfu ya waaminifu. Kama mawimbi, tukio hili likazambaa kwa nguvu toka mji kwa mji, kijiji kwa kijiji. Ushupavu ukatoweka kama baridi kali ya alfajiri kabla ya jua kutokea. Kazi ilikuwa ya namna moja na ile ya nyakati za kurudi kwa Bwana ambako miongoni mwa Israeli wa zamani walifuata ujumbe wa karipio kutoka kwa watumishi wake. Hapo kulikuwa furaha nyingi sana, lakini Zaidi uchunguzi mwingi wa moyo, ungamo la [192]
zambi, na kuacha dunia. Hapo kulikuwa kujitoa wakfu kwa Mungu.

Kwa miendo yote ya dini tangu siku za mitume, hakuna mojawapo yaliojiepusha zaidi kwa upungufu wa kibinadamu na werevu wa Shetani kuliko ile iliokuwa kwa wakati wa masika ya mwaka 1844.

Kwa mwito, "Tazama bwana arusi anakuja," wale waliokuwa wakingojea "wakaamka, wakatengeneza taa zao"; wakajifunza Neno la Mungu kwa usikizi mkuu ambao haukuwako mbele. Hawakukuwa wenye vipawa zaidi, bali wenye kuwa wenye unyenyekevu zaidi na wenye bidii, waliokuwa wa kwanza kutii mwito. Wakulima wakaacha mavuno yao katika mashamba, wafundi wa mashine wakaacha vyombo vyao na kwa furaha wakaenda kutoa maonyo. Makanisa kwa kawaida yakafunga milango yao juu ya ujumbe huu, na kundi kubwa la wale walioukubali wakajitenga kwao. Wasiosadiki waliokusanyika kwa mikutano ya Waadventiste wakaona uwezo wa kusadikisha ukihuzuria ujumbe, "Tazama, bwana arusi anakuja!" Imani ikaleta majibu kwa maombi. Kama manyunyu ya mvua juu ya inchi yenye kiu, Roho ya neema akashuka juu ya watafutao kwa bidii. Wale waliotazamia upesi kusimama uso

kwa uso pamoja na Mkombozi wao wakaona furaha kubwa. Roho Mtakatifu akalainisha moyo.

Wale waliokubali ujumbe wakafikia wakati ambao walitumainia kukutana na Bwana wao. Wakaomba sana mtu kwa mwenzake. Wakakutana mara kwa mara katika mahali pa uficho kushirikiana pamoja na Mungu, na sauti ya maombezi ikapanda mbinguni kutoka mashambani na vichakani. Hakikisho la kibali cha Mwokozi yalikuwa ya lazima zaidi kwao kuliko chakula cha kila siku, na kama wingu lilitia giza katika akili zao, hawakutulia hata walipoona ushuhuda wa neema ya rehema.

## Kukatishwa Tamaa Tena

Lakini tena, wakati wa kutazamia ukapita, na Mwokozi wao hakutokea. Sasa wakaona kama Maria alivyofanya wakati alipokuja kwa kaburi la Mwokozi na kukuta linapokuwa wazi, akapaza sauti na kulia: "Wameondoa Bwana wangu, wala sijui pahali walipomuweka." Yoane 20:13.

Hofu kwamba habari ingeweza kuwa kweli ikatumiwa kama kizuio juu ya ulimwengu usiosadiki. Lakini walipoona hakuna alama za hasira ya Mungu, wakafunika tena hofu yao na kuendelea
[193] delea na laumu lao na cheko. Kundi kubwa lililojidai kuamini wakaacha imani yao. Wenye kuzihaki wakavuta wazaifu na wenye kuogopea vyeo na hawa wote wakajiunga katika kutangaza kwamba ulimwengu unaweza kudumu kwa namna ileile kwa maelfu ya miaka.

Waaminifu waliojitoakwa kweli walikuwa wameacha vyote kwa ajili ya Kristo, na kama walivyoamini, wakatoa onyo lao la mwisho kwa ulimwengu. Kwa hamu kubwa sana walikuwa wameomba , "Kuja Bwana Yesu." Lakini sasa kwa kuchukua tena mzigo wa matata ya maisha na kudumu kwa matusi ya ulimwengu wenye kuzihaki lilikuwa jaribu la kutisha sana.

Wakati Yesu alipopanda juu ya punda na kuingia Jerusalem kama mshindi wanafunzi wake waliamini kwamba alitaka kuketi juu ya kiti cha ufalme cha Dawidi na kukomboa Israeli kwa magandamizi. Kwa matumaini ya juu, wengi wakatandika mavazi yao ya inje kama zulia (tapis) katika njia yake wala kutapanya mbele yake matawi yenye majani mengi ya ngazi. Wanafunzi walikuwa

wakitimiza kusudi la Mungu,lakini wakaangamizwa kwa uchungu mkali. Lakini siku chache zikapita kabla hawajashuhudia kifo cha maumivu makubwa cha Mwokozi na kumlaza ndani ya kaburi. Matumaini yao yakafa pamoja na Yesu. Hata wakati Bwana alipofufuka toka kaburini ndipo wakaweza kufahamu kwamba mambo yote yalitabiriwa kwa unabii.

## Ujumbe Ulitolewa kwa Wakati Uliofaa

Kwa namna ileile Miller na washiriki wake wakatimiza unabii na wakatoa ujumbe ambao Maongozi ya Mungu yalitabiri ulipashwa kutolewa kwa ulimwengu. Hawangeweza kuutoa wangefahamu kabisa mambo ya unabii yanayoelekea uchungu wao, na kutoa ujumbe mwengine kuhubiriwa kwa mataifa yote kabla ya kuja kwa Bwana. Habari za malaika wa kwanza na wa pili zilitolewa kwa wakati unaofaa na zilitimiza kazi ambayo Mungu aliyokusudia waitende.

Dunia ilikuwa ikitazamia kwamba kama Kristo hangetokea, Kiadventiste kingeachwa . Lakini wakati watu wengi walipoacha imani yao kulikuwa wengine waliosimama imara. Matunda ya kazi ya adventiste, roho ya uchunguzi wa moyo, ya kukana dunia na kutengeneza maisha, ikashuhudia kwamba ilikuwa kazi ya Mungu. Hawakusubutu kukana kwamba Roho Mtakatifu alishuhudia kwa mahubiri ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Hawakuweza kuvumbua kosa katika nyakati maalum za unabii. Adui zao hawakufaulu kuangusha maelezo yao ya unabii. Hawakuweza kukubali kukana msimamo uliofikiwa kwa njia na juhudi, kujifunza Maandiko kwa maombi, katika akili zilizoangaziwa na Roho wa Mungu na mioyo [194]
ya kuchomwa kwa uwezo wake wenye uzima, ambao ulisimama imara na kupinga watu wa elimu na usemaji.

Waadventiste waliamini kwamba Mungu aliwaongoza kutoa onyo la hukumu. Wakatangaza, “limechunguza mioyo ya wote waliolisikia, ... ili wale watakaochunguza mioyo yao wenyewe, waweze kujua upande gani ... wangepatikana, kama Bwana angefika sasa wangepaza sauti, ‘Huyu ndiye Mungu wetu, Tumemungoja, naye atatuokoa;’ ao wangeita miamba na milima kuanguka juu yao kuwaficha mbele ya uso wake yeye anayeketi juu ya kiti cha enzi!

Mawazo ya wale walioendelea kuamini kwamba Mungu aliongoza yanaelezwa katika maneno ya William Miller: "Tumaini langu katika kuja kwa Kristo ni la nguvu kwa daima, nimefanya tu, baada ya miaka ya uangalifu, kila nilichoona wajibu wangu kufanya." "Maelfu mengi, kwa mfano wote wa kibinadamu, walifanywa kwa kujifunza Maandiko katika mahubiri ya wakati; na kwa njia ile, katika imani na kumwangiwa kwa damu ya Kristo, wamepatanishwa kwa Mungu."

## Imani Inaimarishwa

Roho ya Mungu ilikuwa ingali inakaa kwa wale ambao hawakukataa nuru kwa wepesi waliopokea na kulaumu ujumbe wa kurudi kwa Yesu "Basi, msitupe mbali matumaini yenu, kwa maana yana zawadi kubwa. Kwa sababu munahitaji uvumilivu, ili mukikwisha kufanya mapenzi ya Mungu, mupate ile ahadi. Kwa kuwa bado kidogo sana, Yeye anayekuja atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki ataishi kwa imani: Naye kama akirudi nyuma, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi si watu wa kurudi nyuma kwa kupotea, lakini sisi ni pamoja nao walio na imani ya kuokoa roho zetu." Waebrania 10:35-39.

Onyo la upole hili linaambiwa kwa kanisa katika siku za mwisho. Linaonyeshwa kwa wazi kwamba Bwana angetokea kwa kukawia. Watu hapa walioambiwa walifanya mapenzi ya Mungu katika kufuata uongozi wa Roho yake na Neno lake; lakini hawakuweza kufahamu kusudi lake katika maisha yao. Walijaribiwa kwa mashaka kwamba Mungu alikuwa akiwaongoza kwa kweli. Kwa wakati huu maneno yalikuwa ya kufaa: "Sasa mwenye haki ataishi kwa imani." Wakainama kwa matumaini ya kukata tamaa, wangaliweza kusimama tu kwa imani katika Mungu na kwa Neno lake. Kwa kukana
[195] imani yao na kukana uwezo wa Roho Mtakatifu ambaye alitumikia katika ujumbe ingekuwa kurudi nyuma kwa uharibifu. Maendeleo yao tu ya salama ilikuwa nuru waliokwisha kupokea kwa Mungu, kuendelea kuchunguza Maandiko, na kungoja kwa uvumilivu na kukesha kwa kupokea nuru zaidi.

# 23 /SIRI YA WAZI YA PAHALI PATAKATIFU

[196]

Maandiko ambayo ni ya juu ya mengine yalikuwa vyote viwili, msingi na nguzo ya katikati ya imani ya kuja kwa Yesu ilikuwa tangazo, "Hata mangaribi na asubui ya siku elfu mbili mia tatu; halafu Pahali patakatifu patatakaswa." Danieli 8:14. Haya yalikuwa maneno ya mazoezi kwa waamini wote juu ya kuja upesi kwa Bwana. Lakini Bwana hakutokea. Waamini walijua kwamba Neno la Mungu halitaweza kushindwa; maelezo yao ya unabii yalikuwa na kosa. Lakini kosa lilikuwa wapi?

Mungu aliongoza watu wake katika mwendo mkubwa wa kuja kwa Yesu. Hangeuruhusu mwisho wake uwe wa giza na uchungu, kulaumiwa kama wa uwongo na wa ushupavu. Ijapo wengi wakaacha kuhesabia nyakati zao za unabii na wakakana msingi ulioimarishwa mwendo, wengine hawakutaka kukataa mambo ya imani na maisha yaliyokubaliwa na Maandiko na Roho wa Mungu. Ilikuwa wajibu wao kushikilia kwa nguvu ukweli waliyokwisha kupata. Kwa maombi ya juhudi wakajifunza Maandiko kwa kuvumbua kosa lao. Kwa namna hawakuweza kuona kosa kwa hesabu zao za nyakati za unabii, wakachunguza zaidi sana fundisho la Pahali patakatifu.

Wakajifunza kwamba hakuna ushahidi wa Maandiko unaokubali maoni ya watu wengi kwamba dunia ni Pahali patakatifu; lakini wakapata maelezo kamili ya Pahali patakatifu; asili yake, pahali, na matumizi:

"Basi hata agano la kwanza lilikuwa na amri ya kuabudu Mungu, na Pahali patakatifu pake pa dunia. Maana hema ilitengenezwa ile ya kwanza iliyokuwa na taa, na meza na mikate ya onyesho kwa Mungu, palipoitwa Pahali patakatifu. Na nyuma ya pazia la pili, ilikuwa hema iliyoitwa Pahali patakatifu pa patakatifu, yenye kifukizo cha zahabu na sanduku ya agano iliyofunikwa na zahabu pande zote, na ndani yake kulikuwa kopo la zabahu yenye mana, na fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vibao vya agano; na juu yake makerubi ya zahabu, yakitia kivuli juu ya kiti cha rehema:" Waebrania 9:1-5.

“Pahali patakatifu” ilikuwa ni hema iliyojengwa na Musa kwa agizo la Mungu kama pahali pa kukaa pa kidunia pa Mwenyezi Mungu. “Na wanifanyie Pahali patakatifu; nipate kukaa katikati yao” (Kutoka 25:8), ilikuwa ni agizo lililotolewa kwa Musa. Hema wala maskani ilikuwa ni umbo kubwa la fahari. Zaidi ya uwanja wa inje, hema yenyewe ilikuwa na vyumba viwili vilivyoitwa Pahali
[197] patakatifu na Pahali patakatifu pa patakatifu, vilivyogawanywa na pazia nzuri sana, Kifuniko cha namna moja kilifunga mlango kwa chumba cha kwanza.

## Pahali Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu

Katika Pahali patakatifu kulikuwa na kinara upande wa kusini pamoja na taa zake saba kutoa nuru mchana na usiku; upande wa kaskazini kulikuwa na meza ya mikate ya onyesho. Mbele ya pazia inayotenga Pahali patakatifu na patakatifu pa patakatifu kulikuwa na mazabahu ya zahabu ya uvumba, ambalo wingu la manukato, pamoja na maombi ya Israeli, yalikuwa yakipanda kila siku mbele za Mungu.

Katika Pahali patakatifu pa patakatifu palisimama sanduku, sanduku ilifunikwa na zahabu, gala ya Amri Kumi. Juu ya sanduku kulikuwa na kiti cha rehema kilichokuwa na makerubi wawili waliofanywa na zahabu ngumu. Ndani ya chumba hiki kuwako kwa Mungu kulionekana katika wingu utukufu lililokuwa katikati ya kerubi.

Baada ya kuwekwa kwa Waebrania katika Kanana, hema ao maskani iliwakombolewa kwa hekalu ya Solomono, ambayo, ijapo ni ya umbo la daima na ya ukubwa wa juu, ikafuata ulinganifu wa namna moja na vyombo vivyo hivyo. Katika umbo hili hema likawako--isipokuwa kwa wakati wa maangamizi wakati wa Danielihata maharibifu yake iliyofanywa na wa Waroma katika mwaka A.D. 70. Hii ni Pahali patakatifu tu duniani ambapo Biblia inatoa maelezo yote, Pahali patakatifu pa agano la kwanza. Lakini agano jipya halina Pahali patakatifu?

Kurudi tena kwa kitabu cha Waebrania, wakatafuta ukweli wakaona kwamba Pahali patakatifu pa agano la pili ao jipya ilionyeshwa katika maneno yaliyokwisha kuelezwa vizuri: “Basi hata agano la kwanza lilikuwa na amri ya kuabudu Mungu, na Pahali

patakatifu pake pa dunia." Kurudi nyuma kwa mwanzo wa sura ya kwanza, wanasoma: "Basi, neno kubwa katika maneno haya tunasoma ni hii: Tuna kuhani mukubwa wa namna hii, aliyeketi mukono wa kuume wa kiti cha Mwenyezi katika mbingu, mutumishi wa Pahali patakatifu, na wa hema ya kweli, ndiyo Bwana aliisimamisha, wala si watu." Waebrania 8:1,2.

Hapa panafunua Pahali patakatifu pa agano jipya... Pahali patakatifu pa agano la kwanza ilitengenezwa na Musa; hii ilitengenezwa na Bwana. Katika patakatifu pale pa kidunia makuhani walikuwa wakitenda huduma yao; katika hii, Kristo, Kuhani wetu Mkuu, alihudumia kwa mukono wa kuume wa Mungu. Hema takat- [198]
ifu moja ilikuwa duniani, na ingine ilikuwa mbinguni.

Hema iliyojengwa na Musa ilifanywa kwa mfano. Bwana alipokuwa akionyesha: "Sawasawa na maneno yote ninayokuonyesha, mufano wa hema, mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mutakavyofanya." "Na angalia uvifanye kwa mufano wao ulioonyeshwa mulimani." Hema ya kwanza ilikuwa "mufano wa wakati wa sasa; ndani yake sadaka na zabihu zilitolewa", mahali pake takatifu "mifano ya vitu vilivyo mbinguni." Makuhani walikuwa wakitumika kwa mufano na kivuli cha vitu vya mbinguni." Kristo hakuingia katika Pahali patakatifu palipofanywa kwa mikono, ndio mufano wa kweli, lakini aliingia mbinguni zenyewe, aonekane sasa mbele ya Mungu kwa ajili yetu." Kutoka 25:9,40; Waebrania 9:23; 8:5; 9:24.

Hema ya mbinguni ni asili kubwa ya hema Musa alijenga ambayo ilikuwa ni mfano. Fahari ya hema ya kidunia ilikuwa mfano wa utukufu wa hekalu lile la mbinguni pahali Kristo anapohudumia kwa ajili yetu mbele ya kiti cha ezi cha Mungu. Ukweli wa maana juu ya hema ya mbinguni na ukombozi wa mwanadamu yalifundishwa na Pahali patakatifu pa kidunia na huduma zake.

## Vyumba Viwili

Nafasi takatifu za mahali patakatifu mbinguni zinafananishwa na vyumba viwili katika Pahali patakatifu duniani. Yohana alijaliwa na maono ya hekalu ya Mungu mbinguni. Alitazama kule "taa saba za moto ziliwaka mbele ya kiti cha enzi." Aliona malaika "mwenye chungu cha zahabu ya uvumba; akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya mazabahu ya zahabu

iliyo mbele ya kiti cha enzi." Ufunuo 4:5; 8:3. Hapa nabii akaona chumba cha kwanza cha Pahali patakatifu pa mbinguni; na aliona "taa saba za moto" na "mazabahu ya zahabu", iliyofananishwa kwa kinara cha zahabu na mazabahu ya uvumba katika Pahali patakatifu pa dunia.

Tena ''hekalu la Mungu likafunguliwa", na akatazama ndani ya pazia juu ya patakatifu pa patakatifu. Na akaona "sanduku ya agano lake" la kufananishwa na sanduku lililojengwa na Musa kwa kuweka ndani amri ya Mungu. Ufunuo 11:19.

Hivyo, wale wanaojifunza fundisho hili wakaone bila shaka kwamba hakika mbinguni kunakuwa hema. Musa alijenga hema ya kidunia akifuata mfano alioonyeshwa. Paulo anafundisha kuwa
[199] mfano ule ulikuwa hema ya kweli ambao unakuwa mbinguni. Na Yoane anashuhudia kwamba aliiona mbinguni.

Ndani ya hekalu mbinguni, Pahali patakatifu pa patakatifu kunakuwa amri ya Mungu. Sanduku inayowekwa amri inafunikwa na kiti cha rehema, ambapo mbele yake Yesu anatetea mwenye zambi kwa ajili ya damu yake. Hapa ndipo kunafananishwa muungano wa haki na rehema katika mpango wa wokovu, muungano ambao unashangaza mbingu yote mzima. Hii ndiyo siri rehema ambamo malaika wanatamani kutazama vile Mungu anaweza kuwa mwenye haki wakati anahesabia haki mwenye zambi anayetubu.

Kazi ya Kristo kama mutetezi wa binadamu, inafananishwa katika Zakaria: "Atajenga hekalu la Bwana; na atachukua utukufu, na atakaa na kutawala juu ya kiti chake [cha Baba] cha enzi; naye atakuwa kuhani kwa enzi yake, na mshauri wa amani atakuwa katikati yao wawili". Zacharia 6:12,13.

"Atajenga hekalu la Bwana". Kwa zabihu yake na upatanisho, kristo ni msingi na mjengaji wa kanisa la Mungu, "jiwe kubwa la pembeni. Katika yeye jengo lote linaunganishwa vema na kukaa hata liwe hekalu takatifu katika Bwana". Waefeso 2:20,21. "Atachukua utukufu". Wimbo wa wale watakaonunuliwa utakuwa: "kwake yeye aliyetupenda na kutuosha zambi zetu kwa damu yake,...kwa yeye utukufu na uwezo hata milele na milele". Ufunuo 1:5,6.

Atakaa na kutawala juu ya kiti chake cha enzi; naye atakuwa kuhani juu ya kiti chake cha ufalme". Ufalme wa utukufu haujaingiliwa bado. Mpaka kazi yake kama mpatanishi imalizike, ndipo Mungu atamtolea ufalme ambao "hautakuwa na mwisho" Luka

1:33. Kama kuhani, Kristo anakaa sasa pamoja na Baba katika kiti chake cha enzi. Juu ya kiti kile cha ufalme kunakuwa yeye "aliyechukua taabu zetu; na kubeba huzuni zetu", ambaye alikuwa "katika mambo yote alijaribiwa sawa sawa na sisi, lakini pasipo kufanya zambi", kusudi aweze kusaidia wale wanaojaribiwa". Isaya 53:4; Waebrania 4:15; 2:18. Mikono iliyojeruhiwa, upande uliochomwa mukuki,nya yo ilioharibiwa, vinamtetea mwanadamu aliye anguka ambaye wokovu wake ulipatikana kwa bei sawa ile.

"Na shauri la salama litakuwa katikati ya wale wawili". Upendo wa Baba ni chemchemi ya wokovu kwa ukoo uliopotea. Yesu aliwaambia wafuasi wake, "Baba yeye mwenyewe anawapenda". Mungu alikuwa "ndani ya Kristo akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe". "Mungu alipenda ulimwengu hata kutoa Mwana wake wa pekee". Yoane 16:27; 2 Wakorinto 5:19; Yoane 3:16.

## Siri ya Mahali Patakatifu Inaelezwa [200]

"Hema ya kweli" mbinguni ni Pahali patakatifu pa agano jipya. Wakati wa kifo cha Kristo, huduma ya kufananisha ilimalizika. Kwa sababu Danieli 8: 14 ilitimilika katika mgawo huu, Pahali patakatifu ambapo maneno haya yanaelekea ni Pahali patakatifu pa agano jipya. Hivyo, unabii, huu "Hata mangaribi na asubui ya siku elfu mbili mia tatu, halafu Pahali patakatifu patasafishwa" unaelekea Pahali patakatifu mbinguni. Lakini kusafishwa kwa pahali patakatifu maana yake ni nini? Mbinguni kunaweza kuwa kitu cha kusafishwa? Katika Waebrania 9 kusafishwa kwa Pahali patakatifu pa duniani na Pahali patakatifu pa mbinguni vinafundishwa wazi :

Karibu vitu vyote vinasafishwa kwa damu, na pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo. Basi, mifano ya mambo yaliyo mbinguni ilipashwa kusafishwa hivyo [kwa damu ya wanyama] lakini vitu vya mbinguni yenyewe kwa zabihu nzuri zaidi kuliko hizi" (Waebrania 9:22,33), kwa damu ya zamani ya Kristo.

## Kutakaswa kwa Pahali Patakatifu

Kusafishwa katika huduma ya kweli kunapaswa kufanyika kwa damu ya Kristo. "Pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo. Ondoleo, ao kuondoa Zambi, ndiyo kazi yenye kutimizwa."

Lakini inawezekana je, zambi kuambatana na Pahali patakatifu mbinguni? Hii inaweza kujifunzwa kwa kuangalia huduma ya mfano, kwa maana makuhani duniani walitumika "kwa mufano na kivuli cha mambo ya mbinguni." Waebrania 8:5.

Huduma ya patakatifu pa kidunia ilikuwa na sehemu mbili. Makuhani walikuwa wakihudumia kila siku katika Pahali patakatifu, lakini mara moja kwa mwaka kuhani mkuu alifanya kazi maalumu ya upatanisho katika Pahali patakatifu pa patakatifu, kwa ajili ya kusafishwa kwa Pahali patakatifu. Siku kwa siku mwenye zambi anayetubu alileta sadaka yake na, kuweka mukono wake juu ya kichwa cha kafara, akaungama zambi zake, katika mufano kuzihamisha kutoka kwake mwenyewe hata kwa kafara isiyokuwa na kosa. Nyama basi alichinjwa. "Kwa kuwa uhai wa mwili ni katika damu." Walawi 17:11. Sheria ya Mungu iliyovunjwa ilidai uhai wa mkosaji. Damu, inayokuwa mufano wa uhai wa mwenye zambi ambaye kosa lake huchukuliwa kwa kafara (mnyama), ilibebwa na kuhani katika Pahali patakatifu na kunyunyizwa mbele ya pazia, nyuma ambapo palikuwa na sheria ambayo mwenye zambi aliy-
[201] ovunja. Kwa ibada hii zambi ikahamishwa katika mfano hata Pahali patakatifu. Mara zingine damu haikupelekwa katika Pahali patakatifu, lakini nyama ikaliwa na makuhani. Ibada mbili hizo zilikuwa mufano wa uhamisho wa zambi kutoka kwa mwenye kutubu hata kwa Pahali patakatifu.

Kwa namna hiyo kazi iliendelea kufanyika muda wa mwaka wote mzima. Zambi za Israeli zilikuwa zikihamishwa kwa Pahali patakatifu, na kazi ya kipekee ikawa ya lazima kwa ajili ya ondoleo lao la zambi.

### Siku Kuu ya Upatanisho

Mara moja kwa mwaka, kwa Siku Kuu ya upatanisho, kuhani akaingia katika Pahali patakatifu pa patakatifu kwa ajili ya kutakaswa kwa Pahali patakatifu. Wana wawili wa mbuzi wakaletwa na kura ikapigwa, "kura moja ni ya Bwana na kura ingine ya Azazeli." Walawi 16:8. Mbuzi wa Bwana akachinjwa kama sadaka ya zambi kwa ajili ya watu, na kuhani alipashwa kuleta damu ndani ya pazia na kuinyunyiza mbele ya kiti cha rehema na pia juu ya mazabahu ya uvumba mbele ya pazia.

"Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kukiri juu yake maovu yote ya wana wa Israeli na makosa yao yote, hata zambi zao zote; naye ataziweka zote juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai na kumutuma jangwani kwa mukono wa mutu aliye tayari, na yule mbuzi atachukua juu yake maovu yao yote mupaka inchi isiyo na watu; ataacha mbuzi kwenda zake jangwani." Walawi 16:21,22. Mbuzi wa Azazeli hakurudi tena katika kambi la Israeli.

Ibada ilikusudiwa kwa kuvuta Waisraeli kwa utakatifu wa Mungu na machukio yake ya zambi. Kila mutu aliombwa kuhuzunisha roho yake wakati kazi hii ya upatanisho ilipokuwa ikiendelea. Kazi zote zikawekwa kando, na Israeli alipashwa kutumia siku yenyewe katika maombi, kufunga, na kuchunguza moyo.

Kiti kingine kilikubaliwa baadala ya mwenye zambi, lakini zambi hazikufutwa kwa damu ya kafara (mnyama); zilihamishwa kwa Pahali patakatifu. Kwa sadaka ya damu mwenye zambi akatambua mamlaka ya sheria, akatubu kosa lake, na akaonyesha imani yake katika Mukombozi atakaye kuja; lakini hakufunguliwa kabisa kwa hukumu ya sheria. Kwa Siku ya Upatanisho kuhani mkuu, anapokwisha kupata sadaka kwa makutano, akaenda ndani ya Pahali patakatifu pa patakatifu. Akanyunyiza damu ya sadaka juu ya kiti cha rehema, mara moja juu ya sheria, kufanya malipizi kwa madai yake. Halafu, kama mwombezi, akachukua zambi juu yake [202]
mwenyewe na kuzibeba kutoka kwa Pahali patakatifu. Kuweka mukono wake juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli, yeye katika mufano akahamisha zambi hizi zote kutoka kwake mwenyewe hata kwa mbuzi. Ndipo mbuzi akazichukua mbali, na ziliangaliwa kwamba zilitengwa milele kutoka kwa watu.

## Uhakika wa Mbinguni

Kitu kilichotendwa katika mufano wa huduma ya Pahali patakatifu pa kidunia, inatendwa katika ukweli katika Pahali patakatifu pa mbinguni. Baada ya kupanda kwake mbinguni Mwokozi wetu akaanza kazi yake kama kuhani mkuu wetu: " Kwa sababu Kristo hakuingia katika Pahali patakatifu palipofanywa kwa mikono, ndio mufano wa kweli, lakini aliingia mbinguni zenyewe, aonekane sasa mbele ya Mungu kwa ajili yetu." Waebrania 9:24.

Utumishi wa kuhani katika chumba cha kwanza, “ndani ya pazia” inayotenga Pahali patakatifu pa patakatifu kwa behewa (uwanja) ya inje, ni mufano wa kazi ambayo Kristo alianza kisha wakati alipo panda mbinguni. Kuhani katika utumishi wa kila siku akaonyesha mbele ya Mungu damu ya sadaka ya zambi, vilevile uvumba ambao unapanda pamoja na maombi ya wa Israeli. Kwa hivyo Kristo anaombea damu yake mbele ya Baba kwa ajili ya wenye zambi na anaonyesha mbele yake, pamoja na manukato ya haki yake mwenyewe, maombi ya waamini waliotubu. Hiyo ndiyo iliyokuwa huduma katika chumba cha kwanza cha Pahali patakatifu katika mbingu.

Huko imani ya wanafunzi wa Kristo wakamfuata wakati alipokuwa akipanda. Hapa matumaini yao yalikuwa, “tumaini gani tuliyo nayo kama nanga ya roho, yote mbili kweli na kuwa imara, na inayoingia ndani ya pazia, pahali alipoingia Yesu kwa ajili yetu, mutangulizi wetu, amekuwa kuhani mkubwa kwa milele.” “Kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Pahali patakatifu alikwisha kupata ukombozi wa milele kwa ajili yetu.” Waebrania 6:19,20; 9:12.

Kwa mda wa karne ya kumi na mnane kazi hii ikaendelea katika chumba cha kwanza cha Pahali patakatifu. Damu ya Kristo ikahakikisha rehema na ukubali wa Baba kwa ajili ya waamini waliotubu, lakini zambi zao zingali zikidumu kwa vitabu vya ukumbusho. Kama katika huduma ya mfano huko kulikuwa na kazi ya upatanisho
[203] kwa mwisho wa mwaka, kwa hivyo kabla ya kazi ya Kristo kwa ajili ya watu kumalizika kunakuwa kazi ya upatanisho kwa ajili ya ondoleo la zambi kwa Pahali patakatifu. Kazi hii ilianza wakati siku 2300 zilipokwisha. Kwa wakati ule Kuhani wetu Mkubwa akaingia Pahali patakatifu pa patakatifu kwa kusafisha Pahali patakatifu.

## Kazi ya Hukumu

Katika agano jipya zambi za mwenye kutubu zinawekwa kwa imani juu ya Kristo na kuhamishwa kweli kwa Pahali patakatifu pa mbinguni. Na kama kusafishwa kwa mfano kwa Pahali patakatifu pa kudunia kulifanywa na ondoleo la zambi ambazo zilipachafua, vivyo hivyo utakaso wa sasa wa mbinguni unatimizwa kwa ondoleo, ao kufutwa, kwa zambi zilizoandikwa pale. Lakini kabla ya jambo

hili kuweza kufanyika uchunguzi unapashwa kufanyika pale wa vitabu vya ukumbusho kuonyesha ni wanani, kwa njia ya toba na imani katika Kristo, wanaostahili kupata faida ya upatanisho wake. Basi utakaso wa Pahali patakatifu kwa hivi unahusika na kazi ya uchunguzi -kazi ya hukumu -ya kutangulia kuja kwa Kristo, kwa maana wakati atakuja, na mushahara wake ni pamoja naye kulipa kila mutu kama ilivyo kazi yake. Ufunuo 22:12.

Kwa hivyo wale waliofuata nuru ya neno la unabii waliona kwamba, badala ya kuja duniani kwa mwisho wa siku 2300 katika mwaka 1844, Kristo aliingia kwa Pahali patakatifu pa patakatifu mno pa mbinguni kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho wa kutangulia kuja kwake.

Wakati Kristo katika uwezo wa damu yake anapoondoa zambi za watu wake kutoka kwa Pahali patakatifu pa mbinguni kwa mwisho wa huduma yake, ataziweka juu ya Shetani, anayepashwa kupata azabu ya mwisho. Mbuzi wa Azazeli akatumwa mbali katika inchi isiyokaliwa, hawezi kuja tena katika makutano ya Waisraeli. Ndivyo Shetani atakavyoangamizwa milele mbele ya Mungu na watu wake, na ataondolewa maisha katika uharibifu wa mwisho wa zambi na wenye zambi.

[204] # 24 /KRISTO ANAFANYA KAZI GANI SASA?

Fundisho la Pahali patakatifu likafungua siri ya uchungu. Likafungua kwa maoni kanuni kamili ya ukweli, yenye uhusiano na ya kulingana, kuonyesha mkono wa Mungu ulioongoza kazi kubwa juu ya kuja kwa Yesu. Wale waliotazamia kwa imani kuja kwake mara ya pili wakamtazamia kutokea katika utukufu, lakini kwa namna matumaini yao hayakufanyikiwa, wakapoteza akili juu ya Yesu. Sasa ndani ya patakatifu pa patakatifu wakatazama tena Kuhani wao mkubwa, kutokea upesi kama mfalme na mkombozi. Nuru kutoka kwa Pahali patakatifu ikaangazia wakati uliopita, wakati wa sasa, na wakati ujao. Ingawa walishindwa kufahamu ujumbe waliopata, kwani ulikuwa wa kweli.

Kosa halikuwa katika kutambua kwa nyakati za unabii, lakini katika tukio kufanyika kwa mwisho wa siku 2300. Kwani yote yaliyotabiriwa na unabii yalitimilika. Kristo alikuja, si duniani, bali katika Pahali patakatifu pa patakatifu pa hekalu katika mbingu; "Nikaona katika maono ya usiku, na tazama, pamoja na mawingu ya mbingu alikuwa mmoja aliye mfano wa mwana wa watu, akakaribia huyu Mzee wa Siku, wakamuleta karibu naye." Danieli 7:13.

Kuja huku kulitabiriwa pia na Malaika: "Na Bwana munayemutafuta atakuja gafula hekaluni mwake; na mujumbe wa agano munayemupenda, tazameni, atakuja, Bwana wa majeshi anasema." Malaki 3:1. Kuja kwa Bwana katika hekalu yake kulikuwa kwa gafula, hakukuzaniwa kwa watu wake. Hawakuwa wakimtazamia pale.

Watu hawakuwa bado tayari kukutana na Bwana wao. Pale kulikuwa kungali kazi ya matayarisho itimizwe kwa ajili yao. Kwa namna walipashwa kufuata kwa imani Kuhani wao mkubwa katika huduma yake, kazi mpya zingeweza kufunuliwa. Ujumbe mwengine ulipashwa kutolewa kwa kanisa.

## Nani Atakayesimama?

Nabii akasema: “Nani atakayevumilia siku ya kuja kwake? na nani atakayesimama wakati atakapoonekana? ... Naye atakaa kama mwenye kusafisha na kutakasa feza, naye atatakasa wana wa Lawi, na atawasafisha kama zahabu na feza, nao watatoa kwa Bwana sadaka kwa haki.” Malaki 3:2,3. Wale wanaokaa duniani wakati teteo ya Kristo yatakapoisha wanapashwa kusimama mbele ya Mungu bila muombezi. Mavazi yao yanapashwa kuwa safi bila doa, tabia zao zenye kutakaswa kutoka zambini kwa damu ya [205]
manyunyu. Kwa njia ya neema ya Mungu na juhudi yao wenyewe ya utendaji wanapashwa kuwa washindaji katika vita na yule muovu. Wakati hukumu ya ukaguzi inapoendelea mbele kule mbinguni, wakati zambi za waamini waliotubu zinapoondolewa kutoka kwa Pahali patakatifu, hapo panapashwa kuwa na kazi ya kipekee ya kuacha zambi miongoni mwa watu wa Mungu duniani. Kazi hii inaonyeshwa katika ujumbe wa Ufunuo 14. Wakati kazi hii itakapotimizwa, wafuasi wa Kristo watakuwa tayari kwa kutokea kwake. Ndipo kanisa ambalo Bwana wetu kwa kuja kwake analopashwa kupokea litakuwa “kanisa la utukufu, pasipo doa wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi.” Waefeso 5:27.

## “Tazama, Bwana Arusi Anakuja”

Kuja kwa Kristo kama Kuhani Mkuu kwa Pahali patakatifu pa patakatifu kwa usafisho wa Pahali patakatifu (Danieli 8:14), kuja kwa Mwana wa watu kwa Mzee wa Siku (Danieli 7:13), na kuja kwa Bwana katika hekalu yake (Malaki 3:11) ni matukio ya namna moja. Jambo hili pia ni mfano wa kuja kwa bwana arusi kwa ndoa katika mfano wa mabikira kumi wa Matayo 25.

Katika mfano, wakati bwana arusi alipofika, “nao waliokuwa tayari waliingia pamoja naye kwa arusi.” Kuja huku kwa bwana arusi kulifanyika mbele ya arusi. Arusi ni mfano wa kupokelewa na Kristo katika ufalme wake. Mji Mtakatifu, Yerusalema Mpya, mji mkubwa (capitale) ambao ni mfano wa ufalme, unaitwa “bibi arusi, mke wa Mwana-kondoo.” Akasema malaika kwa Yoane: “Kuja hapa, nami nitakuonyesha yule bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo.” “Akanichukua katika roho,“nabii asema, “akanionyesha ule

mji mkubwa, Yerusalema mtakatifu, ukishuka toka mbinguni, kwa Mungu." Ufunuo 21:9,10.

Bibi-arusi ni mfano wa Mji Mtakatifu, na mabikira waliotoka kukutana na bwana arusi ni mfano wa kanisa. Katika Ufunuo watu wa Mungu wanaitwa wageni kwa chakula cha arusi. Kama wageni, hawawezi kuwa bibi-arusi. Kristo atapokea kutoka kwa Mzee wa Siku katika mbingu "mamlaka, na utukufu, na ufalme." Yerusalema Mpya, mji mkubwa wa ufalme wake, "umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mme wake." Anapokwisha kupokea ufalme, atakuja kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana kwa ajili ya ukombozi wa watu wake watakaoshiriki kwa chakula cha arusi ya Mwana-Kondoo. Danieli 7:14; Ufunuo 21:2.

[206]

### Wanaongoja Bwana Wao

Tangazo "Tazama, bwana arusi anakuja" liliongoza maelfu ya watu kutazamia kuja kwa Bwana mara moja. Kwa wakati ulioagizwa Bwana-arusi akaja, si duniani, bali kwa Mzee wa Siku katika mbingu, kwa arusi, kupokelewa kwa ufalme wake. "Nao waliokuwa tayari waliingia pamoja naye kwa arusi." Hawakupashwa kuwa pale binafsi, kwa sababu wanakuwa duniani. Wafuasi wa Kristo wanapashwa kungojea Bwana wao atakaporudi kutoka arusini. Luka 12:36. Lakini wanapashwa kufahamu kazi yake na kumfuata kwa imani. Kwa nia hii walisemwa kwenda kwa arusi.

Katika mfano, wale waliokuwa na mafuta katika taa zao wakaingia kwa arusi. Wale ambao, katika usiku wa jaribu la uchungu, waliongoja kwa uvumilivu, wakichunguza Biblia kwa ajili ya nuru wazi zaidi--hawa waliona ukweli juu ya Pahali patakatifu katika mbingu na badiliko la huduma ya Mwokozi. Kwa imani wakamfuata katika kazi yake ndani ya Pahali patakatifu juu. Na wote waliokubali kweli zile zile, kumfuata Kristo kwa imani anavyotenda kazi ya mwisho ya upatanisho, wanaingia kwa arusi.

### Kufunga Kazi ndani ya Pahali patakatifu

Katika mfano wa Matayo 22 hukumu inafanyika mbele ya arusi. Mbele ya arusi mfalme anaingia kuona kama wageni wote wamevikwa mavazi ya arusi, vazi safi (lisilokuwa na mawaa) la tabia

iliyosafishwa katika damu ya Mwana-Kondoo. Ufunuo 7:14, Wote ambao kwa uchunguzi wameonekana kuwa wamevaa vazi la arusi wamekubaliwa na kuhesabiwa haki ya kupata sehemu katika ufalme wa Mungu na kukaa kwa kiti chake cha enzi. Kazi hii ya uchunguzi wa tabia ni hukumu ya uchunguzi, kazi ya mwisho ndani ya Pahali patakatifu kule mbinguni.

Wakati mambo ya wale katika vizazi vyote waliokubali Kristo yanapokwisha kuchunguzwa na kukatwa, ndipo rehema itafungwa na mlango wa rehema utafungwa. Kwa hivyo kwa maneno mafupi ya hukumu, "Nao waliokuwa tayari waliingia pamoja naye kwa arusi: mlango ukafungwa," tumechukuliwa chini kwa wakati ambao kazi kubwa kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu itakapokamilika.

Katika Pahali patakatifu pa kidunia, wakati kuhani mkubwa kwa Siku ya Upatanisho alipoingia kwa Pahali patakatifu pa patakatifu, huduma ndani ya chumba cha kwanza ulimalizika. Vivyo wakati Kristo alipoingia kwa Pahali patakatifu pa patakatifu kufanya kazi ya kumaliza upatanisho, alimaliza huduma yake katika chumba cha [207]
kwanza. Ndipo huduma katika chumba cha pili ikaanza. Kristo ametimiza tu sehemu moja ya kazi yake kama mwombezi wetu, ili kuingia kwa sehemu ingine ya kazi. Alikuwa akiendelea kutetea damu yake mbele ya Baba kwa ajili ya wenye zambi.

Kwa hivi inakuwa kweli kwamba mlango ule wa tumaini na rehema ambazo watu walikuwa nazo kwa miaka 1800 walipata ruhusa ya kukaribia kwa Mungu ulifungwa, mlango mwingine ukafunguliwa. Msamaha wa zambi ukatolewa kwa njia ya uombezi wa Kristo ndani ya Pahali patakatifu pa patakatifu mno,. Hapo kukingali na "mlango wazi" kwa Pahali patakatifu pa mbinguni, mahali Kristo alikuwa akifanya kazi kwa ajili ya mwenye zambi.

Sasa ikaonekana matumizi ya yale maneno ya Kristo katika Ufunuo, yanayosemwa kuelekea wakati huu kabisa: "Maneno haya anasema aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi; naye anayefungua wala hapana mtu anayefunga, naye anafunga wala hapana mtu anayefungua .... Tazama, nimekupa mlango wazi mbele yako na hakuna mtu anayeweza kuufunga." Ufunuo 3:7,8.

Wale ambao kwa imani wanamufuata Yesu katika kazi kubwa ya upatanisho wanapokea faida ya uombezi, huku wale wanaokataa nuru hawatapata faida. Wayuda waliokataa kuamini Kristo kama Mwokozi hawakuweza kupokea rehema kwake. Wakati Yesu

alipopanda mbinguni aliingia Pahali patakatifu pa mbinguni kutoa mibaraka ya upatanisho wake juu ya wanafunzi wake, Wayuda waliachwa katika giza kubwa kabisa kwa kuendelea na kafara zao zabure na sadaka. Mlango ambao watu walipata mbele kwa kupita na kumukaribia Mungu haukuwa wazi tena. Wayuda walikataa kumutafuta kwa njia moja tungaliweza kupatikana, ni kwa njia ya Pahali patakatifu pa mbinguni.

Wayuda wasioamini walionyesha uvivu na kutoamini kwa waliojidai kuwa Wakristo ambao kwa kweli hawajui kazi ya Kuhani wetu Mkuu. Katika kazi ya mfano, wakati kuhani mkuu alipoingia Pahali patakatifu pa patakatifu mno, Israeli yote ililazimishwa kukusanyika kwa Pahali patakatifu na kunyenyekeza roho zao mbele ya Mungu, ili waweze kupata rehema ya zambi na bila "kukatiliwa mbali" ya kusanyiko. Ni kwa maana gani tena siku hii ya mfano wa upatanisho ikiwa kwamba tunafahamu kazi ya kuhani wetu Mkuu na kujua kazi gani tunazo ombwa.

Ujumbe ulitumwa kutoka mbinguni kwa dunia katika siku za Noa, na wokovu wao ulitegemea namna gani walitendea ujumbe ule. Mwanzo 6:6-9, Waebrania 11:7. Katika wakati wa Sodomo, wote ila Loti pamoja na mke wake na mabinti wawili, wakateketezwa na
[208] moto uliotumwa chini kutoka mbinguni. Mwanzo 19. Vivyo hivyo katika siku za Kristo. Mwana wa Mungu akatangaza kwa Wayuda wasioamini: "Nyumba yenu imeachwa kwenu tupu." Matayo 23:38. Kutazama chini kwa siku za mwisho, nguvu isiyokuwa na mwisho ya namna moja inatangaza, kwa ajili ya wale ambao "hawakupokea upendo wa kweli, wapate kuokolewa". "Na kwa ajili ya hiyo Mungu anawaletea nguvu ya upotevu, hata waamini uwongo." 2 Watesalonika 2:10,11. Kwa sababu wanakataa mafundisho ya neno lake, Mungu anaondoa Roho yake na kuwaacha kwa udanganyifu wanaoupenda. Lakini Kristo akingali anaomba kwa ajili ya mwanadamu, na nuru itatolewa kwa wale wanaoitafuta.

Kupita kwa wakati katika mwaka 1844 ulifuatwa na jaribio kubwa kwa wale walioshika imani ya kuja kwa Yesu. Msaada wao ulikuwa nuru ambayo iliongoza mioyo yao kwa Pahali patakatifu pa mbinguni. Kwa namna walivyongojea na kuomba wakaona kwamba kuhani wao Mkuu alikuwa akiingia kwa kazi ingine ya huduma. Kumufuata kwa imani, wakaongozwa kuona vilevile kufungwa kwa kazi ya kanisa. Wakawa na maelezo kamili zaidi ya ujumbe wa

malaika wa kwanza na wa pili, na wakatayarishwa kupokea na kutoa kwa dunia onyo kubwa la malaika wa tatu wa Ufunuo 14.

[209] 

# 25 /SHERIA YA MUNGU ISIYOGEUKA

"Hekalu la Mungu likafunguliwa mbinguni na sanduku ya agano lake likaonekana." Ufunuo 11:19. Sanduku ya agano la Mungu linakuwa ndani ya Pahali patakatifu pa patakatifu, chumba cha pili cha Pahali patakatifu. Katika kazi ya hema ya duniani, ambayo ilitumiwa "katika mfano na kivuli cha vitu vya mbinguni," chumba hiki kilikuwa kikifunguliwa tu kwa Siku kubwa ya Upatanisho kwa ajili ya usafisho wa Pahali patakatifu. Kwa hivyo tangazo kwamba hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni na sanduku ya agano lake lilionekana linaonyesha kwa kufunguliwa kwa Pahali patakatifu pa patakatifu mno pa mbinguni katika mwaka 1844 ambapo Kristo aliingia kufanya kazi ya kumaliza upatanisho. Wale ambao katika imani walimufuata Kuhani wao Mkuu alipoingia kwa huduma yake katika Pahali patakatifu pa patakatifu mno, walitazama sanduku ya agano lake. Kwa namna walivyojifunza fundisho la Pahali patakatifu walipata kufahamu badiliko la kazi ya Mwokozi, na wakaona kwamba alikuwa sasa anahudumia mbele ya sanduku la Mungu.

Sanduku ndani ya hema duniani lilikuwa na vipande mbili vya mawe, ambapo sheria za Mungu ziliandikwa. Wakati hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni, sanduku ya agano lake ilionekana. Ndani ya Pahali patakatifu pa patakatifu mno mbinguni, sheria ya Mungu inatunzwa--sheria iliyosemwa na Mungu na kuandikwa kwa kidole chake juu ya vipande mbili vya mawe.

Wale waliopata kufahamu maana yake waliona, zaidi kuliko mbele, nguvu za maneno ya Mwokozi: "Hata mbingu na inchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja haitaondoka." Matayo 5:18. Sheria ya Mungu, ambayo ni ufunuo wa mapenzi yake, andiko la tabia yake, inapaswa kudumu milele.

Katika orodha ya Amri kumi kunakuwa amri ya Sabato. Roho ya Mungu ikaonyesha wale wanafunzi wa Neno lake lile kwamba walivunja kwa ujinga amri hii kwa kutojali siku ya pumziko ya Muumba. Wakaanza kuchunguza sababu ya kushika siku ya kwanza ya juma. Hawakuweza kupata ushahidi wo wote kwamba amri ya ine

iliondolewa mbali wala kwamba Sabato iligeuzwa. Wakatafuta kwa uaminifu kujua na kutenda mapenzi ya Mungu; sasa wakaonyesha uaminifu wao kwa Mungu kwa kushika Sabato yake takatifu.

Nguvu mingi ilifanywa kwa kuangusha imani ya waamini wa Adventiste. Hakuna mtu aliweza kushindwa kuona kwamba ukubali ule wa kweli juu ya Pahali patakatifu pa mbinguni unahusika na haki za sheria ya Mungu na Sabato ya amri ya ine. Hapa kulikuwa [210]
na siri ya upinzani uliokusudiwa juu ya maelezo wazi ya umoja wa Maandiko yanayofunua huduma ya Kristo ndani ya Pahali patakatifu pa mbinguni. Watu wakatafuta kufunga mlango ambao Mungu alifungua, na kufungua mlango ambao aliufunga. Lakini Kristo alifungua mlango wa huduma ya Pahali patakatifu pa patakatifu. Amri ya ine ilikuwa ndani katika sheria iliyotunzwa pale.

Wale waliokubali nuru juu ya upatanisho wa Kristo na sheria ya Mungu wakaona kwamba haya yalikuwa kweli ya Ufunuo 14, ambayo ni onyo la mara tatu kwa kutayarisha wakaaji wa dunia kwa ajili ya kuja kwa Bwana mara ya pili. (Tazama mwisho wa kitabu, Nyongezo). Tangazo "Saa ya hukumu yake imekuja "linatangaza kweli ambayo inapaswa kutangazwa hata upatanisho wa Mwokozi utakapoisha na atarudi kuchukua watu wake kwake mwenyewe. Hukumu ambayo ilianza katika mwaka 1844 inapaswa kuendelea hata kesi za wote zinapokwisha kukatwa, wote wahai na waliokufa; kwa sababu hiyo itaenea hata kwa kufungwa kwa rehema ya wanadamu.

Ili watu waweze kujitayarisha kusimama katika hukumu, ujumbe unawaagiza kuogopa Mungu, na kumutukuza," na kumwabudu yeye aliyefanya mbingu, na dunia na bahari na chemchemi za maji." Matokeo ya kukubali kwa ujumbe huu wa malaika watatu unatolewa: "Hapa ni uvumilivu wa watakatifu wanaoshika amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:7,12.

Kwa kujitayarisha kwa hukumu, watu wanapashwa kushika sheria ya Mungu, kipimo cha tabia katika hukumu. Paulo anasema: "Wote waliokosa wakiwa na sheria, watahukumiwa kwa sheria, ... katika siku ile Mungu atakapohukumu siri za watu ... kwa Yesu Kristo." "Wale wanaotenda sheria watakaohesabiwa haki." Imani ina maana sana ili kushika sheria ya Mungu; kwani "pasipo imani haiwezekani kumupendeza." "Kila tendo lisilotoka katika imani ni zambi." Waroma 2:12-16; Waebrania 11:6; Waroma 14:23.

Malaika wa kwanza aliita watu kwa "kuogopa Mungu, na kumutukuza" na kumwabudu yeye aliyefanya mbingu na dunia. Kwa kufanya hii, wanapaswa kutii sheria yake. Bila kutii hakuna ibada inayoweza kupendeza Mungu. "Kwa maana kupenda Mungu ni kushika amri zake." 1 Yoane 5:3; Tazama Mezali 28:9.

## Mwito kwa Kuabudu Muumba

Wajibu kwa kuabudu Mungu unaimarishwa juu ya kweli kwamba yeye ni Muumba. "Kujeni, tuabudu na kuinama; Tupige
[211] magoti mbele ya Bwana mwenye kutuumba." Zaburi 95:6; Tazama Zaburi 95:5; Zaburi 100:3; Isaya 40:25,26; 45:18.

Katika Ufunuo 14, watu wameitwa kuabudu Muumba na kushika amri za Mungu. Mojawapo ya amri hizi inaonyesha kwa Mungu kama Muumba: "Siku ya saba ni sabato kwa Bwana Mungu wako: ... Maana kwa siku sita Bwana akafanya mbingu na inchi, bahari na vyote vilivyo ndani yake, akapumzika siku ya saba. Kwa hivi Bwana akabariki siku ya sabato na kuitakasa." Kutoka 20:10,11. Sabato, Bwana anasema, ni "alama, ... mujue ya kuwa mimi ni Bwana Mungu wenu." Ezekieli 20:20. Kama Sabato ingeshikwa kwa wote, mtu angeweza kuongozwa kwa Muumba kama jambo la kuabudu. Hapo hapangalikuwa kamwe mwabudu sanamu, asiyesadiki (Mungu), wala kafiri. Kushika Sabato ni alama ya uaminifu kwa "yeye aliyefanya mbingu na dunia na bahari na chemchemi za maji." Ujumbe unaoagiza watu kuabudu Mungu na kushika amri zake utawaita kwa kipekee muwaite kushika amri ya ine.

Katika tofauti kuwa wale wanaoshika amri za Mungu na imani ya Yesu, malaika wa tatu anaonyesha kwa kundi lingine: "Mtu akiabudu nyama na sanamu yake, na kupokea chapa katika kipaji cha uso wake, ao katika mkono wake, yeye atakunywa mvinyo ya gazabu ya Mungu." Ufunuo 14:9,10. Ni nini inayokuwa mfano wa nyama, sanamu, chapa?

Unabii ambamo mifano hii inapatikana unaanza kwa Ufunuo 12. Joka yule aliyetafuta kuharibu Kristo kwa kuzaliwa kwake ilisemwa kuwa Shetani (Ufunuo 12:9); akavuta Herode kuua Mwokozi. Lakini mjumbe wa Shetani katika kufanya vita juu ya Kristo na watu wake kwa karne za kwanza ilikuwa ufalme wa Roma, ambamo upagani

ulikuwa ni dini iliyoshinda. Kwa hiyo joka ni, kwa namna ya pili, mfano wa Roma ya kipagani.

Katika Ufunuo 13 ni nyama mwingine, "mfano wa chui," ambaye joka akamupa "nguvu zake, na kiti chake cha ufalme na mamlaka nyingi." Mfano huu, kama vile Waprostanti wengi walivyoamini, unakuwa mfano wa dini ya Papa, iliyofuata kwa nguvu (mamlaka) na kiti cha ufalme na mamlaka iliyoshikwa kuanza na ufalme wa Roma. Juu ya nyama aliyekuwa na mfano wa chui inasemwa: "Naye akapewa kinywa cha kusema maneno makubwa, na makufuru... Akafungua kinywa chake atukane Mungu , na kutukana jina lake, na hema yake, nao wanaokaa mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda; akapewa mamlaka juu ya kabila na lugha na taifa." Ufunuo 13:5-7. Unabii huu, karibu kuwa sawasawa pamoja na maelezo ya pembe ndogo ya Danieli 7, unaonyesha bila [212]
shaka Kanisa la Kiroma.

"Akapewa mamlaka kufanya kazi yake miezi makumi ine na miwili"--miaka mitatu na nusu, ao siku 1260, ya Danieli 7--mda ambao nguvu (uwezo) za Papa zilipaswa kugandamiza watu wa Mungu. Mda huu kama ilivyotajwa katika sura zilizotangulia, ulianza na mamlaka ya kanisa la Roma (Papa), A.D. 538, na kumalizika katika mwaka 1798. Kwa wakati ule mamlaka ya Papa ikapata "kidonda cha kufa," na unabii ukatimia, "yeye anayepeleka katika kifungo atachukuliwa katika kifungo."

## Kuinuka kwa Mamlaka Mpya

Kwa jambo hili mfano mwingine umetangazwa: "Kisha nikaona mnyama mwingine akipanda juu toka dunia, naye alikuwa na pembe mbili, mfano wa Mwana-Kondoo." Ufunuo 13:11. Taifa hili ni mbalimbali na yale yaliyoonyeshwa chini ya mifano iliyotangulia. Falme kubwa zilizotawala dunia zilionyeshwa kwa nabii Danieli kama wanyama wa mawindo, waliopanda wakati "pepo ine za mbingu zilivuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa." Danieli 7:2. Katika ufunuo 17:15 malaika anaeleza kwamba maji yanafanyishwa na "Watu" na makutano ya mataifa na lugha". Upepo ni mfano wa mashindano (vita). Pepo ne zinazo shindana juu ya bahari kubwa inaonyesha matendo ya hatari ya ushindi na wapinduzi ambayo falme zilifika kwa enzi.

Lakini nyama aliyekuwa na pembe mfano wa Mwana-kondoo alionekana "akipanda toka dunia." Badala ya kuangusha mamlaka zingine na kujiimarisha mwenyewe, taifa lililokuwa mfano wake lilipaswa kupanda katika inchi isiokaliwa kwanza na likasitawi kwa amani. Linapaswa kutafutwa katika Bara kuu la Magaribi.

Ni taifa gani la Dunia Mpya lilikuwa katika mwaka 1798 likipanda kwa nguvu, kutoa ahadi ya nguvu, na kuvuta uangalifu wa dunia? Taifa moja, na ni moja tu, linalokutana na unabii huu--mataifa ya muungano ya Amerika (United States of America). Karibu sana maneno kabisa kabisa ya mwandishi mtakatifu yalitumiwa bila kufahamu kwa mwandishi wa historia katika kueleza kupanda kwa taifa. Mwandishi mashauri anasema juu ya "siri ya kutokea kwake kwa pahali patupu," na anasema, "Kama mbegu ya kimya tunasitawi katika mamlaka." Gazeti la Ulaya katika mwaka 1850 linaeleza juu ya Amerika "kutokea" na "katika utulivu wa inchi siku kwa siku kuongeza kwa uwezo wake na kiburi."

"Naye alikuwa na pembe mbili, mfano wa Mwana-Kondoo."
[213] Pembe mfano wa mwana-kondoo inaonyesha ujana, hali ya kuwa bila kosa, upole. Miongoni mwa Wakristo wa kwanza waliokimbilia Amerika kwa ajili ya magandamizo ya kifalme na kutovumilia kwa mapadri kulikuwa wengi waliokusudia kuanzisha uhuru wa kiulimwengu na wa dini. Tangazo la uhuru linainua kweli kwamba "watu wote wameumbwa sawasawa" na wanatolewa na haki ya daima kwa "maisha, uhuru, na kutafuta furaha." Sheria inatoa haki kwa watu ya kujitawala, kuhakikisha kwamba wajumbe waliochaguliwa kwa uchaguzi wa kupendwa na watu wote watafanya na kuamuru sheria. Uhuru wa imani ya dini ulitolewa pia. Utawala wa uchaguzi (Republicanism) ya Dini la Kiprotestanti yakawa kanuni za msingi za taifa, siri ya uwezo wake na usitawi. Mamilioni wakatafuta pwani zake, na Amerika ikapanda kwa pahali miongoni mwa mataifa yenye uwezo mwingi zaidi duniani.

Lakini nyama aliyekuwa na pembe mbili, mfano wa mwanakondoo "akasema kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake, na kufanya dunia nao wanaokaa ndani yake waabudu mnyama wa kwanza, ambaye kidonda chake cha mauti kilipona; ... akiwaambia wale wanaokaa juu ya dunia, kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na kidonda cha upanga, naye aliishi." Ufunuo 13:11-14.

Pembe mfano wa mwana-kondoo na sauti ya joka inaonyesha kwa mabishano. Utabiri kwamba itasema "kama joka" na kutumia "maneno kwa uwezo wote wa nyama yule wa kwanza" unatabiri roho ya kutokuwa na uvumilivu na ya kutesa. Na maneno kwamba mnyama aliyekuwa na pembe mbili "naye dunia alifanya" na wale wanaokaa ndani yake waabudu mnyama wa kwanza" inaonyesha kwamba mamlaka ya taifa hili ni kutumia nguvu kwa kushika maagizo fulani ambayo itakuwa tendo la heshima kwa utawala wa kipapa.

Tendo la namna hiyo lingekuwa kinyume kwa asili ya sheria zake za uhuru, kwa taratibu ya maneno ya kukiri Tangazo la Uhuru, na kwa sheria. Sheria inaweka tayari kwamba "Baraza kuu haitaweka sheria kupendelea makao ya dini, wala kukataza uhuru wa matumizi hiyo," na kwamba "hakuna jaribio la dini litakalodaiwa kamwe kama sifa kwa kazi yo yote ya tumaini la watu wote chini ya mataifa ya muungano (United States). Kuvunja wazi kwa kinga hizi (mambo yanayofanya salama) za uhuru kunaonyeshwa katika mfano huu. Mnyama aliyekuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondooanayejitangaza kuwa safi, mtulivu-asiyeumiza-anasema kama joka.

"Akiwaambia wale wanaokaa juu ya dunia, kumfanyia sanamu yule nyama." Hapa panaonyeshwa namna ya serkali ambapo mamlaka ya kufanya sheria inadumu kwa watu, ushuhuda wa kushangaza zaidi kwamba Amerika ni taifa lenye maana fulani. [214]

Lakini "sanamu kwa mnyama" ni nini? Namna gani inafanywa?

Wakati kanisa la zamani lilipochafuka, likatafuta msaada wa uwezo wa kidunia. Matokeo: Kanisa la Roma (Papa), kanisa lililotawala serkali, hasa zaidi sana kwa ajili ya azabu ya uzushi." Ili Amerika ipate kufanya ''sanamu ya mnyama," mamlaka ya dini inapaswa kutongoza serkali kwamba serkali itatumiwa vilevile kwa kanisa kutimiza vifiko vyake mwenyewe.

Makanisa ya Kiprotestanti yale yaliyofuata katika hatua za Roma yameonyesha mapenzi ya namna moja kwa kuzuia uhuru wa zamiri. Mfano ni mateso yaliyoendelea wakati mrefu ya wale wasiokubali mafundisho ya Kanisa la Kiingereza. Wakati wa karne za kumi na sita na kumi na saba, wachungaji na watu wasiokubali kanuni za kanisa walikuwa watu wakulipa feza ya azabu, kufungwa, mateso (azabu kali), na mauti ya mfia dini.

Uasi ukaongoza kanisa la mwanzoni kutafuta usaada wa serkali ya raia. Na jambo hili likatayarisha njia kwa Kanisa la Roma (Papa)--mnyama. Paulo akasema: "ila maasi yale yafike mbele, na mtu yule wa kuasi akafunuliwa." 2 Watesalonika 2:3.

Biblia inatangaza: "Siku za mwisho zitakuwa nyakati za hatari. Kwa sababu watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda feza, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na kushukuru, wasio safi, wasiopenda wenzao, wasiotaka kusamehe, washitaki wa uwongo, wasiojizuiza, wakali, wasiopenda mema, wadanganyifu, wakaidi, wenye kujivuna, wenye kupenda anasa kuliko Mungu; wenye mfano wa kuogopa Mungu, lakini wakikana nguvu zake." 2 Timoteo 3:1-5. "Basi, Roho anasema waziwazi ya kwamba katika nyakati za mwisho watu wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho za kudanganya, na mafundisho ya mashetani." 1 Timoteo 4:1.

Wote wale "hawakupokea mapendo wa kweli, kwamba wapate kuokolewa," watakubali "nguvu ya upotevu, hata waamini uwongo." 2 Watesalonika 2:10,11. Wakati hali hii itakapofikiwa, matokeo ya namna moja yatafuata ilivyokuwa katika karne za kwanza.

Tofauti kubwa ya imani katika makanisa ya Waprotestanti inazaniwa na wengi kama utibitizo kwamba hakuna umoja uliolazimishwa unaoweza kufanywa. Lakini pale kumekuwa kwa miaka nyingi katika makanisa ya Waprotestanti nia iliyoongezeka katika
[215] upendeleo wa umoja. Kwa kulinda umoja kama huo, mazungumzo ya mambo ambayo wote hawakuyakubali yanapaswa kuachwa kudaiwa. Katika bidii ya kulinda umoja kamili, itakuwa tu ni hatua kwa kutumia nguvu.

Wakati makanisa maalum ya Amerika, yanapoungana juu ya mambo kama yale ya mafundisho kama inavyoshikwa kwao katika umoja, yatavuta serkali kulazimisha amri zao na kuimarisha sheria zao, ndipo Amerika ya Kiprotestanti itakapofanya sanamu ya serkali ya Kanisa la Roma, na azabu ya malipo ya raia juu ya wale wasiokubali mafundisho ya kanisa bila mashaka yatakuwa matokeo.

## Mnyama na Sanamu Yake

Mnyama aliyekuwa na pembe mbili "naye anawafanya wote, wadogo na wakubwa, na matajiri na masikini na wahuru na wa-

fungwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, ao katika vipaji vya nyuso zao; na kwamba mtu asiweze kununua wala kuuza asipokuwa na chapa ile, ao jina la mnyama yule, ao hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16,17. Malaika wa tatu anaonya: "Mtu akiabudu mnyama na sanamu yake, na kupokea chapa katika kipaji cha uso wake, ao katika mkono wake, yeye atakunywa mvinyo ya gazabu ya Mungu."

"Mnyama" wa hiyo ibada inayolazimishwa ni wa kwanza, ao ya mfano wa chui, nyama wa Ufunuo 13--Kanisa la Roma (Papa). "Sanamu kwa mnyama" ni mfano wa namna ile ya Dini ya Kiprotestanti iliyokufuru ambayo itasitawi wakati makanisa ya Waprotestanti yanapotafuta msaada wa mamlaka ya serkali kwa ajili ya mkazo wa mafundisho ya kanuni zao. "Chapa ya nyama" inaendelea kuelezwa.

Wale wanaoshika amri za Mungu wanakuwa tofauti na wale wanaoabudu mnyama na sanamu yake na kupokea chapa yake. Uchungaji wa sheria ya Mungu, kwa upande moja, na mvunjo wake, kwa upande mwengine, utafanya tofauti kati ya waabudu wa Mungu na waabudu wa mnyama.

Tabia ya kipekee ya mnyama na ya sanamu yake ni kuvunja amri za Mungu. Asema Danieli, juu ya pembe ndogo, kanisa la Roma (Papa): "Atafikiri kugeuza nyakati na sheria." Danieli 7:25.R.V. Paulo akataja mamlaka ya namna moja "mtu yule wa kuasi" (2 Watesalonika 2:3), aliyejiinua mwenyewe juu ya Mungu. Ila tu kwa kugeuza sheria ya Mungu kanisa la Roma (Papa) liliweza kujiinua lenyewe juu ya Mungu. Mtu ye yote ambaye angeshika sheria kwa kufahamu kama ilivyogeuzwa angekuwa anatoa heshima kubwa kwa sheria za Papa, chapa cha utii kwa Papa pahali pa Mungu. [216]

Kanisa la Roma (Papa) limejaribu kugeuza sheria ya Mungu. Amri ya ine imebadilika hivi kama kuruhusu kushika siku ya kwanza badala ya siku ya saba kama Sabato. Badiliko la kusudi, la kufikiri linaonyeshwa: "Atafikiri kugeuza nyakati na sheria." Badiliko katika amri ya ine kabisa linatimiza unabii. Hapa uwezo wa Papa unajiweka mwenyewe kwa wazi juu ya Mungu. Waabudu wa Mungu watatofautika kwa kipekee kwa kushika kwao kwa amri ya ine, alama ya uwezo wake wa kuumba. Waabudu wa mnyama watatofautika kwa kufanya nguvu ili kupasua ukumbusho wa Muumba, kuinua sheria ya Roma. Ilikuwa kwa ajili ya Jumapili (siku ya kwanza) kama "siku ya Bwana" ambayo mafundisho ya kanisa la Roma yalitetea

kwa mara ya kwanza madai yake ya kiburi. (Tazama Mwisho wa kitabu, Nyongezo). Lakini Biblia inaonyesha siku ya saba kuwa siku ya Bwana. Akasema Kristo: "Basi, Mwana wa watu ndiye Bwana wa sabato vilevile." Marko 2:28. Utazame tena Isaya 58:13; Matayo 5:1719. Maneno yanayotangazwa mara kwa mara kwamba Kristo aligeuza Sabato yamekataliwa na maneno yake mwenyewe.

### Kimya Kamili wa Agano Jipya

Waprotestanti wanatambua "kimya kamili cha Agano Jipya kadiri hakuna agizo lo lote wazi kwa ajili ya Sabato (Jumapili, siku ya kwanza ya juma) wala kanuni halisi kwa kushikwa kwake zinazohusiana nayo."

"Hata kwa wakati wa kufa kwa Kristo, hakuna badiliko lililofanyika katika siku"; na "ni hivyo kama maandiko yanavyoonyesha, wao (mitume) ... hawakutoa agizo lo lote la wazi kuonyesha kuachwa kwa Sabato ya siku ya saba, na kushikwa kwake kwa siku ya kwanza ya juma."

Wakatoliki wa Roma wanatambua kwamba badiliko la Sabato lilifanywa na kanisa lao, na kutangaza kwamba Waprotestanti, kwa kushika Jumapili (siku ya kwanza ya juma), wanatambua mamlaka ya Roma. Maneno yamesemwa: "Wakati wa sheria ya kale, jumamosi (siku ya saba) ilikuwa siku iliyotakaswa; lakini kanisa, lilipoagizwa na Yesu Kristo, na kuongozwa na Roho ya Mungu, likabadilisha Jumapili (siku ya kwanza ya juma: Dimanche) kwa Jumamosi (siku ya saba ya juma:Samedi), kwa hiyo tunatakasa siku ya kwanza, si siku ya saba, Jumapili maana yake, na sasa ni, siku ya Bwana."

Kama alama ya mamlaka ya Kanisa la Wakatoliki, waandishi wa Kanisa la Roma wananena "Tendo kabisa la kugeuza Sabato
[217] kwa Jumapili (siku ya kwanza ya juma), ambalo Waprotestanti wanakubali; ... kwa sababu ya kushika Jumapili (siku ya kwanza ya juma), wanakubali mamlaka ya kanisa kwa kuamuru siku kuu, na kuzitawala chini ya zambi."

Ni nini tena badiliko la Sabato, lakini ni alama, ao chapa, cha mamlaka ya Kanisa la Roma--"chapa ya mnyama"?

Kanisa la Roma halikuacha madai yake kwa mamlaka. Wakati ulimwengu na makanisa ya Waprotestanti wanapokubali sabato ilio-

tungwa na Roma, wakati wanapokataa Sabato ya Biblia, wanakubali kwa kweli majivuno haya. Kwa kufanya vile wanazarau kanuni zinazowatenga kwa Roma--kwamba "Biblia, na ni Biblia tu, ni dini ya Waprotestanti." Kwa namna mwendo kwa ajili yakulazimisha Jumapili (siku ya kwanza ya juma) unapata upendeleo, mwishoni italeta Waprotestanti wote chini ya bendera ya Roma.

Wakristo wa Kanisa la Roma wanatangaza kwamba "kushika Jumapili (siku ya kwanza ya juma) kwa Waprotestanti ni heshima kuu wanatoa, kwa kujichukia wenyewe, kwa mamlaka ya Kanisa [la Katoliki]."7 Kwa kulazimisha kazi ya dini kwa mamlaka ya serkali ni kufanya sanamu kwa mnyama; kwa hiyo kulazimisha kushika Jumapili (siku ya kwanza ya juma) katika Amerika kungekuwa kulazimusha kuabudu ya mnyama na sanamu yake.

Wakristo wa vizazi vilivyopita walishika Jumapili (siku ya kwanza ya juma) wakizani kwamba walikuwa wakishika Sabato ya Biblia, sasa kunakuwa Wakristo wa kweli katika kila kanisa ambao kwa uaminifu wanaamini kwamba Jumapili (siku ya kwanza ya juma) ni agizo la kimungu. Mungu anakubali uaminifu wao na uhaki yao. Lakini wakati kushika Jumapili (siku ya kwanza ya juma) itakapolazimishwa kwa sheria na ulimwengu utaangaziwa juu ya Sabato ya kweli, ndipo ye yote atakayevunja amri ya Mungu kwa kutii amri ya Roma kwa hiyo atakuwa anaheshimu mafundisho ya kipapa kuliko ya Mungu. Anakuwa akitoa heshima kwa Roma. Anakuwa akiabudu mnyama na sanamu yake. Ndipo watu watapokea chapa cha utii kwa Roma--"chapa ya mnyama." Yale hayatafanyika hata mambo yanapowekwa wazi mbele ya watu na watakapoletwa kwa kuchagua kati ya amri za Mungu na amri za watu, ndipo wale wanaoendelea katika kuvunja amri watapokea "chapa ya mnyama."

## Onyo la Malaika wa Tatu

Hofu ya kutisha zaidi iliyoambiwa daima kwa wanadamu inakuwa katika ujumbe wa malaika wa tatu. Watu hawapaswi kuachwa [218]
gizani juu ya jambo hili la maana; onyo linapaswa kutolewa kwa ulimwengu kabla ya kuzuriwa kwa hukumu ya Mungu, ili wote waweze kuwa na bahati ya kuziepuka. Malaika wa kwanza anafanya tangazo lake kwa "kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa." Onyo la

malaika wa tatu ni la kuenea sana, linatangazwa kwa sauti kubwa na litaagiza uangalifu wa ulimwengu.

Wote watajitenga kwa makundi makubwa mawili--wale wanaoshika amri za Mungu na imani ya Yesu, na wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake na wanapokea chapa yake. Kanisa na Serkali itaungana kushurutisha "wote" kwa kupokea "chapa cha mnyama," kwani watu wa Mungu hawataipokea. Nabii anatazama "wale walioshinda yule nyama na sanamu yake, na hesabu ya jina lake, wamesimama kando ya bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu." Ufunuo 15:2.

# 26 /WASHUJAA KWA AJILI YA UKWELI [219]

Matengenezo juu ya sabato katika siku za mwisho yametabiriwa katika Isaya: "Bwana anasema hivi: Shikeni hukumu, na mufanye haki; kwa sababu wokovu wangu ni karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa. Heri mtu anayefanya maneno haya, na mwana wa mtu anayeyashika sana; anayeshika sabato asizivunje, anayezuiza mkono wake usifanye uovu wo wote... Vilevile wana wa mgeni, wanaojiunga na Bwana, kumutumikia, na kupenda jina la Bwana, kuwa watumishi wake, yeyote anayeshika sabato asiivunje, na kushika sana agano langu; hata wale nitawaleta kwa mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya maombi." Isaya 56:1,2,6,7.

Maneno haya yanaelekea kwa wakati wa kikristo, kama inavyoonyeshwa kwa maneno (mstari 8). Hapa ni kuonyesha mbele mkusanyiko wa Mataifa kwa njia ya habari njema, wakati watumishi wake wanapohubiri kwa mataifa yote habari za furaha.

Bwana anaamuru, "Tia muhuri juu ya sheria katikati ya wanafunzi wangu.: Isaya 8:16. Muhuri wa sheria ya Mungu unapatikana katika amri ya ine. Hii tu, ya amri zote kumi, inayoleta maoni ya jina na anwani ya Mutoa sheria. Wakati Sabato ilipogeuzwa kwa mamlaka ya Papa (kanisa la Roma), muhuri uliondolewa kutoka kwa sheria. Wanafunzi wa Yesu wanaitwa kwa kuurudisha kwa kuinua Sabato kama ukumbusho wa Muumba na alama ya mamlaka yake.

Agizo limetolewa: "Piga kelele, usiache, pandisha sauti yako kama baragumu, uhubiri watu wangu kosa lao." Wale ambao Bwana anawataja kama "watu wangu" wanapaswa kukaripiwa kwa ajili ya makosa yao, kundi linalojifikiri wao wenyewe kuwa la haki katika kazi ya Mungu. Lakini kemeo la upole la mwenye kutafuta mioyo linawashuhudia kuvunja amri za Mungu. Isaya 58:1,2.

Kwa hiyo nabii anaonyesha amri ambayo iliyoachwa: "Utanyanyulisha misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza pahali pa kubomoka; Mwenye kurudisha njia za kukalia. Kama ukigeuza mguu wako kutoka katika Sabato, usifanye

mapenzi yako katika siku yangu takatifu na kuita sabato siku ya furaha, siku takatifu ya Bwana, yenye heshima; kama ukiiheshimu, pasipo kufuata njia zako mwenyewe, wala kutafuta mapenzi yako mwenyewe, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utajifurahisha katika Bwana." Isaya 58:12-14.

"Tundu" lilifanywa katika sheria ya Mungu wakati Sabato ilipogeuzwa kwa mamlaka ya Roma. Lakini wakati umefika kwa
[220] tundu kutengenezwa.

Sabato ilishikwa na Adamu katika usafi wake katika Edeni; na Adamu, aliyeanguka lakini akatubu, wakati alipofukuzwa kwa shamba ao cheo chake. Ilishikwa na mababa wote tangu Abeli hata Noa, kwa Abrahamu, hata Yakobo. Wakati Bwana alipookoa Israeli, akatangaza sheria yake kwa makutano.

## Sabato ya Kweli Kila Mara Ilishikwa

Tangu siku ile hata sasa Sabato imeshikwa. Ingawa "mtu wa zambi" alifaulu katika kugandamiza chini ya mguu siku takatifu ya Mungu, lakini ilifichwa katika mahali pa siri roho aminifu zikaitolea heshima. Tangu wakati wa Matengenezo (Reformation), wengine katika kila kizazi wameimarisha kushikwa kwake.

Mambo haya ya kweli katika kuhusiana pamoja na "habari njema ya milele" yatatofautisha kanisa la Kristo kwa wakati wa kutokea kwake. "Hapa ni uvumilivu wa watakatifu wanaoshika amri za Mungu, na imani ya Yesu." Ufunuo 14:12.

Wale waliokubali nuru juu ya Pahali patakatifu na sheria ya Mungu walijazwa na furaha kwa namna walioona umoja wa kweli. Walitamani nuru ya kugawanywa kwa Wakristo wote. Lakini kweli tafauti pamoja na ulimwengu haikukaribishwa kwa wengi waliojidai kufuata Kristo.

Kwa namna haki ya Sabato ilivyoonyeshwa, wengi wakasema: "Tulikuwa tukishika Jumapili (siku ya kwanza) sikuzote, wazazi wetu waliishika. Kushika kwa Sabato mpya kungetutupa inje ya umoja pamoja na ulimwengu. Kundi ndogo linaloshika siku ya saba linaweza kufanya nini juu ya ulimwengu wote unaoshika Jumapili (siku ya kwanza ya juma)?" Kwa mabishano ya namna moja Wayuda wakatoa sababu zao za kukana Kristo. Vivyo hivyo wakati wa Luther, Wakristo wa dini ya Roma wakafikiri kwamba Wakristo wa

kweli walikufa katika imani ya Kikatoliki; kwa sababu hiyo dini ile ilikuwa ya kutosha. Wazo la namna ile lingehakikisha kizuizi zaidi kwa maendeleo yote katika imani.

Wengi walishurutisha kwamba kushika kwa Jumapili (siku ya kwanza ya juma) ilikuwa desturi ya kanisa iliyoenea sana ya kanisa kwa karne nyingi. Kinyume cha mabishano haya ilionyeshwa kwamba Sabato na kushikwa kwake kulikuwa kwa zamani zaidi kuliko, hata kwa zamani za ulimwengu wenyewe--uliyoimarishwa na Mzee wa Siku.

Kwa ukosefu wa ushuhuda wa Biblia, wengi wakashurutisha: "Sababu gani watu wetu wakubwa hawafahamu swali hili la Sabato? [221]
Wachache wanaamini kama unavyo amini. Haiwezekani kuwa kwamba unakuwa na hakika na watu wote waliojifunza kuwa wakosefu."

Kwa kupinga mabishano ya namna hii ilikuwa tu lazima ya kuita Maandiko na matendo ya Bwana pamoja na watu wake katika vizazi vyote. Sababu mara kwa mara Mungu hakuwa akichagua watu waliojifunza na cheo kwa kuongoza katika matengenezo ni kwamba wanatumainia kanuni za imani ya kanisa na desturi za elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini na kutoona haja kamwe ya kufundishwa na Mungu. Watu wanaokuwa na majifunzo ya chini wanaitwa nyakati zingine kutangaza kweli, si kwa sababu wanakuwa wasiojifunza, lakini kwa sababu si watu wenye majivuno ya kukataa kufundishwa na Mungu. Unyenyekevu wao na utii vinawafanya kuwa wakubwa.

Historia ya Israeli wa zamani ni onyesho la kushangaza ya mambo ya maisha ya wakati uliopita ya jamii ya Waadventisti. Mungu aliongoza watu wake katika mwendo wakurudi kwa Yesu,ijapo kama vile alivyoongoza wana wa Israeli kutoka Misri. Kama wote waliotumika kwa umoja katika kazi munamo mwaka 1844 wangepokea ujumbe wa malaika wa tatu na kuutangaza katika uwezo wa Roho Mtakatifu, miaka iliyopita ulimwengu ungekuwa umekwisha kuonywa na Kristo angekuwa amekwisha kuja kwa ajili ya ukombozi wa watu wake.

## Si Mapenzi ya Mungu

Haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba Israeli azunguke zunguke miaka makumi ine jangwani; alitamani kuwaongoza mara moja kwa

Kanana na kuwaimarisha kule, watu watakatifu na wafuraha. Lakini "hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao." Waebrania 3:19. Ni namna ileile, haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba kuja kwa Kristo kupate kuchelewa wakati mrefu na watu wake wadumu miaka mingi sana duniani hii ya zambi na huzuni. Kutoamini kukawatenga kwa Mungu. Katika rehema kwa ulimwengu, Yesu akakawisha kuja kwake, ili wenye zambi wasikie onyo na kupata kimbilio kabla ya hasira ya Mungu kumiminika.

Sasa kama katika vizazi vya kwanza, kutangazwa kwa ukweli kutaamsha upinzani. Wengi kwa kijicho wanashambulia tabia na makusudi ya wale wanaosimama katika kutetea ukweli usiopendwa na wengi. Elia alitangazwa kuwa mwenye kuleta taabu katika Israeli. Yeremia msaliti, Paulo mwenye kuchafua hekalu. Tangu siku ile hata
[222] leo, wale ambao wangekuwa waaminifu kwa kweli wameshitakiwa kuwa kama wafitini, wajushi, ao wenye kutengana.

Kukiri kwa imani kulikofanywa na watakatifu na wafia dini, mifano hiyo ya utakatifu ukamilifu imara, kunatia moyo ndani ya wale wanaoitwa sasa kusimama kama washahidi kwa ajili ya Mungu. Kwa mtumishi wa Mungu kwa wakati huu kunaagizo linalosema: "Paza sauti yako kama baragumu, uhubiri watu wangu kosa lao, na nyumba ya Yakobo zambi zao." "Nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; kwa hivi sikia neno kwa kinywa changu, na uwape maonyo toka kwangu." Isaya 58:1; Ezekieli 33:7.

Kizuizi kikubwa kwa kukubali kweli ni kwamba inahusika na taabu na laumu. Hii ni mabishano tu kinyume cha ukweli ambayo wateteaji wake hawakuweza kamwe kupinga. Lakini wafuasi wa kweli wa Kristo hawangojei ukweli kukubaliwa na watu wengi. Wanakubali msalaba, pamoja na Paulo kuhesabu kwamba "Mateso yetu mepesi yaliyo kwa dakika tu, yanatufanyia utukufu wa milele unaouzito mwingi"; pamoja na mmoja wa zamani, "akihesabu ya kuwa kulaumiwa kwa Kristo ni utajiri mwingi kuliko hazina za Misri." 2 Wakorinto 4:17; Waebrania 11:26.

Inatupasa kuchagua haki kwa sababu inakuwa haki, na kuacha matokeo kwa Mungu. Kwa watu wa kanuni, imani na uhodari, dunia inakuwa na deni kwa ajili ya matengenezo yake makubwa. Kwa watu wa namna ile kazi ya matengenezo kwa wakati huu inapashwa kuendelea mbele.

# 27 /UFUFUO WA KISASA UNAKUWA NA MAFANIKIO NAMNA GANI? [223]

Popote Neno la Mungu lilipohubiriwa kwa uaminifu, matokeo yaliyofuata ni ya kushuhudia asili yake ya kimungu. Wenye zambi walijisikia zamiri zao kuamka. Hakikisho la kosa likashikilia nia zao na mioyo yao. Walikuwa na utambuzi wa haki ya Mungu, na wakapaza sauti: "Nani atakayeniokoa na mwili huu wa kufa?" Waroma 7:24. Kama vile msalaba ulivyofunuliwa, waliona kwamba hakuna kitu kingine bali tabia nzuri tu za Kristo ziliweza kupatanisha kwa ajili ya makosa yao. Kwa damu ya Yesu walikuwa na "ondoleo la zambi zile zilizopita." Waruma 3:25.

Roho hizi zikaamini na zikabatizwa na wakasimama kwa kutembea katika upya wa uzima, kwa imani ya Mwana wa Mungu kwa kufuata hatua zake, kuonyesha tabia yake, na kujitakasa wao wenyewe kama yeye ni mutakatifu. Vitu walivyokuwa wakichukia sasa wakavipenda, na vile walivyokuwa wakipenda wakavichukia. Mwenye kiburi akawa mpole, mtu asiyefaa na wa kujivuna akawa wa maana na mnyenyekevu. Mlevi akawa mwenye busara, mpotovu akawa mtakatifu. Wakristo hawakutafuta "kujipamba kwa kusuka nywele, na kuvaa vitu vya zahabu, ao kuvaa mavazi; lakini ... katika mapambo yasiyoharibika, ndiyo roho ya upole na utulivu iliyo ya damani kubwa mbele ya Mungu." 1 Petro 3:3,4.

Maamsho yaliamshwa na miito ya upole kwa mwenye zambi. Matunda yalionekana katika roho zilizojitenga si kwa kujikana mwenyewe bali wakafurahi kwamba walihesabiwa kustahili kuteswa kwa ajili ya Kristo. Watu wakaona badiliko katika wale waliotangaza jina la Yesu. Ni vile mambo yalivyokuwa katika miaka ya kwanza iliofuata nyakati za uamsho wa dini.

Lakini maamsho mengi ya nyakati za kisasa yanaonyesha tofauti kubwa. Ni kweli kwamba wengi wanatangaza toba, na wengi wanaingia ndani ya makanisa. Hata hivyo matokeo si ya namna kama ya kushuhudia imani kwamba hapo kumekuwa na maendeleo

ya kulingana ya maisha ya kiroho ya kweli. Nuru ambayo inawaka kwa muda ikafa kwa upesi.

Maamsho ya watu wengi mara nyingi yanaamsha sikitiko, hupendeza watu kwa kitu kinachokuwa kipya na cha kwanza. Kwa hivyo wale waliogeuka wanakuwa na haja kidogo kusikiliza kweli ya Biblia. Isipokuwa hudumu ya kanisa inakuwa na kitu cha tabia ya ajabu, kama si vile, haina mvuto kwao.

[224] Kwa kila roho iliyogeuka kweli uhusiano kwa Mungu na kwa vitu vya milele utakuwa ni kitu kikubwa chakuzungumuziwa katika maisha. Ni pahali gani katika makanisa ya watu wengi ya leo kunapatikana roho ya kujitoa kwa Mungu? Waliogeuka hawaache kiburi na mapendo ya dunia. Hawakubali tena kuikana nafsi na kufuata Yesu mpole na mnyenyekevu kuliko mbele ya toba yao. Utawa karibu kutoka kwa wengi wa makanisa.

Ijapo imani ilipunguka mahali pengi sana, kunakuwa wafuasi wa kweli wa Kristo katika makanisa haya. Kabla ya kufika kwa hukumu za Mungu za mwisho, kutakuwa katikati ya watu wa Bwana uamsho wa utawa wa zamani za mababu ambao haujashuhudiwa tangu nyakati za mitume. Roho ya Mungu itamwangiwa. Wengi watajitenga kwa makanisa hayo ambayo mapendo ya dunia hii yaliondoa upendo kwa Mungu na Neno lake. Wahubiri wengi na watu watakubali kwa furaha zile kweli kubwa ambazo zinatayarisha watu kwa kuja kwa Bwana mara ya pili.

Adui wa roho anataka kuzuia kazi hii, na kabla ya kufika kwa mwenendo wa namna hiyo, atafanya nguvu kuuzuia kwa njia ya kuingiza mwigo. Katika makanisa yale ambayo anaweza kuleta chini ya mamlaka yake ataifanya kuonekana kwamba baraka ya kipekee ya Mungu imemwangwa juu yao. Makutano yatashangilia, "Mungu anatumika kwa ajabu," wakati ile kazi ni ya roho ingine. Chini yamtindo wa dini, Shetani atatafuta kueneza mvuto wake kwa ulimwengu wa Wakristo. Hapo kunakuwa mwamsho wa maono, mchanganyiko wa kweli na uwongo, uliotengenezwa vizuri sana kwa kudanganya.

Lakini katika nuru ya Neno la Mungu si vigumu kutambua tabia ya kazi hizi. Pahali pote watu wanapozarau ushuhuda wa Biblia, kugeukia mbali na hizi zilizo zaili zinazo jaribu roho ambazo zinaomba kujikana mwenyewe na kukana dunia, hapo tunaweza kuwa na hakika kwamba baraka ya Mungu haikutolewa. Na kwa

amri, “Mutawatambua kwa njia ya matunda yao,” (Matayo 7:16), ni ushuhuda kwamba kazi hizi si kazi ya Roho ya Mungu.

Ukweli ya Neno la Mungu inakuwa ngao juu ya madanganyo ya Shetani. Kuzarau kweli hizi kulifungua mlango kwa maovu yanayoenea sasa katika ulimwengu. Umuhimu wa sheria ya Mungu umesahauliwa kwa eneo kubwa sana. Wazo mbaya juu ya sheria ya Mungu limeongoza kwa makosa katika toba na utakaso, kwa kushusha kipimo cha utawa. Hapa ndipo panapopatikana siri ya ukosefu wa Roho ya Mungu katika maamsho ya wakati wetu.

## Sheria ya Uhuru [225]

Waalimu wengi wa dini wanatetea kwamba Kristo kwa mauti yake aliondoa sheria. Wengine wanaionyesha kama kongwa mzito wa kuhuzunisha, na kwa kinyume “utumwa” wa sheria walioonyesha “uhuru” wa kufurahia chini ya habari njema.

Lakini si vile manabii na mitume walivyofanya mbele ya sheria takatifu ya Mungu. Akasema Dawidi: “Na nitatembea huru kwa kuwa nimetafuta maagizo yako.” Zaburi 119:45. Mtume Yakobo anatumia Amri kumi kama “sheria .kamili, ya uhuru.” Yakobo 1:25. Mfumbuzi anatangaza baraka juu yao “wanaoshika amri zake (wanaofua nguo zao), wawe na haki ya kula mti wa uzima, na kuingia katika mji kwa milango yake.” Ufunuo 22:14.

Kama ingewezekana kwa sheria kugeuzwa ao kuwekwa pembeni, Kristo hangehitaji kufa kwa kuokoa mtu kwa azabu ya zambi. Mwana wa Mungu alikuja “kutukuza sheria na kuifanyiza kuwa na heshima.” Isaya 42:21. Akasema: “Musizanie nilikuja kuharibu torati”; “hata mbingu na inchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja haitaondoka, hata yote yatimie.” Juu yake mwenyewe akasema: “Ninafurahi kufanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu; Ndiyo, sheria yako ni moyoni mwangu.” Matayo 5:17,18; Zaburi 40:8.

Sheria ya Mungu haibadilike, ufunuo wa tabia ya Muumba wake. Mungu ni mapendo, na sheria yake ni mapendo. “Mapendo ni utimilifu wa sheria.” Asema mwandishi wa Zaburi: “Na sheria yako ni kweli”; “maana maagizo yako yote ni haki.” Paulo anasema: “Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki na njema.” Waroma 13:10; Zaburi 119:142,172; Waroma 7:12. Sheria kama

hiyo inapaswa kuwa ya kuendelea kama Muumba wake. Ni kazi ya toba na utakaso kwa kupatanisha watu kwa Mungu kwa njia ya kuwapatanisha katika umoja pamoja na kanuni za sheria. Katika mwanzo, mutu alikuwa katika umoja kamili pamoja na sheria ya Mungu. Lakini zambi ikamtenga kwa Muumba wake. Moyo wake ulikuwa kwa vita juu ya sheria ya Mungu. "Kwa sababu nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi." Waroma 8:7. Lakini "Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee," ili mutu aweze kupatanishwa kwa Mungu, kurudishwa kwa umoja pamoja na Muumba wake. Badiliko hili ni kuzaliwa kupya, isipokuwa hivyo "hawezi kuona ufalme wa Mungu." Yoane 3:16,3.

[226]

## Kukubali Zambi

Hatua ya kwanza kwa upatanisho na Mungu ni kukubali zambi. "Zambi ni uasi (wa sheria)." "Kwa njia ya sheria zambi inajulikana." 1 Yoane 3:4; Waroma 3:20. Ili kuweza kuona kosa lake, mwenye zambi anapaswa kupima tabia yake kwa kioo cha Mungu kinachoonyesha ukamilifu wa tabia ya haki na kumwezesha kutambua pungufu ndani yake mwenyewe.

Sheria inafunulia mtu zambi zake, lakini haitoi dawa. Inatangaza kwamba kifo ni sehemu ya mkosaji. Injili ya kristo peke yake inaweza kumweka huru kwa hukumu ao uchafu wa zambi. Anapashwa kuzoea kutubu mbele ya Mungu, kwa sheria yake iliyovunjwa, na imani katika Kristo, kafara ya upatanisho wake. Kwa hivyo anapata "ondoleo la zambi zile zilizopita" (Waroma 3:25) na anakuwa mwana wa Mungu.

Je, sasa anakuwa huru kuvunja sheria ya Mungu? Asema Paulo: "Basi, tunafanyiza sheria kuwa bule kwa njia ya imani? Hapana, hata kidogo; lakini tunasimamisha sheria." "Sisi tuliokufia zambi, namna gani tutakaa ndani yake tena?" Yoane anasema: "Kwa maana kupenda Mungu ni kushika amri zake; na amri zake si nzito." Katika kuzaliwa kupya moyo unaletwa katika umoja pamoja na Mungu, katika upatano pamoja na sheria yake. Wakati badiliko hili linafanyika ndani ya mwenye zambi amepita toka mauti hata katika uzima, kutoka kwa kosa na uasi hata kwa utii na uaminifu. Maisha ya zamani yameisha; maisha mapya ya upatanisho, imani,

na mapendo yameanza. Basi “haki ya sheria” “vita itimizwa ndani yetu, tusiotembea kufuata maneno ya mwili, lakini kufuata maneno ya Roho.” Lugha ya nafsi itakuwa: “Ee ninapenda sana sheria yako! Ni mawazo yangu muchana kutwa.” Waroma 3:31; 6:2; 1 Yoane 5:3; Waroma 8:4; Zaburi 119:97.

Bila sheria, watu hawakubali kweli zambi yao na hawaone haja ya kutubu. Hawafahamu moyoni mahitaji yao ya damu ya upatanisho wa Kristo. Tumaini la wokovu limekubaliwa bila badiliko la asili ya moyo wala matengenezo ya maisha. Hivi mabadiliko ya kijuujuu inajaa, na makutano yanaungana na kanisa ambayo hawakuwa wenye kuungama na Kristo.

## Utakaso ni Nini?

Maelezo yenye makosa juu ya utakaso pia yanaonekana kwa kutojali wala kukana kwa sheria ya Mungu. Maelezo haya, ya uwongo katika mafundisho na ya hatari katika matokeo ya maisha, kwa kawaida yanapata kibali. [227]

Paulo anatangaza, “Maana haya ni mapenzi ya Mungu, hata utakaso wenu.” Biblia inafundisha wazi wazi utakaso ni nini na namna gani unaweza kufikiwa. Mwokozi aliombea wanafunzi wake: “Uwatakase kwa kweli; neno lako ni kweli.” Na Paulo anafundisha kwamba waaminifu wanapashwa “kutakaswa na Roho Mtakatifu.’ ‘ 1 Watesalonika 4:3; Yoane 17:17; Waroma 15:16.

Kazi ya Roho Mtakatifu ni nini? Yesu akawambia wanafunzi wake: “Lakini wakati anapokuja yule Roho wa kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli.” Yoane 16:13. Na mwandishi wa Zaburi anasema: “Sheria yako ni ya kweli.” Kwa hivi sheria ya Mungu ni “takatifu na ya haki na njema,” tabia iliyofanywa kwa utii kwa sheria ile itakuwa takatifu. Kristo aliye mufano kamili wa tabia ya namna ile Anasema: “Nimeshika amri za Baba yangu.” “Ninafanya saa zote mambo yanayomupendeza.” Yoane 15:10; 8:29. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa kama yeye--kwa neema ya Mungu kufanya tabia katika umoja pamoja na kanuni za sheria yake takatifu. Huu ni utakaso wa Biblia.

## Ila tu Kwa Njia ya Imani

Kazi hii inaweza kutimizwa tu kwa njia ya imani katika Kristo, kwa uwezo wa kukaa ndani ya Roho ya Mungu. Mukristo atajisikia mwenye mivuto ya zambi, lakini atashikilia vita isiyobadilika juu yake. Hapa ndipo msaada wa Kristo unahitajiwa. Uzaifu wa binadamu unaambatana na nguvu za kimungu, na imani inapaza sauti: "Asante kwa Mungu anayetupa sisi ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorinto 15:57.

Kazi ya utakaso ni ya kuendelea mbele. Wakati katika toba mwenye zambi anapopata amani pamoja na Mungu maisha ya Mukristo imeanza tu. Sasa anapashwa kuendelea katika ukamilifu," kukua "hata kufika kipimo cha kimo cha wa utimilifu wa Kristo." "Ninakaza mwendo hata nifikie mwisho wa zawabu ya mwito mukubwa wa Mungu katika Kristo Yesu." Waebrania 6:1; Waefeso 4:13; Wafilipi 3:14.

Wale wanaozoea maisha ya utakaso wa Biblia wataonyesha unyenyekevu. Wanaona kutostahili kwao wenyewe katika tofauti pamoja na ukamilifu wa Mungu. Nabii Danieli alikuwa mufano wa utakaso wa kweli. Badala ya kujitangaza kuwa safi na mtakatifu, nabii huyu wa heshima akajitambulisha mwenyewe pamoja na wenye zambi wa kweli wa Israeli wakati alipokuwa akimlilia Mungu
[228] kwa ajili ya watu wake. Danieli ; 9:15,18,20; 10:8,11.

Hapawezi kuwa kujiinua mwenyewe, hapana madai ya kujisifu kwa uhuru wa zambi kwa upande wa wale wanaotembea katika kivuli cha msalaba wa Kalvari. Waliona kwamba ilikuwa ni zambi yao ambayo ilianzisha maumivu makuu yaliyovunja moyo wa Mwana wa Mungu, na wazo hili litaongoza kwa kujinyenyekeza. Wale wanaoishi karibu sana na Yesu wanatambua wazi zaidi uzaifu na hali ya zambi ya wanadamu, na tumaini lao moja tu linakuwa katika tabia nzuri ya Mwokozi aliyesulibiwa na kufufuka.

Utakaso sasa unaoendelea mbele kwa sifa katika watu wa dini unaeneza roho ya kujiinua na kutojali kwa sheria ya Mungu ambayo inauonyesha kama jambo la kigeni kwa Biblia. Watetezi wake hufundisha kwamba utakaso ni kazi ya dakika moja, ambayo, katika "imani tu," wanafikia utakatifu kamili. "Uamini tu," wanavyosema, "na mibaraka ni yako." Hapana juhudi ya zaidi kwa upande wa mwenye kupokea inayopashwa kufanywa. Kwa wakati ule ule

wakakataa mamlaka ya sheria ya Mungu, kushurutisha kwamba wamewekwa huru kwa kanuni ya kushika amri. Lakini inawezekana kuwa mutakatifu pasipo kuja katika umoja na kanuni ambazo zinaonyesha tabia ya Mungu na mapenzi yake?

Ushuhuda wa Neno la Mungu unakuwa kinyume cha mafundisho haya ya mtego ya imani pasipo matendo. Si imani inayotafuta kibali cha Mungu bila kushika tabia inayohitajiwa kwa ajili ya rehema ya kutolewa. Ni kiburi. Tazama Yakobo 2:14-24.

Hebu watu wasijidanganye wenyewe kwamba wanaweza kuwa watakatifu wanapovunja kwa makusudi mojawapo ya matakwa ya Mungu. Zambi inayojulikana inanyamazisha ushuhuda wa sauti ya Roho na inatenga nafsi toka kwa Mungu. Ingawa Yoane alidumu kabisa juu ya mapendo, hakusita kufunua tabia ya kweli ya kundi linalojidai kuwa takatifu wakati wanapoishi katika kuvunja sheria ya Mungu. "Yeye anayesema; Nimemujua, wala hashiki amri zake, ni mwongo, wala kweli si ndani yake. Lakini yeye anayeshika neno lake, katika huyu mapendo ya Mungu yamekamilishwa kweli kweli." 1 Yoane 2:4,5. Hapa kuna jaribio ya ushuhuda wa kila mtu. Kama watu wanapungua na kuzarau amri za Mungu, kama "wakivunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kufundisha watu hivyo" (Matayo 5:18,19), tunaweza kujua kwamba madai yao hayana msingi.

Kusema hana zambi ni ushuhuda kwamba yeye anatangaza haya anakuwa mbali kwa utakatifu. Hana wazo la kweli la usafi usiokuwa na mwisho na utakatifu wa Mungu, na uovu na ubaya wa zambi. Zaidi anajitenga mbali kwa Kristo,zaidi anajiona yeye mwenyewe [229]
kuwa mwema.

### Utakaso wa Biblia

Utakaso unahusu hali kamili ya mtu--roho, nafsi, na mwili. Tazama 1 Watesalonika 5:23. Wakristo wanaalikwa kutoa miili yao, "iwe zabihu iliyo hai, takatifu, ya kupendeza Mungu." Waroma 12:1. Kila desturi yo yote inayozoofisha nguvu za mwili ao akili inaondolea mtu uwezo kwa kazi ya Muumba. Wale wanaompenda Mungu kwa moyo wao wote watatafuta daima kuleta nguvu zote za maisha yao kwa umoja pamoja na sheria zinazoendeleza nguvu zao kwa kufanya mapenzi yake. Hawatalegeza wala kuchafua sadaka

wanayotoa kwa Baba wao wa mbinguni kwa anasa ya tamaa wala ulafi.

Furaha yote ya zambi inaelekea kuzoofisha na kuua fahamu za akili na za kiroho; Neno wala Roho ya Mungu inaweza kufanya mguso mdogo kwa moyo. "Tujisafishe wenyewe kwa uchafu wote wa mwili na wa roho, tukitimiza utakatifu katika woga wa Mungu." 2 Wakorinto 7:1.

Ni wangapi wanaojitangaza kuwa Wakristo wanaoharibu sura yao ya kimungu kwa ulafi, kwa kunywa mvinyo, kwa anasa zilizokatazwa. Na kanisa vivyo hivyo hushawishi uovu, kwa kujaza tena mali yake ambayo mapendo kwa Kristo ni zaifu sana kutoa. Kama Kristo angeingia kwa makanisa ya leo na kutazama karamu iliyofanywa pale kwa jina la dini, je, hangalifukuza wale wakufuru, kama alivyofukuzia mbali wabadili feza kwa hekalu?

"Hamujui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, muliyepewa na Mungu? Na ninyi si mali yenu wenyewe; kwa sababu mulinunuliwa kwa bei; basi tukuzeni Mungu katika mwili wenu na katika roho yenu, maana ni ya Mungu." 1 Wakorinto 6:19,20. Yeye ambaye mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu hatafanywa mtumwa wa desturi mbaya. Nguvu zake ni za Kristo. Mali yake ni ya Bwana. Namna gani angetapanya hazina uliyo gabiziwa?

Wanaojitangaza kuwa Wakristo kila mwaka wanatumia feza nyingi kwa anasa mbaya. Mungu wanamuiba kwa zaka na sadaka, wanapoteketeza kwa mazabahu ya tamaa mbaya ya kuharibu zaidi kuliko wanavyotoa kwa kusaidia maskini ao kusaidia maendeleo ya habari njema. Kama wote wanaoshuhudia Kristo wangetakaswa kwa kweli, mali yao, badala ya kuitumia kwa anasa za bure na zenye hasara, yangerudishwa katika hazina ya Bwana. Wakristo wangetoa mufano wa kiasi na kujitoa kafara. Ndipo wangekuwa
[230] nuru ya ulimwengu.

"Tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha maisha" (1 Yoane 2:16) zinatawala wingi wa watu. Lakini wafuasi wa Kristo wanakuwa na mwito takatifu. "Tokeni katikati yao, mukatengwa nao, Bwana anasema, wala musiguse kitu kisicho safi." Kwa wale wanaokubali pamoja na mapatano, ahadi za Mungu ni "Nitakuwa baba kwenu, nanyi mutakuwa kwangu wana na binti, Bwana Mwenyezi anasema." 2 Wakorinto 6:17,18.

Kila hatua ya imani na utii inaleta nafsi kwa uhusiano wa karibu sana na Nuru ya Ulimwengu. Mwangaza safi wa Jua la Haki unaangazia juu ya watumishi wa Mungu, na wanapaswa kurudisha mishale ya nuru yake. Nyota zinatwambia kwamba hapo kuna nuru katika mbingu na kwa utukufu wake zinangaa; kwa hivi Wakristo wanaonyesha kwamba hapo kuna Mungu kwa kiti cha enzi ambaye tabia yake ni bora ya sifa na ya kuiga. Utakatifu wa tabia yake utaonyeshwa katika ushuhuda wake.

Katika sifa njema za Kristo tunakuwa na ruhusa ya kukaribia kwa kiti cha Mwenye uwezo usio na mwisho (Mungu). "Yeye asiyeachilia Mwana wake, lakini alimutoa kwa ajili yetu zote, namna gani atakosa kututolea vitu vyote pamoja naye?" Yesu asema: "Kama ninyi mulio wabaya munajua kuwapa watoto wenu zawadi njema, si zaidi Baba yenu aliye katika mbingu atawapa wote wanaomwomba Roho Mtakatifu?" "Kama mukiomba neno gani kwa jina langu, nitalifanya." "Mwombe, na mutapata, furaha yenu itimizwe." Waroma 8:32; Luka 11:13; Yoane 14:14; 16:24.

Ni heshima ya kila mumoja kuishi ambako Mungu atakao kubali na kubarikia. Si mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni ya kuwa tupate kuwa chini ya hukumu na giza. Hapo hakuna ushuhuda wa unyenyekevu wa kweli katika kwenda pamoja na kichwa cha kuinama chini na moyo unaojaa na mawazo ya uchoyo. Tunaweza kwenda kwa Yesu na kutakaswa na kusimama mbele ya sheria pasipo haya na majuto.

Katika Yesu wana wa Adamu walioanguka wanakuwa "wana wa Mungu." Kwa sababu hii haoni haya kuwaita ndugu zake." Maisha ya mkristo yanapaswa kuwa yale ya imani moja, ushindi, na furaha katika Mungu. "Maana furaha ya Bwana ni nguvu zenu." "Furahini siku zote. Ombeni pasipo kuacha. Katika maneno yote mushukuru; maana maneno haya ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu." Waebrania 2:11; Nehemia 8:10; 1 Watesalonika 5:16-18.

Haya ndiyo yanavyokuwa matunda ya toba ya Biblia na utakaso; na ni kwa sababu ya kanuni kubwa za haki zilizo wekwa katika sheria [231]
zinaangaliwa kwa kutojali kwamba matunda haya yanashuhudiwa kwa shida. Hii ndiyo sababu hapo kunaonyeshwa kidogo sana kazi nyingi ile, yenye kudumu ya Roho ambayo iliyoonyesha maamsha ya kwanza.

Ni kwa kutazama ile tunakuwa wenye kubadilika. Wakati amri hizo takatifu ambamo Mungu amefungulia watu ukamilifu na utakatifu wa tabia yake zimezarauliwa, na akili za watu zimevutwa kwa mafun-disho na maelezo ya watu, hapo kulifuatwa na upungufu wa utawa katika kanisa. Ni wakati tu sheria ya Mungu imerudishwa kwa hali yake ya haki ndipo pale panaweza kuwa na muamsho wa imani ya zamani za kwanza na utawa miongoni mwa watu wake wanaojulikana.

# 28 /KUSIMAMA MBELE YA HABARI YA MAISHA YETU ZILIZOANDIKWA [232]

"Nikaangalia hata viti vya enzi vilipowekwa, na mmoja aliye mzee wa siku akaketi: mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi, kiti chake cha enzi kilikuwa ndimi za moto, na magurudumu yake moto unaowaka. Na mto wa moto ukatoka, ukapita mbele yake, elfu ya maelfu wakamutumikia, na elfu kumi mara elfu kumi walisimama mbele yake: hukumu ikawekwa, vitabu vikafunguliwa." Danieli 7:9,10. R.V.

Ndivyo ilivyoonyeshwa kwa njozi ya Danieli siku kubwa wakati maisha ya watu inapopita katika mkaguo mbele ya Mwamzi wa dunia yote. Mzee wa Siku ni Mungu Baba. Yeye, chemchemi ya viumbe vyote,kisima cha sheria yote, anapaswa kuongoza katika hukumu. Na malaika watakatifu kama wahuduma na washuhuda, wanahuzuria.

"Na tazama, pamoja na mawingu ya mbingu alikuja mmoja aliye mfano wa mwana wa watu, akakaribia huyu Mzee wa Siku, wakamuleta karibu mbele yake. Akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wote, mataifa yote, na lugha zote wamutumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, isiyopita kamwe, na ufalme wake ufalme usioweza kuangamizwa." Danieli 7:13,14.

Kuja kwa Kristo kunakoelezwa hapa si kuja kwake kwa mara ya pili duniani. Anakuja kwa Mzee wa Siku katika mbingu kupokea ufalme ambao utatolewa kwake wakati wa mwisho wa kazi yake kama mpatanishi. Ni kuja huko, na si kuja kwake kwa mara ya pili dunianini, ile iliyopashwa kufanyika kwa mwisho wa siku 2300 katika mwaka 1844. Kuhani wetu Mkuu anaingia Pahali patakatifu pa patakatifu kushughulika katika kazi yake ya mwisho kwa ajili ya mtu.

Katika huduma ya mfano ila wale ambao zambi zao zilihamishwa kwa Pahali patakatifu walikuwa na sehemu katika Siku ya Upatanisho. Vivyo hivyo katika upatanisho kubwa wa mwisho na hukumu ya uchunguzi kesi zilizoangaliwa ni zile za watu wa Mungu

wanaojulikana. Hukumu ya waovu ni kazi iliyotengwa na itafanywa baadaye. “Hukumu inapashwa kuanza katika nyumba ya Mungu.” 1 Petro 4:17.

Vitabu vya ukumbusho katika mbingu vianapaswa kuamua matokeo ya hukumu. Kitabu cha uzima kinakuwa na majina ya wote walioingia daima kwa kazi ya Mungu. Yesu aliambia wanafunzi wake: “Lakini furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa
[233] katika mbingu.” Paulo anasema juu ya watumishi wenzake, “Walio na majina yao katika kitabu cha uzima.” Danieli anatangaza kwamba watu wa Mungu watakombolewa, “kila mtu atakayeonekana ameandikwa katika kitabu.” Na mfumbuaji anasema kwamba wale tu watakaoingia Mji wa Mungu ambao majina yao “walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.” Luka 10:20; Wafilipi 4:3; Danieli 12:1; Ufunuo 21:27.

Katika “Kitabu cha ukumbusho” kumeandikwa matendo mema ya “wale wenye kuogopa Bwana, na kufikiri juu ya jina lake.” Kila jaribu lililostahimiliwa, kila uovu uliozuiwa, kila neno la huruma lililoonyeshwa, kila tendo la (kafara), kila huzuni iliyovumiliwa kwa ajili ya Kristo imeandikwa. “Umehesabu kutangatanga kwangu; Utie machozi yangu ndani ya chupa yako; Haya si katika kitabu chako?” Malaki 3:16; Zaburi 56:8.

## Mukusudi ya Siri

Hapo kunakuwa pia ukumbusho wa zambi za watu. “Kwa maana Mungu ataleta kila kazi hukumuni, pamoja na kila neno la siri, kama likiwa jema ao kama likiwa baya.” Kila neno la bure watu watakalolisema. watatoa hesabu ya neno hili siku ya hukumu.” “Kwa masemo yako utahesabiwa haki, na kwa masemo yako utahukumiwa.” Makusudi ya siri yanaonekana katika kitabu, kwa maana Mungu “atatia nuru maneno yaliyofichwa katika giza, na kuonyesha makusudi ya mioyo.” Muhubiri 12:14; Matayo 12:36,37; 1 Wakorinto 4:5. Mbele ya kila jina katika vitabu vya mbinguni kunaingia kila neno baya, kila tendo la choyo, kila mapashwa yasiyotimizwa, na kila zambi ya siri. Maonyo yaliyotumwa na mbingu ao makaripio yasiyojaliwa, nyakati zilizotumiwa bure, mvuto uliotumiwa kwa wema ao kwa ubaya pamoja na matokeo ya mwisho wake wa mbali, yanaandikwa yote kwa taratibu na malaika mwandishi.

## Kipimo cha Hukumu

Sheria ya Mungu ni kipimo katika hukumu. “Ogopa Mungu, na shika amri zake; maana maneno haya ni yote inayofaa mtu kufanya. Kwa maana Mungu ataleta kila kazi hukumuni.” “Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru.” Muhubiri 12:13,14; Yakobo 2:12.

Wale “wanaohesabiwa kuwa wamestahili” watakuwa na sehemu katika ufufuko wa wenye haki, Yesu akasema: “Lakini wale watakaohesabiwa kuwa wamestahili kupata dunia ile na kufufuka kutoka wafu,... ni wana wa Mungu, wakiwa wana wa ufufuo.” [234]
“Wale waliofanya mema watafufuka kwa ufufuko wa uzima.” Luka 20:35,36; Yoane 5:29. Wafu wenye haki hawatafufuliwa hata baada ya hukumu ambayo watakayohesabiwa kuwa wamestahili kwa “ufufuo wa uzima.” Kwa sababu hiyo hawatakuwako katika nafsi wakati vilivyoandikwa juu ya vingali na chunguzwa kesi zao kukatwa.

Yesu atatokea kama mwombezi wao, kutetea kwa ajili yao mbele ya Mungu. “Na Kama mtu yeyote akitenda zambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.” “Kwa sababu Kristo hakuingia katika Pahali patakatifu palipofanywa kwa mikono, ndio mfano wa kweli, lakini aliingia mbinguni zenyewe, aonekane sasa mbele ya Mungu kwa ajili yetu.” “Naye, kwa sababu hii anaweza pia kuwaokoa wanaokuja kwake Mungu kwa njia yake; maana yeye ni hai siku zote apate kuwaombea.” 1 Yoane 2:1; Waebrania 7:25; 9:24.

Wakati vitabu vya ukumbusho vinapofunguliwa katika hukumu, maisha ya wote walioamini kwa Yesu yanakuja katika ukumbusho mbele ya Mungu. Kuanzia kwa wale walioishi kwanza duniani, Mtetezi wetu anaonyesha kesi za kila kizazi kwa kufuatana. Kila jina linatajwa, kila kesi inachunguzwa. Majina yanakubaliwa, majina yanakataliwa. Wakati mtu ye yote anakuwa na zambi zinazodumu kwa vitabu vya ukumbusho, zisizoungamwa na kusamehewa, majina yao yatafutwa katika kitabu cha uzima. Bwana akamwambia Musa: “Mutu aliyenikosea, ndiye nitakayemwondosha katika kitabu changu.” Kutoka 32:33.

Wote waliotubu kwa kweli na katika imani wakadai damu ya Kristo kama kafara yao ya upatanishi walipata rehema wakaingia katika vitabu vya mbinguni. Kwa namna wanafanywa washiriki

wa haki wa Kristo na tabia zao zinaonekana kuwa katika umoja na sheria ya Mungu, zambi zao zitafutwa mbali, na watahesabiwa wenyekustahili uzima wa milele. Bwana anasema: "Mimi, ndiye anayefuta makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe; nami sitakumbuka zambi zako." "Yeye anayeshinda atavikwa nguo nyeupe, wala sitaondosha jina lake katika kitabu cha uzima; nami nitakiri jina lake mbele ya Baba yangu, na mbele ya malaika zake.' ' "Basi kila mtu anayenikiri mbele ya watu, nitamukiri vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni." Isaya 43:25; Ufunuo 3:5; Matayo 10:32,33.

Mtetezi wa kimungu anaonyesha maombi yale yote ya walioshinda kwa njia ya imani katika damu yake wapate kurudishwa kwa makao yao ya Edeni na kuvikwa taji kama kuwa wariti pamoja naye mwenyewe kwa "mamlaka ya mwanzo." Mika 4:8. Sasa Kristo anauliza ya kuwa mpago wa kimungu katika kuumbwa
[235] kwa mtu upate kutimizwa kama kwamba mtu hakuanguka kamwe. Anauliza kwa ajili ya watu wake si rehema tu na kuhesabiwa haki, bali sehemu katika utukufu wake na kukaa kwa kiti chake cha enzi.

Wakati Yesu anapoombea watu neema yake, Shetani anawashitaki mbele ya Mungu. Anaonyesha ukumbusho wa maisha, upungufu wa tabia, kuwa na tofauti kwa Kristo, kwa zambi zote alizowajaribu nazo kufanya. Kwa sababu ya mambo haya anawadai kuwa watu wake.

Yesu haruhusu zambi zao, lakini anaonyesha toba yao na imani. Anapoomba msamaha kwa ajili yao, anainua mikono yake iliyojeruhiwa mbele ya Baba, kusema: Nimewachora kwa viganja vya mikono yangu. "Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na toba hutauzarau, Ee Mungu." Zaburi 51:17.

## Bwana Anahamakia Shetani

Na kwa mushitaki anasema: "Bwana akuhamakie, Ee Shetani. Ndiyo Bwana aliyechagua Yerusalema, akuhamakie. Hiki si kinga kilichoondoshwa katika moto?" Zekaria 3:2. Kristo atavika waaminifu wake kwa haki yake mwenyewe, ili aweze kuwaonyesha kwa Baba yake "kanisa la utukufu, pasipo alama wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi." Waefeso 5:27.

Ndivyo itakavyotimilika utimilizo kamili wa ahadi ya maagano mapya: "Maana nitasamehe uovu wao, wala zambi yao sitakumbuka

tena." "Katika siku zile na wakati ule, anasema Bwana, uovu wa Israeli utatafutikana, wala uovu hapana; na zambi za Yuda zitafutikana, wala hazitaonekana." "Na itakuwa, yeye aliyeachwa katika Sayuni, na yeye aliyebaki ndani ya Yerusalema, ataitwa mtakatifu, kila mmoja aliyeandikwa katika wale walio hai ndani ya Yerusalema." Yeremia 31:34; 50:20; Isaya 4:3.

## Kufutia Mbali kwa Zambi

Kazi ya hukumu ya uchunguzi na kufutia mbali zambi inapashwa kutimizwa mbele ya kuja kwa Bwana mara ya pili. Katika huduma ya mfano kuhani mkuu alitoka inje na kubariki makutano. Vivyo hivyo Kristo, kwa mwisho wa kazi yake kama mpatanishi, ataonekana" si tena kwa zambi, lakini kwa wokovu." Waebrania 9:28.

Kuhani, katika kuondoa zambi kutoka Pahali patakatifu, aliziungama juu ya kichwa mbuzi wa Azazeli. Kristo ataweka zambi hizi zote juu ya Shetani, mshawishi wa zambi. Mbuzi wa Azazeli akapelekwa mbali "katika inchi isiyo na watu." Walawi 16:22. Shetani, katika kuchukua hatia za zambi alizolazimisha [236]
watu wa Mungu kuzifanya, atafungwa miaka elfu katika inchi isiyokaliwa kama jangwa na mwishoni atateswa kwa azabu ya moto utakaoangamiza waovu. Kwa hivi mpango wa wokovu utafikia utimilifu wake katika kungoa kwa mwisho kwa zambi.

## Kwa Wakati Uliotajwa

Kwa wakati uliotajwa--mwisho wa siku 2300 katika 1844--kazi ya uchunguzi ikaanza na kufutiwa mbali kwa zambi. Zambi zisizoungamwa na kuachwa hazitafutwa kutoka vitabu vya ukumbusho. Malaika wa Mungu wakashuhudia kila zambi na kuiandika. Zambi inaweza kukanwa, kufichwa kwa Baba, mama, bibi, watoto, na kwa rafiki; lakini inawekwa wazi mbele ya mbingu. Mungu hadanganywe kwa matendo yanayoonekana. Hafanyi makosa. Watu wanaweza kudanganywa kwa wale wanaochafuka ndani ya moyo, lakini Mungu anasoma maisha ya ndani.

Ni wazo la kutisha namna gani! Mshindi mkubwa kupita duniani hawezi kurudisha ukumbusho wa matendo ya siku hata moja. Ma-

tendo yetu, maneno yetu, hata makusudi yetu ya siri, ijapo tukiyasahau, yatatoa ushuhuda wake kwa kuhesabiwa haki wala kuhukumiwa.

Katika hukumu matumizi ya kila kipaji yatachunguzwa. Namna gani tumetumia wakati wetu, kalamu yetu ya wino, sauti yetu, mali yetu, mvuto wetu? Tumefanya nini kwa Kristo katika nafsi ya maskini, wenye kuteswa, yatima, ao mjane? Tumefanya nini na nuru pia na kweli tuliyopewa? Ila tu upendo ulioonyeshwa kwa matendo unaohesabiwa kuwa wa kweli. Upendo peke yake mbele ya Mungu wa mbinguni haufanye tendo lo lote la damani.

## Choyo lliyofichwa Imefunuliwa

Mambo yote ya ukaidi wa choyo iliyofichwa yamefunuliwa katika vitabu vya mbinguni. Mara ngapi wakati, mawazo, na nguvu zinazokuwa za Kristo zilitolewa kwa Shetani. Wafuasi wa Kristo wanashughulika katika upataji wa mali ya kidunia ao furaha ya anasa ya ulimwengu. Mali, wakati, na nguvu zinatumiwa kwa maonyesho na anasa; nyakati za bidii kwa kuomba ni chache, kwa kutafuta Maandiko, kuungama zambi.

Shetani anavumbua mashauri mengi yasiyohesabika kwa kutumia mawazo yetu. Mdanganyi mkubwa anachukia mambo makubwa
[237] ya kweli yale yanayoonyesha kafara ya upatanisho na Mpatanishi hodari. Kwake kila kitu kinategemea juu ya kugeuza mawazo kutoka kwa Yesu.

Wale wanaoweza kugawa faida ya upatanisho wa Mwokozi hawapaswi kuruhusu kitu cho chote kujiingiza kwa shughuli yao kukamilisha utakatifu katika kumcha Mungu. Saa za damani, badala ya kuzitoa kwa anasa ao kwa kutafuta faida, zinapashwa kutolewa kwa kujifunza katika maombi kwa Neno la Kweli. Pahali patakatifu na hukumu ya uchunguzi vinapaswa kufahamiwa wazi. Wote wanahitaji ujuzi wa cheo na kazi ya Kuhani wao Mkuu. Kama sivyo itakuwa haiwezekani kutumia kanuni ya imani kwa wakati huu.

Mahali patakatifu huko mbinguni ndipo pahali Kristo anaweka shabaha ya kazi kwa ajili ya wanadamu. Hii ni kwa kila roho inayoishi duniani. Inafungua kwa maoni mpango wa wokovu, kutuleta chini kwakufungwa kwa kukataa kati ya ukamilifu na zambi.

## Maombezi ya Kristo

Maombezi ya Kristo kwa ajili ya mtu katika Pahali patakatifu kule juu ni lazima kwa mpango wa wokovu kama ilivyokuwa na kifo chake msalabani. Kwa njia ya kifo chake akaanza kazi ile ambayo aliyopandia kwa kuitimiza mbinguni. Kwa imani inatupasa kuingia ndani ya pazia, "pahali alipoingia Yesu kwa ajili yetu." Waebrania 6:20. Hapo nuru kutoka kwa msalaba imerudushwa. Hapo tunapata mwangaza zaidi juu ya siri za ukombozi.

"Yeye anayefunika zambi zake hatasitawi: Lakini yeye anayezikiri na kuziacha atapata rehema." Mezali 28:13. Kama wale wanaoachilia (ruhusu) makosa yao wangaliweza kuona namna gani Shetani anavyolaumu Kristo kwa maisha yao, wangeungama zambi zao na kuziacha. Shetani anatumika apate utawala wa moyo wote, na anajua ya kuwa kama mawaa yanafurahiwa, atashinda. Kwa hiyo anatafuta daima kudanganya wafuasi wa Kristo kwa werevu wake wa mauti ambao haiwezekani kwao kuushinda. Lakini Yesu alisema kwa wote wanaoweza kumfuata: "Neema yangu inafaa kwako." "Nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." 2 Wakorinto 12:9; Matayo 11:30. Hebu kusiwe watu wo wote kuzania makosa yao kama siyakuponyeka. Mungu atatoa imani na neema kwa kushinda.

Sasa tunaishi katika siku kubwa ya upatanisho. Wakati kuhani mkuu alipokuwa akifanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, wote walilazimishwa kuhuzunisha roho zao kwa toba ya zambi. Kwa namna ileile, wote wanaotaka majina yao kudumu katika kitabu cha uzima wanapashwa sasa kuhuzunisha roho zao mbele ya Mungu kwa toba ya kweli. Hapo kunapashwa kuwa na uchunguzi mwingi, wa [238]
imani ya moyoni. Roho hafifu iliyopendelewa na wengi inapashwa kuachwa. Hapo kunakuwa vita ya nguvu mbele ya wale wote wanaoshinda mivuto mbaya inayoshindana kwa ajili ya utawala. Kila mtu anapashwa kukutwa pasipo awaa ao kikunjo wala kitu cho chote kama hivi." Waefeso 5:27.

Kwa wakati huu juu ya vitu vyote vingine inafaa kila nafsi kusikia onyo la upole la Mwokozi: "Tazameni, ombeni, maana hamujui wakati ule." Marko 13:33.

## Mwisho wa Wote Umekatwa

Rehema imeisha kwa wakati mfupi kabla ya kuonekana kwa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Kristo akitazama wakati ule, anasema: "Yeye aliye mzalimu azidi kuwa mzalimu; na mwenye uchafu azidi kuwa mchafu; na mwenye haki azidi kufanya haki; na mtakatifu azidi kutakaswa. Tazama, ninakuja upesi na mshahara wangu ni pamoja nami, kulipa kila mtu kama ilivyo kazi yake." Ufunuo 22:11,12.

Watu watakuwa wakipanda na kujenga, kula na kunywa, wote pasipokufahamu ya kuwa hukumu ya mwisho imetangazwa katika Pahali patakatifu mbinguni. Mbele ya Garika, baada ya Noa kuingia katika safina, Mungu akamfungia ndani na kufungia waovu inje; lakini kwa siku saba watu wakaendelea na maisha yao ya kupenda anasa na wakachekelea maonyo ya hukumu. "Ndivyo" asema Mwokozi, "kutakavyokuwa kuja kwa Mwana wa watu." Kwa kimya, bila kuonwa kama mwizi usiku wa manane, saa itakuja ambayo inaonyesha kukata shauri la mwisho wa kila mtu. "Basi angalieni: ... asije na kuwasitusha ninyi gafula, akawakuta mumelala." Matayo 24:39; Marko 13:35,36.

Hali ni yenye hatari ya wale ambao, huendelea kuchoka kwa kukesha kwao, wanageuka kwa mivuto ya dunia. Wakati mtu wa biashara anaposhughulika katika kufuata faida, wakati mwenye kupenda anasa anapotafuta anasa, wakati binti wa desturi ya kuvaa nguo anapotengeneza mapambo yake--inaweza kuwa katika saa ile Mwamzi wa dunia yote atatangaza hukumu, "Umepimwa katika mizani, nawe umeonekana kuwa umepunguka." Danieli 5:27.

## 29 /SABABU GANI ZAMBI ILIRUHUSIWA? [239]

Wengi wanaona kazi ya uovu, na msiba wake na ukiwa, na wanauliza namna gani hii inaweza kuwa chini ya utawala wa Huyu Mmoja asiyekuwa na mwisho katika hekima, uwezo na upendo. Wale wanaotaka kuwa na mashaka wanashikamana na jambo hili na kutafuta sababu ya kukataa manene ya Maandiko matakatifu. Desturi ya asili na mafahamu mabaya ya maandiko yameficha mafundisho ya Biblia kuhusu tabia ya Mungu, asili ya mamlaka yake, na kanuni zake kuhusu zambi.

Haiwezekani kueleza mwanzo wa zambi vilevile kama kutoa sababu kwa ajili ya kuwako kwake (zambi). Kwani kuna mambo mengi ya kutosha inayoweza kufahamiwa juu ya mwanzo na hali ya mwisho ya zambi kufanya onyesho kamili haki na wema wa Mungu. Mungu kwa hekima yo yote hakuwa mwenye madaraka kwa zambi; hapakuwa bila sababu kuondolewa kwa neema ya Mungu, hakuna upungufu katika mamlaka ya kimungu, iliyotoa nafasi kwa uasi. Zambi ni mpelelezi (mdukizi) ambaye kuwako kwake hakuna sababu inayoweza kutolewa. Kuisamehe ni kuitetea. Kama iliweza kusamehewa ingekoma kuwa zambi. Zambi ni onyesho la kanuni inayoleta kwa vita sheria ya upendo, inayokuwa msingi wa serkali ya Mungu.

Mbele ya kuingia kwa zambi amani na furaha ilikuwa katika viumbe vyote. Upendo kwa Mungu ulikuwa mkubwa, upendo kwa mtu na kwa mwingine ulikuwa wa bila ubaguzi. Kristo Mwana wa pekee wa Mungu alikuwa mmoja pamoja na Baba wa milele katika hali, katika tabia, na katika kusudi--ni yeye peke yake ambaye aliweza kuingia katika mashauri yote na makusudi ya Mungu. ‘’Katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni, ... ikiwa ni viti vya wafalme ao usultani ao falme ao mamlaka.” Wakolosayi 1:16.

Sheria ya upendo ilikuwa msingi wa utawala wa Mungu, furaha ya viumbe vyote vilivyoumbwa ilitegemea kwa upatano pamoja na kanuni zake za haki. Mungu hapendezwi na utii wa kulazimishwa,

na kwa wote anatoa uhuru wa mapenzi, kwamba wanaweza kumfanyia kazi bila kulazimishwa).

Lakini kulikuwa na mmoja aliyechagua kuharibu vibaya uhuru huo. Zambi ilianzia kwake, yeye aliyekuwa, baada ya Kristo, aliheshimiwa sana kwa Mungu. Mbele ya kuanguka kwake, Lusifero alikuwa wa kwanza kwa wakerubi wa kufunika, mtakatifu na mwenye usafi. "Bwana Mungu anasema hivi: Ulikuwa muhuri
[240] wa ukamilifu, mwenye kujaa na hekima na ukamilifu wa uzuri. Wewe ulikuwa katika Edeni, shamba la Mungu; kila jiwe la damani lilkuwa kifunuko chako. ... Wewe ulikuwa kerubi wa kufunika mwenye kutiwa mafuta; nami nilikuweka juu ya mlima mtakatifu wa Mungu; umetembea huko na huko katikati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu kwa njia zako tangu siku ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako. ... Moyo wako umenyanyuliwa kwa sababu ya uzuri wako, umeharibu hekima yako kwa sababu ya kungaa kwako." "Nawe ulisema moyoni mwako ... Nitanyanyua kiti changu cha enzi juu kupita nyota za Mungu, Na nitakaa juu ya mlima wa makutano. ... Nitapanda juu kupita vimo vya mawingu, Nitafanana naaliye juu Sana." Ezekieli 28:12-17; 28:6; Isaya 14:13,14.

Kutamani heshima ambayo Baba aliweka juu ya Mwana wake, mtawala huyu wa malaika akatamani kwa uwezo ambao ulikuwa ni mamlaka ya Kristo peke yake kutawala. Sauti isiyopatana sasa ikaharibu mapatano ya mbinguni. Kujiinua kwa nafsi kukaamsha visirani vya uovu katika mioyo ambayo utukufu wa Mungu ulikuwa mkubwa. Baraza za mbinguni zikatetea pamoja na Lusifero. Mwana wa Mungu akaonyesha mbele yake wema na haki ya Muumba na tabia takatifu ya sheria yake. Kwa kuiacha, Lusifero angezarau Muumba wake na kujiletea uharibifu juu yake mwenyewe. Lakini onyo peke likaamsha msimamo. Lusifero akaruhusu wivu wa Kristo kushinda.

Kiburi kikazidisha tamaa ya mamlaka. Heshima za juu zilizotolewa kwa Lusifero zikaleta kutokuwa na shukrani kwa Muumba. Akatamani kuwa sawa sawa na Mungu. Huku Mwana wa Mungu alikuwa Mfalme aliyekubaliwa wa mbingu, mmoja kwa uwezo na mamlaka pamoja na Baba. Katika mipango yote ya Mungu, Kristo alikuwa mshirika, lakini Lusifero hakuruhusiwa kuingia katika makusudi ya kimungu. "Sababu gani," akauliza huyu malaika

mkubwa, "inamupasa Kristo kuwa na mamlaka? Sababu gani yeye anaheshimiwa kupita Lusifero?"

### Manunguniko Miongoni mwa Malaika

Kuacha pahali pake mbele ya Mungu, Lusifero akaendelea kutawanya manunguniko miongoni mwa malaika. Kwa maficho yasiyoelezeka,kwa kuficha kusudi lake la kweli chini ya mfano wa heshima kwa Mungu, akajikaza kuamsha kutorizika juu ya sheria ambazo zilitawala viumbe vya mbinguni, kutangaza kwamba walilazimisha amri isiyohitajika. Kwani tabia zao zilikuwa takatifu, akashur- tisha kwamba malaika walipashwa kutii amri za mapenzi [241]
yao wenyewe. Mungu alimtendea bila haki kwa kuweka heshima kubwa juu ya Kristo. Akadai kwamba hakukusudia kujiinua mwenyewe lakini alikuwa akitafuta kulinda uhuru wa wakaaji wote wa mbinguni, ili waweze kufikia maisha ya juu.

Mungu akavumilia Lusifero muda mrefu. Hakuondolewa cheo kwa kazi yake ya juu ijapo wakati alipoanza kuonyesha madai ya uwongo mbele ya malaika. Mara kwa mara akatolewa rehema ikiwa anakubali kutubu na kutii. Juhudi za namna ile ambayo upendo tu usio na mwisho ulifanya njia yakumpata asadiki ya kosa lake. Mwanzoni manunguniko haya kujulikana kule mbinguni. Lusifero mwenyewe mara ya kwanza hakufahamu tabia ya kweli ya mawazo yake. Kwa namna uchungu wake ulipohakikishwa kuwa bila sababu, Lusifero akasadikishwa kwamba madai ya Mungu yalikuwa ya haki na kwamba ilimupasa kuyaungama mbele ya wote wa mbinguni. Kama angalifanya hivi, angalijiokoa mwenyewe na malaika wengi. Kama angalipenda kurudi kwa Mungu, kutoshelewa kujaza pahali alipoagizwa, angalirudishwa katika kazi yake. Lakini kiburi kikamkataza kutii. Akashikilia kwamba hakuwa na haja ya toba, na akajitoa kabisa katika vita kuu juu ya Muumba wake.

Nguvu zote za akili ya ufundi wake zikaelekeza kwa udanganyifu, kusudi malaika wamuunge mkono. Shetani akaonyesha kwamba alihukumiwa kwa uwongo na kwamba uhuru wake ukapunguzwa. Kwa masingizio ya maneno ya Kristo akapita kwa kusimamia uwongo, kushitaki Mwana wa Mungu juu ya shauri la kumfezelesha mbele ya wakaaji wa mbinguni.

Wote ambao hakuweza kuwapindua kwa upande wake akawashitaki kuwa wenye ubaridi (kutojali) kwa faida ya viumbe vya mbinguni. Akakimbilia kwa maafundisho ya uwongo juu ya Muumba. Ilikuwa ujanja wake kwa kuhangaisha malaika na maneno ya ujanja juu ya makusudi ya Mungu. Kila kitu chepesi akakifunika katika fumbo, na kwa njia ya kupotosha akatia mashaka juu ya maneno yaliyokuwa wazi kabisa kwa Mungu. Cheo chake cha juu kikatoa nguvu kubwa kwa masingizio yake. Akashawishi wengi kuungana pamoja naye katika uasi.

### Uchuki Ukasitawishwa Katika Uasi wa Juhudi

Mungu katika hekima yake akaruhusu Shetani kuendelea na kazi yake, hata roho ya uchuki ikasitawishwa katika uasi. Ilikuwa ni lazima kwa mashauri yake kuendelea kabisa, ili tabia yake ya kweli
[242] iweze kuonekana kwa wote. Lusifero alikuwa mwenye kupendwa sana na viumbe vya mbinguni, na mvuto wake juu yao ulikuwa wa nguvu. Serkali ya Mungu haikuhusikana tu na wakaaji wa mbinguni, lakini kwa dunia zote alizoziumba; na Shetani akafikiri kwamba kama akiweza kuchukua malaika pamoja naye katika uasi, angeweza kuchukua vilevile dunia zingine. Kutumia madanganyo na werevu, uwezo wake kwa kudanganya ulikuwa mkubwa sana. Hata Malaika waaminifu hawakuweza kabisa kutambua tabia yake wala kuona ni kitu gani kazi yake ilikuwa ikiongoza.

Shetani alikuwa akiheshimiwa sana, na matendo yake yote kuvikwa sana na siri, mpaka ilikuwa vigumu kuonyesha kwa malaika tabia ya kweli ya kazi yake. Hata ilipositawi kabisa, zambi haikuonyesha kitu kibaya kilichokuwako. Viumbe vitakatifu havikuweza kutambua matokeo ya kuweka kando sheria ya Mungu. Shetani mwanzoni alisema alikuwa anatafuta kuendelesha heshima ya Mungu na uzuri wa wakaaji wote wa mbinguni.

Katika mipango yake juu ya zambi, Mungu aliweza kutumia tu haki na kweli. Shetani aliweza kutumia mambo ambayo Mungu hakuweza kutumia--uongo na werevu. Tabia ya kweli ya mnyanganyi ilipashwa kufahamiwa na wote. Alipashwa kuwa na wakati kujionyesha mwenyewe kwa kazi zake za uovu.

Ugomvi ambao alianzisha yeye mwenyewe mbinguni, Shetani aliuwekea juu ya Mungu. Uovu wote aliutangaza kuwa matokeo ya

utawala wa Mungu. Kwa hiyo ilikuwa ni lazima kwamba aonyeshe wazi matokeo ya makusudi yake ya kugeuza sheria ya Mungu. Kazi yake mwenyewe ilipashwa kumuhukumu. Viumbe vyote vya ulimwengu vilipashwa kuona mdanganyi kufunuliwa.

Hata wakati ilipokusudiwa kwamba hawezi tena kudumu mbinguni, Mungu wa hekima isiyokuwa na mwisho hakumuangamiza Shetani. Utii wa viumbe vya Mungu unapashwa kuwa juu ya sadikisho la haki yake. Wakaaji wa mbinguni na wa dunia zingine, walipokuwa bila kujitayarisha kufahamu matokeo ya zambi, hawakuweza basi kuona haki na rehema ya Mungu katika maangamizi ya Shetani. Kama angaliangamizwa mara moja, wangemtumikia Mungu kwa hofu kuliko kwa upendo. Mvuto wa mdanganyi haungeharibiwa kabisa, wala roho ya uasi kungolewa kabisa. Kwa faida ya viumbe vyote katika vizazi vyote, Shetani alipashwa kuendelesha kabisa kanuni zake, kwamba mashambulio yake juu ya mamlaka ya Mungu yapate kuonekana katika nuru yake ya kweli kwa viumbe vyote vilivyoumbwa.

Uasi wa Shetani ulipashwa kuwa kwa viumbe vyote ushuhu- da [243]
kwa matokeo ya kuogopesha ya zambi. Kanuni yake ingeonyesha matunda ya kuweka kando mamlaka ya Mungu. Historia ya tendo hili la kuogopesha la uasi lilipashwa kuwa ulinzi wa milele kwa akili takatifu zote kuwaokoa kwa zambi na kwa azabu yake.

Wakati ilipotangazwa kwamba pamoja na washiriki wake wote mnyanganyi mkubwa wa ufalme anapashwa kufukuzwa kutoka kwa makao ya cheo cha furaha, mwongozi muasi (mhuni) akatangaza wazi bila woga zarau kwa ajili ya sheria ya Muumba. Akalaumu sheria za Mungu kama kizuio cha uhuru na akatangaza kusudi lake la kupata kuondoshwa kwa sheria. Kwa kuwekwa huru kwa amri hii, majeshi ya mbinguni wangeweza kuingia juu ya hali ya kujipandisha zaidi katika maisha.

## Kufukuziwa Mbali Kutoka Mbinguni

Shetani na jeshi lake wakatupa laumu la uasi wao juu ya Kristo; kama hawakulaumiwa, kama hawangeasi kamwe. Wagumu na wakiburi, huku wakajitangaza kwa matukano kuwa watu wasiokuwa na kosa na kwamba waliteswa na mamlaka makali. Muasi mkubwa

wa waliomfuata wakafukuzwa kutoka mbinguni. Tazama Ufunuo 12:7-9.

Roho ya Shetani ingali inaendesha uasi duniani katika wana wa uasi. Kama yeye wakaahidia watu uhuru kwa kuvunja sheria ya Mungu. Hakikisho la zambi likaendelea kuamsha uchuki. Shetani anaongoza watu kujihakikisha wao wenyewe na kutafuta huruma ya wengine katika zambi zao. Badala ya kusahihisha makosa yao, wanaamsha hasira juu ya mwenye kukaripia, kama kwamba wanakuwa chanzo cha shida. Kwa kusingizia kwa namna ileile ya tabia ya Mungu kama alivyoyatumia mbinguni, kumfanya kuwa kama mwenye kuzaniwa kama mkali na wa kushurutisha, Shetani akashawishi mtu kwa zambi. Akatangaza kwamba vizuizi visivyo na haki vya Mungu viliongoza kuanguka kwa mtu, kama vilivyoongoza kwa uasi wake mwenyewe.

Katika kufukuziwa kwa Shetani kutoka mbinguni, Mungu alitangaza haki yake na heshima. Lakini wakati mtu alipotenda zambi, Mungu alitoa ushuhuda wa upendo wake kwa kutoa Mwana wake kufa kwa ajili ya taifa lililoanguka. Katika upatanisho tabia ya Mungu imefunuliwa. Mabishanomakubwa ya msalaba yanaonyesha kwamba zambi haikuwa na hekima yo yote kulipizwa juu ya utawala wa Mungu. Wakati wa huduma ya kidunia ya Mwokozi, mdanganyi mkubwa akafunuliwa. Matukano ya wazi ya kutaka kwamba Kristo
[244] amupe heshima kuu, uovu usiolala uliomuwinda pahali po pote, kuongoza mioyo ya makuhani na watu kukataa upendo wake na kulalamika kwa sauti, "Asulibiwe! asulibiwe!" --yote haya yaliamsha mshangao na hasira ya ulimwengu. Mfalme wa zambi akatumia uwezo wake wote na werevu kuharibu Yesu. Shetani akatumia watu kama wajumbe wake kujaza maisha ya Mwokozi kwa mateso na huzuni. Chuki na wivu na uovu, machukio na kisasi, vikaanguka kutoka Kalvari juu ya Mwana wa Mungu.

Sasa kosa la Shetani likaonekana wazi. Alifunua tabia yake ya kweli. Mashitaki ya uwongo ya Shetani juu ya tabia ya Mungu yakaonekana katika nuru yao ya kweli. Alimshitaki Mungu juu ya kutafuta kujiinua mwenyewe katika kuomba utii kwa viumbe vyake na akatangaza kwamba wakati Muumba alipolazimisha wote kujikana mwenyewe, Yeye mwenyewe hakutumia kujikana mwenyewe na hakutoa kafara yo yote. Sasa ilionekana kwamba Mtawala wa ulimwengu alitoa kafara kubwa sana ambayo upendo uliweza

kufanya, “maana, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe.” 2 Wakorinto 5:19. Kusudi aharibu zambi Kristo akajinyenyekea mwenyewe na kuwa mtiifu hata mauti.

### Mabishano kwa Ajiii ya Mtu

Mbingu yote ikaona haki ya Mungu kufunuliwa. Lusifero alidai kwamba wanadamu wa zambi wangekuwa mbali ya ukombozi. Lakini azabu ya sheria ikaanguka juu yake aliyekuwa sawa na Mungu, na mtu akawa huru kukubali haki ya Kristo na kwa njia ya toba na kujishusha kwa kushinda nguvu za Shetani.

Lakini Kristo hakuja duniani kufa kwa ajili ya kukomboa mtu tu. Alikuja kuonyesha kwa dunia zote kwamba sheria ya Mungu ni sheria isiyobadilika. Mauti ya Kristo inaihakikisha kuwa isiyogeuka na inaonyesha kwamba haki na rehema ndiyo msingi wa utawala wa Mungu. Katika hukumu ya mwisho itaonekana kwamba hapana sababu kwa ajili ya zambi kuwako. Wakati Mwamzi wa dunia yote atakapo muuliza Shetani, “Sababu gani uliasi juu yangu?” Mwanzishaji wa zambi hataweza kutoa sababu.

Katika kupaza sauti kwa Mwokozi, “Imekwisha, “tarumbeta ya mauti ya Shetani ililia. Vita kuu ikakusudiwa, kungoa kwa mwisho kwa uovu kukahakikishwa. Kwa maana “siku inakuja, inawaka kama tanuru; na wenye kiburi wote, na wote wanaotumika uovu watakuwa kama makapi makavu; na siku itakayokuja itawateketeza, Bwana wa majeshi anasema; hata haitawaachia, wala shina wala tawi.” Malaki 4:1. Uovu hautaonekana tena kamwe. Sheria ya [245]
Mungu itaheshimiwa kama sheria ya uhuru. Viumbe vyote vilivyojaribiwa na kuhakikishwa havitageuka kamwe kwa kumtii yeye ambaye tabia yake imeonekana kama upendo usiopimika na hekima isiyo na mwisho.

[246] 

## 30 /SHETANI NA MTU KATIKA VITA

"Na nitatia uadui katikati yako na mwanamuke, na katikati ya uzao wako na uzao wake; ataponda kichwa chako, na wewe utaponda kisingino chake." Mwanzo 3:15. Uadui huu si wa tangu awali. Wakati mtu alipovunja sheria ya Mungu, hali yake ikawa mbaya, katika umoja na Shetani. Malaika walioanguka na watu wabaya wakajiunga katika urafiki wa kutokuwa na matumaini. Kama Mungu hakujitia kati, Shetani na mtu wangaliingia katika mapatano kumpinga Mungu wa mbinguni, na jamaa lote la binadamu lingalijiunga katika upinzanii kwa Mungu.

Wakati Shetani aliposikia kwamba uadui ulipashwa kuwa kati yake na mwanamuke, na kati ya uzao wake na uzao wa mwanamuke, alijua kwamba kwa sababu yo yote mtu alipashwa kuwa mtu asiyeweza kupinga uwezo wake.

Kristo alitia uadui ndani ya mtu kumpinga Shetani. Pasipo neema hii ya kugeuka na nguvu inayomfanya mpya, mtu angaliendelea kuwa mtumishi tayari daima kufanya mapenzi ya Shetani. Lakini kanuni mpya katika nafsi inaleta vita; uwezo ambao Kristo anatoa unawezesha mtu kushindana na mkorofi mkuu. Kuchukia sana zambi badala ya kuipenda kunaonyesha kanuni kabisa kutoka juu.

Uadui kati ya Kristo na Shetani ulionekana wazi namna dunia ilivyompokea Yesu. Usafi na utakatifu wa Kristo uliamsha juu yake uchuki wa wasiomuogopa Mungu. Kujikana kwake kulikuwa laumu la duhakikisho kwa wenye kiburi na wapenda anasa ya mwili. Shetani na malaika wabaya wakaungana na watu wabaya kupinga ya Mshindi wa kweli. Uadui wa namna moja unaonyeshwa kwa wafuasi wa Kristo. Ye yote anayesimama imara kwa jaribu ataamsha hasira ya Shetani. Kristo na Shetani hawawezi kupatana. Na wote wanaotaka kuishi maisha ya utawa katika Kristo Yesu watapata mateso." 2 Timoteo 3:12.

Wajumbe wa Shetani wanatafuta kudanganya wafuasi wa Kristo na kuwavuta kwa utii wao. Wanapotosha Maandiko kwa kutirniza

kusudi lao. Roho iliyotia Kristo kwa mauti inaamsha waovu kuharibu wafuasi wake. Yote hii inaonyeshwa mbele katika ule unabii wa kwanza: "Na nitatia uadui katikati yako na mwanamuke, na katikati ya uzao wako na uzao wake."

Sababu gani Shetani hakutani na ushindani mkubwa? Kwa sababu askari za Kristo wanakuwa na uhusiano mdogo sana pamoja na Kristo. Zambi haiwachukizi kama ilivyomchukiza Bwana wao. Hawajitoi kwa kupigana nayo. Tabia ya mkuu wa giza imewafanya [247] vipofu. Wengi hawajui kwamba adui wao ni mkubwa mwenye nguvu za kupigana kumpinga Kristo. Hata wahuduma wa habari njema hawaoni ushaihidi wa kazi yake. Wanaonekana kutojali kuwako kwa hakika kwake.

## Adui Mwangalifu

Adui huyu mwangalifu yuko anajiingiza katika kila jamaa, katika kila njia, katika makanisa, katika ma Baraza ya mataifa, katika manyumba ya sheria, katika baraza za hukumu, Kuleta matatizo, kudanganya, kukosesha, po pote kuharibu nafsi na miili ya wanaume na wanawake, na watoto. Anaharibu jamaa, kupanda uchuki, vita, fitina, na uuaji wa mtu kwa kusudi. Na ulimwengu unaonekana kuzania mambo haya kama kwamba ni Mungu aliyeyaweka na yanapashwa kuwako. Wote wasiokusudia kuwa wafuasi wa Kristo wanakuwa watumishi wa Shetani. Wakati Wakristo wanapochagua jamii ya wasiomwogopa Mungu, wanajihatarisha wao wenyewe kwa majaribu. Shetani anajificha mwenyewe kwa macho na anafunika kifuniko chake cha udanganyi kwa macho yao.

Kufuatana na desturi za dunia anageuza kanisa kwa dunia, hageuzi kamwe dunia kwa Kristo. Kujizoeza zambi kutaifanya isionekane kuwa mbaya sana. Wakati katika njia ya kazi tunaletwa katika kujaribiwa, tunaweza kuwa na hakika kwamba Mungu atatulinda; lakini tukijiweka sisi wenyewe chini ya jaribu tutaanguka upesi ao baadaye.

Mjaribu mara kwa mara anatumika kwa mafanikio zaidi katika wale bila shaka wasiojizania kuwa chini ya mamlaka yake. Kipawa na elimu ni kimtu ni zawadi za Mungu; lakini wakati hizi zinapoongoza mbali kutoka kwake, zinakuwa mtego. Mara nyingi mtu

mwenye elimu ya akili na wa tabia ya kupendeza ni chombo kizuri katika mikono ya Shetani.

Musisahau kamwe onyo la maongozi ya Mungu la kutangaza tangu karne nyingi hata wakati wetu. "Muwe na kiasi na kuangalia; mpinzanii wenu Shetani, kama simba anayenguruma anayezungukazunguka akitafuta mtu amumeze." "Vaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kusimama juu ya hila za Shetani." 1 Petro 5:8; Waefeso 6:11. Adui wetu mkubwa anajitayarisha kwa mashambulio yake ya mwisho. Wote wanaomfuata Yesu watakuwa katika vita pamoja na adui huyu. Zaidi sana Mkristo anapoiga Mfano wa Mungu, na
[248] zaidi hakuna shaka atajiweka mwenyewe alama kwa mashambulio ya Shetani.

Shetani alishambulia Kristo kwa majaribu makali na hila; lakini alikomeshwa katika kila vita. Kushinda kule kote kunatuwezesha sisi kishinda. Kristo atatoa nguvu kwa wale wote wanaoitafuta. Hakuna mtu asipokubali yeye mwenyewe anaweza kushindwa na Shetani. Mjaribu hana uwezo wa kutawala mapenzi ao kulazimisha mtu kufanya zambi. Anaweza kutia ao kuanzisha taabu, lakini hapana uchafu. Jambo la hakika kwamba Kristo alishinda linapasa kutia moyo wafuasi wake kwa nguvu kupigana vita juu ya zambi na Shetani.

# 31 /PEPO WACHAFU [249]

Malaika wa Bwana na pepo wachafu wanaonyeshwa wazi katika Maandiko na wanaingia katika historia ya wanadamu. Malaika watakatifu wale "wanaotumikia watakaoriti wokovu" (Waebrania 1:14) wanazaniwa kwa wengi kama pepo za waliokufa. Lakini Maandiko inaonyesha hakika kwamba hawa si pepo inayoachana na mwili wa waliokufa.

Mbele ya kuumbwa kwa mtu, malaika walikuwa wakiishi, kwani wakati misingi ya dunia ilipowekwa, ''nyota za asubui waliimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa furaha." Yobu 38:7. Nyuma ya kuanguka kwa mtu, malaika walitumwa kulinda mti wa uzima mbele ya mwanadamu kufa. Malaika wanakuwa wakubwa kwa cheo kuliko watu, kwa kuwa mtu aliumba "chini kidogo kupita malaika ". Zaburi 8:5.

Nabii anasema, "Nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi." Mbele ya Mufalme wa wafalme wanangojea- "ninyi watumishi wake, munaofanya mapenzi yake," "mukisikiliza sauti ya neno lake," "majeshi ya malaika elfu nyingi." Ufunuo 5:11; Zaburi 103:20,21; Waebrania 12:22. Kama wajumbe wa Mungu wanatoka, kama "kuonekana, kwa kumulika kwa umeme," mruko wao mwepesi sana. Malaika aliyetokea kwa kaburi la Mwokozi, sura yake "kama umeme," ikawaletea walinzi kwa ajili ya hofu kutetemeka, na "wakawa kama wafu." Wakati Saniaribu alipomtukana Mungu na kuogopesha Waisraeli, "malaika wa Bwana alitoka, akapiga katika kambi ya Waasuria watu elfu mia moja makumi mnane na tano." Ezekieli 1:14; Matayo 28:3,4; 2 Wafalme 19:35.

Malaika wanatumwa kwa kazi ya rehema kwa wana wa Mungu. Kwa Abrahamu, kwa ahadi za baraka; kwa Sodomo, kuokoa Loti kwa maangamizo; kwa Elia, karibu kuangamizwa katika jangwa; kwa Elisa, kwa magari ya farasi ya moto alipofungiwa ndani na adui zake; kwa Danieli, wakati alipoachwa kuwa mawindo ya simba; kwa Petro, alipohukumiwa kifo katika gereza ya Herode; kwa wafungwa kule Filipi; kwa Paulo katika usiku wa zoruba juu ya bahari; kwa

kufungua akili ya Kornelio kwa kukubali habari njema; kwa kutuma Petro pamoja na habari njema ya wokovu kwa mgeni wa Kimataifa--kwa hivi malaika watakatifu walitumikia watu wa Mungu.

[250]

## Malaika Walinzi

Malaika mlinzi amewekwa kwa kila mfuasi wa Kristo. "Malaika ya Bwana anapiga kambi kuzunguka wale wanaomwogopa, na anawaokoa." Akasema Mwokozi, juu ya wale wanaomwamini: "Mbinguni malaika zao wanatazama siku zote uso wa Baba yangu." Zaburi 34:7; Matayo 18:10. Watu wa Mungu, walihatarishwa kwa uovu usiolala wa mfalme wa giza, wanaahidiwa na ulinzi usiokoma wa malaika. Matumaini ya namna hiyo yanatolewa kwa sababu kunakuwa na nguvu kubwa za uovu za kukutana nazo--nguvu zisizohesabika, imara na zisizochoka.

Pepo wachafu, kwa mwanzo waliumbwa pasipo zambi, walikuwa sawasawa kwa tabia, uwezo, na utukufu pamoja na viumbe vitakatifu vile vinavyokuwa sasa wajumbe wa Mungu. Lakini walipoanguka katika zambi, wanashiriki pamoja kwa kufezeresha Mungu na uharibifu wa watu. Kwa kuungana pamoja na Shetani katika uasi, wanashirikiana katika vita kupigana na mamlaka ya Mungu.

Historia ya Agano la Kale inataja kuwapo kwao, lakini kwa wakati Yesu alipokuwa duniani pepo wachafu wakaonyesha uwezo wao kwa namna ya ajabu sana. Kristo alikuja kwa ajili ya ukombozi wa mtu, na Shetani akakusudia kutawala ulimwengu. Akafanikiwa katika kuimarisha ibada ya sanamu katika kila upande wa dunia isipokuwa Palestina. Kwa inchi ile tu ambayo haikujitoa kamili kwa mshawishi, Yesu akakuja, kunyosha mikono yake ya upendo, kualika wote kupata msamaha na amani kwake. Majeshi ya giza yakafahamu kwamba kama kazi ya Kristo inapata ushindi, mamlaka yao ingekuwa karibu kumalizika.

Kwamba watu wamekuwa na pepo mbaya inasemwa wazi katika Agano Jipya. Kwa hivi watu walioteswa si kwa sababu tu ya magonjwa ya kawaida; Kristo alifahamu kuwako kwa chanzo cha magonjwa na nguvu ya pepo wachafu. Wenye pepo wachafu kule Gadara, wenye wazimu wa hali mbaya, kujinyonga, kujitapa, kutosha povu, kukasirika, walikuwa wakijitesa wao wenyewe na

kuhatarisha wote waliopaswa kuwakaribia. Kutokwa kwao kwa damu, kukabadili hali ya mwili na mawazo yenye kuhangaika yalionyesha ajabu ya kufurahisha sana mfalme wa giza. Mumojawapo wa pepo wachafu wakutawala wanaoteswa akatangaza, "Jina langu ni Legioni: maana: Jeshi." Marko 5:9. Katika jeshi la Roma legioni ilikuwa ya kuanzia watu elfu tatu hata elfu tano. Kwa agizo la Yesu pepo wachafu wakatoka kwa watu wao waliokuwa wanatesa, kuwaacha wanapotu- lia, wenye akili, na wapole. Lakini pepo [251]
wachafu wakarusha kundi la nguruwe katika bahari, na kwa wakaaji wa Gadara hasara kubwa ikazima mibaraka Kristo aliyoitoa; mponya wa Mungu akalazimishwa kutoka. Tazama Matayo 8:22-34. Kwa kulaumu hasara yao juu ya Yesu, Shetani akaamsha choyo cha woga kwa watu na kuwakataza kusikiliza maneno yake.

Kristo akaruhusu pepo wachafu kuangamiza nguruwe kama laumu kwa Wayuda waliolea wanyama najisi kwa ajili ya faida. Kama Kristo hakuzuia pepo wachafu, wangalitumbukiza si nguruwe tu, bali wachungaji wao pia na wenye nguruwe ndani ya bahari.

Tena, jambo hili liliruhusiwa ili wanafunzi waweze kushuhudia uwezo mkali wa Shetani juu ya wote wawili mtu na mnyama, ili wasiweze kudanganywa kwa mipango yake. Ilikuwa vilevile mapenzi yake kwamba watu walipashwa kutazama uwezo wake kuvunja utumwa wa Shetani na kufungua wafungwa wake. Ingawa Yesu Mwenyewe alitoka, watu waliookolewa kwa ajabu sana wakaendelea kutangaza rehema ya Mkarimu wao.

Mifano mingine imeandikwa: Binti wamwanamuke wa Sirofoinike, aliyesumbuliwa vikali kwa Shetani, ambaye Yesu alifukuza kwa neno lake (Marko 7:26-30); kijana aliyekuwa na pepo ambayo mara kwa mara "kumtupa katika moto, na katika maji, amwangamize." (Marko 9:17-27); mwenye pepo, aliyeteswa na pepo ya ibilisi mchafu aliyechafua Sabato tulivu kule Kapernaumu (Luka 4:33-36)--wote waliponyeshwa kwa Mwokozi. Karibu kila mfano, Kristo akasema pepo mchafu kama kitu chenye akili, kumwagiza kutotesa mtu wake tena. Waabuduo kule Kapernaumu "wote wakashangaa sana, wakasemezana wao wenyewe wakisema: Neno gani hili; kwani kwa mamlaka na uwezo anaamuru pepo wachafu, nao wanatoka." Luka 4:36.

Kwa ajili ya kupata uwezo wa ajabu, wengine wakakaribisha mvuto wa Shetani. Mambo haya bila shaka hayakuwa na ugomvi

pamoja na pepo wachafu. Kwa kundi hili kulikuwa wale waliokuwa na pepo ya uaguzi--Simon Magus, Elima mchawi yule, na kijakazi mwenye pepo aliyefuata Paulo na Sila kule Filipi. Tazama Matendo 8:9,18; 13:8; 16:16-18.

Hakuna wanaokuwa katika hatari kubwa kuliko wale wanaokana kuwako kwa Shetani na malaika zake. Wengi wanajali mashauri yao wanapoona wao wenyewe kuwa wakifuata hekima yao wenyewe. Kwa namna tunavyokaribia mwisho wa wakati, wakati Shetani anapashwa kutumika kwa uwezo mkubwa kudanganya, anaeneza mahali pote imani kwamba yeye hakuwako. Ni kanuni yake kujificha
[252] mwenyewe na namna yake ya kutumika.

Mwongo mkubwa anaogopa kwamba tutakuwa wenye kutambua mipango yake. Kwa kuficha tabia yake ya kweli akajifanya mwenyewe aonyeshwe kama kitu cha kuchekelea ao cha kuzarau. Anapendezwa kufafanishwa kama mwenye kuchekesha, mwenye msiba, nusu mnyama na nusu mwanadamu. Anapendezwa kusikia jina lake linapotumiwa katika mchezo na kicheko. Kwa sababu amejificha mwenyewe na akili kamili, swali linaulizwa sana popote: "Je, kiumbe cha namna hii kinakuwako kweli?" Ni kwa sababu Shetani anaweza kwa upesi kutawala mawazo ya wale wanaokuwa bila kufahamu mvuto wake kwamba Neno la Mungu linafungua mbele yetu nguvu za siri yake, kwa hivi kutuweka kwa angalisho.

Tunaweza kupata kimbilio na wokovu katika uwezo mukubwa wa Mkombozi wetu. Tunachunga vizuri sana nyumba zetu kwa mapingo na kufuli kulinda mali yetu na maisha kwa watu waovu, lakini ni marahaba kufikiri juu ya malaika waovu kushindana na mashambulio yake tunayokuwa nayo, katika nguvu zetu wenyewe, hakuna ulinzi. Kama wakiruhusiwa, wanaweza kuvuta mioyo yetu, kutesa miili yetu, kuharibu mali yetu na maisha yetu. Lakini wale wanaomfuata Kristo wanakuwa salama chini ya ulinzi wake. Malaika wanaopita katika nguvu wanatumwa kuwalinda. Waovu hawawezi kuvunja ulinzi aliyoweka Mungu kwa ajili ya watu wake.

# 32 /NAMNA YA KUMSHINDA SHETANI

[253]

Vita kuu kati ya Kristo na Shetani ni karibu kuisha, na mwovu huyo anazidisha mara mbili juhudi zake kwa kuvunja kazi ya Kristo kwa ajili ya mtu. Kwa kushikilia watu katika giza na ugumu wa moyo hata upatanishi wa Mwokozi umalizika ndiyo shabaha anayoitafuta kutimiza. Wakati ubaridi unapokuwa mwingi ndani ya kanisa, Shetani hajali. Lakini wakati roho zinapochunguza, "Nifanye nini nipate kuokolewa?" anakuwa pale kupiganisha uwezo wake kupinga Kristo pia na kupinga mvuto wa Roho Mtakatifu.

Kwa wakati moja wakati malaika walipokuja kujionyesha wao wenyewe mbele ya Bwana, Shetani akakuja vilevile miongoni mwao, si kwa ajili ya kuinama mbele ya Mfalme wa Milele, lakini kuharakisha makusudi yake maovu ya kushindana na wenye haki. Utazame Yobu 1:6. Yeye anahuzuria wakati watu wanapoabudu, kutumika kwa juhudi kutawala mawazo ya wanaoabudu. Kwa namna anavyoona mjumbe wa Mungu kutafuta Maandiko, anaandika yote juu ya fundisho litakalofundishwa. Ndipo anatumia werevu wake na akili ili habari isiweze kufikia wale ambao anawadanganya kwa jambo halisi lile. Yule anayehitaji onyo zaidi atashurutishwa katika kazi ya jambo fulani ao kwa njia ingine atapata kizuizi kwa kusikia neno.

Shetani anaona watumishi wa Mungu wakilemewa kwa sababu ya giza inayofunika watu. Anasikia maombi yao kwa ajili ya neema ya Mungu na uwezo kwa kuvunja mvuto wa ubaridi na uvivu. Halafu kwa nguvu mpya anajaribu watu kwa anasa ya tamaa ao kujifurahisha, na kwa hivyo anaua akili zao ili washindwe kusikia mambo kabisa wanayohitaji zaidi kujifunza.

Shetani anajua kwamba wote wanaozarau maombi na Maandiko watashindwa kwa mashambulio yake. Kwa hiyo anavumbua kila kitu cha kuvuta moyo. Wasaidizi wake wa mkono wa kuume wanakuwa na juhudi siku zote wakati Mungu anakuwa kwa kazi. Wataonyesha watumishi wa kweli wa Kristo wenye kujikana kama wanaodanganywa ao wanaodanganya. Ni kazi yao kusingizia makusudi ya kila tendo bora, kueneza mambo ya kuchongea, na kuamsha

mashaka katika mioyo ya wajinga. Lakini inaweza kuonekana upesi wanakuwa watoto wa nani, ambao mfano ni wa nani wanaoufuata, na wanafanya kazi ya nani. "Mutawatambua kwa njia ya matunda yao." Matayo 7:16; utazame vilevile Ufunuo 12:10.

[254]

## Kweli Inatakasa

Mdanganyi mkubwa anakuwa na wazushi wengi waliofanywa tayari kupendeza onjo mbalimbali ya wale ambao angeharibu. Ni mpango wake kuleta ndani ya kanisa watu wasiofaa, wasiogeuza wale watakaoshawishi mashaka na kutoamini. Wengi wasiokuwa na imani kamili katika Mungu wanakubali kanuni zingine za kweli na wanajifanya kuwa Wakristo, na kwa hivi wanawezeshwa kuingiza kosa kama mafundisho ya maandiko. Shetani anajua kwamba kweli, iliyokubaliwa katika upendo, inatakasa nafsi. Kwa hiyo anatafuta kubadilisha maelezo ya uwongo, mifano, injili ingine. Tangu mwanzo, watumishi wa Mungu wamebishana juu ya waalimu wa uwongo, si kama watu wabaya tu, bali kama wenye kufundisha uwongo wa kufisha kwa nafsi. Elia, Yeremia, Paulo, kwa nguvu walipinga wale waliokuwa wakigeuza watu kutoka kwa Neno la Mungu. Ule uhuru ambao unaangaliarau imani kamili hafifu haikupata nafasi kwa hawa watetezi watakatifu wa kweli.

Maelezo yasiyofahamika vizuri na ya kujiwazia tu juu ya Maandiko na maelezo yenye kupingana katika ulimwengu wa Kristo yanakuwa ni kazi ya adui wetu mkubwa kwa kuchafua akili. Ugomvi na fitina miongoni mwa makanisa vinatokana mara nyingi na kupinganisha Maandiko kwa kuunga mkono maelezo ya kupendeza.

Kwa kusimamia mafundisho ya uwongo, wengine wanashikilia juu ya maneno ya Maandiko wanayotenga kando kwa maneno mengine, kutumia maneno nusu ya fungu kama kuhakikisha msimamo wao, huku sehemu iliyobaki inapoonyesha maana kuwa kinyume kabisa. Kwa werevu wa nyoka wanajiingiza wenyewe nyuma ya maneno ya kutengwa yaliyofasiriwa kufurahisha tamaa za mwili. Wengine wanashikilia juu ya sura na mifano, wanayatafsiri kwa kupendeza mawazo yao, pamoja na heshima kidogo kwa ushuhuda wa Maandiko kama mfasiri wake mwenyewe, halafu kuonyesha mambo ya upumbavu wao kama mafundisho ya Biblia.

## Biblia Yote ni Kiongozi

Wakati ambapo kujifunza kwa Maandiko kunapoauzwa pasipo roho ya maombi na inayoweza kufundishwa, mafungu ya waziwazi kabisa yatakuwa ya kupotea maana yake ya kweli. Biblia yote inapashwa kutolewa kwa watu kama vile inavyosomwa.

Mungu alitoa neno la haki la unabii; malaika na hata Yesu Mwenyewe alikuja kujulisha kwa Danieli na Yoane vitu ambavyo "vilivyopashwa kuwa upesi." Ufunuo 1:1. Mambo ya maana inay-ohu- su wokovu wetu hayakufunuliwa kwa namna ya kutatiza na [255] kuongoza vibaya mtafutaji mwaminifu wa kweli. Neno la Mungu ni wazi kwa wote wanaojifunza sana kwa moyo wenye kuomba.

Kwa kilio, Ukarimu, watu ni vipofu kwa mashauri mpinzani. Anafaulu kuondosha Biblia na kutumia mawazo mengi ya kibinadamu; sheria ya Mungu inawekwa pembeni; na makanisa yanakuwa chini ya utumwa wa zambi yanapojitangaza kuwa huru.

Mungu ameruhusu garika ya nuru kumiminwa ulimwenguni kwa mvumbuzi ya elimu ya ulimwengu wa vyumbe vyo (science). Lakini hata watu wa elimu zaidi, kama hawaongozwi na Neno la Mungu, wanapotea katika kujaribu kuchunguza mahusiano ya maarifa (science) na ufunuo.

Maarifa ya kibinadamu ni ya kipande na si kamili; kwa hiyo wengi hawawezi kupatanisha maoni yao ya maarifa (science) pamoja na Maandiko. Wengi wanakubali tu maelezo kama mambo ya ujuzi, na wanafikiri kwamba Neno la Mungu ni la kujaribiwa kwa "elimu inayoitwa elimu kwa uwongo." 1 Timoteo 6:20. Kwa sababu hawawezi kueleza Muumba na kazi zake katika sheria za asili, historia ya Biblia inazaniwa kama isioweza kutumainiwau. Wale wanaokuwa na mashaka juu ya Agano la Kale na Agano Jipya kwa mara nyingi wanakwenda hatua mbali zaidi na kutosadiki kuwako kwa Mungu. Walipoachilia nanga yao, wanagonga juu ya miamba ya kutokuwa waaminifu kwa Mungu.

Ni kazi kubwa ya uongo wa Shetani kudumisha watu kubahatisha kwa mambo ambayo Mungu hakuyaulisha. Lusifero akawa bila kurizika kwa sababu siri zote za makusudi ya Mungu hazikufunuliwa kwake, na akakataa maneno yale yaliyofunuliwa. Sasa anatafuta kujaza watu kwa roho ya namna ileile na kuwaongoza pia kutojali amri wazi za Mungu.

Wapungufu wa mafundisho ya kiroho yanayotolewa na moyo wa kujikana, kwa namna vinavyoelezwa, kukubaliwa na kupokelewa kwa bidii kubwa. Shetani anakuwa tayari kutoa kwa tamaa ya moyo, na anapokeza hila za udanganyifu badala pa Kweli. Ilikuwa kwa namna hii ambayo dini ya Roma (papa) ilipata mamlaka yake kwa roho za watu. Na katika kukataa kweli kwa sababu inahusikana na msalaba, Waprotestanti wanafuata njia ile ile. Wote wanaojifunza manufaa na mashauri, ili wasiweze kuwa na tofauti na ulimwengu, wataachwa kupata "uharibifu usiokawia" wakizania ni kweli. 2 Petro 2:1. Yeye anayetazama kwa kuchukia udanganyifu moja atapokea mara hiyo mwingine. "Na kwa maneno haya Mungu anawaletea nguvu ya upotevu, hata waamini uwongo: ili wahukumiwe wote
[256] wasioamini kweli, lakini walifurahi katika uzalimu." 2 Watesalonika 2:11,12.

## Makosa ya Hatari

Miongoni mwa vyombo vya ushindi zaidi vya mdanganyi mkubwa ni maajabu ya uwongo ya imani ya roho za watu waliokufa (spiritisme). Kwa namna watu wanavyokataa kweli wanatekwa kwa udanganyifu.

Kosa lingine ni mafundisho yanayokana Umungu wa Kristo, kudai kwamba hakuwako mbele ya kuja kwake kwa ulimwengu huu.

Maelezo haya yanakausha maneno ya Mwokozi wetu juu ya uhusiano wake na Baba na kuwako kwake siku zote za mbele. Yanaharibu imani katika Biblia kama ufunuo kutoka kwa Mungu. Kama watu wanakana ushuhuda wa Maandiko juu ya Umungu wa Kristo, ni bure kubishana nao; hakuna mabishano, hakuna neno hata wazi la kuweza, kuwasadikisha; Hakuna anayeshikilia kosa hili anayeweza kuwa na wazo la kweli la Kristo wala la mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi wa mtu.

Tena kosa lingine ni imani kwamba Shetani haishi kama kiumbe chenye nafsi, kwamba jina linalotumiwa katika Maandiko ni kufananisha tu mawazo mabaya ya watu na tamaa.

Mafundisho kwamba kuja kwa mara ya pili kwa Kristo ni kuja kwake kwa kila mtu wakati wa mauti ni uongo kwa kupotosha akili kusahau kwa kuja kwake mwenyewe katika mawingu ya mbingu.

Shetani basi amekuwa akisema, ‘’Tazama, yeye ni katika vyumba vya ndani” (Tazama Matayo 24:23-26), na wengi wamepotea katika kukubali udanganyifu huu.

Tena watu wa maarifa wanadai kwamba hakuna jibu la kweli linaweza kuwako kwa kuomba; hii ingekuwa uvunjaji wa sheria-mwujiza, na miujiza haiwezi kuwako. Ulimwengu, wanasema, unatawaliwa katika sheria zisizobabilika, na Mungu Mwenyewe hafanye kitu kinyume kwa sheria hizi. Kwa hivi wanafananinisha Mungu kama amelazimishwa katika sheria zake mwenyewe--kana kwamba sheria za Mungu zingekataza uhuru wa Mungu. Fundisho la namna hii linapinga ushuhuda wa maandiko.

Je, miujiza haikufanywa na Kristo na mitume wake? Mwokozi yule yule anapendezwa basi kusikiliza maombi ya imani kama vile alivyotembea kwa wazi miongoni mwa watu. Hali ya viumbe vinashirikiana na hali ya Mungu. Ni sehemu ya mpango wa Mungu kutusaidia, katika jibu kwa ombi la imani, lile ambalo hangali- toa [257]
tusilouliza.

## Mipaka ya Neno

Mafundisho ya uwongo miongoni mwa makanisa yanaondoa mipaka iliyowekwa na Neno la Mungu. Wachache wanasimamia kwa kukataa kweli moja tu. Wengi wanaweka kando mojawapo kwa ingine ya kanuni za kweli, hata wanapokuwa wasioamini.

Makosa ya elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini ya kupendezwa na watu wengi yaliendesha roho nyingi kwa moyo wa mashaka (sceptisim). Haiwezekani kwao kukubali mafundisho ambayo yanayopinga maelezo ya watu juu ya haki, rehema na wema. Kwa hivi mambo haya yanaonyeshwa kama mafundisho ya Biblia, anakataa kuyakubali kama Neno la Mungu.

Neno la Mungu linaangaliwa bila tumaini kwa sababu linakemea na kuhukumu zambi. Wale wasiotaka kutii wanafanya nguvu kupindua mamlaka yake. Wengi wanakufuru ili kutetea uzarau wa kazi yao. Wengine pia, ni wapenda raha kwa kutimiza kitu cho chote ambacho kinaomba kujikana mwenyewe, wanatunza sifa kwa ajili ya hekima kubwa kwa kuteta Biblia.

Wengi wanaona kama sifa kusimama upande wa kutoamini, mashaka, na kukufuru. Lakini chini ya mfano mwema kutapatikana

kujitumaini mwenyewe na kiburi. Wengi wanapendezwa katika kupata kujua kitu fulani katika Maandiko kutatiza roho za wengine. Wengine kwa sababu ya kwanza kwa upande usiofaa kwa upendo tu wa mabishano. Lakini wakisha kuonyesha wazi kutoamini, wanajiunga pamoja na wasiomwongopa Mungu.

### Ushuhuda wa Kufaa

Mungu ametoa katika Neno lake ushuhuda wa kutosha wa kuonyesha tabia yake. Lakini akili zenye mpaka zinakuwa si zakutosha kabisa kufahamu makusudi ya Mungu. “Hukumu zake hazivumbulikani, na njia zake hazifutikani!” Waroma 11:33. Tunaweza kutambua upendo usio na mpaka na rehema iliyoungana na uwezo usio na mwisho. Baba yetu aliye mbinguni atafunua kwetu kwa namna inavyotosha kwa ajili ya uzuri wetu kujua; zaidi ya pale tunapashwa kutumainia Mkono ule unaokuwa ni Mwenye mamlaka yote, Moyo unaojaa upendo.

Mungu hataondoa kamwe sababu zote za kutoamini. Wote wanaotafuta sababu za kuwekea mashaka yao watazipata. Na wale wanaokataa kutii hata kila kizuizi kinapokwisha kuondolewa
[258] hawatakuja kwa nuru kamwe. Moyo usiofanywa upya unakuwa katika uadui na Mungu. Lakini imani inatiwa moyo kwa Roho Mtakatifu na itasitawi kama inavyolindwa. Hakuna mtu anaweza kuwa na nguvu katika imani pasipo nguvu imara. Kama watu wakijiruhusu wenyewe kubishana, mashaka yatapata msingi zaidi.

Lakini wale wanaokuwa na mashaka na kutotumaini hakikisho (assurance) la neema yake wanapatisha haya Kristo. Wanakuwa miti isiyozaa inayozuia nuru ya jua kwa mimea mingine, kuiletea kufifia na kufa chini ya baridi ya kivuli. Kazi ya maisha ya watu hawa itatokea kama ushuhuda usiokoma juu yao.

Kunakuwa lakini sababu moja tu ya kufuata kwa wale ambao kwa uaminifu wanatamani kuwa huru kwa kutokuwa na mashaka. Badala ya kuuliza yale wasiyofahamu, waachwe watoe ukubali kwa nuru ambayo imekwisha kuangaza juu yao, na watapata nuru kubwa zaidi.

Shetani anaweza kuonyesha mfano karibu sana kufanana na kweli ule unaodanganya wale wanaotaka kudanganyiwa, wanaotamani kuepuka kafara iliyohitajiwa katika kweli. Lakini ni kitu

kisichowezekana kwake kushika chini ya uwezo wake nafsi moja inayotaka kwa uaminifu, kwa bei yo yote, kujua ukweli. Kristo ndiye kweli, "Nuru ya kweli inayotia nuru kila mtu anayekuja katika ulimwengu." "Kila mtu akipenda kufanya mapenzi yake, atajua habari za yale mafundisho." Yoane 1:9; 7:17.

Bwana anaruhusu watu wake kupata kwa majaribu makali ya kutesa, si kwa sababu anapendezwa wala kufurahishwa katika taabu yao, bali kwa sababu jambo hili ni la lazima kwa ushindi wao wa mwisho. Hakuweza, kwa uthabiti kwa utukufu wake mwenyewe, kuwalinda kutoka kwa jaribu, kwa sababu kusudi la jaribu ni kuwatayarisha kupinga mivuto yote ya uovu. Hata waovu wala mashetani hawawezi kufunga kuwako kwa Mungu kwa watu wake kama wataungama na kuacha zambi zao na kudai ahadi zake. Kila jaribu, la wazi wala la siri, linaweza kupingwa kwa kufanikiwa. "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, lakini kwa Roho yangu, Bwana wa majeshi anasema." Zekaria 4:6.

"Naye ni nani atakayewaumiza ninyi, kama ninyi mkiwa wenye bidii katika maneno yale yaliyo mema?" 1 Petro 3:13. Shetani anafahamu vizuri kwamba roho inayokuwa zaifu zaidi inayokaa ndani ya Kristo inakuwa na nguvu zaidi kuliko mshindani kwa majeshi ya giza. Kwa sababu hiyo anatafuta kufukuzia mbali waaskari wa msalaba kutoka kwa boma lao lenye nguvu, huku anapolala akijificha, tayari kuangamiza wote wanaosubutu kwa udongo wake. Ila tu katika kutegemea Mungu na utii kwa amri zake tunaweza [259]
kulindwa.

Hakuna mtu anayekuwa salama kwa siku moja ao saa moja pasipo kuomba. Omba Bwana kwa ajili ya hekima kwa kufahamu Neno lake. Shetani ni mbingwa katika kutumia Maandiko, kuweka mafasirio yake mwenyewe kwa mafungu ambayo anatumaini kutuletea kikwazo. Inatupasa kujifunza kwa unyenyekevu wa moyo. Huku tunapopashwa mara kwa mara kujilinda juu ya mashauri ya Shetani, inatupasa kuomba kwa imani siku zote; "Na usitulete katika majaribu." Matayo 6:13.

[260] # 33 /NI KITU GANI KINACHOLALA NG'AMBO YA PILI YA KABURI

Shetani aliyechochea uasi huko mbinguni, alitaka kushawishi wakaaji wa dunia kuungana katika vita yake ya kumpinga Mungu. Adamu na Hawa walikuwa na furaha kamili katika utii kwa sheria ya Mungu--ushuhuda wa daima wa kupinga madai ya Shetani ulioweka mbele katika mbingu ya kuwa sheria ya Mungu ilikuwa ya taabu. Shetani akakusudia kuanzisha maanguko yao, ili aweze kumiliki dunia na hapa kuimarisha ufalme wake kwa kupingana na Aliye Juu.

Adamu na Hawa walikuwa wakionywa juu ya adui wa hatari huyu, lakini alikuwa akitumika katika giza, kuficha kusudi lake. Kutumia nyoka kama chombo chake, ndipo kiumbe cha mfano wa kupendeza, akamwambia Hawa: "Ndiyo, Mungu amesema: Msile ya miti yote ya shamba?" Hawa akajihatarisha (akasubutu) kusemana naye na akaanguka mateka kwa uongo wake: "Mwanamuke akamwambia nyoka: Matunda ya miti ya shamba tunaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya shamba Mungu amesema: Musile matunda yake wala musiyaguse, musife. Na nyoka akamwambia mwanamuke; Hakika hamutakufa, kwani Mungu anajua ya kama siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama miungu, mukijua uzuri na ubaya." Mwanzo 3:1-5.

Hawa akakubali, na kwa mvuto wake (mwanamuke) Adamu akaongozwa katika zambi. Wakakubali maneno ya nyoka; wakaonyesha kutotumaini Muumba wao na kuwaza ya kama alikuwa akizuia uhuru wao.

Lakini ni kitu gani Adamu alichopata kujua kuwa maana ya maneno, "Kwa maana siku utakapokula, hakika utakufa"? Je, alipaswa kuongozwa katika maisha ya kujiinua zaidi? Adamu hakuona jambo hili kuwa maana ya hukumu ya Mungu. Mungu alitangaza ile kama azabu kwa ajili ya zambi yake, mtu alipashwa kurudi kwa mavumbi: "Kwa sababu mavumbi wewe, na utarudi kwa mavumbi." Mwanzo 3:19. Maneno ya Shetani, "Macho yenu yatafunguliwa,"

yalionekana kuwa ya kweli katika maana hii tu: macho yao yakafunguliwa kutambua ujinga wao. Wakajua ubaya na kuonja tunda la uchungu wa uasi.

Mti wa uzima ulikuwa na uwezo wa kudumisha uzima. Adamu angeendelea kufurahia ruhusa ya uhuru wa kukaribia mti huu na kuishi milele, lakini wakati alipofanya zambi akazuiwa kwa mti wa uzima na akastahili kifo. Kufa ikaondoa kutokufa. Pale hapangalikuwa na tumaini kwa uzao ulioanguka kama Mungu, kwa kafara [261] ya Mwana wake, hangeleta kutokufa karibu nao. Na hivi ''kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi," Kristo "ameleta uzima na maisha yasiyokoma nuru ni kwa njia ya Habari Njema." Katika Kristo tu kutokufa kunaweza kupatikana. "Anayeamini Mwana ana uzima wa milele; na asiyemwamini Mwana hataona uzima." Waroma 5:12; 2 Timoteo 1:10; Yoane 3:36.

## Uwongo Mkubwa

Yule aliyeahidi uzima katika uasi alikuwa mdanganyi mkubwa. Na tangazo la nyoka katika Edeni--"Hakika hamutakufa"--lilikuwa hubiri la kwanza lililohubiriwa daima juu ya kutokufa kwa roho (nafsi). Lakini tangazo hili, la kubaki tu kwa mamlaka ya Shetani, linakaririwa kwa mimbara na kukubaliwa kwa watu wengi kwa upesi kama mbele kwa wazazi wetu wa kwanza. Hukumu ya Mungu, "Nafsi inayofanya zambi itakufa" (Ezekieli 18:20) inafanywa kwa kutaka kuonyesha, Nafsi inayofanya zambi, haitakufa, lakini itaishi milele na milele. Kama mtu angalipewa ruhusa ya uhuru ya kukaribia mti wa uzima, baada ya kuanguka kwake, zambi zingalifanywa kukaa milele. Lakini hakuna hata mtu mmoja wa jamaa ya Adamu aliyeruhusiwa kuonja (kutwaa) tunda linalotoa uzima. Kwa hiyo hapo hakuna mwenye zambi wa kuishi milele.

Baada ya Kuanguka, Shetani akaalika malaika zake kufundisha imani katika kutokufa ya milele kwa asili ya mtu. Akiisha kuingiza watu kukubali kosa hili, ilikuwa ni kuwaongoza kuzania kama mwenye zambi angeishi katika mateso ya milele. Sasa mfalme wa giza anamuonyesha Mungu kuwa sultani mkali mwenye kutaka kisasi, kutangaza ya kama anatumbukiza katika jehanum wote wasiompendeza, ya kama wakati wanapojinyonga katika ndimi za moto wa milele, Muumba wao anawatazama chini na kurizika. Kwa

hivi ibilisi mukubwa anavika Mtenda mema kwa mwanadamu tabia zake. Ukali ni tabia ya Shetani. Mungu ni mapendo. Shetani ni adui anayejaribu mtu afanye zambi na baadaye akamwangamiza kama awezavyo. Ni mambo ya kuchukiza upendo, rehema, na haki, mafundisho kwamba wafu waovu wanateseka katika jehanum inayowaka ya milele, kwamba kwa zambi za maisha mafupi ya kidunia wanateseka malipizi makali katika maisha yote ya Mungu!

Ni mahali gani katika Neno la Mungu mafundisho ya namna ile inapatikana? Je, mawazo ya wema wa watu wote yageuzwe kwa ukali waushenzi? Hapana, yale si mafundisho ya Kitabu
[262] cha Mungu. "Ninavyoishi, Bwana Mungu anasema, sina furaha kwa kufa kwa mwovu; lakini mwovu aache njia yake apate kuishi; geukeni, geukeni mukaache njia yenu mbaya; kwani kwa sababu gani munataka kufa?" Ezekieli 33:11.

Je, Mungu anapendezwa katika kushuhudia mateso yasiyomalizika? Je, Yeye anapendezwa na maumivu wala mazomeo na kilio cha nguvu cha viumbe vinavyoteseka anavyoshikilia katika ndimi za moto? Je, sauti hizi za kuchukiza ziwe sauti za nyimbo katika sikio la yule ambaye ana Upendo Pasipo Mwisho (Mungu)? Loo, matukano gani ya kutiisha! Utukufu wa Mungu hauongezwe kwa kudumisha zambi kupitiamilele na milele.

### Ujushi wa Maumivu Mabaya ya Milele

Uovu ulifanyika kwa sababu ya ujushi wa maumivu mabaya ya milele. Dini ya Biblia, inajaa na upendo na wema, inatiwa giza kwa imani ya mambo ya uchawi na inavikwa na hofu kubwa. Shetani amepakaa rangi tabia ya Mungu kwa rangi za uwongo. Muumba wetu wa rehema anaogopwa, na kuhofiwa, hata kuchukiwa. Maoni ya kutisha ya Mungu ambayo yameenea po pote ulimwenguni kutoka kwa mafundisho ya mimbara yamefanya mamilioni ya watu wenye mashaka na wasiokuwa waaminifu.

Maumivu mabaya ya milele ni mojawapo ya mafundisho ya uwongo, mvinyo wa gazabu yake (Ufunuo 14:8; 17:21), ambayo Babeli inafanya wote kunywa. Wahuduma wa Kristo walipokea ujushi huu kwa Roma kama walivyokubali sabato ya uwongo. Kama tukiacha Neno la Mungu na kukubali mafundisho ya uwongo kwa

sababu wababa zetu waliyafundisha, tunaanguka chini ya hukumu iliyotangazwa kwa Babeli; tunakunywa mvinyo wa gazabu yake.

Kundi kubwa linaongozwa kwa kosa la upande mwingine. Wanaona Maandiko yanayoonyesha Mungu kama mwenye upendo na huruma na hawawezi kuamini kwamba atatupa viumbe kwa jehanum inayowaka milele. Kushikilia kwamba nafsi kwa kawaida ni ya milele, wakaishia kwamba watu wote wataokolewa. Kwa hivyo mwenye zambi anaweza kuishi katika anasa ya kupendeza nafsi, kutojali matakwa ya Mungu, na kukubaliwa na Mungu. Mafundisho ya namna hiyo, yanategemea kwa rehema ya Mungu lakini bila kujali haki yake, yanafurahisha moyo wa tamaa za mwili.

### Wokovu wa Watu Wote Si Fundisho la Biblia

Wanaoamini katika wokovu wa watu wote wanageuza Maandiko. [263]
Mhubiri anayejulikana wa Kristo anakariri uwongo ulioenezwa na nyoka katika Edeni, "Hakika hamutakufa." "Siku mutakayokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama miungu. " Anatangaza ya kama mwovu zaidi katika wenye zambi--muuaji, mwizi, mzinzi--baada ya kifo ataingia katika hali ya furaha ya milele. Hadizi za kweli za kupendeza, zinazofaa kwa kupendeza moyo wa tamaa za mwili!

Kama ingekuwa kweli kwamba watu wote wangepita mara moja mbinguni kwa saa ya mwisho ya mauti, tungeweza vema kutamani mauti kuliko uzima. Wengi wameongozwa katika imani hii kumaliza wala kukomesha maisha yao. Kulemezwa na hatari na uchungu, inaonekana rahisi kuvunja mwendo wa maisha na kupanda upesi katika hali ya raha ya makao ya milele.

Mungu ametoa katika Neno lake ushuhuda wazi ya kama ataazibu wavunjaji wa sheria yake. Je, yeye anakuwa mwenye rehema vilevile hata asitimize haki juu ya mwenye zambi? Tazama kwa msalaba wa Kalvari. Mauti ya Mwana wa Mungu inashuhudia kwamba "mushahara wa zambi ni mauti" (Waroma 6:23), kwamba kila uvunjaji wa sheria ya Mungu unapashwa kupata malipizi. Kristo asiyekuwa na zambi akawa mwenye zambi kwa ajili ya mtu. Akavumulia hatia za zambi na maficho ya uso wa Baba yake hata moyo wake ukapasuka na maisha yake kuangamizwa--yote haya ili wenye zambi waweze kukombolewa. Na kila nafsi ambayo in-

akataa kushirikiana na upatanisho uliotolewa kwa bei ya namna ile anapaswa kuchukua kwa nafsi yake mwenyewe hatia na azabu ya zambi.

## Masharti Yameelezwa

"Mimi nitamupa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure." Ahadi hii ni ya wale tu wanaokuwa na kiu. "Yeye anayeshinda atariti maneno haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwana wangu." Ufunuo 21:6,7. Mashairi yameelezwa. Kwa kuriti vitu vyote, inatupasa kushinda zambi.

"Lakini haitakuwa heri kwake mwovu." Muhubiri 8:13. Mwenye zambi anajiwekea mwenyewe "hasira kwa siku ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayelipa kila mutu kwa kadiri ya matendo yake;" "mateso na taabu juu ya kila nafsi ya mutu anayefanya uovu." Waroma 2:5,6,9.

"Hakuna mwasherati wala mutu muchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye uriti katika ufalme wa Kristo na Mungu." "Heri wale wanaofula nguo zao, wawe na amri kwendea
[264] mti wa uzima, na kuingia katika muji kwa milango yake. Lakini inje ni imbwa, na wachawi, na wazini, na wauaji, na wanaoabudu sanamu, na kila mutu anayependa uwongo na kuufanya." Waefeso 5:5, ARV; Ufunuo 22:14,15.

Mungu amewatolea watu tangazo la kanuni ya matendo na zambi. "Waovu wote atawaharibu." ''Lakini wakosaji wataharibiwa pamoja; mwisho wa waovu utaharibiwa." Zaburi 145:20; 37:38. Mamlaka ya serikali ya Mungu itaharibu maasi, lakini haki ya kulipiza kisasi itakuwa aminifu pamoja na tabia ya Mungu kama wa rehema, na wema.

Mungu hashurutishe mapenzi. Hapendezwi na utii wa utumwa. Anataka ya kama viumbe vya mikono yake watampenda kwa sababu anastahili upendo. Angaliwatakia wamtii kwa sababu wanakuwa na shukrani ya akili kwa hekima yake, haki, na wema.

Kanuni za serkali ya Mungu zinakuwa katika umoja pamoja na amri ya Mwokozi, "Pendeni adui zenu." Matayo 5:44. Mungu anatimiliza haki kwa waovu kwa ajili ya uzuri wa viumbe vyote na hata kwa ajili ya uzuri wa wale ambao hukumu zake zitakapowatazama. Angewafurahisha kama awezavyo. Amewazunguusha na alama za

upendo wake na kuwafuatisha na matoleo za rehema; lakini wanazarau upendo wake, wanavunja sheria yake, na kukataa rehema yake. Kupokea daima zawadi zake, wanampatisha haya Mtoaji. Bwana anavumilia ukaidi wao wakati mrefu; lakini je, atawafunga waasi hawa kwa upande wake, kuwalazimisha kufanya mapenzi yake?

### Hawakutayarishwa Kuingia Mbinguni

Wale waliochagua Shetani kuwa kiongozi wao hawakutayarishwa kuingia machoni pa Mungu. Kiburi, uongo, uasherati, ukali, yamekazwa katika tabia zao. Je, wanaweza kuingia mbinguni kukaa milele pamoja na wale ambao waliwachukia duniani? Kweli haitaweza kuwa ya kupendeza kwa mwongo; upole hautaweza kutuliza kujisifu; usafi hauwezi kukubaliwa kwa mwovu; upendo usiotaka faida hauonekane wa kuvuta kwa mwenye choyo. Ni furaha gani mbingu ingeweza kutoa kwa wale wanaoshughulika sana katika faida za kujipendeza nafsi?

Je, wale ambao mioyo yao imejazwa na uchuki kwa Mungu, kwa kweli na kwa utakatifu, wanaweza kuchanganyika pamoja na makutano ya mbinguni na kujiunga katika nyimbo zao za sifa? Miaka ya rehema ilitolewa kwao, lakini hawakuzoeza moyo wao kupenda usafi. Hawakujifunza kamwe lugha ya mbinguni. Sasa ni [265]
kuchelewa.

Maisha ya maasi kumpinga Mungu haikuwastahilisha kwa mbinguni. Usafi wake na amani yangekuwa ni mateso kwao; utukufu wa Mungu ungekuwa moto unaoteketeza. Wangetamani sana kukimbia kutoka mahali pale patakatifu na wangekaribisha vizuri maangamizi, ili waweze kufichwa kutoka usoni pake yeye aliyekufa kwa kuwakomboa. Mwisho wa waovu anaimarishwa kwa uchaguzi wao wenyewe. Kufukuzwa kwao kutoka mbinguni ni kwa kujichagulia wao wenyewe na ni haki na rehema kwa upande wa Mungu. Kama maji ya Garika mioto ya siku kuu inatangaza hukumu ya Mungu kwamba hakuna dawa ya waovu. Mapenzi yao imetumiwa katika maasi. Wakati uzima unapoisha, ni kuchelewa sana kugeuza mawazo yao kutoka kwa uasi hata wa utiifu, kutoka kwa uchuki hata kwa mapendo.

## Mshahara wa Zambi

"Kwa maana mshahara wa zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu." Wakati ambao uzima ni uriti wa wenye haki, mauti ni sehemu ya waovu. "Mauti ya pili" inawekwa kinyume na uzima wa milele. Waroma 6:23; tazama Ufunuo 20:14.

Kwa matokeo ya zambi ya Adamu, mauti imewekwa juu ya uzao wote wa wanadamu. Wote sawasawa huenda chini kaburini. Na kwa njia ya mpango wa wokovu, wote wanapashwa kuletwa kutoka kwa makaburi yao: "kutakuwa ufufuo wa wafu, wote wenye haki na wasio haki pia." "Kwa sababu kama katika Adamu wote wanakufa, hivyo wote katika Kristo watafanywa wahai." Lakini tofauti imefanywa kati ya makundi mawili inayoletwa: "Wote walio katika makaburi watasikia sauti yake, nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliofanya mabaya, kwa ufufuo wa hukumu." Matendo 24:15; 1 Wakorinto 15:22; Yoane 5:28,29.

## Ufufuo wa Kwanza

Wale "wanaohesabiwa kuwa wamestahili" kwa ufufuo wa kwanza ni "heri na Watakatifu". "Juu ya hawa mauti ya pili haina nguvu." Luka 20:35; Ufunuo 20:6. Lakini wale wasiopata msamaha kwa njia ya toba na imani wanapaswa kupokea "mishahara ya zambi," azabu "kufwatana na matendo yao," kuishi katika "mauti ya pili."

Kwani ni jambo lisilowezekana kwa Mungu kuokoa mwenye zambi katika zambi zake, anamwondolea maisha yake ambayo
[266] makosa ilinyanganya na ambaye amejionyesha mwenyewe kwamba hastahili. " Maana bado kidogo na mwovu hatakuwa; ndiyo utafikiri sana pahali pake, naye hatakuwa," "Na watakuwa kama hawakuwa mbele." Zaburi 37:10; Obadia 16. Wanazama katika usahaulifu usiokuwa na matumaini ya milele.

Hivi ndivyo itakavyofanywa mwisho wa zambi. "Umeharibu waovu, Umefuta jina lao kwa milele na milele. Adui wamekoma, wameachwa ukiwa kwa milele." Zaburi 9:5,6. Yoane katika Ufunuo anasikia wimbo wa furaha wa sifa usiochafuliwa na sauti

hata moja ya kutopatana. Hakuna nafsi za watu zinazotukana Mungu wakati wanapojinyonga katika maumivu mabaya isiyokuwa na mwisho kamwe. Hakuna viumbe vya taabu katika jehanum watakaochanganyisha na yawe yao ya nguvu pamoja na nyimbo za waliookolewa.

Juu ya kosa kuhusu maisha ya milele ya asili kunabaki mafundisho ya ufahamu katika mauti. Kulingana na maumivu mabaya ya milele, ni kinyume kwa Maandiko, kwa akili, na kwa mawazo yetu ya kibinadamu.

Kufuatana na imani ya watu wengi, waliokombolewa katika mbingu wanafahamu yote yanayofanyika duniani. Lakini namna gani ingekuwa na furaha kwa wafu kujua mateso ya walio hai, kuwaona wakiendelea na huzuni, uchungu, na maumivu makuu ya maisha? Na ni chukizo la namna gani kuamini ya kama mara pumzi inapotoka mwilini nafsi ya roho isiyotubu inawekwa kwa ndimi za jehanum!

Maandiko yanasema nini? Mtu hana ufahamu katika mauti: "Pumuzi yake inatoka, anarudia udongoni; siku ileile mafikiri yake yanapotea." "Maana walio hai wanajua ya kwamba watakufa: lakini wafu hawajui kitu, ... Mapendo yao na kuchukia kwao na wivu wao umepotea; wala hawana sehemu tena milele katika neno lo lote linalofanyika chini ya jua.' ' "Kwa kuwa Hadeze haiwezi kukusifu, wala kufa hakuwezi kukutukuza; wale wenye kushuka kwa shimo hawawezi kutarajia kweli yako. Mwenye uhai, mwenye uhai, ndiye atakayekusifu, kama mimi leo." "Maana katika mauti hapana ukumbusho juu yako, Katika Hadeze nani atakayekupa asante?" Zaburi 146:4; Muhubiri 9:5,6; Isaya 38:18, 19 ; Zaburi 6:5.

Petro siku ya Pentekote akatangaza ya kwamba Dawidi "alikufa, akazikwa, na kaburi lake ni kwetu hata leo." "Maana Dawidi hakupanda katika mbingu." Matendo 2:29,34. Neno ya kwamba Dawidi akingali katika kaburi hata ufufuo linaonyesha kwamba wenye haki hawaende mbinguni wanapokufa.

Akasema Paulo: "Maana kama wafu hawafufuliwi, basi Kristo
hakufufuliwa: na kama Kristo hakufufuliwa, imani yenu ni bure; [267]
mungali katika zambi zenu. Basi wao waliolala katika Kristo wamepotea." 1 Wakorinto 15:16-18. Kama kwa miaka 4000 wenye haki walikwenda mara moja katika mbingu wakati wa kifo, namna gani

Paulo amesema ya kwamba kama hakuna ufufuo, "na wao waliolala katika Kristo wamepotea"?

Wakati alipokuwa karibu kuacha wanafunzi wake, Yesu hakuwambia ya kwamba wangekuja mara moja kwake: "Ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali," Akasema "Na kama ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali, nitakuja tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu." Yoane 14:2,3. Paulo anatwambia zaidi ya kwamba "Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, na sauti kubwa, na sauti ya malaika mukubwa, na pamoja na baragumu ya Mungu: Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliobaki, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, kukutana na Bwana katika hewa, na hivi tutakuwa pamoja na Bwana milele. Na anaongeza: "Basi mufarijiane kwa maneno haya." 1 Tesalonika 4:1618. Katika kuja kwa Bwana, minyororo ya kaburi itavunjika na "wafu katika Kristo" watafufuliwa kwa uzima wa milele.

Wote watahukumiwa kwa kupatana na mambo yaliyoandikwa katika vitabu na kulipwa kama vile matendo yao yalivyokuwa. Hukumu hii haitafanyika katika mauti. "Kwa maana ameweka siku, atakayohukumu dunia kwa haki." "Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, elfu kumi, ili afanye hukumu juu ya watu wote." Matendo 17:31; Yuda 15.

Lakini kama wafu wamekwisha kufurahishwa na mbingu ao kujinyonga katika ndimi za moto ya jehanum, ni haja gani ya hukumu ijayo? Neno la Mungu linaweza kufahamika katika mafikara ya kawaida. Lakini ni fikara gani la haki tunaweza kuona wala hekima ao haki katika maelezo inayokubaliwa na wengi? Je, wenye haki watapokea sifa, "Verna, mutumwa mwema na mwaminifu, ... ingia katika furaha ya bwana wako," wakati walikuwa wakikaa machoni pake kwa miaka mingi? Je, waovu wameitwa kutoka taabuni kupokea hukumu kutoka kwa Mwamzi, "Ondokeni kwangu, ninyi muliolaaniwa, endeni katika moto wa milele"? Matayo 25:21,41.

Maelezo juu ya maisha ya milele ya nafsi ya roho yalikuwa mojawapo ya mafundisho ya uwongo ambayo Roma ilipokea kutoka kwa ushenzi. Luther aliyapanga pamoja na hadisi kubwa (za uwongo) vinavyofanya sehemu ya mtu wa uchafu ya maagizo ya Roma. Biblia inafundisha ya kwamba wafu wanalala hata ufufuo.

Pumziko la heri kwa wenye haki waliochoka! Wakati ukiwa mrefu ao mfupi, lakini ni wakati kwao. Wanalala; wanaamshwa [268] kwa baragumu ya Mungu kwa maisha ya milele ya utukufu. "Kwa sababu baragumu italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na kuoza. ... Lakini wakati ule wa kuoza utakapovaa kutokuoza, na ule wa mauti utakapovaa kutokufa, wakati ule litakapotimia neno lililoandikwa; Mauti imemezwa kwa ushindi". 1 Wakorinto 15:52-54.

Kuitwa kutoka kwa usingizi wao, wanaanza kufikiri ni wapi waliishia. Shituko la mwisho lilikuwa ni maumivu makali ya mauti; wazo la mwisho, kwamba walikuwa wakianguka chini ya uwezo wa kaburi. Wanapofufuka kutoka kaburini, wazo lao la kwanza la furaha, litakaririwa katika shangwe la ushindi: Ee mauti, uchungu wako ni wapi?" 1 Wakorinto 15:55. "Ee kaburi, kushinda kwako ni wapi?

## [269] 34 /NI WANANI WANAOKUWA “PEPO” KATIKA IMANI YA ROHO ZA WATU WALIOKUFA HURUDI NA KUJIONYESHA NA KUONGEA NA WATU?

Mafundisho ya maisha ya milele ya kawaida, mara ya kwanza yaliletwa kutoka kwa hekima ya kishenzi na katika giza ya maasi makubwa yaliyounganishwa katika imani ya Kikristo, yakaondosha kweli ambayo “wafu hawajui kitu.” Muhubiri 9:5. Wengi wanaamini ya kwamba pepo za wafu ni “roho za kutumikia, zilizotumwa kutumikia wale watakaoriti wokovu.” Waebrania 1:14.

Imani ya kwamba roho za wafu zinarudi kutumia walio hai ikatayarisha njia kwa imani ya wafu ya kisasa kuwa roho za watu waliokufa hurudi kujionyesha na kuongea na watu. Kama wafu wanakuwa na majaliwa na maarifa inayopita zaidi ile waliyokuwa nayo mbele, sababu gani kutorudi duniani na kufundisha wa hai? Kama roho za wafu zinatangatanga kwa rafiki zao duniani, sababu gani hazipelekane habari nao? Namna gani wale wanaoamini katika uaminifu wa kibinadamu katika mauti wanaweza kukana “nuru ya Mungu” iliyotolewa na roho tukufu? Hapa kuna mferezi unaoweza kuangaliwa kama takatifu ambamo shetani anatumika. Malaika walioanguka wanaonekana kama wajumbe kutoka ulimwengu wa kiroho.

Mfalme wa mabaya anakuwa na uwezo wa kuleta mbele ya watu mfano wa rafiki waliokufa. Mfano ni kamilifu, ulifatishwa kwa uzahiri wa ajabu. Wengi wanafarijika na hakikisho ya kwamba wapenzi wao wana furaha mbinguni. Bila mashaka ya hatari, wanatoa sikio kwa roho za kudanganya, na mafundisho ya mashetani.” 1 Timoteo 4:1.

Wale waliokwenda kwa kaburi bila kujitayarisha wanadai kuwa na furaha na kuwa mahali pa cheo bora huko mbinguni. Wageni wa uwongo kutoka kwa ulimwengu ya mapepo (spirits) mara ingine hutoa maonyo halisi yanayoshuhudia kuwa hakika. Halafu, kwa hivi

tumaini linapatikana, wanafundisha mafundisho yale yanayongoa Maandiko. Kwa sababu kwamba wanataja mambo mengine ya kweli na palepale kutabiri mambo ya wakati ujao jambo hilo linatoa mfano wa hakika, na mafundisho yao ya uwongo yanakubaliwa. Sheria ya Mungu huwekwa kando, Roho ya neema huzarauliwa. Pepo wanakana Umungu wa Kristo na wanaweka Muumba kwa cheo pamoja na wao wenyewe.

Wakati inakuwa kweli kwamba matokeo ya udanganyifu mara [270]
kwa mara yamepokewa kwa hila kama maonyesho ya kweli, pale kulikuwa, vilevile, maonyesho ya kupambanua ya uwezo wa ajabu, kazi kabisa ya malaika waovu. Wengi wanaamini ya kwamba imani yakuwa roho za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu ni ujanja tu wa kibinadamu. Kama ikiletwa mbele ya maonyesho ambayo hawawezi kuizania namna ingine isipokuwa kama ni ya ajabu, watadanganyiwa na kuyakubali kama uwezo mkubwa wa Mungu.

Kwa msaada wa Shetani wachawi wa Farao wakaiga kazi ya Mungu. Tazama Kutoka 7:10-12. Paulo anashuhudia kwamba kuja kwa Bwana kutatanguliwa na "kutenda kwa Shetani na uwezo wote, na ishara na maajabu ya uwongo". 2 Watesalonika 2:9,10. Na Yoane anatangaza: "Naye anafanya mastaajabu makubwa, hata kufanya moto kushuka toka mbingu juu ya dunia, mbele ya watu. Naye anawakosesha wale wanaokaa juu ya dunia, kwa mastaajabu yale aliyopewa kufanya. Ufunuo 13:13, 14. Si mambo ya ujanja tu yaliyotabiriwa hapa. Watu wanadanganyiwa na mastaajabu ambayo wajumbe wa Shetani wanafanya, si yale wanayotaka kufanya.

## Mwito Wa Shetani Kwa Wenye Akili

Kwa watu wenye elimu naustaarabu mfalme wa giza anaonyesha imani ya kuwa na roho za watu waliokufa na kujionyesha na kuongea na watu (spiritisme) katika mifano yake safi zaidi na ya akili. Anapendezwa sana na wazo la tendoo la kushangaza kwa furaha na maelezo yenye uwezo wa kushawishi ya mapendo na wema. Anaongoza watu kutumia kiburi sana katika hekima yao wenyewe ili ndani ya mioyo yao waaibishe Bwana wa Milele.

Shetani anadanganya watu sasa kama alivyodanganya Hawa katika Edeni kwa njia ya kuamsha tamaa ya nguvu kwa ajili ya kujiinua.

"Mutakuwa kama miungu," anatangaza, "mukijua uzuri na ubaya". Mwanzo 3:5. Imani ya kuwako kwa roho za watu waliokufa inafundisha" kwamba mtu ni kiumbe cha maendeleo... karibu ya kichwa cha uungu". Tena; "Hukumu itakuwa ya haki, kwa sababu ni hukumu ya kila mtu binafsi.... Kiti cha enzi ni ndani yako". Na mwingine anasema: "Kila kiumbe cha haki na kikamilifu ni Kristo".

Kwa hivyo Shetani aligeuza tabia ya zambi ya mtu mwenyewe kuwa amri ya pekee ya hukumu. Hii ni maendeleo, si kwenda juu, bali kwenda chini. Mtu hawezi kuinuka juu kuliko cheo chake cha
[271] usafi wala wema. Kama nafsi ndiyo kipeo chake kikamilifu cha juu kuliko, hatafikia kamwe kwa kitu cho chote kinachoinuka zaidi. Neema ya Mungu tu inakuwa na uwezo kwa kuinua mtu. Kuachwa upekee, maendeleo yake inapaswa kwenda chini.

### Mwito kwa Kupenda Anasa

Kwa ulafi, kupenda anasa, uasherati, imani ya kuwa na roho za watu waliokufa (spiritisme) inaonyesha umbo la uwongo la werevu kidogo. Katika mifano yao mbaya sana wanapata kitu ambacho kinachokuwa katika umoja na tamaa zake. Shetani anaandika hesabu ya zambi kila mtu kutenda halafu anajihazali ya kwamba saa za kufaa zisipunguke kwa kupendeza mvuto. Anajaribu watu kwa njia ya kutojizuia kwa kupunguza nguvu za mwili, akili na za mafundusho mazuri. Anaharibu maelfu katika mazoezi wa kufurahisha tamaa, kuharibu tabia yote nzima. Na kutimiza kazi yake, pepo wanatangaza kwamba "maarifa ya kweli yanamuweka mtu juu ya sheria yote"; "cho chote kinachokuwa, kinakuwa haki"; ya kwamba "Mungu hahukumu", na ya kwamba "zambi zote... zinakuwa bila kosa". Wakati watu wanapoamini ya kwamba tamaa ni sheria ya juu zaidi, ya kwamba uhuru ni ruhusa, ya kwamba mtu ni juu yake mwenyewe tu, nani anayeweza kushangaa ya kwamba uchafu unajaa kwa kila mkono? Wengi kwa moyo wanakubali maongozi ya tamaa mbaya. Shetani anachukua maelfu katika wavu lake wanaodai kufuata Kristo.

~~Lakini Mungu ametoa nuru ya kutosha kuvumbua mtego huo~~. Msingi kabisa wa imani ya kuwa kwa roho za watu waliokufa unakuwa kwa vita ikipiganisha Maandiko. Biblia inasema ya kwamba wafu hawajui kitu, ya kwamba mawazo yao yamepotea; hawana sehemu katika furaha wala huzuni ya wale wanaokuwa duniani.

Tena zaidi Mungu amekataza maarifa ya hila yamazungumzo na roho za wafu. “mashetani”. Kama hawa wageni kutoka dunia zingine walikuwa wakiitwa, wanatangazwa na Biblia kuwa “pepo za mashetani”. Tazama Hesabu 25:1-3; Zaburi 106:28; 1 Wakorinto 10:20; Ufunuo 16:14. Kutendeana pamoja nao kulikatazwa katika azabu ya kufa. Walawi 19:31; 20:27. Lakini imani ya kuwa roho za watu waliokufa (spiritisme) imefanya njia yake katika jamii za ujuzoi wakweli ikashambulia makanisa, na kupata upendeleo katika majamii ya wafanya sheria, hata katika majumba ya wafalme. Udanganyifu mkubwa huu ni uamsho katika hila mpya ya uchawi uliohukumiwa zamani. [272]

Kwa kuonyesha ubaya zaidi wa watu kama katika mbingu, Shetani anasema kwa ulimwengu: “Si kitu ukiamini wala usipoamini Mungu na Biblia, uishi kama unanvyopenda; mbingu ni makao yako”.

Neno la Mungu linasema: “Ole wao wanaoita uovu mema, na wanaita mema uovu; wanaoweka giza kwa nuru, na nuru giza.” Isaya 5:20.

## Biblia llifananishwa kama Habari za Uwongo

Mitume, wanafananishwa na pepo za uwongo, wanafanywa, kwa kukanusha mambo waliyoandika wakati walipokuwa kwa dunia. Shetani anafanya ulimwengu kuamini ya kwamba Biblia ni habari za uwongo, kitabu kilichopendeza kwa utoto wa taifa, lakini, sasa kuzaniwa kama kisiuchofaa. Kitabu kinachopaswa kumuhukumu yeye na wafuasi wake anakiweka katika kivuli; Mwokozi wa ulimwengu anamfanya kuwa kama mtu yo yote. Na waaminifu katika mifano ya kiroho wanajaribu kufanya kuonekana kwamba hakuna kitu cha muujiza katika maisha ya Mwokozi wetu. Miujiza yao wenyewe, inatangaza, kwa mbali zaidi kazi za Kristo.

Imani ya kuwa roho za watu waliokufa (spiritisme) inajitwalia sasa umbo la Kikristo. Lakini mafundisho yake hayawezi

kukanushwa wala kufichwa. Katika mfano wake wa sasa unakuwa ya hatari zaidi, wa hila, udanganyifu. Inajidai sasa kukubali Kristo na Biblia. Lakini Biblia inafasiriwa kwa namna ya kupendeza kwa moyo mpya. Mapendo inakuwako kama sifa bora ya Mungu, lakini inaaibishwa kwa tamaa zaifu kufanya tofauti ndogo kati ya uzuri na ubaya. Mashitaki ya Mungu ya zambi, matakwa ya sheria yake takatifu yanachungwa mbali na kuonekana kwa macho. Mifano inaongoza watu kukataa Biblia kama msingi wa imani yao. Kristo anakaniwa kama mbele, lakini udanganyifu hautambuliwe.

Wachache wanakuwa na wazo la haki la uwezo wa kudanganwa wa imani ya kuwa na roho za watu waliokufa (spiritisme). Wengi wanavuta vibaya nao kwa kupendeza tu uchunguzi. Wangejazwa na hofu kuu kwa wazo la kujitoa kwa utawala wa pepo. Lakini wanajitayarisha kwa kiwanja kilichokatazwa, na mharibu wautumia uwezo wake, na anawashikilia kuwa watumwa. Hakuna kitu kingine kisipokuwa uwezo wa Mungu, kwa jibu kwa maombi ya bidii, inayowezakuokoa nafsi hizi.

[273] Wote wanaolinda zambi inayojulikana kwa makusudi wanaalika majaribu ya Shetani. Wanajitenga wenyewe kutoka kwa Mungu na ulinzi wa malaika zake, na wanakuwa pasipo mateteo. "Na wakati wanapokuambia: Tafuta habari kwa watu wenye roho na kwa walozi wafumu, wanaolialia kama ndege na kunungunika, sema, haifai kwa watu kutafuta kwa Mungu wao? Waenda kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Kwa sheria na kwa ushuhuda! Kama hawasemi sawasawa na neno hili, kweli hapana asubui kwao." Isaya 8:19, 20.

Kama watu wangekusudia kupokea ukweli juu ya asili ya mtu na hali ya wafu, wangeona katika imani ya kuwa roho ya watu waliokufa (spiritisme) uwezo wa Shetani na miujiza ya uwongo. Lakini wengi wanafunga macho yao kwa nuru, na Shetani anafuma mitego yake kwao. "Kwa sababu hawakupokea mapendo kwa kweli, wapate kuokolewa," kwa sababu hii, "Mungu anawaletea nguvu ya upotevu, hata waamini uwongo." 2 Watesalonika 2:10, 11.

Wale wanaopinga imani ya kuwako kwa roho ya watu waliokufa (spiritisme) wanashambulia Shetani na malaika zake. Shetani hataacha hatua (=2,54cm) moja ya uwanja ila tu akisukumwa kwa nguvu na wajumbe wa mbinguni. Anaweza kutumia Maandiko na atapotosha maana ya mafundisho Wale watakaosimama kwa wakati

huu wa hatari wanapashwa kufahamu wao wenyewe ushuhuda wa Maandiko.

Pepo za mashetani wanaoiga ndugu ao rafiki watatokea kwa huruma za mapendo kwetu na watafanya miujiza. Inatupasa kuwazuia kwa njia ya kweli ya Biblia ya kwamba wafu hawajui kitu cho chote na ya kwamba wale wanaotokea ni pepo za mashetani.

Imani yao yote haikuanzishwa kwa Neno la Mungu watadanganyiwa na kushindwa. Shetani "anatumika na madanganyo yote ya uovu, " Na madanganyo yake yataongezeka. Lakini wale wanaotafuta maarifa ya kweli na safi nafsi zao katika utii watapata katika Mungu wa kweli ulinzi wa hakika. Mwokozi angetuma upesi kila malaika kutoka mbinguni kulinda watu wake kuliko kuacha nafsi moja inayotumaini kushindwa na Shetani. Wale wanaojifariji wenyewe kwa uhakikisho kwamba hakuna azabu kwa ajili ya mwenye zambi, wanaokataa kweli ambayo Mbingu inayotoa kama ulinzi kwa siku ya taabu, watakubali madanganyo yaliyotolewa na Shetani, madai ya imani ya madanganyo za watu waliokufa (spiritisme).

Wenye kuzihaki wanazani mizaha matangazo ya Maandiko juu ya shauri la wokovu na malipo yatakayokuja ya wanaokataa kweli.
Wanageuza jambo la kutia huruma kwa mawazo ya ushupavu, uzaifu, [274]
na mafundisho ya uchawi kama kutii matakwa ya sheria ya Mungu. Wamejitoa wote kwa mshawishi, wamejiunga karibu sana naye na kujazwa na roho yake, ili wasiwe na upungufu kutoka katika mtego wake.

Msingi wa kazi ya Shetani uliwekwa kwa matumaini iliyotolewa kwa Hawa katika Edeni: "Hakika hamutakufa". "Siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama Mungu mukijua uzuri na ubaya." Mwanzo 3:4,5. Kipeo chake cha madanganyo kitafikia katika mabaki ya mwisho ya wakati. Asema nabii: "Nikaona pepo wachafu watatu waliofanana na vyura, wakatoka kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule nabii wa uwongo kama vyura. Maana ndio pepo za mashetani, wanaofanya alama, na kutoka na kwenda kwa wafalme wa ulimwengu wote, kuwakusanya kwa vita ya siku ile kubwa ya Mungu Mwenyezi." Ufunuo 16:13, 14.

Ila tu wale wanaolindwa na uwezo wa Mungu katika imani katika Neno lake, ulimwengu mzima utapita kwa nguvu katika njia

za madanganyo haya. Watu wanajitumbukiza upesi kwa salama ya ajali, kuamshwa tu na kumiminika kwa hasira ya Mungu.

# 35 /UHURU WA ZAMIRI UNATISHWA [275]

Kanisa la Roma sasa linapendelewa sana na Waprotestanti kuliko miaka ya zamani. Katika inchi hizo ambamo Kanisa la Kikatoliki linapata mwendo wa kuunganisha kwa kupata mvuto, mawazo yanaanza kusimamiwa ya kwamba hakuna tofauti sana juu ya mambo ya lazima kama ilivyozaniwa na ya kwamba ukubali ule mdogo kwa upande wetu utatuongoza katika mapatano bora pamoja na Roma. Kulikuwa wakati Waprotestanti walifundisha watoto wao ya kwamba kutafuta umoja na Roma kungekuwa kutokuwa na uaminifu kwa Mungu. Lakini ni tofauti kubwa ya namna gani tunaona katika taarifa ya sasa!

Watetezi wa dini ya Rome (Papa) wanatangaza kwamba kanisa limeshitakiwa uwongo, ya kwamba si haki kuhukumu kanisa la leo kwa utawala wake wa mda wa karne nyingi za ujinga na giza. Wanarehemu ukali wake wakuogopesha kwa ushenzi wa nyakati zile.

Je, watu hawa hawakusahau madai ya kutoweza kukosa kulikowekwa na uwezo huu? Roma inadai ya kwamba "kanisa halikukosa kamwe; wala kukosa kwa wakati ujao, kufuatana na Maandiko, halitakosa daima."

Kanisa la Roma halitaacha kamwe madai yake kwa kutoweza kukosa (infallibilité). Acha vizuizi (amri) vilivyoamriwa sasa na serikali za dunia vitoshwe na Roma irudishwe katika mamlaka yake ya kwanza, na hapo kwa upesi ingekuwa uamsho wa uonevu wake na mateso.

Ni kweli ya kwamba Wakristo wa kweli wanakuwako katika ushirika wa kanisa la Kikatoliki la Roma. Maelfu katika kanisa lile wanamtumikia Mungu kufuatana na nuru bora wanayokuwa nayo. Mungu anatazama na upendo wa huruma juu ya nafsi hizi, zilizolelewa katika imani ile ya kudanganya na isiyotosheleka. Ataleta mishale ya nuru kupenya giza, na wengi watakamata misimamo yao pamoja na watu wake.

Lakini Kanisa la Roma kama chama haliko tena katika umoja na habari njema ya Kristo sasa kuliko kwa wakati wa kwanza. Kanisa la Roma linatumia shauri lo lote kwa kupata utawala wa ulimwengu, kuanzisha tena mateso, na kuharibu mambo yote ambayo Waprotestanti wamefanya. Kanisa la Kikatoliki liko linapata nafasi kwa pande zote. Angalia kuongezeka kwa makanisa yake. Tazama uwingi wa vyuo vyao vikubwa (colleges) na seminaires, vinavyosimamiwa na
[276] Waprotestanti. Tazama usitawi wa utaratibu wa sala katika Uingereza na maasi ya mara kwa mara kwa vyuo vya Wakatoliki.

## Mapatano na Ukubali

Waprotestanti wamesaidia ama kupendelea mafundisho ya Kanisa la Papa; wamefanya mapatano na mkubaliano ambayo wakatoliki wenyewe wameshangaa kuyaona. Watu wanafunga macho yao kwa tabia ya kamili ya Kanisa la Roma. Watu wanahitaji kupinga maendeleo ya adui huyu wa hatari kwa uhuru wa watu na dini.

Wakati msingi wa kanisa la Roma linaimarishwa juu ya madanganyo, si la ushenzi na ujiinga. Huduma ya dini ya Kanisa la Roma kawaida ni ya kuvuta sana. Maonyesho yake mazuri sana mengi na kanuni kubwa za dini zinavuta watu na kunyamazisha sauti ya akili na zamiri. Jicho linavutwa kwa uzuri. Makanisa mazuri kabisa, maandamano makubwa ya ajabu, mazabahu ya zahabu, sanduku za kuwekea vitu vitakatifu za johari, mapicha mazuri, na muchoro bora vinavuta wenye kupenda uzuri. Muziki ni waajabu. Nukta za muziki nzuri za kutoka kwa sauti kubwa za kinanda zinachanganyika na nyimbo tamu sana za sauti nyingi kama inavyoongeza katika madari ya nyumba ya juu sana na sehemu ndefu ya nguzo ya majengo makubwa ya kanisa yake, yanavuta akili ya uchai na heshima.

Utukufu huu wa inje na ibada vinacheka tamaa za nafsi yenye kugonjwa ya zambi. Dini ya Kristo haihitaji mivuto ya namna hiyo. Nuru inayongaa kutoka kwa msalaba inaonekana safi na ya kupendeza na hakuna mapambo ya inje yanayoweza kuongeza damani yake ya kweli.

Mawazo ya juu ya ufundi, malezi ya kupendeza tamaa, mara kwa mara yanatumiwa na Shetani kuongoza watu kusahau mahitaji ya nafsi na kuishi kwa ajili ya ulimwengu huu tu.

Fahari na sherehe ya kuabudu kwa Kikatoliki kunakuwa na uwezo wa kuvuta (kushawishi) kufanya mabaya, nzuri wakupoteza akili, na hiyo, wengi wamedanganyika. Wanajipatia uhakikisho juu ya Kanisa la Roma kuwa mlango wa mbinguni. Hakuna hata mmoja ila tu wale wanaoweka miguu yao kwa msingi wa kweli, ambao mioyo yao hufanywa upya kwa Roho ya Mungu, wanakuwa salama juu ya mvuto wake. Mfano wa utawa pasipo uwezo ni kitu kile wengi wanatamani.

Madai ya Kanisa kwa haki kwa ya kusamehe zambi yanaongoza [277] wafuasi wa Roma kujisikia huru kwa zambi, na agizo la maungamo linaelekea vile vile kutoa ruhusa kwa uovu. Yeye anayepiga magoti mbele ya mtu aliyeanguka na anafungua katika maungamo mawazo ya siri ya moyo wake anapoteza cheo cha nafsi yake. Katika kufunua zambi za maisha yake kwa padri--mwenye kufa wa kosa-cheo cha tabia yake ni chini, na anakuwa mchafu kwa hiyo. Mawazo yake juu ya Mungu ni ya kushusha cheo katika mfano wa mwanadamu aliyeanguka, kwa sababu kuhani anasimama kama mjumbe wa Mungu. Ungamo hili la haya la mtu kwa mtu ni chemchemi ya siri ambamo kumebubujika uwingi wa uovu unaochafua ulimwengu. Kwani kwa yeye anayependa anasa, ni kupendeza zaidi kuungama kwa mtu wa mauti kuliko kufungua roho kwa Mungu. Ni jambo la kupendeza zaidi kwa kiumbe mwanadamu kutubu kuliko kuacha zambi; ni rahisi kuhuzunisha wala kutesa mwili kwa nguo ya gunia kuliko kusulubisha tamaa za mwili.

## Mfano Wa Kushangaza

Wakati walipozarau kwa siri kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo juu ya sheria ya Mungu, walikuwa wa kali kwa inje katika kushika amri zake, kuzilemeza kwa masharti yanayofanya utii kuwa mzito. Kama vile Wayuda walivyojidai kuheshimu sheria, vivyo hivyo watu wa kanisa la Roma wanajidai kwa heshima ya msalaba.

Wanaweka misalaba kwa makanisa yao, mazabahu yao, na mavazi yao. Po pote alama ya msalaba kwa inje inaheshimiwa na kutukuzwa. Lakini mafundisho ya Kristo yanazikwa chini ya desturi za uongo na malipizi makali. Roho aminifu zinalindwa katika woga wa hasira ya Mungu aliyechukizwa, wakati wakuu wa kanisa wengi wanaishi katika anasa na tamaa ya mwili.

Ni juhudi ya daima ya Shetani kusingizia tabia ya Mungu, asili ya zambi, na matokeo kwenye mti wa kuchoma wafia dini katika vita kuu. Madanganyo yake yanatoa watu ruhusa kwa zambi. Kwa wakati ule ule anaanzisha mawazo ya uwongo juu ya Mungu ili wamwangalie kwa hofu na chuki kuliko kwa upendo. Kwa njia ya mawazo yaliyopotoshwa juu ya tabia za Mungu, mataifa ya kishenzi waliongozwa kuamini kafara za kibinadamu kuwa za lazima kwakupata mapendo ya Mungu. Mambo makali ya kuogopesha yametendwa chini ya mifano mbalimbali ya ibada ya sanamu.

[278] **Umoja wa Upagani na Ukristo**

Kanisa la Katoliki la Roma, kwa kuunganisha upagani na Ukristo, na, kama upagani, kusingizia tabia ya Mungu, lilitumia basi matendo makali. Vyombo vya mateso vilishurutisha watu kukubali mafundisho yake. Wakuu wa kanisa wakajifunza kuvumbua njia za kufanyiza mateso makubwa iwezekanavyo bila kuondoa maisha ya wale wasingekubali madai yake. Kwa mara nyingi yule aliyeteswa alipokea mauti kuwa kufunguliwa kuzuri.

Kwa wafuasi wa Roma kanisa lilikuwa na malezi ya shida, njaa, ya mateso ya mwili. Kwa kupata kibali cha Mungu, wenye kutubu walifundishwa kupasua vifungo ambavyo Mungu alivifanya kwa kubariki na kufurahisha maisha ya mwanadamu duniani. Uwanja wa kanisa unakuwa na mamilioni ya watu waliotoa maisha yao kwa masumbuko ya bure, kwa kukomesha, kama machukizo kwa Mungu, kila wazo na nia ya huruma kwa viumbe wenzao.

Mungu hakuweka kamwe mojawapo ya mizigo hii mzito juu watu wo wote. Kristo hakutoa mfano kwa wanaume na wanawake kujifungia wenyewe katika nyumba ya watawa (monasteres) ili kuweza kustahili kuingia mbinguni. Hakufundisha kamwe ya kwamba mapendo yanapashwa kukomeshwa.

Papa anadai kuwa mjumbe mkubwa wa Kristo. Lakini je, Kristo alijulikana daima kutupa watu kwa gereza kwa sababu hawakumtolea heshima kubwa kama Mfalme wa mbingu? Je, sauti yake ilisikiwa kuhukumu kwa mauti wale wasiomkubali?

Kanisa la Roma sasa linaonyesha uso mzuri kwa ulimwengu, kufunika kwa maneno ya kujitetea ukumbusho wake wa maovu ya kuchukiza. Limejivika lenyewe mavazi ya mfano wa Kikristo, lakini

linakuwa lisilobadilika. Kanuni yo yote ya dini ya Roma katika vizazi vya wakati uliopita inakuwako leo. Mafundisho yaliyoshauriwa kwa miaka ya giza yangali yanashikwa. Dini ya Roma ambayo Waprotestanti wanaheshimu sasa ni ileile iliyotawala katika siku za Matengenezo (Reformation), wakati watu wa Mungu waliposimama kwa hatari ya maisha yao kufunua zambi lake.

Kanisa la Roma ni kama vile unabii ulivyotangaza kwamba lingekuwa, ni kukufuru kwa nyakati za mwisho. Tazama 2 Watesalonika 2 :3,4. Chini ya mfano wa kigeugeu linaficha sumu isiyobadilika ya nyoka. Je, uwezo huu, ambao ukumbusho wake kwa miaka elfu umeandikwa katika damu ya watakatifu, utakubaliwa kama sehemu ya kanisa la Kristo?

### Badiliko katika Kanisa la Protestanti [279]

Madai yamewekwa katika inchi za Kiprotestanti ya kwamba Dini ya Kikatoliki inakuwa tofauti kidogo kwa Dini ya Kiprotestanti kuliko nyakati za zamani. Hapo kumekuwa badiliko; lakini badiliko haliko katika kanisa la Roma. Kanisa la Katoliki linafanana sana na Kanisa la Kiprotestanti linalokuwa sasa kwa sababu Kanisa la Kiprotestanti kiliharibika tabia sana tangu siku za Watengenezaji (Reformateurs).

Makanisa ya Kiprotestanti, kutafuta mapendeleo ya ulimwengu, yanaamini kila kitu kibaya kuwa kizuri, na kama matokeo wataamini mwishoni kila kitu kizuri kuwa kibaya. Wanakuwa sasa, kama ilivyokuwa, kujitetea kwa Roma kwa ajili ya mawazo yao isiyokuwa na mapendo kwake, kuomba musamaha kwa "ushupavu" wao. Wengi wanasihi sana ya kwamba giza ya kiakili na yakiroho iliyokuwa pote wakati wa Miaka ya Katikati ilisaidia Roma kueneza mambo ya uchawi na mateso, na ya kwamba akili kubwa zaidi ya nyakati za sasa na kuongezeka kwa wema katika mambo ya dini kunakataza mwamsho wa kutovumilia. Watu wanacheka sana wazo la kwamba mambo ya namna ile yanaweza kutokea kwa nyakati za nuru. Inapaswa kukumbukwa lakini ya kwamba kwa namna nuru inapotolewa zaidi, na zaidi giza ya wale wanaopotea na kuikataa itakuwa kubwa.

Siku ya giza kubwa ya walio elimishwa imesaidia kwa mafanikio ya kanisa la Roma (Papa). Siku ya nuru kubwa ya walioelim-

ishwa nayo itasaidia vile vile. Katika miaka iliyopita wakati watu walipokuwa pasipo maarifa ya ukweli, maelfu walikamatwa kwa mtego, bila kuona wavu uliotandikwa kwa nyanyo zao. Katika kizazi hiki wengi hawatambui wavu na wanatembea ndani yake mara moja bila kufikiri. Wakati watu wanapotukuza mafundisho yao wenyewe juu ya Neno la Mungu, akili inaweza kutimiza maumivu makubwa kuliko ujinga. Kwa hivyo elimu ya uwongo ya wakati huu utahakikisha mafanikio ya kutayarisha njia kwa kukubali kanisa la Roma (Papa), kama kukataa kwa maarifa kulivyofanya katika Miaka ya Giza.

## Kushika Siku ya Kwanza (Jumapili)

Kushika siku ya kwanza (jumapili) ni desturi ilioanzishwa na Roma, ambayo anadai kuwa alama ya mamlaka yake. Roho ya Kanisa la Roma (Papa)--ya mapatano kwa desturi za kidunia, heshima kwa desturi za kibinadamu juu ya amri za Mungu--inaenea sehemu zote za makanisa ya Waprotestanti na kuwaongoza kwa kazi
[280] ya namna moja ya kutukuza Siku ya kwanza (Jumapili) ambayo kanisa la Roma limeigeuza mbele yao.

Sheria za kifalme, baraza za kawaida na maagizo ya kanisa zilizokubaliwa na mamlaka ya kidunia zilikuwa ni hatua ambazo siku kuu za kishenzi zilifikia cheo cha heshima katika dunia la Wakristo. Mpango wa kwanza wa kulazimisha watu wote kushika Siku ya kwanza ya juma ilikuwa sheria iliyotolewa na Constantine. Ingawa ilikuwa kweli sheria ya kipagani, ilikazwa na mfalme akiisha kukubali dini ya Kikristo.

Eusebius, kama askofu aliyetafuta upendeleo wa watawala, na aliyekuwa rafiki wa kipekee wa Constantine, akaendesha matangazo ya kwamba Kristo alihamisha Sabato na kuiweka kwa siku ya kwanza (dimanche). Hakuna ushuhuda wa Maandiko uliotolewa kuwa uhakikisho. Eusebius yeye mwenyewe, bila kuwa na hakikisho akatangaza uwongo wake. “Vitu vyote,” anasema, “Kila kitu kilichokuwa kazi ya kufanya kwa Sabato, hivi tumevihamisha kwa siku ya Bwana”. 2

Kwa namna Kanisa la Roma lilipoimarishwa, kutukuzwa kwa Siku ya Kwanza kukaendelea. Kwa wakati mfupi siku ya saba iliendelea kushikwa kama Sabato, lakini baadaye badiliko likafanyika.

Baadaye Papa akatoa maagizo ya kwamba padri wa wilaya alipaswa kukaripia wanaoharibu siku ya kwanza (dimanche) wasilete msiba mkubwa juu yao wenyewe na kwa jirani.

Amri za baraza zilizo hakikisha upungufu, wakubwa wa serkali wakaombwa sana kutoa amri ambayo ingeogopesha mioyo ya watu na kuwalazimisha kuacha kazi kwa siku ya kwanza (dimanche). Kwa mkutano wa wakubwa wa kanisa uliofanywa Roma, mipango yote ya mbele ikahakikishwa tena na kuingizwa katika sheria ya kanisa na kukazwa na wakubwa wa serikali.3

Lakini ukosefu wa mamlaka ya maandiko kwa ajili ya kushika siku ya kwanza (dimanche) ukaleta mashaka. Watu wakauliza haki ya waalimu wao kwa ajili ya kutia pembeni tangazo hili, "Siku ya saba ni Sabato kwa Bwana Mungu wako," ili kuheshimu siku ya jua. Kwa kusaidia ukosefu wa ushuhuda wa Biblia, mashauri mengine yalikuwa ya lazima.

Musimamizi wa nguvu wa siku ya kwanza (dimanche), ambaye karibu mwisho wa karne ya kumi na mbili alizuru makanisa ya Uingereza, akapingwa na washuhuda waaminifu kwa ajili ya kweli; na kwa hivi nguvu yake ilikuwa ya bure hata akatoka kwa inchi wakati moja. Wakati aliporudi, akaleta mkunjo waonyesho ambayo alidai kutoka kwa Mungu mwenyewe, iliyokuwa na agizo la kulazimisha watu kushika siku ya kwanza (dimanche), pamoja na matisho ya [281]
ajabu kuogopesha wasiotii. Maandiko haya ya damani yalisemwa wala kutajwa kuwa ya kuanguka kutoka mbinguni na kupatikana pale Yerusalema juu ya mazabahu ya Simeona Mtakatifu, katika Golgotha. Lakini, kwa kweli yaliandikwa katika jumba kubwa la askofu kule Roma. Madanganyo na maandiko ya uwongo yalikuwa katika miaka yote yakihesabiwa ya kweli kwa watawala wa kanisa la Roma. (Tazama kwa Mwisho wa Kitabu (Nyongezo), hati kwa ukarasa 37.)

Lakini ijapo walifanya nguvu kwa kuanzisha utakatifu wa Siku ya kwanza (dimanche) wakuu wa kanisa la Roma wao wenyewe kwa wazi wakatubu kwamba sabato inatoka kwa mamlaka ya Mungu. Katika karne ya kumi na sita baraza la Papa ikatangaza: "Acha Wakristo wote wakumbuke ya kwamba siku ya saba ilitakaswa na Mungu, na ilikubaliwa na kushikwa, si kwa Wayuda tu, lakini na kwa wengine wote wanaodai kuabudu Mungu; ingawa sisi Wakristo

tumebadilisha Sabato yao kwa Siku ya Bwana."4 Wale waliokuwa wakiharibu sheria ya Mungu walikuwa wanajua tabia ya kazi yao.

Mufano wa kushangaza wa mipango ya Roma ulitolewa katika mateso marefu ya mauaji juu ya Waldenses (Vaudois), wengine wao walikuwa washika Sabato. (Tazama Nyongezo.) Historia ya makanisa ya Ethiopia na Abyssinia ni ya maana ya kipekee. Katikati ya huzuni ya Miaka ya Giza, Wakristo wa Afrika ya Kati walifichama kwa uso wa dunia na wakasahauliwa na ulimwengu na kwa karne nyingi wakafurahia uhuru katika imani yao. Mwishoni Roma ikajifunza juu ya maisha yao, na mfalme wa Abyssinia akadanganywa hata akakubali Papa kama mjumbe mkubwa wa Kristo. Amri ikatolewa kukataza kushikwa kwa Sabato chini ya malipizi makaii.5 Lakini uonevu wa Papa (kanisa la Roma) kwa upesi ukawa nira ya kutia uchungu sana ambayo watu wa Abyssinia wakakusudia kuivunja. Wakuu wa Roma wakafukuziwa mbali kwa mamlaka yao na imani ya zamani ikarudishwa.

Wakati makanisa ya Afrika yalipokuwa yakishika Sabato katika utii kwa amri za Mungu, wakaepuka na kufanya kazi siku ya kwanza (dimanche) kwa kufuatana na desturi ya kanisa. Roma ikavunja Sabato ya Mungu kwa kujiinua mwenyewe, lakini makanisa ya Afrika, yakajificha karibu miaka elfu moja, hayakushirikiana kwa uasi huu. Walipoletwa chini ya Roma, wakalazimishwa kuweka pembeni kweli na kutukuza sabato ya uwongo. Lakini kwa upesi walipopata tena uhuru wao wakarudia kutii amri ya ine. (Tazama Nyongezo).

Mambo haya yanaonyesha wazi uadui wa Roma kwa ajili ya
[282] Sabato ya kweli na wasimamizi wake. Neno la Mungu linafundisha ya kwamba mambo haya yanapashwa kutendeka tena kwa namna kukaririwa kama vile Wakatoliki na Waprotestanti wanajiunga kwa kutukuza siku ya kwanza (dimanche).

**Mnyama wa Pembe Mbili Mfano wa Mwana-Kondoo**

Unabii wa Ufunuo 13 unatangaza ya kwamba mnyama wa pembe mbili mfano wa mwana-kondoo atafanya "dunia na wanaokaa ndani yake" kuabudu kanisa la Rome--lililofananishwa na mnyama "alikuwa mfano wa chui. "Mnyama wa pembe mbili itasema vilevile "wale wanaokaa juu ya dunia, kufanyia sanamu yule mnyama".

Tena, naye anawafanya wote, "wadogo na wakubwa, na matajiri na maskini na wahuru na wafungwa," wapokee chapa cha mnyama. Ufunuo 13:11-16. Amerika ni uwezo uliofananishwa na nyama yule wa pembe mbili mfano wa mwana-kondoo. Unabii huu utatimilika wakati Mwungano wa mataifa ya Amerika watakapokaza kushika siku ya kwanza (dimanche), ambayo Roma inadai kama hakikisho kwa mamlaka yake.

"Nikaona kimoja cha vichwa vyake, kama kimetiwa kidonda cha kufa; kidonda chake cha kufa kikapona; dunia yote ikastaajabia mnyama yule". Ufunio 13:3. Kidonda cha kufa kinaonyesha kuanguka kwa kanisa la Roma (Papa) katika mwaka 1798. Baada ya hii, asema nabii, "kidonda chake cha kufa kikapona: na dunia yote ikastaajabia nyama yule". Paulo akataja ya kwamba "mwana wa uharibifu" ataendelea na kazi yake ya madanganyo kwa mwisho kabisa wa wakati". 2 Tesalonika 2:3-8. Na "watu wote wanaokaa juu ya dunia watamwabudu, wale, majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima". Ufunuo 13:8. Katika Ulimwengu wa Zamani na mpya, kanisa la Papa litapokea heshima kwa heshima iliyotolewa kwa siku ya kwanza (dimanche).

Tangu katikati ya karne ya kumi na tisa, wanafunzi wa unabii wameonyesha ushuhuda huu kwa ulimwengu. Sasa tunaona maendeleo ya upesi kwa utimilifu wa unabii. Kwa waalimu wa Waprotestanti kunakuwa na madai ya namna moja ya mamlaka ya Mungu kwa ajili ya kushika siku ya kwanza (dimanche), na ukosefu wa namna moja wa ushuhuda wa maandiko, kama kwa waongozi wa kanisa la Roma (Papa). Tangazo ya kwamba hukumu za Mungu zinafikia watu kwa ajili ya kuvunja sabato ya siku ya kwanza (di-manche) litarudiliwa: tayari linaanza kulazimishwa.

Ni ajabu kwa werevu, Kanisa la Roma. Linaweza kusoma kitu gani kinapaswa kuwa--ya kwamba makanisa ya Waprotestanti yana- [283]
toa heshima yake kwa Roma wanapokubali sabato ya uwongo na ya kwamba wanajitayarisha kuikaza kwa namna kanisa lenyewe lilifanya katika siku zilizopita. Kwa upesi gani litapata usaada wa Waprotestanti katika kazi hii si vigumu kuelewa.

Kanisa la Wakatoliki wa Roma linafanya muungano mkubwa chini ya mamlaka ya Papa, mamilioni ya washiriki wake katika kila inchi wanaagizwa utii kwa Papa, hata taifa lao liwe la namna gani wala serkali yao. Ijapo wanaweza kuapa kiapo kuahidi uaminifu

kwa serikali, lakini kinyume cha hii kunakuwa kiapo wala naziri ya uaminifu kwa Roma.

Historia inashuhudia juu ya nguvu ya uerevu wa Roma kujiingiza mwenyewe katika mambo ya mataifa, kuweza kupata ustawi, kuendesha makusudi yake mwenyewe, hata kwa maangamizi ya watawala na watu.

Ni majivuno ya Roma kwamba hawezi kubadili kamwe. Waprotestanti hawajui wanalolifanya wanapokusudia kukubali usaada wa Roma kwa kazi ya kutukuza siku ya kwanza (dimanche). Kwa namna wanavyoelekea kwa kusudi lao, Roma inakusudia kuimarisha mamlaka yake, kujipatia tena uwezo wake uliopotea. Acha kanuni kwanza liimarishwe na kanisa liweze kutawala uwezo wa serikali; na desturi za dini ziweze kukazwa na sheria za dunia; kwa kifupi, ya kwamba mamlaka ya kanisa na ya serikali itatawala zamirina ushindi wa Roma umehakikishwa.

Jamii ya Waprotestanti itajifunza namna gani makusudi ya Roma inavyokuwa, ila tu wakati unapokwisha kupita kwa kuepuka mtego. Linasitawi kwa utulivu katika mamlaka. Mafundisho yake yanatumia mvuto katika vyumba vya sheria, katika makanisa, na katika mioyo ya watu. Linaimarisha nguvu zake kuendesha maangamizo yake wakati mda utakapofika kwa kushangaza. Yote linayotumaini (kanisa) ni mahali pafaapo. Ye yote atakayeamini na kutii Neno la Mungu atapata laumu na mateso.

# 36 /MAPIGANO YA KARIBU SANA [284]

Tangu mwanzo kabisa wa vita kubwa mbinguni, kusudi daima la Shetani lilikuwa kuvunja sheria ya Mungu. Kwa yeye kufikia kusudi lake ni kukataa sheria yote ama kukataa mojawapo ya amri zake, matokeo yatakuwa namna moja. Mtu anayekosa "katika neno moja tu" anaonyesha zarau kwa sheria yote; mvuto wake na mfano yanakuwa kwa upande wa kosa; anakuwa mwenye kukosa juu ya yote". Yakobo 2:10.

Shetani amepotesha mafundisho ya Biblia, na kwa hivi makosa yakaingia katika imani ya maelfu. Mapigano makubwa ya mwisho kati ya ukweli na uwongo ni juu ya amri ya Mungu, kati ya Biblia na dini ya uwongo na mambo ya asili. Biblia inafikia wote, lakini wachache tu wanaoikubali kama kiongozi cha uzima. Katika kanisa wengi wanakana nguzo za imani ya Kristo. Uumbaji, kuanguka kwa mtu, upatanisho wa Yesu Kristo kwa kufa kwake, na sheria ya Mungu hutawaliwa yote ao sehemu. Maelfu wanaizania kuwa kama ushuhuda wa uzaifu kuweka tumaini kamili katika Biblia.

Ni rahisi kufanya sanamu na maelezo ya uwongo kama kufanya sanamu ya mti ao jiwe. Kwa kueleza Mungu vibaya, Shetani anaongoza watu kumzania katika tabia ya uwongo. Sanamu ya utilivu imewekwa katika pahali pa Mungu mwenye uhai kama anavyofuniliwa katika Neno lake, katika Kristo, na katika kazi ya uumbaji. Mungu wa watu hodari wengi, watunga mashairi, watu wa siasa, waandishi wa habari kwa magazetu-wa vyuo vikubwa (universités) vingi, hata wavyama vya elimu ya tabia na za Mungu na dini (théologie) ni afazali kidogo kuliko Bali, mungu wa jua wa Foiniki katika siku za Eliya. Hapana kosa linalofika kwa ujasiri zaidi juu ya mamlaka ya Mungu, hapana linalokuwa mbaya zaidi katika matukio yake, kuliko mafundisho ya kwamba sheria ya Mungu haina na masharti tena. Ufikiri ya kama wahuduma wenye kujulikana walikuwa wakifundisha kwa wazi ya kuwa sheria zinazotawala inchi yao hazikuwa za lazima, ya kama zilizuia mambo ya uhuru wa watu na haiwa-

pashwi kutiiwa; muda gani watu kama wale wangevumiliwa katika mimbara?

Ingekuwa muaminifu zaidi kwa mataifa kuvunja sheria zao kuliko kwa mtawala wa viumbe vyote kutangua sheria yake. Jaribio la kufanya nafasi sheria ya Mungu lilijaribiwa katika Ufransa wakati kukana Mungu ulipokuwa na uwezo wa kutawala. Ilionyeshwa ya kwamba kwa kutupa amri ambazo Mungu aliamuru ni kukubali
[285] kanuni ya mtawala wa uovu.

## Kuweka Kando Sheria ya Mungu

Wale wanaofundisha watu kutunza sheria za Mungu kwa urahisi wanapanda uasi kwa kuvuna uasi. Kuacha amri iliyoamuriwa kwa sheria ya Mungu kuweka yote kando, na sheria za kibinadamu kwa upesi hazitajaliwa. Matokeo ya kutangua amri za Mungu ingekuwa kama hazikutumainiwa. Mali hayangekuwa tena na usalama. Watu wangekamata milki ya jirani zao kwa jeuri, na walio hodari zaidi wangekuwa watajiri kuliko. Maisha yenyewe hayangeheshimiwa Kiapo cha ndoa hakingedumu tena kuwa kama boma kwa kulinda jamaa. Yeye aliyekuwa na uwezo angekamata mke wa jirani yake kwa jeuri. Amri ya tano ingekuwa kando pamoja na ya ine. Watoto hawangekataa kukamata maisha ya wazazi wao kama kwa kufanya vile wangeweza kupata tamaa ya mioyo yao iliyoharibika. Ulimwengu uliostaarabika ungekuwa kundi la wezi na wauaji wa siri, na amani na furaha ingekomeshwa duniani.

Tayari mafundisho haya yamefungua milango ya uovu ulimwenguni. Bila sheria na uovu vinafiagia kama pepo kali ya kipwa. Hata katika nyumba za wale wanaojidai kuwa Wakristo kunakuwa unafiki, mvunjo wa urafiki, usaliti wa matumaini matakatifu, upendeleo wa tamaa mbaya. Kanuni za dini, msingi wa maisha ya ushirika, unaonekana wa kutikisika sana karibu kuanguka. Wavunja sheria waovu mara kwa mara wanafanywa kuwa wenye kupokea mambo ya uangalifu kama kwamba walifikia sifa nzuri. Matangazo makubwa yametolewa kwa makosa yao. Mtambo wa kupiga chapa unatangaza maelezo ya uasi wa uovu, kuingiza wengine katika madanganyo, wizi, na uuaji. Kupumbazuka kwa kosa, kukosa kuwa na kiasi kwa kutisha na uzalimu wa namna yo yote ulipasa kuamsha mambo yote. Ni kitu gani kinaweza kufanyika kuzuia mwendo wa uovu?

## Kukosa Kiasi Kumetia Wengi Katika Mashaka

Baraza za hukumu zimeharibika, watawala wamevutwa na tamaa kwa faida na upendo wa anasa za mambo ya uasherati. Kukosa kiasi kumetia wengi katika mashaka hivyo Shetani amekuwa na utawala karibu kamili juu yao. Wana sheria wamapotoshwa, wanavutwa kwa feza (rushwa), wamedanganyika. Ulevi na ulafi, udanganyifu wa kila namna, unaonekana miongoni mwa wale wanaosimamia sheria. Sasa Shetani hawezi tena kulinda ulimwengu chini ya utawala kwa [286] njia ya kuzuia Maandiko, anatumia njia zingine kwa kutimiza kusudi lile lile moja. Kwa kuharibu imani katika Biblia ni kutumia pia kuharibu Biblia yenyewe.

Ni kama katika miaka ya kwanza, alikuwa akitumika katika makanisa kuendelesha mashauri yake. Kwa kupinga mambo ya ukweli yasiyokuwa ya watu wengi katika Maandiko, wanatumia maelezo ambayo yanapenda kueneza mbegu za mashaka. Kushikama na kwa kosa la Papa la maisha ya milele ya asili na ufahamu wa mtu katika mauti, wanakataa ulinzi wa kipekee juu ya madanganyo ya elimu ya kuwa roho za watu waliokufa kurudi na kujionyesha na kuongea na watu (spiritualisme). Mafundisho wa maumivu mabaya ya milele yameongoza wengi kuwa kutoamini Biblia. Kwa madai ya amri ya ine yanavyoshurutisha, inaoonekana ya kuwa kushika Sabato ya siku ya saba kunaamriwa; na kwa namna inavyokuwa njia moja tu kwa kujiokoa wenyewe kwa shuguli ambayo hawataki kuifanya, waalimu wa watu wote wakatupilia mbali sheria ya Mungu na Sabato pamoja. Kama matengenezo ya Sabato inavyoenea, kukataa huku kwa sheria ya Mungu kwa kuepuka amri ya ine kutakuwa karibu kuenea pote. Waongozi wa dini wanafungua mlango kwa kumkana Mungu, kwa imani ya kuwa roho za watu waliokufa kurudi na kujionyesha na kuongea na watu (spiritualisme), na zarau kwa sheria takatifu ya Mungu-daraka la kutisha kwa uovu unaokuwako katika jamii la Kikristo.

Kwani jamii lilelile linalodai ya kama mkazo wa kushika siku ya kwanza (dimanche) kungesitawisha mafundisho yahali ya kijamii. Ni mojawapo ya mashauri ya Shetani kuchanganya uwongo na ukweli shauri laonekana kuwa njema. Waongozi wa mwendo wa siku ya kwanza (dimanche) wangeshindania matengenezo ambayo watu wanahitaji, kanuni katika umoja pamoja na Biblia; lakini wakati

ambao kunakuwa na madai pamoja na hizi kinyume kwa sheria za Mungu, watumishi wake hawawewzi kujiunga pamoja nao. Hakuna kitu kinachoweza kuthibitika kuweka kando amri za Mungu kwa ajili ya amri za watu.

Katika makosa mawili makubwa, kutokufa kwa nafsi na utakatifu wa siku ya kwanza (dimanche), Shetani ataleta watu chini ya madanganyo yake. Wakati kosa la kwanza linapowekwa msingi wa imani ya kuwa roho za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu (spiritualisma), kosa la mwisho hufanya kifungo cha huruma pamoja na Roma. Waprotestanti wa Umoja wa Mataifa ya Kiamerika watakuwa wa kwanza kunyoosha mikono yao ngambo ya shimo kubwa kushika mkono wa imani ya kuwa roho za watu
[287] walikufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu (Spiritualisme); wakifikia kwa shimo kubwa kukumbatia mikono na mamlaka ya Roma. Na chini ya mvuto wa umoja huu wa mara tatu, inchi hii itafuata katika hatua za Roma kwa kukanyanga haki za zamiri.

Kwa namna imani ya kuwa roho za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu (spiritualisme) , inakuwa na uwezo mkubwa kwa kudanganya. Shetani yeye mwenyewe "hujigeuza". Ataonekana kama malaika wa nuru. Kwa njia ya imani ya kuwa roho za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu, miujiza itafanyika, wangonjwa wataponyeshwa, na maajabu mengi yasiyokukanishwa yatafanyika.

Wafuasi wa kanisa la kiroma wanaojisifu juu ya miujiza kuwa alama ya kanisa la kweli watadanganyika upesi kwa uwezo huu wa kufanya miujiza; na Waprotestanti, wanapokwisha kutupia mbali ngao ya ukweli, watadanganyika vile vile. Wafuasi wa kanisa la Roma, Waprotestanti, na watu wapendao anasa za dunia wataonekana vivyo hivyo katika umoja huu mabadiliko makubwa kwa ajili ya toba ya ulimwengu.

Kwa njia ya imani ya kuwa roho za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu (spiritualisme), Shetani hutokea kama mtenda mema wa kabila, kuponyesha magonjwa na kuonyesha kawaida mpya ya imani ya dini, lakini wakati ule ule anaongoza wengi kwa maangamizi. Kukosa kiasi kunaondoa akili; mapendeleo ya anasa, vita, na kumwanga damu hufuata. Vita huamsha tamaa mbaya sana ya nafsi na kufutia kwa milele mateka wake walioloanishwa katika uovu na damu. Nikusudi la Shetani kuchochea

mataifa kwa vita, kwani anaweza kupotosha watu kwa matayarisho ya kusimama kwa siku ile ya Mungu.

Shetani amejifunza siri za maumbile, na anatumia uwezo wake wote kutawala mwanzo kadiri Mungu anavyoruhusu. Ni Mungu anayelinda viumbe vyake kutoka kwa mharibu. Lakini jamii ya Ukristo limeonyesha zarau kwa sheria yake, na Bwana atafanya kile alichotangaza ya kwamba-angeondoa ukingaji wa ulinzi wake kwa wale wanaoasi kwa sheria yake na kukaza wengine kufanya pamoja. Shetani anakuwa na utawala wa wote ambao Mungu asio walinda kwa kipekee. Atasaidia na kusitawisha wengine, ili kuzidisha makusudi yake wenyewe; na ataleta taabu kwa wengine, na kuongoza watu kuamini ya kama ni Mungu ndiye anayewatesa.

Anapotokea kama tabibu mkuu anayeweza kuponya magonjwa yao yote, Shetani ataleta ugonjwa na msiba hata miji ya watu waingie kwa maangamizi. Katika misiba baharini na inchini, katika mateketeo makubwa, katika tufani kali na mvua ya mawe, katika [288]
zoruba, garika, kimbunga, mawimbi ya maji kujaa, na tetemeko la inchi, katika namna maelfu, Shetani anatumia uwezo wake. Anaondolea mbali mavuno yenye kukomea yote, na njaa na taabu hufuata. Hugawanya mawaa ya mauti angani, na maelfu huangamia.

Ndipo mdanganyifu mkubwa atashawishi watu kutwika taabu zao zote kwa wale wanaokuwa na utii kwa amri za Mungu ni laumu la daima kwa wakosaji. Itatangazwa ya kama watu wanamkosea Mungu juu ya mvunjo wa siku ya kwanza, ya kwamba zambi hii imeleta misiba ambayo haitakoma hata kushika kwa siku ya kwanza kutakapo kazwa kabisa. “Wale wanaoharibu heshima kwa ajili ya siku ya kwanza wanazuia kurudishwa kwa majaliwa ya Mungu na kufanyikiwa”. Kwa hivyo mashitaki yaliyofanywa ya zamani juu ya watumushi wa Mungu yatakaririwa. “Wakati Ahaba alipomuona Eliya, Ahaba akamwaambia: Ni wewe mwenye kutaabisha Israeli”? 1 Wafalme 18:17,18. Uwezo wa kufanya miujiza utatumia mvuto wake juu ya wale wanaomtii Mungu kuliko watu. “Pepo” watatangaza ya kama Mungu amewatuma kusadikisha wanaokataa siku ya kwanza kwa kosa lao. Watalilia uovu mkubwa ulimwenguni na kusaidia ushuhuda wa waalimu wa dini ya kama hali iliopoteza cheo cha mafundisho imaletwa na ukufuru wa siku ya kwanza

Chini ya utawala wa Roma, wale walioteseka kwa ajili ya habari njema walishitakiwa kama watenda maovu katika mapatano pamoja

na Shetani. Ndivyo hivyo itakavyokuwa sasa. Shetani ataletea wale wanaoheshimu sheria ya Mungu kushitakiwa kuwa watu wanaoleta hukumu duniani. Kwa njia ya kutisha anajaribu kutawala zamiri, anasukuma watawala wa dini na wa dunia kukaza sheria za kibinadamu katika kuasi sheria ya Mungu.

Wale wanaoheshimu Sabato ya Biblia watashitakiwa kuwa adui wa sheria na ukimya, kuvunja amri za maana za kijamii, kuleta machafuko ya mambo ya utawala na makosa, na kuita hukumu za Mungu inchini. Watashitakiwa juu ya chuki kwa serekali. Wajumbe wanaokana kanuni ya sheria ya Mungu wataonyesha kwa mimbara shuguli ya utii kwa utawala wa dunia. Katika vyumba vikubwa vya kufanya sheria na baraza za hukumu, wanaoshika amri watahukumiwa. Rangi ya uwongo itatolewa kwa maneno yao; maana mbaya kuliko itawekwa kwa mashitaki yao.

Wakuu wa kanisa na serekali watajiiunga kwa kushawishi ao kushurutisha wote kuheshimu siku ya kwanza. Hata katika watawala wa Kiamerika wenye uhuru na wenye kufanya sheria watakubali matakwa ya watu wote kwa ajili ya sheria ya kukaza kushika siku
[289] ya kwanza. Uhuru wa zamiri ambao umegaramishwa kwa kafara kubwa hauta heshimiwa tena. Katika kuja kwa karibu kwa shindano tutaona kuonyesha kwa mfano maneno ya nabii, "Joka akakasirikia yule mwanamke, akakwenda zake kufanya vita juu ya wazao wake waliobaki, wanaoshika amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo". Ufunuo 12:17.

# 37 /MAANDIKO MLINDA SALAMA YETU PEKEE

[290]

Watu wa Mungu wanaongozwa kwa maandiko kama mlinda usalama wao kwa kupinga mvuto wa wa waalimu wa uongo na roho za giza. Shetani hutumia kila shauri lo lote iwezekanavyo kuzuia watu kupokea maarifa ya Biblia, kwa usemi ao maneno yake ya waziinafunua madanganyifu yake. Madanganyo makubwa ya mwisho ni karibu kufunguliwa mbele yetu. Mpinga Kristo atafanya kazi yake ya ajabu mbele ya macho yetu kwa ukaribu kutakuwa mfano wa kufanana na iliyo ya kweli ambayo itakuwa haiwezekani kutofautisha kati yao isipokuwa kwa Maandiko. Wale wanaojitahidi kutii amri zote za Mungu watapingwa na kuzarauliwa. Kwa kuvumilia jaribu, wanapaswa kufahamu mapenzi ya Mungu kama inavyofuniliwa katika Neno lake. Hapana mtu bali wale ambao wamaimarisha akili kwa kweli za Biblia watakaosimama katika vita kubwa ya mwisho.

Mbele ya kusulibiwa kwake mwokozi alielezea wanafunzi wake ya kama alipashwa kuuawa na kufufuka tena. Lakini maneno yaliondolewa mbali kutoka kwa mawazo ya wanafunzi. Wakati jaribu lilipofika, kifo cha Yesu kikaharibu kabisa matumaini yao kama kwamba hakuwaonya mbele. Kwa hivyo katika mambo ya unabii na wakati ujao umefunuliwa wazi mbele yetu kwa kama ulivyofunuliwa kwa wanafunzi na Kristo mwenyewe. Tukio zinazo ambatana na wakati wa kufungwa wakati wa majaribu na kazi ya matayarisho kwa wakati wa taabu yanaonyeshwa wazi. Lakini wengi hawanaufahamu wa kweli hizi za maana sana, na wakati wa taabu utafika utawakuta wasiokuwa tayari.

Wakati Mungu anapotuma maonyo, anaagiza kila mtu kujaliwa na sababu kwa kukubali ujumbe. Hukumu za kutisha juu ya kuabudu mnyama na sanamu yake(Ufunuo 14:9-11) inapashwa kuongoza wote kujifunza namna alama ya mnyama inavyokuwa na namna gani ya kuepuka kuipokea. Lakini jamii ya watu hawataki ukweli wa Biblia, kwa sababu unazuia tamaa za moyo wa zambi. Shetani anatoa mambo ya udanganyifu wanaopenda.

Lakini Mungu atakuwa na watu watakaodumisha Biblia, na ni Biblia peke yake, kama kawaida ya mafundisho yote na msingi wa matengenezo yote. Nia za watu waliojifunza, matoleo ya elimu ya kweli, makusudi ya baraza za kanisa, sauti ya watu wengi-hakuna mojawapo ya haya yanapashwa kuzaniwa kama ushahidi
[291] kwa kukubaliana ao kutokubali mafundisho yo yote. Inatupasa kudai zahiri "Bwana anasema hivi". Shetani anaongoza watu kutazama kwa wachungaji, kwa waalimu wa elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini kama viongozi vyao, badala ya kuchunguza Maandiko wao wenyewe. Kwa kutawala waongozi hawa, anaweza kuvuta wengi.

Wakati Kristo alipokuja, watu wa kawaida walimsikia kwa furaha. Lakini mkuu wa ukuhani na watu wenye kuongoza wakajiingiza wao wenyewe katika uzalimu; wakakataa ushuhuda wa Umasiya wake. "Namna gani inakuwa", watu wakauliza, "ya kama watawala wetu na wandishi waliojifunza hawaamini Yesu? Waalimu kama wale walioongoza taifa la Wayuda kukataa Mkombozi wao.

## Kutukuza Mamlaka Ya Kibinadamu

Kristo alikuwa na maoni ya unabii kwa kazi ya kutukuza mamlaka ya kibinadamu kutawala zamiri, ambalo lilikuwa jambo la laana la kitisha katika vizazi vyote. Maonyo yake si kufuata viongozi vipofu waliowekwa kwa ukumbusho kama onyo la upole kwa vizazi wakati vijavyo.

Kanisa la Roma linawekwa akiba ya haki ya kutafsiri Maandiko kwa mapadri. Ingawa matangenezo ilitoa Maandiko kwa wote, lakini kanuni ya namna moja iliyoshikwa kwa Roma inazuia wengi katika makanisa ya Kiprotestanti kutochunguza Biblia wao wenyewe. Wanafundishwa kukubali mafundusho yake kama ilivyofasiriwa na kanisa. Maelfu wanasubutu kutopata kitu, lakini ni wazi katika maandiko, ile inayokuwa kinyume kwa imani yao.

Wengi wanakuwa tayari kutoa nafsi zao kwa mapadri. Wanapita mbali ya mafundusho ya Mwokozi karibu bila kuonywa. Lakini je, wanakuwa wahudumu wasioweza kukosa? Namna gani tunaweza kutumaini uongozi wao isipokuwa tunajua kutoka kwa Neno la Mungu ya kama wanakuwa wachukuaji wa nuru? Ukosefu wa uhodari wa mafundisho unasukuma wengi kufuata watu waliojifunza, na wanakuwa wenye kufungwa bila kuwa na matumaini katika

kosa. Wanaona ukweli kwa wakati huu katika Biblia na wanasikia uwezo wa Roho Mtakatifu kufikia matangazo jake, huku wakiruhusu mapadri kuwarudisha kutoka kwa nuru. Shetani anafunga wengi kuwafunga na kamba za hariri za upendo kwa wale wanaokuwa adui za msalaba wa Kristo. Kifungo hiki kinaweza kuwa cha wazazi, cha jamii, cha ndoa ao ujamii wa jamaa nyingi kuwa pamoja. Nafsi chini ya mvuto wao hauna uhodari wa kutii nia zawajibu wao.

Wengi hudai ya kama si kitu cho chote mtu anachoamini, kama [292]
tu maisha yake yakiwa kamili. Lakini maisha yanafanywa na imani. Kama ukweli unakuwa ndani unafikia kipimo na tunauzarau, tunaukataa kwa kweli, kuchagua giza badala nuru.

Ujinga hauachiliwi kwa ajili ya kosa la zambi, kama pale kunakuwa na nafasi yo yote, kwa kujua mapenzi ya Mungu. Mtu mmoja anayesafiri anafika mahali ambapo panakuwa njia nyingi na mti wenye mkono wa kuonyesha njia mahali gani kila moja inaongoza. Kama akizarau alama na kukamata njia yo yote inayoonekana kuwa ya haki, angeweza kuwa yakini, lakini katika kubahatisha kule kote atapatikana mwenyewe kwa njia mbaya.

### Shuguli ya Kwanza na ya Juu Sana

Haitoshi kuwa na makusudi mema, kufanya kitu mtu anachofikiri kuwa cha haki ao kite muhuduma anachowaambia kuwa cha haki. Anapashwa kuchunguza maandiko kwa ajili yake mwenyewe. Anakuwa na amani inayoonyesha kila alama ya njia ya safari ya kwenda mbinguni, na hapashwe kuamini kitu cho chote.

Ni wajibu wa kwanza na ya juu sana kwa kila kiumbe chenye akili kujifunza kwa Maandiko mambo inayokuwa ya kweli, ndipo kutembea katika nuru na kutia wengine moyo kufuata mfano wake. Inatupasa kutengeneza nia zetu sisi wenyewe kwa namna tutakavyojibu sisi wenyewe mbele ya Mungu.

Watu waliojifunza, kwa ujanja wa hekima kubwa, wanafundisha ya kama Maandiko yanakuwa na siri, maana ya kiroho si ya kutambulikana katika lugha iliyotumiwa. Watu hawa ni waalimu wa uwongo. Lugha ya Biblia inapashwa kuelezwa kufuata maana yake zahiri, ila tu kama mfano ao picha inatumiwa. Kama watu wangekamata tu Biblia kama inavyosomwa, kazi ingetimizwa ambayo ingeleta maelfu katika zizi la Kristo maelfu juu ya maelfu wanaotan-

gatanga katika makosa. Sehemu nyingi za Maandiko ambazo wenye hekima wanazozania kutokuwa za maana zinajaa na faraja kwa yeye anayefundishwa katika shule la Kristo. Ufahamu wa ukweli wa Biblia hauko zaidi kwa uwezo akili ilioletwa kwa uchunguzi kama kwa umoja wa kusudi, tamaa ya juhudi baada ya haki.

### Matokeo ya Zarau ya Maombi na Kujifunza Biblia

Biblia haipashwi kujifunzwa pasipo maombi. Roho Mtakatifu peke yake anayetuwezesha kuona umuhimu wa vitu rahisi kufahamiwa, ao kutuzuia kupotoa mambo magumu ya kweli. Malaika
[293] wa mbinguni wanatayarisha moyo kufahamu Neno la Mungu. Tupendezwa kwa uzuri wake, kugombezwa kwa maonyo yake na kutiwa nguvu na ahadi zake. Mara kwa mara majaribu huonekana kuwa na nguvu nyingi sana kwa sababu yule aliyejaribiwa hawezi mara hiyo kukumbuka ahadi za Mungu na kukutana na Shetani anayekuwa na silaha za Maandiko. Lakini malaika wanazunguka wale wanaotaka kufundishwa, na wataleta kwa ukumbusho wao ukweli unayohitajiwa.

"Yeye atawafundisha ninyi vitu vyote, na kuwakumbusha ninyi vitu vyote niliyowaambia ninyi". Yoane 14:26. Lakini mafundusho ya Kristo yanapashwa kwanza kuwekwa katika akili ili Roho ya Mungu ayalete katika ukumbusho wetu katika wakati wa hatari.

Ajali ya makutano mengi sana inakuwa karibu kukusudiwa. Kila mshiriki wa Kristo inampasa kudai kwa bidii: "Bwana unataka nifanye nini"? Matendo 9:6. Inatupasa sasa kutafuta maarifa ya ndani na ya nguvu katika vitu vya Mungu. Hatuna na wakati kwa kupoteza. Tunakuwa kwa udongo wa kupendeza wa Shetani. Zamu wa Mungu usilale!

Wengi hushangilia wao wenyewe kwa matendo mabaya ambayo wasiyoyafanya. Haitoshi ya kama wao ni miti katika bustani ya Mungu. Inawapasa kuzaa matunda. Katika vitabu vya mbinguni wanaandikwa kama walimaji wa udongo. Kwani kwa wale waliozarau rehema ya Mungu na wakatumia vibaya neema yake, moyo na upendo wa uvumilivu ungali ukitetea.

Wakati wa mvua hakuna tofauti ya kuonekana kati ya miti na miti ingine; lakini wakati wa kipwa na upepo na majira ya baridi inapofika, miti isiyokauka inadumu imara wakati miti ingine inapo

ponoa majani yao. Acha upinzani uamke, acha kutovumilia kutikisika tena, acha mateso iwashwe, na mapenzi yasiyo na bidii na ya unafiki ikubali imani; lakini Mkristo wa kweli atasimama imara, imani yake kuzidi kuwa hodari; tumaini lake kuzidi kungaa, kuliko siku za mafani-kio.

"Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, unaofikisha mizizi yake karibu ya mto; hautaona woga wakati wa jua kali linapokuja, lakini majani yake yatakuwa mabichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda", Yeremia 17:8.

[294] # 38 /UJUMBE WA MUNGU ULIO WA MWISHO

"Nyuma ya maneno haya nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kubwa; na dunia ikangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kubwa, akisema: Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkubwa, umekuwa makao ya mashetani, na boma la kila pepo mchafu na boma la kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;

Na nikasikia sauti nyingine toka mbinguni ikisema: Tokeni kwake, watu wangu, musishirikiane na zambi yake, wala musipokee mapigo yake". Ufunuo 18:1,2,4.

Matangazo yaliyofanywa na malaika wa pili ya Ufunuo 14 (fungu 8) ni ya kukaririwa, pamoja na mtajo mwingine wa machafuko yaliokuwa yakiingia katika Babeli tangu ujumbe ulipotolewa mara ya kwanza.

Hali ya kitisha inaelezwa hapa. Kwa kila kukataa kwa ukweli akili za watu zitakuwa giza sana, mioyo yao mikaidi zaidi. Wataendelea kukanyanga mojawapo ya maagizo ya amri kumi hata wanapotesa wale wanaoishika kuwa takatifu. Kristo anawekwa kwa sifuri juu ya zarau lililowekwa kwa Neno lake na kwa watu wake.

Ungamo la dini litakuwa ni tendo la kudanganya kwa kuficha uovu wa msingi kabisa. Uaminifu katika imani ya kuwa roho za watu waliokufa hurudi na kujionyesha na kuongea na watu (spiritualisme) inafungua mlango kwa mafundisho ya mashetani, na kwa hivyo mvuto wa malaika wabaya utaonekana katika makanisa. Babeli umejaza kipimo cha zambi zake, na maangamizo ni karibu kuanguka.

Lakini Mungu akingali na watu katika Babeli, na waaminifu hawa wanapashwa kuitwa kutoka ili wasishirikiane na zambi zake na "wasipokee mapingo yake". Malaika anashuka toka mbinguni kuangazia dunia kwa utukufu wake na kutangaza zambi za Babeli. Mwito umesikilika: "Tokeni kwake, watu wangu". Matangazo haya yanakuwa onyo ya mwisho kutolewa kwa wakaaji wa dunia.

Nguvu za dunia, kuungana kwa vita kupinga amri za Mungu, zitaamuru ya kama "wote, wadogo na wakubwa, na matajiri na masikini na wahuru na wafungwa" (Ufunuo 13:16) watakubali desturi za kanisa kwa kushika sabato ya uwongo. Wote wanaokataa mwishoni watatangazwa wenye kustahili mauti. Kwa upande mwingine, sheria ya Mungu inaagiza siku ya pumziko ya Mungu inaonya hasira juu ya wote wanaovunja amri zake.

Kwa matokeo, ndivyo ilivyoletwa wazi mbele yake, ye yote atakayekanyanga juu ya sheria ya Mungu na kutii sheria ya kibi- [295]
nadamu anapokea alama ya mnyama, ishara ya uaminifu kwa uwezo anaouchagua kutii badala ya Mungu. "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, yeye naye atakunywa katika mvinyo wa gazabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake". Ufunuo 14:9,10.

Hakuna mmoja anayeteseka na hasira ya Mungu mpaka kweli inapokwisha kuletwa nyumbani kwa moyo wake na zamiri na inapokataliwa. Wengi hawakupata kamwe bahati ya kusikia mambo ya ukweli wa kipekee kwa wakati huu. Yeye anayesoma kila moyo hataacha mmoja anayetamani kweli kudanganywa kama matokeo ya mashindano. Kila mmoja anapashwa kuwa na nuru ya kutosha kufanya mpango wake kwa akili.

## Jaribu Kubwa la Uaminifu

Sabato, jaribu kubwa la uaminifu, ni ukweli hasa unaopingwa. Huku kushika sabato ya uwongo kutakuwa neno la kukiri la utii kwa mamlaka yanayo mpinga Mungu, kushika kwa Sabato ya kweli ni ushahidi wa uaminifu kwa Muumba. Wakati kundi moja linapopokea alama ya nyama, lingine hupokea muhuri wa Mungu.

Maonyo ya kwamba kukosa uvumulivu wa dini kungepata utawala, ya kama kanisa na serkali wangetesa wale wanaoshika amri za Mungu, yangetangazwa pasipo sababu na kwa upuzi. Lakini kwa namna kushika kwa siku ya kwanza (dimanche) kunatikiswa mahali pengi sana, jambo lililokuwa halikusadikiwa kwa wakati mrefu linaonekana kuwa karibu, na ujumbe utaleta tukio ambalo lisingaliweza kuwako mbele.

Katika kila kizazi Mungu ametuma watumishi wake kukemea zambi ulimwenguni na katika kanisa. Watengenezaji (réformateurs)

wengi, kwa kuingia kwa kazi yao, wakakusudia kutumia busara nyingi katika kushambulia zambi za kanisa na za taifa. Wakatumainia, kwa mfano wa maisha safi ya Kikristo, kuongoza watu kurudi kwa Biblia. Lakini Roho wa Mungu akaja juu yao; pasipo hofu ya matokeo, hawakuweza kuzuia kuhubiri mafundisho zahiri ya Biblia.

Kwa hivyo ujumbe utatangazwa. Bwana atatumika kwa njia ya vyombo vinyenyekevu vinavyojitia wakuf wenyewe kwa kazi yake. Watumukaji watastahilishwa zaidi kwa kupakwa mafuta ya roho Mtakatifu kuliko kwa mafundisho ya vyama vya vitabu. Watu watalazimishwa kuendelea mbele na juhudi takatifu , kutangaza maneno ambayo Mungu anayotoa. Zambi za Babeli zitafunuliwa.
[296] Watu watashitushwa. Maelfu hawajasikia kamwe maneno kama haya. Babeli ni kanisa, lililoanguka kwa sababu ya zambi zake, kwa sababu ya kukataa kwake kwa ukweli. Jinsi vile watu wanavyo kwenda kwa walimu wao na maswali "je, mambo haya ni hivyo"? Wahubiri wanaonyesha mifano kwa kutuliza zamiri iliyoamshwa. Lakini kwa namna wengi wanapouliza zahiri "Bwana anasema hivi", kazi ya mapadri ya watu wengi itaamsha makutano yanayopenda zambi kwa kutukana na kutesa wale wanao tangaza.

Mapadri watatumia juhudi zaidi za kupita uwezo wa kibinadamu kwa kufungia mbali nuru, kwa kuzuia mabishano ya maswali haya ya maana sana. Kanisa linaomba kwa mkono hodari wa mamlaka ya serikali, na katika kazi hii, wafuasi wa kanisa la kiroma na waprotestanti huungana. Kwa namna mwenendo wa mkazo wa siku ya kwanza (dimanche) unapokuwa wa nguvu zaidi, washikaji wa amri watatishwa kwa kulipa feza na kifungo. Wengine wanatolewa vyeo vya mvuto na wengine zawadi zingine kwa kukana imani yao. Lakini jibu lao ni "Mtuonyeshe kutoka katika Neno la Mungu kosa letu". Wale walioshitakiwa mbele ya baraza wanafanya ushuhuda wa nguvu wa ukweli, na wengine wanaowasikia huongozwa kwa kukata shauri la kushika amri zote za Mungu. Kama sivyo maelfu hawangeweza kujua kitu juu ya mambo haya ya kweli.

Utii kwa Mungu ungetendewa kama uasi. Mzazi atatumia ukali kwa mtoto mwenye kuamini. Watoto wataondolewa katika urithi na kufukuzwa kutoka nyumbani. "Na wote wanaotaka kuishi maisha ya utawa katika Kristo Yesu watapata mateso". 2 Timoteo 3:12. Kuwa kama wateteaji wa ukweli wanapokataa kuheshimu siku ya kwanza

(dimanche) wengine wataingizwa gerezani, wengine watahamishwa, wengine watatendewa kama watumwa. Kwa namna roho ya Mungu atakavyoondolewa kutoka kwa watu hapo kutakuwa maendeleo ya kigeni. Moyo unaweza kuwa na jeuri sana wakati uchaji wa Mungu na upendo yanapoondolewa.

### Machafuko Yanakaribia

Kwa namna machafuko yanavyokaribia, jamii kubwa ya walioungama imani katika ujumbe wa malaika wa tatu, lakini hawakutakasiwa kwa njia ya utii kwa ukweli, wataacha nia yao na kujiunga kwa upinzani. Kwa kujiunga pamoja na ulimwengu wamefikia kuona mambo karibu ya nuru ya namna moja, na wanachagua upande wa watu wengi. Watu ambao kwanza walifurahi katika ukweli wanatumia kipawa chao na hadizi za kupendeza kwa kuongoza vibaya roho. Wanakuwa adui wakali wa ndugu zao wa [297]
kwanza. Waasi hawa ni wajumbe wa nguvu wa shetani kwa kueleza vibaya na kushitaki wanaoshika Sabato na kuchochea watawala kwa kuwapinga.

Watumishi wa Bwana wametoa onyo. Roho ya Mungu imewalazimisha. Hawakushauriana na faida zao za mda, wala hawakutafuta kulinda sifa yao ao maisha yao. Kazi inaonekana kuwa mbali kabisa na uwezo wao kuitimiza. Kwani hawawezi kurudi nyuma. Kuona uzaifu wao, wanakimbilia kwa Mwenye Uwezo kwa kutaka nguvu.

Nyakati mbalimbali katika historia zimeonyeshwa na maendeleo ya ukweli wa kipekee, uliofanyizwa kwa mahitaji ya watu wa Mungu kwa wakati ule. Kila ukweli mpya umefanya namna yake juu ya upinzani. Mabalozi wa Kristo wanapashwa kufanya wajibu wao na kuacha matokeo kwa Mungu.

### Upinzani Umeongezeka kwa Kimo Kipya

Jinsi ushindani umeongezeka kwa nguvu nyingi; watumishi wa Mungu wanahangaika tena, kwani inaonekana kwao ya kama wameleta taabu. Lakini zamiri na Neno la Mungu vinawahakikishia ya kama mwenendo wao ni wa haki. Imani yao na uhodari umeongezeka pamoja na ujushi. Ushuhuda wao ni “Kristo ameshinda nguvu za dunia, je, tutaogopa ulimwengu uliokwisha kushindwa”?

Hakuna mtu anayeweza kutumikia Mungu pasipo kujiweka kwa kosa yeye mwenyewe kinyume cha ushindani wa majeshi ya giza. Malaika waovu watamshambulia, kukilisha hatari ya kuwa mvuto wake unapata mawindo kutoka mikononi mwao. Waovu watatafuta kumtenga kwa Mungu kwa njia ya majaribu ya kutamanisha. Wakati haya hayafaulu, uwezo hutumiwa kwa kushurutisha zamiri.

Lakini kwa namna Yesu anavyodumu kuwa Muombezi wa mtu katika pahali patakatufu juu, mvuto unaozuia wa Roho Mtakatifu huonekana kwa watawala na watu. Wakati watawala wetu wengi wanapokuwa wajumbe wa nguvu wa Shetani, Mungu vivyo hivyo anakuwa na wajumbe wake miongoni mwa watu wanaongoja katika taifa. Watu wachache watadumu kwa kuzuia maendeleo ya nguvu ya uovu. Ushindaji wa adui wa ukweli utazuiwa ili ujumbe wa malaika wa tatu uweze kufanya kazi yake. Onyo la mwisho litasimamisha uangalifu wa watu hawa waongozi, na wengine watalikubali nakusi-
[298] mama pamoja na watu wa Mungu kwa wakati wa taabu.

## Mvua Ya Mwisho Na Kilio Cha Nguvu

Malaika anayeungana na malaika wa tatu ni kwa kuangazia dunia yote na utukufu wake. Ujumbe wa malaika wa kwanza ulipelekwa kwa makao yote ya utumishi ulimwenguni, na katika inchi zingine kulikuwa na usikizi wa dini kubwa sasa ulioshuhudiwa tangu wakati wa matengenezo. Lakini hizi zinapashwa kupita kwa onyo la mwisho la malaika wa tatu.

Kazi itakuwa ya namna moja na ile ya Siku ya Pentecote. "Mvua ya kwanza" ilitolewa kwa kufungua wa habari njema kuwezesha kuotesha mbegu ya damani; vivyo hivyo "mvua ya mwisho" itatolewa kwa mwisho wake wa kuivya kwa mavuno. Hosea 6:3; Yoeli 2:23. Kazi kubwa ya habari njema si ya kufunga na onyesho ndogo zaidi la uwezo wa Mungu kuliko kutazama mwanzo wake. Unabii uliotimia katika kumiminiwa kwa mvua ya kwanza kwa kufungua kwa habari njema yanapashwa kutimia vile vile katika mvua ya mwisho wake. Hapo ndipo panakuwa "nyakati za ufufuko" ambazo mtume Petro alikuwa akitazamia mbele. Matendo 3:19, 20.

Watumishi wa Mungu, nyuso zao kungaa na utakaso mtakatifu, wataharikisha toka mahali mbali mbali kutangaza habari njema kutoka mbinguni. Miujiza itafanyika, wagonjwa wataponyeshwa.

Shetani vivyo hivyo anatumika na maajabu ya kudanganya, hata kushusha moto kutoka mbinguni. Ufunuo 13:13. Kwa hivyo wakaaji wa dunia watashawishiwa kuchagua upandeunao kuwa wao.

Ujumbe huu utachukuliwa si kwa mabishano sana ni kwa tendo lauhakikisho wa ndani wa Roho ya Mungu. Mabishano yame-onyeshwa, vitabu vilitumia mvuto wavyo, lakini wengi wamezuiwa kwa kufahamu kabisa ukweli. Sasa ukweli umeonekana wazi kabisa. Mahusiano ya ujamaa, mahusiano ya kanisa ni zaifu kudumu kuwa waana waaminifu wa Mungu sasa. Lakini wajumbe waliochanganyika kupinga ukweli, hesabu kubwa huchukua kituo chao kwa upande wa Bwana.

[299] # 39 /WAKATI WA TAABU

"Kwa wakati ule Mikaeli atasimama, Mfalme Mkubwa anayesimama kwa ajili ya wana wa watu wako; na kutakuwa wakati wa taabu, kama usivyokuwa mbele tangu wakati taifa lilipokuwa hata wakati ule: na kwa wakati ule watu wako wataponyeshwa, kila mtu atakayeonekana ameandikwa katika kitabu." Danieli 12:1.

Wakati ujumbe wa malaika wa tatu unamalizika, watu wa Mungu watakuwa wametimiza kazi yao. Wamepokea, "mvua ya mwisho" na wanajitayarisha kwa saa ya kujaribiwa inayokuwa mbele yao. Jaribu la mwisho limekwisha kuletwa duniani, na wote waliohakikishwa kuwa watiifu (waaminifu) kwa amri za Mungu wamepokea "muhuri wa Mungu aliye hai." Ndipo Yesu anapomaliza uombezi wake katika Pahali patakatifu kule juu na kusema kwa sauti kuu, "Imefanyika". "Yeye aliye muzalimu azidi kuwa muzalimu; na mwenye uchafu azidi kuwa mchafu; na mwenye haki azidi kufanya haki; na mtakaifu azidi kutakaswa": Ufunuo 22:11. Kristo amefanya upatanisho kwa ajili ya watu wake na amefutia mbali zambi zao. "Na ufalme na mamlaka, na ukubwa wa falme chini ya mbingu" (Danieli 7:27) ni karibu kutolewa kwa wariti wa wokovu, na Yesu kutawala kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Wakati anapoacha Pahali patakatifu, giza inafunika wakaaji wa dunia. Wenye haki wanapaswa kuishi machoni pa Mungu Mtakatifu pasipo mwombezi. Kizuio juu ya waovu kimeondolewa, na Shetani anakuwa na mamlaka kamili juu ya wasiotubu. Kwa mwisho Roho ya Mungu imeondolewa. Ndipo Shetani anatumbukiza wakaaji wa dunia katika taabu kubwa ya mwisho. Malaika wa Mungu wanaacha kushika kwa kuzuia pepo kali ya tamaa ya wanadamu. Ulimwengu wote utahusika katika maangamizo ya kuogopesha zaidi kuliko yale ambayo yalifika juu ya Yerusalema ya zamani. Hapo kunakuwa majeshi sasa tayari, zinangoja tu ruhusa ya Mungu, kueneza ukiwa po pote.

Wale wanaoheshimu sheria ya Mungu watazaniwa kuwa sababu ya mateso ya kuogopesha na umwangaji wa damu ambavyo vinajaza

dunia kwa taabu. Uwezo uliofatana na onyo la mwisho umekasirisha waovu, na Shetani atachochea roho ya uchuki na mateso juu ya wote waliopokea ujumbe.

Wakati kuwako kwa Mungu kuliondolewa kutoka kwa taifa la Wayuda, wakuhani na watu waliendeleya kujizania wenyewe kuwa wateule wa Mungu. Utumishi katika hekalu ilikuwa ikiendelea; siku kwa siku baraka ya Mungu ilikuwa ikitakiwa juu ya watu wenye kosa [300]
ya damu ya Mwana wa Mungu. Vivyo hivyo wakati hukumu isiyobadilika ya Pahali patakatifu inapokwisha kutangazwa na mwisho wa ulimwengu ulikuwa wenye kuwekwa milele, wakaaji wa dunia hawataitambua. Kawaida za dini zitakuwa zikiendeleshwa na watu wale ambao Roho ya Mungu imeondolewa; juhudi ya shetani kwa kutimiza nia zake mbaya atachukua mfano wa juhudi ya Mungu

Kwa namna Sabato inavyokuwa jambo la upekee la ushindani po pote katika jamii ya Wakristo wote, italazimishwa ya kwamba wachache wanaosimama katika upinzani kwa kanisa na serekali hawapashwi kuvumiliwa, ya kwamba ni bora kwao kuteswa kuliko mataifa yote kutupwa katika fujo. "Inafaa kwetu kayafa akasema mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, na kwa hiyo taifa lote lisiangamie", Yoane 11:50. Neno hili litaonekana la kutibitisha; amri mwishoni itatolewa juu ya wale wanaotukuza Sabato ya amri ya ine, kuwashitaki na kutoa uhuru kwa watu baada ya wakati fulani kuwaua. Kanisa la Roma kwa wakati wa ulimwengu wa mkufuru wa Kiprotestanti katika ulimwengu wa sasa atafuata njia ileilne. Watu wa zamani na Mungu watatumbukuzwa katika musukosuko hiyo ya taabu inaonyesha kama wakati wa taabu yake yakobo. Yeremia 30:5-7. Usiku wa Yakobo wa uchungu, wakati alipo shindana katika maombi kwa kuokolewa kutoka kwa Esau (Mwanzo 32:24-31) inaonyesha tendo la watu wa Munguwakati wa taabu. Sababu ya udanganyifu uliotumiwa kwa kupatabaraka kutoka kwa baba yakeambayo ilikuwaya Esau, Yakobo alikimbia, alipojulishwajuu ya vitisho vya kifo vilivyofanywa na ndugu yake. Baada ya kukaa miaka nyingi mbali na kwao, akachagua kurudi inchini yake ya asili. Alipofikamipakani akajazwa na hofu kwa habari ya kumkaribia Esau, akahakikisha kuwa nduguye atalipisha kisasi. Tumaini pekee la Yakobo lilikuwa ni rehema za Mungu; ulinzi wake wa kipekee ulipashwa kuwa ni maombi.

### Wakati wa Taabu ya Yakobo

Peke yake pamoja na Mungu, akaungama zambi zake kwa unyenyekevu sana. Taabu katika maisha yake ilifika. Katika giza akaendelea kuomba. Gafula mkono ukawekwa juu ya bega lake. Akafikiri kwamba adui ndiye alikuwa akitafuta maisha yake. Kwa nguvu zote za kukata tamaa akapigana kwa nguvu na adui wake. Wakati siku ilipoanza kucha, mgeni akatumia nguvu zisizokuwa za kibinadamu. Yakobo akaonekana kukauka na akaanguka, muombaji zaifu, mwenye kulia kwa shingo la mshindani wake wa siri.
[301] Akajua nyuma ya kwamba alikuwa malaika wa agano aliyekuwa akigombana naye. Alidumu katika majuto wakati mrefu kwa ajili ya zambi yake; sasa anapashwa kuwa na matumaini ya kwamba alisamehewa. Malaika akasihi sana, "Uniache niende, ni mapambazuko", lakini mzee mkuu akapandisha sauti, "Sitakuacha kwenda mpaka utakaponibariki". Yakobo akaungama uzaifu wake na kutostahili kwake, huku akatumainia rehema za Mungu mwenye kulinda maagano. Kwa njia ya toba na kujitoa, kiumbe hiki cha mauti na mwenye zambi akashindana na Mtukufu wa mbinguni.

Shetani akamshitaki Yakobo mbele ya Mungu kwa sababu ya zambi yake; akashawishi Esau kusafiri na kinyume chake. Wakati wa usiku wa mzee mkuu wa kushindana, Shetani akajaribu kumkatisha tamaa na kuvunja tumaini lake kwa Mungu. Alivutwa karibu kukata tamaa; lakini akatubu kwa kweli juu ya zambi yake na kushikilia Malaika imara nakaendelea na maoni yake pamoja na vilio vya juhudi hata akashinda.

Kwa namna Shetani alivyomshitaki Yakobo, ataendelea na masitaka yake juu ya watu wa Mungu. Anakuwa na taarifa sahihi ya zambi alizokuwa wakiwajaribu nazo kutenda na anatangaza ya kwamba kwa haki hawezi kuwasamehe zambi zao kwani kumwangamiza na malaika zake. Anadai ya kwamba watolewe mikononi mwake kuangamizwa.

Bwana anamruhusu kuwajaribu iwezekanavyo. Tumaini lao kwa Mungu, imani yao, itajaribiwa kwa ukali. Wanapo jikumbusha yalipopita, imani yao inazama, kwani kwa maisha yao yote wanaweza uzuri ndogo. Shetani anajaribu kuwatisha kwa mafikara kuwa kezi zao hakuna matumaini. Anatumaini pia kuharibu imani

yao ili wajitoe kwa majaribu na kugeuza utii wao kutoka kwa Mungu.

## Maumivu Makuu ambao Mungu Atalaumiwa

Kwani maumivu ambayo watu wa Mungu wanateseka nayo si hofu ya mateso. Wanaogopa ya kwamba katika kosa fulani ndani yao wenyewe watashindwa kupata utimilifu wa ahadi ya Mwokozi: "Mimi nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kufikia dunia yote". Ufunuo 3:10. Je, wangeonekana kuthibitishwa kuwa wasiostahili kwa sababu ya makosa yao wenyewe ya tabia, ndipo jina takatifu la Mungu lingelaumiwa.

Wanaonyesha kwa toba yao ya wakati uliopita wa zambi zao nyingi na kuomba ahadi ya mwokozi: "Ao ashike nguvu zangu, afanye salama nami; Ndiyo afanye salama nami". Ysaya 27:5. Ijapo kuteseka kwa mashaka na msiba, hawaachi maombezi yao. [302] Wanaweka mshiko wa Mungu kama Yakobo alivyoweka mshiko wa Malaika; na msemo wa roho zao ni "Sitakuacha kwenda, kama haunibariki."

## Zambi Zilifutiliwa Mbali

Katika wakati wa taabu, kama watu wa Mungu walikuwa na zambi zisizoungamwa kuonekana mbele yao wanapoteseka na hofu na maumivu makali, wangezamishwa. Kukata tamaa kungaliondoa imani yao, na hawangeweza kumuomba Mungu kwa ajili ya wokovu. Lakini hawakuficha maovu kwa kuyafunua. Zambi zao zimetangulia kwa hukumu na zimefutiliwa mbali, na hawataweza kuzikumbuka.

Bwana anaonyesha katika matendo yake pamoja na yale ya Yakobo ya kwamba kwa ginsi yo yote hawezi kuvumilia uovu. Wote wanaoachilia ao kuficha zambi zao na kuziruhusu kudumu katika vitabu vya mbinguni bila kuziungama na bila kusamehewa watashindwa na Shetani. Zaidi wanapoheshimu nia wanapoishikilia, ni uhakikisho wa ushindi adui waoa. Wale wanaochelewesha matayarisho hawataweza kuyapata wakati wa hatari, wala wakati wo wote unaofuata. Kesi za wote kama wale ni bila tumaini.

Historia ya Yakobo pia ni matumaini ya kwamba Mungu hatatupa wale ambao, waliodanganywa katika zambi, na wamerudi

kwake na toba ya kweli. Mungu atatuma malaika kuwafariji wale wanaokuwa katika hatari. Jicho la Bwana ni juu ya watu wake. Ndimi za moto ya tanuru inaonekana karibu kuwateketeza, lakini Mtakasaji atawaleta kama zahabu iliyojaribiwa ao kutakaswa katika moto.

### Imani lnayovumilia

Wakati wa taabu na maumivu makuu yanayokuwa mbele yetu yatadai imani ile inayoweza kuvumilia ulegevu, kukawia, na njaa, imani ambayo haitalegea katika majaribu makali. Ushindi wa Yakobo ni ushuhuda wa nguvu ya maombi ya kushurutisha. Wote watakaoshikilia ahadi za Mungu, kama alivyofanya, watafaulu kama alivyofaulu. Kushindana na Mungu--namna gani wachache wanaojua umuhimu wake! Wakati mawimbi ya kukata tamaa yanapopita kwa nguvu juu ya mwombaji, namna gani wachache wanashikamana katika imani na ahadi za Mungu.

Wale wanaotumia imani ndogo tu sasa wanakuwa katika hatari
[303] kubwa ya kuanguka chini ya mamlaka ya madanganyo ya Shetani. Na hata kama wanavumilia jaribu watatumbukia katika wasiwasi kubwa wakati wa taabu kwa sababu hawakuifanya kamwe kuwa zoezi la kumtumaini Mungu. Inatupasa sasa kutibitisha ahadi zake.

Kila mara taabu ni kubwa linapofikiriwa aotendwa la mbele kuliko wakati ule kwa hakika linapashwa kutendeka ao kuonekana, lakini hii si kweli juu ya wakati wa taabu unaokuwa mbele yetu. Maelezo mengi ya wazi hayawezi kuikia ukubwa wa majaribu. Kwa wakati ule wa shida kila nafsi inapashwa kusimama yenyewe mbele ya Mungu.

Sasa, wakati kuhani wetu Mkubwa anapofanya upatanisho kwa ajili yetu, inatupasa kutafuta kuwa wakamilifu katika Kristo. Si kwa wazo ambalo mwokozi wetu aliweza kuwezeshwa kujitoa kwa uwezo wa majaribu. Shetani anapata ndani ya mioyo ya kibinadamu mahali padogo ambapo anaweza kupata tegemeo la kusimamisha mguu; tamaa fulani ya zambi inatunzwa pale, na kwa njia ambayo majaribu yake kusimamia uwezo wao. Lakini Kristo anajitangaza mwenyewe: "Mkubwa wa dunia hii anakuja; na yeye hana kitu ndani yangu." Yoane 14:30. Shetani hakuweza kupata kitu ndani ya Mwana wa Mungu ambacho kingeweza kumwezesha kupata ushindi.

Hapakuwa zambi ndani yake ambayo Shetani angeweza kutumia kwa faida yake. Hii ni kawaida ambayo inapashwa kujitenga kwao watakaosimama katika wakati wa taabu.

Ni katika maisha haya ambayo tunapashwa kujitenga na zambi, katika imani kwa damu ya Kristo ya upatanisho. Mwokozi wetu wa damani anatualika kujiunga kwake sisi wenyewe, kuunga uzaifu wetu kwa nguvu zake, kutostahili kwetu kwa matendo mema yake. Inabaki kwetu kushirikiana mbingu katika kazi ya kulinganisha tabia zetu kwa mfano wa Mungu.

Kazi ya Shetani ya kudanganya na uharibifu itafikia kipimo cha juu (mwisho) wakatiwa taabu. Maono ya kuogofya ya tabia isiyokuwa ya kibinadamu karibu yatafunuliwa katika mbingu, kwa alama ya uwezo wa kazi za miujiza ya mashetani. Pepo wabaya wataendelea kwa "falme za dunia" na kwa ulimwengu wote, kuwashurtisha kuungana na Shetani katika mapigano yake ya mwisho juu ya serkali ya mbinguni. Watu watatokea kudai kuwa Kristo Mwenyewe. Watafanya maajabu ya kuponya na kujifanya kuwa na mambo ya ufunuo kutoka mbinguni kupinga Maandiko.

Kama tendo la kutukuzwa katika ukubwa hadithi iliotungwamakusudi ya kuingizwa kama mchezo mbele ya watu wa madanganyo, Shetani mwenyewe atajifanya kuwa Kristo. Kanisa lilitazamia wakati mrefu kuja kwa Mwokozi kama utimilizo wa ma- [304]
tumaini yake. Sasa mshawishi mkubwa atafanya kuonekana kwake ya kwamba Kristo amekuja. Shetani atajionyesha mwenyewe kama kiumbe chenye utukufu cha wangavu wa kushangaza, kufanana na sifa ya Mwana wa Mungu katika Ufunuo. Ufunuo 1:13-15.

Utukufu unaomzunguka unapita kila kitu ambacho macho ya kibinadamu (wanaokufa) hayajaona kamwe. Shangwe ya ushindi italia, "Kristo amekuja!" Watu watamsujudia . Atanyosha mikono yake juu na kuwabariki. Sauti yake itakuwa ya kupendeza, lakini inapojaa na sauti tamu zinazofuatana. Kwa sauti ya huruma ataonyesha mambo mengine ya kweli ya ''mbinguni yaliotamkwa na Mwokozi. Ataponyesha magonjwa, na baadaye, katika tabia yake ya kujitia kwa mamlaka ya Kristo, anajidai kuweza kubadili Sabato na kuiweka kwa siku ya kwanza (dimanche). Anatangaza ya kwamba wale wanaoshika siku ya saba kuwa takatifu wanatukana jina lake. Hii ni madanganyo ya nguvu isiyoweza kuzuiwa na mtu. Watu wengi

wanatoa usikizi kwa mambo haya ya uchawi, wakisema, Huu ni "uwezo mkubwa wa Mungu", Matendo 8:10.

## Watu wa Mungu Hawataongozwa Vibaya

Lakini watu wa Mungu hawataongozwa vibaya. Mafundisho ya kristo huyu wa uwongo hayaako kwa mapatano na Maandiko. Baraka yake itatamkwa juu ya waabuduo wa mnyama na sanamu yake, ni kundi kabisa ambalo Biblia inatangaza ya Kwamba gazabu ya Mungu pasipo kuchanganywa itamiminwa.

Tena zaidi, Shetani hakuruhusiwa kuiga namna ya majilio ya Kristo. Mwokozi ameonya watu wake juu ya madanganyo kwa jambo hili. "Kwa sababu Wakristo wa uwongo watasimama, na manabii za uwongo, nao wataonyesha alama kubwa na maajabu wapate kudanganya kama ikiwezekana, hata wachaguliwa... Basi kama wakiwaambia ninyi: Tazama yeye ni jangwani; musitoke; Tazama, yeye ni katika vyumba vya ndani nyumbani, musisadiki. Kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaangaza hata mangaribi; hivi kuja kwa Mwana wa watu kutakavyokuwa vile". Matayo 24:24-27. Utazame vilevile Matayo 25:31; Ufunuo 1:7; 1 Watesalonika 4:16,17. Kuja huku, hapo hakuna namna ya kuiga. Itashuhudiwa kwa ulimwengu wote mzima.

Ila wanafunzi wa juhudi tu wa Maandiko waliokubali upendo wa kweli watakaolindwa kwa madanganyo ya nguvu yanayofanya dunia kuwa mateka. Kwa ushuhuda wa Biblia hawa watavumbua
[305] mdanganyi huyu kwa umbo la uwongo wake. Je, watu wa Mungu sasa wanakuwa wenye imara sana kwa Neno lake ili wasingejitoa kwa ushuhuda wa mashauri yao? Je, katika shida ya namna hii, wangeshikamana kwa Biblia, na kwa Biblia pekee?

Wakati watawala wa Kikristo watakapotangaza agizo juu ya wenye kushika amri kuondolewa kwa ulinzi wa serkali na kuwaacha kwa wale wanaotaka maangamizi yao, watu wa Mungu watakimbia kutoka katika miji na vijiji na kushirikiana pamoja katika makundi, kukaa katika mahali pa ukiwa sana na pa upekee. Wengi watapata kimbilio katika ngome za milima, kama Wakristo wa mabonde ya Piedmont (Vaudois). (Tazama sura ya ine). Lakini wengi katika mataifa yote na makundi yote, wa juu na chini, watajiri na maskini, weusi na weupe, watatupwa katika utumwa usio na haki kabisa na

wa jeuri. Wapenzi wa Mungu watapitia kwa siku za taabu kufungiwa ndani ya gereza ya fito za chuma, kupewa hukumu ya kuuawa, labda kuachiwa kufa katika giza, gereza la kuchukiza mno.

Je, Bwana atasahau watu wake kwa saa hii ya majaribu? Je, alimsahau muaminifu Nuhu, Loti, Yusufu, Elia, Yeremia, ao Danieli? Ingawa adui wakiwasukuma kwa nguvu katika gereza, lakini kuta za gereza haziwezi kukata habari kati ya nafsi zao na Kristo. Malaika watakuja kwao katika vyumba vya kifungo vya kipekee. Gereza itakuwa kama jumba la mfalme, na kuta za giza zitaangaziwa kama vile Paulo na Sila walipokuwa wakiimba usiku wa manane katika gereza ya Wafilipi.

Hukumu za Mungu zitajia wale wanaotaka kuangamiza watu wake. Kwa Mungu, azabu ni "tendo la kigeni". Isaya 28:21; utazame vilevile Ezekieli 23:11. Bwana ni mwenye"rehema na mwenye neema, si mwepesi kwa hasira, mwema na kweli nyingi, ... akisamehe uovu na makosa na zambi". Lakini "hataachilia wenye zambi hata kidogo". Kutoka 34:6, 7; Nahamu 1:3. Taifa inalostahimili wakati mrefu, na linalojaza kipimo cha uovu wake, mwishoni litakunywa kikombe cha hasira pasipo kuchanganywa na rehema.

Wakati Kristo anapomaliza uombezi wake katika Pahali patakatifu, hasira (ghazabu) pasipo kuchanganywa itahofishwa juu ya wale wanaoabudu mnyama itamiminwa. Mapigo kwa Misri yalikuwa ya namna moja na hukumu zenye eneo kubwa zaidi zile ambazo zinapaswa kuanguka duniani mbele kabisa ya wokovu wa mwisho wa watu wa Mungu. Asema mfumbuzi: "Ikaanguka jipu mbaya, zito, juu ya watu wenye chapa ya mnyama, na wale walioabudu sanamu yake. "Bahari "ikakuwa damu kama damu ya mfu". Na "mito na chemchemi za maji; zikakuwa damu". Malaika anatangaza: "Wewe mwenye haki, Bwana, ... kwa sababu umehukumu hivi. Kwani wal- [306]
imwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu kunywa; nao wamestahili". Ufunuo 16:2-6. Kwa kuhukumu watu wa Mungu hukumu ya mauti, kwa kweli wamehesabiwa makosa ya damu yao kama ingemwagika na mikono yao. Kristo alitangaza kwa Wayahudi wa wakati wake kosa ya damu yote ya watu watakatifu iliyomwagika tangu siku za Abeli (Matayo 23:34-36). Kwani walikuwa na roho ya namna moja kama wauaji hawa wa manabii.

Kwa pigo linalofuata, uwezo unatolewa kwa jua "kuunguza watu kwa moto". Ufunua 16:8,9. Manabii wanaeleza wakati

huu wakutisha: "Mavuno ya shamba yameharibiwa... miti yote ya shamba imekauka kwa sababu furaha imekauka katika wana wa watu". "Wanyama wanamlio wa huzuni makundi ya mifungo yanafzaika, sababu nawana malisho.... Maji ya mito yamekauka, na moto umekula malisho ya jangwa". Joel 1:11,12, 18-20.

Mapigo haya si ya mahali pote, lakini yatakuwa mapigo ya kutisha zaidi isiyofahamika kamwe. Hukumu zote zilizotangulia kufungwa kwa rehema zilikuwa zikichanganyika na rehema. Damu ya Kristo imelinda mwenye zambi kwa kiasi kamili cha kosa lake; lakini kwa hukumu ya mwisho, hasira si ya kuchanganywa na rehema. Wengi watatamani ulinzi wa rehema ya Mungu ambayo walikuwa wakiizarau.

Wakati wanapoteseka na kusumbuliwa, wakati wanapoteseka na njaa, watu wa Mungu hawataachwa kuangamizwa. Malaika watawatolea mahitaji yao. "Atapewa chakula chake; maji yake hayatakosekana". "Mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha". Isaya 33:16; 41:17.

Lakini kwa maonyo ya kibinadamu itaonekana ya kwamba watu wa Mungu wangepashwa upesi kutia muhuri kwa ushuhuda wao kwa damu yao, kama walivyofanya wafia dini mbele yao. Ni wakati wa maumivu makuu ya kutisha. Waovu wameshangilia. "Imani yenu inakuwa wapi sasa? Sababu gani Mungu hawaokoi kwa mikono yetu kama munakuwa kweli watu wake"? Lakini wanaongojea wanakumbuka Kristo alipokufa juu ya msalaba wa Kalvari. Kama Yakobo, wote wanashindana na Mungu.

### Makundi ya Malaika Wanalinda

Malaika wanatua kwa wale waliolinda neno la uvumilivu la Kristo. Wameshuhudia shida yao na wamesikia maombi yao.
[307] Wanangojea neno la Mkuu wao kuwanyakua kwa hatari yao. Lakini wanapashwa kungojea wakati mrefu kidogo. Watu wa Mungu wanapashwa kunywa kikombe na kubatizwa kwa ubatizo. Matayo 20:20-23. Lakini kwa ajili ya wateule wakati wa taabu utafupishwa. Mwisho utakuja upesi kuliko watu wanavyotazamia.

Ingawa amri ya kawaida imeweka wakati washika amri wanapoweza kuuawa, adui zao kwa sababu zingine wataharakisha amri na kujaribu kuondoa maisha yao. Lakini hakuna mtu

anayeweza kupita walinzi waliotua kuzunguka kila nafsi aminifu. Wengine walishambuliwa wakati wa kukimbia kwao kutoka mijini, lakini panga zilizoinuliwa juu yao zikavunjika kama majani makavu. Wengine wakalindwa na malaika katika hali ya watu wa vita.

Katika vizazi vyote viumbe vya mbinguni wamekamata sehemu ya juhudi katika mambo ya watu. Wamekubali kukaribisha na wanadamu, kutenda kama viongozi kwa wasafiri wajinga, wakafungua milango ya gereza na kuweka huru watumishi wa Bwana. Wakaja kusukuma jiwe kwa kaburi la Mwokozi.

Malaika wanazuru mikutano ya waovu, kama walivyokwenda Sodomo, kuhakikisha kama wamepitisha mpaka wa uvumilivu wa Mungu. Bwana, kwa ajili ya wachache wanamtumikia kwa kweli, anazuia misiba na anazidisha utulivu wa makutano. Wenye zambi wanafahamu kidogo sana ya kwamba wandeni kwa maisha yao juu ya waaminifu wachache ambao wanafurashwa kwa kuwagandamiza.

Kila mara katika baraza za ulimwengu huu, malaika wamekuwa wanenaji. Masikio ya kibinadamu yamesikiliza kwa miito yao, midomo ya kibinadamu yamezihakia mashauri yao. Wajumbe hawa wa mbinguni wametibitisha vyema kuliko wao wenyewe kuweza kutetea kisa cha waliozulumiwa kuliko wateteaji wao wenye uwezo wa kusema vema. Wameshinda na kufunga waovu wale wangeleta mateso kwa watu wa Mungu.

Kwa tamaa ya bidii, watu wa Mungu wanangojea ishara za kuja kwa Mfalme wao. Wakati wale wanaoshindana wanapoendesha maombi yao mbele ya Mungu, mbingu zaangaza na mapambazuko ya siku ya milele. Kama sauti tamu za nyimbo za malaika maneno yanaanguka kwa sikio: "saidia anakuja. " Sauti ya Kristo inakuja kutoka kwa milango wazi: "Tazama, ninakuwa pamoja nanyi. Msiogope. Nimepigana vita kwa ajili yenu, na katika jina langu munakuwa zaidi kuliko washindaji."

Mwokozi mpenzi atatuma msaada wakati tunapouhitaji. Wakati wa taabu ni hatari ya kutisha kwa watu wa Mungu, lakini kila mwamini wa kweli anaweza kuona kwa imani upindi wa ahadi ukimzunguka. "Hivi watu waliokombolewa na Bwana watarudi, [308]
watafika Sayuni na kuimba; Furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; watapata shangwe na furaha; huzuni na kulia kutakimbia". Isaya 51:11.

Kama damu ya washuhuda wa Kristo ilimwangika kwa wakati huu, uaminifu wao haungekuwa ushuhuda kusadikisha wengine kwa ajili ya kweli, kwa maana moyo mgumu umefukuza nyuma mawimbi ya rehema hata yasirudi tena. Kama wenye haki wanapashwa sasa kuanguka kuwa mawindo kwa adui zao, ingekuwa ushindi kwa mtawala wa giza. Kristo amesema: "Muje, watu wangu, mwingie ndani ya vyumba vyenu, na kufunga milango yenu nyuma yenu; mujifiche kwa dakika kidogo, hata wakati kasirani hii inapopita. Kwa maana tazama, Bwana anakuja kutoka pahali pake kuazibu wenye kukaa duniani kwa ajili ya uovu wao". Isaya 26:20,21.

Wokovu utakuwa wa utukufu wa wale waliongojea kwa uvumilivu kwa ajili ya kuja kwake na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima.

## 40 /WATU WA MUNGU WANAKOMBOLEWA [309]

Wakati ulinzi wa sheria za kibinadamu zitakapoondolewa kutoka kwa wale wanaoheshimu sheria ya Mungu, katika inchi mbalimbali kutakuwa mwendo wa namna moja kwa ajili ya maangamizi yao. Kwa namna wakati ulioamriwa katika agizo unapokaribia, watu watafanya shauri pamoja usiku mmoja shauri la kuangamiza kwa pigo litakalonyamazisha washupavu na wasiotii.

Watu wa Mungu wengine wapo katika vyumba vya gereza, wengine mwituni na katika milima--wanaomba ulinzi wa Mungu. Watu wenye silaha, wakilazimishwa na malaika waovu, wanajitayarisha kwa kazi ya mauti. Sasa, kwa saa ya mwisho kabisa, Mungu atajitia kati kati: "Mutakuwa na wimbo kama vile wakati wa usiku, wakati karamu takatifu inapotakaswa; na furaha ya moyo kama vile mtu anavyokwenda... katika mlima wa Bwana, aliye Mwamba wa Israeli. Na Bwana atafanya sauti yake ya utukufu kusikiwa, naye ataonyesha kushuka kwa mkono wake, wa nuru, kwa gazabu ya kasirani yake, na ulimi wa moto unaokula, pamoja na zoruba na garika na mvua ya mawe": Isaya 30:29,30.

Makutano makubwa ya watu waovu yanakuwa karibu kushambulia juu ya mawindo yake, wakati giza kubwa, nzito kuliko usiku, inaanguka duniani. Ndipo upindi wa mvua unazunguka mbingu kuonekana kuzunguka kila kundi la maombi. Makutano yenye kasirani yamefungwa. Makusudi ya hasira yao yamesahauliwa. Wanatazama kwa mfano wa agano la Mungu na kutamani kulindwa kwa utukufu wake.

Kwa watu wa Mungu sauti imesikiwa, kusema, "Tazama". Kama Stefano wanatazama na wanaona utukufu wa Mungu na wa Mwana wa watu katika kiti chake cha enzi. Tazama Matendo 7:55, 56. Wanatambua alama za unyenyekevu wake, na wanasikia ombi, "nataka sana hawa ulionipa wakae pamoja nami pahali nilipo". Yoane 17:24. Sauti imesikiwa ikisema, "Wanakuja, watakatifu, wapole, na safi! Wameshika neno la uvumilivu wangu".

Kwa usiku wa manane Mungu anaonyesha uwezo wake kwa ajili ya ukombozi wa watu wake. Jua linatokea likingaa kwa nguvu zake. Alama na maajabu yanafuata. Waovu wanatazama kwa hofu kuu kwa tokeo lile, huku wenye haki wakitazama alama za ukombozi wao. Katikati ya mbingu zenye hasira kukaonekana nafasi moja wazi ya utukufu usioelezeka na pale sauti ya Mungu ikatokea kama sauti ya maji mengi, ikisema, "imefanyika! " Ufunuo 16:17.

[310] Sauti inatetemesha mbingu na dunia. Hapo ni tetemeko kubwa la inchi, "hata tangu watu walipokuwa juu ya dunia halikuwa namna ile, namna lilivyokuwa kubwa tetemeko hili. " Ufunuo 16:18. Miamba iliyopasuka ikatawanyika pande zote. Bahari ikatikisatikisa kwa hasira kali. Hapo kunasikiwa mlio wa nguvu wa tufani kama sauti ya mashetani. Upande wa juu wa inchi ukapasuka. Misingi yake yenyewe yaonekana kutoweka. Miji yenye bandari iliyokuwa kama Sodomo kwa ajili ya uovu imemezwa kwa maji yenye hasira. "Babeli ule mkubwa" ukakumbukwa mbele ya Mungu, "kupewa kikombe cha mvinyo ya gazabu ya kasirani yake. " Ufunuo 16:19. Mvua ya mawe makubwa sana ikafanya kazi yake ya uharibifu. Miji yenye kiburi inaangushwa chini. Majumba ya fahari ambayo watu walitolea mali nyingi yao ikafunikwa na ikageuka mavumbi mbele ya macho yao. Kuta za gereza zimevunjika kwa vipande vipande, na watu wa Mungu wamewekwa huru.

Makaburi yamefunguka, na "wengi wao wanaolala mavumbini mwa inchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, na wengine kwa haya na kuzarauliwa kwa milele". "Na wale waliomuchoma", wale ambao walichekelea maumivu makali ya kifo cha Kristo, na wapinzani (adui) wakali zaidi wa kweli yake, watafufuka kuona heshima inayowekwa kwa waaminifu na watiifu. Danieli 12:2; Ufunuo 1:7.

Umeme kali utafunika dunia kwa shuka la ndimi ya moto. Juu ya ngurumo (radi), sauti za ajabu na hofu kubwa, zinatangaza mwisho wa waovu. Wale waliokuwa wenye kujisifu na wenye kutaka vita, wakali kwa wenye kushika amri za Mungu, sasa wanatetemeka kwa woga. Mashetani wanatetemeka wakati watu wanapoomba rehema.

## Siku ya Bwana

Asema nabii Isaya: " Kwa siku ile mtu atatupa sanamu yake ya feza, na sanamu yake ya zahabu, walizojifanyizia kuziabudu, kwa panya na kwa popo; waingie katika mapango ya miamba, na ndani ya pahali pa juu ya mawe yaliyo pasukapasuka, toka mbele ya hofu ya Bwana, na toka utukufu wa mamlaka yake, wakati atakaposimama kutikisatikisa sana dunia". Isaya 2:20, 21.

Wale waliotoa vyote kwa ajili ya Kristo sasa wanakuwa katika salama. Mbele ya ulimwengu nausoni kwa mauti wameonyesha uaminifu wao kwake yeye aliyekufa kwa ajili yao. Nyuso zao, juzijuzi zilikuwa zenye kufifia na zenye kukonda, sasa zinangaa kwa ajabu. Sauti zao zinainuka kwa wimbo wa ushindi: "Mungu ni [311] kimbilio letu na nguvu yetu, Msaada aliye karibu sana wakati wa mateso. Kwa hivi hatutaogopa, hata inchi ikibadilika, na hata milima ikihamishwa moyoni mwa bahari; Hata maji yao yakinguruma na kuchafuka, hata milima ikitikisika kwa kiburi chake". Zaburi 46:1-3.

Wakati maneno haya ya tumaini takatifu yanapopanda kwa Mungu, utukufu wa mji wa mbinguni unapita kwa milango inayofunguka kidogo. Ndipo pale panatokea kinyume cha mawingu mkono unaoshika mbao mbili za mawe. Sheria ile takatifu, iliyotangazwa kwa Sinai, imefunuliwa sasa kama kanuni ya hukumu. Maneno yanakuwa wazi ili wote waweze kuyasoma. Ukumbusho umeamshwa. Giza ya imani ya mambo ya uchawi na uzushi imesafishwa kwa kila wazo.

Ni vigumu kueleza hofu kuu na kukata tamaa kwa wale waliokanyanga sheria ya Mungu. Kwa kufanya urafiki na ulimwengu, wameweka kando maagizo yake na wakafundisha wengine kuzivunja. Sasa wamehukumiwa kwa sheria ile ambayo wameizarau. Wanaona ya kwamba wanakuwa bila kisingizio. Adui za sheria ya Mungu wanakuwa na wazo mpya juu ya kweli na mapashwa. Kuchelewa sana wanaona ya kwamba Sabato ni muhuri wa Mungu mwenye uhai. Ni kuchelewa sana wanaona msingi wa mchanga ambapo juu yake walijenga. Wamekuwa wakipigana kumpinga Mungu. Waalimu wa dini wameongoza roho kwa jehanum (kupotea milele) walipokuwa wakidai kuwaongoza kwa Paradiso. Ni madaraka makubwa ya namna gani ya watu katika kazi takatifu, matokeo ya kutisha namna gani kwa kutokuamini kwao!

## Mfalme wa Wafalme Anatokea

Sauti ya Mungu imesikilika kutangaza siku na saa ya kuja kwa Yesu. Israeli wa Mungu anasimama kwa kusikiliza, nyuso zao zikaangaziwa na utukufu wake. Karibu pale kukatokea kwa upande wa mashariki wingu nyeusi dogo. Ni wingu linalomzunguka Mwokozi. Kwa utulivu wa heshima watu wa Mungu wakalitazama kwa namna lilikuwa likikaribia, hata linapokuwa wingu jeupe kubwa, upande wa chini wake ni utukufu kama moto unaoteketeza, na upande wa juu wake upindi wa mvua wa agano. Sasa si "Mtu wa huzuni", Yesu anapanda (farasi) kama mshindi mkubwa. Malaika watakatifu, makutano makubwa yasiyohesabika, wanamtumikia, "elfu elfu, na elfu kumi mara elfu kumi". Kila jicho linamwona Mfalme wa uzima. Taji la utukufu linakuwa katika kipaji cha uso
[312] wake. Uso wake unashinda (muangaza) wa jua la saa sita. "Naye ana jina llienya kuaandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA". Ufunuo 19:16.

Mufalme wa wafalme anashuka juu ya wingu, amefunikwa katika moto unaowaka. Dunia inatetemeka mbele yake: "Mungu wetu atakuja, wala hatanyamaza; Moto utakuia mbele yake, Na tufani inayovuma sana itamuzunguka. Ataita mbingu zilizo juu na inchi, ili apate kuhukumu watu wake". Zaburi 50:3,4.

"Na wafalme wa dunia, na watu mashuhuri, na matajiri, na kila mtumwa, na kila mtu mwenye uhuru wakajificha katika pango na chini ya miamba: Mutuangukie, mutufiche mbele ya uso wake yeye anayeketi juu ya kiti cha ufalme, na gazabu ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku kubwa ya gazabu yake imekuja na nani anayeweza kusimama"? Ufunuo 6:15-17.

Mabishano ya mizaha yamekoma, midomo ya uwongo imenyamazishwa. Hakuna kitu kinachosikiwa lakini sauti ya maombi na sauti ya kilio. Waovu wanaomba kuzikwa chini ya miamba kuliko kukutana na uso wake yeye waliyezarau. Sauti ile iliyoingia kwa sikio la maiti, wanajua. Mara ngapi inakuwa sauti zile za upole ziliwaita kwa toba. Mara ngapi ilikuwa ikisikiwa katika maombi ya rafiki, ya ndugu, ya Mkombozi. Sauti ile inayoamsha ukumbusho wa maonyo yaliyozarauliwa na miito iliyokataliwa.

Kunakuwa wale waliochekelea Kristo katika unyenyekevu wake. Alitangaza: "Tangu sasa mutaona Mwana wa watu akiketi kwa

mkono wa kuume wa uwezo, na akija katikati ya mawingu ya mbingu”. Matayo 26:64. Sasa wanamutazama katika utukufu wake; wanapashwa sasa kumwona yeye kukaa kwa mkono wa kuume wa uwezo. Pale kunakuwa Herode mwenye kiburi aliyechekelea cheo chake cha ufalme. Pale panakuwa watu waliomvika taji la miiba juu ya kichwa chake na katika mkono wake fimbo ya kifalme ya kufananisha--wale walioinama mbele yake kwa kutoa heshima ya kumzihaki, waliomtemea mate Mfalme wa uzima. Wanatafuta kukimbia mbele ya uso wake. Wale waliopigilia misumari kwa mikono yake na miguu wanatazama alama hizi kwa hofu na majuto.

Kwa hofu ya wazi wazi makuhani na watawala wanakumbuka matukio ya Kalvari, namna gani, walipotikisa vichwa vyao katika shangwe ya uovu wa Shetani, wakapaaza sauti, “Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa yeye mwenyewe”. Matayo 27:42. Kwa sauti kubwa kuliko kelele, “Asulibiwe, asulibiwe”! ambayo ikavuma katika Yerusalema, inaongeza maombolezo ya kukata tamaa, ‘’Yeye ni Mwana wa Mungu”! Wanatafuta kukimbia mbele ya uso wa Mfalme wa wafalme. [313]

Katika maisha ya wote wanaokataa kweli kunakuwa na nyakati ambapo zamiri inaamka, wakati nafsi inaposumbuliwa na masikitiko ya bure. Lakini mambo haya ni nini kulinganisha na majuto ya siku ile! Katikati ya hofu kuu yao wanasikia watakatifu kupaaza sauti: “Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, Tuliyemungoja, naye atatuokoa”. Isaya 25:9.

Sauti ya Mwana wa Mungu inaita kwa kuamsha watakatifu wanaolala. Po pote duniani wafu watasikia sauti ile, na wale wanaoisikia wataishi, jeshi kubwa la kila taifa, na kabila na lugha na jamaa. Kutoka kwa nyumba ya gereza ya wafu wanakuja, wanapovikwa utukufu wa milele, kupaaza sauti: “Ee mauti, kushinda kwako ni wapi? Ee mauti, uchungu wako ni wapi”? 1 Wakorinto 15:55.

Wote wanaamka kutoka makaburini wakiwa kwa hali ileile waliyopoingia nayo kaburini. Lakini wote wanafufuka pamoja na upya na nguvu za ujana wa milele. Kristo alikuja kurudisha na kuponya kile kilichopotea. Atabadilisha miili yetu ya unyonge na kuzifanya kama wake mwili mtukufu. Mwili wa mauti na wa kuharibika, mara moja unaoharibika na zambi, unakuwa sasa kamilifu, mzuri na wa kuishi milele. Madoo na ulema vimebaki ndani

ya kaburi. Waliokombolewa “watakua” (Malaki 4:2) kwa kimo kamili cha uzao katika utukufu wake wa kizazi cha kwanza, alama za mwisho za laana za zambi zimeondolewa. Waaminifu wa Kristo wataonyesha mfano kamili wa Bwana wao katika roho na nafsi na mwili.

Wenye haki walio hai wamebadilika “kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua kwa jicho”. Kwa sauti ya Mungu wamefanywa watu wa maisha ya milele na pamoja na watakatifu waliofufuka watachukuliwa juu kumlaki Bwana wao katika mawingu. Malaika “watakusanya wachaguliwa wake toka pepo ine, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho mwingine”. Matayo 24:31. Watoto wadogo wamechukuliwa kwa mikono ya mama zao. Rafiki walioachana wakati mrefu kwa ajili ya mauti wameunganika, hakuna kuachana tena kamwe, na pamoja na nyimbo za furaha wanapanda pamoja kwa mji wa Mungu.

## Katika Mji Mtakatifu

Po pote kwa jeshi lisilohesabika la waliokombolewa kila jicho limekazwa kwa Yesu. Kila jicho linatazama utukufu wake ambaye “uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu ye yote, na sura [314] yake zaidi ya watoto wa watu”. Isaya 52:14. Juu ya vichwa vya washindaji Yesu anaweka taji ya utukufu. Kwani kila mmoja kule kunataji ambalo lina “jina jipya” lake mwenyewe (Ufunuo 2:17) na mwandiko “Utakatifu kwa Bwana”. Katika kila mkono kumewekwa tawi la ngazi la ushindi na kinubi chenye kungaa. Ndipo, wakati malaika wenye kuamrisha wanapopiga sauti, kila mkono unapiga juu ya nyuzi na mguso wa ufundi mzuri sana, mkazo wa masauti. Kila sauti inainuliwa kwa sifa za shukrani: “Kwa yeye aliyetupenda na kutuosha zambi zetu kwa damu yake, na kutufanya kuwa wafalme wa makuhani kwa Mungu na Baba yake; kwa yeye ni utukufu na uwezo hata milele na milele”. Ufunuo 1:5,6.

Mbele ya makutano ya waliokombolewa ni Mji Mtakatifu. Yesu anafungua milango, na mataifa yaliyolinda ukweli wanaingia ndani. Ndipo sauti yake imesikiwa, “Kujeni, ninyi muliobarikiwa na Baba yangu, mriti ufalme muliotengenezewa tangu kuumbwa kwa ulimwengu”. Matayo 25:34. Kristo anaonyesha kwa Baba yake ununuzi wa damu yake, kusema; ‘’Tazama, mimi ni hapa pamoja

na watoto ulionipa “Wale ulionipa niliwachunga”. Waebrania 2:13; Yoane 17:12. Ee, furaha ya saa ile wakati Baba wa milele, kutazama kwa waliokombolewa, watatazama mfano wake, uharibifu wa zambi ukisha ondolewa, na binadamu mara ingine tena katika umoja na Mungu!

Furaha ya Mwokozi ni kwa kuona, katika ufalme wa utukufu, mioyo iliyookolewa kwa maumivu yake makali na unyenyekevu. Mtu aliyeokolewa atashiriki katika furaha yake; wanatazama wale waliopatikana kwa njia ya maombi yao, kazi, na kafara ya upendo. Shangwe itajaa katika mioyo yao wakati wanapoona yule aliyeokoa wengine, na hawa zaidi na wengine.

## Wanadamu Wawili Wanakutana

Wakati waliookolewa wanapokaribishwa kwa mji wa Mungu, hapo kunakuwa kilio cha shangwe nyingi. Wanadamu wawili ni karibu kukutana. Mwana wa Mungu anapashwa kupokea baba wa taifa letu--aliyeumbwa, aliyefanya zambi, na kwa ajili ya zambi yake alama za msalaba zinakuwa kwa sura ya Mwokozi. Wakati Adamu alipotambua alama za misumari, kwa unyenyekevu anaanguka yeye mwenyewe kwa miguu ya Kristo. Mwokozi anamwinua na kumwalika kutazama tena kwa makao ya Edeni ambapo amehamishwa kwa wakati mrefu.

Maisha ya Adamu yalijazwa na huzuni. Kila jani lililokufa, kila [315]
nyama wa kafara, kila doa juu ya utakatifu wa mtu, ilikuwa ukumbusho wa zambi yake. Maumivu ya majuto yalikuwa ya kutisha sana wakati alipokutana na laumu zilizotupwa juu yake mwenyewe kama sababu ya zambi. Kwa uaminifu akatubu zambi yake, na alikufa katika tumaini la ufufuko. Sasa, kwa njia ya upatanisho, Adamu amerudishiwa hali ya kwanza.

Alipojazwa na furaha, anatazama miti ambayo ilikuwa mara ya kwanza furaha yake, matunda yake yeye mwenyewe alikuwa akikusanya mbele ya kuwa na hatia. Ameona mizabibu ambayo mikono yake mwenyewe ilikomalisha, maua aliyoyapenda zamani kulinda. Hii ni Edeni iliyorudishwa kweli!

Mwokozi akamwongoza kwa mti wa uzima na akamwalika kula. Akatazama mkutano wa jamaa yake waliokombolewa. Ndipo akatupa taji lake kwa miguu ya Yesu na kumkumbatia Mkombozi.

Akagusa kinubi, na sehemu ya juu pa mbingu ikarudisha mwitiko wa sauti za wimbo wa ushindi: “Anastahili Mwana kondoo” aliyechinjwa”. Ufunuo 5:12. Jamaa ya Adamu inatupa taji zao kwa miguu ya Mwokozi wanapoinama wakiabudu. Malaika walilia kwa kuanguka kwa Adamu na wakafurahi wakati Yesu alipofungua kaburi kwa wote walioamini kwa jina lake. Sasa wanatazama kazi ya ukombozi kutimizwa na kuunga sauti zao kwa kusifu.

Kwa “bahari ya kioo iliyochanganyika na moto” wamekutanika kundi la watu ambao “waliomshinda yule mnyama na sanamu na alama yake, na hesabu ya jina lake”. Wale elfu mia moja na makumi ine na ine waliokombolewa katika watu, na wanaimba “wimbo mpya” wimbo wa Musa na wimbo wa Mwana-Kondoo. Ufunuo 15:2,3. Hakuna mtu bali wale elfu mia moja na makumi ine na ine watakaoweza kujifunza wimbo ule, kwa maana ni wimbo wa mambo ya maisha ambayo hakuna jamii ingine walikuwa nayo”. Hawa ndio wanaofuata Mwana-Kondoo kila pahali anapokwenda. “Hawa waliochukuliwa kutoka katikati ya wahai, ni “malimbuko ya kwanza kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo”. Ufunuo 14:4,5. Walipitia katika wakati wa mateso makubwa ambayo hayajakuwako tangu taifa lilikuwako; walivumilia maumivu makuu ya wakati wa taabu ya Yakobo; walisimama pasipo mwombezi katika kumiminwa kwa mwisho kwa hukumu za Mungu. “Wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo”. “Na katika vinywa vyao haukuonekana uwongo; maana wao ni pasipo kilema” mbele ya Mungu. “Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala joto lo lote. Kwani Mwana-Kondoo,
[316] aliye katikati ya kiti cha enzi atawachunga, naye atawaongoza hata chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atapangusa machozi yote katika macho yao”. Ufunuo 7:14; 14:5; 7:16,17.

## Waliokombolewa katika Utukufu

Katika vizazi vyote wateule wa Mwokozi wametembea katika njia nyembamba. Wametakaswa katika tanuru ya mateso. Kwa ajili ya Yesu wakavumilia uchuki, masingizio, kujinyima, na hasara za uchungu. Walijifunza ubaya wa zambi, uwezo wake, kosa yake, msiba wake; wanaitazama na machukio makuu. Maana ya kafara isiyokuwa na mwisho iliyofanywa kwa ajili ya dawa yake in-

awanyenyekeza na kujaza mioyo yao na shukrani. Wanapenda sana kwa sababu walisamehewa sana. Tazama Luka 7:47. Washiriki wa mateso ya Kristo, wanastahili kuwa washiriki wa utukufu wake.

Wariti wa Mungu wanatoka kwa vyjumba vya orofani, vibanda vibovu, gereza, mahali wauaji wanaponyongwa kwa sheria, milimani, jangwani, mapangoni. Walikuwa "maskini, wakiteswa, kusumbuliwa". Mamilioni walienda kwa kaburi wakilemezwa na sifa mbaya kwa sababu walikataa kujitoa kwa Shetani. Lakini sasa hawateseki tena, hawatawanyike tena, na hawaonewe. Toka sasa wanasimama wanapovaa mavazi ya utajiri kuliko nguo watu walioheshimiwa sana wa dunia waliyovaa, kuvikwa na mataji ya utukufu zaidi kuliko yale yaliyovikwa kwa paji la uso ya wafalme wa dunia. Mfalme wa utukufu amepanguza machozi kwa nyuso zote. Wanatoa wimbo wa sifa, wazi, tamu, na wakupatana. Wimbo wa furaha ukaenea katika miruko ya mbinguni: "Wokovu kwa Mungu wetu anayeketi juu ya kiti cha enzi, na kwa Mwana-Kondoo". Na wote wakaitika, "Amina: Baraka na utukufu, na hekima, na shukrani, na heshima, na uwezo, na nguvu kwa Mungu wetu hata milele na milele". Ufunuo 7:10,12.

Katika maisha haya tunaweza tu kuanza kufahamu asili ya ajabu ya wokovu. Kwa ufahamu wetu wenye mpaka tungeweza kufikiri zaidi kwa kweli haya na utukufu, uzima (maisha) na mauti, haki na rehema, yanayokutana katika msalaba; lakini kwa mvuto zaidi wa nguvu za akili yetu tunashindwa kuelewa maana yake kamili. Urefu na upana, urefu wa kwenda chini na urefu wa kwenda juu, wa upendo wa ukombozi unafahamika kidogo tu. Shauri la wokovu halitafahamika kamili, hata wakati waliokombolewa wanapoona kama wanavyoonwa na kujua kama wanavyojulikana; lakini katika vizazi vya milele kweli mpya itaendelea kufunuliwa akili ya ajabu na furaha. Ijapo masikitiko na maumivu na majaribu ya dunia yanapo- [317]
malizika na sababu imeondolewa, watu wa Mungu watakuwa na maarifa ya kupambanua, na akili ya kufahamu bei ya wokovu wao. Msalaba utakuwa ni wimbo wa waliookolewa milele. Katika Kristo aliyetukuzwa wanamtazama Kristo aliyesulibiwa. Haitasahauliwa kamwe ya kwamba Mwenye Enzi wa mbinguni alijinyenyekeza mwenyewe kwa kuinua mtu aliyeanguka, ili achukue kosa na haya ya zambi na kuficha uso wa Baba yake hata misiba ya ulimwengu uliopotea unapovunja moyo wake na kuangamiza maisha yake.

Muumba wa dunia yote akaweka pembeni utukufu wake sababu ya upendo kwa mtu--hii itaamsha milele mshangao wa viumbe vyote. Wakati mataifa ya waliookolewa wanapomtazama Mkombozi wao na kujua ya kwamba ufalme wake ni wa kutokuwa na mwisho, wanaendelea katika wimbo: "Anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, na aliyetukomboa kwa Mungu kwa damu yake mwenyewe ya damani!"

Siri ya msalaba inaeleza siri zote. Itaonekana ya kwamba yeye anayekuwa pasipo mwisho kwa hekima hangefanya shauri lingine kwa ajili ya wokovu wetu isipokuwa kafara ya Mwana wake. Malipo kwa ajili ya kafara hii ni furaha ya kujaza dunia na viumbe vilivyokombolewa, vitakatifu, vya furaha, na vya milele. Hii ni damani ya nafsi ambayo Baba anatoshelewa kwa bei iliyolipwa. Na Kristo mwenyewe, kwa kutazama matunda ya kafara yake kubwa, anatoshelewa.

# 41 /DUNIA KATIKA UHARIBIFU [318]

Wakati sauti ya Mungu inapogeuza utumwa wa watu wake, pale panakuwa na muamko wa kutisha wa wale waliopoteza vyote katika vita kubwa ya maisha. Kupofushwa na madanganyo ya Shetani watajiri wakajisifu wenyewe kwa ukuu wao kwa wale wasiofanikiwa sana. Lakini hawakujali kulisha wenye njaa, kuvika wale waliokuwa unchi, kufanya kwa haki, na kupenda rehema. Sasa wameondolewa vyote vilivyowafanya kuwa wakubwa na wameachwa ukiwa (maskini). Wanatazama kwa hofu juu ya kuangamia kwa sanamu zao. Wameuzisha nafsi zao kwa ajili ya anasa ya dunia na hawakuwa watajiri kwa Mungu. Maisha yao ni ya kushindwa, anasa zao zimegeuka kuwa uchungu. Faida ya maisha yao yote imepotea kwa wakati moja. Watajiri wanalilia kuangamia kwa nyumba zao kubwa, kutawanyika kwa zahabu yao na feza, na hofu ya kwamba wao wenyewe wanapashwa kuangamia pamoja na sanamu zao. Waovu wanaomboleza ya kwamba matokeo ni vile inavyokuwa, lakini hawatubu kwa maovu yao.

Mhubiri aliyefanya ukweli kwa kafara makusudi ya kupata upendeleo wa watu sasa anatambua mvuto wa mafundisho yake. Kila mustari ulioandikwa, kila neno lililotamkwa lililoongoza watu kudumu katika kimbilio la uwongo limetawanya mbegu: na sasa anatazama mavuno. Bwana anasema: "Ole wao wachungaji, wanaoharibu na kutawanya kondoo za malisho yangu! ... Angalieni, nitaleta juu yenu uovu wa matendo yenu". "kwa uwongo mumehuzunisha moyo wao walio haki, nisiowahuzunisha; nakutia nguvu mikono ya mwovu, hata asigeuke toka njia yake ya uovu, na kuponyeshwa hai". Yeremia 23:1,2; Ezekieli 13:22.

Wahubiri na watu wanaona ya kuwa wameasi juu ya Muumba wa sheria yote ya haki. Kuweka pembeni maagizo ya Mungu kulitoa mwinuko kwa maelfu ya nguvu za uovu, hata dunia ikawa mfereji moja mkubwa wa zambi. Hakuna lugha inayoweza kueleza tamaa ya wasiowaaminifu wanapotazama wale walivyopoteza milele--uzima wa milele.

Watu wanashitakiana wao kwa wao kwa ajili ya kuwaongoza kwa uharibifu, lakini wote wanaunganika kwa kukusanya hukumu yao ya uchungu mkubwa juu ya wachungaji wasiokuwa waaminifu waliotabiri "maneno ya laini" (Isaya 30:10), walioongoza wasikilizaji wao kufanya ukiwa sheria ya Mungu na kutesa wale wangeishika kama takatifu. "Tumepotea"! wameomboleza, "na
[319] ninyi ndio munaokuwa sababu yenyewe". Mikono iliyowatawaza zamani kwa heshima itanyanyuliwa kwa ajili ya uharibifu wao. Po pote kunakuwa vita na umwangaji wa damu.

Mwana wa Mungu na wajumbe wa mbinguni wamekuwa katika vita pamoja na muovu, kwa kuonya, kuangazia, na kuokoa wana wa watu. Sasa wote wamefanya mipango (makusudi) yao; waovu wameungana kabisa na Shetani katika vita kupigana na Mungu. Mabishano si ya Shetani peke yake, lakini pamoja na watu. "Bwana ana mashindano na mataifa". Yeremia 25:31.

## Malaika wa Mauti

Sasa malaika wa mauti anaenda mbele, anaonyeshwa katika ndoto ya Ezekieli kwa watu wanaokuwa na silaha za kuchinja, kwao agizo limetolewa: "Ueni kabisa mzee na kijana, na wote wawili wasichana, na watoto wadogo, na wanawake, lakini musikaribie mtu aliye na alama ile juu yake; na anzieni kwa pahali pangu patakatifu", ''halafu wakaanza kwa wazee walio mbele ya nyumba, "wale waliojidai kuwa walinzi wa kiroho wa watu. Ezekieli 9:6.

Walinzi wa uwongo wanakuwa wa kwanza kuanguka. "Kwa maana tazama, Bwana anakuja kutoka pahali pake kuazibu wenye kukaa duniani kwa sababu ya uovu wao; na dunia itafunua damu yake, na haitafunika tena watu wake waliouawa". "Na itakuwa siku ile makelele makubwa toka kwa Bwana yatakuwa katikati yao; nao watakamata kila mtu mkono wa jirani yake, na mkono wake utanyanyuliwa juu ya mkono wa jirani yake" Isaya 26:21; Zekarai 14:13.

Katika vita yenye wazimu ya tamaa kali zao wenyewe na kwa kumiminika kwa gazabu ya Mungu isiyo changanywa, wakuhani waovu wanaanguka, watawala, na watu. "Na waliouawa wa Bwana siku ile watakuwa toka mwisho wa dunia hata mwisho wa dunia". Yeremia 25:33.

Kwa kuja kwa Kristo waovu wataangamizwa kwa mwangaza wa utukufu wake. Kristo atachukua watu wake kwa mji wa Mungu, na dunia itafanyiwa utupu kwa wakaaji wake. "Tazama Bwana anafanya dunia kuwa utupu, na anaiharibu, na anaipindua, na kuwasambaza popote wakaaji wake... Inchi itafanywa kuwa utupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; kwa maana Bwana amesema neno hili... kwa sababu wamevunja sheria, wamegeuza amri, wamevunja agano la milele. Kwa sababu hii laana imekula dunia, na watu wanaokaa ndani yake wanaonekana kuwa na laumu: kwa hivi wakaaji wa dunia wamechomwa". Isaya 24:1,3,5,6. [320]

Dunia inaonekana kama jangwa lenye ukiwa. Miji imeharibiwa na tetemeko, miti kungolewa, miamba iliyopasuka duniani imetawanyika juu ya uso wa dunia. Mapango makubwa yanaonyesha alama mahali milima ilipasuka kutoka kwa misingi yao.

## Uhamisho wa Shetani

Sasa matukio yamefanyika yaliyoonyesha mbele heshima ya kazi ya mwisho kwa Siku ya upatanisho. Wakati zambi za Israeli zilipoondolewa kutoka Pahali patakatifu kwa uwezo wa damu ya sadaka ya zambi, mbuzi wa Azazeli alionyeshwa hai mbele ya Bwana. Kuhani mkuu akaungama juu yake "maovu yote ya wana wa Israeli,... kuyaweka juu ya kichwa cha mbuzi". Walawi 16:21. Vilevile, wakati kazi ya upatanisho katika Pahali patakatifu pa mbinguni itakapotimia, ndipo, mbele ya Mungu na malaika wa mbinguni na jeshi la waliookolewa, zambi za watu wa Mungu zitawekwa juu ya Shetani; atatangazwa kuwa na kosa ya uovu wote aliolazimisha wao kuufanya. Kama vile mbuzi wa Azazeli aliochukuliwa katika inchi isiyokaliwa na watu, vivyo hivyo Shetani atahamishwa kwa dunia yenye ukiwa.

Baada ya kuonyesha mambo ya ajabu ya kuja kwa Bwana, mfunuaji anaendelea: "kisha nikaona malaika akishuka toka mbingu, mwenye ufunguo wa shimo lisilo na mwisho, na munyororo mkubwa katika mkono wake. Akamshika yule joka mkubwa, yule nyoka ya zamani, anayeitwa Diabolo na Shetani, akamufunga miaka elfu, na akamutupa katika shimo lisilo na mwisho, na kumufunga, na kutia muhuri juu yake, asipate kudanganya mataifa tena, hata ile

miaka elfu itimie; na nyuma ya hayo inapashwa afunguliwe wakati kidogo”. Ufunuo 20:1-3.

“Shimo lisilo na mwisho” ni mfano wa dunia katika machafuko na giza. Kutazamia siku kubwa ya Mungu, Yeremia anatangaza; “Niliangalia inchi, na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; niliangalia mbingu, nazo hazikuwa na nuru. Niliangalia milima, na tazama, zilitetemeka, na vilima vyote vilitikisika polepole. Nikaangalia, na tazama, hakuna mtu hata mmoja, na ndege zote za mbingu wamekimbia. Nikaangalia, na tazama, shamba lililozaa sana limekuwa jangwa, na miji yake yote ilikuwa imebomoka”. Yeremia 4:23-26.

Hapa ndipo makao ya Shetani pamoja na malaika wake waovu kwa miaka 1000. Amefungiwa kwa dunia hii, hatakuwa na ruhusa ya kuingia kwa dunia zingine kwakujaribu na kusumbua
[321] wale ambao hawajaanguka kamwe. Kwa nia hii “amefungwa”. Hakuna anayebakia ambaye anaweza kutumia uwezo wake juu yake. Amekata kwa kazi ya mudanganyifu na uharibifu ambayo ilikuwa anasa yake ya pekee.

Isaya alipokuwa akitazamia maangamizi ya Shetani, anapaza sauti: “Umeanguka toka mbinguni, namna gani, Ee, Lusifero, mwana wa asubui! Umekatwa hata kufika udongo, Wewe uliyeangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako: Nitapanda mbinguni, nitanyanyua kiti changu cha enzi juu kuliko nyota za Mungu: ... Nitafanana na Mkuu Sana. Kwani hivi utashushwa mpaka Hadeze, Kwa pande za mwisho za shimo. Wao wanaokuona watakutazama kwa kubanua sana; watakufikiria, wakisema: Huyu ndiye mtu aliyetetemesha dunia, aliyetikisa wafalme; aliyefanya dunia kama jangwa, na aliyeharibu miji yake; yule asiyefungua nyumba ya wafungwa wake? Isaya 14:12-17.

Kwa mda wa miaka 6000, nyumba ya gereza ya Shetani imepokea watu wa Mungu, lakini Kristo amevunja vifungo vyake na kufungua wafungwa. Peke yake pamoja na malaika wake waovu anafahamu moyoni tokeo la zambi: “Wafalme wote wa mataifa, wao wote wanalala katika utukufu, Kila mmoja ndani ya nyumba yake mwenyewe (kaburi);

Lakini wewe umetupwa inje kutoka kaburi lako, Kama tawi linalochukiza... Hutaungwa pamoja nao katika maziko: Kwa sababu umeiharibu inchi yako, na kuua watu wako.” Isaya 14:18-20.

Kwa mda wa miaka 1000, Shetani ataona matokeo ya uasi wake juu ya sheria ya Mungu. Maumivu yake ni mingi sana. Sasa ameachwa kwa kufikiri sana sehemu aliyofanya tangu alipoasi na kutazamia mbele kwa hofu kubwa kwa wakati ujao wa kutisha wakati atakapopashwa kuazibiwa.

Kwa mda wa miaka 1000 katikati ya ufufuo wa kwanza na wa pili, hukumu ya waovu itafanyika. Paulo anaonyesha kwa hii kama tukio linalofuata kurudi kwa Yesu. 1 Wakorinto 4:5. Wenye haki wanatawala kama wafalme na makuhani. Yoane anasema: "Nikaona viti vya enzi, nao wakakaa juu yao vilevile, nao wakapewa hukumu... Watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye miaka elfu". Ufunuo 20:4-6.

Kwa wakati huu "watakatifu watahukumu dunia". 1 Wakorinto 6:2. Kwa umoja na Kristo wanahukumu waovu, kukata kila jambo kufuatana na matendo yaliyotendwa katika mwili. Ndipo sehemu ambayo waovu wanapaswa kuteswa nayo imetolewa, kufuatana na matendo yao, na imeandikwa juu ya majina yao katika kitabu cha mauti. [322]

Shetani na malaika waovu wamehukumiwa na Kristo na watu wake. Paulo anasema: "Hamujui ya kwamba tutawahukumu malaika"? 1 Wakorinto 6:3. Yuda anatangaza: "Hata malaika wasiolinda enzi yao giza kwa hukumu ya siku ile kubwa". Yuda 6.

Kwa mwisho wa miaka 1000, ufufuo wa pili utafanyika. Halafu waovu watafufuliwa kutoka katika wafu na kuonekana mbele ya Mungu kwa ajili ya utimilizo wa "hukumu iliyoandikwa". Zaburi 149:9. Ndivyo Mfunuaji anasema: "Na wafu waliobaki hawakuwa hai hata itimie ile miaka elfu". Ufunuo 20:5. Na Isaya anatangaza juu ya wenye zambi: "Nao watakusanywa pamoja, kama vile kukusanya kwa wafungwa katika shimo, na watafungwa katika kifungo, na *nyuma ya siku nyingi wataangaliwa"*. Isaya 24:22.

[323] # 42 /AMANI YA MILELE: VITA IMEMALIZIKA

Kwa mwisho wa miaka 1000, Kristo anarudi duniani akisindikizwa na waliokombolewa na jamii ya malaika. Anaagiza wafu waovu watoke kupokea maangamizi yao. Wanatoka, wengi sana kama mchanga wa bahari, wanapokuwa na alama za ugonjwa na mauti. Tofauti namna gani kwa wale waliofufuka katika ufufuko wa kwanza!

Macho yote inageuka kutazama utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa sauti moja majeshi ya waovu wanapaza sauti: "Amebarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana"! Matayo 23:39. Si mapendo yanayoongoza maneno haya. Nguvu ya kweli inalazimisha maneno kutoka kwa midomo isiyotaka. Kama vile waovu walivyokwenda katika makaburi, ndivyo hivyo wanafufuka pamoja na uadui wa namna moja kwa Kristo na roho ya namna ileile ya uasi. Hawatapewa wakati wa rehema mpya kwa kuponyesha maisha yao ya wakati uliopita.

Nabii anasema: "Na miguu yake itasimama siku ile juu ya mlima wa Mzeituni, ... na Mlima wa Mzeituni utapasuka katikati yake". Zakaria 14:4. Wakati Yerusalema mpya unaposhuka toka mbinguni, utapumzika kwa pahali palipotayarishwa, na Kristo, pamoja na watu wake na malaika, wanaingia kwa mji mtakatifu.

Wakati alipokatwa kazi yake ya kudanganya, mtawala wa uovu alikuwa maskini na mwenye huzuni, lakini kwa namna wafu waovu wanapofufuka na anapoona makutano makubwa kwa upande wake, matumaini yake yanarudi. Anakusudia si kutokuacha vita kubwa. Atapanga wapotevu chini ya bendera yake. Kwa kukana Kristo wamekubali amri ya mwongozi mwasi, tayari kufanya mapenzi yake. Lakini, kweli kwa werevu wake wa kwanza, hakubali yeye mwenyewe kuwa Shetani. Anadai kuwa mwenyewe wadunia wa haki ambaye alinyanganywa uriti bila sheria. Anajionyesha mwenyewe kama mkombozi, kuhakikisha watu wake waliodanganyiwa ya kwamba uwezo wake umewaleta kutoka kwa makaburi yao. Shetani anawafanya wazaifu kuwa wenye nguvu, na kuwa-

sukuma wote kwa nguvu zake mwenyewe kuwaongoza kukamata makao ya mji wa Mungu. Akatazama kwa mamilioni yasiyohesabika ya waliofufuliwa kutoka kwa wafu, na akatangaza ya kwamba kama muongozi wao anaweza kupata tena kiti chake chaenzi na ufalme.

Katika makutano makubwa haya kunakuwa na taifa lenye maisha marefu lile lililoishi mbele ya garika, watu wa kimo kirefu sana [324] na wa akili nyingi; watu ambao kazi zao za ajabu zikaongoza ulimwengu kuabudu akili zao, lakini mambo ya uvumbuzi wa ukali na uovu wao ikafanya Mungu kuwaharibu kutoka kwa viumbe vyake. Pale kunakuwa wafalme na wajemadari wasioshindwa kamwe kwa vita. Katika mauti hawa hawakupata badiliko. Wanapotoka kwa kaburi, wanaendeshwa kwa tamaa ya namna ileile ya kushinda wale waliowatawala wakati walishindwa.

### Shambulio la Mwisho la Kumpinga Mungu

Shetani anashauriana pamoja na watu kuwa wakubwa. Wanatangaza ya kwamba jeshi ndani ya mji ni ndogo kwa kulinganisha na la kwao na linaweza kushindwa. Wafundi wa ujuzi wanafanya vyombo vya vita. Waongozi wa askari wanapanga watu wa vita katika makundi na sehemu.

Mwishoni agizo la kuendelea mbele linatolewa, na jeshi lisilohesabika likaendelea, jeshi ambalo nguvu zenye kuunganika za vizazi vyote hazikuweza kamwe kuwa sawa. Shetani anakuwa mbele, wafalme na waaskari nao wanafuata. Kwa utaratibu wa kiaskari makundi katika mistari yakaendelea mbele ya uso wa dunia iliyovunjika hata kwa Mji wa Mungu. Kwa agizo la Yesu, milango ya Yerusalema Mpya ikafungwa, na majeshi ya Shetani yanajitayarisha kwa kushambulia.

Sasa Kristo anatokea kutazama adui zake. Mbali juu ya mji, juu ya msingi wa zahabu yenye kungaa, ni kiti cha enzi. Juu ya kiti hiki cha enzi Mwana wa Mungu anakaa, na pembeni yake ni raia ya ufalme wake. Utukufu wa Baba wa Milele unamuzunguka Mwana wake. Kungaa kwa kuwako kwake kunatoka juu ya milango, kujaza dunia na mwangaza.

Karibu sana na kiti cha enzi kunakuwa wale waliokuwa zamani na bidii katika kazi ya Shetani, lakini walipo ondoshwa kama vinga kutoka motoni, wakafuata Mwokozi wao kwa bidii sana. Wanaofu-

ata ni wale waliokamilisha tabia katikati ya uwongo na uasi, walioheshimu sheria ya Mungu wakati walimwengu walipoitangaza kuwa iliondolewa, na mamilioni, wa vizazi vyote, waliouawa kama wafia dini kwa ajili ya imani yao. Mbali zaidi kunakuwa "makutano makubwa sana yasiyoweza mtu kuyahesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, ... wamevikwa mavazi myeupe, na matawi ya mitende katika mikono yao". Ufunuo 7:9 . Vita yao imemalizika, ushindi wao umepatikana. Tawi la ngazi linafananisha shangwe, nguo yeupe ni alama ya haki ya Kristo ambayo saa
[325] imekuwa yao.

Katika msongano wote ule pale hakuna watu wa kuhesabia wokovu kwao wenyewe kwa wema wao wenyewe. Hakuna kitu kinachosemwa cha kile walichoteseka nacho; sauti ya msingi ya kila wimbo wa sifa ni, Wokovu kwa Mungu wetu na kwa Mwana-Kondoo.

### Hukumu Inatangazwa Juu ya Waasi

Mbele ya wakaaji waliokusanyika wa dunia na wa mbinguni kwa mkutano na kuviikwa taji kwa Mwana wa Mungu. Na sasa, kuvikwa mamlaka makubwa na uwezo, Mfalme wa wafalme anatangaza hukumu juu ya waasi waliovunja sheria yake na kutesa watu wake. "Nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, naye anayeketi juu yake, dunia na mbingu zikakimbia uso wake; na pahali pao hapakuonekana. Nikaona wafu, wakubwa na wadogo, wamesimama mbele ya Mungu, na vitabu vikafunuliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, kilicho cha uzima; na wafu wakahukumiwa katika mambo haya yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao". Ufunuo 20:11, 12.

Wakati jicho la Yesu linapoangalia juu ya waovu, wanakuwa na ufahamu wa kila zambi waliyoitenda. Wanaona pahali miguu yao ilipoacha njia ya utakatifu. Majaribu ya kuvuta ambayo waliimarisha kwa anasa katika zambi, wajumbe wa Mungu waliozarauliwa, maonyo yaliyokataliwa, mawimbi ya rehema yaliyorudishwa kwa ukaidi, moyo usiotubu--yote inaonekana kama yameandikwa kwa maandiko ya moto.

Juu ya kiti cha enzi kunafunuliwa msalaba. Kwa maoni kamili kukatokea mambo ya kuanguka kwa Adamu na hatua za kufuatana

katika shauri la wokovu. Kuzaliwa kwa unyenyekevu kwa Mwokozi; maisha yake ya kawaida; ubatizo wake katika Yorodani; kufunga na majaribu katika jangwa; huduma yake kufunua kwa watu mibaraka ya mbinguni; siku zilizojaa na matendo ya rehema, usiku wa kukesha katika maombi kule milimani; mashauri ya hila ya tamaa na uovu ambayo yalilipa faida zake; maumivu makali ya siri katika Getesemane chini ya uzito wa zambi za ulimwengu; usaliti wake kwa kundi la wauaji, matukio ya usiku ule wa kitisho kikuu-mfungwa asiyeshindana aliyeachwa na wanafunzi wake, aliyeshitakiwa katika jumba la kuhani mkuu, katika chumba kikubwa cha hukumu cha Pilato, mbele ya Herode mwenye hofu, aliyechekelewa, kutukanwa, kuteswa, na kuhukumiwa kufa--yote yanaelezwa kwa wazi.

Na sasa mbele ya makutano yaliyowayawaya maoni ya mwisho [326] yanafunuliwa; Mteswaji mvumulivu akakanyanga njia ya Kalvari; Mfalme wa mbinguni kutundikwa msalabani; makuhani na walimu wakachekelea maumivu makali ya kukata roho yake; giza kubwa sana kuonyesha wakati wakati Mkombozi wa ulimwengu alipotoa maisha yake.

Ajabu ya kutisha inaonekana kama tu ilivyokuwa. Shetani na watu wake hawana uwezo wa kugeuza na kutoka kwa picha. Yeyote aliyehusika kwa kufanya tendo anakumbuka sehemu aliyoifanya. Herode, aliyewaua watoto wasiokuwa na kosa wa Betelehemu; chanzo Herodias, ambaye juu ya nafsi yake kunadumu damu ya Yoane Mtabizaji; mzaifu, Pilato mwenye kulinda wakati; askari wenye kuchekelea; msongano wa watu wenye wazimu waliopaaza sauti, "damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu"! --kutafuta namna yote bila kuweza kujificha kutoka kwa utukufu wa uso wake Mungu, wakati waliokombolewa wanapotupa taji zao kwa miguu ya Mwokozi, kuapaaza sauti, "Alikufa kwa ajili yangu"!

Hapo kuna Neno, mkatili mkali na muovu, kutazama utukufu wa wale aliowatesa na kwa maumuvu yao akapata furaha ya kishetani. Mama yake anashuhudia kazi yake mwenyewe, namna gani tamaa alizoendelesha na mvuto wake na mfano zimezaa matunda katika mauaji yaliyoletea dunia kutetemeka.

Hapo kunakuwa mapadri wa Papa na maaskofu waliojidai kuwa mabalozi wa Kristo, huku walipokuwa wakitumia mbao zenye vyango vya kutundikia watu, gereza, na kigingi kwa kutawala watu Wake. Hapo panakuwa maaskofu wenye kiburi waliojiinua wenyewe

juu ya Mungu na wakasubutu kugeuza sheria ya Mungu Aliye juu. Wale waliojidai kuwa wababa wanakuwa na hesabu ya kutoa kwa Mungu. Kwa mda kitambo unapopita wamefanywa kuona ya kwamba Mwenye Kujua yote anakuwa na wivu wa sheria yake. Wanajifunza sasa ya kwamba Kristo anatambua faida zake pamoja na watu wake wanaoteseka.

Ulimwengu mzima wenye uovu unasimama kwakushitaki kwa ajili ya maasi makubwa juu ya kupinga serkali ya mbinguni. Hawana yeyote kwa kutetea maneno yao; hawana sababu yo yote; na hukumu ya mauti ya milele inatangazwa juu yao.

Waovu wanaona kile walichopotewa kwa sababu ya uasi wao. “Yote hii”, nafsi iliyopotea inalia, “ningaliweza kuwa nayo, Ee, upumbafu wa namna gani! nimebadili amani, furaha, na heshima kwa ajili ya ubaya, sifa mbaya, na kukata tamaa”. Wote wanaona ya kwamba kufukuzwa kwao mbinguni ni kwa haki. Katika maisha yao wametangaza: “Hatuwezi kuwa na mtu huyu (Yesu) kutawala
[327] juu yetu”.

### Shetani Ameshindwa

Kama vile katika bumbuanzi waovu wanatazama ibada ya kuvikwa kwa taji kwa Mwana wa Mungu. Wanaona mikononi mwake mbao za sheria ya Mungu walizozizarau. Wanashuhudia nguvu ya ibada kutoka kwa waliookolewa; na kama wimbi la sauti za nyimbo zinapoenea kwa makutano inje ya mji, wote wanapaaza sauti, “Haki na kweli ndizo njia zako, wewe Mfalme wa watakatifu”. Ufunuo 15:3. Kwa kuanguka na kumusujudu, wakamuabudu mfalme wa uzima.

Shetani anaonekana kama anahangaika. Mara kerubi wa kufunika, anakumbuka mahali gani ameanguka. Kutoka kwa baraza pahali alipoheshimiwa zamani ameondolewa milele. Anaona sasa mwingine anayesimama karibu ya Baba, malaika wa umbo lenye utukufu. Anajua ya kwamba cheo cha malaika huyu kingeweza kuwa chake.

Ufahamu unakumbuka makao ya hali yake ya usafi, amani na kutoshelewa ilivyokuwa yake mpaka wakati wa uasi wake. Anakumbuka kazi yake miongoni mwa watu na matokeo yake--uadui wa mtu kwa watu wenzake, maangamizi ya kutisha ya maisha, kupinduka

kwa viti vya enzi, makelele, vita, na mapinduzi. Anakumbuka bidii zake za daima kwa kupinga kazi ya Kristo. Anapoangalia matunda ya kazi yake anaona tu kushindwa. Mara kwa mara katika maedeleo ya vita kuu amekuwa akishindwa na kulazimishwa kuacha.

Kusudi la muasi mkuu lilikuwa daima kuhakikisha kuwa serkali ya Mungu ndiyo msimamizi wa uasi. Ameongoza makundi mengi kukubali maelezo yake. Kwa maelfu ya miaka mkuu huyu wa mapatano ya kufanya mabaya amelicha uwongo kuwa haki. Lakini wakati umefika sasa wakati historia na tabia ya Shetani zitakapofunuliwa. Katika juhudi yake ya mwisho kwa kuondoa Kristo kwa kiti cha enzi, kuharibu watu Wake, na kukamata makao ya Mji wa Mungu, mshawishi mkubwa amekwisha kufunuliwa kabisa. Wale waliojiunga naye wanaona kushindwa kabisa kwa kazi yake.

Shetani anaona ya kwamba uasi wake wa mapenzi haukumstahilisha kuingia mbinguni. Amezoeza nguvu zake kwa vita kumpinga Mungu; usafi na umoja wa mbinguni ungekuwa kwake mateso makubwa. Anainama chini na kukubali haki ya hukumu yake.

Kila swali la kweli na kosa katika mashindano ya siku nyingi limefanywa wazi sasa. Matokeo ya kuweka pembeni sheria za Mungu yamewekwa wazi mbele ya macho ya viumbe vyote. Historia [328]
ya zambi itasimama milele kwa wote kama ushuhuda ya kwamba pamoja na kuwako kwa sheria ya Mungu kunafungwa furaha ya viumbe vyote alivyoviumba. Viumbe vyote, vya uaminifu na vyenye uasi, kwa mapatano pamoja vinatangaza, "Haki na kweli njia zako, wewe Mfalme wa watakatifu".

Saa imefika wakati Kristo anapashwa kutukuzwa juu ya kila jina linalotajwa. Kwa ajili ya furaha inayowekwa mbele yake--ya kwamba aliweza kuleta wana wengi katika utukufu--akavumilia msalaba. Anaangalia kwa waliookolewa, waliofanywa upya kwa mfano wake mwenyewe. Anatazama ndani yao matokeo ya kazi ya roho yake, na anatoshelewa. Isaya 53:11. Kwa sauti ambayo inawafikia makutano, wenye haki na waovu, anatangaza: "Tazama biashara wa damu yangu! Kwa ajili ya hawa niliteseka, kwa ajili ya hawa nilikufa".

## Mwisho Mkali Sana wa Waovu

Tabia ya Shetani inaendelea bila kubadilika. Uasi kama maji mengi yenye kupita kwa nguvu tena yamejipenyeza kwa nguvu. Anakusudia kutoacha vita yenye kukata tamaa ya mwisho ya kupambana na Mfalme wa mbinguni. Lakini kwa mamilioni isiyohesabika yote ambayo aliyoshawishi katika uasi, hakuna anayekubali sasa mamlaka yake. Waovu wamejazwa na uchuki wa namna moja kwa Mungu unaoongozwa na Shetani, lakini wanaona ya kwamba hoja lao halina matumaini. "Kwa sababu umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu, kwa hivi, tazama, nitaleta wageni juu yako, watu wa mataifa wenye kuogopesha, na watachomoa panga zao juu ya uzuri wa hekima yako, nao watatia uchafu kungaa kwako. Watakuleta chini kwa shimo. ... nitakuharibu, Ee kerubi la kufunika, kutoka katikati ya mawe ya moto... nitakutupa hata inchi, nitakulaza mbele ya wafalme, wapate kukuona ... nitakufanya kuwa majivu juu ya inchi mbele ya wote wanaokutazama ... utakuwa maogopesho, wala hutakuwa tena hata milele". Ezekieli 28:6-8, 16-19.

"Maana kasirani kali ya Bwana ni juu ya mataifa yote". "Atanyeshea waovu mitego; Moto na kiberiti na upepo wa kuchoma zitakuwa fungu la kikombe chao". Isaya 34:2; Zaburi 11:6. Moto utashuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Dunia itaharibika. Miako ya moto unaoteketeza inatoka kwa nguvu kutoka kwa kila shimo kubwa linalokuwa wazi. Miamba halisi inakuwa motoni. Na viumbe vya asili vitayeyushwa kwa moto mkali, na inchi na kazi zilizo
[329] ndani yake zitateketea. 2 Petro 3:10. Uso wa dunia utaonekana kama fungu moja kubwa lililoyeyuka--, ziwa la moto lililochafuka. Maana ni "siku ya kisasi cha Bwana, mwaka wa malipo, kwa ubishi wa Sayuni". Isaya 34:8.

Waovu wanaazibiwa "kama ilivyo kazi yao". Shetani atateswa si kwa ajili ya uasi wake pekee, bali kwa ajili ya zambi zote alizozilazimisha watu wa Mungu kuzitenda. Katika ndimi za moto waovu watakuwa kwa maangamizi ya mwisho, shina na matawi-Shetani ni shina lenyewe na wafuasi wake ni matawi. Azabu kamili ya sheria ilijiliwa; matakwa ya haki yametimizwa. Kazi ya Shetani ya uharibifu imekomeshwa milele. Sasa viumbe vya Mungu vimekombolewa milele kwa majaribu yake.

Wakati dunia inapofunikwa kwa moto, wenye haki wanakaa kwa salama ndani ya Mji Mutakatifu. Wakati Mungu anakuwa kwa waovu kama moto unaoteketeza, anakuwa ngao kwa watu wake. Tazama Ufunuo 20:6; Zaburi 84:11.

"Nikaona mbingu mpya na dunia mpya; kwa maana mbingu za kwanza na dunia ya kwanza zimekwisha kupita". Ufunuo 21:1. Moto utakaoteketeza waovu utasafisha dunia. Kila alama ya laana imeondolewa mbali. Hakuna jehanum inayowaka milele itakayoendelea mbele ya waliokombolewa matokeo ya kutisha ya zambi.

## Kumbusho ya Kusulubiwa

Ukumbusho moja peke unaodumu: Mkombozi wetu atachukua hata milele alama za kusulubiwa kwake, alama pekee za kazi ya ukali ambazo zambi imetenda. Katika miaka ya milele vidonda vya Kalvari vitaendelea kuonyesha sifa yake na vitatangaza uwezo wake.

Kristo alihakikishia wanafunzi wake ya kwamba alikwenda kuandalia makao kwa ajili yao katika nyumba ya Baba yake. Lugha wala maneno ya binadamu hayatoshi kueleza zawadi ya wenye haki. Itajulikana tu kwa wale wanaoitazama. Hakuna wazo lenye mpaka linaloweza kufahamu utukufu wa Paradiso ya Mungu!

Katika Biblia uriti wa waliokombolewa unaitwa "inchi". Waebrania 11:14-16. Huko Mchungaji wa mbinguni ataongoza kundi lake kwa chemchemi za maji ya uzima. Huko kunakuwa na vijito vyenye kutiririka, safi kama jiwe lingaalo, na pembeni yao miti yenye kutikisika inayotupa vivuli vyao kwa njia zilizotayarishwa kwa ajili ya waliokombolewa wa Bwana. Inchi kubwa tambarere zinainuka kuwa vilima vya uzuri, na milima ya Mungu inapandisha vilele vyao virefu. Katika inchi tambarare hizo za amani, pembeni [330]
ya vijito hivyo vya uzima, watu wa Mungu, waliokuwa wasafiri na wanaohangaika watapata makao.

"Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; na watapanda mizabibu, na watakula matunda yake: hawatajenga na mtu mwingine kukaa ndani yake; hawatapanda, na mtu mwingine kula matunda yake: ... Na wachaguliwa wangu watafurahia kazi ya mikono yao". "Jangwa na inchi kavu zitafurahi; na jangwa litashangilia na kutoa maua kama waridi". "Na imbwa mwitu atakaa pamoja na mwanakondoo, na chui atalala chini pamoja na mwana-mbuzi; na mtoto

mudogo atawaongoza... Hawataumiza wala kuharibu wote katika mulima wangu wote mtakatifu”. Isaya 65:21, 22; 35:1; 11:6,9.

Maumivu hayawezi kuwako mbinguni. Hakutakuwa na machozi tena, Hakutakuwa tena mafuatano ya maziko. “Wala mauti haitakuwa tena; wala maombolezo, wala kilio: ... kwa maana maneno ya kwanza yamekwisha kupita”. “Wala hapana mwenyeji atakayesema, mimi ni mgonjwa; watu wanaokaa ndani yake watasamehewa uovu wao”. Ufunuo 21:4; Isaya 33:24.

Huko ni Yerusalema Mpya, muji mkubwa wa inchi mpya yenye utukufu. “Mwangaza wake ulikuwa mfano wa jiwe la bei kubwa, kama jiwe la yaspi, safi kama bilauri”. “Na mataifa ya waliookolewa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa dunia wataleta utukufu na heshima yao ndani yake”. “Tazama hema ya Mungu ni pamoja na watu, naye atakaa pamoja nao, nao watakuwa watu wake, na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao, na atakuwa Mungu wao”. Ufunuo 21:11,24,3.

Ndani ya Muji wa Mungu “wala hautakuwa usiku tena”. Ufunuo 22:5. Hautakuwa kuchoka tena. Tutaona ubaridi daima wa asubui bila mwisho wake. Nuru ya jua itatanguliwa na mwangaza wa ajabu ambao si wa kuumiza, lakini ambao unapita mbali sana mwangaza wa wakati wa saa sita yetu. Waliookolewa watatembea katika utukufu wa siku zote.

“Nami sikuona hekalu ndani yake, kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo ndio hekalu lake”. Ufunuo 21:22. Watu wa Mungu wanakuwa na ruhusa ya kuendelea kuwa na umoja wazi na Baba na Mwana. Sasa tunaangalia mufano wa Mungu kama katika kioo, lakini ndipo tutamwona uso kwa uso, pasipo pazia ya giza katikati.

[331]

## Ushindi wa Upendo wa Mungu

Huko upendo na huruma ambavyo Mungu mwenyewe alivyopanda katika roho yatapata mazoezi ya kweli na mazuri kabisa. Umoja ulio safi pamoja na viumbe vitakatifu na waaminifu wa vizazi vyote, vifungo takatifu vinavyofunga pamoja “jamaa lote mbinguni na duniani”--hivi vinasaidia kuanzisha furaha ya waliokombolewa. Waefeso 3:15.

Huko, akili ya kuishi milele zitatazama sana na furaha ya milele maajabu ya uwezo wa uumbaji, siri za upendo wa ukombozi. Kila akili itakuzwa, kila uwezo wa kufahamu utaongezwa. Upataji wa maarifa hautaondoa utendaji. Mambo makubwa sana yataendeshwa mbele, tamaa za juu sana zitafikiwa, tamaa za nguvu zitatimilika. Na tena hapo kutatokea vimo vipya vya kushinda, maajabu mapya ya kushangaa, kweli mpya ya kufahamu, makusudi mapya ya kuita nguvu za akili na roho na mwili.

Mali yote ya ulimwengu itafunguliwa kwa waliokombolewa wa Mungu. Wanapofunguliwa kwa mauti, wataruka bila kuchoka kwa dunia za mbali. Watoto wa dunia wataingia katika furaha na hekima ya viumbe vile havikuanguka na kugawanya hazina za maarifa yaliyopatikana kupitia vizazi kwa vizazi. Pamoja na ndoto isiyo na giza watatazama kwa utukufu wa uumbaji--jua na nyota na mambo yote, yote katika utaratibu wao ulioagizwa kuzunguka kiti cha enzi cha Mungu.

Na miaka ya milele, kama inavyopita upesi, italeta daima na zaidi mambo ya funuo tukufu ya Mungu na ya Kristo. Watu watakavyojifunza zaidi habari ya Mungu, ndivyo zaidi watakayoshangaa juu ya tabia yake. Kwa namna Yesu atakavyofunua mbele yao utajiri wa ukombozi na kazi bora za kushangaza katika mashindano makubwa na Shetani, mioyo ya waliokombolewa wanafurahi sana na kufanya ibada, na sauti elfu kumi mara elfu kumi zinaungana kuongeza nguvu la itikio la wimbo wa sifa.

“Na kila kiumbe kilicho mbinguni na juu ya dunia na chini ya dunia na vile ndani ya bahari, na vyote vilivyo ndani yake, nilivisikia, vikisema: Baraka na heshima na utukufu na uwezo kwa yeye anayeketi juu ya kiti cha enzi, na kwa Mwana-Kondoo hata milele na milele”. Ufunuo 5:13.

Vita kuu imekoma. Zambi na wenye zambi hawako tena. Ulimwengu wote mzima ni safi. Kwa Yeye aliyeumba vyote, kunajaa uzima na nuru na furaha po pote katika ufalme za anga pasipo mpaka. Kutoka kwa chembe ndogo hata kwa ulimwengu mkubwa sana, vitu vyote, vyenye uhai na vitu visivyokuwa na uhai, katika uzuri wao pasipo kivuli na furaha kamili, vitatangaza ya kwamba Mungu ni upendo.

* * * * *

[332]

# NYONGEZO

Ukarasa 33 **MAJINA YA HESHIMA.** Papa Innoncent III alitangaza kwamba mtawa mkuu wa Roma ni "Mwongozi kwa nafasi ya Mungu juu ya dunia, si kama mtu tu, lakini kama Mungu mwenyewe kabisa". Tazama kitabu kinachoitwa *DECRATELS OF THE LORD PAPE GREGORY IX, liber 1, title 7, ch. 3 Corp. Jur. Canon. (2d Leipzig ed. 1881), col. 99.*

Juu ya jina la heshima hii " Bwana Mungu Papa", tazama maandiko juu ya *Extravagantes of Pope John XXII, title 14, Ch. 4, Declaramus.* Katika maandiko an Antwerp edition of the Extravagantes, ya mwaka 1584, maneno *"Dominum Deum nostrum Papan"* (Bwana Mungu wetu Papa) yanaonekana katika kurasa ya 153.

Ukarasa 33. **HALI YA KUTOKOSA.** Tazama *Philip Schaff, The creeds of Christetendom, vol. lI, Dogmatic Decrees of the Vatican Council, pp. 234-271; The Catholic Encyclopedia, vol. VII, art. "Infallibility"; James Cardinal Gibbons, The Faith of Our Fathers (Baltimore : John Murphy Co., 110 th ed., 1917) chs. 7, 11.*

Ukarasa 33. **IBADA YA SANAMU.** "Ibada ya sanamu...ilikuwa moja kati maovu ya Kikristo ambayo yalitambaa ndani ya kanisa kwa siri, karibu bila watu kuchunguza.ao kutambua.. Kidogo kidogo, desturi ikafuata ingine kutokana na ibada hiyo, na kanisa ikaanguka ndani ya ibada ya sanamu, ... karibu bila kukemewa; na wakati walijaribu kufanya juhudi ya kuingoa, uovu ulionekana kuwa mwenye kuzidi sana na hauwezi kuondolewa *J. Mendham, The General Council, the Second of Nicaea, Utangulizi, pp. iii-vi.*

Juu ya habari ya mazungumuzo na mipango ya Baraza ya Nicaea, mwaka 787 A.D ilikusanyika kwa kusimamisha ibada ya sanamu, tazama maandiko *A Select Library of Nicene and PostNicene Fathers, second series, vol XIV, pp 521-587 (New York, 1900); C.J. Hefele, A History of the Councils of the Churches, From the Original Documents, bk. 18, Ch. 1, secs. 332,333; Ch. 2, Secs. 345352 (T. and T. Clark, ed. 1896), vol. 5, pp. 260-304, 342-372.*

Ukarasa 34. **SHERIA YA SIKU YA KWANZA YA CONSTANTI-NO,** sheria hii imetolewa katika Kilatini na katika fasiri ya Kiingereza ndani ya kitabu kinachoitwa *Philip Schaff's "History of the Christian Church"* (historia ya kanisa la Kikristo) kilichoandikwa na *Philip Schaff, vol III, 3 d period, Ch. 7, sec 75, p.38o,* [333] *foot note 1. Tazama mazungumuzo katika kitabu cha Albert Henry Newman, A Manual of Church History (Philadelphia: The American Baptist Publication Society, 1933), rev. ed., vol. I, PP. 305-307; na katika kitabu cha L. E. From, The Prophetic Faith of Our Fathers (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Assn, 1950), vol. I, pp. 376-381.*

Ukarasa 35. **TAREHE ZA UNABII.** Kanuni ya muhimu katika maelezo ya nyakati za unabii ni kanuni ya siku-mwaka-ambayo inakamata siku moja ya wakati wa unabii kama mwaka mumoja wa kalendari ya wakati. Sababu fulani fulani za Biblia juu ya kanuni hii ni kama zifuatazo : (1) kanuni ya siku-mwaka inapatana na kanuni ya kueleza mifano ya nyama kama falme, pembe kama uwezo, bahari kama watu, na kazalika. (2) Bwana, anaposema katika Hesabu 14:34 na katika Ezekieli 4:6 anaunga mukono kanuni hii. (3) siku 2300 (miaka) ya Danieli 8:14 inafunika historia ya falme za wa Medi na Wapersia, wa Giriki na Waroma, kama vile malaika anavyoeleza katika mistari 19-26 ( kwa wakati wa mwisho maono haya yatatimia ). Falme hizi zilidumu kwa nyakati ndefu zaidi ya siku za kawaida 2300. Hakuna lolote litakalo stahili isipokuwa kanuni ya siku-mwaka (4) Danieli 11 ni upanuo wa unabii wa Danieli 8, lakini Danieli 11 si unabii wa mufano. Mara tatu unabii huu unasema juu ya "miaka" (mistari 6, 8, 13) sawasawa na "siku" katika Danieli 8:14. (6) Malaika alielezea Danieli kwamba unabii haya yanaelekea "wakati wa mwisho" (8:19, 26; 10:13, 14). Kama "siku" zingekuwa na namna ilivyo wazi, unabii a haungekuwa na maana.(7) Siku moja kama mwaka ilikuwa kawaida ya kusema katika kiebrania cha Agano la Kale. Tazama Walawi 25:8; Mwanzo 29:27. (8) Kitabu cha Ufunuo kinafungua unabii wa Danieli, kikionyesha kwamba kutimilika kwazo ni kwa wakati ujao wakati wa mitume. Zaidi ya hayo, kanuni ya siku _ mwaka ilitambuliwa na kukubaliwa wanafunzi waangalifu wa Biblia kama kanuni yenye sheria. Wamoja waa wanafunzi hawa kunakuwa Joachim wa Floris, Wychiffe, Joseph

Mede, bwana Isaac Newton, Askofu Thomas Newton, Alexander Keith na wengine wengi.

Ukarasa 37. **MAANDIKO YA UWONGO.** Miongoni mwa maandiko yaliyokubaliwa kwa kawaida kuwa ya uwongo: Donation of Constantine na Pseudo-Isidorian Decretals inakuwa ya muhimu sana. Tazama maandiko *The New Schaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge, vol.III. "Donation of Constantine"* (Zawadi ya Constantino).

[334] Maandiko hii "Pseudo-Isidorian Decreals" ilikuwa mabarua ya uwongo yalioandikwa kwa wa Papa wa kwanza kutoka Clementino (mwaka 100 A.D nyuma ya Kristo) hata Papa Gregoire Mkuu (mwaka 600 A.D nyuma ya Kristo) na baadaye yalichanganywa na mkusanyo wa maandiko ya karne ya tisa kusudi wanazania kwamba yaliandikwa na "Isidore Mercator". Udanganyifu wa "Pseudo-lsidorian" kufanyizwa kama jengo kunakubaliwa sasa.

Ukarasa wa 38. **TOHARANI** . Dr Joseph Faa Di Bruno anaeleza hivi toharani: "Toharani, ni hali ya mateso baada ya maisha haya, ambayo zile roho zinafungwa kwa muda, zile ambazo huaga maisha aya baada ya kusamehewa zambi za mauti kama kwa alama na kosa, na kama kwa mateso ya milele ambayo yalisababishwa nao, lakini ambao wangali na deni ya kulipa kwa mateso ya fulani, kama vile vile roho zile ambazo zinaaga dunia zikiwa na makosa ya zambi ndogo ndogo *tu-Catholic Belief, p. 196 (ed. 1884; imprimatur Archbishop of New York). Tazama The Catholic encyclopedia, vol.XII, art. "Purgatory".*

Ukarasa 39. **UNUNUZI WA MUSAMAHA** (indulgences). Kwa historia kamili ya kila kitu ya mafundisho juu ununuzi wa musamaha, tazama mafundisho *The Catholic Encyclopedia art. "Indulgences", vol VII; A.H Newrman, A Mannual of Church History (Kanuni ya Historia ya kanisa) Philadelphia: The American Baptist Publication Society, 1953 vol. II, pp. 53,54,62.*

Ukarasa 44. **SABATO KATIKATI YA WAFUASI WA WALDENSE** Kunakuwa ushahidi unao kuwako juu ya kushika sabato ya siku ya saba miongoni mwa Waldense. Habari moja juu ya mahakama ya Papa ambayo mbele yake kulipelekwa wafuasi fulani wa Waldense wa Marovia katikati ya karne ya kumi na tano, inatangaza kwamba miongoni mwa Waldense "wengi walitukuza Sabato ya Wayuda". *Johann Joseph Ignaz Von Dollinger, Beitrage*

*Zur Sektengeschichte des Mittelalters (Contributions to the Historya of the Sects of the Middle Ages), Munich, 1890, part 2, p. 661.*

Ukarasa 49. **AMRI JUU YA WAFUASI WA WALDENSE.** Kipande cha barua ya Papa (Innocent VIII, 1487) kupinga wa Waldense kimetolewa katika fasiri ya kiingereza, ndani ya maandiko *Dowling's History of Ramanism, bk. 6, ch. 5, sec. 62 (ed. 1871).*

Ukarasa 53. **UNUNUZI WA MUSAMAHA.** Tazama nukta [335]
kwa p. 39.

Ukarasa 53, 60. **WYCLIFFE.** Kwa mandiko ya asili ya barua za Papa za kupinga Wycliffe pamoja na tafsiri ya Biblia katika kiingereza, tazama *Jonn Foxe, Acts and Monuments of the Church (London: Pratt Townsend, 1870) vol. Ill, pp. 4-13; Merle d'aubigné, The History of the Reformation in the sixteenth Century (historia ya Matengenezo katika karne ya kumi na sita) (London): Blackie and Son, 1885), vol. IV, div. 7. p. 93; Philip Schaff, History of the Christian Church (New York: Chas. Scribner's Sons, 1915), vol. V Part 2, p. 317.*

Ukarasa 54. **HALI YA KUTOKUKOSA** Tazama nukta kwa p.33.

Ukarasa 64. **UNUNUZI WA MUSAMAHA** Tazama nukta p. 39.

Ukarasa 64. **BARAZA LA CONSTANCE.** Vitabu vya siku hizi juu ya Baraza hii ni: *K. Zähringer, Das Kardinal Kollegium auf dem Konstanzer Konzil (Munster, 1935); Th. F. Grogau, The Conciliar Theory as it Manifested Itself at the Council of Constance (Washington, 1949); Fred A Kremple, Cultural Aspects of the Council of Constance and Basel (Ann Arbor, 1955).*

Tazama *John Huss, Letters (barua), 1904; E.J. Kitts, Pape John XXIII and Master John Huss (London, 1910); D. A. Schaff, John Huss (1915); na Matthew Spinka, John Huss and the Czech Reform (1941).*

Ukarasa 81. **UNUNUZI WA MUSAMAHA** Tazama nukta kwa p.39

Ukarasa 146. **MWENENDO WA WASHIRIKI WA JAMII LA YESU (JESUITISM)**. Kuhusu washiriki wa Jamii la Yesu, tazama kitabu *Concerning Jesuits,* kilitayarishwa na *Rev. John Gerard, S.J. (London: otholic Truth Society, 1902).* Katika kazi hii, wanasema kwamba "msingi maalumu wa utaratibu wote wa

Jamii ni roho ya utii kamili: “Acha kila mtu”, anaandika St. Ignatius, “mashawishwa mwenyewe kwamba wale wanaoishi chini ya utii wanapashwa kujiruhusu wao wenyewe kuendeshwa na kuongozwa na maagizo ya Mungu kupitia wakubwa wao, sawa kama vile wangekuwa maiti, ambayo inajiruhusu kupelekwa mahali popote na kutendewa hali yoyote ao kama vile fimbo (gongo) la mzee analolitumia kulishika mkononi kwa namna yote anayoweza” p.6.
[336]
Ukarasa 147. **MAHAKAMA YA PAPA.** Tazama kitabu *The Catholic Encyclopedia, vol. VIII, art. “Inquisition”; na E. Vacandard, The Inquisition: A Critical and Historical Study* ***of the Coercive Power of the Church*** *(New York: Longmans, Green, and Company, 1908).*

Kuhusu maoni ya watu ambao si wakatoliki, tazama *Philip Van Limborch, History of the Inquisition; Henry C. Lea, A History of the Inquisition in the Middle Ages, 3 vols.*

Ukarasa 166. **SABABU ZA MAPINDUZI YA UFARANSA.** Tazama *H. Von Sybel, History of the French Revolution, bk.5, ch. 1, pars. 3-7; H. T. Buckle, History of Civilization in England, chs. 8, 12, 14 (New York, ed. 1895), vol.I, pp.364-366, 369-371, 437, 540, 541, 550; Blackwood’s Magazine, vol. XXXIV, no 215 (November, 1833), p. 739; J.G. Lorimer, An Historical Sketch of the Protestant Church in France, ch. 8, pars. 6, 7.*

Ukarasa 167. **TAREHE ZA UNABII** Tazama nukta kwa p. 35.

Ukarasa 167. **JUHUDI ZA KUFUTA NA KUANGAMIZA BIBLIA.** Baraza la Toulouse liliamuru: “Tunakataza watu wasioviongozi wa dini kuwa na maandiko ya Agano la Kale na agano Jipya...Tunawakataza vikali sana zaidi kuwa na vitabu hivi katika lugha ya kusemwa na wakaaji wote”. ” Makao, nyumba nyenyekevu sana za wamaskini, na hata maficho ya chini chini ya wale watu wanaosadiki kuwa na Maandiko yataangamizwa. Watu hawa watawindwa ndani ya pori na pango na mtu ye yote atakayewapatia ulinzi atahukumiwa vikali”. *Council Tolosanum, Gregory IX, (Papa Gregori wa IX) Anno chr. 1229. Canons 14, 2.* Baraza hili lilikaa lilifanyika wakati wa vita ya Papa kupinga watu wa Albi (kwa kifaran-sa albigeois).

“Tauni hili (Biblia) ilikuwa imekwisha kufikia eneo kubwa kwa namna watu fulani walikuwa wamejichagu lia mapadri wao wenyewe, na hata wahubiri fulani ambao waligeuza na kuharibu ukweli

wa habari njema na kufanya habari njema mpya juu ya makusudi yao wenyewe... (wanajua kwamba) mahubiri na maelezo ya Biblia inakatazwa kwa washiriki". *Acts of Inquisition, Philip Yan Limborch, History of the Inquisition, ch. 8.*

Kwa Baraza la constance kwa mwaka 1415, Wycliffe alihukumiwa akisha kufa kama "yule maskini wa kunuka tauni ya [337] uzushi wa kulaaniwa ambaye alivumbua tafsiri mpya ya Maandiko katika lugha yake ya asili".

Upinzani kwa Biblia wa kanisa la Kikatoliki la Roma uliongezeka kwa sababu ya usitawi wa vyama vya Biblia. Kwa tarehe 8, mwezi wa 12, mwaka 1866, Papa Pius IX, katika barua yake kwa Maaskofu wote, inayoitwa *Quanta Cura,* alitoa hesabu ya makosa munane na kuelezwa chini ya vipindi kumi mbalimbali. Chini ya kipindi IV tunapata orosa ya: "Ujamaa, Ukomunisti, vyama vya kisirisiri, vyama vya Biblia... Tauni za aina hii zinapashwa kuangamizwa kwa njia zote ziwezekanavyo". Katika miaka ya karibu kulitokea mabadiliko ya kushangaza na ya hakika katika kanisa la Kikatoliki la Roma. Kwa upande moja kanisa limekubali tafsiri nyingi zilizotayarishwa kufuatana na lugha ya asili ya Biblia; kwa upande mwingine liliendelesha kujifunza kwa Maandiko matakatifu kwa njia ya kugawia watu bure na kwa njia ya mashirika ya Biblia. Kanisa, lakini, linaendelea kujiwekea haki ya pekee ya kueleza Biblia kufuatana na nuru na desturi yake mwenyewe, ili kutibitisha yale mafundisho ambayo hayaambatane na mafundisho ya Biblia.

Ukarasa 173. **UTAWALA WA KUTISHA** Kwa utangulizi aminifu kwa historia ya Mapinduzi ya Ufaransa, tazama *L. Gershoy, The French Revolution (1932). G.Lefebvre, The Coming of the French Revolution* (kuja kwa mapinduzi ya Ufransa) *(Princeton. 1947); na H. Von Sybel, History of The French Revolution, 4 vols. (1869). Angalia na A. Aulard, Christianity and the French Revolution (London, 1927),* ambacho ndaniyake historia inaendelea hata 1802 ni majifunzo bora.

Ukarasa 175. **WATU WENGI WA HALI YA CHINI NA WAHESHIMIWA WA HALI YA JUU** *Angalia H. Von Holst, Lowell Lectures on French Revolution,* lecture 1; tena angalia *Taine, Ancient Regime; na A Young, Travels in France.*

Ukarasa 177. **MALIPIZI.** Angalia *Thos. H. Gill, The Papal Drama, bk. 10 E. de Presensé, The Church and The French Revolution,* (kanisa na mapinduzi ya Ufransa) *bk. 3, ch. 1.*

Ukarasa 177. **UKATILI WA UTAWALA WA KUTISHA.** Angalia *M.A. Thiers, History of rhe French Revolution (New York, ed. 1890, tr. by F. Shobert), vol. 3, pp. 42-44, 62-74, 106; F.A. Mignet,*
[338] *History of the French Revolution (Bohn, ed. 1894), ch. 9, par. 1; Sir Archibald Alison, History of Europe, From the Commencement of the French Revolution to the Restoration of Bourbons, vol.l, ch. 14 (New York, ed. 1872), vol. 1, pp. 293-312.*

Ukarasa 179. **MUZUNGUKO WA MAANDIKO.** Kwa mwaka 1804, kutokana na *Mr William Canton, wa shirika la Biblia linaloitwa "British and Foreign Bible Society",* Biblia zote zinazokuwa ulimwenguni, zilizoandikwa kwa mikono ao kwa machini, ukihesabu kila tafsiri katika kila inchi, kwa kuhesabiwa hazikuwa zaidi ya milioni ine.

Tangu 1816 1981, Shirika la Biblia la Amerika peke yake lilichapisha nakala (copies) 98.200.951 za Biblia yote nzima na nakala za hesabu za Biblia 3.396.127.592. Kwa mwaka 1981, Shirika la Biblia la Amerika lilichapisha nakala za Biblia yote nzima 3.365.779. Shirika za Biblia zingine ziliongeza mamilioni mengi za nakala kwa hesabu hizi.

Ukarasa 179. **UJUMBE KWA INCHI YA KIGENI** Kazi ya kuhubiri injili ya kanisa la kristo la mwanzo ilikuwa kwa kweli imekufa kwa mwaka 1000, na ilifuatwa na mashambulio ya vita za Papa. Wakati wa Matengenezo kazi ya kuhubiri injili katika ugenini ilionekana kuwa hafifu. Uamsha wa utawa ulizaa waeenezaji wa injili. Kazi la kanisa ya la Moravi kwa karne la kumi na munane ilikuwa ya kuonekana sana, na kulipatikana shirika fulani za waenezaji wa injili ambazo zilizofanywa na Uingereza kwa ajili ya kazi katika inchi za kikoloni ya Amerika ya kaskazini. Lakini jambo muhimu zaidi la kazi ya uenezaji wa injili ulioanza karibu mwawka 1800, kwa "wakati wa mwisho" (Dan. 12-4). Katika mwaka 1792, Shirika la Uenezaji wa injili la Wabatista lilituma Carey kwa inchi ya India. Kwa mwaka wa 1795, Shirika la *London Missionary* lilitengenezwa na shirika lingine kwa mwaka 1799, ambalo kwa mwaka 1812 liligeuka kuwa shirika linaloitwa *Church Missionary Society.* Nyuma kidogo Shirika la Uenezaji wa Injili la WaMe-

todisti wa Wesley (Wesleyan Methodist Society) likaafanya. Katika mwaka 1812 Muungano wa inchi za Amerika ulianzisha shirika linaloitwa *American Board of Commissioners for Foreign Missions* (Baraza la Amerika la Wajumbe kwa inchi za kigeni na kwa mwaka ule Adoniran Judson akatumwa huko Calcutta. Mwaka uliofuata akaweka makao yake pale Burma. Kwa mwaka 1814 kulianzishwa Muungano wa Uenezaji wa Injili wa Wabatista wa Amerika. Kwa mwaka 1837 kulianzishwa Baraza linaloitwa *Presbyterian Board of* [339]
*Foreign Missions.*

"Kwa mwaka 1800 nyuma ya Yesu, wingi wa Wakristo wa nguvu walikuwa vizazi vya wale ambao wamageuka mbele ya mwaka 1500 nyuma ya Kristo... Sasa kwa karne ya kumi na tisa, dini ya Kristo iliongezeka... Hakuna wakati wa maendeleo ule ambao kanisa la Kikristo liliinuka kwa mashirika kwa wingi wa namna hii. Hakuna wakati kanisa la kikristo liliikuwa na mguso wa moyo wa watu wa Ulaya ya Mangaribi. Juhudi nyingi hizi ndizo zilileta kazi ya kuanzisha shirika ya Uenezaji wa Injili, ambayo kwa karne ya kumi na tisa iliongeza watu na mvuto wa Kikristo". *Kenneth Scott Latourette, A History of the Exppansion of Christianity, vol. IV, The Great Century, A.D 1800 A.D. 1914 (New Yorks: Harper and Bross., 1914), pp. 2-4.*

Ukarasa 203. **SIKU MOJA KWA MWAKA MMOJA** Angalia nukta kwa p.35.

Ukarasa 205. **MWAKA 457 MBELE YA YESU.** Kwa uhaki wa tarehe ya mwaka 457 mbele ya Yesu kwamba ni mwaka wa saba wa utawala wa mfalme Artasasta, angalia *S.H. Horn na L.H. Wood, The Chronology of Ezra 7 (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1953); E.G. Kraeing, The Brooklyn Museum Aramaic Papyri (New Haven or London, 1953), pp. 191-193; "The Seventh -day Adventist Bible Commentary" (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1954), vol. Ill, pp. 97-110.*

Ukarasa 209. **KUANGUKA KWA UFALME WA UTURKIA** Katika wakati wote wa Matengenezo, Uturkia ulikuwa unaleta woga kila wakati kwa Ulaya ya Kikristo; maandiko ya Watangenazaji yanajaa na hukumu juu ya utawala wa Uturkia. Tangu wakati huu waandishi wa Kikristo walihusika na daraka la Uturkia katika tukio ya wakati ujao, na waandishi wa maelezo juu ya unabii wameona

uwezo wa Uturkia na kuanguka kwake kulikotangazwa na Maandiko mbele ya wakati.

Kwa unabii wa "sasa, siku, mwezi, mwaka", kama sehemu ya baragumu la sita, Josiah Litch alionyesha matumizi ya wakati wa unabii, wa kumaliza Uhuru wa Uturkia kwa mwezi wa munane, mwaka 1840.

Kitabu cha Uriah Smith kinachoitwa Thoughts on Daniel and the Revelation (Mawazo juu ya Danieli na Ufunuo), rev.ed.of 1944, kinazungumza juu ya hesabu ya wakati wa utabiri huu kwa namna
[340] ya unabii kwa karasa za 506-517.

Ukarasa 232. **KANZU ZA MUPANDO.** Hadizi ambayo inasema kwamba Waadventist walitengeneza kanzo ambazo watapanda nazo "kumulaki Bwana hewani" ilitungwa na wale ambao walitamani kulaumu mahubiri kuhusu kurudi kwa Yesu. Uchunguzi wa uangalifu ulionyesha uwongo kwa hadizi hii.

Maandiko ya kanusha hadizi hii ya kanzu za kukaa kwa kupanda mbinguni, tazama *Francis D.Nichol, The midnight Cry (Washington, D.C.: Review and Herald Publushing Association, 1944), chs.25-27, and Appendices H.J.tazama pia LeRoye From, The Prophetic Faith of Fathers (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1954), vol. IV, pp 822-826.*

Ukarasa 269. **UJUMBE MARA TATU.** Ufunuo 14-6,7 inasema mbele ya wakati juu ya utangazaji wa ujumbe wa malaika wa kwanza. Kwa hivyo nabii anaendelea: "Malaika mwingine akamfuata akisema: Umeanguka, umeanguka, Babeli,... na malaika wa tatu akawafuata. Neno lililotafsiriwa hapa "akafuata" maana yake ni "kwenda pamoja na", "kufuata mmoja", "kwenda naye". Tena maana yake ni "kusindikiza". Wazo walitaka kutoa ni la "kwenda pamoja", "kuwa pamoja". Wazo la Ufunuo 14:8,9 si kwamba malaika wa pili na wa tatu walifuata tu malaika wa kwanza katika hatua ya wakati, lakini wazo ni kwamba walienda pamoja naye. Ni watatu tu kwa utaratibu wa kutokea kwao. Lakini wakisha tokea, wanaendelea pamoja.

Ukarasa 352. **CHEO CHA UWEZO WA MASKOFU WA ROMA.** Angalia kitabu cha *James Cardinal Gibbons, Faith of Our Fathers (Baltimore: John Murphy Co., 110th ed., 1917), chs. 5,9,10,12.*

Ukarasa 352. **SABATO MIONGONI MWA WALDENSE.** Angalia nukta kwa p. 44.

Ukarasa 353. **KANISA LA ETIOPIA NA SABATO.** Kanisa la Etiopia linaloitwa Kopta (Coptic) lilishika Sabato ya siku ya saba mpaka hapo majuzijuzi. Waetiopia vile vile walishika siku ya Kwanza (dimanche). Uchungaji wa Sabato ya siku ya saba, kwa kweli karibu kumesimama katika Etiopia ya sasa. Kuhusu maelezo ya washahidi waliojionea kwa macho mambo ya siku za dini katika
Etiopia, angalia *Pero Gomes de Teixeira, The Discovery of Abissinia* [341]
*by the Portuguese in 1520* (kilichotafsiriwa kwa kingereza huko *London: British Museum, 1938), p.79; Father Francisco Alvarez, Narrative of the Portuguese Embassy to Abyssinia During the Years 1520-1527, in the Records of the Hakluyt Society (London, 1881), vol. LXIV, pp. 22-49.*

**Maneno yengine** na vitabu vilivyotagiwa waweza kuyachunguza katika kitabu kama hiki kwa lugha ya Kingereza: *From Here to Forever.*